

# **UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

## **ISAYA: NABII NA SIKU ZAKE SURA YA 1-39**

NA BOB UTLEY,  
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI  
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO  
AGANO LA KALE, VOL.11A

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS  
2010

Haki miliki ©2001 by Bible Lessons International, Marshall, Texas (Iliyosahihishwa 2006, 2010) Haki zote zimehifadhiwa. Si rukusa kwa sehemu yeyote ya kitabu hiki kuzalishwa kwa namna yeyote au kwa jinsi yeyote pasipo kibari cha mchapishaji.

Bible Lessons International  
P. O. Box 1289  
Marshall, TX 75671-1289  
1-800-785-1005

ISBN

Msingi wa andiko la kibibia lililotumika katika fasihi hii ni:

New American Standard Bible (Update, 1995)  
Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by  
The Lockman Foundation  
P. O. Box 2279  
La Habra, CA 90632-2279

Migawanyo ya aya na muhtasari wa kichwa cha habari vile vile uchaguzi wa vifungu ni kutoka:

1. The New King James Version, Copyright ©1979, 1980, 1982 by Thomas Nelson, Inc. Likitumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.
2. The New Revised Standard Version of the Bible, Copyright ©1989 by the Division of Christian Education of National Council of the Churches of Christ in the U. S.A. Likitumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.
3. Today's English Version is used by permission of the copyright owner, The American Bible Society, ©1966, 1971. Likitumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.
4. The New Jerusalem Bible, copyright ©1990 by Darton, Longman & Todd, Ltd. and Doubleday,a division of Bantam Doubleday Dell Publishing Group, Inc. Likitumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

[www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

# ORODHA YA YALIYOMO

Maelezo sahihi ya Vyanzo vya kiufundi vilizotumika katika fasili hii .....	i
Maelezo sahihi ya muundo wa maneno ya Kiebrania yanayogonganisha fasili ya maandiko .....	iii
Vifupisho Vilivytumika Katika Fasihi Hii.....	ix
Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia!.....	x
Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika.....	xii
Fasihi	
Utangulizi wa Kitabu cha Isaya .....	01
Isaya 1 .....	10
Isaya 2 .....	38
Isaya 3 .....	54
Isaya 4 .....	63
Isaya 5 .....	69
Isaya 6 .....	84
Isaya 7 .....	96
Isaya 8 .....	104
Isaya 9 .....	117
Isaya 10 .....	125
Isaya 11 .....	134
Isaya 12 .....	142
Isaya 13 .....	146
Isaya 14 .....	153
Isaya 15 .....	166
Isaya 16 .....	171
Isaya 17 .....	176
Isaya 18 .....	183
Isaya 19 .....	188
Isaya 20 .....	198
Isaya 21 .....	201
Isaya 22 .....	208
Isaya 23 .....	218
Isaya 24 .....	225
Isaya 25 .....	235

Isaya 26 .....	243
Isaya 27 .....	254
Isaya 28 .....	261
Isaya 29 .....	270
Isaya 30 .....	280
Isaya 31 .....	293
Isaya 32 .....	298
Isaya 33 .....	309
Isaya 34 .....	318
Isaya 35 .....	325
Isaya 36 .....	330
Isaya 37 .....	337
Isaya 38 .....	349
Isaya 39 .....	357
Kiambatisho cha Kwanza: Utangulizi wa Ushairi wa Kiebrania .....	360
Kiambatisho cha Pili: Utangulizi wa Unabii wa Agano la Kale .....	363
Kiambatisho cha Tatu: Mapitio Mafuti ya Kihistoria .....	367
Kiambatisho cha Nne: Majedwali	
1. Kipindi cha Matukio Muhimu katika Agano la Kale.....	374
2. Wafalme na Matukio ya Wababeli, Washamu, na Utawala wa Kinasaba wa Kiyunani.....	376
3. Wafalme wa Tawala Zilizogawanyika.....	380
Kiambatisho cha Tano: Kauli ya Kimafundisho .....	383

## MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO

Majina ya Uungu, 1:1.....	12
Upendeleo wa Kinjilisti wa Bob, 1:3 .....	16
Uchaguzi/Maamuzi ya Kabla na Hitaji kwa ajili ya Ulinganifu wa Kithiolojia,1:3 .....	17
Haki, 1:4 .....	19
Utakaso, 1:4 .....	22
Bwana wa Majeshi, 1:9 .....	24
Mabaki, maana Tatu, 1:9 .....	25
Fasihi ya Kimashariki, 1:16.....	28
Agano, 1:19 .....	30
Mtazamo wa Kibiblia Kuhusu Kileo na Ulevi 1:22.....	32
Moto, 1:31 .....	36
Enzi hii na Enzi Ijayo 2:2 .....	40
Kwa Nini Siku za Mwisho ni Zenye Kuleta Mabishano 2:2.....	41
Mwamuzi, Haki, Hukumu katika Isaya 3:1 .....	56
Utukufu, 3:8 .....	58
Kuuabudu Mwezi 3:18 .....	61
Yesu Mnazareti, 4:2 .....	65
Vitabu Viwili vya Mungu, 4:3 .....	66
Mashariki Karibu ya Mbali Uzani na Vipimo, 5:10 .....	74
Wafu Wako Wapi?, 5:14 .....	77
Utaratibu wa Mazishi, 5:25.....	82
Lugha ya Kibinadamu iliyotumika Kumwelezea Mungu, 6:1 .....	86
<i>Seraphim</i> , 6:1 .....	87
Takatifu, 6:3 .....	88
Utatu, 6:8 .....	91
Toba Katika Agano la Kale, 6:10.....	93
Wanawake Katika Biblia, 8:3.....	107
Jiwe Kuu la Pembeni, 8:14-15.....	113
Uwakilishi wa namba katika Maandiko, 11:12 .....	139
Shetani, Tambuzi za Kimuktadha Katika Sura ya 14 .....	155
Majitu, 14:9.....	160
Ibada kwa Walio Katika Huzuni, 15:1.....	169

Wema ( <i>Hesed</i> ), 16:5.....	173
Ibada ya Ustawi Katika Mashariki Karibu ya Mbali, 17:8.....	179
AKujua, 19:21.....	195
Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu Katika Agano la Kale, 22:25.....	214
Fasihi ya Matukio ya siku za Mwisho, Tambuzi za Kimuktadha Katika Sura ya 24.....	226
Ardhi, Nchi na dunia, 24:1.....	227
Wazee, II Yohana 1.....	234
Mambo ya Ajabu, 25:1.....	237
Maneno yanayotumika kuelezea Mafunuo ya Mungu, 26:8.....	248
Pembe Zitumiwazo na Israeli, 27:13.....	260
Fidia/Komboa, 29:22.....	277
Kivuli, 30:2.....	282
Nabii (Maneno Tofauti ya Kiebrania), 30:10.....	286
Milele (OLAM), 32:14.....	303
Utu wa Roho, 32:15-20.....	305
Amani, 32:17.....	306
Wokovu, 33:2.....	312
Pepo Wabaya, 34:11-15.....	322
Maombi ya Kusihi, 37:21-24.....	343
Malaika wa Bwana, 37:36.....	347
Maneno ya Msamaha, 38:17.....	355

## **MAELEZO MAFUPI YA VYANZO VYA KIUFUNDI VILIVYOTUMIKA KWENYE MFULULIZO WA FASIHI HII**

### I. Maneno/misamiati

Kuna maneno mengi mazuri mbali mbali yanayopatikana katika lugha ya Kiebrania cha kale.

- A. *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* kilichoandikwa na Francis Brown, S. R. Driver, na Charles A. Briggs. Yanaegemea juu ya misamiati ya Kijerumani ya William Gesenius. Yanajulikana kwa vifupisho vya BDB.
- B. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na Ludwig Koehler na Walter Baumgartner, yaliyotafasiliwa na, M. E. J. Richardson. Yanajulikana kwa vifupisho vya KB.
- C. *A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na William L. Holladay na inaegemea juu ya maneno ya Kijerumani (#A).
- D. Idadi tano mpya za usomaji wa neno la kithiolojia lililoandikwa *The New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, kilichohaririwa na Willem A. Van Gemeren. Yanajulikana kwa vifuapisho vya NIDOTTE.

Ambapo kuna aina ya maneno muhimu, nimeonyesha tafasiri mbali mbali za Kiingereza (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB) toka kwenye tafasiri za “neno-kwa-neno” na “mlinganyo wa nguvu” (kama vile Gordon Fee & Douglas Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 28-44).

### II. Visarufi

Utambulisho wa kisarufi mara nyingi huzingatia juu ya John Joseph Owens' *Analytical Key to the Old Testament* katika juzuuy ya nne. Hili limehakikiwa na Benjamin Davidson's *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon of the Old Testament*. Vitu vingine vya kusaidia kwa ajili ya visarufi na sintaksi ambazo zinatumika sana katika vipengere vya juzuuy za agano la kale za mtiririko wa “kuelewa Biblia” ni “ule msaada wa mfuatano wa watafasiri” toka kwa United Bible Societies. Kimeandikwa “kitabu kidogo cha mkononi .”

### III. Kimaandiko

Mimi nimejikita kwenye uvuvio wa konsonanti za maneno ya Kiebrania(sio katika hoja za vowel za Kimosoreti na maoni.kama ilivyo katika maandiko yote yaliyonukuliwa kwa mkono,kwenye maandiko ya kale, kuna baadhi ya sura zenye maswali. Hili huwa hivyo mara nyingi kwa sababu ifuatayo:

- A. *hapax legomenon* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano la Kale la Kiebrania)
- B. Maneno ya kinahau (maneno na vifungu ambavyo maana yake iliyo wazi imekwisha potea)
- C. Kutojulikana kihistoria (kukosekana kwa habari kuhusu ulimwengu wa kale)
- D. Wingi wa elimu-maana ya Kisemitiki wa misamiati finyu ya Kiebrania
- E. Matatizo yanayohusianishwa na uandishi wa maaandishi ya Kiebrania ya kale ya waandishi wa mwanzo kwa kutumia mkono.
- F. Waandishi wa Kiebrania waliosomea huko Misri waliojisikia kuwa huru kuyahariri maandiko waliyoyanakili kwa ajili ya kuyafanya kuwa kamili na ya kueleweka wakati wa siku zao (NIDOTTE kur. 52-54).

Kuna vyanzo mbali mbali vya maneno na maandiko ya Kiebrania nje ya tamaduni ya kimaandiko ya Kimasoreti.

1. Torati ya Kisamaria
2. Magombo ya Bahari ya Chumvi

3. Baadhi ya sarafu, herufi na vigae vya vyungu vilivypatikana baadaye (vipande vya vigae vya vyungu vilivytumika kuandikiapo maandiko), lakini kwa maeneo mengine,hakuna uhusiano wa kimachapisho katika Agano la Kale kama yale yaliyoko katika machapisho ya Agano Jipya la Kiyunani. kwa ajili ya ufasaha wa makala mazuri juu ya uendelevu wa kimaandiko ya andiko la Kimasoreti (miaka ya 900 B.K) angalia “Uendelevu wa andiko la Agano la Kale” na Bruce K. Waltke katika toleo la NIDOTTE, juzu. 1, kur. 51-67.

Andiko la Kiebrania lililotumika ni *Biblia Hebraica Stuttgartensia* toka German Bible Society, 1997, ambayo inaegemea juu ya Leningrad Codex ( 1009 B.K). Mara chache, matoleo ya kale (maandiko ya kale ya Kiyunani, Kiarama Targums, Syriac Peshitta, na Latin Vulgate) yanazungumzika kama Kiebrania ni kigumu au kinatatiza kwa wazi.

## **MAELEZO SAHIHI YA MUUNDO WA KIVITENZI VYA KIEBRANIA**

### **AMBAVYOVINAGONGANA NA FASILI YA MAANDIKO**

#### I. Maendeleo mafupi ya kihistoria ya Kiebrania

Waebrania ni sehemu ya kifamilia ya lugha ya Shemu kusini mwa Asia. Jina (lililotolewa na wasomi wa sasa) limetokana na Mwana wa Nuhu, Shemu (kama vile Mwa. 5:32; 6:10). Kizazi cha Shemu kimeorodheshwa katika Mwa. 10:21-31 kama Waarabu, Washamu, Waarameni, na Waashuru.

Kiukweli, baaadhi ya lugha za Kisemiti zinatumia na mataifa yaliyooodheshwa katika ukoo wa Hamu (kama vile Mwa. 10:6-14), Wakaanani, Wafoeniki, na Waethiopia.

Waebrania ni sehemu ya kikundi cha kaskazini Magharibi mwa lugha hizi za Kisemiti. Wasomi wa leo wana mifano ya kikundi cha lugha ya kale toka :

- A. Waamori (*Mari Tablets* tokea karne ya 18 K.K. huko Akadi)
- B. Wakaanani (*Ras Shamra Tablets* tokea karne ya 15 Ugariti)
- C. Wakaanani (*Amarna Letters* tokea karne ya 14 wakaanani wa huko Akadi)
- D. Wafoeniki (Waebrania walitumia alfabeti za Wafoeniki)
- E. Wamoabu (Mawe ya mfalme Mesha, 840 K.K.)
- F. Waaramaiki (lugha rasmi ya Himaya ya Uajemi iliyyotumika katika Mwa. 31:47; Yer. 10:11; Dan. 2:4b-6; 7:28; Ezr. 4:8-6:18; 7:12-26 na iliongewa na Wayahudi katika karne ya kwanza huko Palestina

Lugha ya Kiebrania iliiwa "lugha ya Kaanani." Mara ya kwanza iliiwa "Kiebrania" katika utangulizi Mhubiri (Hekima ya Yoshua Bin Sira) kuhusu 180 K.K. na baadhi ya maeneo mengine ya awali, kama vile *Anchor Bible Dictionary*, juzu 4, kur. 205na kuendelea) sana sana yanakaribiana kufanana na Wamoabu na khabila lililotumika huko Ugariti. Mifano ya ya Waebrania wa kale wanaopatikana nje ya Biblia ni

1. Kalenda ya Gaza, 925 K.K. (andiko la kijana wa shule)
2. Andiko /ujumbe wa Siloam, 705 K.K (maandiko yaliyopatikana katika njia za chini)
3. Vigae vya waebrania, 770 K.K (kodi inanakiriwa kwenye vigae vya chungu)
4. Herufi zilizoandikwa kwenye vigae, 587 K.K (mawasiliano kwenye vita)
5. Mihuri na sarafu za watu wa Makabi
6. Baadhi ya maandiko yaliyopatikana katika magombo ya Bahari ya Chumvi
7. Maandiko mbali mbali (kama vile "lugha[Kiebrania]", "ABD 4:203 nakuendelea)

Kama ilivyo lugha zingine za Kisemiti, inaanishwa na maneno yaliyoundwa na konsonanti tatu (mizizi mitatu ya kikonsonanti). Ni lugha thabiti isiyopindika. Mizizi mitatu ya konsonanti inabeba msingi wa maana ya neno, wakati kiambishi awali, kiambishi tamati, au maneno ya nyongeza yanaonyesha utendaji wa kisarufi (voweli zinaongezeka baadae, kama vile Sue Green, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, uk 46-49).

Misamiati ya Kiebrania inaonyesha tofauti kati ya lugha ya mjazo na ushairi. Maana ya neno imehusianishwa na asili ya ngano/hadithi (sio usanifu wa lugha). Mchezo wa neno na mchezo wa sauti ni vitu vya kawaida (*paronomasia*)

#### II. Dhana ya utabiri

##### A. VITENZI

Neno la kawaida linalotarajiwa ni KITENZI, KIWAKILISHI, KIIMA (likiwa na vivumishi vyake), KISHAMIRISHO (kikiwa na vivumishi chake). KITENZI cha msingi kisicho pungua ni *Qal*, chenyé muundo wa UMOJA, JINSI YA KIKE, na TIMILIFU. Ni namna misamiati ya Kiebrania na Kiaramaiki inavyopangwa. VITENZI vinanyumbulishwa majina kuonyesha

1. Namba-umoja, wingi, umiliki wa vitu viwili
2. Jinsi-jinsi ya kiume na jinsi ya kike (isio na jinsi)
3. Dhamira-elekezi, tegemezi, shurutishi (kwa kulinganisha lugha za Magharibi ya leo, uhusiano wa kitendo kuelekea ukweli halisi)
4. Njeo-(dhana)

WAKATI TIMILIFU, inayomaanisha kutimiliza, kwa maana ya kuanza, kuendelea, na kuhitimisha kitendo. Mara zote muundo huu ultumika kwa ajili ya kitendo kilichopita,

- a. tukio linatokea. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema “muundo mzima ulioelezewa kwa wakati timilifu pia umezingatiwa kuwa wenye uhakika. Wakati usiotimilifu unaweza kuonyesha hali ya kuwezekana au shauku au yenye kutarajiwa, lakini wakati timilifu unaliona hili kama lenye uhakiki, halisi na kweli” (uk. 36). S. R. Driver, *A Treatise on the Use of the Tenses in Hebrew*, inaielezea kama: wakati timilifu unaofanya kazi kuonyesha vitendo vyenye kutimilizwa ambavyo hakika vinasimama wakati ujao, lakini vinachukulia kama vyenye kujitegemea juu ya kusudi lisilobadilika la nia thabiti ambalo laweza kuongewa kama kitu halisi kilichochukua nafasi: kwa hiyo suluhisho, ahadi, au tamko, hasa lile la ki-Ungu mara nydingi linatamkwa katika njeo ya wakati timilifu” (uk. 17 mf., utimilifu wa kinabii). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anauelezea muundo wa kimaneno kwa namna hii:  
“....inaiangalia hali kutokea nje, kwa ukamili wake. Kwa namna hiyo kinaelezea ukweli mrahisi, ingawa kinawezakuwa ni kitendo au hali (ukijumuisha hali ya kuwa au fikra). Kinapotumika katika vitendo, mara nydingi inakitazama kitendo kama kilicho kamili toka kwenye hoja ya mzungumzaji mwenye ustadi au msimuliasi (ikiwa ni kamili au sio kamili kwa maana ya uhalisia au ukweli na sio hoja). Utimilifu unaweza kuhusika katika kitendo /hali ya wakati uliopita, uliopo ao ujao. Kama ilivyoelezewa hapo juu, muda, ambaao unashawishi namna gani mtu anaweza kutafasiri utimilifu kwenda kwenye njeo ya lugha iliyobobea kama Kiingereza, lazima ipimwe toka kwenye muktadha” (uk. 86)
  - b. WAKATI USIOTIMILIFU, unaoelezea kitendo kilichoko katika mchakato (kisichotimilifu, chenyе kujirudia, chenyе kuendelea, au chenyе udharura), mara nydingi huenenda kuelekea lengo. Mara nydingi muundo huu ultumika kwa kitendo cha wakati uliopo na ujao. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema “NYAKATI ZOTE ZISZOTIMILIFU zinawakilisha hali yakutokukamilika. Zinaweza kuwa ni zenyе kujirudia au kuendelea au za dharura. Kwa maneno mengine, au kwa sehemu Fulani inaanza au kiasi Fulani inahakikiwa. Kwa namna zozote katika baadhi ya maana haijamalizika, yaani., haijakamilika” (uk. 55). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anasema “ni vigumu kupunguza kiini cha kutokutimia kwenda dhana moja, kwa vile inajumuisha vyote dhima na dhamira. Muda mwingine wakati usiotimilifu hutumika kwa namna ya kuarifu na kutengeneza maelezo pingamizi. Wakati mwingine inakitazama kitendo zaidi kitegemezi, kama kinadharia, dharura, chenyе kuwezekana na nakadharika” (uk. 89)
  - c. Neno lililoongezewa *waw*, linalounganisha KITENZI kwenye kitendo cha KITENZI kilichopita
  - d. Dhana SHURUTISHI, inayosimamia juu ya uhiari wa mnenaji na kitendo muhimu cha wasikilizaji
  - e. Katika Uyahudi ya kale muktadha mpana uliweza kuamua mwelekeo wa muda wa uandishi uliokusudiwa.
- B. Miundo mikuu saba iliyobadilishwa na maana zake. Kiuhalsia miundo hii inatenda pamoja na nyenzake katika muktadha na haipaswi kutengwa
1. *Qal (Kal)*, ni muundo wa kawaida na wa msingi katika miundo yote. Unadokeza kitendo rahisi au hali ya nafsi. Hakuna kisababishi au ulazima uliotumika.
  2. *Niphil*, ni muundo wa pili ulio wa kawaida sana. Mara nydingi huwa katika hali ya KUTENDWA, lakini muundo huu pia hutenda kama wenye kubadilishana na kujirejea. Pia hauna kisababishi au ulazima uliotumika.
  3. *Piel*, muundo huu ni muundo tendaji na huelezea kuhsu kukifanya kitendo kuwa katika hali ya nafsi. Maana ya msingi ya shina la neno *Qal* inajitokeza au kuendelea kwenye hali ya nafsi.

4. *Pual*, ni neno mfanano TENDWA wa neno *Piel*. Mara nyngi huelezewa kwa KIAMBATA
5. *Hithpael*, ambalo ni shina la kujirejea au kubadilishana. Linalezeza usisitiasi wa kitendo au hali ya kudumu ya kitendo kulinganisha na shina la neno *Piel*. Muundo adimu TENDWA unaitwa *Hothpael*.
6. *Hiphil*, ni muundo tendaji wa usababishaji shina tofauti na neno *Piel*. Unawezakuwa na dhana ya ruksa, lakini mara nyngi unarejelea kwenye sababu ya tukio. Ernst Jenni, Mjerumani mwenye asili ya kiebrania mwana sarufi, anaamini kuwa neno *Piel* linadokeza kitu fulani kuja kwa hali ya nafsi, wakati *Hiphil* inaonyesha jinsi inavyotokea.
7. *Hophal*, ni neno mlingano TENDWA kulinganisha na neno *Hiphil*. Haya mashina ya mwisho mawili ndiyo madogo yaliyotumika kati ya yale mashina saba.

Wingi wa habari hii unapatikana toka *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, cha Bruce K. Waltke na M. O'Connor, kur. 343-452

Chati ya kundi na kisababishi chake. Namna moja katika uelewa wa muundo wa KITENZI cha Kiebrania ni kukiangalia chenyewe katika kipengere cha mahusiano ya IRABU. Baadhi ya mashina ya maneno yanatofautiana na mashina ya maneno mengine (yaani *Qal* - *Niphal*; *Piel* - *Hiphil*), chati iliyoonyeshwa hapa chini inajaribu kuangazia kwenye utendaji wa msingi wa mashina ya KITENZI na visababishi vyake.

IRABU au KIIMA	HAKUNA KUNDI LINALOFUATA	KUNDI TENDAJI LINALOFUATA	KUNDI TENDEWA LINALOFUATA
TENDAJI	<i>Qal</i>	<i>Hiphil</i>	<i>Piel</i>
YA KATI TENDWA	<i>Niphal</i>	<i>Hophal</i>	<i>Pual</i>
KUJIREJEA/KUTENDEANA	<i>Niphal</i>	<i>Hiphil</i>	<i>Hithpael</i>

Chati hii imechukuliwa toka katika majadiliano mazuri ya muundo wa kivitenzi katika uelewa wa utafiti wa lugha ya Akkadia (kama vile Bruce K. Waltke, M. O'Conner, *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, ukurasa wa 354-359)

R. H. Kennett, *A Short Account of the Hebrew Tenses*, ametoa onyo lenye kufikirika kuwa muhimu. "mara nyngi nimeweza kuanzisha katika mafundisho, kuwa kiongozi cha wanafunzi kilicho kigumu katika vitenzi nya Kiebrania ni kupata maana iliyoelezewa katika fikra za Waebrania wenyewe; kuwa ndiyo kusema, kuna tabia ya kutoa kwa mwelekeo wa kufanana kwa kila njeo za Kiebrania kama namba fulani ya muundo wa Kilatini au Kiingereza ambapo njeo hiyo mahsus kwa kawaida yaweza kutafasiriwa. Matokeo ni kushindwa kutofautisha wingi wa hivi vivuri venye maana, ambavyo vinatoa uhai aina hiyo na nguvu kwenye lugha ya Agano la Kale. Ugumu katika matumizi ya vitenzi nya Kiebrania uko tu katika hoja ya mtizamo, kwa hiyo moja kwa moja yanatofautiana na ya kwetu, kutokana na kile Waebrania wanaangalia kitendo; muda wa mambo, ambao pamoja nasi ni upendeleo wa kwanza, kama neno lenyewe, "njeo" linavyoonyesha, kwao kuwa ni chaguo la pili. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa mwanafunzi kwa uwazi aweze kuchukua, sio kwa wingi miundo ya Kilatini au Kiingereza ambayo inaweza kutumika kutafasiri kila njeo za Kiebrania, bali kiasi Fulani dhana ya kila kitendo, kama kilivyowasilishwa katika fikra za Waebrania. Jina la 'njeo' kama liliyotumika katika vitenzi nya Kiebrania vinapotosha. Kile kinachoitwa 'njeo' za Kiebrania hakielezei muda lakini kwa kidogo hali ya kitendo. Hakika hakikuwekwa kwa ajili ya kuleta mkanganyiko ambao ungaliweza kutokea kuitia matumizi ya neno 'kauli' kwa namna zote mbili ya nomino na vitenzi, 'kauli' zingalikuwa nzuri zaidi kwenye usanifu kuliko 'njeo.' Mara nyngi ni lazima kitu kiwekwe akilini kuwa haiwezekani kutafasiri kitenzi cha Kiebrania kwenda kwenye Kiingereza bila kutumia udhibiti ambao haupo kabisa katika Kiebrania. Waebrania wa mwanzo kamwe hawakufikiria kitendo chawenza kuwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao, lakini walifikilia tu kwenye *utimilifu* yaani.,

kitendo kilichokwisha tendeka, au *kisicho timilifu*, yaani., kama katika njia ya kusonga mbele. Tunaposema kuwa njeo Fulani ya Kiebrania wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao katika Kiingereza, hatumaanishi kuwa mawazo ya Kiebrania ya hicho kama wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao, lakini tu kuwa lazima itafasiliwe katika Kiingereza.

Wakati wa kitendo Waembrania hawakujaribu kuelezea kwa namna yeyote ya muundo wa kuongea kwa maneno (utangulizi na uk.1). kwa angalizo la pili, Sue Groom, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, anatukumbusha sisi, “hakuna namna ya kuweza kujua ikiwa muundo wa wasomi wa sasa wa elimu-maana na uhusiano wa maana katika lugha zilizokufa au kupotea ni taswira ya fikra zao, au lugha zao mama, au maeneo hayo yalikuwepo katika Waembrania wenye hadhi” (uk. 28).

- C. Dhamira (ambazo ni mifanano ilichukuliwa toka kwenye lugha za kimagharibi ya sasa)
  - 1. Imetokea, inaendelea kutokea (NI KAULI ELEKEZI), mara nyingi inatumia njeo WAKATI TIMILIFU au WAKATI UNAOENDELEA ( KAULI ZOTE ENDELEVU ziko katika KAULI ELEKEZI).
  - 2. Itatokea, ingalia tokea (KAULI TEGEMEZEI)
    - a. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU ya wazi
      - 1) Zenye KUFUNGAMANA (likiongezwa herufi h), nafsi ya kwanza KAULI ISIOTIMILIFU ambayo mara nyingi huelezea kutakia heri, hitaji, au kutia moyo (yaani., matendo ya hiari ya mzungumzaji)
      - 2) ASILI NA UFAFANUZI ZAIDI WA NENO (badiliko la ndani), mtu wa tatu KAULI ISIOTIMILIFU (inawezakuwa mtu wa pili katika sentensi kanushi) ambayo mara nyingi inaelezea ombi, ruhusa, maonyo, au ushauri
    - b. Hutumia njeo ya WAKATI TIMILIFU ikiwa na *lu* au *lule*. Miundo hii inafanana na sentensi YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI katika lugha ya Koine ya huko Uyunani. Maelezo yasiyo sahihi (Kishazi chenye kuelezea tamko ndani ya sentensi yenye masharti) yenye kuleta hitimisho lisilo sahihi (Kishazi kikuu ndani ya sentensi yenye masharti).
    - c. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU na muktadha wa *lu*, vile vile maelekezo wa wakati ujao, kuangalia matumizi ya KAULI TEGEMEZEI. Baadhi ya mifano inapatikana kwa J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament* ni Mwa.13:16; Kumb. 1:12; I Fal. 13:8; Zab. 24:3; Isa. 1:18 (kama vile kur. 76-77).
- D. *Waw* – Kinyume chake/yenye matokeo yaliyofuatana/rejeshi. Huu muonekano wa kipekee wa isimu zenye kushughulikia kupanga maneno ya kisarufi ya Kiebrania imeleta mkanganyiko mkubwa kwa miaka mingi. Imetumika kwa namna nyingi mara nyingi ikizingatia juu ya uwasilishaji. Sababu ya mkanganiyiko ni wale wasomi wa mwanzo walikuwa watu wa Ulaya na wakajaribu kutafasiri katika ulelewa wa lugha zao za asili. Na hili lililopoonekana kuwa gumu wakaanza kulaumu lugha ya Kiebrania kuwa ni ya zamani, lugha ya kikale. Lugha za Ulaya ni NJEO (za muda) zinazoegemea kwenye VITENZI. Baadhi ya namna na madokezo ya visarufi yaliainishwa na herufi WAW ambayo iliongezwa kwenye shina la KITENZI TIMILIFU au KITENZI ISIOTIMILIFU. Hii inabadilisha namna ya kitendo kilivyo tazamwa.
  - 1. Katika simulizi za kihistoria VITENZI vinaunganishwa pamoja katika mfuatano vikiwa na mwongozo wa kawaida
  - 2. Kiambishi awali cha *waw* kinaonyesha uhusiano maalum kikiwa na KITENZI kilichopita.
  - 3. Muktadha mpana mara nyingi ni kiini cha uelewa wa mfuatano wa KITENZI. VITENZI vya Kisemiti haviwezi kutathimini utengano. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anaeleza utofauti wa Waembrania katika matumizi ya neno wawkabla ya KAULI TIMILIFU na KAULI ISIOTIMILIFU (kur. 52-53). Kama wazo la msingi la KAULI TIMILIFU ni muda uliopita, kuongezeka kwa neno *waw* mara zote linatenda kwa dhana ya wakati ujao. Hili pia ni kweli kwa KAULI ISIOTIMILIFU ambayo wazo lake la msingi ni la wakati uliopo au wakati ujao; kuongezeka kwa neno *waw* lililowekwa katika wakati uliopita. Hili ni badiliko la muda lisilo la kawaida ambalo linaelezea kungezeka kwa neno *waw*, sio kwenye badiliko la maana yake ya msingi ya njeo yenye. KAULI TIMILIFU ya neno *waw* inatenda kazi vizuri kwenye unabii, wakati KAULI ISIOTIMILIFU ya neno *waw* inatenda vizuri kwenye simulizi (kur. 54,68). Watts anaendeleza

ufafanuzi wake, " kwa ajili ya kuonyesha tofauti iliyopo ya msingi kati ya neno *waw* kiunganishi na neno *waw* linalojirudia, utafasiri ufuatao unatolewa:

- 1) Neno *waw* ambalo ni kiunganishi hutokea mara nyingi kuonyesha ufanano.
- 2) Neno *waw* kwa mfululizo linatokea mara zote kuonyesha mwendelezo. Ni muundo pekee wa neno *waw* unaotumika ukiwa na mfululizo wa kauli isiotimilifu. Uhusiano kati ya kauli zisizotimilifu zilizounganishwa nayo yaweza kuwa ni mfuatano wa muda, matokeo ya kimantiki, sababu za kimantiki, au tofauti za kimantiki. Kwa namna yejete ile kunamfuatano"(uk.103)

E. KITENZIJINA-Kuna aina mbili ya vitenzijina

1. KITENZIJINA CHA MOJA KWA MOJA, chenye "nguvu, kinachojitegemea, kinachoshambulia maelezo yaliyotumika kwa ajili ya matokeo ya kuvutia.....kama kiima, mara nyingi hakina kitensi kilichoandikwa, kitensi 'kuwa' kikiwa kinaeleweka, hakika, neno linabaki kusimama lenyewe wazi,"(J. Wash Watts, *ASurvey of Syntax in the Hebrew Old Testament,*" uk. 92).
2. KITENZIJINA KINACHOJENGA, ambacho "kinahusiana kisarufi kwenye sentensi na vihusishi, viwakilishi milikishi, na uhusiano uliojengeka" (uk.91). J. Weingreen, *A Practical Grammar for Classical Hebrew*, anaelezea hali ya muundo:  
"ikiwa maneno mawili (au zaidi) yanaunganikana kwa karibu ambapo kwa pamoja yanatengeneza wazo moja ambatani, neno lenye kujitegemea (au maneno) yanasemekana kuwa katika hali ya muundo." (uk. 44).

F. VIWAKILISHI VYA KUULIZA

1. Mara zote huonekana kwanza kwenye sentensi.
2. Umuhimu wa kufasiri
  - a. *ha-* haitarajia mwitikio
  - b. *halo'*- mwandishi anategemea jibu la "ndiyo"

KAULI HASI

1. Mara nyingi hujitokeza kabla ya maneno yenye lenyewe yanayo kanushwa.
2. Neno mojawapo kanushi ni *lo'*.
3. Neno *al* lina kidokezo dharura na hutumika likiwa na asili na ufanuzi zaidi wa neno.
4. Neno *lebhilti*, linamaanisha "ili kwamba.....sio" linatumika likiwa na VITENZIJINA.
5. Neno *'en* linatumika likiwa KAULI ENDELEVU.

G. SENTENSI ZENYE MASHARTI

1. Kuna aina nne ya sentensi zenyenye masharti ambazo kimsingi zinafanana katika lugha ya Koine ya huko Ugiriki.
  - a. Kitu Fulani kinaonekana kuwa kikitokea au mawazo kama yaliyyotimilizwa (DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani)
  - b. Kitu Fulani kinyume na ukweli ambacho utimilisho wake hauwezekani (DARAJA LA PILI)
  - c. Kitu fulani ambacho kinawezekana au hata kuonekana kutokea(DARAJA LA TATU)
  - d. Kitu fulani ambacho ni yumkini kutokea, kwa hiyo utimilisho ni agharabu(DARAJA LA NNE)
2. ALAMA ZA VISARUFI
  - a. Vinafikiliwa kuwa kweli au hali iliyopo inatumia KAULI TIMILIFU ELEKEZI au KAULI ENDELEVU na mara zote kishazi kidogo kinatambulishwa kwa
    - 1) *'im*
    - 2) *Ki*
    - 3) *hin* au *hinneh*
  - b. muundu ulio kinyume na ukweli mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU kikiwa na utangulizi wa KIAMBATA *lu* au *lule*
  - c. zaidi muundo wenye uyumkini mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU katika kishazi kidogo, mara zote *'im* au *ki* vinatumika kama kauli ya mwanzo ENDELEVU
  - d. Yumkini muundo mdogo hutumia KAULI TEGEMEZEI ISIOTIMILIFU katika kishazi kidogo na mara zote *'im ni* utambulisho wa KAULI ENDELEVU.

## **VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII**

AB Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman  
ABD Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman  
AKOT Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens  
ANET Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard  
BDB A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs  
IDB The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick  
ISBE International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr  
JB Jerusalem Bible  
JPSOA The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)  
KB The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner  
LAM The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa  
LXX Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970  
MOF A New Translation of the Bible by James Moffatt  
MT Masoretic Hebrew Text  
NAB New American Bible Text  
NASB New American Standard Bible  
NEB New English Bible  
NET NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition  
NRSV New Revised Standard Bible  
NIDOTTE New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren  
NIV New International Version  
NJB New Jerusalem Bible  
OTPG Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith  
REB Revised English Bible  
RSV Revised Standard Version  
SEPT The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970  
TEV Today's English Version from United Bible Societies  
YLT Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young  
ZPBE Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney

# **NENO TOKA KWA MWANDISHI**

## **NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?**

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuvia kuandika ili kuwesha ujumbe wa Mungu uweze kuelewka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanailewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeoyote mtafasiri mionganii mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

### **KANUNI YA KWANZA**

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwalishwa. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuvia wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni-ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

### **KANUNI YA PILI**

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nydinge. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiante na mtizamo mzima kuelekeea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara, kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyeokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nydingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua, kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima.. Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS<sup>4</sup>). Andiko hili iliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.
2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafasiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya

zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.

3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS<sup>4</sup> na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenyе mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley

Juni 27, 1996

Haki Miliki © 2013 [Bible Lessons International](#)

# **MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:**

## **UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA**

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeoyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenyewe tafakuri zenyenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeoyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuaminii uliouunganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenyenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kuitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenyewe kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
  - Wapokeaji wa mwanzo
  - Ujumbe ulioandikwa
  - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo waliosoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenywewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyo simama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliye vuvuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
  - a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
  - b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
  - c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
  - d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
  - e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
  - f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihii zinazotumiwa siku hizi zilizopelekeea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenywewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yaloandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufaishi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

### **III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia**

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kuitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasi wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekeea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

#### **1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji**

- a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti, kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadhairia
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
  - 3) Ufanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
- c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayolezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
- d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu

- 1) Agano la kale
  - a) Simulizi za waebrania
  - b) Mashairi ya waebrania (fasihii za hekima, zaburi)
  - c) Unabii wa ki-Ebrania (lughaa ya mijazo, shairi)
  - d) Alama za siri za ki-sheria
- 2) Agano jipya
  - a) Simulizi (Injili, matendo)
  - b) Hadithi za mafumbo (Injili)
  - c) Barua/nyaraka
  - d) Fasihi za mafunuo

## **2. Mzunguko pili wa usomaji**

- a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
- b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
- c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## **3. Mzunguko wa tatu wa usomaji.**

- a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenye.
- b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
  - 1) Mwandishi
  - 2) Tarehe
  - 3) Wapokeaji
  - 4) Kusudu mahsusii la uandishi
  - 5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
  - 6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
- c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
- d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## **4. Mzunguko wa nne wa usomaji**

- a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
  - 3) Ufanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
  - 1) Misemo ya kujirudia Waefeso 1:6, 12, 14
  - 2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
  - 3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
- c. Taja vipengele vifuatavyo:-
  - 1) Istilahi muhimu
  - 2) Istahili zisizo za kawaida
  - 3) Muundo muhimu wa kisarufi
  - 4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
- d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
  - 1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
    - a) Vitabu vya thiolojia
    - b) Biblia za marejeo
    - c) Itifaki
  - 2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutohakana

- nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuvuwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
- 3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
  - e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
    - 1) Soma biblia
    - 2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mgononi na kamusi
    - 3) Tangulizi za biblia
    - 4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

#### **iv. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.**

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”. Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuvuwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafasiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unaufuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana”lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwangi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

#### **v. Sura ya utafasiri wa kiroho.**

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyeketu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18

"Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale amba Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."

2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:

Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.

3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## **VI. Njia hizi za Fasiri**

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa fasihii umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:*

1. Maeleo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihii imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihii kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maeleo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
  - a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
  - b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
  - c. The New King James Version (NKJV)
  - d. The New Revised Standard Version (NRSV)
  - e. Today's English Version (TEV)
  - f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
  - a. Mazingira ya fasihii

- b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
  - c. Habari za kisarufi
  - d. Usomaji wa neno
  - e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
- a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
  - b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
  - c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
  - d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
- a. Tofauti za mswada
  - b. Maana ya maneno mbadala
  - c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
  - d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA ISAYA

## I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Isaya ananukuliwa mara kwa mara zaidi katika Agano Jipya kuliko manabii wengine (zaidi ya mara 411). Ujumbe wake ulikuwa mojawapo hali ya uungu mmoja ya ujumla isiyoshikiliwa kimsimamo na mpango wa ukombozi kwa uumbaji wote.
1. Mungu mmoja
  2. ulimwengu mmoja
  3. imani moja
- B. Isaya ni kitabu cha kupendeza sana cha kimasih.
1. wana maalum wa Zama Mpya, sura za 7-14
  2. Wimbo wa Mtumishi, 41:1-4; 42:1-9; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12 (yawezekana 61:1-3)
  3. Ufalme wa kimasih ujao (Zama mpya), sura za 56-66. Kuanguka kwa Mwanzo 3 sio neno la mwisho!
- C. E. J. Young, katika *An Introduction to the OT*, anaeleza kwamba:
1. "Kitabu cha Isaya kinachukluliwa kuwa kitabu cha unabii mkuu katika Agano la Kale," ukurasa wa 168.
  2. "Katika manabii wote wa Israeli, Isaya alielewa kwa ukamilifu zaidi ufahamu wa Mungu na mpango wake kwa ajili ya vizazi," ukurasa wa 171.
  3. "Katika utambuzi wa kiroho hapitwi na chochote katika Agano la Kale lote," ukurasa wa 172.

## II. JINA LA KITABU

- A. Kitabu kinaitwa jina kwa jina la msemaji wake wa kinabii.
- B. Jina Lake Linamaanisha "wokovu wa YHWH" au "YHWH anaokoa." Jina la Kiebrania linaloishia na herufi "iah" yanakuwa ni vifupisho vya maneno kwa ajili ya YHWH, kama ilivyo kwa majina mengi ya kingereza ambayo yanaanza na "j" na irabu, mfano Joshua (Yoshua) na Joel (Yoeli).

## III. UTAKATIFUZAJI (CANONIZATION)

- A. Hili ni gombo la kwanza kati ya nne za manabii wa mwisho.
1. Isaya
  2. Yeremia
  3. Ezekiel
  4. Kumi na mbili (manabii wadogo wadogo)
- B. Ilikubalika mapema na kuwekwa kwenye ukamilifu katika maandiko matakatifu ya Israeli.

## IV. AINA YA FASIHI

- A. Ufanisi wa kifasihi wa Isaya unapita manabii wote wa Agano la Kale. Uwezo wake wa kucheza na lugha na ushairi ni wa kushangaza na kuvutia. Kitabu zaidi ni ushairi (angalia Kiambatisho cha kwanza).
- B. Ni ngumu sana kukaa chini na kusoma Isaya yote kwa wakati mmoja. Ni ngumu kuainisha kitabu. Hii ni kwasababu Isaya alikuwa muhubiri, sio tu mwandishi au mhariri. Kitabu chake kinawandikia jumbe zake za kuzungumzwa kwa kipindi kirefu sana cha muda. Hizi zimeunganishwa kwa pamoja wakati mwingine
1. kwa maudhui
  2. kwa mfuatano wa matukio
  3. kwa matukio yanayoathiri Israeli
  4. kwa taratibu za kimila za Mashariki ya Karibu ya kale ambazo ni tofauti na za kwetu
  5. zaidi zsana kwa maneno ya msingi na matumizi ya maneno

## V. UANDISHI

- A. Mitazamo ya Wayahudi juu ya uandishi
1. The Talmud's *Baba Bathra* 15 ilisema kuwa Hezekia na watu wake waliandika (yaani walihariri au kukusanya/kutunga) Isaya, Mithali, Muhubiri, na Wimbo Uliobora.
  2. Ben Sirah, katika *Ecclesiasticus* 49:17-25, kilichoandikwa mnamo mwaka wa 185 k.k., alisema, "Isaya, mwana wa Amozi," alikiandika kitabu (1:1; 12:1; 13:1).
  3. II Nyakati 32:32 inathibitisha maono ya Isaya, kama inavyofanya sambamba katika Wafalme (II Wafalme. 18:19-20:19 anatwambia kuhusu mtu).
    - a. Alitokea katika familia yenyeheshima ya kifalme katika Yerusalem, yawezekana hata mpwa kwa Mfalme Uzzia.
      - (1) baadhi ya ushahidi kwamba "iah" (kama jina linavyoishia), ambalo ni kifupisho cha YHWH, ilifanyika karibia kati ya ufalme
      - (2) Uwezekano wa Isaya kumfikia Mfalme Uzia pia unatusaidia kufahamu muunganiko wa familia yake
      - (3) Angalia Talmud, "Meg." 10b
    - b. Alioa nabii mke (8:3).
      - (1) mwana wa kwanza, "Shear-Jashub," ambayo inamaanisha "mabaki yatakayorudi"
      - (2) mwana wa pili, "Maher-shalal-hash-baz" (8:3), ambayo inamaanisha "kuharakisha mateka,kuharakisha mali"
    - c. Isaya alikuwa na huduma ya kinabii ndefu zaidi kati ya manabii wengine wote wa Agano la Kale. Alikuwa msemaji wa Mungu katika Yuda tokea kipindi cha Yotham (742-735 k.k.) mpaka kile kipindi cha Hezekia (715-687 k.k.) kukiwa na uwezekano wa hata kufikia katika utawala wa Manasse (687-642 k.k.); Manasse yawezekana alikuwa mshauri mwenza kutokea mnamo mwaka 696 k.k.
    - d. Ikiwa II Nyakati 26:22 inamaanisha kwa Isaya, hivyo alikuwa mwandishi rasmi na mtunzaji wa nyaraka za kifalme za wafalme.
    - e. Desturi inasema alichanwa ka msumeno ndani alipopachikwa kwenye gogo (kama vile *Assumption of Isaiah*) wakati wa utawala wa Manase (kama vile Waembrania 11:37).
  4. Moses ben Samuel Ibn Gekatilla, mnamo mwaka wa 110 b.k, anasema kwamba sura za 1-39 ni za Isaya, lakini sura za 40-66 ziliandikwa wakati wa kipindi cha Hekalu la Pili (Kipindi cha Uajemi, 538-430 k.k.).
  5. Ibn Ezra (mnamo mwaka 1092-1167 b.k) ikifuatiwa na uongozi wa Gekatilla's na kukataliwa, au angalau akiulizwa, sura za 40-66 kwa karne ya 8 ya Isaya.
- B. Maoni ya Kizuoni ya kisasa juu ya uandishi
1. Muhtasari mzuri wa kihistoria unapatikana katika R. K. Harrison's *Introduction to the OT*, Eerdmans, 1969.
  2. Mjadala mzuri wa sababu za kiufundi kwa kuelezea waandishi wawili unaweza kupatikana katika S. R. Drivers' *Introduction to the Literature of the OT*, kuchapishwa tena mwaka 1972.
  3. Hakuna Maandiko ya kiebrania au kiyunani (LXX) yaliyowahi kupatikana ambayo yanaonesha mgawanyiko katika sura za 1-39 na 40-66.
    - a. Kuna nafasi ya mstari mwishoni mwa sura ya 33 katika mabaki ya magombo ya bahari ya chumvi. Hii inamaanisha mgawanyiko katika kipengele hiki na sio sura 39. 3
    - b. Kunaonekana kuwa na muundo wa usambamba kati ya 1-33 na 34-66. Huu muundo wa pande mbili umejikita katika siku za mwandishi mwenywewe na alafu siku za usoni, ilikuwa kawaida katika manabii wa kiebrania (kama vile Ezekiel, Daniel, na Zekaria).

4. Uanazuoni wa kisasa hauna umoja wa ukubaliano juu ya waandishi wangapi au wapi kugawa kitabu.
- C. Baadhi ya sababu kwa ajili ya umoja wa Isaya
1. Misamiati ishirini na tano inapatikana katika vipengele vyote viwili vya Isaya ambavyo havipatikani mahali pengine katika Agano la Kale (NIV, utangulizi kwa Isaya, ukurasa wa 1014).
  2. Jina/Cheo “Mtakatifu Pekee wa Israeli” inatokea mara 13 katika sura za 1-39 na mara 14 katika sura za 40-66 na mara sita tu katika vitabu vyote vingine vya Agano la Kale.
  3. Yesu, katika Yohana 12:38,40, ananukuu katika Isa. 53:1 na 6:10 na hivyo kuchukua sifa za wote Isaya.
  4. Vifungu vya habari kutoka Isaya 40-66 vinapewa sifa kwa Isaya katika Mt. 3:3; 8:17; 12:17; Luka 3:4; 4:17; Yohana 1:23; Mdo. 8:28; na Rum. 10:16-20.
  5. Hakuna ushahidi wa kimaandiko kwa mgawanyiko wa kitabu katika sura ya 39 (MT, DSS, au LXX).
  6. Hakuna historia ya nabii mkuu anayetajwa (Deutro-Isaiah) katika karne ya R. K. Harrison, katika *Introduction to the OT*, anatoa maoni yake juu ya somo, “Hoja kutoka katika mtindo wa kifasihi zilikuwa tupu kabisa mwishoni mwa karne ya kumi na nane, lakini katika ufahamu wa maarifa mapana ya lugha za Mashariki ya Karibu ya kale sasa wamedhania nafasi ya juu kidogo kwa umuhimu. Somo kabisa la uangalifu wa mtindo ilikuwa na hali ya kupendeza sana kwa waumini wa nadharia ya uchambuzi wa kifasihi ya Graf-Wellhausen, ambaye hakuona kusitasita katika kila mambo yaliyokuwa yakipitiwa yanayohusiana na mwandishi wa kibiblia, na hata kukataa sehemu ya kiwango chake hicho chake kwasababu ya muundo wa kifasihi na misamiati ya kila sura haikutokea kufa na ufanano. Inavyoonekana haikutokea kwa wale wachunguzi wa mwanzo kwamba ilikuwa inawezekana tu kugeuza baadhi ya dhana za mtindo wa m mwandishi wa kale na matokeo yake usomaji wa makini wa nyaraka ukapewa yeche na kwamba kule kutanguliwa na kukataliwa kwa sehemu au yote ya hicho kiasi ingethibitishwa tu kwa kigezo cha baadhi ya udhibiti mkali wa nje” (ukurasa wa 776).
- D. Baadhi ya sababu kwa uandishi wa mara mbili wa Isaya.
1. Katika sura za 40-66 jina la “Isaya” halitajwi.
  2. Sura za 40-66 haishabihiani na mazingira ya kihistoria ya Isaya.
  3. Kunaonekana kuwepo kwa kuchanganya kwa rejea za Isaya kwa:
    - a. kuvamiwa kwa Ashuru, uhamishoni, na hukumu
    - b. kuvamiwa kwa Babeli, uhamishoni, na hukumu
  4. Kuna baadhi za sababu kwa kuwa na baadhi ya nadharia kadhaa za uandishi.
    - a. kubadilika kwa mazingira ya kihistoria
      - (1) kabla ya kuvamiwa kwa Yuda, 1-39
      - (2) uhamishoni, 40-55
      - (3) Baada ya uhamisho wa Yuda, 56-66
      - (4) katika Isaya 1-39 Hekalu halitawahi kuanguka 40-66 inavyoonekana limekwisha anguka. Mwandishi anaonekana kuwa uhamishoni.
    - b. kubadilika kwa masharti kuwafunua wateule wa Mungu
      - (1) mtoto wa kimasih
      - (2) Mtumishi anayeteseka
      - (3) Israeli kama
        - (a) mke, 50:1
        - (b) mtumishi wa YHWH, 54:17

5. Wanazuoni wa kisasa wenye msimamo mkali

- a. Kauli ya E. J. Young kuhusu sura za 56-66 ni za msaada, "uwezekano mwingine ni ule wa kuongozwa na Roho, nabii zilizokusanywa na mhariri kutoka kwa manabii tofauti tofauti wa shule la Isaya katika maudhui ya msingi ya kipengele hiki," (ukurasa wa 188).
- b. Kauli ya R. K. Harrison, "Waandishi wa sasa wanashikilia msimamo kwamba Isaya kama ilivyo wingi wa maandiko ya kinabii yaishiyo hata leo, yanawakilisha makusanyo ya kauli zilizotolewa nyakati tofauti tofauti na kama vile kazi hizo hazitoi faida ya kuteda kwao kutoka katika ile iliyoruhusiwa na nabii zingine kubwa za Agano la Kale. Katika muunganiko huu ni muhimu kutambua kwamba hoja zimejikita juu ya tofauti za mtindo na uelezeo wa kifasihi ni kwa ghafla inaathiriwa na mtindo huu, kwakuwa makusanyo yanaweza kuchukuliwa kwa namna ya kuwakilisha mtindo mzima wa mwandishi juu ya vipindi vingine tofauti vya shughuli za ubunifu. Kuhesabiwa haki kwa ajili ya kuelezea kazi kama makusanyo katika namna bora ya neno hilo linapewa uzuri kwa mstari wa ufunguzi wa unabii ambao unaundwa kutiwa kichwa kwa kazi, na kuzungumza kibayana juu yam abo mya kiufuno kwa Isaya Mwana wa Amozi alipokea katika maono juu ya Yuda na Yerusalemu katika siku za Uzia, Yotham, Ahazi, na Hezekia. Kama ilivyo kwa makusanyo yote ni ushaidi wa wazi kwamba kitabu kilichojaa uchaguzi tu wa nabii takatifu na mahubiri yanayopatikana, na kuna uwezekana mkubwa kwamba Isaya alitoa nyaraka zaidi kuliko kuliko zilizobaki katika kitabu chake. Asili ya unabii kama makusanyo yanaoneshwa zaidi kwa uwepo wa maelezo ya ziada katika Isa. 2:1 na 13:1, ambayo yanaeza kuwa yamewakilishwa, au kuelekeza kwenye uwepo wa, makusanyo ya mwanzo ya kauli za kinabii," (ukurasa wa 780).

6. Mtindo wa Kifasihi sura za 40-66 ni tofauti na zile za 1-39.

E. Maelezo ya kuhitimisha juu ya uandishi

1. Wanazuoni wa ki-Mungu wanaendelea kukataa kuhusu namna gani kitabu chetu cha Isaya cha Agano la Kale kilikuja kuwa katika muundo wa sasa (kama vile DSS na MT). Msisitizo mkuu lazima uwekwe katika uvuvio wake na uaminifu katika kufunua tabia na makusudi ya YHWH.
2. Lazima tukatae madhanio yoyote ambayo yanakataa ufunuo wa uaminifu kuitia Isaya. Hii pia inajumuisha kukataliwa kwa kabla wa kukataliwa kwa unabii unaotabiriwa na kushushwa kwa Agano la Kale kwa kutojumuishwa kwa hadithi za wakati wa sasa za wanadamu wakati wa sasa.

VI. TAREHE

A. Isaya ni sehemu ya manabii wa karne ya 8.

1. Yona, Amosi, na Hosea katika Ufalme wa Kaskazini (Israeli), wakati wa Utawala wa Yeroboamu II (786-640 k.k.)
2. Isaya na Mika katika ufalme wa Kusini (Yuda)

B. Alizaliwa mnamo mwaka 760 k.k na alitwa rasmi katika huduma ya kinabii mnamo mwaka 742 k.k. katika mwaka ambao Uzia alikufa (6:1). Uzia pia anaitwa Azaria (783-742 k.k.).

C. Isaya alikuwa na huduma kutoka siku za mwishoni mwa Uzia (783-742 k.k.) kuitia Yotham (742-735 k.k.), Ahazi (735-715 k.k.), Hezekia (715-687 k.k.), na katika utawala wa Manase (687-642 k.k.) kwasababu Isaya anatabiri/anaandika kifo cha Sanakarebu katika 37:38 (yaani 681 k.k.) D. R. K Harrison anasema kwamba kitabu ni makusanyo ya maandiko ya manabii na mahubiri ya miaka

mingi kupitia. Mwishowe ilikusanywa na kuhaririwa baada ya kifo cha nabii mnamo mwaka wa 630 k.k.

VII. MAZINGIRA YA KIHISTORIA YA MANABII WA KARNE YA NANE

A. Nyaraka za kibiblia zinapatikana katika

1. II Wafalme 14:3-17:6
2. II Nyakati 25-28
3. Amosi
4. Yona
5. Hosea
6. Isaya
7. Mika

B. Muhtasari rahisi kabisa wa hali ya ibada za sanamu kati ya watu wa Mungu inaweza kuonekana katika Hosea.

1. 2:16, "Hawataniita Mimi tena Baali"
2. 4:12-14, ". . . binti wanafanya ukahaba . . ."
3. 4:17, "Efraimu amejiunga na sanamu; mwacheni"
4. 13:2 "wanadamu wanabusu ndama!" (ibada)

C. Mazingira ya Kijamii

1. Ulikuwa ni muda wa kufanikiwa kiuchumi na kupanuka kijeshi kwa wote Israeli na Yuda. Hatahivyo mafanikio haya yalikuwa yenye faida tu kwa tabaka la matajiri. Maskini walikuwa wamenyonywa na kudharauliwa. Ilikuwa inaonekama kama "maisha duni na kuuwawa" yalifanyika sanamu!
2. Ustahimilivu wa kijamii na mali za wote Israeli na Yuda inahusiana na visababishi kadhaa.
  - a. Utawala mrefu na wenye mafanikio wa Yeroboamu II (786-746 k.k.) katika Kaskazini na Uzia (783-742 k.k.) huko kusini
  - b. Kushindwa kwa Ashuru wa Shamu Adad-Nirari III katika 802 k.k.
  - c. Kukosekana kwa mgogoro kati ya Israeli na Yuda
  - d. Utozwaji kodi na unyonyaji wa njia za kibashara kutokea kaskazini mpaka kusini kupitia daraja la nchi kavu la Palestina kulisababisha ukuaji wa ghafla wa kiuchumi, hata starehe kwa matajiri
3. Ille "Ostraca ya Samaria," ambayo inawekwa katika tarehe wakati wa kipindi cha Yeroboamu II, inaonekana kuashiria mpangilio wa kiutawala na utaratibu wa kitaasisi kama wa Suleimani. Hii inathibitisha kupanuka kwa uwazi kati ya "walio nacho" na "wasionacho."
4. Kukosekana kwa ukweli wa matajiri ni wazi unachukuliwa kaika Amosi ambaye anaitwa "nabii wa haki ya jamii." Rushwa ya kimahakama na kufanywa uongo kwa uzito wa kibashara ni mifano mizuri miwili ya kutendwa vibaya kwa kle kilichozoleka inavyoonekana katika wote Israeli na Yuda. D. mazingira ya kidini
  1. Ulikuwa ni muda wa shughuli nyingi za kidini za nje lakini imani ya kweli kidogo sana. Ibada ya Uzao wa Kanaani ilikuwa imeunganishwa katika dini ya Israeli. Watu walikuwa waabudu sanamu lakini waliita dini ya YHWH. Mwenendo wa watu wa Mungu kuelekea muunganiko wa kisiasa ulikuwa umewajumuisha katika ibada ya kipagani na shughuli.
  2. Ibada ya Sanamu ya Israeli inatajwa katika II Wafalme 17:7-18.
    - a. Katika mstari wa 8 walifuatisha namna ya ibada ya Wakanaani.
      - (1) Ibada ya ustawi (kama vile Mambo ya Walawi 18:22-23)
        - (a) sehemu za juu, mstari 9, 10, 11

- (b) nguzo takatifu (Baali), mistari ya 10, 16
- (c) Asherim, mstari wa 16, hivi vilikuwa viwakilishi vya mbao za Masuria wa kike wa Baali. Zilikuwa aidha nyama zilivofanywa kwa ndama au miti iliyo hai.(2) ulozi, mstari wa 17. Hii ilishutumiwa katika Mambo ya Walawi 19-20 na Kumbu kumbu la Torati 18.
- b. Katika mstari wa 16 waliendelea kuabudu ndama wa dhahabu wawili, wakiashiria YHWH, waliowekwa katika Dani na Betheli kwa Yeroboamu I (I Wafalme 12:28-29).
  - c. Mstari wa 16 waliabudu miungu ya anga ya Babeli:jua, mwezi, nyota na mkusanyiko wa sayari na vitu vya anga.
  - d. Mstai wa18 waliabudu mungu moto wa ustawi wa-Foinike, *Molech*, kwa kuwatoa sadaka watoto (kama vile Mambo ya Walawi 18:21; 20:2-5). Tendo hili linaitwa *molech*; halikuwa jina la mungu.
3. Ibada ya Baali (kama vile W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, ukurasa wa 82 na kuendelea)
    - a. Chanzo bora kabisa cha ki-akiolojia ni "Ba'al Epic kutoka Ugarit ." (Hadithi ya Baali kutoka Ugarit)
      - (1) Inamuelezea Baali kama mungu wa majira anayekufa na kuinuka. Alishindwa na Mot na kufungiwa kuzimu. Maisha na uhai wote ulikwisha. Lakini akisaidiwa na mungu mke (*Anat*), anainuka na kumshinda Mot kila majira ya kipupwe. Alikuwa mungu wa ustawi aliyekuwa akiabudiwa kwa miujiza ya kuiga iga.
      - (2) Alikuwa akijulikana pia kama Hadad.
    - b. *EI* aliкуwa ni mungu mkuu wa miungu ya Wakanaani, lakini umaarufu wa Baali uliteka nafasi yake.
    - c. Israeli aliкуwa amehamasishwa zaidi na hali ya kuabudu Baali kupitia Yezebeli ambaye ambaye aliкуwa Mfalme wa binti wa Tiro. Alichaguliwa na Omri kwa ajili ya kijana wake, Ahabu.
    - d. Katika Israeli aliкуwa akiabudiwa katika maeneo ya sehemu za nyumbani. Alikuwa akiwakilishwa na jiwe lililoinuliwa. Suria wake, Ashera, anawakilishwa na nguzo za kuchonga ikiwakilisha mti wa uzima
  4. Vyanzo kadhaa na aina za ibada za sanamu vinatajwa.
    - a. nguzo ya dhahabu huko Betheli na Dan waliokuwa wamepangwa na Yeroboamu I kumwabudu YHWH.
    - b. Kuabudu mungu wa ustawi wa Tiro na mungu wa kike katika eneo la maeneo ya juu
    - c. Kuabudu miungu kwa umuhimu kulihusishwa katika muungano wa kisiasa wa siku hiyo
- D. Muhtasari mfupi wa kuvamiwa kwa Ashuru na Babeli wakati wa karne ya nane ambayo iliathiri Palestina.
1. Manabii wane wa karne ya nane walikuwa wakijihuisha wakati wa kuinuka kwa ufalme wa Hedekeli-Frati wa Ashuru. Mungu angetumia taifa hili katili kuhukumu watu wake, na hasa Israeli.
    - a. Tukio la kibayana lilikuwa mageuzi ya muungano wa kisiasa na kijeshi kwa muungano wa Yordani ulio julikana kama "Syro-Ephramatic League" (735 k.k.). Shamu na Israeli walijaribu kulazimisha Yuda kuungana nao dhidi ya Ashuru. Badala yake Ahazi alituma barua kwa Ashuru kwa ajili ya msaada. Mfalme wa kwanza mwenye nguvu wa Ashuru, Tiglath-Pileser III (745-727 k.k.), aliiitikia changamoto ya kijeshi na kuvamia Shamu.

- b. Baadaye mfalme wa Ashuru aliypandikizwa Hoshea (732-722 k.k.), katika Israeli pia aliasi, akikata shauri kwa Misri. Shalmaneser V (727-722 k.k.) alivamia Misri tena. Alikufa kabla ya Israeli hajakaliwa na kutiishwa lakini aliyemfuatia kimadaraka, Sargon II (722-705 k.k.), aliutwaa mji mkuu Samaria mnamo mwaka 722 k.k. Ashuru ilisafirisha zaidi za wana wa Israeli 27,000 katika tukio hili kama Tiglath-Pileser alivyo peleka uhamishoni maelfu hapo kabla mnamo mwaka 732 k.k.
- 2. Baada ya kifo cha Ahazi (735-715 k.k.) muungano mwingine wa kijeshi ulitengenezwa nan chi za ukanda wa Yordani na Misri dhidi ya Ashuru (714-711 k.k.). Ulikuwa ukijulikana kama "Uasi wa Ashdodi." Miji mingi ya Kiyudea iliharibiwa wakati Ashuru alipovamia tena. Mwanzoni Hezekia alisaidia muungano huu lakini baadaye aliondoa msaada wake.
- 3. Hatahivyo, muungano mwingine tena ulijaribu kuchukua fursa ya kifo cha mfalme mwenye nguvu wa Ashuru Sargon II, mnamo mwaka 705 k.k., pamoja na uasi mwingi mwingine uliotokea ambao ulitokea katika ufalme wote wa kiashuru.
  - a. Hezekia alishiriki kikamilifu uasi huu. Katika ufahamu wa changamoto hii Senakarebu (705-681 k.k.) alivamia (701 k.k.) Palestina na akafanya hema karibu na jiji la Yerusalem (II Wafalme 18-19; Isaya 36-39), lakini jeshi lake kimiujiza liliharibiwa na Mungu.
  - b. Kumekuwapo na maswali kati ya wanazuoni kama ni kwa kiasi gani na mara ngapi Senakeribu alivamia (mfano John Bright ana uvamizi mmoja mnamo 701 k.k. na nyingine yawezekana mnamo 688 k.k., kama vile *The History of Israel*, ukurasa wa 270).
  - c. Hezekia aliachwa kama mabaki ya Kiashuru lakini kwasababu ya udhihirishwaji wa kiburi chake (39:1-8). Yerusalem aliangukia kwa Nebukadneza mnamo mwaka 587-586 k.k.
- 4. Isaya kibayana alitabiri urejesho wa watu wa Mungu chini ya Koreshi II, mtawala wa Uajemi Kati (41:2-4; 44:28; 45:1; 56:11). Ninawi (mji mkuu wa Ashuru) ulianguka mnamo mwaka wa 612 k.k. kwa Babeli, lakini mji wa Babeli ulianguka mnamo mwaka wa 539 k.k. kwa Jeshi la Koreshi. Mnamo mwaka 538 k.k. Koreshi alitoa tamko kwamba watu wote waliopelekwa uhamishoni ikijumuisha Wayahudi wangerudishwa nyumbani. Hata alitoa fedha kutoka katika hazina yake kwa ajili ya kujenga upya mahekalu ya kitaifa. Alikuwa mtu anayehusudu uchawi na aliyetaka miungu yote kumpa kibali yeche.

## VIII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

- A. Ainisho Fupi
  - 1. Sura za 1-39, nabii na siku zake
  - 2. Sura za 40-66 (au yawezekana 40-55 na 56-66), zama mpya
- B. Sura za 1-39, mazingira ya kihistoria za siku za Isaya (kabla ya uhamisho)
  - 1. Sura za 1-6, chini ya mfalme Uzia na Yotham
  - 2. Sura za 7-14, chini ya mfalme Ahazi
  - 3. Sura za 15-39, chini ya mfalme Hezekia (Sura za 36-39 ni sambamba na II Wafalme 18:13-20:19)
- C. Sura za 40-66, wakati wa uhamisho na kipindi kabla ya uhamisho, ni aina za ufalme wa baadaye
  - 1. Kama sura za 1-39 zianaaksi mahubiri ya Isaya na ni dhahiri uwasilishaji wa kinywa, sura za 40-55 zinaaksi mazingira mapya. Hukumu ya Mungu imekuja na sasa marejesho ni maudhui makubwa. Kuna pia mguso wa kimuundo kwamba sura hizi hazihusiano sana na uwasilishwaji wa kinywa kama uwasilishwaji wa uandishi.
  - 2. Sura za 1-39 kidhahiri zinahusu tishio la kiashuru na tishio na kibabeli katika aina, kibayana katika sura za 13-14, 21 na 39. Sura za 40-55 zinahusiana na kipindi cha kiajemi na urejeshwaji wa watu wa Mungu kwenye nchi ya Ahadi.

3. Sura za baadaye za Isaya, 56-66, ni za matukio ya siku za mwisho zikitumia sitiari za kihistoria kutoka Mashariki ya Karibu ya kale kuonesha matukio ya mbele ya ibada za kiujumla kwa imani moja kwa YHWH.
- D. Ugumu wa uaninishaji wa Isaya

1. Wanazuoni wengi wa kisasa wanagawa kitabu katika angalau sehemu mbili: sura za 1-39 na 40- 66. R. K. Harrison: sura za 1-33 na 34-66 kwa sababu ya uwazi katika maandiko ya DSS. Huu mgawanyo wa wazi wa DSS kati ya sura za 33 na 34 imetuinulia maoni kwamba Isaya alizalishwa na wafuasi wake katika juzu hizi mbili. W. H. Brownlee amependekeza kwamba juzu mbili ziakisiiane katika muundo.

	<b>Juzu 1</b>	<b>Juzu 2</b>
Sura za1-5	kuharibiwa na kurejeshwa	sura za 34-35
sura za 6-8	Historia za kimaisha	sura za 36-40
sura za 9-12	wakala wa Baraka za kimungu na hukumu	sura za 41-45
Sura za 13-23	ibada dhidi ya nguvu ya kigeni	sura za 46-48
Sura za 24-27	ukomboziwa kiujumla na kukombolewa kwa Israeli	sura za 49-55
sura za 28-31	mahubiri ya kimaadili	sura za 56-59
sura za 32-33	kurejeshwa kwa taifa	sura za 60-66

2. Baadhi ya shabaha ya maainisho ktika mazingira ya kihistoria, wakati wengine wakiweka shabaha katika maudhui ya kimasih

	<b>NIV</b>	<b>Leupold</b>
sura za 7-12	“Unabii ulioanzishwa na Waarmu ana tishio la Wana wa Israeli dhidi ya Yuda”	“Kitabu cha Immanuel”
sura za 28-33	“Ole Sita: Tano za kukoswa uaminifu wa Israeli na moja juu ya Ashuru”	“Kitabu cha Sayuni” (Jiwe Kuu la Pembeni)

3. Baadhi ya mifano ya kutoeleweka kwa vipengele vya kifasihi (sura za 1-12)

- a. Muainisho wa sura za 1-12 na E. Y. Young, kurasa za 211-214
  - (1) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda na Yerusalem
    - (a) 1:1-31 mashitaka makuu
    - (b) 2:1-4:6 utawala wa Masihi na hukumu juu ya watu
    - (c) 5:1-30 kushamiri kwa uovu wa Yuda
    - (d) 6:1-13 maono ya Isaya juu ya Bwana
    - (e) 7:1-12:6 Unabii unaozungumzwa wakati wa utawala wa Ahazi
  - (2) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda na Yerusalem
    - (a) 1:1-31 mashitaka makuu
    - (b) 2:1-4:6 utawala wa Masihi na hukumu juu ya watu
    - (c) 5:1-30 kushamiri kwa uovu wa Yuda
    - (d) 6:1-13 maono ya Isaya juu ya Bwana
    - (e) 7:1-12:6 Unabii unaozungumzwa wakati wa utawala wa Ahazi
- b. Muainisho wa sura za 1-12 na R. K. Harrison, kurasa wa 764
  - (1) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 1-5
  - (2) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 6-8
  - (3) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 9-12
- c. Muainisho wa sura 1-12 na Toleo la NIV Study Bible, kurasa wa 1016
  - (1) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 1-5
  - (2) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 6-8
  - (3) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda, sura ya 9-12

- ii. Nidhamu ya Bwana kwa Yuda (2:6-4:1)
- iii. Kurejeshwa kwa Sayuni (4:2-6)
- (c) hukumu ya taifa na uhamisho (sura ya 5)
- (d) agizo la pekee la Isaya (sura ya 6)
- (2) Sura za 7-12
  - (a) Ahazi anaonywa asiogope Waaramu na muungano wa Wana wa Israeli (sura ya 7)
  - (b) mwana wa Isaya na mwana wa Daudi (8:1-9:7)
  - (c) Hukumu dhidi ya Israeli (9:8-10:4)
  - (d) Ufalme wa kiashuru na ufalme wa kidaudi (10:5-12:6)
    - i. kuharibiwa kwa kiashuru (10:5-34)
    - ii. kuanzishwa kwa ufalme wa kiadaudi (sura za 11)
    - iii. wimbo wa furaha kwa ajili ya ukombozi (sura ya 12)

**IX. KWELI KUU**

- A. Isaya alishikilia Yuda katika uaminifu kwenye agano la ki-Daudi (II Samueli 7), Lakini pia alirejerea kwenye kusudi la asili la agano la ki-Ibrahimu (Mwanzo 12:1-3), ambalo lilikuwa ni Mungu kuchagua Israeli ili kuchagua ulimwengu (yaani Kutoka 19:5-6). Ni kwa kushangaza kiasi gani huku kutawala kwa ujumla kwa YHWH namna kulivyo. Mungu sio tu kwamba atarejesha Israeli, bali atapanua mpango wake wa ukombozi kwa ulimwengu mzima!
- B. Isaya kibayana alitabiri uamsho wa matukio ya kiulimwengu katika siku zake ye ye mwenyewe na katika siku za baadaye (hivyo hivyo Mika). Ufalme huu ni mtakatifu nani wa ulimwengu wote (vile vile kwa Mika). Hivi vyote ni vipengele vya uungu mmoja vitakatifu vya kiukombozi.
- C. Isaya kwa uwazi anaonesha utupu na ujinga wa watu wa Mungu katika kutumaini katika nguvu za kibinadamu, ulimwengu ulioanguka. Ukombozi utakuja kutokea kwa YHWH tu!
- D. Isaya anafunua tabia tatu zenye nguvu sana za mpango wa Mungu za ukombozi.
  - 1. Masihi ajaye
  - 2. Masihi kama mtumishi mwenye kuteseka
  - 3. Utawala wa kiulimwengu wa Masihi

# ISAYA 1

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Uasi wa Watu wa Mungu		Andiko juu ya		Jina
1:1-3	1:1	1:1	1:1	1:11
(2-3)	Udharimu wa Yuda	Mtiririko wa kwanza wa mafunuo	Anawakaripia watu wake	Dhidi ya watu Wasio na Shukrani
		1:2-4 (2-3)	1:2-31 (2-3)	1:2-9 (2-3)
1:4 (4)	(4)		1:4-6	
1:5 (5-6)	1:5-9 (5-6)	(5-6)		
1:7-9 (7-9)	(7-9)	(7-9)	1:7-9	
Mungu Alikuwa Ametosheka				Dhidi ya Unafiki
1:10-15 (10-15)	1:10-17 (10-11) (12-15)	(10-17)	1:10-14	1:19-20 (10)
			1:15-17	(11-17)
1:16-17 (16-17)	(16-17)			
Hebu na Tufikiri				
1:18-20 (18-20)	1:18-20 (18-20)	(18-20)	1:18-20	(18-20)
Sayuni Kutenda Mabaya, Kukombolewa	Mji Uliopotoka		Mji wenyе Dhambi	Ombolezo la Yerusalamu
1:21-23 (21-23)	1:21-23 (21-23)	(21-23)	1:21-23	1:21-28 (21)
				(22-23)
1:24-26	1:24-31		1:24-26	

(24-26)	(24-26)	(25-26)	(24)
1:27-31 (27-31)	(27-31)	(27-31)	(25)
1:27-28			(26)
			Dhidi ya Miji iiyotengwa
1:29-31		1:29-31 (29-31)	

\*Ingawa hazikuvuviwa, mgawanyo wa aya ni ufunguo wa uelewa na ukifuata kusudio la mwandishi wa awali. Kila tafasiri ya kisasa imegawanyika na kuifupisha aya. Kila aya ina mada kuu, ukweli kuu, au wazo kuu. Kila toleo linafupisha mada hiyo katika njia yake tofauti. Jinsi unavyosoma andiko, jiulize mwenyewe ni tafasiri ipi inafaa kwenye uelewa wako juu ya somo na mgawanyo wa aya.

Katika kila sura lazima tusome biblia kwanza na kujaribu kutambua somo lake (aya), kwa hiyo linganisha uelewa wetu na matoleo ya kisasa. Mara tu unapoelewa kusudi la mwandishi wa awali kwa kufuata mantiki na uwasilishaji wake tunaweza kuielewa biblia. Mwandishi tu wa awali ndiye aliyevuviwa-wasomaji hawana mamlaka ya kubadiri au kuufanya marekebisho ujumbe. Wasomaji wa biblia wana majukumu ya kutumia ukweli uliovuviwa katika siku zao na maisha yao. Angalia kuwa maandiko yote ya kiufundi na vifupisho vimeelezea kwa upana katika Kiambatisho cha Kwanza, cha Pili na cha Tatu.

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama sehemu /kipengele cha utangulizi)**

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu nimwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

## **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kwa uhalisia manabii walitumia miundo ya viwango vitatu vyikisha jumbe zao.
1. Kwa namna ya kimahakama (kama vile mist. ya 2,18)
2. Nyimbo za maombolezo (kama vile mist. ya 24-26)
3. Ufunuo wa ahadi

B. Inastaajabisha kwamba wito walsaya umenukuiliwa katika sura ya 6. Kuna muhutasari pekee wa utangulizi katika mst. wa1. Hata hivyo, huu muhutasari mfupi unaeleza kuhusu urefu na kipindi cha huduma ya Isaya. Mara nyingi ni matoleo pekee yaliyochaguliwa, ushahiri, na yale yanayohusiana na Isaya ndiyo yaliyonukuliwa hapa, aidha na yeze mwenyewe baadaye katika huduma yake ama na wafiasi wake baada ya kifo chake. R. K. Harrison anakiita kitabu hiki mkusanyiko wa matukio mbali mbali.

1. Sura ya 1 inaweza kuwa muhutasari wa kitabu kizima. Jumbe zile zile zinarudiwa kupitiamandaiko ya Isaya. Toleo lililo mashuhuri zaidi ni lile la dhambi za Yuda la
  1. upotokaji wa agano la kimataifa
  2. kuamini katika mwendelezo wa desturi na liturgia
  3. ukosefu wa haki za kijamii
  4. ibada za sanamu

Matokeo ya Mambo ya Walawi 26 naKumbukumbu la Torati 28 lazima yaza matunda ikiwa Mungu ni mkweli wa neno lake! Matokeo ya dhambi inayojulikana ni halisi kama zilivyo ahadi za upendo wa YHWH, namna ya kujali na ulinzi. Haya yako katika pande mbili za agano moja! Kumbuka makusudi yahukumu yalikuwa ni kwa urejesho wa ushirika wa karibu, kama ule wa Bustani ya Edeni kabla ya Anguko, mfano wa Mungu kuharibiwa!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 1:1-3

<sup>1</sup>Haya ni maono ya Isaya, mwana wa Amozi, aliyoyaona katika habari za Yuda na Yerusalem, siku za Uzia na Yothamu na Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda.

<sup>2</sup>Sikieni, enyi mbingu, tega sikio, Ee nchi,  
kwa maana Bwana amenena;  
Nimewalisha watoto na kuwalea, nao wameniasi.

<sup>3</sup>Ng'ombe amjua bwana wake,  
Na punda ajua kibanda cha bwana wake;  
Bali Israeli hajui, watu wangu hawafikiri.

**1:1 “maono”** Neno hili (BDB 302) linatumika katika maana ya “ujumbe wa kiufunuo” (kama vile 29:7; Mik. 3:6). Haya maneno “maono” na “ndoto” yanafanana katika 29:7 kama vile Dan. 7:1). Mara nyingi ndoto hutokeea usiku na maono hutokeea nyakati zote mchana na usiku. Neno hilil linaonekana kueleza juu ya mabadiliko ya hali ya matokeo ambapo Mungu, kupitia stiari, nahau, navitu vinavyoonekana, huzungumza juu ya ufunuo maalum. Kweli hizi ni za ki-Ungu, si mwanadamu. Huenda Isaya uliziumba jumbe, lakini maudhui yalitoka kwa Mungu! Ni vigumu kueleza kuhusu mwonekano wa uvuvio, lakini matokeo ni yak i-Ungu, jumbe za kimamlaka. Hapa, katika muktadha huu wa mstari huu wa ufunguzi, hili neno linatumika mara chache wa ujumbe walsaya (kama vile 2:1; 13:1; Amosi 1:1; Mika 1:1; Hab. 1:1).

▣“Isaya” Hili neno (BDB 447) linamaanisha “YHWH anaokoa” ama “wokovu wa YHWH” (hakuna KITENZI). Neno “iah” linapoitokeza mwishoni mwa jina la Kiebrania, linamaanisha uaminifu na pia kusimama kwa ajili ya jina la agano la Mungu, YHWH (kama vile Kut. 3:14).

### MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

#### A. E/(BDB 42, KB 48)

1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, “kuwa shupavu” au “kuwa mwenye nguvu” (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).

2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra), akaitwa “baba wa miungu” na “bwana wa mbinguni”
  3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
    - a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sanaBDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
    - b. *El-Roi* (“Mungu aonaye” au “Mungu ajifunuaye Mwenyewe” BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
    - c. *El-Shaddai* (“Mungu Mkuu” au “Mungu mwenye huruma zote” au “Mungu wa mlima”), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
    - d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
    - e. *El-Berit* (Mungu wa Agano”), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46
  4. *El* inalinganishwa na
    - a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
    - b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, “Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
    - c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
    - d. “wivu” katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
    - e. “rehema” katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
    - f. “mkuu na mzuri” katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
    - g. “maarifa” katika I Sam. 2:3
    - h. “kimbilio langu” katika II Sam. 22:33
    - i. “mlipa kisasi wangu” katika II Sam. 22:48
    - j. “mtakatifu” katika Isa. 5:16
    - k. “muweza” katika Isa. 10:21
    - l. “wokovu wangu” katika Isa. 12:2
    - m. “mkuu na mwenye nguvu” katika Yer. 32:18
    - n. “anayepatiliza: katika Yer. 51:56
  5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El*, *Elohim*, *YHWH*, kurudiwa)
- B. *Elyon*(BDB 751, KB 832)
1. Maana yake ya msingi ni “juu,” “aliyetukuzwa,” au “kuinuliwa” (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; 18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
  2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
    - a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
    - b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
    - c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
    - d. *El* - Hes. 24:16
    - e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya “Mungu aliye Juu”) katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
  3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
    - a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
    - b. Balaamu, Hes. 24:15
    - c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
    - d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)
- C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
  2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahim walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
  3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)

4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104).

Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.

6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitensi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
7. Inashangaza kwamba jina lililozoleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
  - a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa “wingi wa ukuu,” mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
  - b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7).
  - c. Inawezekana hata inaksi ufunuo wa Agano Jipywa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipywa Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
  - a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
  - b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).

Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.

2. Katika Mwanzo 4:26 inasema “wanadamu wakaanza kuliiitia jina la BWANA” (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utanii maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
  - a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, “kuonesha upendo wa dhati”
  - b. kutoka katika mzizi wa kiarabu “kupuliza” (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
  - c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) “kuzungumza”
  - d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha “Yeye anayetosheleza,” au “yeye anaye anzisha”
  - e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* “Yeye ambaye yupo,” au “Yeye aliyepo sasa” (katika namna ya wakati ujao, “Yeye atakayekuwako”)
  - f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* “yeye asababishaye kuwa”
  - g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania “kuishi” (mfano Mwanzo. 3:20), maana “Mungu mmoja tu aishiye milele”
  - h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, “nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa” au “nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa” (kama vile J. Wash Watts, A

- Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
- (1) *Yah* (mfano Hallelu – *yah*, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
  - (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
  - (3) *Yo* (majina mfano Joel)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lilitofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania “mmiliki,” “Mkuu,” “mume,” “bwana”—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka “bwana.” Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
  4. Kama ilivyo kwaEl, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusositiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
    - a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwanzo. 22:14
    - b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal HALI YA KUENDELEA*, Kutoka. 15:26
    - c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651, Kutoka. 17:15
    - d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel HALI YA KUENDELEA*), Kut. 31:13
    - e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
    - f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
    - g. *YHWH - Ro’l* (YHWH ni mchungaji wangu,BDB 217 & 944, *Qal HALI YA KUENDELEA*), Zab. 23:1
    - h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
    - i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa,BDB 217 & 1027), Eze. 48:35

▣“Amozi” Mtu huyu (BDB 55) anatajwa katika uhusiano na Isaya pekee. Mzizi wa msingi unamaanisha “uweza,” “nguvu,” ama “ukuu.”

▣“aliyoyaona” KITENZI hiki, (חִזְׁוָעַן BDB 302, KB 301, *Qalcha KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kinatokana na mzizi ule ule, “muonaji” (חִזְׁוָעַן) na ni sawa na neno “mwonaji” (חִזְׁוָעַן). Hiki kinatumika kwa kurudiwa rudiwa katika Isaya (kama vile Mika 1:1).16

▣“Uzia” Tamaduni zinasema kwamba Isaya alikuwa na uhusiano na Uzia (“YHWH ndiye nguvu yangu”), Suala hili haliwezi kushikiliwa, bali ushahidi unagusia katika uelekeo huu. Huyu Mfalme aliyemcha Mungu alikufa kwa ugonjwa wa ukoma mnamo 742 K.K. Pia anajulikana katika Biblia kama Amazia (“YHWH ndiye msaada wangu”). Ili kuvifahamu vipindi maalumu vyawafalme hawa na uhusiano waona wafalme wa Israeli, angalia Kiambatisho cha Nne.

**1:2“Sikieni, enyi mbingu, tega sikio, Ee nchi”**Hizi KAULI mbiliSHURUTISHIzinatokana na mizizi tofauti tofauti,lakini maana yake ya kimsingi ni ile ile.

1. *sikieni*, BDB 1033, KB 1570, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile mist. 10,15,19; 6:8,9 (mara mbili),10, n.k.
2. *tega sikio*, BDB 24, KB 27, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile 1:2,10; 8:9; 28:23; 32:9; n.k.

Hii ilikuwa njia ya kiishara ya kuwaogofya watu wake katika kuutambua uasi wao. YHWH alianzisha mahakama ya malalamiko dhidi ya watu wake! Ungazi huu unafanana na Mika 1:2, Isaya nabii wa sasa wa Yudea.

Jambo hili linaumba hatua ya sura ya 2, ambayo pia ni kigungu cha kimahakama. Mungu anazungumza na watu wake kupia malalamiko. Hii ni mbinu ya kawaida ya kifasihi katika upande wa Manabii (yaani, Mik. 6:6-8; Yer. 2: 1 na Kuendelea; Rum. 8:3 na kuendelea). Hii ni hatua ya kawaida katika Agano la Kale ya kutoa ushahidi wa aina mbili kwa ajili ya kuthibitisha ushuhuda (kama vile Kumb. 4:26; 30:19; 31:28; 32:1; Zab. 50:4).

■ “**mbingu**” (BDB 1029) hapa neno hili linarejelea eneo la angani juu ya uso wa dunia ambao ulikuwa sehemu ya uumbaji (kama vile Mwanzo 1). Katika muktadha huu neno hili halirejelei juu ya “makao ya Mungu.”

■ “**kwa maana Bwana amenena**” Hili ni jina la agano la Uungu wa Israeli. Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:1.

■ “**Nimewalisha watoto na kuwalea**” Hapa tena Mungu anaelezwa katika lugha ya kibinadamu, maneno ya kifamiliakama mzazi mwenye upendo wa Hosea 11:1-4 (pia tambua Kut. 4:22; Kumb. 32:6; Yer. 3:4; 31:9, angalia Mada Maalum katika 6:1). Ufanano bora zaidi wa mwanadamu kuitambua tabia na matendo ya YHWH ni (1) mzazi; (2) mwenza wa ndoa; na (3) mkombozi wa karibu.

■ “**wameniasi**” Hiki KITENZI (BDB 833, KB 981, *Qal cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kinamaanisha tendaji, wailiyopotoka, waliofunguliwa macho, uhasi binafsi (kama vile 1:28; 43:27; 46:8; 53:12; 59:13; 66:24).

■ “**mimi**” Dhambi ni upotofu wa awali dhidi ya Mungu (kama vile. 39:9; II Sam. 12:13; Zab. 41:4; 51:4). Norman H. Snaith, *The Distinctive Ideas of the Old Testament*, anasema “(manabii) walifikiri juu ya hili (dhambi) kama uasi kuliko kosa” (uk. 65). Dhambi ni kule kuinajisi sura na ufananao wa Mungu ndani ya mwanadamu (kama vile Mwa. 1:26,27). Mungu aliutaka ulimwengu umjue yeye! Alimchagua (Abramu), mtu wa nyumba ya (Yakobo), na taifa (Israeli) kujifunua kwa wanadamu wote (angalia Mada Maalum katika 1:3), lakini Israeli alishindwa kuuakisi ufanano na huruma ya YHWH. Hawa walimwasi “waliofunguliwa macho.” Asili ya dhambi ni “mimi,” zaidi yangu kwa gharama yo yote!

**1:3** Mstari huu umekuwa ukijulikana vema,mithali ya kiutamaduni.Hata wanyama walio kimya hawaung’ati mkono unaowalisha, bali Yuda anafanya hivyo!

■ “**Bali Israeli hajui**” Hiki KITENZI “hajui” (BDB 393, KB 390, *Qalcha KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) hakimaanishi dhana ya jambo hili, bali ufahamu binafsi wa mtu (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5). Israeli hawakumtambua muumbaji wao, mwokozi,na mlinzi wao kwa sababu hawakusikiliza (kama vile 5:12,13; 6:9-13; 30:9).

■ “**watu wangu**” Hii ni lugha ya kiagano (kama vile Hosea 1-3,11). Yapaswa kukumbukwa kwamba katika Agano la Kale, uteule ni uanzilishi Mungu wa awali wa uchaguzi wa Ibrahim na Israeli. Kuna jukumu sawa baada ya uanzilishi wa uchaguzi wa Mungu unaojulikana kama agano. Huu unahuishisha jukumu la pande zote.

## MADA MAALUM: UPENDELEO WA KIINJILISTI WA BOB

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Jer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walioumbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaoanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza

- kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israeli. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahimu, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
  - a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
  - b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
  - c. Mika 4:1-3
  - d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihirishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya limejikita shabaha yake juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumaini utaendelea kuchukua muda kusoma [Mada Maalum:Kwanini Ahadi za kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti sana na Ahadi za kiagano za Agano Jipya](#). Unaweza ukaipata mtandaoni katika wavuti [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

## **MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAJAALIWA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA**

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya

linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kупingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inabitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile.Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu mvutano wa kitheolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyigi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwengine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jazi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihilisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhumu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kitheolojiaya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibowi kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maneneo na punguza kwa mwengine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

■“**hawafikirii**” Hiki KITENZI (BDB 106, KB 122, *Hithpalel* cha WAKATI ULIO TIMILIFU) katika shina hili kinamaanisha “kuwa katika umakini.” Tatizo lilikuwa ni ukosefu wa maarifa, lakini kutokuwa tayari kutii (kama vile 6:9,10; Kumb. 4:6; 32:29). Hawa walilizika kwa udharimu wa udini (kaida za utamaduni wa Israeli), lakini pasipo kuisha maisha muhimu ya mrefu ya imani, toba, na tumaini binafsi! Asili ya kweli inafafanuliwa katika 5:18-23, hasa.Mst wa 21 (kama vile Mika 4:12). Hawa walikuwa watu wa agano kwa jina lao, lakini si watu wa agano ndani ya mioyo yao (kama vile Rum.2:28-29; 9:6)!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:4**

**“Ole wake,**  
**taifa lenye dhambi,**  
**watu wanaochukua mzigo wa uovu,**  
**wazao wa watenda mabaya, watoto wanaoharibu;**  
         **wamemwacha Bwana,**  
**wamemdharau yeye aliye Mtakatifu wa Israeli,**  
**wamefarakana naye na kurudi nyuma.**

**1:4“Ole wake”**Hiki KIHISISHI (BDB 222) kinatanbulisha semi za hukumu (kama vile 10:5; 17:12; 28:1; 29:15; 31:1; 45:9,10; Amosi 5:18; 6:1).

▣ “taifa lenye dhambi” Neno la kawaida “lenye dhambi” (BDB 306, KB 305, *Qalya KAULI TENDAJI ENDELEVU*) linamaanisha “kukosa chapa.” Hili neno “taifa” nigoy (BDB 156). Neno hili mara nyigi linatumika kwa Mataifa, lakini linaweza kurejelea juu ya Israeli (kama vile Kut. 19:5-6). Jina Israeli lilimaanisha kuwa taifa takatifu (kama vile Kut. 19:5-6), bado aliendelea kuwa taifa lenye dhambi. Ni mafunuo ya marajio ya namna gani!

▣ “**watu wanaochukua mzigo wa uovu**” Hili neno “kubebeshwa mizigo” ama “zito” (BDB 458) ni stiari nyingine ya kuifafanua dhambi kama mzigo juu ya mgongo wa mwanadamu (kama vile Mt. 11:28). Maneno yote ya Kiebrania yenye kuizungumzia dhambi yanahusiana na kutotii ama kubebeshwa mizigo (yaani, kukusa chapa) kwa sababu neno la Kiebrania lenye kumaanisha haki linalotumika kwa Mungu linamaanisha “pima kamba” ama “rula.”

## MADA MAALUM: HAKI

“Haki” ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana. Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinazelezwa kama “halali” au “haki” (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsia ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsia ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na “mafunjo ya mto” ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii anatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu. Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wawili halisi walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21). Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko, hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliiko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya aagano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, mahakama ya haki)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kusingiziwa)
3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii wa mtindo wa maisha
4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, iliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo. Dhana inaitwa “haki kwa neema kupitia imani” (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani “mwenye haki” katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa rabbi aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiqlilotumika* katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu,

Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano(tazama Mada Maalumu: Agano). YWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipyta ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipyta (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana). Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utotauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Klingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufulo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoleka]).

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenyewe kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu wa Edeni. Biblia inaanza kati Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipyta vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
  - a. Warumi 3:26
  - b. 2 Wathesalonike 1:5-6
  - c. 2 Timotheo 4:8
  - d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
  - a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
  - b. Mathayo 27:19
  - c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki. Mambo ya Walawi 19:2
  - a. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
  - a. Warumi 3:21-31
  - b. Warumi 4
  - c. Warumi 5:6-11
  - d. Wagalatia 3:6-14
5. Iliyotolewa na Mungu
  - a. Warumi 3:24; 6:23
  - b. 1 Wakorintho 1:30
  - c. Waefeso 2:8-9
6. Iliyopokelewa kwa imani
  - a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
  - b. 2 Wakorintho 5:7,21
7. kupitia matendo ya Mwana
  - a. Warumi 5:21
  - b. 2 Wakorintho 5:21
  - c. Wafilipi 2:6-11
8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki

- a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
  - b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
  - c. Waefeso 1:4; 2:10
  - d. 1 Timotheo 6:11
  - e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
  - f. 1 Yohana 3:7
  - g. 1 Petro 2:24
9. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
- a. Matendo 17:31
  - b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenyе dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

1. agizo la Mungu
2. zawadi ya Mungu
3. tendo la Kristo
4. maisha yapasayo kuyaishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudу, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana Naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohona 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na Barua Zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa na kipengele cha kuachiliwa. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
2. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Kathoriki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

**“wazao wa watenda mabaya, watoto wanaoharibu”** Kifungu hiki kinaoneka kuhusiana na Kut. 20:5 ambapo maisha ya uovu mzazi yalimwambukiza watoto. Tambua ufanano uliopo.

1. taifa, mst. wa 4
2. wenyе kuchukua mzigo wa uovu, mst. wa 4
3. watu watenda mabaya, mst. wa 4
4. watoto wanao haribu, mst. wa 4

Pia tambua vishazi vyenye ufanano vinavyofuatia.

1. wamemwacha (BDB 736, KB 806, *Qal yaKAULI YA WAKATI TIMILIFU*) Bwana
2. wamemdharau (BDB 610, KB 658, *Piel ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) ye ye aliye Mtakatifu wa Israeli
3. wamefarakana (BDB 266, KB 267, *Niphchal ya Kauli ya wakati timilifu*) naye

Yote haya yanazungumzia matendo ya wenyе ufahamu, lakini wenyе kuasi, watu wa agano (tambua idadi ya maneno ya picha fauti za dhambi). Kwa matendo na chaguzi zao wanamkataa YHWH! Haya mashina ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU yanadokeza juu ya mtazamo ulioimarishwa!

Iliwapasa watu hawa kubarikiwa “uzao” (BDB 282) wa Ibrahim (kama vile Mwa. 12:7; 13:15,16;16:10; 22:17,18; 24:7; 26:3,4,24; 28:13,14; 32:12), lakini wamekuwa “uzao” wa watenda mabaya! Ni huzuni iliyoje ya uhusiano na fursa uliyopotea (kama vile Luka 12:48)!

■ “aliye Mtakatifu wa Israeli” Hili ni ji a lenye upendeo kwa Uungu katika Isaya (kama vile 1:4; 5:19; 10:17,20; 12:6;17:7; 29:19,23; 30:11,12,15; 31:1; 37:23; pia katika sehemu ya pili ya Isaya, 40:25; 41:14,16,20; 43:3,14,15; 45:11; 47:4; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9,14). Kwa kuwa yeye ni “mtakatifu,” yawapasa watu watu wake kuwa watakatifu (kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; I Pet. 1:16).

Hili, jina katika maana hii, linaeleza kutowezekana kwa mvutano wadhambi, watu walioanguka kukubaliana kujenga kiwango cha taifa takatifu. Agano la Musa halikuwa na uwezekano wa kutunzwa (kama vile Matendo ya amaitume 15; Wagalatia 3; Waebrania). Agano la Kale ilikuwa njia ya kuonyesha kutowezekana kwamwanadamu kuyakubalia maagizo ya Mungu, bado aliendelea kuwa nao, kuwa kwao, akiwaandaakwa ajili ya kukabiliana na hali yao ya anguko. Yeye hakuyaashushusha maagizo yake, bali aliyatoa kupitia Masihi wake. Agano Jipy (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) ni agano la imani na toba, si utendaji wa mwanadamu, inagawa linaangukia katika Ufanano na Kristo (kama vile Yakobo 2:14-26). Mungu huwapenda watu wanaoiakisi tabia yake kwa mataifa (kama vile Mt. 5:48).

## MADA MAALUM : UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO

Kitabu cha Agano jipy kinadai kwamba wenyе dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumto mtu hatiani).

Lakini Agano Jipy pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, niutakaso.

Mwitikio wa Awali	Ufanano na Kristo Endelevu
Matendo 26:18	Warumi 6:19
Warumi 15:16	2 Kor. 7:1
1 Wakorintho 1:2-3; 6:11	Waefeso 1:4; 2:10
2 Wathesalonike 2:13	1 Wathesalonike 3:13; 4:3-4,7, 5:2
Waebrania 2:11, 10:10,14; 13:12	1Timoteo 2:15 2 Timoteo 2:21
2 Petro 1:2	1 Petro 1:15-16 Waebrania 12:14

■ “wamefarakana naye na kurudi nyuma” Kiuhalsia kifungu hiki ni “wamerudi nyuma” (BDB 30, kama vile 44:25). Tungeweza kusema, “kwa kukusudia wamerudi nyuma na kumwacha” (kama vile mst. wa 2).

## ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:5-6

<sup>5</sup>Mbona mnataka kupigwa hata sasa,  
hata mkazidi kuasi?  
Kichwa chote ni kigonjwa,  
moyo wote umezimia.  
<sup>6</sup>Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake;  
bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha;  
havikufungwa,  
havikuzongwa-zongwa,  
wala havikulainishwa kwa mafuta.

**1:5** Hapa watu wa Mungu wanabainishwa kama watu wenye udhaifu wa kimwili. Huu ni mfano mzuri wa ugonjwa wa kimwili unaosimama kama stiari ya dhambi (kama vile 53:4-6; Zab. 103:3; Hos.5:13). Uponyajinwa kimwili si sehemu ya ahadi ya upatanisho, bali ndiyo msamaha kamili na timilifu! Dhambi na maradhi ni mambo yanayohusiana (kama vile Yohana9:2; Yakobo 5:5).

▣“**Mbona**” Matoleo ya NKJV, NRSV, TEV, NIV, RSV, na ASV kwa usahihin kabisa yanalitafsri neno hili kama “kwa nini” (BDB 752 II), kifungu ambacho kianatazamia katika sababu ya kuendelea kwa uasi huu. “Kadri mnavyoendea katika uasi wenu” KITENZI hiki (BDB 414, KB 418, *Hiphilcha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kinadokeza juu ya jambo lililorudiwa, mtazamo wa uasi unoendelea dhidi ya mapenzi sahihi ya Mungu yaliyofunuliwa.

▣“**Kichwa chote. . . moyo wote**” Ufananao huu unadokeza juu ya juu yamwili wote wa mtu (mawazo, makusudi, na matendo). Kifungu cha pili pia kinapatikana katika Yer.8:18 na Omb. 1:22, ambacho kinaonyesha kuwa hiimiliwa nahau ya kawaida.

**1:6**“**jeraha**” Hii NOMINO (BDB 1071) inadokeza “utilifu,” “ukosefu wa hatia,” ama “uaminifu.” Katika muktadha huu nommino hii inatenda kazi kama stiari ya

1. maisha pasipo uaminifu (kama vile Mwa. 20:5,6; Zab. 78:72; 101:2)
2. mtu asiye na afya njema (kama vile Zab. 38:3)

Hili kumbusho la mst.wa6 linalezea juu ya hatua za kitabibu.

1. kubandua
2. iliyofungwa kwa kitambaa maalum
3. iliyolainishwa kwa mafuta (mafuta kama tiba, kama vile Luka 10:34; Yakobo 5:14)

Mtu (ama taifa) ambaye kidonda chake hakikusafishwa vema na kitambaa kilichofungwa kisingekuwa na matumaini ya kupona (kama vile Hosea 6:1).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:7-9

- <sup>7</sup>Nchi yenu ni ukiwa;  
miji yenu imeteketezwa kwa moto;  
nchi yenu, wageni wameila mbele ya macho yenu;  
nayo ni ukiwa, kana kwamba imeangamizwa na wageni.  
<sup>8</sup>Na binti Sayuni ameachwa kama kibanda katika shamba la mizabibu,  
kama kipenu katika shamba la matango,  
kama mji uliohusuriwa.  
<sup>9</sup>Kama Bwana wa majeshi asingalituachia mabaki machache sana,  
tungalikuwa kama Sodoma,  
tungalifanana na Gomora.

**1:7** Maelezo hayayanaakisi tendo la uhamisho, huenda ni mashambulizi ya Kiashuru mnamo 701 K.K. na ujio wa Israeli mnamo 723 K.K. au huenda ujio wa watu wa Babeli katika Yuda mnamo 586 K.K. Kumbuka kitabu cha Isaya, ni mkusanyiko wa vifungu mbalimbali vyta maneno. Muundo barabara wa kihistoriahauelezwi. Mara kwa mara mashairi yake yanaweza kurejerea matoleo tofauti tofauti. Haya pia yanaweza kuwa yameundwa kwa ajili ya utata uliokusudiwa wa Kumbukumbu 28.



<b>NASB, NKJV</b>	“ <b>wageni</b> ”
<b>NRSV</b>	“ <b>waliokuja</b> ”
<b>TEV, NJB</b>	“ <b>waliotoka nje</b> ”

Hii KAULI YA WAKATI ENDELEVU (BDB 266, KB 267, Qalya KAULI TENDAJI ENDELEVU, mara mbili) inamdokeza mtu mwenye kutoka nyumba tofauti, kabilia, taifa (kama vile 25:2,5; 29:5; 61:5), mara nyingi ni adui wa watu wa agano. YHWH uwahukumu watu wake kwa kuwatumia maadui wa kipagani (kama vile 10:5).

**1:8“binti Sayuni”** Shauku ya mzazi kwa mtoto inaanza katika mst. wa2. Hapa maelezo yanaendelea katika sitiari ambayo itajitokeza tena katika fasihi ya kinabii.

1. binti Sayuni, Isa. 1:8; 10:32; 16:1; 37:22; 52:2; 62:11; Yer. 4:31; 6:23; Omb. 1:6; 2:1,4,8; 2:18; Mik. 4:8,10,13; Zef.3:14; Zek. 2:10; 9:9
2. binti Yeresalemu, Isa. 37:22
3. binti Yuda, Omb. 2:2,5,13,15; Mika 4:8
4. binti Tiro, Zab. 45:12
5. binti Babeli, Zab. 137:8; Isa. 47:1 (binti bikra); Yer. 50:42; 51:33; Zek. 2:7
6. binti wa watu wangu, Isa. 22:4; Yer. 4:11; 6:26; 8:11,19,21,22; 9:1,7; Omb. 2:11; 3:48;4:6,10
7. binti aliye bikra, Isa. 23:12; 37:22; Yer. 14:17; 46:11; Omb. 1:15; 2:13
8. binti ya Misri, Yer. 46:24
9. binti wa Edomu, Omb. 4:21,22
10. binti wa Tarshishi, Isa. 23:10
11. binti wa Wakaldayo, Isa. 47:1,5
12. binti mwaminifui, Yer. 31:22

Mara nyingi ilikuwa ni nahau iliyorejelea makazi ya taifa fulani, mkoaa, au mji.

▣“**kama kipenu katika shamba la matango**” Kifungu hiki kunarejelea juu ya udhaifu, umbo lepesi (kama vile 24:20) ambalo linalochaguliwa wakati wa mavuno kama makazi kwa ajili ya kulinda na kutunza mazao dhidi ya wezi. Pasipo Mungu watu wake hawana ulinzi ama tumaini (kama vile mst. wa 9).

**1:9 “Bwana wa Majeshi”** Angalia Mada Maalum ifuatayo,

### **MADA MAALUM: BWANA WA MAJESHI**

Hili jina la ki-Uungu, "Bwana wa Majeshi" (kama vikele 1 Sam. 1:3,11 kama matumizi ya kwanza ya kuwepo kwa mamia kadhaa) linaundwa na

- A. Jina la Mungu la agano, YHWH. Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu
- B. Neno la kijeshi "majeshi" (BDB 838, KB 994) linaweza kudokeza
  1. malaika kwa ujumla (kama vile Neh. 9:6)
  2. jeshi la malaika wa mbinguni (kama vile 1 Sam. 17:45; Dan. 8:10; Luka 2:13)
  3. kusanyiko la kimalaika (kama vile 1 Fal. 22:19; Dan. 7:10)
  4. watu wa YHWH (kama vile Kut. 12:41, ambayo inaakisi Kut. 3:8,10 kama inavyojejelea juu ya Israeli, kama vile 2 Sam. 7:27)
  5. jeshi la mwanadamu (yaani, Mwa. 21:22,32; Hes. 2:4,6; Amu. 8:6; 9:29)
  6. nuru ya mbinguni wakati wa usiku (yaani, "majeshi," Mwa. 2:1; Isa. 45:12), inafikiriwa kuwa nguvu za kiroho (yaani, Babeli kuabudu jua mwezi na vitu vyote katika jeshi la mbinguni, kama vile Kumb. 4:19; 17:3; 2 Fal. 17:16; 21:3,5; 23:4-5; 2 Nya. 33:3,5; Yer. 8:2; 19:13)
  7. Hili linakuwa jina la YHWH katika Amosi 4:13; 5:27 (likiwa na KIBAINISHI katika Amosi 3:13; 6:14; 9:5 na pasipo KIBAINISHI katika Amosi 5:14,15,16; 6:8; 1 Fal. 19:10,14). Hili liliidokeza mapigano ya YHWH kwa niaba ya Israeli.
  8. Kuna matumizi mahususi katika Yos. 5:14-15 ambayo yanaweza kurejelea kwa Mikaeli, malaika wa kiulinzi kwa Israeli. Jina hili kwa namna fulani lina ufanano na Malaika wa Bwana kama uwakilishi wa Mungu Mwenyewe (huenda kambala ya Kristo kufanya katika umbo la kibinadamu).

■ “asingalituachia mabaki” Kifungu kinarejelea juu ya hukumu kali ya Ashuru na/au uhamisho wa Babali wa watu wa Mungu kutoka katika Nchi ya Ahadi. Hili linadokeza dhana ya “mabaki ya uaminifu” wa waumini (kama vile 10:20-22; 11:11,16; 37:4,31,32; 46:3, angalia Mada Maalum hapao chini), ambao Paulo anawarejelea na kwenda zaidi kwa kuyatazamia na kupanua wigo kwa kuwahusisha Mataifa katika Rum. 9:19-29! Si kila mtu atakayeokolewa!

### **MADA MAALUM : MABAKI, (BDB 984, KB 1375), NAMNA TATU**

Dhana ya Agano la Kale ya kifungu cha "mabaki matakatifu" ni kigezo cha sasacha Manabii (hasa manabii wa karne ya nane na Yeremia). Neno hili linatumika katika maana tatu:

1. wale waliomudu kuishi ndani ya uhamisho (yaani Ezra 9:8,14-15; Neh. 1:2-3; Isa. 10:20-23; 17:4-6; 37:4,31-32; 46:3; Yer. 23:3; 31:7-8; 42:15,19; 44:12,14,28; Mika 2:12; 5:7-8; 7:18; Hag. 1:12-14; 2:2; Zek. 8:6,11-12)
2. wale waliobaki kuwa waaminifu kwa YHWH (yaani, Isa. 4:1-5; 11:11,16; 28:5; Yoeli 2:32; Amosi 5:14-15)
3. wale walio sehemu ya matengenezo mapya ya siku za mwisho na uumbaji mpya (yaani, Amosi 9:11-15; Zek. 8:6)

Ule mfano wa udongo katika Marko 4:1-20 na Mt. 13:1-23, ambao unanukuu Isa. 6:9-10, ni mfano mzuri wa namna Agano Jipya linavyolielewa neno hili (pia nukuu Rum. 9:6 katika kuirejelea Israeli ya siku za Paulo).

Haya "mabaki" ya Agano Jipya yameundwa na Wayahudi waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:27-29) na Mataifa waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:24-26). Makundi yote yanazungumziwa katika Rum. 9:30-35; 11:11-24,25-32. Kuamini juu ya Israeli si suala la rangi (yaani, Rum. 9:6; 2:18-19), bali kuliamini kundi la wafuasi waaminifu wa mambo mapya wa Mungu, ufunuo kamili katika Yesu. Kulizungumza hili kunaonekana kuwa ni kuyakataa maandiko ya Agano la Kale (yaani, Yer. 31:7-9; Mika 5:7-8) kuhusu taifa la Israeli kuwa mabaki. Tafadhari tazama katika Mada Maalumu yangu: Kwa nini Ahadi za Agano la Agano la Kale Zinaonekana kuwa Tofauti Sana na Ahadi za Agano Jipya? Injili hubadilisha kila kitu!

■ “Sodoma na Gomora” Hili nio dokezo la kihistoria la hukumu ya Mungu iliyonukuliwa katika Mwanzo 18-19.Hii miji ya Wakanaani ilikuja kuwa methali ya pande zote uovu na hukumu ya Mungu ya uovu.

### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 1:10-15**

- <sup>10</sup>Lisikieni neno la Bwana,  
enyi waamuzi wa Sodoma;  
tegeni masikio msikie sheria ya Mungu wetu,  
enyi watu wa Gomora.
- <sup>11</sup>Huu wingi wa sadaka zenu mnavitolea una faida gani?  
Asema Bwana. Nimejaa mafuta ya kafara za kondoo waume,  
na mafuta ya wanyama walionona;  
nami siifurahii damu ya ng'ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume.
- <sup>12</sup>Mjapo ili kuonekana mbele zangu,  
ni nani aliyetaka neno hili mikononi mwenu,  
kuzikanyaga nyua zangu?
- <sup>13</sup>Msilete tena matoleo ya ubatili;  
uvumba ni chukizo kwangu;  
mwezi mpya na sabato, kuita makutano;  
siyawezi maovu hayo na makutano ya ibada.
- <sup>14</sup>Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa,  
nafsi yangu yazichukia;  
mambo hayo yanilemea;  
nimechoka kuyachukua.

<sup>15</sup> Nanyi mkunjuapo mikono yenu,  
nitaficha macho yangu nisiwaone; naam,  
mwombapo maombi mengi,  
sitasikia; mikono yenu imejaa damu.

**1:10-15** Ulinzi walsraeli dhidi ya uthibiti wa Mungu wa mist. ya 2-6 ndiyo ucha Mungu wake!

**1:10** “**Lisikieni. . .tegeni sikio**” Hizi KAULI SHURTISHI mbili za mst. wa2 zinarudiwa.

▣“**enyi watu wa Sodoma . . . enyi watu wa Gomora**” Yuda ni kama Sodoma na Gomora, wote ni viongozi na watu waliopotoka kimaadili. Kifungu hiki ni dosari inayoshtua kwa watu wa agano, kama ilivyokuwaya mst. wa4.26

□

NASB	“ <b>sheria</b> ”
NKJV	“ <b>matakwa</b> ”
NRSV, TEV	“ <b>fundisho</b> ”

Hili nineno Torati (BDB 435). Tambua uwezekano wa maana nyinginezo. Katika muktadha huuhili linarejea juu ya (1) Maandiko; (2) mahubiri ya manabii; au (3) mafundisho ya makuhani. Hawa waliyafahamu mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, lakini walichagua kutoyafuata.

**1:11** “**Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani**” Yapaswa kukumbukwa, hili si shambulizi juu ya sadaka kama vile, bali ni mtazamo unaohusu namna watu wanavyotoa sadaka zao (kama vile 29:13; Hos. 6:6; Amosi 5:21-27; Mika. 6:6-8). Desturi zinaweza kuwa na maana ikiwa litafuatana na mtazamo wa haki kumhusu Mungu (kama vile Zab. 50). Tazama *Hard Sayings of the Bible*, kr. 207-208, 274-275.

▣“**Nimejaa**” Hiki KITENZI (BDB 959, KB 1302, Qalya KAULI TIMILIFU) kinachomaanishakukaushwa ama kujazwa.

▣“**kafara**” Kifungu hiki kinarejelea juu ya sadaka za jumla za kuteketezwa ambazo ziliashiria kujitoa moja kwa moja au kwa jumla kwa Mungu.

▣“**mafuta ya kondoo dume**” Kifungu hiki kinarejelea juu ya dhabihu ambapo sehemu pekee ya mnyama animal (matumbo ya ndani ya mwanakondoo) ilipotolewa sadaka madhabahuni nan a sehemu zingine zilizobaki alipewa kuhani ama aliyetoa sadaka kula chakula kama ushirika na Mungu na nyumba yake, marafiki, na majirani. Nyama ya mnyama mkubwa isingetumzwa na ilipaswa kuliwa haraka.

▣“**nami siifurahii**” Hiki KITENZI (BDB 342, KB 339, Qalcha KAULI ISIO TIMILIFU) kinadokeza ukubalifu wa sadaka za YHWH. Nahau ya mara kwa mara ilikuwa “marufu mazuri” (kama vile Mwa. 8:21; Kut. 29:18,25). Hata hivyo, YHWH alizikataa ibada za watu hawa (kama vile mist. ya 10-15).

**1:12** “**kuonekana mbele zangu**” Kifungu hiki kinaurejelea uwepo wa mtu Hemani/Hekaluni (yaani, Kut. 23:17). Walikuwa hawaji kwa ajili ya ibada ya kweli, bali kwa ajili ya utaratibu wa liturujia!

**1:13** “**matoleo ya ubatili**” Neno hili (BDB 996) linamaanisha “tupu,” “bure,” “pasipo cho chote.” Hii inaweza kurejelea juu ya

1. ibada ya sanamu (Yona 2:8; Zab. 31:6)
2. sadaka (hapa)
3. watu wenye uovu (Isa. 5:18)
4. matumizi ya jina la Mungu (Kut. 20:17; Kumb. 5:11; Zab. 139:20)
5. maneno ya uongo (Isa. 59:4)

■ “uvumba ni chukizo kwangu” Hili neno “uvumba” (BDB 882) linamaanisha “kile kinachopaa.” Kwa hiyo, neno hili linaweza kurejelea juu ya

1. sadaka za moshi
2. manukato ya uvumba (mara nyingi mchanganyiko wa manukato unaowekwa juu ya sadaka) amamoshi unaotoka katika madhabahu ya vumba mbele ye pazia la hema/hekalu

Haya ni maneno yenye nguvu! Yananikumbusha juu ya mahubiri ya Hekalu la Yeremia<sup>16</sup> ya Yeremia 7. Taratibu za ibada naliturjia zimeondoa toba na imani. Hawa walikuwa vipofu na viziwi (kama vile Isa. 6:9-10). Wameumba miungu, lakini wameikataa imani ya kweli (kama vile II Tim. 3:5). Jambo linalohuzunisha ni kwamba wanafikiri kuwa walikuwa sawa na Mungu! Walifikiri kuwa walikuwa watu wake! Walikuwa kinyume, kama zilivyo dini nyingi, ilivyo kawaida, wanadini makini katika kila enzi.

Hili neno “chukizo” (“BDB 1072) kwa Mara ya kwanza linatumika katika Kumbukumbu la Torati, Mithali, na Ezekieli. Hili linaeleza juu ya mwitikio wa Mungu kwa vitu vingi.

1. kujamiina kwa jinsia moja, Law. 18:22
2. dhambi nyingine za kujamiihana, Law. 18:26,27,29,30
3. ibada ya sanamu, Kumb. 7:25,26; 12:31;14:3; 17:4; 27:15; 32:16; II Fal. 16:3; 23:13; Yer. 32:35
4. sadaka za wanyama walio na dosari, Kumb. 17:1
5. matendo yaliyo sirini, Kumb. 18:9,12
6. kuchanganya mavazi ya kijinsia, Kumb. 22:5
7. ujira wa kahaba, Kumb. 23:18; I Fal. 14:24
8. kuolewa tena baada ya taraka, Kumb. 24:4
9. dhuruma za kibashara, Kumb. 25:16; Mit. 11:1; 20:10,23
10. mtu kaidi, Mit. 3:32; 6:16; 8:7; 11:20; 12:22; 15:26; Yer. 7:10
11. sadaka za mtu mbaya, Mit. 15:8,9; 21:27
12. majivuno, Mit. 16:5
13. viongozi wasio tenda haki, Mit. 16:12
14. apotoshaye haki, Mit. 17:15
15. matoleo ya ubatili pasipo maisha ya imani, Isa. 1:13

■ “Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa” Kumbuka Waembrania walitumia mwzi kusoma kalenda. Kila sikukuu ilikuwa muhimu na kila mwezi mpya (kama vile Hes. 28:11-15; II Fal. 4:23; Isa.66:23) ulikuwa na nafasi Fulani ya kidini pamoja na sikukuu tatu kwa mwaka zilizoteuliwa katika torato ya Musa (kama vile Kut. 23:14-17; 34:18-26; Mambo ya Walawi 23; Kumb. 16:1-17).

**1:14** Sarufi ya Kiebrania hapa inaharibiwa kwa sababu ya isia kubwa zinazoelezwa nalsaya badala ya Mungu. VITENZI vitatu vya kwanza vyote ni KAULI TIMILIFU (vimekamilika).

**1:15 “mkunjuaapo mikono yenu”** Tambua kwamba “kukunjua mikono” kifungu hiki kiko katika herufi za mlazo, wambapo inaanishwa kuwa hakiko katika andiko la Kiebrania. Kukunjua mikono (kama vile Kut. 9:29,33; I Fal. 8:38,54; II Nya. 6:12) na kuinua macho juu mbinguni (kama vile Yohana 11:41; 17:1) ilikuwa mikao ya kawaida kwa Waembrania kwa ajili ya maombi. Mungu anakataa kusikiliza (kama vile. 8:17; 54:8; 59:2; Kumb. 31:17; Yer. 11:11; Eze.8:18) maombi ya watenda dhambi wa Yudea katika nyakati zao za mahitaji kwa sababu walikuwa wakija kwake wakati wa maombi kama walivyomwendea kwa sadaka. Ambapo,sadaka nyingi hazikukubalika kwaYHWH, kwa vyuo vyote waliomba maombi mengi pasipo na imani ya ndani na toba.

■ “mikono yenu imejaa damu” Hii inarejelea juu ya mauaji ya kutisha na au mauaji ya kukusudia kwa wasi na hatia.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:16-17

<sup>16</sup>Jiosheni, jitakaseni;

ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu;

acheni kutenda mabaya;

<sup>17</sup>jifunzeni kutenda mema;

**takeni hukumu na haki;  
wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake;  
mteteeni mjane.**

**1:16-17** Nabii anaeleza moyo waYHWH katika mtiririko wa amri zifuatazo.

1. Jiosheni, BDB 934, KB 1220, *Qal* ya KAULISHURUTISHI
2. jitakaseni, BDB 269, KB 269, *Hithpael* ya KAULISHURUTISHI
3. ondoeni uovu wote, BDB 693, KB 747, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
4. achene kutenda mabaya, BDB 292, KB 292, *Qal* ya KAULISHURUTISHI
5. jifunzeni kutenda mema, BDB 540, KB 531, *Qal* ya KAULISHURUTISHI
6. takeni hukumu na haki, BDB 205, KB 233, *Qal* ya KAULI SHUTUTISHI
7. wasaidieni walioonewa, BDB 80, KB 97, *Pielya* SHURUTISHI (huenda “msaidieni anayenyenyeswa”)
8. mpatieni yatima haki yake, BDB 1047, KB 1622, *Qal* ya KAULISHURUTISHI
9. mteteeni mjane, BDB 936, KB 1224, *Qalya* KAULISHURUTISHI

Tambua kwamba mapenzi ya YHWH yanaelezwa katika namna ya matendo yahuruma ya haki ya mtu (kama vile Mt. 25:31-46). Mtu hawezi kuwa na haki ya inayohusiana na Mungu na wakati anamchukia na kumkataa ndugu yake wa agano.

Mara nyingi kuna mkanganyiko kuhusu imani ya kibiblia. Hii inajikita katika tabia ya Mungu (yaani, neema, hurumajau katika matendo ya waumin? Na jibu ni “ndiyo”! Mfano mzuri wa uwiano wa agano (mara nyingi huanzishwa na Mungu) unalinganisha na Eze. 18:31 pamoja naEze. 36:26-27 (pia angaliaEfe. 2:8-9,10)!

## **MADA MAALUM: FASIHI YA KIMASHARIKI (ukinzani wa kibiblia)**

1. Utambuzi huu wa ndani (yaani, kwamba Biblia ni kitabu cha mashariki, si kitabu cha magharibi) umekuwa msaada zaidi kwangu binafsi kama mtu anayependa na kuiamini Biblia kama Neno la Mungu. Katika kujaribu kuichukulia Biblia kwa umakini inakuwa dhahiri kwamba maandiko tofauti tofauti yanaifunua kweli katika uteuzi, si katika namna za kimfumo. Andiko moja lililovuvuviwa haliwezi kufuta ama kushusha andiko lingine lililovuvuviwa! Kweli huja katika kuyafahamu Maandiko (Maandiko yote, si sehemu tu, iliyovuvuviwa, kama vile 2 Tim. 3:16-17), si kunukuu kifungu kimoja (kuhakiki maandiko)!
2. Kweli nyingi za kibiblia (fasihi ya mashariki) zinawasilishwa katika mtindo wa lahaja ufanano wa kimafumbo (kumbuka waandishi wa Agano Jipy, isipokuwa Luka, ni wanafikra wa Kiebrania, walioandika katika Kiebrania cha kawaida. Fasihi ya Hekima na Fasihi ya Ushahiri inawasilisha kweli katika mfuatano. Huu ufanano kinzani hutenda kazi kama fumbo. Huu uigaji wa ufanano hutenda kazi kama ufanano wa vifungu). Kwa kiasi fulani yote kwa ni ya kweli kwa usawa! Mafumbo haya ni ya kimaumivu kwa mapokeo ya kimadhehebu yaliyotunzwa kwa upendo mkubwa!
  - a. Maamuzi ya kabla dhidi ya utashi huru wa mwanadamu
  - b. Ulinzi wa mwamini dhidi ya hitaji la ustahimilivu(angalia Mada Maalum: Uatahimilivu)
  - c. Dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
  - d. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama Mwanadamu
  - e. Yesu kuwa sawa na Baba dhidi ya Yesu aliyejekuwa mtii kwa Baba
  - f. Biblia kama neno la Mungu dhidi ya uandishi wa kibinadamu
  - g. Kutotenda dhambi (ukamilifu, kama vile Warumi 6) dhidi ya kutenda dhambi kidogo
  - h. Kuhesabiwa haki kwa mwanzo moja kwa moja dhidi ya utakaso endelevu (angalia Mada Maalum: Utakaso)
  - i. Kuhesabiwa haki kwa imani (Warumi 4) dhidi ya kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo (kama vile Yakobo 2:14-26)
  - j. Uhuru wa Mkristo (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33) dhidi ya wajibu wa Mkristo (kama vile Gal. 5:16-21; Efe. 4:1)

- k. Mungu apitaye uwezo wa kibinadamu dhidi ya uwepo wake wa kila mahali
- l. Hatimaye Mungu asiyejulikana dhidi ya Mungu ajulikanaye katika maandiko na ndani ya Kristo.
- m. Sitiari nyingi za Paulo kwa ajili ya wokovu
  - (1) Uasilihaji (kupanga mtoto/kumtwaa)
  - (2) Utakaso
  - (3) kuhesabiwa haki
  - (4) Kukombolewa
  - (5) Kutukuza
  - (6) Majaaliwa
  - (7) Upatanisho
- n. Ufalme wa Mungu uliopo dhidi ya ule utakaotimia mbeleni
- o. Toba kama zawadi ya Mungu (kama vile Mdo.11:18; Rum. 2:4; 2 Tim. 2:25) dhidi ya toba kama mwitikio wa lazima kwa ajili ya wokovu (kama vile Marko 1:15; Mdo. 20:21)
- p. Agano la Kale ni la kudumu dhidi ya Agano la Kale limekwisha kupita na ni batili na utupu (kama vile Mt. 3:17-19 dhidi ya Mt. 5:21-48; Warumi 7 dhidi ya Wagalatia 3)
- q. Waamini ni watumishi/watumwa au wana/warithi

**1:17**

<b>NASB</b>	<b>“wasaidieni walio onewa”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“msaidieni anaye nyanyaswa”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“waachilieni wanaao wanaoneawa”</b>
<b>TEV</b>	<b>“wasaidieni wanaonyanyaswa”</b>
<b>NJB</b>	<b>“dhibitini machafuko”</b>
<b>LXX</b>	<b>“mkomboeni yule anayetendewa visivyo”</b>
<b>Peshitta</b>	<b>“tendeni mema kwa yule anayeonewa”</b>

Toleo la MT lina kifungu “watendeeni haki wanaeonewa” (kinapatikana hapa tu), lakini KITENZI hiki kinamaanisha “kuiitwa mbarikiwa” au “kutenda haki” (BDB 80, KB 97, *Piel YA KAULI SHURUTISHI*), ambacho hakiendani na muktadha. Huenda ni mabadiliko bora ya silabi za toleo la MT kutokana na kifungu “wanaoneea” hadi “wale wanaonewa” (yaani, *Qal ya KAULI ENDELEVU*, BDB 330).

▣“yatima. . .mjane”Joz hii ni alama ya wale wote wanaonewa na wasiowezeshwa kijamii (kama vile Kut. 22:21-22; Kumb. 24:17,19,20,21; Ayibu 24:3; Ps. 68:5;Yer. 7:6; Omb. 5:3; Eze. 22:7; Zek. 7:10;Mal. 3:5). Hivi vigungu vinatumika kwa pamoja mara nyingi kataiaka Kumbukumbu la Torati kama shamirisho la utunzaji binafsi na umakini YHWH (yaani, Kumb. 10:18; Zab. 10:14,18; 68:5; Yer. 49:11).Kundi hili hasa niutawala wa mfalme katika ANE ambao ulikuwa na jukumu la kuhakikisha uwepo wa haki yakijamii na usawa!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:18-20**

<sup>18</sup>Haya, njoni, tusemezane,  
asema Bwana.  
Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana,  
zitakuwa nyeupe kama theluji;  
zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.  
<sup>19</sup>Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi;  
<sup>20</sup>bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga;  
maana kinywa cha Bwana kimenena haya.

**1:18-20 “Haya, njoni, tusemezane”**Nabii ametumia fasihi ya stiari ya “kipengele cha kimahakama” (yaaani, YHWH anawatarakisha watu wake) kuufikisha ujumbe wa jukumu binafsi na matokeo yake! Huu ufanano wa mazungumzo ya ndani ya mahakama unaendelea. YHWH yu tayari kuwasamehe watu wake ikiwa watu wake

watatubu na kutii! Ikiwa watakataae, matokeo ya kulitii agano yatajitokeza (Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 28). Kuna VITENZI viwili vinatueleza juu ya mwaliko wa Mungu kwa Yuda kusemezana kupertia Hukumu ya Kiungu.

1. Haya, njoni (hasa “tembea,” “enenda”), BDB 229, KB 246, *Qal ya KAULI SHURUTISHI*
2. tusemezane, BDB 406, KB 410, *Niphal ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO*, kama vile Ayubu 23:7

Tambua matokeo ikiwa (kwanzakishazi cha “kama”, mst. wa 19) yanatokea kwa usahihhi (yaani, makubaliano na kutii, mst. wa 19).

1. dhambai iliyosamehewa (kutoka nyekundu sana hadi kuwa nyeupe kama theruji)
2. dhambi iliyosamehewa (kutoka nyekundu sana hadi kuwa kama sufu)
3. kula mema ya nchi

Tambua matokeo (ya pili kishazi “kama”) ikiwa watakataa (BDB 549, KB 540, *Pielya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) na uasi (BDB 598, KB 632, *Qalya KAULI TIMILIFU*). Hawa wataangamizwa (BDB 37, KB 46, *Qaya KAULI TENDEWA YA WAKATI USIO TILIFU*).

Inatia shauku kwamba Mungu Mkuu anawaita watu wa agano lake kuitikia kwa usahihhi. Hii ni siri ya mpango wa awali na mapenzi huru. Yote yako sawa. Haya yanaunda uelekeo muhimu wa uhusiano wa agano lililoanzishwa na Mungu, lakini yanahitaji mwitikio kwa upande wa watu wake. Ule ushirika wa Mwanzo 1-2 unarejezwa katika namna ya kukombolewa, uhusiano wa agano. Matokeo ya Anguko yanaweza kugeuzwa (hata ndani ya muda mfupi). Angalia Mada Maalum: Agano katika 1:19.)

▣“**zenu zижапокува nyekundu sana**” Kumbukakwambavitu viliwyokuwa vimepakwa rangi katika kipindi kile cha ulimwengu wa kale visingeweza kubadilishwa (yaani, havikuwa na weupe). Msamaha wa Mungu (na usahafulifu) ni wa ajabu lakini inawezekana (kama vile Zab. 103:11-14; Isa. 38:17; 43:25; 44:22; Mik. 7:19)! Mungu anaposamehe, Husahau! Vema! Rangi nyekundu kama stiari ya dhambi inaweza kutokana na kifungungu cha mwanzo “mikono yenu imeja damu” kilichotajwa katika mst. wa 15.

**1:19** Hapa kuna kejeli katika ya mst. wa 19, “utii utafungua mlango wa utele” (lit. “kula mema ya nchi”; hiki KITENZI [BDB 37, KB 46, *Qal ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*], ambayo mara nyingi imekuwa mapenzi ya Mungu) na KITENZI kile kile katika mst. wa 20 kinachotafsriwa “kuangamizwa” (*Qalya KAULI TENDEWA YA WAKATI USIO TIMILIFU* au *Pialya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*), kama wakikataa kutubu na kuitikia. Kuna Baraka za kiagano na madaraka na haya yote yanahusiana (kama vile Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbula Torati 27-29)!

▣“**Kama mkikubali na kutii**” Kumbuka maagano yaliyo katika Agano la Kale yote ni ya kimasharti na mengine nhayana masharti. Mengine si ya masharti kama zilivyo ahadi za Mungu, lakini ni ya kimasharti kwa mwitikio wa mwanadamu (kama vile Luka 6:46; Yakobo 2:14-26)

## MADA MAALUM : AGANO

Neno la Agano la Kale berith (BDB 136, KB 157), sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenye kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu mmoja wa kweli anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi unaonekana katika dhana ya agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. wito wa Abramu (kama vile Mwanzo 12)
3. agano pamoja na Abramu (kama vile Mwanzo 15)
4. utunzaji wake na ahadi kwa Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Kumbukumbu la Torati 27-29)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya". Mvutano kwa wazi unawenza kuonekana katika kulinganisha Eze. 18 na Eze. 36:27-38.). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na lile Jipya. Malengo ya haya yote ni sawa:

1. urejesho wa ushirika uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uanzishwaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu.

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubalifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathabitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo, Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, bali ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani, Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika kitabu cha Waebrania.

**1:20“maana kinywa cha Bwana kimenena haya”** Neno la Mungu halitapita (kama vile Isa. 24:3; 25:8; 40:8; 55:10-11; Mt. 5:18; 24:35; Luka 16:17)! Tumaini la waumini liko huwa katika

1. sifa ya Mungu isiyobadilika
2. uaminifu wa ahadi zake
3. ukweli wa mafunuo yake

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:21-23**

<sup>21</sup>Mji huu uliokuwa mwaminifu umekuwaje kahaba!

Yeye aliyejaa hukumu ya haki;

haki ilikaa ndani yake,

bali sasa wauaji!

<sup>22</sup>Fedha yako imekuwa takataka,

divai yako imechanganya na maji.

<sup>23</sup>Wakuu wako ni waasi,

na rafiki za wevi;

kila mtu hupenda rushwa,

hufuata malipo;

hawampatii yatima haki yake,

wala maneno ya mjane hayawawasilii.

**1:21-23** Hiki kipengele kinazungumzia Yerusalemu ya siku za Isaya, sehemu maalum ambayo YHWH alilisababisha jina lake kudumu (kama vile Kut. 12:5,11,14). Sasa sehemu hii haina uaminifu tena na haitimizi matakwa ya agano (kama vile mst. wa 23). Kipengele hiki kinabainishwa kwa radha za maombolezo ya Kiebrania ama mapigo, ambayo nimbinu nyingine ya kawaida ya unabii wa kifasihi (yaani, wimbo wa maziko). Tambua ukiukaji wa kimaagano.

1. mauaji (kama vile Kut. 20:13, ya kuwaza, makusudu ya kuuondoa uhai, BDB 953, KB 1283, kama vile Yer. 7:9; Hos. 4:2)
2. wakuu kama waasi
3. marafiki wa walevi
4. wenye kupenda rushwa (kama vile 5:23; Kut. 23:6,8; Kumb. 16:19; I Sam. 8:3; Zab. 26:10; Amosi 5:12; Mika 3:11; 7:3)
5. wenye kutaka malipo
6. hawampatii yatima haki yake
7. maneno ya mjane hayawawasilii (kama vile Kut. 22:21-24; Yer. 5:28; 7:6; 22:3; Eze. 22:7; Zek. 7:10) Ukiukwaji huu wa agano la Musa umewekwa katika muhtasari katika Kumbukumbu la Torati. Tambua kwamba Yuda anashtumiwa kwa kulikiuka agano, katika muktadha huu haumaanishi ibada za sanamu (ikiwa kuna neno "kahaba" katika mst. wa 21 lenye kumaanisha ibada za ustawi za Wakaanani).

**1:21 "mwaminifu"** Tazama Mada Maalum: Amini, Tumaini, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale katika 7:4-9.

**1:22** Hizi ni stiari mbili zenyenye kumaanishammomonyoko wa maadili wa Yuda. Mwanzoni huyu alikuwa safi, lakini sasa amekuwa na shingo ngumu kuititia chaguzi na matendo yake!

▣  
**NASB**            “divai”

**NKJV, NRSV,**

**TEV, NJB**        “mvinyo”

Hili ni neno la kawaida la mvinyo (angalia Mada Maalum ifuatayo). Hiki kiwawakilishi cha JINSIA YA KIKE WINGI kimetokea hapa tu. Kwa sababu ya mzizi huu huu wenye kuhusiana katika lugha ya Kiakadia, neno hili linaweza kurejelea pombe aina ya bia, bia ambayo imefifilishwa (yaani, iliyoharibiwa) kwa kutumia maji.

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA JUU YA KILEO NA ULEVI

Maneno ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. *Tirosh* – Hii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya" BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi hiki huongezwa ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya

1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
2. *Neos oinos* (divai mpya) – ni neno linalofanana la Kiyunani sawa na *tirosh* (kama vile Marko 2:22).
3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

I. Matumizi ya Kibiblia

- A. Agano la Kale
    - 1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
    - 2. Divai ni sehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
    - 3. Mvinyo ilitumika katika sherehe za Israeli (kama vile Kumb. 14:26)
    - 4. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2; Mit. 31:6-7).
    - 5. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnoni– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amosi 4).
    - 6. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
    - 7. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
    - 8. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).
  - B. Kipindi cha utulivu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya
    - 1. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
    - 2. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai ni kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa ya kulevy ya yanahitajika." (BB 58b).
  - C. Agano Jipya
    - 1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
    - 2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
    - 3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
    - 4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
    - 5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima moja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
    - 6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
    - 7. Ulevi huleta majuto (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).
- II. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia
- A. Mkazo wa Kiupembuzi
    - 1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
    - 2. Ulevi ni tatizo kubwa.
    - 3. Waamini katika baadhi ya tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).
  - B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka iliyokusudiwa
    - 1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote mazuri.
      - a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
      - b. vitu vyote visivyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
      - c. Vitu vyote vilivyo vya kisheria– 1 Kor. 6:12; 10:23
      - d. Vitu vyote vilivyo safi – Titus 1:15
    - 2. Mwanadamu aliyeanguka amezitumia vibaya karama za Mungu kwa kuzifanya kazi nje ya mipaka ya Mungu aliyoikusudia.
  - C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (kama vile Rum. 14:14,20).
- III. maelezo ya kufungia
- A. kuwe na uhakika na uzoefu wako, thiolojia, na utafasiri wa kibilia havimshushi thamani Yesu na tamaduni za Kikristo/ Kiyahudi za karne ya kwanza! Kiuhakika hawakuwa wenye kujizuiya kunywa mvinyo.
  - B. Mimi sitetei jamiii ya watumia pombe. Hata hivyo, wengi wamekwenda mbali juu ya nafasi ya Biblia kuhusu somo hili na sasa kudai kuwa wenye haki sana wakisimamia juu ya upendeleo wa kimadhehebu/

- kitamaduni.
- C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 vimetoa mwanga na mwongozo uliosimamia juu ya upendo na heshima kwa wapendwa wengine na uenezaji wa injili katika tamaduni zetu, na sio uhuru binafsi au ukosoaji wa kimaamuzi. Kama Biblia ndio chanzo pekee cha imani na utendaji, kwa hiyo yawezekana wote tulifikirie jambo hili.
  - D. Tukijizuiya kabisa kunywa mvinyo kama yalivyo mapenzi ya Mungu, tunadokeza nini kuhusu Yesu, pia tamaduni za sasa za wale wanaotumia kileo mara kwa mara (mf. Ulaya, Israel, Argentina)

**1:23**

**NASB, NKJV,**

**LXX, Peshitta**            “**malipo**”

**NRSV, TEV,**

**REB**                    “**zawadi**”

**NJB**                    “**hongo**”

Neno hili (BDB 1024) limejitokeza hapa tu katika Agano la Kale. BDB inasema kuwa hili linamaanisha “zawadi” ama “hongo” (linafanana na neno kutoa hongo [BDB 1005] katika mstari wa hapo awali). Mzizi wa msingi unaweza kuhusiana na (1) *shalom* (BDB 1024), “amani,” “afya,” “umoja,” au (2) “kutoa malipo mara mbili” (BDB 1024, kama vile 59:18; NIDOTTE, juzu 4, uk.143). Katika Yerusalem amani ilikuwa kwa wale wenye udharimu tu, matajiri, makundi yenye nguvu katika jamii.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 1:24-26**

<sup>24</sup> **Kwa hiyo, asema Bwana, Bwana wa majeshi,**

**Mwenye enzi, wa Israeli,**

**Nitapata faraja kwa hao wanipingao,**

**nitatwaa kisasi kwa adui zangu;**

<sup>25</sup> **nami nitakuelekezea wewe mkono wangu,**

**na kukutakasa takataka zako kabisa,**

**na kukuondolea bati lako lote;**

<sup>26</sup> **nami nitarejeza upya waamuzi wako kama walivyokuwa hapo kwanza,**

**na washauri wako kama hapo mwanzo;**

**baada ya hayo utaitwa, Mji wa haki,**

**mji mwaminifu.**

**1:24-26** YHWH anazungumza juu ya mipango ya baadaye ya skuwarejeshs watu wake (kama vile mst. wa 26) baada ya hukumu juu ya utawala ulio dharimu.

1. “Nitapata faraja,” mst. wa 24, BDB 636, KB 688, *Niphal* ya KAULI ISIO TIMILIFU iliyotumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
2. “nitatwaa kisasi kwa adui zangu,” mst wa 24, BDB 667, KB 721, *Niphal* ya KAULI KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
3. “nami nitakuelekezea wewe mkono wangu,” mst.wa 25. BDB 996, KB 1427, *Hiphilya* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
4. “na kukutakasa takataka zako kabisa,” mst wa 25, BDB 864, KB 1057, *Qal/YA* KAULI ISIO TIMILIFU yenye kutumika katika maana ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
5. “na kukuondolea bati lako lote,” mst. wa 25, BDB 693, KB 747, *Hiphilya* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
6. “nitarejeza upya waamuzi wako,” mst wa 26, BDB 996, KB 1427 *Hiphil/YA* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
7. “washauri wako,” mst wa 26 (ni sawa na #6, KITENZI kimoja, SHAMIRISHO mbili; hivi lazima vihusiane na kipindi cha Uhamisho)

Elewa kwamba hukumu ni kwa ajili ya urejesho (kama vile mst wa 27)!

**1:24** Tambua majina mawili ya Uungu katika mst. wa24!

1. - 2. Bwana wa Majeshi (*adon*, YHWH, kama vile Zab. 110:1; NIDOTTE, juzu 4, kr.1297-1298
3. Shujaa wa Yakobo (kama vile Mwa. 49:24; Zab. 132:2,5; Isa. 49:26; 60:16)

**1:25-26 “wako. . .wako”** Hii mistari miwili inatumia JINSI ZA KIKE ZA UMOJA za kudokeza kwamba YHWH anazungumza juu ya mji wa Yuda usio mwaminifu, Yerusalem, pamoja na hali yake ya kiuchumi, kijeshi, na nguvu ya kidini.

Kama mist.ya19 na 20 ilivyotumia KITENZI kile kile katika namna za kutofautisha, ndivyo ilivyo, kwa mist. ya 25 na 26 kwa

1. nami nitakuelekezea wewe mkono wangu, BDB 996, KB 1427, *Hiphil* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
2. nitarejeza, BDB 996, KB 1427, *Hiphilya* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO

Neno hili hili linatumika katika mst. wa27, “warejeshaji” (BDB 996, KB 1427, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU) kutoa ufanuzi juu ya wale walioguswa na hukumu na haki na Mungu.

**1:26“Mji wa haki”** Haya ni mageuzi ya kejeli ya mst. wa 21? Yerusalem si “kahaba,” tena bali imerejezwa, ni mwanamke mwaminifu (yaani, neno “mji” ni JINSI YA KIKE). Mwishowe amekuwa na sifa yake kamili, ya mwaminifu kwa Mungu, mwaminifu kwa agano lake, na mwaminifu kwa kila mtu!

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 1:27-31**

<sup>27</sup>Sayuni itakombolewa kwa hukumu,  
na waongofu wake kwa haki.

<sup>28</sup>Lakini kuharibika kwao wakosao nao wenyе dhambi kutatokea wakati mmoja,  
nao wamwachao Bwana watateketezwa.

<sup>29</sup>Kwa maana watatahayarika kwa sababu ya mialoni mliyotamani,  
nanyi mtaabishwa kwa sababu ya bustani mlizozichagua.

<sup>30</sup>Maana mtakuwa kama mwaloni ambaao majani yake yakauka,  
na kama bustani isiyo na maji.

<sup>31</sup>Na mtu hodari atakuwa kama makumbi,  
na kazi yake kama cheche ya moto;

nao watawaka pamoja,  
wala hapana atakayewazima.

**1:27-28** Tambua ufanano.

1. mst. wa 27, watu wa mji uliorejezwa (mst. wa 26 aya ya 3 na 4) watabainishwa kwa “hukumu” na “haki”
2. mst. wa 28, yule akataaye kutubu (kurudi) “atateketezwa” na “watateketezwa”

Hivyo, kuna usawa wenyе ufanano ndani ya mist. ya 27 na 28, lakini ufanano wenyе kukinzana kati ya mist. 27 ya 28.

Kuna swali moja kuhusu mst. wa 27. Je! Huu unaeleza juu ya kile anachokifanya Mungu na kile atakachokifanya au unaeleza juu ya uaminifu wa watu wa agano? Jibu ni “ndiyo.” Mungu huwataka watu wenyе haki kuiakisi tabia yake kwa mataifa yaliyopotea. Ubora huu nithabiti (Mungu) na kiima (waumini).

**1:29** Mstari huu unaeleza juu ya Yuda kuabudu sanamu. Hii inarejea juu ya

1. kumwabudu *Baali*, *Ashera* chini ya miali ya majabali (yaani, *Ashera* aliashiriwa na miti iliyoleta ikidumu kwa muda mrefu aungozo iliyochongwa, kama vile 57:5, ambayo pia ainataja juu ya kuwatoa watoto kama dhabihu kwa Moleki)
2. kuabudu miti iliyotengwa (miungu ya asili, kama vile 65:3; 66:17)
3. kufanya ibada katika bustani mara nyingi kunahusiana na kuabudia sehemu ya maficho. Katikafasihi ya mahekalu ya ANE na bustanini mara nyingi vilihusiana.

Inapaswa kuongezwa kwamba inawezekana kwamba hii ibara (mist ya 27-31) inarejelea juu ya matabaka ya jamii Yudea yenye yenye kutumiavibaya madaraka nakuwa na tamaa ya mali. Marejeleo yaliyo katika mst. wa 29 ni ya

uchaguzi wa mali (yaani, ukiukaji wa pendo maalum la YHWH kwa wale wasio na mali, wanaochukiwa, wasio na mamlaka) na wale wasio abudu sanamu (yaani, ukiukaji wa upekee wa YHWH).

Soma sura hii na fanya uamuzi mwenyewe! Kwa vyo vyote vile, inashindikana kuiakisi tabia ya YHWH kwa mataifa!

**1:30 “yakauka”** Hiki KITENZI (BDB 615, KB 663, *Qal CHA KAULI TENDAJI ENDELEVU*) kinatumika kistiani kutoweka upesi kwa mwanadamu (kama vile 34:4; 64:6; Zab. 90:5-6).

**1:31** Mara nyingi moto unahusiana na hukumu autendo la kusafisha (yaani, 6:13; Yer. 4:4; 7:2; Amosi 5:6)

## MADA MAALUM : MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

A. Chanya

1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
3. Hipikia (kama vile Kut. 12:8; Isay 44:15:16; Yohana 21:9)
4. Husafisha (kama vile Hes. 31:22-23; Mit. 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Eze. 1:27; Waebrania 12:29)
6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 118:24)
7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile. Matendo 2:3)
8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)

B. Hasi

1. Huunguza (kama vile Yos. 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7)
2. Huangamiza (kama vile Mwa. 19:24; Walawi 10:1-2)
3. Hasira (kama vile Hes 21:28; Isay 10:16; Zek 123:6)
4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17)
5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile. Ufunuo 13:13)

C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.

1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos. 8:5; Sefania 3:8)
2. Humimina moto (kama vile Nah. 1:6)
3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt 25:41; Yuda aya ya 7)
4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile Mt. 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu. 8:7; 16:8; 20:14-15)

D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru

1. Mwa.15:17
2. Kutoka 3:2
3. Kutoka 19:18
4. Zaburi 18:7-15; 29:7
5. Eze. 1:4, 27; 10:2
6. Ebr. 1:7; 12:29

E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaani, chachu, simba) moto unawezza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.



NASB                  “**mtu hodari**”

NKJV, NRSV,

NJB                  “**mwenye nguvu**”

LXX, Peshitta      “**nguvu zao**”

REB                  “**mti mkubwa**”

JB                  “**watu wa tabaka la juu**”

Hiki KIVUMISHI (BDB 340) kinapaitikana hapa tu na katika Amosi 2:9, maandiko yote yanahusiana na miti (kama vile mist.ya 29,30). Huenda toleo la REB ni bora zaidi. Hili linarejelea sanamu zikiwemo mbao, miti, ama bustani.

▣“**makumbi**” Hili neno (BDB 654), katika muundo wake wa KITENZI, mara nyingi linamaanisha “*kupukutika*” (kama vile 33:9,15), lakini NOMINO, iliyotumika mara mbili katika Aganola Kale, inarejeleakamba/uzi (mnyororo)unaotokana na kamba (Amu. 16:9).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana

1. Ni kwa namna gani Isaya alitumika kama nabii mkuu wa Yuda?
2. Kwa nini Mungu anazungumza maneno haya machachekatika lugha maneno hayo ya kibinadamu?
3. Je! Mungu anachukizwa na dhabihu?
4. Fafanua jukumu la mtu katika wakovu, Agano la Kale na Agano Jipya.

## ISAYA 2

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Utawala wa Mungu ulimwenguni	Nyumba ya Mungu ijayo	Andiko la pili juu ya	Amani ya milele	Amani ya milele
2:1	2:1-4	2:1 Tumaini Jipya	2:1-5	2:1-5
2:2-4 (2-4)	(2-4)	2:2-4 (2-4)	(2-3) (4)	(2-3) (4)
		Siku ya Bwana		
2:5-11 (5-11)	2:5-9 (5)	2:5-22 (5-22)	kiburi kitaharibiwa (2:6-8)	(5) Utukufu wa Enzi ya Yahweh (2:6-22) (6-8) 9-10
	2:10-11 (10-11)		2:10-18	
Siku ya kutambuliwa yaja			2:9	(11-16)
2:12-22 (12-22)	2:12-22 (12-18)			(17) (18-19)
	(19) (20-21)		19-21	
	(22)		(2:22)	(21) (22)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. wa xvi katika sehemu ya utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujsomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kii cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Sura ya 2 inaanza na tungo nyingine ya ufunguzi 1:1. Inawezekana kwamba wahariri au watungaji wanaweka mahubiri/maono/jumbe za Isaya pamoja kwa kuzingatia

1. mtiririko (ambapo chini ya mfalme)
2. somo
3. maneno ya kukumbuka
4. mbinu na mfumo wa kifasihi usuijulikana
5. nakala ya kuandikwa kadhaa za jumbe za Isaya

Angalia dokezo katika toleo la The Jewish Study Bible, ukurasa wa 787.

- B. Sura hii ni hasa imeshehemu jumbe za Isaya.
  1. tumaini kwa mataifa yote kuitia watu wa ganao (mistari ya. 2-4)
  2. hukumu kwa kuvunja agano na kutenda uovu (mistari ya 5-22)
- C. YHWH anataka watu watakatifu, wenye haki na wa agano kuakisi tabia yake kwa mataifa ili kwamba waweze kumuitikia kwake kwa Imani na Haki (kama vile 45:22; 49:6; 60:3; 66:18,23).
- D. Kumbuka katika vipengele hivi nya kifasihi nya kishairi (maono), havilazimishi maelezo au kujifunza misamiati kwa aina moja bali utaratibu mzima wa usambamba, mafumbo ya kimaneno na ulinganifu! Shairi zima linamaanisha kuelezea kweli kuu moja! Kuwa mwangalifu juu ya kuchukua na kuchagua maudhui, maneno au kweli ambayo wewe mwenyewe ndio unapendelea au ambayo yanashabihiana na mfumo wa kithiolojia. Mwache Isaya azungumze!
- E. Kwasababu ya maudhui yanayounganisha (kuhukumiwa na kubarikiwa), sura za 2-4 zinaunda kipengele cha kifasihi
- F. Kitabu kilichonisaidia kuelewa lugha ya kinabii na ya siku za mwisho ni D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*, IVP, ISBN 0-838-2653-X.

## AINISHO FUPI

- A. Wimbo wa kimafumbo, mistari ya 1-6
- B. Fasiri za kiishara, mistari wa 7-41
- C. Matokeo ya hukumu ya YHWH, mistari ya 8-30
  1. mfuatano wa Ole, mistari ya 8-23
  2. Hukumu, mistari ya 24-30
    - a. asili, mistari wa 25
    - b. mvamizi, mistari ya 26-30

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 2:1**

<sup>1</sup> Hili ni neno aliloliona Isaya mwana wa Amozi katika habari za Yuda na Yerusalem.

**2:1** Haijajulikana bado kwanini jumbe za Isaya zinaelezewa kama

1. maono, 1:1; 29:7 (BDB 302, kama vile Mika 3:6)
2. aliona, 1:1; 2:1; 13:1; 26:11; 33:17; 48:6; 57:8 (kama vile Mika 1:1)

Huu ndio ujuzi wa Ufunuo. Unakuja kwa njia mbali mbali kwa waandishi tofauti tofauti wa kibiblia (maono, ndoto, kufanyika mwili kwa Mungu, maneno, n.k). Wakisasa hawajui uhuru kiasi gani waandishi moja mmoja (waandishi, wahariri na watungaji) walitakiwa kuutengeneza muundo na kuwasilisha ujumbe wa Mungu. Kidhahiri walitumia ujuzi wao wa lugha na misamiati. Hata bila uelewa kaili na kamilifu juu ya namna gani ufunuo unafanya

kazi, dhana ni muhimu! Jumbe hizi za Mungu zilizotolewa kupertia mtu aliwekwa kimasharti kihistoria kwa muda maalumu na kundi, lakini zibaki za kufaa kwa watu wote nyakati zote! Msingi wa ufasiri mzuri ni kwamba kusudio la mwandishi wa asili aliyeuvuviwa lazima kiwe ni kigezo kwa ajili ya fasiri (maana moja lakini umuhimu mwingi na matumizi)

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 2:2-4

<sup>2</sup> Na itakuwa

katika siku za mwisho,  
mlima wa nyumba ya Bwana  
utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima;  
na mataifa yote watauende makundi makundi.

<sup>3</sup> Na mataifa mengi watakwenda na kusema,

Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana,  
nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake,  
nasi tutakwenda katika mapito yake  
maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalem.

<sup>4</sup> Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi,

atawakemea watu wa kabilia nyingi; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu;  
taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine,  
wala hawatajifunza vita tena kamwe.

**2:2-4** Aya fupi inaweka muhtasari mtazamo wa Agano la Kale kwenye sehemu na kusudi la watu wa agano (sawasawa na Mika 4:1-5). Walitakiwa kuwa nuru kwa mataifa (kama vile 51:4,5; Luka 24:47)! Angalia Mada Maalum katika 1:3.

**2:2 “katika siku za mwisho”** Tungo hii inamaanisha matazamio ya baadaye ya mwandishi fulani wa kibiblia (angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura ya 14, “The Language of Eschatology,” kurasa za 243- 271). Iliashiria muda wa kutimilizwa kwa makusudi ya Mungu.

1. Ufalme wa kimasih, Mwanzo 49:1 (hasa 49:10); Hesabu 24:14-25 (hasa 24:17); Isa. 2:2; Yer. 48:47; 49:39; Ezek. 38:8,16
2. uasi wa Israeli, Kumb. 31:29
3. Kurudi kwa Israeli kwa YHWH kwa toba na imani, Kumb. 4:30; Hos. 3:5; Yer. 23:19-22 (hasa 23:20)
4. uvamizi wa wakati wa mwisho juu ya watu wa agano, Ezek. 38:16; Dan. 2:28; 10:14 (yawezekana Zaburi 2)
5. uhamisho, Amosi 4:2

Ni muktadha tu unaoweza kuelezea kipindi gani. Kuwa makini na thiolojia yako ya kimfumo!

#### MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

Yesu	Paulo	Waebrania (Paulo)
Mt. 12:32; 13:22,39	Warumi 12:2	Ebr.1:2
Marko 10:30	1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18	6:5
Luka 16:8; 18:30; 20:34-35	2 Kor. 4:4	11:3
	Wagalatia 1:4	
	Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12	
	1 Timotheo 6:17	
	2 Timotheo 4:10	
	Tito 2:12	

Katika thiolojia ya Agano Jipy a zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyeketu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liilivytabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipy wa uliopo tayari, lakini bado!

■ “Mlima wa nyumba ya BWANA” Hii inamnaanisha kwa hekalu lilielowekwa juu ya Mlima Moria katika Yerusalem. Ilikuwa ni sehemu ya ibada kuu kwa YHWH (mahali aliposababisha jina lake kukaa, cf. Deutkama vile Kumb. 12:5,11,14,18,21,26; 14:25; 15:20; 16:2,6,11,15; 17:8,10; 18:6; 26:2; 31:11).

Toleo la NIV Study Bible (kurasa za 962-3) inatoa maoni ni kwa namna gani katika Isaya maudhui ya mlima wa Bwana ambapo mataifa yote yatakuja katika siku za mwisho (kama vile 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:25; 66:20).

Katika namna ya kukuzwa huku kwa mlima Sayuni (yaani Yerusalem, mahali pa hekalu la YHWH) inachukuliwa kama hadithi ya kidini (kama vile NIDOTTE, vol. 4, kurasa za 1314-1321). Kwa ajili ya miungu Wakanaani kukaa katika mlima Zaphoni huko kusini ya mbali (kama vile Isa. 14:13), lakini Zaburi 48:2 inabadilisha taswira ya mlia Sayuni. YHWH yuko juu sana ya miungu ya Wakanaani!

Dhana hii hii ya hekalu au mji kuinuliwa pia inapatikana katika vitabu vya Mesopotamia (kama vile The Weidner Chronicle, maelezo ya Ki-Ashuru, unabii wa Marduk). Hivyo dhana ni ya kipekee kwa Isaya.

■ Tazama lugha ya kisitiari ikitumika kuelezea sehemu kuu ya ufunuo wa YHWH kwa uzao wa Ibrahimu.

1. “mwangalizi wa milima,” yaani sehemu ya ufunuo wa kweli
2. “iliyoinuliwa juu ya milima,” kiwakilishi cha utawala wa enzi na ujumuishi
3. “mataifa yote yataielekea,” hii siku zote limekuwa lengo la YHWH, kama vile Mwanzo. 3:15; 12:3; Kutoka 19:5-6; Zab 22:27; 66:1-4; 86:8-10; Isa. 12:4-5; 25:6-9; 42:6-12; 45:22-23; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:23; Mika 4:1-4; Mal. 1:11; Yohana 3:16; 4:42; I Tim. 2:4; Tito 2:11; II Pet. 3:9; I Yohana 2:1; 4:14! Haya ni matokeo ya asili ya hali ya kuabudu Mungu mmoja.

## MADA MAALUM: UTABIRI WA AGANO LA KALE JUU YA WAKATI UJAO DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA (“UTANGULIZI WA MUHIMU” KWA UFUNUO)

Wakati wote wa kujifunza kwangu matukio ya siku za mwisho nimejifunza kwamba Wakristo wengi hawana mfuatano wa matukio ya siku za mwisho au hawataki kuukuza. Kuna baadhi ya wakristo ambao wanaweka shabaha zao au wanaamua kujikita kwenye eneo la Ukristo kwa sababu za kithiolojia, kisaikolojia au kidini. Wakristo hawa wanaonekana kuchanganyikiwa na kwa namna gani itamalizika na kwa namna fulani kukosa umaana wa injili! Waaminio hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu ya siku za mwisho, lakini wanawenza kushiriki katika upelekaji wa injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Waaminio wengi wanathibitisha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kupelekeea kwa siku za mwisho kwa ahadi za Mungu. Matatizo ya kiufasiri yanaibuka kutoka kwa namna gani kilele hiki cha muda kitakuja kutoka katika mtazamo kadhaa ya kibiblia (Angalia [Mada Maalum:Ukinzani katika Maandiko](#))

1. mvutano katika ya nadharia za kinabii za agano la kale na nadharia za kitume za Agano Jipyä
2. mvutano kati ya hali ya kuabudu Mungu mmoja (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalum)
3. mvutano katika ya hali ya kipengele chenye masharti cha maagano ya kibiblia na ahadi ("ikiwa.. .ndipo") na hali isiyo na masharti ya uaminifu wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka
4. mvutano kati ya aina za fasihi za Mashariki ya Karibu na nadharia za magharibi za kifasihi
5. mvutano kati ya ufalme wa Mungu kwa sasa na ule wa baadaye.
6. mvutano kati ya imani katika kurudi punde kwa Kristo na imani kwamba baadhi ya matukio lazima yatokee kwanza.

Ebu kwanza tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine

#### **MVUTANO WA KWANZA** (vipengele vya kijiografia, kitaifa na kikabila vya Agano la Kale dhidi ya waaminio wote katika ulimwengu)

Manabii wa Agano la Kale walitabiri kurejeshwa kwa ufalme wa Kiyahudi katika Palestina ukiwekwa kitovu Yerusalem ambapo mataifa yote ya nchi yatakusanyika kusifu na kutumikia mtawala wa Ki-Daudi, lakini Yesu au Mitume wa Agano Jipyä hawajikiti katika agenda hii. Je kwani Agano la Kale halijavuviwa (kama vile Mt. 5:17-19)? Je waandishi wa Agano jipyä wameondoa sehemu muhimu za matukio ya siku za mwisho?

Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu:

1. manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. waandishi wa siku za mwisho (kama vile Ezek. 37-39; Dan. 7-12; Zek.)
3. Kipindi kati ya kuandikwa kwa Agano la Kale na Agano Jipyä, waandishi wa siku za mwisho wa kiyahudi wasio wakanoni (kama I Enoch, ambaye anaelezewa katika Yuda)
4. Yesu mwenyewe (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21)
5. maandiko ya Paulo (kama vile I Kor. 15; II Kor. 5; I The. 4-5; II The. 2)
6. maandiko ya Yohana (I Yohana na Ufunuo).

Je haya yote kwa ufasaha yanafundisha ajenda ya siku za mwisho (matukio, mpangilio wa matukio, watu?) Ikiwa sio, kwanini? Je si kwamba wote wamevuvuviwa (isipokuwa maandiko ya kiyahudi ya kati ya kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipyä)?

Roho alifunua kweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na vipengle ambavyo wangeweza kuelewa. Hatahivyo kupitia ufunuo endelevu Roho amepanua dhana hizi za matukio ya siku za mwisho kwa mtazamo wa kijumla ("siri za Kristo," kama vile Efe. 2:11-3:13. Angalia Mada Maalum katika 10:7).

Hii hapa ni baadhi ya mifano inayoelekeana kwa umuhimu:

1. Jiji la Yerusalem katika Agano la Kale linatumika kama sitiari ya watu wa Mungu (Sayuni), lakini

inakadiriwa katika Agano Jipyka kama neno linaloeleza ukubalifu wa Mungu wa watubuo wote na wanadamu waaminio (Yerusalemu mpya ya Ufunuo 21- 22). Upanuzi wa kithiolojia wa jiji la kibayana la kimwili katika watu wapya wa Mungu (Wayahudi na Mataifa waaminio) inaakisiwa kwa kuoneshwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa mwanadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata haijakuwako Myahudi yeyote au mji mkuu wa kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (kama vile Mwanzo 12:1-3) ilijumuisha Mataifa (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5).

2. Katika Agano la Kale adui za watu wa Mungu ni mataifa yazungukayo mataifa ya Mashariki ya Karibu ya Kale, lakini katika Agano Jipyka wamepanua kwa watu wasio amini, walio kinyume na Mungu na waliovuviwa kishetani. Vita vimehamisha kutoka kijiografia, kimgogoro wa kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (kamavile Wakolosai).
3. Ahadi ya nchi ya ambalo ni jambo kuu sana katika Aano la Kale (Ahadi kwa mababa wa imani katika Mwanzo, kama vile Mwanzo 12:7; 13:15; 15:7,15; 17:8) sasa imekuwa kwa dunia yote. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa dunia iliyotengenezwa upya, sio Mashariki ya Karibu tu au kutojumuisha (kama vile Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ni dhana za kinabii za Agano la Kale zilizopanuliwa ni
  - a. uzao wa daudi saa umetahiriwa kiroho(kama vile Rum. 2:28-29)
  - b. watu wa agano sasa wanajumuisha Mataifa (kama vile Hos. 1:10; 2:23, akinukuu katika Warumi 9:24-26; pia Mambo ya Walawi 26:12; Kutoka 29:45, ikinukuliwa katika II Kor. 6:16-18 na Kutoka 19:5; Kumb. 14:2, ikinukuliwa katika Tito 2:14)
  - c. hekalu sasa ni Yesu (kama vile Mt. 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia kanisa la mahali pamoja (kama vile I Kor. 3:16) au mwamini mmoja mmoja (kama vile I Kor. 6:19)
  - d. Hata Israeli na tungo zinazofunua tabia za Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (yaani “Israeli,” kama vile Rum. 9:6; Gal. 6:16, yaani “ufalme wa makuhani,” kama vile I Pet. 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Nadharia ya kinabii imetimilizwa, imepanuliwa na sasa imekuwa jumuishi. Yesu na waandishi wa kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kwa namna ile ile ya Manabii wa Agano la Kale (kama vile Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecy and Fulfillment*). Wafasiri wa kisasa wanaojaribu kulifanya nadharia ya Agano la Kale kuwa ya maana ya wazi au ya tabia ya kawaida kugeuza ufunuo katika kitabu cha kiyahudi kabisa na kulazimisha maana! Waandishi wa Agano Jipyka hawawakatai manabii wa Agano la Kale lakini wanaonesha ufanyaji wao kazi wa kilele wa kiulimwengu. Hakuna mpangilio au mfumo wa kimantiki kwa matukio ya siku za mwisho ya Yesu au Paulo. Makusudi yao kimsingi ni ukombozi na sio uchungaji.

Hatahivyo, hata ndani ya Agano Jipyka kuna mvutano. Hakuna mfumo wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika njia nyingi Ufunuo kwa kushangaza unatumia Maelezo ya Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala yamafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko 13)! Inafuata aina ya fasihi iliyoanzisha na Ezekieli, Daniel na Zekaria lakini ilikuzwa wakati wa kipindi kati ya uandishi wa Agano la Kale na Agano Jipyka (fasihi ya kiyahudi ya siku za mwisho). Hii inaweza kuwa ilikuwa nji ya Yohana kuunganisha Maaagano ya Kale na Jipyka. Inaonesha utaratibu wa zama-kuu ya uasi wa kibinadamu na kujizatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini lazima itambuliwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha, watu na matukio ya Agano la Kale, inafasiri kwa ufahamu na namna ya karne ya kwanza ya Rumi (kama vile Ufunuo 1:7).

#### **MVUTANO WA PILI** (hali ya kuabudu Mungu mmoja dhidi ya wateule wa Mungu)

Msisitizo wa kibiblia upo juu ya Mungu binafsi, kiroho, muumbaji-mkombozi (kama vile 8:10; Isa.

44:24; 45:5-7,14,18,21- 22; 46:9; Yer. 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake ilikuwa hali ya kuabudu Mungu mmoja (angalia [Mada Maalum: Ibada kwa Mungu mmoja](#)). Mataifa yote yanayozunguka yalikuwa ni waabudu miungu wengi. Kuwepo kwa Mungu mmoja ni moyo wa ufunuo wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 6:4). Uumbaji ni jukwaa kwa kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, waliofanywa kwa sura yake na mfano (kama vile Mwanzo 1:26-27). Hatahivyo, mwanadamu aliasi, akitenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi na kusudi (kama vile Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa na lenye nguvu sasa na hakika alihaidi kukomboa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mwanzo 3:15)!

Mvutano unainuka pale ambapo Mungu anachagua kumtumia mwanadamu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu waliobakia. Wateule wa Mungu wa Ibrahim na Wayahudi kama ukuhani wa kikuhani (kama vile Kutoka 19:4-6) kulisababisha kiburi badala ya huduma, kutengwa badala ya kujumuishwa. Wito wa Mungu kwa Ibrahim ulijumuishwa Baraka za kimakusudi kwa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3). Lazima ikumbukwe na kusisitizwa kwamba uchaguzi wa Agano la Kale ulikuwa kwa ajili ya huduma, sio wokovu. Israeli yote haijawahi kuwa sawa na Mungu, haijawahi kukombolewa kimilele kwa msingi tu wa haki yake (kama vile Yohana 8:31-59; Mt. 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (kama vile Mwanzo 15:6, ikinukuliwa kutoka Warumi 4). Israeli ilipoteza lengo lake (kanisa sasa ni ufalme wa kikuhani, kama vile 1:6; II Pet. 2:5,9), twakibadilisha majukumu kuwa upendeleo, huduma kuwa msimamo maalum! Mungu anachagua mmoja ili achague wote.

#### **MVUTANO WA TATU (maagano yenyenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)**

Kuna mvutano wa kithiolojia au fumbo kati ya maagano yenyenye masharti na yale yasiyo na masharti. Ni hakika kweli kwamba kusudi/mpango wa Mungu na ukombozi sio wa kimasharti (kama vile Mwanzo 15:12-21). Hatahivyo, mwitikio wa kimajukumu wa kibiadamu siku zote huwa ni wa kimasharti!

Ile “ikiwa. . . basi” ya utaratibu huu unatokea kote katika Agano la Kale na Agano Jipy. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha mkanganyiko mkubwa. Wafasiri wamejifanya kuweka shabaha juu ya moja tu “pembe ya mkanganyiko,” Uaminifu wa Mungu au juhudzi za mwanadamu, utawala wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Vyote ni vya kibiblia na ni vya muhimu (Angalia [Mada Maalumaaa; Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la uwiano wa Kithiolojia](#))

Hii inahusiana na matukio ya siku za mwisho, kwa ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Israeli; Hadhi yake inajumuishwa (kama vile Ezek. 36:22-38). Maagano yenyenye masharti na yale yasiyo na masharti yanakutana katika Kristo (kama vile Isa. 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kinategemea ukombozi wa wote watakaotubu na kuamini, sio nani alikuwa baba yako/mama yako, sio Israeli, ni msingi wa maagano yote ya Mungu na ahadi. Ikiwa kuna maelezo ya kithiolojia katika Biblia, sio kanisa bali Israeli (kama vile Mdo. 7 na Gal. 3).

Kusudio la ulimwengu la kutangaza injili limepitia kwa kanisa (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Bado ni agano la kimasharti! Hii sio kumaanisha kwamba Mungu amekataa kabisa Wayahudi (kama vile Rum. 9-11). Kuna weza kuwa kuna mahali na kusudi la siku za mwisho, kuamini Israeli (kama vile Zek 12:10).

#### **MVUTANO WA NNE (nadharia ya kifasihi ya Mashariki ya Karibu dhidi ya nadharia za kimagharibi).**

Aina za fasihi ni kipengele muhimu katika usahihi wa kufasiri Biblia. Kanisa limeendelea katika mazingira ya kidesturi ya kimagharibi (kiyunani). Fasihi ya mashariki zaidi ni ya kimafumbo, ya kisitiari na kiishara kuliko kuwa ya kisasa, nadharia za desturi za kifasihi za kimagharibi (angalia [Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki \(ukinzani wa kibiblia\)](#)). Imejikita kwa watu, matukio na mazingira kuliko kweli

ziazopendekezwa. Wakristo wamekuwa na hatia ya kutumia historia na nadharia za kifasihi kufasiri nabii za Kibiblia (zote Agano la Kale na Agano Jipy). Kila kizazi na jambo la kijiografia limetumia desturi yake, historia na ubayana wake kufasiri Ufunuo. Kila mmoja wao amekuwa na makosa! Ni kiburi kufikiria kwamba desturi za kisasa za kimagharibi ni shabaha ya unabii wa kibiblia!

Aina ya fasihi ambayo kutoka kwake mwandishi wa asili na aliyeuvuviwa anachagua kuandika ni mkataba wa kifasihi na mwandishi. Kitabu cha Ufunuo sio masimulizi ya kihistoria. Ni muunganiko wa barua (sura za 1-3), unabii na zaidi fasihi ya nyakati za mwisho. Ni mbaya kuifanya Biblia kusema zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili kama ilivyo kuifanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa! Kiburi cha wafasiri na mafundisho hata zaidi isivyokuwa sawa katika kitabu kama ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana katika fasiri sahihi ya ufunuo. Shida yangu ni kusikia na kushughulikia Biblia nzima, sio baadhi ya sehemu zilizochaguliwa. Mtazamo wa mashariki wa Biblia inawasilisha ukweli katika jozи zilizojaa mvutano. Mwenendo wetu wa magharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa usiokatalika lakini usio na uwiano! Nafikiri inawezekana kuondoa angalau baadhi ya vizuizi katika kufasiri Ufunuo kwa kutambua makusudi yake yanayobadilika kuelekea vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni dhahiri kwa wafasiri wengi kwamba Ufunuo lazima ufasiriwe katika ufahamu wa siku zake wenyewe na aina yake ya fasiri. Mkabiliano wa kihistoria kwa Ufunuo lazima ushughulikiwe na wasomaji wa kwanza wangefanya na wangelewa. Kwa namna nyingi wafasiri wa kisasa wamepoteza maana za viwakilishi vya kitabu. Msukumo mkubwa wa kwanza wa Ufunuo. Ulikuwa ni kutia moyo waamini watesekao. Ilicesha namna Mungu anavyoshughulikia historia (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale); Ilikiri kwamba historia inaenda kuelekea mwisho wa uteuzi, hukumu au baraka (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale). Ilikiri katika muktadha wa upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na utawala wa siku za mwisho wa kiyahudi wa karne ya kwanza!

Inafanya kazi katika njia hizihizi za kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inachukua mahangaiko ya kiulimwengu ya jumla ya mazuri na mabaya. Maeleo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yamepotea kwetu lakini yasiyo na nguvu wala ukweli wa kufariji. Wakati wafasiri wanajaribu kulazimisha maeleo ya ufunuo kwenye historia ya sasa, utaratibu wa fasiri za uongo!

Inawezekana kwamba maeleo ya kitabu yanaweza kufanyika fasihi isiyo ya kawaida tena (kama ilivyokuwa katika Agano la Kale kuhusiana na kuzaliwa, kuishi na kufa kwa Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha Waaminio kama walivyokabiliana na kuchinjwa na kiongozi mpinga-Mungu (kama vile II The.2) na desturi. Hakuna mtu anayeweza kujua kutimilizwa huku kwa kibayana kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko13; na Luka 21) na Paulo (kama vile I Kor. 15; I The. 4-5; na II The. 2) pia inafanya dhahiri kihistoria. Kudhania, kufikiria na mafundisho vyote hivi sio sahihi. Fasiri ya matukio ya siku za mwisho yanaruhusu mabadiliko. Mshukuru Mungu kwa taswira na viwakilishi ambavyo vinapita masimulizi ya kihistoria! Mungu anawawala na kushughulikia mabo yake; Anatawala; Anakuja!

Fasiri nyingi za kisasa zinakosa suala la uchaguzi wa aina ya fasihi ya uwasilishaji! Wafasiri wa kisasa wa Magharibi mara kwa mara wanatafuta mfumo sahihi uliowazi wenye mantiki wa kithiolojia kuliko kuchukuliana na aina ya fasihi yenye utata, wakilishi ya kitamthilia ya matukio ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezewa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake, "Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

"Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthilia wa maandiko haya na kukumbuka njia ambayo lugha inatumika kama chombo cha kuelezea ukweli wa kidini, tutakuwa tumefanya kosa kubwa sana katika uelewa wetu wa matukio ya siku za mwisho na kimakosa kujaribu kufasiri maono yake kana kwamba ni kitabu cha riwaya ya kawaida na kinachojihuisha kuelezea matukio ya kihalisia na historia inayoandikika. Kujaribu njia ya pili ni kukimbia katika kila mtindo wa matatizo ya fasiri. Zaidi sana inapelekea kwenye uharibifu wa maana ya msingi katika lugha za hadithi za kufikirika za Mungu

mtawala katika Kristo na fumbo la utawala wake ambao unaunganisha uweza na upendo (kama vile 5:5,6; Simba ndiye mwana kondoo)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake *Biblical Interpretations* alisema:

"Hakuna fasihi ingine ya Biblia ambayo imesomwa kwa dhati na shauku kubwa na kwa matokeo yenyekukatisha tama kama vitabu nya matukio ya siku za mwisho. Aina hii ya fasihi ilipata shida kutokana na historia ya kimajanga ya kufasiriwa vibaya kwasababu ya kukosekana kwa uelewa wa msingi wa muundo wake wa fasihi, mpangilio na kusudi. Kwasababu ya madai yake sana ya kufunua kile ambacho karibia kinatokea, vitabu nya mwisho wa ulimwengi vimekuwa vinatazamwa kama mwongozo kuelekeaa katika kuyajua juu mambo yajayo. Kosa kubwa zaidi katika mtazamo huu ni dhana kwamba muuundo wa vitabu nya rejea ni umri wa msomaji wa sasa kuliko kuwa wa mwandishi. Huu mkabiliano usio kuwa na mwongozo wa matukukio ya siku za mwisho (hasa Ufunuo) unaifanya kazi kama vile ni namba za siri ambazo matukio ya kisasa yanaweza kutumika kutafsiria viwakilishi nya andiko. . .Kwanza, mfasiri lazima atambue kwamba vitabu nya siku za mwisho vinazungumzia jumbe zake kupertia uwakilishi wa kiishara. Kufasiri ishara kibayana wakati inapokuwa kisitiari ni kupotosha fasiri. Tatizo sio kama matukio katika za mwisho ni ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa sio ya kihistoria; yanaweza kuwa kweli yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anayawasilisha na kuzungumza maana zake kupertia taswira na nadharia" (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, iliyohaririwa na Ryken, Wilhost na Longman III:

"Wasomaji wa leo mara kwa mara wanashangazwa na kuchanganywa na aina hii ya fasihi. Taswira isiyotegemewa na ya nje ya uzoefu wa ulimwengu huu. Kuichukilia Fasihi hii kwa inavyoonekana inawaacha wasomaji wengi wakikwaruza kwaruza wakiwa wamejizatiti 'nini kitatokea wakati,' hivyo kukosa kusudio la ujumbe wa maandiko ya siku za mwisho" (ukurasa wa 35).

### **MVUTANO WA TANO (ufalme wa mungu uliopo sasa lakini wa baadaye)**

Ufalme wa Mungu ni wa sasa na ni wa baadaye. Hili fumbo la kithiolojia linafanyika shabaha katika hatua ya matukio ya siku ya mwisho. Ikiwa mtu atategemea kutimilizwa kwa kibayana kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Israeli hivyo ufalme wa Mungu zaidi unafanyika urejesho wa Israeli kwenye eneo lao la kijiografia na utawala wa kabla wa kithiolojia! Hii ingepelekeea kwamba Kanisa kwa siri linanyakuliwa katika sura ya 5 na sura zilizosalia zinahusiana na Israeli (lakini angalia dokezo katika Ufunuo 22:16).

Hatahivyo ikiwa shabaha ipo katika ufalme kuanzhishwa na Masihi anayetabiriwa katika Agano la Kale, alafu lipo na kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo na alafu inaweka shabaha kwenye kufanyika mwili, maisha, mafundisho, kifo na kufufuka kwa Kristo. Msisitizo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa. Ufalme umekuja, Agano la Kale limetimilizwa katika kujitoa kwa wokovu kwa Kristo kwa wote na sio utawala wake wa Milenia na baadhi! Ni kwa kweli na hakika kwamba Biblia inazungumza juu ya ujio wote wa Kristo, lakini wapi ambapo msisitizo unawekwa? Inaonekana kwangu kwamba nabii nyngi za Agano la Kale zinalenga juu ya ujio wa kwanza, uanzishwaji wa ufalme wa Kimasihi (kama vile Danieli 2). Katika namna nyngi huu utawala wa Mungu unafananishwa na utawala wa milele wa Mungu (kama vile Danieli 7). Katika Agano la Kale shabaha ipo katika utawala wa Mungu wa milele, japo namna ya udhihirisho wa utawala huo ni huduma ya Masihi (kama vile I Kor. 15:26-27). Sio swali la nini ni kweli; vyote ni kweli lakini msisitizo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya wafasiri wanafanya kulenga kwenye utawala wa milenia wa Masihi (kama vile Ufunuo 20) kwamba wamekosa shabaha ya kibiblia juu ya utawala wa milele wa baba. Utawala wa Kristo ni tukio la kuanzia kama kiashiria. Kama kuja kwa mara mbili huku kwa Kristo hakukuwa dhahiri katika Agano la Kale, wala haitakuwa pia kutawala kwa muda kwa Masihi!

Msingi wa mahubiri na mafundisho ya Yesu ni ufalme wa Mungu. Ni vyote sasa (katika wokovu na huduma), na baadaye (katika utawala mkuu wa ulimwengu na nguvu). Ufunuo, ikiwa utalenga kwenye utawala wa kimasahi wa kimelenia (kama vile Ufunuo 20), itakuwa mwanzo tu na sio kilele (kama vile Ufunuo 21-22). Sio dhahiri kutoka katika Agano la Kale kwamba utawala wa muda ni mughimu; ukweli ni kwamba utawala wa Kimasahi wa Danieli 7, ni wa milele na wala sio wa ki-milenia.

### **MVUTANO WA SITA** (kurudi kwa hakika kwa Kristo dhidi ya kuchelewa *Parousia*)

Waamini wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, ghafla na bila taarifa (kama vile Mt. 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; angalia [Mada Maalum:Kurudi Punde](#)). Lakini katika kila kizazi kitarajachao cha waamini hata hivyo kimekosea! Ukaribu (uharaka) wa kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye nguvu lililohaidiwa kwa kila kizazi, lakini ukweli kwa mmoja tu (na yule aliyeteseka na huyo tu). Waaminio lazima waishi kama vile anarudi kesho, lakini apange na kufanya kazi Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20) ikiwa atakawia.

Baadhi ya vifungu katika Injili na I na II Wathesalonike wamejikita katika kukawia katika Kuja kwa Mara ya Pili (*Parousia*). Kuna baadhi ya matukio ya kihistoria ambayo lazima yatokee kwanza:

1. kuhubiriwa kwa injili ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
2. ufunuo “mwanadamu mdhambi” (kama vile Mt. 24:15; II The. 2; Ufunuo 13)
3. mateso makuu (kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (kama vile Mt. 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ni siku yako ya mwisho lakini panga na jifunze kwa ajili ya huduma yako ya baadaye!

### **MWENDELEZO NA UWIANO**

Lazima isemwe kwamba shule tofauti tofauti za fasiri za siku za mwisho zote zinajumuisha ukweli nusu. Wanaelezea na kufasiri vizuri baadhi ya maandiko. Tatizo linatokana na mwendelezo na uwiano. Mara kwa mara kuna mpangilio wa kauli za kupendekeza ambazo zinatumia maandiko ya kibiblia kujaza mafuvu yaliyowekwa kabla ya kithiolojia. Biblia haifunui mantiki, mtitiriko wa matukio na mfumo wa siku za mwisho. Iko kama albamu ya familia. Picha ni za kweli lakini siku zote hazipo katika mpangilio, katika muktadha katika mfuatano wa kimantiki. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka kwenye albamu na vizazi vya baadaye vya ndugu wa familia hawajui hakika namna ya kuzirudisha. Msingi wa fasiri sahihi wa Ufunuo ni kusudio la mwandishi wa asili kama inavyofunuliwa katika uchaguzi wake wa ina ya fasihi anayoitumia. Wafasiri wengi wanajaribu kubeba vifaa vyao vya kutenda kazi na taratibu kutoka katika aina zingine za fasihi za Agano Jipya kwenda kwenye fasiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha kwenye Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kupangilia muundo wa kithiolojia na kuruhusu Ufunuo kufanya kazi kama kielelezo.

Lazima nikiri kwamba naikabili fasiri hii juu ya Ufunuo nikiwa na baadhi ya uoga na wasiwasi si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini ni kwasababu ya kiwango cha mkanganyiko ulioletwa na ufasiri wa kitabu hiki na kuendelea kusababisha kati ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli wakati wanadamu wote wanakuwa waongo (kama vile Rum. 3:4)! Tafadhali tumia fasiri hii kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana ya mwisho kama kielekezi na sio mwongozo, kama “vipi ikiwa,” na sio “hivyo Bwana asema.” Nimekuja kugundua usio kwa uso mapungufu yangu mwenyewe, ubaguzi na ajenda ya kithiolojia. Lakini pia nimeona yale ya wafasiri wengine. Inakaribia kuonekana kwamba watu wanatafta Ufunuo kile wanachotegemea kukipata. Aina ya fasihi inajipelekea yenyewe katika matumizi mabaya!

Hata hivyo ipo katika Biblia kwa makusudi. Imewekwa katika kama hitimisho “neno” sio kwa ajali au

bahati mbaya. Ina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa watoto wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Tumuunge mkono, sio kutengeneza magenge; Ebu tukiri kile kilicho wazi na kilicho cha msingi na kikuu, sio yote yanaweza, yataweza au yangeweza kuwa kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

■ “**mataifa yote yataielekea**” Hiki KITENZI (BDB 625, KB 676, *Qal KAULI TIMILIFU*) kinaashiria kujaa kwa njia yam to wa maji, kama chemichemi za Artesian. Ni Sitiari ya kumiminika kwa watu kusikokoma kwa YHWH.

**2:3** Tazama ombi la mataifa.

1. “njoo,” BDB 229, KB 246, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. “Hima twendeni katika mlima wa BWANA,” BDB 748, KB 828, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU* ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI.
3. “kwamba atufundishe juu ya njia Zake,” BDB 434, KB 436, *Hiphil KAULI ISIO TIMILIFU* ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI
4. “kwamba tuweze kutembea katika njia zake,” BDB 229, KB 246, *Qal HALI YA KUSIHI*
5. “kwamba sheria (mafundisho) yatatangulia Sayuni,” BDB 422, KB 425, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU* ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI

■ “**njia Zake**” Neno hili (BDB 73) linatumika mara kadhaa katika Isaya (kama vile 2:3; 3:12; 26:7,8; 30:11; 33:8; 40:18; 41:3) na inatoka hasa katika Mithali (kama vile 1:19; 2:8,13,15,19,20; 3:6; 4:14,18; 5:6; 8:20; 9:15; 10:17; 12:28; 15:10,19,24; 17:23; 22:25). Kisitiari iliashiria mtindo wa maisha ya imani ambayo yalihiwa na kuenenda katika (kama vile Kutoka. 16:4; Isa. 30:20; 42:24; Yer. 9:12; 26:4; 32:23; 44:10,23; Zek 7:12) mafundisho ya Mungu. Sitiari hii ya mtindo wa maisha wa kuishi kwa uaminifu kulifanyika jina na wadhifa wa kwanza wa kanisa la Agano Jipya, “The Njia” (kama vile Yohana 14:6; Mdo 9:2; 19:9,23; 22:4; 24:14,22; 18:25-26)

■ “**Sayuni**” Yerusalem (kama Rumi) lilijengwa juu ya vilima saba. Sayuni (BDB 851, maana yake hajjulikani) kilikuwa kilima ambapo jiji la asili la Wakanaani liitwalo Yebusi au Salemu lilijengwa (kama vile I Wafalme 8:1; II Nyakati 5:2). Kama Yerusalem ilivyokua ilifanyika njia yay a kumaanisha jiji zima na hekalu (kama vile mstari wa 3, mstari wa 6 na 7; Yer. 50:28; 51:10).

**2:4 “Atahukumu. . .na kutoa maamuzi”** Hivi VITENZI viwili (BDB 1047, KB 1622 na BDB 406, KB 410) vinaelezea mantiki na maamuzi ya mtawala mwenye hekima. YHWH na Masihi wake ni watawala wenye hekima wa kilele!

■ Uwepo wa Bwana na mafundisho yatasababisha mataifa kuacha uvamizi wao juu ya watu wa Mungu (kama vile Zaburi 2; Ezekiel 38-39). Watatafta amani (kama vile 9:6-7; 11:6-9; 57:19; Hos. 2:18; Zekaria 9:10).

■ “**panga zao ziwe majembe**” Hii ni nahau kwa ajili ya amani. Kinyume chake kinatokea katika Yoeli 3:10

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:5-11**

<sup>5</sup> Enyi wa nyumba ya Israeli, njoni, twende katika nuru ya Bwana.

<sup>6</sup> Maana wewe umewaacha watu wako, nyumba ya Israeli,

kwa sababu wamejaa kawaida za mashariki,

nao ni wapiga ramli kama Wafilisti,

na wanapano mikono na wana wa wageni. <sup>7</sup> Tena nchi yao imejaa fedha na dhahabu,

wala hapana mwisho wa hazina zao;

tena nchi yao imejaa farasi,

wala hapana mwisho wa magari yao.

<sup>8</sup> Tena nchi yao imejaa sanamu;

huabudu kazi ya mikono yao,

vitu vilivofanywa kwa vidole vyao wenyewe.

<sup>9</sup> Mtu mnyonge huinama, na mtu mkubwa hujidhili;

kwa hiyo usiwasamehe.<sup>10</sup> Ingia ndani ya jabali;  
 ukajifiche mavumbini mbele za utisho wa Bwana,  
 mbele za utukufu wa enzi yake.<sup>11</sup>  
**Macho ya mwanadamu yaliyoinuka yatashushwa chini,**  
**na kiburi cha mwanadamu kitainamishwa,**  
**naye Bwana, yeye peke yake, atatukuzwa siku hiyo.**

**2:5** Tazama usambamba kati ya mstari wa 3 (mataifa) na mstari wa 5 (Wana wa Israeli). Mtindo wa maisha ya imani ni ushahidi wa uhusiano wa kibinagsi wa kutumaini katika Mungu. Wanadamu lazima waijue kweli, na kuishirikisha kwa wengine! Mataifa yalitakiwa kujifunza hili kutoka kwa Israeli, lakini hawakufany hivyo! Ile “nuru ya BWANA” ufunuo wa kweli (kama vile 60:1-2,19-20). Kuabudu nuru wakati wa anga la usiku ni ufunuo wa uongo. Mstari huu unaweza ukawa kukataliwa kwa ibada ya nyota na vitu vya anga kunakofanywa na Wa-Babeli (kama vile mstari wa 6). YHWH na Masihi wake ni nuru ya kweli kwa ajili ya mataifa (kama vile 9:2; 42:6; 49:6; 51:4; 53:11).

**2:6-9** Mistari hii inaelezea kwanini YHWH aliacha (BDB 643, KB 695, *Qal KAULI TIMILIFU*) watu wake mwenyewe wa Agano

1. Wamejawa na ushawishi kutoka mashariki, mstari wa 6.
2. Wao ni wapunga pepo (BDB 778 II), kama Wafilisti, mstari wa 6.
3. Wanaangalia makubaliano na watoto wa wageni, mstari wa 6.
4. Ni matajiri na wenye nguvu kijeshi (na wanatumaini katika vitu hivi), mstari wa 7 (tazama marudio ya pande tatu ya “kujazwa,” BDB 567, KB 583, *Niphal KAULI ISIO TIMILIFU* katika mistari ya 7 na 8).
5. Ni waabuduo sanamu, mstari wa 8 (kama vile 17:8; 37:19; 40:19; 44:17).
6. Wanawatenda watu wa kawaida na wasio na cheo kwa dharau, kama vile mstari wa 9 (kama vile mistari ya 11,17; Inawezekana kwamba mstari huu ni sambamba na mstari wa 8 inamaanisha ibada ya sanamu, kama vile toleo la NKJV). Tunaweza kujifunza nini kutoka katika hili?! Juu ya #6 hapo juu (mstari wa 9), toleo la NASB na la NKJV yanafasiri kama katika lingine katika mfululizo wa maelezo ya namna gani watu wa agano wanafanya kazi, lakini NRSV na TEV yanafasiri hili kama muhtasari na mstari wa mwisho ni ombi kwa YHWH, sio kuwasamehe (Peshitta) au kauli ya YHWH kwamba hatowasamehe (LXX)

**2:6**

<b>NASB, NRSV</b>	“ <b>kutoka mashariki</b> ”
<b>NKJV</b>	“ <b>njia za mashariki</b> ”
<b>TEV, JPSOA</b>	“ <b>kutoka mashariki</b> ”
<b>Peshitta</b>	“ <b>siku za zamani</b> ”
<b>REB</b>	“ <b>wafanya biashara</b> ”

Toleo la UBS Hebrew OT Text Project linatoa “kutoka mashariki” au “kutoka nyakati za zamani” (zote zenye maana zinazowezekana kuwa NOMINO, BDB 869) alama ya “B” (baadhi wana shaka). Toleo la NEB na REB yanaongeza konsonanti moja na kulifanya “wafanyabiashara.” Inaonekana kumaanisha ushawishi wa kidini kutoka mashariki (yaani Shamu, Ashuru, Babeli) ambayo yaliharibu imani ya Israeli.

▣“**wapiga ramli**” Ikiwa hii ilimaanishwa kuwa usambamba wa kimakini pamoja na mstari hapo juu, inawezekana kwamba Nomino sambamba na “wapiga ramli,” kama vile “waaguzi” (kama vile Mambo ya Walawi 19:26; Kumb. 18:9-12), kimakosa imetoka nje ya MT. Toleo la MT sio andiko la kiebrania la asili zaidi au la kale mwanzoni kabisa. Halina matatizo ya kimaandiko! Hatahivyo, kumbuka kwamba matatizo ya aina hii hayaathiri mafundisho makubwa.

<b>NASB</b>	“ <b>wanapatana na wana wa wageni</b> ”
<b>NKJV</b>	“ <b>wanapendezwa na wana wa wageni</b> ”

NRSV	“wanapiga makofi na wageni”
TEV	“wanafuata desturi za kigeni”
NJB	“inaendeshwa na wageni”
LXX	“watoto wa wageni wamezaliwa kwao”
Peshitta	“walizaa na kutunza watoto wengi wa wageni”
REB	“watoto wa wageni wako kila sehemu”
JPSOA	“wanadumu katika desturi za wageni”

Neno “watoto” halipo katika toleo la MT. Hiki KITENZI (1) “wanapiga mikono” (BDB 706 I, KB 765, *Hiphil KAULI ISIO TIMILIFU*) au (2) “kudumu” (BDB 974, kama vile NIDOTTE, vol. 3, ukurasa wa 1769) ni tata. Inaweza kumaanisha

1. muamala wa kibashara
2. muungano wa kisiasa
3. urafiki
4. uthibitisho wa desturi za wageni

Kidhahiri katika muktadha imani ya pekee inachakachuliwa!

**2:7** Maelezo haya ya uongozi wa kiyudea una mkanganyiko wa moja kwa moja katika Kumbu. 17:16-17. Wanadamu walio na rasilimali wanatabia ya kutumaini kwao (kama vile 31:1), lakini mstari wa 22 (kama vile 31:3) unaonesha kushindwa kutumaini katika rasilimali mwili na watu!

**2:9 “mtu. . .mtu”** Mstari wa 9 ni wa mistari miwili, yenye usambamba wa kisawe (kama vile II Wafalme. 7:10). Misamiati miwili ya zaidi kwa ajili ya mtu/mwanadamu ipo katika usambamba.

1. *adam*, BDB 9, kama vile Mwanzo 1:26; 6:1,5,6,7; 9:5,6
2. *ish*, BDB 35, Mwanzo 2:23; Hes 23:19

#### NASB, NKJV

NRSV, TEV	“usiwasamehe”
NJB, NIV	“usiwalee”
LXX	“usiwasamehe”
REB	(imeondoa kama chakavu, kama vile gombo la bahari ya chumvi na tanbihi ya JB)

Hiki KITENZI (BDB 669, KB 724, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU*) ikimaanisha “kuinua” au “kubeba.” Hapa ina namna ya “kubeba kwa kuondoa” (yaani kuondoa dhambi zao). Hii inaweza kuwa mshangao kutoka kwa Isaya mwenyewe

**2:10-11** Mistari hii miwili inaelezea ushauri wa YHWH kwa waasi/wavunjaji hawa wa agano (mstari wa 10a).

1. kuingia mwamba, BDB 97, KB 112, *Qal KAULI SHURUTISHI* (yaani hii inauhusiano na mistari ya 19-21, kama vile Ufunuo 6:15-17)
2. kuficha katika uvumbi, BDB 380, KB 377, *Niphal KAULI SHURUTISHI*

Wanatakiwa kuficha kutoka kwa (mstari wa 10b)

1. hofu ya Bwana, kama vile mistari ya 19,21
2. fahari ya Mfalme wake (kama vile mistari ya 11c, 19,21; II The. 1:9)

Matokeo yake yatakuwa (mstari wa 11, tazama katika usambamba mstari wa 17)

1. macho ya kiburi ya wanadamu yatashushwa, BDB 1050, KB 1631, *Qal KAULI TIMILIFU* (kinyume cha mstari wa 9)
2. kiburi cha mwanadamu kitanyenyekewa, BDB 1005, KB 1458, *Qal KAULI TIMILIFU* (kinyume cha mstari wa 9, kama vile 13:11; 23:9; II Kor. 10:5)
3. Bwana pekee atatukuzwa katika siku hiyo, BDB 960, KB 1305, *Niphal KAULI TIMILIFU* (tazama katika usambamba mstari wa 17 na tungo kuhusu “hofu” na “fahari” ya YHWH katika mistari ya 19c na 21b)

Baadhi ya Wafasiri wanafikiri kwamba mstari wa 10 unamuhimiza mwenye haki kujifisha mbali na hukumu ijayo ya YHWH juu ya waovu (kama vile NIDOTTE, vol. 2, ukurasa wa 377), lakini katika muktadha (yaani mstari ya 19-21) inamaanisha wavunjaji wa agano.

**2:11 “katika siku hiyo”** Hii inamaanisha siku za mwisho za mstari wa 2a. Inafanyika maudhui matawala katika Amosi. Dhamira ya Isaya inarudiwa katika mstari wa 12 (kama vile 2:20; 3:17; 5:30; 28:5-6; Amosi 2:16; 8:9; Hos. 2:18).

Uuumbaji tambuzi (wanadamu na malaika) siku moja watasimama mbele ya muumbaji wake na kutoa hesabu ya uwakili wao wa maisha. YHWH ni mwadilifu, Mungu mwenye maadili; uumbaji ni uadilifu, uumbaji wa kiadilifu. Wanadamu hawavunji sana sheria za Mungu sana kama wanavyojivunja wenyewe katika sheria za Mungu. Sheria ni kwa ajili ya ulinzi wake katika ulimwengu ulioanguka lakini wanadamu wanaona kama kuminywa kwa uhuru wao/kubanwa na kupoteza uhuru binafsi. Siku moja kila uumbaji wenyewe kujitambua, wanadamu na malaika watatoa hesabu yao mbele za Mungu!

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 2:12-22**

<sup>12</sup> Kwa maana kutakuwa siku ya Bwana wa majeshi juu ya watu wote wenyewe kiburi na majivuno,

na juu ya yote yaliyoinuka;

nayo yatashushwa chini.

<sup>13</sup> Na juu ya mierezi yote ya Lebanon iliyo mirefu na kuinuka,

na juu ya mialoni yote ya Bashani;

<sup>14</sup> na juu ya milima mirefu yote,

na juu ya vilima vyote vilivyoinuka;

<sup>15</sup> na juu ya kila mnara mrefu,

na juu ya kila ukuta ulio na boma;

<sup>16</sup> na juu ya merikebu zote za Tarshishi,

na juu ya kila taswira ipendezayo.

<sup>17</sup> Na majivuno ya mwanadamu yatainamishwa,

na kiburi cha watu kitashushwa;

naye Bwana, ye ye peke yake, atatukuzwa siku hiyo.

<sup>18</sup> Nazo sanamu zitatoweka kabisa.

<sup>19</sup> Na watu wataingia ndani ya pango za majabali,

na ndani ya mashimo ya nchi,

mbele za utisho wa Bwana na utukufu wa enzi yake,

Atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia.

<sup>20</sup> Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha,

na sanamu zake za dhahabu,

walizojifanya ili kuziabudu, kwa fuko na popo;

<sup>21</sup> ili aingie ndani ya pango za majabali,

na ndani ya tundu za miamba iliyopasuka,

mbele za utisho wa Bwana na utukufu wa enzi yake,

atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia.

<sup>22</sup> Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi yake i katika mianzi ya pua yake;

kwa maana hudhaniwaje kuwa ni kitu?

**2:12-13** Tambua matumizi ya kurudiwa ya maneno yakiashiria kiburi, wanadamu na mataifa yenye majivuno.

1. “yeyote mwenye kiburi” (BDB 144)
2. “na mwenye kiburi” (BDB 926, KB 1202, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU* (tazama muundo huo huo katika mistari ya 13, 14), mstari wa 12
3. “yeyote aliyeinuliwa” (BDB 669, KB 724, *Niphal KAULI TENDAJI ENDELEVU* (tazama muundo ule ule katika mistari ya 13,14), mstari wa 12
4. “miti yote ya Lebanon yenye viburi na kuinuliwa,” mstari wa 13 (sitiari kwa ajili ya binadamu na mataifa)

**2:12 “Kwa maana kutakuwa siku ya Bwana wa majeshi juu ya watu wote wenyе kiburi na majivuno”** Hii haifuatishi andiko la Kiebrania. Toleo la MT lina “Kwa maana siku ya BWANA wa majeshi” (kama vile NKJV). Fasiri ya NASB inajaribu kuunganisha hili kwa 1:18.

**2:12-16** Tazama matumizi ya kurudiwa rudiwa ya “dhidi” (BDB 752).

1. dhidi ya kila mtu mwenye majivuno na kiburi, mstari wa 12
2. dhidi ya wote waliojiinua, mstari wa 12
3. dhidi ya miti yote ya Lebanoni yenyе maivuno na kujiinua, mstari wa 13
4. dhidi ya mikuyu yote ya Bashan (ambayo pia inakiburi na kujiinua), mstari wa 13
5. dhidi ya milima yenyе viburi, mstari wa 14
6. dhidi ya vilima vilivyo inuliwa, mstari wa 14
7. dhidi ya kila mnara mrefu, mstari wa 15
8. dhidi ya kila kuta zenyе ngome, mstari wa 15
9. dhidi ya meli zote za Tarshishi, mstari wa 16
10. Dhidi ya mbinu zote zenyе kupendeza, mstari wa 16 (neno hili “mbinu” [BDB 967] linatokea hapa tu na maana yake haijajulikana; inaonekana kuwa sambamba na “meli za Tarshishi” katika mstari wa 16a) Bwana huwapinga wenyе viburiu (kama vile mistari ya 11 na 17).

**2:13** Kwasababu ya maelezo juu ya ibada ya sanamu ya miti (1:29) na bustani (1:29-30) na kwamba YHWH atawachoma moto, mtu aweza kushangaa ikiwa kutajwa huku kwa miti yenyе viburi inaaksi

1. majivuno na kiburi cha mataifa
2. ibada ya sanamu iliyounganishwa na miti

Kwasababu ya muktadha pana (yani mfululizo wa “dhidi”) mbadala wa kwanza unaonekana kuwa bora. Tatizo la kiburi cha wanadamu linawekwa kimutahsari katika mstari wa 17 (ambayo inaweza kuwa dhima ya kitabu kizima).

**2:16 “na juu ya merikebu zote za Tarshishi”** Angalia kidokezo katika 23:1.

**2:17** Hili ni wazo sambamba kwa mstari wa 11, ambayo ni kinyume cha kile viongozi waovu na jamii tajiri walifanya kwa maskini na wanyenye kevu katika mstari wa 9. Wengi wanaona mstari huu kama dhima ya kimuhtasari wa kitabu kizima!

**2:18** Kuabudu sanamu kutakoma moja kwa moja (kama vile 21:9) kwasababu ya kuabudu kwao “utupu” (kama vile 30:22; 31:7; 40:18-20; 44:9-20; 46:5-7)!

**2:19 “atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia”** KITENZI cha kwanza “inuka” (BDB 877, KB 1086, *Qal* TUNGO ISIYO NA KIKOMO) inaweza kuashiria

1. Kutokeka katika tukio, Kut. 1:8; Kum. 34:10; Waamuzi 5:7; II Wafalme 23:25
2. inuka kwa ajili ya tendo (kutoka katika Enzi yake), Hesabu 10:35; II Nyakati 6:41; Ayubu 31:14; Zab 76:9; 132:8

KITENZI cha pili “kutetemeka” (BDB 791, KB 888, *Qal* TUNGO ISIYO NA KIKOMO) inaelezea uumbaji wa kimwili kama mmuumbaji wake anavyo karibia (kama vile 13:13; 24:1,19,20; Zab. 18:7; 68:7-8; Hag. 2:6). YHWH anaweza kuja kwa ajili ya Baraka au hukumu. Katika muktadha huu ni kwa ajili ya hukumu!

**2:20-21** kufafanua mstari wa kwanza wa mstari wa 10, wanadamu watajaribu kukimbia mbali na Mungu

1. katika mapango katika miamba (kama vile mstari wa 21)
2. katika mashimo ya ardhi

Watajaribu kuondoa miungu yao ya sanamu ya thamani

1. kuondoa mashushushu (maana ya neno haijulikani. LXX lina “ubatili”; REB ina “wanyama wasukumao mavi ya ng’ombe”; JPSOA lina “mbweha wapao” [aina ya popo, hivyo sambamba na mstari wa pili wa ushairi]. Inaonekana kuhusiana na KITENZI “kuchimba” [BDB 343])
2. kuondolea kwa popo

Mistari hii miwili ni mfuatano wa TUNGO ZISIZO NA UKOMO .

1. kuabudu (kifasihi, “kuabudu”), BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* TUNGO ISIYO NA UKOMO

2. kwa mashushushu (kifasihi. “kuchimba”), BDB 343, KB 340, *Qal TUNGO ISIYO NA UKOMO*
3. kuelekea ndani, BDB 97, KB 112, *Qal TUNGO ISIYO NA UKOMO*
4. kuinuka, BDB 877, KB 1086, *Qal TUNGO ISIYO NA UKOMO*, yenyé muundo uleule sawa na mstari wa 19 (mstari wa 5)
5. kutetemeka (kifasihi. “kuogopesha,” BDB 791, KB 888, *Qal TUNGO ISIYO NA UKOMO*, sawasawa na mstari wa 19 (mstari wa 5)

Katika toleo la IVP *Bible Background Commentary* “Tenzi za kisumeri za wa- Enheduanna kwa miungu ya kike ya Inanna kutoka katika milenia ya tatu inaelezea miungu ya kutetemeka kama popo waelekeao katika mashimo yao kutokakatika uwepo wa mungu mke wa kutisha” (ukurasa wa 588). Hii inamaana kwamba inatakiwa ibakie uwezekana kwamba ni sanamu zenyewe kwamba walichukuliwa na wadudu (wadudu wasukumao mavi ya ng’ombe) au wanyama wachimbao wakitafuta mahali salama kutoka kwa ujio wa YHWH kwasababu hawakuwe kutembea wenyewe.

**2:22** YHWH anaamuru heshima kwa maisha ya kibinadamu (“kukomesha,” BDB 292, KB 292, *Qal KAULI SHURUTISHI*) kwasababu inategemeana na zawadi ya Mungu ya uhai (“kupulizia pumzi,” *ruah*). Mwanadamu anahama (cf. Ps.kama vile Zaburi 144:3-4) Huu ni ukweli ambao nadharia ya kutoamini kuwepo kwa Mungu kunakohitaji kusikiwa!

## ISAYA 3

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mungu atawaondo Viongozi	Hukumu juu ya Yuda na Yerusalemu	Utwala huria katika Yerusalemu	Machafuko huko Yerusalemu	Utwala huria katika Yerusalemu
3:1-12 (1b-12)	3:1-9 (1-3)	3:1-15 (1-5)	3:1-5	3:1-15 (1-15)
	(4-5) (6-7) (8-9)	(6-8) (9-12)	3:6 3:7 3:8-9	
	3:10-12 (10-12)		3:10-11	
			3:12a 3:12b	
Mungu atahukumu	Ukandamizaji na starehe Zalaaniwa		Bwana awahukumu watu wake	
3:13-15 (13-15)	3:13-4:1 (13-15)	(13-15)	3:13-15	
Wanawake wa Yuda Washtumiwa		Unyanyasaji wa wanawake wa Yerusalemu	Onyo kwa wanawake wa Yerusalemu	Wanawake wa Yerusalemu
3:16-26 (16-17) (24-26)	(16-17) (18-23) (24-26)	3:16-4:1 (16-17) (24b-4:1)	3:16-17 3:18-23 3:24 3:25-4:1	3:16-17 (16-17) 3:18-23 3:24 (24) Mateso huko Yerusalemu 3:25-4:1 (25)
	(4:1)			

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkaao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 3:1-12

<sup>1</sup> Kwa maana, tazama,

Bwana, Bwana wa majeshi,

awaondolea Yerusalem na Yuda egemeo na tegemeo;

tegemeo lote la chakula na tegemeo lote la maji;

<sup>2</sup>mtu hodari na mtu wa vita; mwamuzi na nabii;

mpiga ramli na mzee;

<sup>3</sup>jemadari aliye juu ya watu hamsini,

na mtu mstahifu, na mshauri, na fundi aliye mstadi,

na mganga ajuaye uganga sana.

<sup>4</sup>Nami nitawapa watoto kuwamiliki,

na watoto wachanga kuwatawala.

<sup>5</sup>Nao watu wataonewa, kila mtu na mwenziwe,

na kila mtu na jirani yake;

mtoto atajivuna mbele ya mzee,

na mtu mnyonge mbele ya mtu mwenye heshima.

<sup>6</sup>Mtu atakapomshika ndugu yake ndani ya nyumba ya baba yake,

akisema, Wewe una nguo, ututawale wewe;

na mahali hapa palipobomoka pawe chini ya mkono wako;

<sup>7</sup>basi, siku ile atainua sauti yake, akisema, Mimi sitakuwa mponya watu;

kwa maana ndani ya nyumba yangu hamna chakula wala mavazi;

wala hamtanifanya kuwa mtawala juu ya watu hawa.

<sup>8</sup>Kwa maana Yerusalem umebomolewa na Yuda wameanguka,

kwa sababu ulimi wao na matendo yao ni kinyume cha Bwana,

hata wayachukize macho ya utukufu wake.

<sup>9</sup>Kuonekana kwa nyuso zao kwashuhudia juu yao,

wafunua dhambi yao kama Sodoma, hawaifichi.

Ole wa nafsi zao, kwa maana wamejilipa nafsi zao uovu.

<sup>10</sup>Waambieni wenye haki ya kuwa watakuwa heri,

kwa maana watakula matunda ya matendo yao

<sup>11</sup>Ole wake mtu mbaya; shari itakuwa kwake,

kwa maana atapewa ijara ya mikono yake.

<sup>12</sup>Katika habari za watu wangu, watoto ndio wanaowaonea,

na wanawake ndio wanaowatawala. Enyi watu wangu,

wakuongozao wakukosesha, waiharibu njia ya mapito yako.

**3:1** Sura ya tatu inaendeleza utabiri wa unabii wa hukumu ya YHWH juu ya Yerusalem na Yuda.

▣“**Bwana Mungu wa majeshi**”Cheo kwa ajili ya Mungu wa Israeli kimetumika mara kadhaa mwanzoni mwa kitabu cha Isaya (kama vile 1:24;3:1;10:16,33;19:4).Angalia maelezo kamili katika 1:24 na Mada Maalum katika 1:1

▣ “anawaondolea” KITENZI hiki (BDB 693, KB 747, *Hiphil WAKATI ENDELEA*) katika shina la neno *Hiphil* likimaanisha “kuondoa” au “kuhamisha.”

1. YHWH kuondoa ugonjwa wa Israeli, Kut. 23:25; Kumb. 7:15
2. Israeli kuondoa vitu vilivyo laaniwa (yaani., dhambi ya Akani), Yosh 7:13
3. Israeli kuiweka mbali miungu ya kigeni, Amu. 10:16
4. Sauli kuwaondolea wenyepopo na wachawi, I Sam. 28:3
5. Watu binafsi wakuondolewa sheria za Mungu, II Sam. 22:23; Zab. 18:23

Lakini kumbuka hapa ni Mungu mwenyewe aliondoa msaada wa Yuda, nguvu na uongozi wa ibada za kisanamu.

1. Tegemeo (hasa “kiongozi,” BDB 1044) la chakula, mst. 1
2. Tegemeo (hasa “kiongozi”) la maji, mst. 1
3. Mtu hodari, mst. 2
4. Mtu wa vita, mst. 2
5. mwamuzi, mst. 2
6. nabii, mst. 2, kama vile. 9:14-15; 28:7; 29:10
7. mpiga ramli, mst. 2
8. mzee, mst. 2, kama vile. 9:14-16
9. jemedari a watu hamsini, mst. 3
10. mtu mstahifi, mst. 3
11. mshauri, mst. 3
12. fundi stadi, mst. 3, kama vile 40:20 (mtengeneza sanamu)
13. mganga aliye mganga, mst. 3

kumbuka, hukumu ilikuwa ya YHWH, mzazi mwenye upendo, mwenye kuwafunza nidhamu wanawe ili kwamba wawehodari, wenyefuraha, na mwanga kwa mataifa. Uangalizi wake binafsi kwa Yuda ilikuwa ni alama ya upendo na uhusika wake. Aliwapenda kiasi kwamba hakutaka kuwaacha katika dhambi zao!

### MADA MAALUM: HAKIMU, HUKUMU, NA HAKI (עִשְׁׁרָה) KATIKA ISAYA

Hili ni neno lililotumika kwa upana sana (BDB 1047, KB 1622) katika Agano la Kale. Toleo la NIDOTTE, juzu ya 4, uk. 214, limeainisha mgawanyo wake na umuhimu wake.

Torati, 13%, waamuzi wa kibinadamu

Viatabu vya kihistoria, 34%, viongozi wa kibinadamu

Vitabu vya hekima, 22%, kazi za kiungu

manabii, 31%, hasa kazi za kiungu

kumbuka jedwali lifuatalo kutoka kitabu cha Isaya:

YHWH kama mwamuzi	Mesih kama mwamuzi	Israel's Ideal Judges	Wamuzi bora wa Kiisraeli
2:4	9:7	1:17	1:23
3:14	11:3, 4	26:8	3:2
4:4	16:5	56:1	5:7
5:16	32:1	58:2, 8	10:2
28:6, 17, 26	40:14		59:4, 9, 11, 14, 15
30:18	42:1, 3, 4		
33:5, 22	51:4, 5		
61:8	53:8		
66:16			

Israeli ilipaswa kuaksi tabia ya YHWH kwa mataifa. Ilishindwa, kwa hiyo YHWH akainua Mwisraeli mmoja "bora" kutimiliza ufunuo binafsi ulimwenguni (yaani., Masihi, Yesu wa Nazareti, Kristo Yesu, kama vile Isa. 52:11-53:12)!



NASB

“yote ruzuku na tegemeo”

NKJV

“akiba na hazina”

NRSV	<b>“tegemeo na egemeo”</b>
TEV	<b>“ni kila kitu na kila mmoja ambaye watu humtegemea”</b>
NJB	<b>“ni rasilimali na mtoaji”</b>
LXX	<b>“mtu hodari na mwanamke hodari”</b>
Peshitta	<b>“riziki na egemeo”</b>
REB	<b>“kila tegemeo na riziki”</b>

Andiko la Kimasoreti lina muundo wa JINSI YA KIKE na JINSI YA KIUME ya neno משעו, ambalo BDB inalielezea kama “egemeo na tegemeo”(kama vile II Sam. 22:19). Katika kitabu cha Walawi 26:26 ni “tegemeo la chakula.”

### 3:3

NASB	<b>“mganga aliye mganga”</b>
------	------------------------------

NKJV, NRSV,

REB	<b>“mganga stadi”</b>
TEV	<b>“kila mmoja atumiaye uganga kudhibiti matukio”</b>
NJB	<b>“mpiga ramli”</b>
LXX	<b>“mponyaji hodari”</b>
Peshitta	<b>“mshauri stadi”</b>

NOMINO (BDB 538) inamaanisha “kuashiria” au “mcheshi.” Mwanzoni lilirejerea kucheza na nyoka (kama vile Zab. 58:6; Mhu. 10:11; Yer. 8:17). Lilikuwa kuashiria mazunguzo laini (kama vile 26:16; II Sam. 12:19; Zab. 41:8). Neno lile lile linatumika katika 3:20 kwa ajili ya hirizi zilizovaliwa na wanawake wa Yudea. Linarejerea kwenye masuala ya kiganga na hirizi, zilizokuwa zimekatazwa kwa Israeli na Yuda.

**3:4** Uongozi wa wazee wa Yuda wataondoshwa (na YHWH mwenyewe) hata kwa viwango vya juu. Vijana wasiozaa matunda na wasi na maana ndio wataongoza (kama vile Mhu. 10:16).

□

NASB	<b>“wana”</b>
NKJV, NRSV	<b>“watoto”</b>
NJB	<b>“vijana”</b>
LXX, Peshitta	<b>“wenye kudihaki”</b>

Tofauti ni kati ya andiko la Kimasoreti (BDB 760, “ukware,” kama vile Kumb. 22:14,17; Zab. 141:4) Na kusahihishwa kuelekea neno (BDB 760, “watoto,” kama vile Zab. 8:3). Yote yanaonekana kustahili katika muktadha.

**3:5-6** Ukandamizaji na dhuluma vimeelezewa.

1. Kukandamizana kati ya mtu na mtu
2. Kukandamizwa na majirani
3. Mivutano ya vizazi hadi vizazi
4. Mivutano ya kijamii
5. Mivutano ya kifamilia

**3:7-12** Mtu wa familia atakaye chaguliwa kuongoza hataikubali nafasi hiyo kwa sababu ya vurugu zinazoendelea (Yuda amejeruhiwa[1:6], ni Mungu tu awezaye kuponya [30:26] na familia (yaani., Yuda) kuasi dhidi ya YHWH.

1. Ulimi wao ni kinyume na YHWH, mst. 8
2. Matendo yao ni kinyume na YHWH, mst. 8
3. Wanaasi dhidi ya uwepo wake wa utukufu, mst. 8
4. Upendeleo washuhudiwa nyusoni mwao, mst. 9
5. Uovu wao waonyeshwa kama wa sodoma, mst. 9
6. Wamejilipa nafsi zao uovu, mst. 9

7. Huvuna kile wanachokipanda, mistari. 10-11
  - a. haki
  - b. uovu
8. wanakandamizwa na viongozi vijana (kama vile mst. 4), mst. 12
9. wanatawaliwa na wanawake, mst. 12
10. wawaongozao huwapotosha, mst. 12
11. huiharibu njia ya mapito yao, mst. 12

athari hizi za uasi ni ushahidi wa Kumb. 28:15-68.

Toleo la JPSOA linaiweka mistari ya 10 na 11 katika mabano.

### 3:8

<b>NASB, NRSV</b>	<b>“uwepo wa utukufu wake”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“macho ya utukufu wake”</b>
<b>TEV</b>	<b>“Mungu mwenyewe”</b>
<b>NJB</b>	<b>“kuangalia kwa utukufu wake”</b>
<b>LXX</b>	<b>“utukufu wao”</b>
<b>Peshitta</b>	<b>“ukuu wa utukufu wake”</b>
<b>REB</b>	<b>“utukufu wake”</b>

Andiko la Kimasoreti linafuatiwa kwa karibu na toleo la NKJV. Neno “macho” linawasilisha uwepo binafsi wa Mungu. Neno “utukufu” (*kabod*, BDB 458)ni neno la kawaida, lakini lenye elimu-maana pana.

## MADA MAALUM: UTUKUFU

Dhana ya kibiblia ya neno “utukufu” ni ngumu kuielezea. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yalitumia neno *doxa* kutafasiri yapata maneno ishirini ya Kiebrania. Limetumika mara nyingi kote katika agano Jipywa kwa namna mbali mbali. Limetumika kwa Mungu, Yesu, mwanadamu, na ufalme wa Kimasihi.

Katika Agano la Kale neno lililokuwa likijulikana kwa ajili ya neno “utukufu” (*kabod*, BDB 458, KB 455-458) mwanzoni lilikuwa ni neno la kibashara kwa joji ya vipimo (“kuwa na uzito,” KB 455). Kile ambacho kilikuwa ni kizito kilihesabiwa kuwa cha thamani. Mara nyingi dhana ya mng’aro iliongezwa kwenye neno kuelkezea ukuu wa Mungu (kama vile Kut. 19:16-18; 24:17; 33:18; Isa. 60:1-2). Yeye pekee ndiye wa thamni na mwenye kuheshimiwa (kama vile Zab. 24:7-10; 66:2; 79:9). Aling’aa zaidi kwa mwanadamu kuweza kustahimili, hivyo akaamua kufunikwa na wingu, au moshi (kama vile Kut. 16:7,10; 33:17-23; Isa. 6:5). YHWH kiukweli aweza tu kujulikana kupitia Kristo (kama vile Yohana 1:18; 6:46; 12:45; 14:8-11; Col.1:15; 1 Tim. 6:16; Heb. 1:3; 1 Yn 4:12).

Kwa ajili ya mjadala kamili wa neno *kabod*, angalia Mada Maalum: Utukufu (Agano la Kale). Utukufu wa waamini ni kuwa waweze kuielewa injili na utukufu katika Mungu, na sio ndani yao wenywewe (kama vile 1 Kor. 1:29-31; Yer. 9:23-24). Kwa maelezo zaidi, angalia NIDOTTE, juzu ya 2, kur. 577-587.

**3:9 “Kuonekana kwa nyuso zao kwashuhudia juu yao”** Matoleo ya Kialama Targums yana kifungu “upendeleo katika kutoa hukumu (dhuluma za kisheria na rushwa) zinawahukumu.” Huu wavezakuwa ni mchezo juu ya macho ya Bwana yaliyotajwa katika mst. 8 dhidi ya mtizamo wa watenda dhambi ya Yudea katika mst.9.

▣**“wafunua dhambi yao kama Sodoma”** Tena, kama ilivyo katika 1:10, Isaya analinganisha dhambi za jamii ya Yudea na dhambi za Sodoma (kama vile Mwanzo 19). Hawa viongozi wa Yudea (na familia zao) walikuwa wanalingishia waziwazi kiburi chao, mali walizo nazo na kuwanyonya walio dhaifu na wasio na kitu kwenye jamii. Sodoma ilikuwa na majivuno (Ezek. 16:50) na YHWH akawaangamiza, vivyo hivyo, kwa Yuda (mst. 16) na wao pia wataangamizwa (mistari ya 16-26, somo linaanzia toka kwa wanawake wenye majivuno mpaka Yerusalemu yenye majivuno).

▣ “**wamejilipa nafsi zao uovu**” Wanavuna kile walichopanda (kama vile mistari ya 10-11). Hii ni kanuni ya kiroho. Mungu ni mwadilifu na hata uumbaji wake. Wanadamu hujiondoa wenyewe kutoka katika vipimo vya Mungu. Tunavuna kile tulichopanda. Hili ni kweli kwa waamini(lakini haiathiri wokovu) na wasio waamini (kama vile Ayubu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mith. 24:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; I Kor. 3:8; II Kor. 5:10; Gal. 6:7-10; II Tim. 4:14; I Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).

### 3:12

**NASB, NKJV,**

NRSV	“ <b>watoto ndio wanaowaonea,na wanawake ndio wanaowatawala</b> ”
TEV	“ <b>wakopeshaji wanawaonea watu wangu na wanaowakopesha huwalaghai</b> ”
NJB	“ <b>wale wanaowaonea huwaibia, na wapokonyaji huwatawala juu yao</b> ”
LXX	“ <b>watozaji huwabana ninyi na wapokonyaji huwatawala juu yenu</b> ”
Peshitta	“ <b>wana wa wafalme huwadondosha, na wanawake watawatawala ninyi</b> ”
REB	“ <b>wakopeshaji huwabana watu wangu waziwazi, na kuwatoza riba juu yao</b> ”
JPSOA	“ <b>watawala wa watu wangu ni watoto, na wanawake ndiyo huwatawala</b> ”

Andiko la Kimasoreti lina neno “watu wangu,wanaowaonea,watoto na wanawake watawatawala.” Kwa uwazi kabisa matoleo ya TEV, NJB, na REB yanafuatisha tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania (hubadilisha “wanawake,” נִשְׁמָת, BDB 61 kwenda “wakopeshaji” [1] BDB 673 I, kama vile 24:2, KAULI TENDAJI YENYE HALI YA KUENDELEA UMOJA na neno אֲשֶׁר, kama vile 24:2 or [2] BDB 674 I, KAULI TENDAJI YENYE HALI YA KUENDELEA UMOJA na neno נֵשֶׁה, kama vile Kut. 22:25).

Hivi vifungu vingalikuwa

1. kiuhalisia
    - a. mwana wa mfalme
    - b. akidhibitiwa na
      - (1) “mama malkia” mwenye nguvu
      - (2) wakeza wana wa mfalme
      - (3)wanawake katika mahakama
- Stiari ya wiki na uongozi uliozoleka



NASB, NRSV	“ <b>kanganya</b> ”
NKJV	“ <b>angamiza</b> ”
NJB	“ <b>futilia mbali</b> ”
LXX	“ <b>potosha</b> ”
Peshitta	“ <b>sumbuliwa</b> ”
REB	“ <b>kuharibu</b> ”

KITENZI (BDB 118, KB 134, *Piel* WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kuzingira” au “kumeza” (kama vile Kut. 15:12;Hes. 16:30,32,34; 26:10; Kumb. 11:6). Katika shina la neno *Piel* pia linamaanisha “kupunguka,” lakini pia linatumika kama stiari kwa ajili ya maangamizo au kitu Fulani kinachochanganya (kama vile 9:16; 19:3; 28:7). Wanazuoni bado wangali wakijadili uwezekano wa ufanano/mizizi mmoja, miwili, au mitatu ya Kiebrania yenye kutumia herufi zile zile tatu (בַּלְעָם).

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 3:13-15

<sup>13</sup>Bwana asimama ili atete, asimama ili awahukumu watu.<sup>14</sup>Bwana ataingia katika kuwahukumu wazee wa watu wake na wakuu wao; Ninyi ndinyi mliokula shamba la mizabibu; vitu mliviyowateka maskini vi ndani ya nyumba zenu. <sup>15</sup>Ni nini maana yake, ninyi kuwaonea watu wangu, na kuseta nyuso za maskini? Asema Bwana, Bwana wa majeshi.

**3:13-15** YHWH anaingia kwenye mjadala (yaani eneo la mahakama, kama vile 1:2) na viongozi wa watu wake (wazee na wana wa wafalme). Wameiangamiza jumuiya yake (yaani., “mizabibu,” mst. 14). Wamechukua fursa za maskini, wanyonge, na wasiojiweza katika jamii.

Wanatumia muundo wa kisheria visivyo (kama vile mst.9) kwa faida yao , na sasa lazima wasimame mbele ya hukumu ya YHWH.

Manabii wanashikiria uwajibikaji wa Israeli/Yuda kwenye matakwa ya agano la Musa, utii umekuwa na matokeo na kutokutii kumekuwa na matokeo!

### 3:13

NASB, NKJV,

TEV, NJB,

LXX, Peshitta,

REB                  “**watu**”

NRSV                “**watu**”

HALI YA UMOJA inakuja toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yakifuatiwa na toleo la Peshitta. Andiko la Kimasoreti lina HALI YA WINGI. Katika muktadha huu HALI YA UMOJA inafaa zaidi kwa sababu nabii anawaelezea Wayudea (yaani., mst.14). katika muktadha mwagine kwenye Isaya”mataifa,” “**watu**,” umetumika. Muktadha, muktadha, muktadha! Andiko la Kimasoreti halina makosa! Muktadha lazima uwe kiongozi cha mwisho!

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 3:16-26

<sup>16</sup>Bwana akasema tena, Kwa sababu binti za Sayuni wana kiburi, na kuenenda na shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao; <sup>17</sup>Basi, kwa hiyo, Bwana atawapiga binti za Sayuni kwa pele za utosini, na Bwana ataifunua aibu yao. <sup>18</sup>Siku hiyo Bwana atawaondolea uzuri wa njuga zao, na kaya zao; <sup>19</sup>na pete za masikio, na vikuku, na taji zao; <sup>20</sup>na dusumali, na mafurungu, na vitambi, na vibweta vya marashi, na matalasimu; <sup>21</sup>na pete, na azama, <sup>22</sup>na mavazi ya sikukuu, na debwani; na shali, na vifuko; <sup>23</sup>na vioo vidogo, na kitani nzuri, na vilemba, na utaji. <sup>24</sup>Hata itakuwa ya kuwa badala ya manukato mazuri kutakuwa uvundo, na badala ya mishipi, kamba; na badala ya nywele zilizosukwa vizuri, upaa; na badala ya kisibau, mavazi ya kigunia; na kutiwa alama mwilini kwa moto badala ya uzuri. <sup>25</sup>Watu wako waume wataanguka kwa upanga, na mashujaa wako vitani. <sup>26</sup>Na malango yake yatalia na kuomboleza, naye atakuwa ukiwa, atakaa chini.

**3:16-26** YHWH anawashutumu wake na mabinti wa viongozi wasomi, na wenye mali.

1. Kuenenda kwa kiburi (“vichwa juu” au “shingo zilizonyooshwa”)
2. Walaghai (yaani., wenye macho ya kutamani)
3. Wenye hatua za madaha (yaani., hatua fupi, za haraka, kama mtoto)
4. Wenye kuvutia, wakiwa na jnuga miguuni mwao

YHWH will (mgeuzo halisi wa kibibia)

1. Atawapiga kwa pele (hapa tu, BDB 705, KB 764)
2. Atawaondolea njuga zao
3. Atawaondolea mavazi ya sikukuu
4. Atawaondolea marashi yao
5. Atawaua waume zao na wapendwa wao

Usomaji wa Biblia ya Kiyahudi, ukitumia tafasiri ya toleo la JPSOA na tanbihi, ikitaja kuwa wingi wa vitu katika mistari ya 18-24 hajulikani. Yaweza kurejerea kwenye vitu maalum vya urembo au alama za ibada za sanamu. Zilizokuwa zikivaliwa na wababa na wamama.

### 3:16

NASB, NJB                “**kuliza njuga**”

NKJV, Peshitta            “**kupiga njuga**”

NRSV                    “**kuliza njuga**”

TEV                      “**huliza vikuku vilivyoko miguuni mwao**”

KITENZI (BDB 747, KB 824, *Piel* CHA WAKATI USIOTIMILIFU) kinaonyesha sauti inayotolewa na njuga kwa namna mtu anavyotembea (yaani., kuvuta usikivu). Mzizi unapatikana hapa na Mhu. 7:22.

**3:17**

**NASB, NJB,**

**REB** “**huziacha nyuso zao wazi**”

**NKJV** “**huzifunua sehemu zao za siri**”

**NRSV, Peshitta** “**huziacha wazi sehemu zao za siri**”

**TEV** “**hunya nywele zao na kuacha upara**”

**LXX** “**huacha wazi sura zao**”

Andiko la Kimasoreti linatumia neno adimu (BDB 834) lenye kumaanisha

1. matundu (kwa ajili ya mlango), I Fal. 7:50
2. sehemu za siri (viungo vya uzazi vya mwanamke), Isa. 3:17 (?)

kuna mzizi wa lugha ya Akkadia (KB 983) wenye kumaanisha “paji la uso,” ambao pia ni chaguo. Majivuno haya, kuvala vizuri, wanyonyaji wa mali watanyenyekea!

**3:18 “njuga”** Fasihi ya awali ya Biblia inayasema haya yanarejerea “pambo la juu.” Kama ilivyo kwa “pambo la mwandamo wa mwezi” huu uwaksishaji wa kuuabudu mwezi humaanisha kuliabudu juu.

□“**kaya zao**” Hii (BDB 962) ilikuwa ni alama ya kuubudu mwezi.

1. Juu ya ngamia wa vitani, Amu. 8:21
2. Juu ya wafalme wa Kimidiani, Amu. 8:26
3. Juu ya wanawake wa Yudea, Isa. 3:18

Mfano mwingine wa wazi wa ibada ya sanamu!

## **MADA MAALUM: KUUABUDU MWEZI**

Kuabudu mwezi kulikuwa ni simulizi iliyosambaa Mashariki Karibu ya kale ikianzia na Sumeri (ustaarabu wa kwanza unaojulikana). Kulikuwa na namna ya wote mwanamke na mwanaume kwenye simulizi. Kiasili mungu mwezi alikuja kutokana na ubakaji wa mungu mke wa ngano, *Ninlil* by *Enlil*, mungu wa anga. *Enlil* alifikuzwa nje ya miungu na kuhukumiwa chini ya ulimwengu kwa matendo yake, lakini wakati *Ninlil* alipojua kwamba alikuwa na mtoto alijiunga naye. Mtoto, *dhambi*(au*Zin*), alikubaliwa kupanda katika anga kila usiku.

Kuabudu mwezi kulikusudiwa katika vipindi/hatua tofauti tofauti:

1. Mwezi mpya – *Asimbabbar*
2. Mwezi mmeguko – *Sin*
3. Mwezi wote – *Nana*(ki-Sumeria “kuangaziwa” kutoka *En-su*, “bwana wa hekima”)

Majina haya kimsingi yanamaanisha “bwana mwenye hekima” (yaani *Suen*) au “kumulikia” (*Nanaa*), waliabudu katika Uru ya Wakaldayo. Jiji lenyewe mara kwa mara liliitwa Nannar. Jozi zenye rutuba ziliabudiwa katika ziggurats (piramidi kubwa zilizo tambarare juu) zilizokuwa katika mji. Yule Mungu juu (*Shamash*) alikuwa mzaliwa wa kwanza kwa wenzi na baadaye *Ereshkigal* (malkia wa ulimwengu wa chini) na *nanna* (Malkia ya anga/mbingu).

Ibada/ dini ilisambaa maeneo yote ya Kusini Mashariki ya Mashariki ya Karibu ya kale, lakini maeneo makubwa na vituo vikubwa vilikuwa ni

1. Uru
2. Harani
3. Tema
4. Kanaani

## 5. Makka

Kimsingi hadithi hii imeunganisha na mkazo wa ustawi pamoja na kuabudu vitu vya anga.

**3:20 “vibweta vya marashi”** Neno (BDB 108) lililotafasiri “vibweta” kiuhalisia ni “nyumba.” Moja ya mfasiri wa agano la kale, J. Alec Motyer anafikiria hili laweza kurejerea kwenye “skafu ndefu” (uk. 58). Kuna mengi ambayo sisi wa kisasa hatuyaelewi kuhusu maelezo ya tamaduni za Mashariki ya Karibu ya Mbali ambayo mara nyingi utafasiri wetu ni wa kiubashiri wenyewe kuegemea kwenye ufanano na muktadha. Hakuna kati ya maelezo haya ni ya muhimu kwenye uelewa wa dhana pana na masuala ya kithiolojia. Mengi kwa ukubwa wake yanafurahisha, lakini sio ya muhimu kuweza kukupeleka kwenye uelewa wa kiini cha ukweli wa aya. Usiangalie tu kwenye mambo madogo madogo.

**3:24 “badala ya mishipi, kamba”** Hili linaonekana kurejerea kwa wafungwa waliofungwa pamoja wakitembea kwenda uhamishoni kwa Waashuru.



NASB, NKJV	“ <b>kutiwa alama mwilini badala ya uzuri</b> ”
NRSV, TEV	“ <b>badala ya uzuri, aibu</b> ”
NJB, REB	“ <b>huweka alama mwilini badala ya uzuri</b> ”
Peshitta	“ <b>kwa vile uzuri wao utaharibiwa</b> ”
LXX	-----limeondolewa-----

Andiko la Kimasoreti lina neno “kutiwa alama mwilini badala ya uzuri.” Neno “kutiwa alama” linatokana na BDB 464 (kuchoma, chanjo, tia alama). Neno “aibu” katika toleo la NRSV na TEV haliko katika andiko la kimasoreti, lakini linapatikana katika gombo la Isaya toka kwenye DSS (1QIsa.).

**3:26** Yerusalem (“JINSI YA KIKE”, mistari ya 25,26) inatazamwa kama mwanamke anayelia kwa ajili ya kupoteza. Uvaaji wa kisherehe huko Sayuni umerejeshwa katika kitabu cha Isaya 61:3, pia kumbuka Zak. 3:4 (mstari wa 22 na Zak. 3:4 ndio unaochangia lile lile neno adimu kwa ajili ya mavazi ya kisherehe

## ISAYA 4

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mabaki Wanaandaliwa	Sayuni anafanywa upya	Urejesho wa Yerusalem	Yerusalemu itarejeshwa upya	Chipukizi wa Yahweh
4:1				
4:2-6	4:2 (2)	4:2-6	4:2-6	4:2-6 (2)
	4:3-6			

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuvuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kii ni cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:1**

<sup>1</sup> Na siku hiyo wanawake saba watamshika mtu mume mmoja wakisema, Tutakula chakula chetu, na kuvaan nguo zetu wenyewe, lakini tuitwe tu kwa jina lako; utuondolee aibu yetu.

**4:1-4** Toleo lililotafsiriwa la JPSOA linagawa andiko katika sehemu mbili za ushairi na lugha ya mjazo moja.

1. Aya 1b-3
2. Aya 4
3. Aya 5-6 lugha ya mjazo

Mengi ya matoleo mengine yamechukuwa 4:1 pamoja na sura 3:16-4:1. Pia hayaziundi aya hizi kwa namna ya ushairi. Toleo la NKJV lina mst . 2 na NJB lina mistari 2-6 kama moja ya shairi lefu la ki-muktadha (JB lina mashairi yaliyogawanyika kwenye mstari wa 2-3 na 4-6), lakini mengi ya nyingine ni kama lugha za mjazo. Hii inatuonyesha kuwa ni kwa jinsi gani ni vigumu kutambua pale ambapo andiko ni la mtiririko usio wa kishairi au la kishairi na pia ni wapi asili/jambo lilipoharibikia. Kuwa makini na sura za kisasa na migawanyo ya aya! Sio mwongozo uliovuvuviwa!

**4:1** Aya hii inaonekana ina muunganiko na 3:6 (VITENZI tofauti, 3:6, BDB 1074 na 4:1, BDB 304, lakini vyote vina maana ya “kushikilia kwa nguvu”). Kwa uhakika yawezakuwa na muunganiko na zama za kimasih (yaani 4:2, “tawi”). Shairi la kiebrania ni gumu “kulifunga”. Mara nyingi unazunguka kwenye maneno na kwenye mambo yanayofanana.

■“wanawake saba” saba ni namba ya ukamilifu kwa fikra za Kiyahudi kuielezea Mwanzi 1. Hivyo basi, hii, kama ilivyo 3:25-26, inarejerea kwa wakazi wote wa Yerusalem/Yuda.

■“watamshika” Hiki KITENZI(BDB 304, KB 302,*Hiphil KAULI TIMILIFU*) inaonyesha mtu Fulani akishikamana na mwingine au kitu kingine ( yaani „Kumb. 22:25; 25:11; I Sam. 15:27; 2 Sam. 1:11; I Fal. 1:50; 2 Fal.2:12; 4:27; Mit. 7:13; 26:17; Zak. 8:23).

■“tuitwe tu kwa jina lako” Jina lilikuwa ni alama ya mtu na tabia zake. Makusudi ya jambo hili yanafunuliwa kwenye kifungu kifuatacho, “utuondolee aibu yetu” (BDB 62, KB 74, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU*). Nani awezae kufanya hivi?

1. Wenyewe haki wa sura ya 3:10
2. “tawi” la Kimasih kwenye 4:2-6.

■“utuondolee aibu yetu” NOMINO hii (BDB 357) yaweza kurejerea

1. Alama ya dhambi zao na uasi dhidi ya YHWH
2. Ujane wao pasipo watoto kwa sababu wanaume wote wamefia vitani (toleo la NASB Study Bible, uk. 965, NIDOTTE, juzu. 2 uk. 75

Isaya 54:4 inafaa kwa chaguzi zote mbili kwa sababu “ujane” ingalirejerea kutalikiwa (yaani sitiari za kisheria) na YHWH.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:2-6

<sup>2</sup>Siku hiyo chipukizi la Bwana litakuwa zuri, lenye utukufu, na matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza, kwa ajili ya Waisraeli wale waliookoka. <sup>3</sup>Tena itakuwa ya kwamba ye ye aliyebakati katika Sayuni, na ye ye aliyeachwa ndani ya Yerusalem, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalem; <sup>4</sup>hapo Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao binti za Sayuni na kuisafisha damu ya Yerusalem kati yake, kwa roho ya hukumu na kwa roho ya kuteketeza. <sup>5</sup>Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, Bwana ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa sitara. <sup>6</sup>Kisha kutakuwa na hema kuwa uvuli wakati wa mchana kwa sababu ya hari, na kuwa mahali pa kukimbilia na kujificha wakati wa tufani na mvua.

**4:2 “siku hiyo”** Hii inarejerea wakati ujao ambapo YHWH atakuja (kwa kubariki au kuhukumu) watu wake (kama vile 2:2,11,12,20; 3:7,18; 4:1,2). Hii ni mada yenye kuirudia katika kitabu cha Isaya. Ni vigumu jambo hili kuwa la uhakika kama linatajwa kwenye kumbukumbu za Isaya kwa

1. Urejesho kutoka uhamishoni uliofanywa na Zerubabeli na Yoshua wakati wa utawala wa uajemi (yaani Ezra na Nehemia)
2. Urejesho uliofanywa na wamakabayo kipindi cha utawala wa Selucid
3. Kuja kwa kristo mara ya kwanza (kuanzishwa kwa enzi mpya )
4. Kuja kristo mara pili (kukamilishwa kwa enzi mpya)

Angalia ni kwa jinsi gani nabii alitembea kutoka kwenye msingi, hukumu inamalizika kwa msingi wa kukamilisha msamaha na urejesho! Hii ni aina ya maandiko ya kinabii. Moja haliwezi kupatikana pasipo lingine! Makusudi ya hukumu mara zote huwa ni urejesho.

■“chipukizi la BWANA” kuelezea cheo hiki (BDB 855, tafsiri ya Kiarama ya sehemu ya Agano la Kale inatafasiri kama masih) ngoja mimi nitoe dondo Kutoka kwenye fasiri ya Danieli na Zakaria ambapo neno pia limetumika (lakini kama tahadhari, ni lazima tuwe makini juu ya uteuzi wa maana stadi kila mahali neno au kifungu

kimetumika –muktadha,muktadha,muktadha ni muhimu sana). Neno hili labda limeendelea kwa muda mrefu kutoka kumbukumbu hadi utele ulio bora zaidi kwa mteule wa Mungu atakaye rejesha huo utele (yaani chipua, chipukizi).

Ngoja nikushilikishe muhtasri kutoka kwenye fasiri yangu ya Zakaria.

**Zek. 3:8 “chipukizi”** hii inaweza kuwa “chipukizi” (BDB 855). Hiki ni cheo kingine cha Kimasihi (kama vile . 6:12; Isa. 4:2; 11:1; 53:2; Yer. 23:5; 33:15). Angalia mjadala kamili na Mada Maalum: Yesu Mnazareti katika Dan. 4:15. cheo hiki kilitumiwa na Zerubabeli kwenye 6:12 kama alama ya kifalme ya uzao wa kiroho . inashangaza kwamba kimetumika kwenye muktadha huu, ambao unatilia mkazo tabia ya kikuhanzi ya masihi. Tabia mbili za ukombozi (kuuhani, kama vile. Isaya 53)na kiongozi mtawala,(mfalme kama vile Isa.9:6-7) vimeungana kwenye kitabu cha Zakaria ( kama vile sura ya 4.)

**Zek. 6:12 “chipukizi”** neno hili (BDB 855) linamaana ya “kuchipuka” ( kama vile. 3:8; 6:12; Isa. 4:2; 11:1; 53:2; Yer. 23:5; 33:15). Hiki ni cheo cha masihi. Katika kitabu cha Zakaria kinarejerea kwa Zerubabeli kama aina ya masihi (kama vile. Ibn Ezra na Rashi). Jina Zerubabeli kwa lugha ya Akkadia, linamaanisha “chipukizi la Babeli.” Ni wazi jina lake lilivutia tangu alipoanza kulijenga upya tena hekalu mwaka wa 516 K.K, lakini ni kweli kabisa linamrejerea Yesu. Cheo hiki na kulingana na KITENZI (“chipukizi litakuwa,” *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) inaonekana pamoja kwenye aya hii.

## MADA MAALUMU: YESU MNAZARETI

Kuna maneno mbalimbali ya Kiyunani ambayo Agano Jipyaa hutumia kumzungumzia Yesu.

- A. Haya ni maneno ya Agano Jipyaa
  1. Nazareti – mji katika Galilaya (kama vile Luka 1:26; 2:4,39,51; 4:16; Matendo 10:38). Mji huu hautajwi katika vyanzo vya wakati huu, bali umekutwa katika kumbukumbu ya maandishi ya baadaye. Kwa upande wa Yesu kuwa alitoka Nazareti haikujitosheleza (kama vile Yohana 1:46). Alama ya msalaba wa Yesu ambayo imeliweka jina la eneo hili ilikuwa alama ya aibu kwa Wayahudi.
  2. Nazarēnos – pia inataja maeneo ya kijiografia (kama vile Luka 4:34; 24:19).
  3. Nazōraios – inaweza kuurejea juu ya mji, lakini pia ingeweza kuwa mwaminifu na mtenda haki Masihi wa Kiebrania "Utanzu" (netzer, BDB 666, KB 718 II, kama vile Isa. 11:1; maana zinazokaribiana, BDB 855, Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; iliyodokezwa katika Ufu. 22:16). Luka akilitumia hili kumhusu Yesu katika 18:37 na Matendo 2:22; 3:6; 4:10; 6:14; 22:8; 24:5; 26:9.
  4. Iliyohusiana na #3 nāzir (BDB 634, KB 684), ambalo linamaanisha "aliywakifishwa kwa maana ya nadhiri."
- B. matumizi ya Kihistoria ya neno nje ya Agano Jipyaa.
  1. Lilimaanisha kundi la ausi la Kiyahudi (Mkristo wa awali) (nāsōrāyyā ya Kiaramu).
  2. Lilitumika katika mzunguko wa Kiyahudi kuwatambulisha waamini katika Kristo (kaa vile Matendo 24:5,14; 28:22, nosri).
  3. Lilikuja kuwa neno la kawaida katika kumaanisha waamini katika makanisa ya Kisiria (Kiaramu). "Mkisto" lilitumika katika makanisa ya Kyunani kumaanisha waamini.
  4. Wakati mwengine baada ya kuanguka kwa Yerusalem, Wafarisayo walikusanyika huko huko Jamnia na walichochea utengano rasmi kati ya sinagogi na kanisa. Mfano wa aina ya maapizo ya mazungumzo dhidi ya Wakristo unapatikana katika "the Eighteen Benedictions" from Berakoth 28b-29a, ambayo "Wanazareti." "Wanazareti na waasi waliweza kutoweka kwa muda mfupi; walifutwa kutoka katika kitabu cha uzima na kutoandikwa kuwa walikuwa na imani."
  5. Ilitumiwiwa na Justin Martyr, Dial. 126:1, ambaye alitumia netzer ya (Isa. 11:1) kumhusu Yesu.
- C. Maoni ya Mwandishi  
Nashangazwa sana na herufi za maneno, Ingawa nafahamu kwamba hili ni jambo geni kusikika katika Agano la Kale "Yoshua" ina herufi mbalimbali katika Kiebrania. Maelezo yafuatayo yanenisababisha

kubaki na mashaka kama maana yake dhahiri :

1. kama vile maana yake ya karibu na neno la Kimasihi "tawi" (netzer) au neno lililo sawa nāzir (aliyepakwa mafuta kwa maana ya nadhiri)
2. vidokezo hasi vya eneo la Galilaya kuyahusu mataifa
3. uchache au kutokuwepo kwa uthibitisho wa fasili za sasa kukusu mji wa Nazareti katka Galilaya
4. inatoka katika kinywa cha pepo katika maana ya hukumu (yaani, "Umekuja kutuangamiza?").

Kwa wasifu kamili wa masomo ya kundi la neno hili, tazama Colin Brown (ed.), *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzu. 2, uk. 346 au Raymond E. Brown, Birth of the Messiah, kur. 209-213, 223-225.

■ Maelezo ya YHWH juu ya neno "chipukizi" (NKJV, NRSV, JB)

1. zuri, BDB 840, kama vile. Yer. 3:19 (mara nyingi limetumika kwa ajili ya nchi ya ahadi kwenye Dan. 8:9; 11:16,41)
2. La kupendeza, BDB 458 ina maanisha "utele," "heshima," na "utukufu" ("utukufu," BDB 802, pia kwenye aya hii)

Maneno haya mawili mara nyigi yametumika pamoja (kama vile 13:19; 28:1,4,5).

Baadhi ya matoleo yamechukua aya hizi kama kielelezo cha ukuaji wa mmea nyakati za urejesho (LXX,Peshitta, TEV, NJB, REB, NET Bible). Kwa maana ya masihi na nyakati za urejesho ni msamiati inayohusiana (sehemu ya kwanza ya mst . 2; sehemu ya pili nchi ya ahadi yenye kuzaa matunda).

■ “mwokozi wa Israeli” Isaya anawafafanulia na kuwaelezea wao mara kwa mara (kama vile . 10:20; 37:31,32; angalia Mada Maalumu katika 1:9), lakini ni kundi gani analolifafanulia? Tazama maoni yaliyo wazi kwenye mst. 2.

Roho ni mwandishi wa kweli wa maandiko . katika unabii na sura za ufunuo mara nyingi uandishi wa wanadamu hauna ufahamu wa kutosha juu ya ukubwa wa jumbe zake. Nafikilia kwamba sura hizi zina maana nyingi zaidi (yaani , Sensus Plenier),lakini huo ufunuo endelevu unabainisha maana iliyokusudiwa. Mara nyingi ukamilishaji wa mawazo mengi ndio ule wenye kuunganisha kusudio kamili la ujumbe wa kiroho (yaani ., 7:14). Hata hivyo , kanuni sahihi za ufasiri lazima zianze na “dhamira ya mwandishi” kama sehemu ya mwanzo na kutathmini andiko lolote la Kibiblia na uwasilishaji wa aina yejote.

**4:3** Aya hii huenda ndiyo ilisababisha wayahudi katika siku za Yeremia ambae hakuchukuliwa uhamishoni kujitazama wao kama watu waliopendelewa na YHWH,lakini Ezekiel anaonyesha hili sio jambo. YHWH kimsingi atashughulika wanaorudi (kama vile Ezra and Nehemia).

■ “ kila mmoja aliyeandikwa mionganoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalem ” kuna suala la tafasiri mbili .

1. Ikiwa hili linarejerea kwenye maisha huko Yerusalem mji mkuu wa Yuda au “Yerusalem mpya.” Alama ya zama mpya (kama vile Ufunuo 21)? Je hili ni la matukio ya kihistoria au matukio ya siku ya mwisho?
2. Kitabu cha uzima (tazama mada maalumu inayofuata)

## MADA MAALUMU:VITABU VIWILI VYA MUNGU

A. Mungu amejifunua katika namna mbili.

1. asili (yaani, uumbaji, kama vile Zab.19:1-6; iitwayo "mapinduzi asilia")
2. Maandiko (kama vile Zab. 19:7-14; yaitwayo "mapinduzi maalumu/kipekee")

Ndiyo maana sifikiți yakwamba daima lazima kuwepo mvutano kati ya sayansi na imani, kweli yote ni kweli ya Mungu. Tafadhali angalia maoni yangu kuhusu Mwanzo 1-11 mtandaoni katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

B. Kuna vitabu viwili vilivyotajwa katika Dan. 7:10 na Ufu. 20:12.

1. Kile"kitabu cha matendo" kilicho na sababu zote na matendo ya wanadamu, yote yaliyo mema na mabaya. Katika maana hii, hii ni stiari ya kumbukumbu ya Mungu na y a kwamba siku moja wanadamu wote watatoa hesabu ya utumishi wa vipawa vya maisha yao kwa Muumba wao.
  - a. Zab 56:8; 139:16
  - b. Isaya 65:6

- c. Malaki 3:16
  - d. Ufunuo 20:12-13
2. Kile "kitabu cha uzima" chenyе kilicho orodhesha wale walio na imani/waliotubu/walio utii uhusiano na YHWH/ Yesu. Hii ni stiari ya kumbukumbu ya Mungu ya wale waliokombolewa na kuunganishwa na mbingu.
- a. Kutoka 32:32-33
  - b. Zab. 69:28
  - c. Isaya 4:3
  - d. Danieli 12:1
  - e. Wafilipi 4:3
  - f. Waebrania 12:23
  - g. Ufunuo 3:5; 13:8; 17:8; 20:12,15; 21:27
  - h. Pia kilichotajwa katika I Enoch 47:3; 81:1-2; 103:2; 108:3

Hivi vitabu vinawakilisha uaminifu wa Mungu kwa Neno lake. Kwa wale walioasi na kukataa, anazikumbuka dhambi zao; kwa wale waliotubu, kuamini, kutii, kutumika, na kustahimili, Yeye husahau dhambi zao (kama vile Zab. 103:11-13; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Mika 7:19). Jambo hili hutupa uhakika mwingi na ujasiri wa kutobadilika kwa Mungu, sifa ya huruma, ahadi, na utoaji. Mungu ni mwaminifu! Jambo alilolifuna kumhusu ni la kweli!

#### **4:4** Hii aya ina sitiari mbili kwa ajili ya utakaso wa kiroho

- 1. kusafisha
  - a. kuosha kabisa, BDB 934, KB 122, *Qal KAULI TIMILIFU*
  - b. takasa (kifasihi. "ng'arisha"), BDB 188, KB 216, *Hiphil KAULI ISIO TIMILIFU* (ina dokezo la kidhabihu, kama vile. 2 Nya. 4:6; Ezek. 40:38)
- 2. moto
  - a. Roho ya hukumu, kama vile. 28:6
  - b. Roho wa moto, kama vile. 1:31; 9:19 (angalia Mada Maalumu: Moto katika 1:31).

Inawezekana kabisa kwamba "roho" (*ruah*) Ingalipaswa kufahamika kama upepo wenye kuleta uharibifu wa hukumu ya YHWH. Yuda atahukumiwa na kusafishwa kwa ukaidi wa uasi wake.

▣ "uchafu" Hili ni neno lenye nguvu (BDB 844) ambalo limetumika kama dhambi.

- 1. Isaya 28:8 matapishi ya mwanadamu
- 2. Isaya 36:12 kinyesi cha wanadamu (kama vile Kumb. 23:14; Ezek. 4:12)

▣ "binti za sayuni" Hii ni sitiari iliyotumika kwa Yerusalem kwenye 3:16-26. inafanana na "Yerusalem".

▣ "umwagaji damu" Hii (BDB 196) ni sitiari kwa ajili ya kudhamiria kuua. Hapa yumkini linarejerea juu ya unyonyaji wa maskini na kuwatenganisha kijamii (yaani, "kutoka katikati yake").

**4:5** Hili ni dokezo la kihistoria kwa uwepo wake binafsi wa YHWH na uangalizi wakati wa kutoka na kipindi cha mizunguko ya safari ndefu jangwani. Inamaanisha Shekinahwingu la utukufu (yaani Kut. 13:21,22; 40:38; Hes. 9:15-23; Zab. 78:14; 99:7; 105:39). Yeye (au malaika wake) binafsi aliwaongoza watu wake tena kwa kuwapa mahitaji yao kwa wingi.

▣ "BWANA ataumba" KITENZI hiki (BDB 135, KB 153, *Qal KAULI TIMILIFU*) kimetumika pekee kwenye uumbaji wa Mungu (kama vile . Mwa. 1:1).

▣ "uvuli" neno hili (BDB 342 I) linaweza kumaanisha

- 1. Ulinzi wa kufunikwa kama vile mawingu ya *Shekinah* (juu ya watu wote, kama vile katika kitabu cha Kutoka na mizunguko ya safari ndefu jangwani)
- 2. Kufunikwa kwa ajili ya harusi (kama vile Zab. 19:5; Yoeli 2:16)

Wengine wana husunisha hii sitiari ya sherehe na mwanamke aliye kata tamaa 4:1, wakati watoa maoni wengine wana husunisha na hema takatifu na urejesho wa hekalu la wakati ujao katika Yerusalem, ambapo utaonyesha muunganiko wa YHWH/Masihi na watu wake katika sitiari ya ndoa (kama vile. 5:1; Hosea 1-3; Efe. 5:21-33).

**4:6** kuna sitiari nyingi zilizounganishwa ili kuonyesha ulinzi wa YHWH (kutoka kwenye joto na dhoruba)

1. Kibanda, BDB 697, kama vile . 1:8; Zab . 27:5; 31:20; wazo lingine ni kwenye 32:2
2. ukimbizi, BDB 340
  - a. NOMINO, Isa. 25:4
  - b. KITENZI, Isa. 14:23; 57:13
  - c. katika Zaburi, 14:6; 46:1; 61:4; 62:7,8; 71:7; 73:28; 91:2,9; 94:22; 142:5
3. baadhi ya maandiko kutoka katika kitabu cha Isaya, “ulinzi” BDB 731,kama vile . 17:10; 27:5

mara nyingi hizi sitiari zinanrejerea YHWH kama

1. Ndege jike alindavyo (yaani chini ya uvuli wa mbawa zake)
2. Ngome imara au mwamba imara (kama vile Zab. 18:1)

waaminio wanaweza kuamini ulinzi na uwangalizi wa Mungu wao wa agano! Yeye yuko pamoja nasi na kwa ajili yetu, kama iwapo tutatubu, tutaa mini, tutatii, tutamtumikia, na kuvumilia. Agano limeahidi (manufaa) na kuwajibika (wajibu). Wote tuna matokeo!

## ISAYA 5

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mfano wa shamba La mizabibu	Mungu anaisikitikia mizabibu	Wimbo wa shamba la mizabibu	Wimbo wa shamba la mizabibu	Wimbo wa shamba la mizabibu
5:1-2 (1-2)	5:1-7 (1b-2)	5:1-2 (1-2)	5:1-2 (1-2)	5:1-4 (1-4)
5:3-6 (3-6)		5:3-4 (3-4)	5:3-4	
		5:5-6 (5-6)	5:5-6	5:5-7 (5-7)
5:7 (7)	(7)	5:7-10 (7-10)	5:7 (7)	
Ole kwa watenda Maovu	Hukumu imekaribia juu ya watenda maovu		Uovu utendwao na watu	Laana
5:8-12 (8-12)	5:8-10 (8-10)		5:8-10	5:8-10 (8-10)
	5:11-12 (11-12)	5:11-13 (11-13)	5:11-14	5:11-14 (11-14)
5:13-17 (13-17)	5:13-17 (13-17)	5:14-17 (14-17)	5:15-17	5:15-17 (15-17)
5:18-23 (18-23)	5:18-19 (18-19)	5:18-24 (18-24)	5:18-19	5:18-19 (18-19)
	5:20 (20)		5:20	5:20 (20)
	5:21 (21)		5:21	5:21 (21)
	5:22-23 (22-23)		5:22-25	5:22-24 (22-24)
5:24-25 (24-25)	5:24-25a (24-25a)			Hasira ya YHWH
	5:25b (25b)	5:25-30 (25-30)		5:25 (25)
				YHWH awaita wavamizi
5:26-30 (26-30)	5:26-30 (26-30)		5:26-29	5:26 (26)

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **UTAFITI WA MAMBO YALIYOPITA**

- A. Ni vigumu kujua muktadha wa kihistoria wa sura hii. Inaweza kutumika sehemu yeote ya huduma ya mahubiri ya Isaya. Waandishi wa leo hawajui ni namna gani kitabu cha kinabii kilivytungwa.
- B. Inavyoonekana huu wimbo wa jadi uliimbwa kwenye baadhi ya mikusanyiko ya taifa la Yuda. Haijulikani kama ilikuwa ni kwenye hekalu au sehemu za soko.
- C. Ni muhimu kukumbuka kuwa fursa huleta uwajibikaji (Luka 12:48).
- D. Madekezo kwenye nyimbo za jadi yanapatikana sehemu mbalimbali katika Agano Jipy (kama vile Mt. 21:33-46; Marko 12:1-2; Luka 20:9-19).
- E. Lazima ikumbukwe kuwa Yuda, wakati wa huduma ya kinabii ya Isaya, ilikuwa haswa taifa lenye mafanikio na ustawi mwangi. Ustawi huu ukaleta udhaifu wa kiroho na utegemezi juu ya rasilimali za mwanadamu badala ya Mungu na ahadi zake za agano na mahitaji.

### **MAELEZO MAFUPI KWA MUHTASARI**

- A. Wimbo wa kimafumbo, kur. 1-6
- B. Tafasiri ya kikejeri, uk. 7
- C. Matokeo ya hukumu ya YHWH, kur. 8-30
  1. Mlolongo wa majonzi, kur. 8-23
  2. Hukumu, kur. 24-30
    - a. ya viumbe hai, uk. 25
    - b. wavamizi, kur. 26-30

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 5:1-2**

<sup>1</sup>Na nimwimbie mpenzi wangu wimbo wa mpenzi wangu katika habari za shamba lake la mizabibu. Mpenzi wangu alikuwa na shamba la mizabibu, Kilimani penye kuzaa sana:<sup>2</sup>Akafanya handaki kulizunguka pande zote, Akatoa mawe yake, Akapanda ndani yake mzabibu ulio mzuri, Akajenga mnara katikati yake, Akachimba shinikizo ndani yake; Akatumaini ya kuwa utazaa zabibu, Nao ukazaa zabibu-mwitu.

**5:1 “na nimwimbie”** Hiki KITENZI cha kiutangulizi (BDB 1010, KB 1479, Qal HALI YA KUSIHI) pia kimetumika katika 26:1 na 42:10. NOMINO pia inajitokeza katika mstari wa 1. Mara nyingi nyimbo zilitumika kuashiria tukio fulani (kama vile Kut. 15:1; Hes. 21:17; Amu. 5:1; I Sam. 18:6). Hapa wimbo umetumika kuleta usikivu kwa wapititaji, ili kwamba waweze kusimama na kusikiliza.

■“**mpenzi wangu.....wimbo wa mpenzi**” Haya ni maneno mawili tofauti ya Kiebrania. La kwanza (BDB 391) mara nyingi linatumika katika ushairi wa mmoja wa familia. La pili (BDB 187) linatumika mara nyingi katika Wimbo ulio Bora kwa ajili ya mpenzi. Hapa linarejerea kwa rafiki maalum kwa ajili ya matarajio maalum kwa anaye miliki. Hili lingalivuma vizuri kwa jamii ya kikulima ya Yuda.

■“**mizabibu**” Matunda ya mizabibu (au mzabibu) ilikuwa ni alama ya utaifa wa Israeli (yaani Kut. 15:17; Zab. 8:8; Yer. 2:21; 12:10) kama ilivyo kwenye mti wa mzeituni na njija. Yuda ilionekana kwa manabii kama “watu wa Mungu” walio wa kweli.

■“**kilimani penye kuzaa sana**” Neno “kilimani” kwa maana iliyo wazi ni “pembe” (BDB 901) likitumika kwa maana ya kilima kilichojitenga kikijielekeza sehemu nzuri ya kupokea mwanga wa jua na sehemu ya mteremko kuweza kutililisha maji. “kilima” chenyewe haswa kimeandaliwa kupandwa miti ya mizabibu “bora”, kwa ajili ya mavuno mazuri! KIVUMISHI “penye kuzaa sana” kwa maana iliyowazi ni “mimba iliyosta” (BDB 1032), ambayo ni stiari ya kuzaa sana na utele wa matunda (kama vile 28:1,4).

**5:2** kuna mchezo wa maneno juu ya KITENZI (BDB 793, KB 889) katika mistari ya 2-5, uliyotumika mara saba. Imetasiriwa kama

1. kuzaa, mst. 2 (mara mbili)
2. fanya, mst. 4 (mara mbili), kile Mungu atafanya kwa ajili ya mizabibu yake
3. kuzaa, mst. 4 (mara mbili)
4. fanya, mst. 5, kile Mungu atafanya kwa mizabibu-mwitu

■“**akafanya handaki kuzunguka pande zote, akatoa mawe yake**” Hiki KITENZI cha kwanza (BDB 740, KB 810, *Piel CHA WAKATI ULIOTIMILIFU*) kinapatikana hapa tu katika Agano la Kale. Toleo la KJV lina neno “zungukwa.” Ingawa siamini kuwa hii ndio tafasiri sahihi ya neno la Kiebrania, inayoendana na muktadha. Pindi mawe yalikuwa yanaondolewa toka kwenye maeneo ya mwamba huko Palestina, yalikuwa yamerundikwa kwenye ua. Mara nyingi mizabibu ilikuwa ikilindwa na mtaro (pia maana nyingine inayowezekana ya KITENZI cha kwanza) ukiwa na ua wa mawe (LXX, Peshitta, Vulgate). Hakika inawezekana kuwa Isaya anaelezea mbinu ya matuta ya mkingamo. Mawe yangalitumika kulinganisha sehemu za shamba. Pia yawezekana kuwa mawe yaliweza kurundikwa pamoja na kutumika kutunza kishada cha matunda yasiweze kugusa chini (James Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, kur. 360-363).

■“**mzabibu ulio mzuri**” Hili linarejerea kwenye matunda yaliyoiva yajulikanayo kwa “rangi ya zambarau” (BDB 977 I, kama vile Yer. 2:21). Matunda haya yalipata jina lake toka kwenye bonde la Palestina (kama vile Amu. 16:4). Yametajwa katika Yer. 2:21 kama matunda yaliyo ghali na kuchambuliwa toka kwenye aina mbalimbali za matunda. Hivi viungo vya mzabibu vimetajwa kwenye kifungu cha Kimasihi (kama vile Mwa. 49:11).

■“**mnara**” Huu (BDB 153, “mnara wa ulinzi” ulijengwa kwa mawe yaliyo chimbiliwa toka kwenye shamba) ulikuwa kwa ajili ya kusudi la kiulinzi na mara nyingi ultumika kipindi cha uapandaji na wakati wa mavuno miezi ya tisa (lingalitumika kwa kusudi lile lile kama liliivyo neno “kibanda” liliilotajwa katika 1:8). Neno lile lile laweza kurejea mnara wa kivita (kama vile Isa. 2:15). Muktadha, muktadha, muktadha!

■“**Akachimba shinikizo ndani yake**” Hili lingalikuwa ni mbonyeo mfupi wa kutengenezwa kwenye mwamba ambaa uliwasaidia wanawake kuweza kukandamiza matunda kwa miguu yao na baadaye kuyapitisha mahali ambapo maji ya matunda/tui lilihofadhiwa.

□

NASB	"usiozaa matunda"
NKJV, NRSV,	
NJB, REB	"zabibu mwitu"
TEV, JB	"kila mzabibu ulikuwa mchachu"
LXX	"miiba"

Neno la Kiebrania (BDB 93) laweza kurejea kwenye

1. majani yenyeye kutoa harufu mbaya, UMOJA, kama vile Ayubu 31:40

2. vitu vyenye kutoa harufu mbaya, vitu visivyo na thamani, WINGI

msingi wa mzizi wa neno unarejerea kwenye harufu mbaya ya

1. mzoga, Isa. 34:3 (cf. 5:25); Joel 2:20; Amos 4:10

2. nzige, Joeli 2:20 (stiari kwa ajili ya mwanajeshi aliyekufa)

andiko la Kimasoreti katika muktadha huu linarejerea kwenye "mizabibu mwitu," ambayo haikuwa mitamu na minene, lakini midogo na michachu, isiofaa kutengeneza mvinyo.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:3-6

<sup>3</sup>Na sasa, enyi wenyeyeji wa Yerusalem, nanyi watu wa Yuda, amueni, nawasihi, kati ya mimi na shamba langu la mizabibu. <sup>4</sup>Je! Ni kazi gani iliyoweza kutendeka ndani ya shamba langu la mizabibu nisiyotenda? Basi, nilipotumaini ya kuwa litazaa zabibu, mbona lilizaa zabibu-mwitu? <sup>5</sup>Haya basi, sasa nitawaambieni nitakalolitenda shamba langu la mizabibu; nitaondoa kitalu chake, nalo litaliwa; nitabomoa ukuta wake, nalo litakanyagwa; <sup>6</sup>nami nitaiharibu; wala halitapogolewa wala kulimwa, bali litamea mbigili na miiba; nami nitayaamuru mawingu yasinyeshe mvua juu yake.

**5:3** Nabii anaufanya umati wa watu uingie kwenye mchakato wa maamuzi. Kuna hoja ya uwasilishaji wa hotuba. Watahukumu wao wenyewe! KITENZI "kuhukumu" (BDB 1047, KB 1622) ni *Qal KAULI SHURUTISHI* na kinafanana na Mt. 21:40.

**5:4** Swali hili ndio kiini cha wimbo wa mafumbo. Mungu alifanya kila kitu kwa watu wake, lakini wakamkataa.

**5:5-6** Nabii, akimzungumza kwa ajili ya YHWH, anatangaza (BDB 393, KB 390, *Hiphil HALI YA KUSIHI*) kile atakifanya kwa mzabibu wenyeye kukatisha tamaa (yaani., Juda).

1. Kumwondolea ua, matokeo yake ataliwa na wanyama
2. Kuzivunja kuta zinazomzunguka, matokeo yake mizabibu kuweza kuangushwa chini
3. Kukataa kutegemewa, matokeo yake waridi mwitu na miiba itatokeza (kama vile 7:23,25; 9:18; 27:4)
4. Akakataa kuleta mvua, matokeo yake utanyauka na kufa (kama vile Kumb. 28:23-24)

**5:6** "nami nitaiharibu" KITENZI (BDB 1011, KB 1483) ni *Qal KAULI ISIOTIMILIFU*. YHWH ataifanya mizabibu yake "iharibike" (BDB 144). Neno hili linapatikana hapa tu. Laweza kumaanisha "mwisho" au "maangamizo." Hukumu ya Mungu ni kamili na ya mwisho (kama vile mst. 30)! Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya sura ya 7-12! Patakuwepo na siku mpya (sura ya 40-55) na mbingu mpya na nchi mpya (sura ya 56-66).

▣ "name nitayaamuru mawingu yasinyeshe mvua juu yake" Mazingira yamekuwa, na yanaendelea, kuharibiwa na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwa. 3:17-19 na Rum. 8:19-26). Yanatumiwa na Mungu kwa ajili ya kubariki au kuhukumu (yaani., Law. 26:4; Kumb. 11:14; 28:12; Amosi 4:7; Zak. 14:17).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:7

**7** Kwa maana shamba la mizabibu la Bwana wa majeshi ndilo nyumba ya Israeli, na watu wa Yuda ni mche wake wa kupendeza; akatumaini kuona hukumu ya haki, na kumbe! Aliona dhuluma; alitumaini kuona haki, na kumbe! Alisikia kilio.

**5:7 “nyumba ya Israeli”** Neno hili kikawaida linaonekana kurejerea kwa Wayahudi wote kwa pamoja kabla ya kugawanyika kisiasa katika mwaka wa 922 K.K., ingawa katika mstari huu neno linarejea kwa Yuda. Kwa wakati huu katika historia ya watu wa Mungu, mataifa yao yaligawanyika katika makabila kumi ya Kaskazini yaliyojulikana kama Israeli, Efraimu, au Samaria na makabila matatu ya Kusini yaliyojulikana kama Yuda, ambayo yanajumuisha Benjamini, Simioni, na hasa ya Kilawi/Kikuhanzi.

▣ “**haki . . . dhuluma. . . haki. . . kilio cha machungu**” Haya ni masihala juu ya sauti mbili tofauti katika Kiebrania ambayo haiwezi kuzalishwa katika tafasiri ya Kiingereza: טְשִׁמָּה, Mishpat (haki) dhidi ya. (תְּשִׁמָּה, Mispach (dhuluma, BDB 705) na זְדָקָה, Zedakah (haki) dhidi ya צְדָקָה, Zeakah (kilio cha uchungu). Matarajio mengine ya kibiblia yaliyo kinyume.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:8-12

<sup>8</sup>Ole wao waongezao nyumba baada ya nyumba, na kuweka shamba karibu na shamba, hata hapana nafasi tena, nanyi hamna budi kukaa peke yenu kati ya nchi! <sup>9</sup>Bwana wa majeshi asema katika masikio yangu, Hakika majumba mengi yatakuwa ukiwa, naam, majumba makubwa, mazuri, yatakuwa hayana watu. <sup>10</sup>Kwa maana shamba la mizabibu la eka kumi litatoa bathi moja tu, na homeri ya mbegu itatoa efa tu. <sup>11</sup>Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo; wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani yao! <sup>12</sup>Na kinubi, na zeze, na matari, na filimbi, na mvinyo, zote ziko katika karamu zao; lakini hawaiangalii kazi ya Bwana wala kuyafikiri matendo ya mikono yake.

#### 5:8

NASB, NKJV,

NJB, REB

“Ole”

NRSV, JPSOA

“salale!”

TEV

“mmeangamizwa”

Kuna majadiliano kati ya watoa maoni ikiwa kuna “ole” sita au saba (BDB 222) zilizoorozeshwa. Neno “ole” kwa maana iliyo wazi sio la Kiebrania (BDB 17, ambalo linaonyesha kuomboleza, kama vile 3:9,11; 6:5; 24:16). Ushauri wa tafasiri hii toka BDB ni “ah,” “alas,” au “ha” (kama vile 1:4;10:1,5; 17:12; 28:1). Inajaribu kuelezea maumivu ya kutoridhika na hali inayoendelea au matokeo yake. Walianza na matokeo ya hukumu juu ya Yuda kwa sababu ya kukaa kwao toka kwenye agano la Mungu. Kimsingi wananaorodhesha dhambi za jamii ya Wayudea.

▣ “**wale waongezao nyumba baada ya nyumba, na kuongeza shamba baada ya shamba**” Hili linarejerea kwenye wamiliki wa mashamba wenyewe ubiniasi wanaowanyonya masikini kwa kuchukua mashamba ya mababu zao (yaani., shamba walilogawiwa na Joshua) ili kujilimbikizia mashamba zaidi na zaidi kwa ajili yao wenye (kama vile Yer. 22:13-17; Mika 2:2). Sheria ya Musa ilijaribu kulinda mashamba yaliyochukuliwa kwa kutangaza “mwaka wa yubilei” (kama vile Law. 25:8-55; Hes. 36:4). Mashamba yote yalilazimika kurejeshwa kwa wamiliki wa kikabila wa mwanzo kwa kila mwaka wa hamsini. Inagwa hakuna kumbukumbu katika Agano la Kale kwa Israeli kuweza kuheshimu hili kwa kuyaachilia, bado yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kuyaelezea.

**5:9** Ufunguzi wa mst. 9 ni wa kimsitizo, ukiwa hauna KITENZI, hasa kifungu “katika masikio yangu, Bwana wa Majeshi.” Haya ni madai ya wazi ya ufunuo wa maneno ya kiungu (kama vile 22:14)! Huu sio ujumbe wa Isaya, wala fikra za Isaya! YHWH anapiga kelele kwa watu wake wasiotii kupitia manabii wake.

Hukumu hii inafanana na ile ya kwenye kitabu cha Amosi 5:11 na Mika 6:15. Matarajio ya wenye mali na viashilio vya unyonyaji kwenye jamii havitatokea. Hawatafurahia mafanikio yao ya wizi! Tunavuna kile tulichokipanda (angalia muhtasari katika 3:10-11).

**5:10 “shamba la mizabibu la heka kumi”** “heka” kwa maana iliyo wazi ni “vitu viwili” au “jozi” (BDB 855, kama vile I Sam.14:14), ambayo inaonyesha wanyama waliofungwa pamoja kwa makusudi ya kulima. “jozi” moja ilikuwa ni idadi ya shamba ambalo maksai angweza kulilima kwa siku moja.

■ “litatoa bathi moja tu” Neno “bathi” (BDB 144 II) ni kipimo cha kimiminika katika Kiebrania na ni sawa na nane ya kumi ya kipimo cha galoni. Katika muktadha huu ni stiari kwa ajili ya kutopata mazao kwenye shamba ulilojtwalia kwa nguvu.

## MADA MAALUM: UZANI NA VIPIMO VYA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE (USOMAJI WA VIPIMO)

Uzani na vipimo vilivyotumika katika masuala ya biashara vilikuwa ni vya muhimu katika uchumi wa kilimo hapo kale. Biblia inawasihi Waisrael kuwa wasiwe na upendeleo kwenye mambo yao wanayoyafanya na wengine (kama vile Law. 19:35-36; Kumb. 25:13-16; Mith. 11:1; 16:11; 20:10). Tatizo kubwa lilikuwa sio tu uaminifu, bali kutokuwepo na istilahi zilizo sawa na muundo uliotumika huko Palestina. Inaonekana kuwa palikuwepo jozi mbili za uzani; moja “nyepesi” na nyingine “nzito” kwa kila idadi (angalia *The Interpreter's Dictionary of the Bible*, juzu ya 4, uk. 831). Pia muundo wa desimali (ulioegamia kwenye sehemu ya 10) wa Misri umekuwa ukijumuishwa na sehemu ya 6 huko Mesopotamia.

Wingi wa “vipimo” na “idadi” vilivyotumika vilitokana na sehemu ya mwili wa mwanadamu, wanyama, mizigo, vibebeo vya wakulima, hakuna hata kimoja kilichokuwa sawia. Kwa hiyo, chati hapa chini ni makadilio tu na ya majaribio. Njia rahisi ya kuonyesha uzani na vipimo iko katika jedwali la kimahusiano

### I. Maneno ya ujazo yanayotumika mara nyingi

- A. Vipimo vya vitu vikavu
  - 1. Homeri (BDB 330, yumkini "mzigo wa punda," BDB 331), mf., Law. 27:16; Hosea 3:2
  - 2. Lateki (AU lethech, BDB 547, yumkini inadokeza katika Hosea 3:2)
  - 3. Efa (BDB 35), mf., Kut. 16:36; Law. 19:36; Ezek. 45:10-11,13,24
  - 4. Se'ah (BDB 684), mf., Mwa. 18:6; 1 Sam. 25:18; 1 Fal. 18:32; 2 Fal. 7:1,16,18
  - 5. Homeri (BDB 771 II, yumkini "mganda" [safu ya mbegu zilizoanguka], BDB 771 I), mf., Kut. 16:16,22,36; Law. 23:10-15
  - 6. Hini (BDB 798, "sehemu ya kumi" ya efa), mf., Kut. 29:40; Law. 14:21; Hes. 15:4; 28:5,13
  - 7. Kibaba (BDB 866), kama vile 2 Fal. 6:25
- B. Vipimo vya vimiminika
  - 1. Kori (BDB 499), mf., Ezek. 45:14 (inawezakuwa kipimi cha vitu vikavu, kama vile II Nya. 2:10; 27:5)
  - 2. Bathi (BDB 144 II), mf., I Fal. 7:26,38; II Nya. 2:10; 4:5; Isa. 5:10; Ezek. 45:10-11,14
  - 3. Hini (BDB 228), mf., Kut. 29:40; Law. 19:36; Ezek. 45:24
  - 4. Logi (BDB 528), kama vile Law. 14:10,12,15,21,24
- C. Chati (iliyochukuliwa toka kwa Roland deVaux, *Ancient Israel*, juzu. 1, uk. 201 na *Encyclopedia Judaica*, juzu. 16, uk. 379)

Homeri (kikavu) =Kori kimiminika au kikavu	1						
Efa (kavu) =bathi (kimiminika)	10	1					
Se'ah (kikavu)	30	3	1				
Hini (kimiminika)	60	6	2	1			
Homeri (kikavu)	100	10	-	-	1		
Kibaba (kikavu)	180	18	6	3	-	1	
Logi (kimiminika)	720	72	24	12	-	4	1

### II. Istilahi za uzani zinazotumika mara kwa mara

- A. Uzani wa aina tatu unaotumiwa mara nyingi ni talanta, shekeli, na gera.
1. Kipimo kikubwa katika Agano la Kale ni taranta. Toka Kutoka 38:25-26 tunajifunza kuwa taranta moja ni sawa na shekeli 3,000 (yaani., "uzani wa jumla," BDB 503)
  2. Neno shekel (BDB 1053, "uzani") hutumia mara nyingi kama inavyodhaniwa, lakini hakijaelezewa katika andiko. Kuna thamani mbali mbali za shekeli zilizotajwa katika Agano la Kale.
    - a. "kipimo cha kibiashara" (toleo la NASB la Mwa. 23:16)
    - b. "shekeli ya madhabahuni" (toleo la NASB la Kut. 30:13)
    - c. "kwa uzani wa Mfalme" (toleo la NASB la II Sam. 14:26), pia uliitwa "uzani wa Kifalme" kwenye mafunjo ya Elephantine.
  3. Gera (BDB 176 II) ilithaminiwa na shekeli 20 (kama vile Kut. 30:13; Law. 27:25; Hes. 3:47; 18:16; Ezek. 45:12). Uwiano ulitofautiana toka Mesopotamia hadi Misri. Israeli ilifuatisha uthaminishaji uliokuwa ukitumika huko Kaanani(Ugariti)
  4. Mina (BDB 584) inathaminishwa na shekeli 50 au 60. Neno hili linapatikana hasa katika vile vitabu vya Agano la Kale (yaani Ezek. 45:12; Ezra 2:69; Neh. 7:71-72). Ezekiel ikitumia uwiano wa 1 ya 60, wakati Wakaanani walitumia uwiano wa 1 ya 50.
  5. Beka (BDB 132, "nusu ya shekeli," kama vile Mwa. 24:22) imetumika mara mbili katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 24:22; Kut. 38:26) na inathaminishwa na nusu shekeli. Jina lake linamaanisha "kugawanya."

B. Chati

1. Imesimamia juu ya Vitabu vitano vya Torati

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekel	3,000	50	1		
Beka	6,000	100	2	1	
Gera	60,000	1,000	20	10	1

2. Ikisimamia juu ya Ezekiel

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekeli	3,600	60	1		
Beka	7,200	120	2	1	
Gera	72,000	1,200	20	10	1

□ **"na homeri ya mbegu itatoa efa tu"** Tena hii ni stiari inayoashiria kwa ajili ya kutopata matunda kwa shamba lilitotwalia bila haki. Tunajifunza toka kwa Ezek. 45:11 kuwa palikuwepo na efa kumi kwenye homeri moja; kwa hiyo, hili linalezea kuwa ikiwa mkulima atapanda kiasi cha paundi mia moja atavuna kumi tu.

**5:11 "ole wao waamukaoasubuhi na mapema, wapate kufuata kileo "** Dhambi ifuatayo iliyotajwa ni moja vurugu ya kutafuta maisha mazuri toka asubuhi mpaka jioni. Inahitajika kusisitizwa kuwa Biblia hailaumu juu ya mvinyo, lakini inalaumu juu ya utumiaji vibaya wa mvinyo. Hii stiari ya kinywaji kikali inatumika katika Isaya 28. Sura zingine zenyenye kusikitisha juu ya somo hili zinapatikana katika Mhu. 20:1 na 23:29-35.

Hata hivyo, mmoja lazima aongeze ulinganifu wa Zab. 104:1-4. "kinywaji kikali" (BDB 1016) ni neno la Kiebrania lenye kuelezea uongezaji wa mbegu zenyenye kutengeneza chachu kwenye mvinyo. Angalia Mada Maalum: Kileo na Ulevi sura ya 1:22

**5:12 "karamu zao zikisindikizwa na"** Hii ni namna ya kuzungumzia shughuli za kitamaduni za siku. Inaelezea daraja la kitajiri lilitotolewa kwenye starehe za kidunia.

▣ “**hawaiangalii kazi ya Bweana, wala kuyafikiria matendo ya kazi ya mikono yake**” Watu wa agano la Mungu waliokataa kusikia na kuyaelewa mapenzi ya Mungu ndiyo mada inayojirudia (kama vile 1:2-3,10a; 5:12,13,24; 6:9-10; 30:9). Mungu alikwisha kuwapa masikio na macho ya kiroho (kama vile Kumb. 29:4), lakini upofu na uziwi wao kwa pamoja umesababisha Mungu kuondoa uwezekano wa kuyaelewa (kama vile Isa. 6:9-10; 29:9-10). Sikitiko la huu mstari ni kwamba Wayudea wa siku za Isaya walikuwa wakitegemea juu ya mali na njama zao badala ya kupata mahitaji toka kwa Mungu wao wa agano. Mtu anatakiwa kulinganisha mst.24d,e na Kumb. 8:11-12.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 5:13-17**

<sup>13</sup>Kwa sababu hiyo watu wangu wamechukuliwa mateka, kwa kukosa kuwa na maarifa; na watu wao wenye cheo wana njaa, na wengi wao waona kiu sana. <sup>14</sup>Kwa hiyo kuzimu kumeongeza tamaa yake, kumefunua kinywa chake bila kiasi; na utukufu wao, na wingi wao, na ghasia yao, naye pia afurahiye mionganoni mwao, hushuka na kuingia humo. <sup>15</sup>Na mtu mnyonge ainamishwa, na mtu mkubwa amedhilika, na macho yao walioinuka hunyenyekewa, <sup>16</sup>bali Bwana wa majeshi ametukuzwa katika hukumu, na Mungu aliye Mtakatifu ametakaswa katika haki. <sup>17</sup>Ndipo wana-kondoo watakapolisha kama katika malisho yao wenyewe, na mahali pao waliowanda, palipoachwa ukiwa, wageni watakula.

**5:13-17** Hapa kuna orodha ya kile kitakachotokea kwa wazawa wa Yuda wenye mali, na wanyonyaji.

1. Kuchukuliwa mateka, mst. 13
2. Kuwa na njaa, mst. 13
3. Kuona kiu, mst. 13
4. Kuzimu kuwameza, mst. 14
5. hunyenyekewa, mst. 15
6. kudhalilishwa, mst. 15 (mara mbili)
7. wageni watakula vinono vya mali walizonazo, mst. 17

**5:13 “kwa sababu watu wangu wamechukuliwa mateka kwa kukosa kuwa na maarifa”** Huu ni utabiri wa wazi wa wa watu waliochukuliwa mateka. Pamekuwepo na baadhi ya mitazamo kuhusu ikiwa hili linarejerea kwa mateka waliochukuliwa huko Ashuru (722 K.K.) kati ya makabila kumi ya Kaskazini au watu wa Yuda walichukuliwa mateka huko Babeli (yaani., 605, 597, 586, 582 K.K.) kati ya yale makabila ya kusini. Muktadha wa haraka unaonekana kujistahilisha wenyewe (hili ni la kawaida katika kitabu cha Isaya, yavezekana ni kwa kusudi Fulani). Ashuru inatajwa hasa katika Isa. 7:18 na 10:5nakuendelea. Nafikiria kuwa 13:1-14:27 pia inarejerea kwa Ashuru ambayo iliwangamiza mji wa Babeli na mfalme wa Ashuru akakikalia kiti, “mfalme wa Babeli.”

Kutaja kwa mateka nje ya nchi ya ahadi ni wa kusikitisha. Kaanani ilikuwa imeahidiwa kwa kizazi cha Ibrahimu. Hivyo agano na wazee wa kale lilibatilishwa kwa sababu ya ukaidi wa Yuda juu ya mataka ya agano. Walifurahi na kung’ang’ania kwenyehi ahadi, lakini wakatupilia mbali matakwa ya agano (kama vile Yeremia 7).

Katika maana ya kithiolojia huu ufanano wa Mwanzo 2 (ushirika kamilifu wa Mungu na mwanadamu) na Mwanzo 3 (uasi wa kufunguka macho kwa Adamu na Eva). Mwanadamu aliondolewa kutoka katika bustani ya Edeni (kama vile Mwa. 3:24). Hili ilikuwa la kushangaza na lisilotarajiw! Vivyo hivyo, ufunuo wa mateka. Kile kilichofikiliwa na Mungu kuwa cha kudumu kiliathiriwa na dhambi ya mwanadamu. Katika njia kama hiyo “agano jipya” la Yer. 31:31-34 na Ezek. 36:22-38 ilikuwa ni agano la kusikitisha. Maagano ya milele yalizidi kuwa mbadala kwa sababu ya kutoweza kwa mwanadamu kushindwa kutenda nafasi yao ya agano. Kwa hiyo, ushirika mpya na Mungu ungalihitajika kutambulika ukiegamia juu ya

1. utendaji wa Mungu (moyo mpya, fikra mpya)
2. mwanadamu kuwezeshwa na Roho wa Mungu kuwa watii

Mungu anahitaji watu wenye haki kuaksi tabia yake kwa ulimwengu uliopotea na wenye uhitaji (yaani., mataifa). Maana ya hiyo “haki” imebadilika. Uwezo wa mwanadamu unathibitisha kuwa wakutotoshereza (kama vile Wagalatia 3). Agano la kale ilikuwa na maana ya kuushangaza uwezo wa mwanadamu!

■ “**kwa kukosa kwao maarifa**” Hii ni kukataliwa kwa maarifa kuliko kusudiwa, na sio ujinga (kama vile Isa. 1:3; Hos. 4:6,14). Yuda anaasi juu ya mapenzi ya Mungu yaliyodhihilishwa (yaani., agano la Musa). Aliiacha wazi njia iliyokuwa ikilindwa!

**5:14 “kuzimu kumeongeza tamaa yake, kumefunua kinywa chake bila kiasi”** “kuzimu” ni neno la Kiebrania (BDB 982) ambalo linarejerea kwenye” ulimwengu wa wafu.” Hapa inanafsisha mnyama akiwa na kiu ya ulafi (kama vile Mhu.1:12; 27:20; Hab. 2:5)

## MADA MAALUMU: WALIOKUFA, WAKO WAPI? (*SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS*)

- I. Agano la Kale
  - A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol*) (hakuna mizizi yenyе chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
  - B. Tabia za shimoni (*sheol*)
    - 1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
    - 2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
    - 3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
    - 4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
    - 5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
    - 6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
    - 7. panahusiana na *utelekezaji* (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa. . . Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
    - 8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
    - 9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*, Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
    - 10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
    - 11. kule watu huitwa *Rephaim* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
    - 12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11
- II. Agano Jipya
  - A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
  - B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheol*)
    - 1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
    - 2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
    - 3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luk 10:15; 16:23-24
    - 4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Luk 16:23
  - C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
    - 1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Luk 23:43
    - 2. Sehemu ya waovu iitwayo “kwenye vifungo vya giza”, iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa “shimoni” Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3
  - D. *Gehenna*
    - 1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, “bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
    - 2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama

vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.

3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
  - a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
  - b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
  - c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
  - d. panafanana na *Sheol*, Mt. 5:29-30; 18:9
  - e. Panaainisha waovu kama "wana wa Jehanamu" Mt. 23:15
  - f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
  - g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimon, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimon, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
  - h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41
- E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimon (*sheol*), kuzimu(*hades*) na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa
  1. kiasili watu wote walikwenda shimon/kuzimu
  2. uzoefu wao wa (memba/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
  3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawesi kutengeneza andiko juu ya mfano.

### III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

- A. Agano jipya halifundishi juu ya "zinaa ya nafsi," ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
  1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
  2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
  3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla
- B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
  1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
  2. Ibrahimu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk 12:26-27; Luk 16:23
  3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
  4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
  5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mpya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
  6. Paulo anadai kuwa waamini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

### IV. Mbinguni

- A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
  1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
  2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26

3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)
- B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).
- C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msembo (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia

- A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*  
 B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

▣ “na utukufu wao, na wingi wao, na ghasia yao, naye pia afurahiye mionganoni mwao, hushuka na kuingia humo”  
 Hii inaonyesha matarajio yaliyo kinyume!

**5:15 “Na mtu mnyonge ainamishwa, na mtu mkubwa amedhilika”** Hili linarejerea kwenye hukumu juu ya jamii yote (kama vile 2:9,12,17). Kunaonekana kutokuwepo kwa tofauti ya kimuktadha kati ya maneno ya Kiebrania kwa ajili ya mtu, ambaye ni Adamu (NASB, “mtu anayejulikana”) na Isaya (NASB, “mtu wa muhimu”).

▣ “na macho yao walioinuka hunyenyekezwa” Hii ni mada inayojirudia kote katika maandiko na imejirudia kidogo katika njia tofauti kwenye mst.20 na 21 kuititia stiari ya nuru na giza.

**5:16 “bali Bwana wa majeshi ametukuzwa katika hukumu”** Uzao wa Ibrahim ulichaguliwa kumdhiihirisha Mungu. Walitakiwa kumdhiihilisha katika uaminifu wao wakitarajia jamii iliyo imara na yenye utosherevu au watamdhiihilisha Yeye ndani ya kutotii kwao ambako kuliwapelekea kwenye hukumu. Waamini ni mashuhuda (kama vile Mt. 5:13-16). Swali ni kuwa,sisi ni mashahidi wa aina gani?

▣ “na Mungu aliye Mtakatifu ametakaswa katika haki” Huu ni ushirika mfanano wa mstari wa ushairi uliopita. Ushairi wa Kiebrania lazima utafasiliwe katika mwanga wa ufanano!

**5:17 “Ndipo wana-kondoo watakapolisha kama katika malisho yao wenyewe, na mahali pao waliowanda, palipoachwa ukiwa, wageni watakula.”** Pamekuwepo na mijadala mingi kati ya watoa maoni kuhusu uhusiano kamili wa huu mstari kwenye muktadha unaoendelea. Baadhi wanaseme

1. unarejerea kwenye uangalizi wa Mungu kwa wale waliobaki katika ile nchi
2. unarejerea kwenye hukumu ya Mungu kwa matajiri wenye kumiliki ardhi
3. unarejerea kwenye mabaki ya Wayahudi waliobaki baada ya kukimbilia uhamishoni
4. unarejerea kwa watu wa mataifa waliorudi tena kukaa kwenye himaya ya Yuda baada ya wazawa kukimbilia uhamishoni

inavyoonekana kwangu kuwa muktadha wa haraka kwa ajili ya hukumu lazima viendane na uharibifu na hukumu ya matajiri na uharibifu wa mali iliyonunuliwa.Ni ardhi ya jumuiya sasa!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:18-23**

<sup>18</sup>Ole wao wavutao uovu kwa kamba za ubatili, na dhambi kama kwa kamba za gari! <sup>19</sup>Wasema, Na afanye haraka, aihimize kazi yake, tupate kuiona; na likaribie shauri lake aliye Mtakatifu wa Israeli, tupate kuliona.

<sup>20</sup>Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru

**badala ya giza; watiao uchungu badala ya utamu, na utamu badala ya uchungu! <sup>21</sup>Ole wao walio wenyewe hekima katika macho yao wenye, na wenyewe busara katika fikra zao wenye! <sup>22</sup>Ole wao walio hodari kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenyewe nguvu kuchanganya vimeo; <sup>23</sup>wampao haki mwenye uovu, ili wapewe ijara, na kumwondolea mwenye haki haki yake!**

**5:18-23** Ubei mwininge wa “ole” juu ya watenda maovu umetajwa kwa sababu

1. mst. 18, huukumbatia uovu kama mnyama aliye kwenye kamba
2. mst. 19, humwitaji YHWH kwa upesi kutimiliza ahadi zake za agano (pasipo kuchunguza mahitaji ya agano)
3. mst. 20, hili laweza kuhusiana na lile la mst. 19. Pale Mungu asipotenda kulingana na matakwa yao, huuita utendaji wake ni wa kiovu, wa giza na wa uchungu
4. mst. 21, wanadhani hekima yao kuwa ya kweli na ya Mungu kuwa isio ya kweli (mistari. 19-20)
5. mst. 22, wamelewa kwa kileo chenye nguvu
6. mst. 23, hupindisha haki ili wapate ijara yao

wanatawala kwa hila za ubinafsi!

**5:18-19“Ole wao wavutao uovu kwa kamba za ubatili, na dhambi kama kwa kamba za gari”** Kwa habari za Kiebrania haijulikani. Hili linaonekana kurejerea kwenye kundi la watu amba wamechaguliwa kama wenye kutenda wasiomwamini Mungu. Wanakubaliana kuwepo kwa Mungu kithiolojia, lakini wakikataa kutembea katika maarifa haya. Wamechagua kuishi kana kwamba hapakuwepo na Mungu na hata kukejeri uwepo wake (kama vile mst 19). wakizishikilia dhambi zao kwa gharama ye yeyote ile! Wamefungwa/kushikiliwa kwenye maisha ya ubinafsi wao!

**5:19** Kuna amri mbalimbali katika mistari huu.

1. Na afanye haraka, BDB 554, KB 553, *Piel KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika katika maana ya KAULI AMRISHI
2. Na aharakishe, BDB 301, KB 300, *Hiphil HALI YA KUSIHI*
3. Na likaribie shauri lake aliye Mtakatifu wa Israeli, BDB 897, KB 1132, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika katika maana ya KAULI AMRISHI (“aliye Mtakatifu wa Israeli” ni wadhifa kwa ajili ya Uungu ulio wa kawaida katika kitabu cha Isaya; angalia muhtasari katika 1:4)
4. Tupate kuliona, BDB 97, KB 112, *Qal HALI YA KUSIHI*
5. Ili kwamba tupate kulijua, BDB 393, KB 390, *Qal HALI YA KUSIHI*

Huu mistari unaweza kuelezewa kimuktadha kwa mistari wa 12! Kiukweli hawahitaji kuyaolewa mapenzi na makusudi ya Mungu kwa sababu wamejikita kwenye mapenzi na makusudi yao. Matokeo ya anguko (Mwanzo 3) yanaendelea!

Toleo la NASB Study Bible linatengeneza hoja ya kufurahisha kuhusu #1 na #2 hapo juu.

“maneno ya Kiebrania ‘na afanye haraka’ na ‘aharakishe’ yanaendana na ile sehemu ya kwanza na ya tatu ya jina ‘Maher-shalal-hash-baz’ (likimaanisha ‘kuteka nyara, na kuchukua mateka,’ angalia 8:1,3), angeliweza kuvutika kwenye vijembe vya dhihaka za dhambi zao” (uk. 967).

**5:20 “ole wao wasemao kuwa uovu ni wema, na wema ni uovu”** Wengi wanasema kuwa hili linarejerea kwa waamuzi wa Israeli. Ingawa hilo linafaa kwenye mistari ya 18-23, linaonekana kwangu kuwa rejeo kwenye jamii kwa ujumla, halikuziiliwa kwenye kundi la waamuzi. Huu ni mfano wa kusikitisha wa majonzi kwa kile kilichotokea pindi nuru yetu inakuwa giza (kama vile Mt. 6:22-23). Anguko la kwenye Mwanzo 3 limeathiri eneo lote la uadiilifu wa viumbe hai vilivyoumbwa kwa sura na mfano wa Mungu wa haki!

**5:21 “ole wao walio wenyewe hekima katika macho yao wenye, na busara katika fikra zao wenye”** Hili tena linarejerea kwenye dhambi ya majivuno (yaani., matokeo ya Mwanzo 3). Yumkini ni moja ya sura ya kiwango cha juu ya kwenye kitabu cha Yer. 9:23-24. Hekima ya kweli ni ile ya kumjua na kumwamini Mungu! Wanadamu wamepofushwa wenye na dhambi, na mambo yao wenye (kama vile Mhu. 26:5,12,16; 28:11).

**5:22 “ole wao walio hodari kunywa kileo”** Isaya anatumia kejeri kwa sababu neno “shujaa” kwa kawaida linarejerea kwa “watu hodari wa vita,” lakini katika muktadha huu linarejerea kwenye “vinywaji vyenye nguvu” na wala sio matumizi ya kijeshi.

▣“chenye nguvu” Pamekuwepo na baadhi ya maswali kwa kile (BDB 1016) hili neno linakirejerea.

1. Kuchanganya mvinyo na maji, 1:22, kama Wayunani na Warumi, lakini maandiko ya Isaya yanarejerea kwenye mvinyo isio bora, na sio mvinyo ya kawaida
2. Mvinyo wa zamani ulio wenye nguvu ukichanganywa na ule mpya
3. Mvinyo uliochanganywa na wa matunda mengine au asali, ambao huifanya ileweshe zaidi (hawakuwa na vinywaji vilivyo chachushwa vyenye kiwango kikubwa cha pombe, kama ilivyo sasa)

Huu ni muundo wa NOMINO wa KITENZI “kulewa.” Ulevi unalaaniwa mara nyingi katika maandiko (kama vile 5:11,22; 28:7; 56:12; Mith. 20:1; 23:29-35; Micah 2:11). Hata kimetumika kama stiari kwa ajili ya hukumu ya YHWH (kama vile Zab. 75:8). Angalia Mada Maalum katika 1:22.

**5:23 “wawapao haki wenyewe uovu”** Hii ni sehemu kwenye ubeti wa wimbo ambayo watoa maoni hujadili kutokuwepo na ole saba. Swali la kifasiri ni ikiwa kuna ole saba (hesabu timilifu) au ole sita (hesabu ya mwanadamu isio timilifu). Kutotenda haki kumelaaniwa katika Isa. 1:23; 10:1-2 (kama vile Kut. 23:8; Kumb. 10:17; 16:19; Mith.17:23; Mika 3:11; 7:3).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:24-25

<sup>24</sup>Kwa hiyo kama vile mwali wa moto uteketezavyo mabua makavu, na kama manyasi makavu yaangukavyo katika mwali wa moto; kadhalika shina lao litakuwa kama ubovu, na ua lao litapeperushwa juu kama mavumbi; kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana wa majeshi, na kulidharau neno lake aliye Mtakatifu wa Israeli. <sup>25</sup>Kwa sababu hiyo hasira ya Bwana imewaka juu ya watu wake, naye amenyosha mkono wake juu yao; akawapiga, navyo vilima vilitetemeka, na mizoga yao ilikuwa kama takataka katika njia kuu. Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali, lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa.

**5:24** Moto ni stiari kwa ajili ya hukumu na utakaso (yaani., manyasi makavu na mabua makavu yateketeavyo kwa haraka, Kama vile 33:11; 47:14; Yoeli 2:5; Mt. 4:1). Angalia Mada Maalum: Moto katika 1:31.

▣“kadhalika shina lao litakuwa kama ubovu, na ua lao litapeperushwa juu kama mavumbi” Hii ni stiari ya Kiebrania kwa ajili ya uteketezaji.

▣“kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana wa Majeshi, na kuridharau neno lake aliye Mtakatifu wa Israeli” Hii ndiyo sababu kwa ajili ya Hukumu. Ulikuwa ni ukaidi, na makusudi kwa watu wa Yudea kumkataa Mungu wao wa agano.(hasa mst. 19). Tambua sifa mbili kwa ajili ya Uungu. Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:1.

**5:25 “kwa sababu hiyo hasira ya Bwana imewaka juu ya watu wake”** Hukumu itaanzia nyumbani mwa watu wa Mungu. Hasira ya Mungu ni mada ya kibiblia kama ulivyo upendo! Hasira imesisitizwa hata kwenye uwepo wa nuru kubwa (kama vile Luka 12:48).

▣“na vilima vikitetemeka” Wengi wamefikiri kuwa hili linarejerea kwenye tetemeko lililoandikwa siku zile za Uzia (kama vile Amosi 1:1; Zak. 14:5). Hata hivyo, yawezakuwa ni ukosoaji mno wa Mungu kufanyika mwili. Viumbe vyote vitatetemeka kwenye ujio wa Muumba wao. Picha hii ni ya kawaida katika Agano la Kale (yaani., 64:3; Kut. 19:18; Yer. 4:24; Yoeli 2:10; Nah. 1:5).

▣“na mizoga yao ilikuwa kama takataka katika njia kuu” Watu wa agano la kale walisikitshwa na miili iliyotapakaa, imeoza, iliyowachwa wazi, au kuliwa na wanyama (yaani., Ezek. 39:4,17-20; Nahum3:3). Maziko yaliyostahili yaliathiri furaha ya mtu baada ya kufa. Ilikuwa ni laana na kitu cha kushangaza kwa mtu kutozikwa (kama vile I Sam. 31:8-13).

## MADA MAALUMU:TARATIBU ZA MAZISHI

- I. Mesopotamia
  - A. Mazishi sahihi yalikuwa muhimu sana kwa maisha ya baadae yenyeye furaha ambayo daima yalitazamwa kama mwendelezo wa maisha yaliyopo hapa, (tazama Mada Maalumu: Wafu wako wapi?).
  - B. Mfano wa laana ya watu wa Mesopotamia ni, "Ardhi haiwezi kuzipokea maiti zenu "
- II. Agano la Kale
  - A. Mazishi yaliyo sahihi yalikuwa muhimu sana (kama vile Mhu. 6:3).
  - B. Yalifanyika haraka sana (kama vile Sara katika Mwanzo 23 na Raheli katika Mwa. 35:19 na tazama Kumb. 21:23).
  - C. Mazishi yasiyo sahihi yalikuwa ishara ya kukataliwa na dhambi.
  - 1. Kumbukumbu la torati 28:26
  - 2. Isaya 14:20
  - 3. Yeremia 8:2; 22:19
  - D. Mazishi yalifanyika kama iwezekanavyo, katika vyumba vyaa familia vya ndani kwa ndani katika maeneo ya nyumbani (yaani , alilala na babazake").
  - E. Hapakuwa na mafuta ya kupaka maiti isioze kama ilivyo kuwa Misri. Mwanadamu alitoka mavumbini na atarudi mavumbini (mf.Mwa. 3:19; Zab. 103:14; 104:29 Pia angalia Mada Maalumu: Uchomaji maiti.
  - F. Katika sheria za dini za Kiyahudi ilikuwa vigumu kuweka usawa wa heshima kamili na kuukabili mwili katika dhana ya kuinajisi sherehe kunakohusishwa na maiti.
- III. Agano Jipyaa
  - A. Mazishi ya haraka yalifuatia kifo, kwa kawaida ilikuwa ndani ya masaa ishirini na nne.Wayahudi kwa kawaida walilinda kaburi kwa siku tatu, wakiamini kuwa nafsi ingeweza kuurudia mwili ndani ya siku hizo (kama vile Yohana 11:39).
  - B. Mazishi yalijumuisha kuosha na kufunika maiti kwa manukato(kama vileYohana 11:44; 19:39-40).
  - C. Hapakuwa na utofauti katika taratibu za maziko kati ya Wayahudi na Wakristo (au kitu kilichowekwa kaburini) katika karne ya kwanza huko Palestina.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:26-30

<sup>26</sup>Naye atawatweke bendera mataifa toka mbali, Nayee atawapigia miunzi tokea mwisho wa nchi; Na tazama, watakuja mbio mbio upesi sana. <sup>27</sup>Miongoni mwao hakuna achokaye wala kukwaa; Hakuna asinziaye wala kulala usingizi; Wala mshipi wa viuno vyao hautalegeea. Wala ukanda wa viatu vyao hautakatika;<sup>28</sup>Mishale yao ni mikali, na pindi zao zote zimepindika; Kwato za farasi zao zitahesabika kama gumegume; Na gurudumu zao kama kisulisuli; <sup>29</sup>Ngurumo yao itakuwa kama ya simba; Watanguruma kama wana-simba; Naam, watanguruma na kukamata mateka, Na kuyachukua na kwenda zao salama, Wala hakuna mtu atakayeokoa<sup>30</sup>Nao watanguruma juu yao siku hiyo Kama ngurumo ya bahari; Na mtu akitazama nchi, ataona giza na dhiki Nayo nuru imetiwa giza katika mawingu yake.

**5:26 "Naye atawatweke bendera mataifa toka mbali"** "Bendera" (BDB 651) ilikuwa ni njia ya kijeshi kuwasiliana (kama vile 11:12; 18:3; 30:17; 31:9; 49:22). Yawezakuwa ni chanya (urejesho) au hasi (uvamizi) ikitegemeana na muktadha. Katika muktadha huu inashiria wavamizi kuvamia!

Hiki ni kifungu haswa chenye umuhimu kwa ajili ya sababu zifuatazo: (1) tambua kuwa Mungu yuko katika udhibiti wa historia, historia zote, vile vile pia viumbe vyote; (2) tambua kuwa aliwatweke bendera kwa mataifa ya wapagani. Wengi wameuona mstari huu kama dokezo kwenye Kumb. 28:49-57.

Ndani ya kitabu cha Isaya inaonekana kuwa rejeo kwenye ujumuisho wa watu wa mataifa (kama vile Isa. 1:2-4; 11:9,10,11; 27:13; 49:22; 56:7; 62:10; 66:19)! Neno "mataifa" katika andiko la Kimasoreti liko katika HALI YA WINGI, goyim. Watafasiri wa kisasa wanilibadili kuwa katika HALI YA UMOJA, hata hivyo, HALI YA UMOJA yumkini inarejerea kwenye uvamizi wa jeshi la kukodiwa lililoundwa kutokana na mataifa mengi. Ashuru na Babeli waliwaandikisha wanajeshi wa jeshi lililoshindwa kwa nafasi za vyeo vyao.

■“**atawapiglia mluzi**” Hii ni stiari kwa ajili ya YHWH akiyaita mataifa ya wapagani kuingia kwenye vita na watu wake walio wakosaji (kama vile 7:18). Mzizi ule ule wa neno (BDB 1056) pia unamaanisha “busu” kama alama ya maudhi, mshangao, au dhihaka.

■“**toka miisho ya dunia**” Hiki ni kifungu chenye kukosoa mno. Inaonyesha mataifa nje ya ulimwengu wa mahali wa siasa na biashara za kila mara. Inaaksi laana ya agano la Kumb. 28:49.

**5:27-30** Hii sehemu ya ubeti wa wimbo inaelezea juu ya jeshi la uvamizi lisiloonekana. Mshangao wa haya maelezo ni kuwa unafuatisha maneno yaliyotumika kuiezea Israeli iliyo aminifu katika Isa. 40:29-31. Mungu yuko kinyume na agano la watu wake! Atawapigania juu ya jeshi vamizi la wapagani (kama vile Habakkuk 1-2).

**5:28 “kama upepo wa kisurisuri”** Neno (BDB 693) linaelezea juu ya dhoruba yenyе kuleta maangamivu.

1. Maana iliyo wazi, Isa. 17:13; 21:1; Job 21:18; 37:9; Ps. 83:15
2. stiari, Isa. 29:6; Jer. 4:12-13
  - a. ya wapanda farasi wa YHWH, Isa. 66:15; Yer. 4:13
  - b. ya wavanizi aliowatuma YHWH, Isa. 5:28

**5:29 “hakuna mtu atakayeokoka”** Hii KAULI YENYE HALI YA KUENDELEA (BDB 664, KB 717, *Hiphil* KAULI ENDELEVU ) inamaanisha “kupokonya” au “kuokoa” (kama vile 42:22; 43:13; 47:14; Hos. 5:14; Mika 5:8). Matendo ya YHWH ni ya uhakika. Hapana mtu au hakuna kitu kiwezacho kuharibu mapenzi yake (yaani., hukumu au wokovu).

**5:30b,c** Nchi yenyе nuru ya YHWH imekuwa nchi ya giza. Jeshi la kipagani linadhihirisha juu ya ushindi wa Kiungu uliopangwa! Ni matarajio yaliyo kinyume kiasi gani!!!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenywewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa nini Isaya aliichagua njia hii (nyimbo za jadi) ya kuwasilisha ukweli?
2. Ni ipi tofauti kati ya hukumu tendaji ya muda na hukumu tendwa ya muda? (kama vile Romans 1:24, 28)
3. Ni kipi kiini cha ukweli kuhusu wimbo wa mafumbo? Unatumikaje kwenye siku zetu za leo?
4. Orodhesha dhambi zilizodokezwa kwenye mistari ya 8-23.
5. ni taifa lipi ambalo mistari ya 26 na kuendelea linarejerewa na kwa nini?

## ISAYA 6

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Maono ya Isaya 6:1-5 (3b)	Isaya anaitwa kuwa Nabii 6:1-5 (3b)	Kuitwa kwa Isaya 6:1-5 (3b)	Mungu anamuita Isaya kuwa nabii 6:1-3 (3b) 6:4	Kuitwa kwa Isaya 6:1-3 (3b) 6:4-5
6:6-7	6:6-7 (7b)	6:6-13	6:6-7	6:6-10 (7b)
Agizo la Isaya 6:8-13 (9b-10) (11b-13)	6:8 (8b) 6:9-10 (9b) (10) 6:11-13 (11b-13)	6:8a 6:8b 8b (9b-13)	6:9-10 6:11a 6:11b-13a 6:13b	6:8a (8b) (9b-10) 6:11-13

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi katika sehemu ya utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuvuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiuu cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kumekuwepo na swali siku zote kuhusu kwanini wito wa Isaya kwenye huduma inatokea sura ya 6 na sio sura ya 1
  1. Vitabu vya Agano la Kale vimepangiliwa katika namna ambayo watu wa kisasa na haswa wa magharibi hawaelewi. Mara kwa mara haviafuate mtiririko ambayo inashangaza wafasiri wengi wa isasa. Vina maudhui lakini katika mtindo wa mbinu ya usambamba katika ngazi ya ubeti.
  2. Inawezekana kwa hakika kwamba sura ya 1-5 ni utangulizi wa jumla kwa maudhui ya kitabu kizima. Maudhui mengi kama siyo yote yametambulishwa.
    - a. dhambi za watu wa agano
    - b. madhara ya kutotii
    - c. urejesho kupitia mteule Ajaye
    - d. siku mpya ya haki

- e. utawala wa kiujumla wa Mungu katika mazingira ya kinadharia (Edeni kurejeshwa)
- B. Toleo la Jewish Study Bible (ukurasa wa 796) unatoa maoni ya kushangaza juu ya kuwekwa kwa sura ya 6. Tanbihi inaelezea kwamba sura ya 6 sio mwanzo wa huduma ya Isaya bali majukumu mapya. Katika sura za 1-5 nabii anaitakla Yuda itubu lakini baada ya ufunuo wa 6:9-10, haitokei tena katika unabii wote (sura za 7-66) kuita watu kutubu. Hukumu ni halkika na isiyokwepeka. Kuna tumaini ya siku mpya lakini ni baadaye ya tumaini tu.
- C. Kama sura ya 6 inafunua hukumu mbaya na ya kutisha na kamili ya YHWH juu ya watu wa agano wasio kuwa na utii, sura ya 12 inafunua siku mpya ya tumaini na urejesho. Hata mamlaka ya kimisionari yanafanywa upya (kama vile 12:4-5). Huu mvutano wa kithiolojia ni tabia ya ujumbe wa nabii. Zina hamasisha agano la Ki-Musa la
  - 1. madhara ya kutotii na
  - 2. ahadi ya utii

## AINISHO FUPI

- A. Isaya alimuona Mungu kama alivyo. Mistari ya 1-4
- B. Isaya alijiona yeye mwenyewe sawasawa kama alivyokuwa. Mstari wa 5
- C. Isaya alijiona jamii yake namna ilivyokuwa. Mstari wa 5
- D. Isaya alikuwa ameteakaswa ili kutumikia. Mistari ya 6-7
- E. Isaya alikuwa tayari kwenda. mistari ya 9-13

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 6:1-5

<sup>1</sup> Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu. <sup>2</sup> Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. <sup>3</sup> Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake. <sup>4</sup> Na misingi ya vizingiti ikitikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.

<sup>5</sup> Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea;  
kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu,  
nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu;  
na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi.

**6:1 “mfalme Uzia”** Uzia (792-740 k.k.) alikuwa mmoja wa wafalme wa kiungu wa Yuda (kama vile II Wafalme 15:3; II Nyakati 26:4-5). Inawezekana kwamba Isaya na Uzia walikuwa na uhusiano wa kiundugu (“iah” inawezekana ikawa ilikuwa viambishi tamati vya majina ya kifalme). Uzia alitoa uvumba (ambao ni makuhani wa kilawi tu wangeweza kutoa) na alitandikwa na ukoma (kama vile II Wafalme 15:5; II Nyakati 26:16-23). Uzia anaitwa Azaria katika II Wafalme 15 na Uzia katika II Nyakati 26. Uzia (“nguvu zangu ni YHWH”) ilikuwa ni jina la enzi au tunajifunza kutoka II Nyakati 26:17 kwamba Kuhani Mkuu alikuwa pia anaitwa Azaria, hivyo kupunguza mkanganyiko II Nyakati anatumia Uzia. Ilikuwa ni siku za giza kwa Isaya na Yuda alipokufa mnamo mwaka 740 k.k. Yuda ilikuwa imekwisha imarika katika utawala wake.

❑“**nalimwona Bwana**” Ilikuwa imani ya kawaida kwamba kumuona Mungu ilimaanisha kuona mauti (kama vile Mwanzo 16:13; Kutoka 33:20; I Wafalme 19:13; Isa. 6:5; Yohana 1:18; 6:46; I Tim. 6:16). Huu ulikuwa wakati wa maumivu makali sana! Inavyoonekana, Isaya alikiona kiti cha enzi cha Mungu na vazi lake lakini si uso wake (kama vile Yohana 12:41).

Kuna baahi ya maandiko ya Agano la Kale ambayo yanamaanisha kuwa Mungu anaweza kuonekanika.

1. Musa, Kutoka. 33:11; Hesabu. 12:8; Kumb. 34:10
2. Musa, Haruni, Nadabu, Abihu, na wazee sabini, Kutoka 24:10-11

Maswali yanaendana na matokeo ya mtu mdhambi katika uwepo wa Mungu mtakatifu. Ni swali la ushirika wa karibu wa kibinafsi. Inavyoonekana kuona sio jambo la msingi lakini mahusiano yanaanzishwa na Mungu!

■“**Bwana**” Hii inafasiriwa kutoka katika neno la Kiebrania *adonai* (BDB 10, angalia Mada Maalum katika 1:1). Baadhi ya Maandiko ya kale ya Kiebrania “YHWH.”

■“**kiti cha enzi**” YHWH kuchukuliwa kama picha kukaa katika kiti cha enzi inachukuliwa kwanza katika maono ya mahakama ya kimbingu | Wafalme 22:19; Zaburi 103:19; na baadaye katika Isaya 66:1. Katika Ezekiel 1 na 10 Kiti cha enzi cha YHWH ni gari lake la farasi linalohamishiwa (yaani mbali na hekalu la Yerusalem). Hii ni lugha ya kibinadamu ya Mashariki ya karibu (kama vile mstari wa 5; Ufunuo 4:2,3; 20:11, angalia N. T. Wright, *The Language and Imagery of the Bible*, kurasa 172-182).

## MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UNGU

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Ungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
  - A. Viungo vya mwili
    1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
    2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
    3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
    4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
    5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
    6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
    7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
    8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
    9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
    10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
    1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
    2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
    3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
    4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
    5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
    6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
  - C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
    1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
    2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
    3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
    4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
  - D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
    1. Baba
      - a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
      - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
      - c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
    2. Mzazi – Hosea 11:1-4
    3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
    4. Kijana mpandwa mwaminifu-Hosea 1-3
- II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
  - B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
  - C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwengine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yejote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
  - D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadiliwa kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).
- III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika The International Standard Bible Encyclopaedia, kurasa za. 152-154

▣ “na pindo za vazi lake” Mavazi ya kifalme yalikuwa na urefu mkubwa sana. Isaya alimuona Mungu kama watu wa siku zake walivyomtegemea yeye kuwa. Alikuwa katika hekalu la kimbingu (kama vile Waibrania 9:11,24; Ufunuo 5-6). Wafasiri wengi wameona vazi hili refu kama njia ya kuficha tabia za uso wa Mungu (kama ilivyo moshi katika mstari wa 4). Ilikuwa kama kijifuniko kitu kama *Shekinah* Wingu la utukufu wakati wa kipindi cha kuzunguka jangwani.

## 6:2 “Maserafi” angalia Mada Maalum ianayofuata.

### MADA MAALUM: MASERAIFI (BDB 977 II, KB 1360, #4)

- A. Isaya 6 inajumuisha kutajwa kwao tu katika Biblia.
- B. Ni vyeo vya kiwango fulani vya kimalaika ambaao majina yao yana maana ya "wale wachomwao" (BDB 977 II). Neno linatoka katika mzizi "kuchoma" (BDB 976).
- C. Katika Ufunuo 4:8, inaonekana kwamba *Maserafi* na *Makerubi* yanaunganishwa. "viumble majitu" wanaonekana kama *Makerubi* wenyewe mabawa mawili (Kutoka 25:19) au mbawa nne (Ezek. 1:6-14), lakini katika Ufunuo wana mabawa sita na wanakaa mahali pa *Seraphim*.
- D. Yawezekana yanahuasiana na
  1. "nyoka wapao," Hes. 21:8; Kumb. 8:15; Isa. 14:29; 30:6 (BDB 977 I pamoja na BDB 733)
  2. neno la Kimisri *serref* ("mlinzi griffin," muunganiko wa simba na tai)
  3. "nyoka wenyewe mabawa," kutoka Tut-anhk-kiti cha enzi cha amoni (ANEP 415-417)
  4. mzizi mwengine wa Kiebrania (BDB 978), ikimaanisha "Mkuu," katika kiarabu inaitwa "sharafa," ikimaanisha "kuwa wa tahamani" (2 PER, vol. 5, ukurasa wa 349)
- E. Katika simulizi za Kiyahudi zinaunganishwa pamoja na "radi."
- F. Kuna mengi sana juu ya ulimwengu wa roho ambaao Mungu amechagua kutofunua kwetu. Kuwa mwangalifu juu ya (1) madhanio; (2) nadharia za kimantiki; na(3) yakiunganisha hadithi za kufikirika za kishujaa za kipagani!

## 6:2 “mabawa sita” inashangaza juu ya matumizi ya mbawa zake.

1. Kufunika macho yao. Utukufu wa Mungu unapita kawaida hata kwa malaika wahudumiao kitu cha enzi.
2. Kufunika miguu yao. Kuwa makini juu ya kugeuza maelezo ya kufanyika mwili kwenda kwenye vitu vya kawaida au viumble. Mara kwa mara miguu ni kupunguza ukali wa maneno ya sehemu za siri (kama vile 7:20; Kutoka 4:25; Waamuzi 3:24; Ruth 3:4,7,8,14; I Sam. 24:3), lakini hapa kwasababu ya Mt. 22:30, yawezekana sio. Hii inaweza kuwa ishara ya unyenyekevu mbele ya utakatifu (Kama vile Kutoka 3:5).
3. kupaa ili kuweza kufanya kazi za kutumwa na Mungu haraka haraka (kama vile mstari wa 6)

## 6:3 “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu” Utakatifu ni Dhima kuu ya Isaya.

1. שְׁתִּירָה, KIVUMISHI, BDB 872, "takatifu," "iliyowekwa wakfu"
  - a. utakatifu wa
    - 1) Mungu, 5:16; 6:3 (mara tatu)
    - 2) Jina lake, 40:25; 49:7; 57:15
    - 3) maagano yake, 57:15
    - 4) Sabatho yake, 58:13
2. שְׁתִּירָה, KITENZI, BDB 872, "kutengwa," "kutakaswa"
  - a. tabia ya Mungu, 5:16; 29:23
  - b. Mungu, 8:13; 65:5
  - c. malaika wa Mungu, 13:3
  - d. jina la Mungu, 29:23
  - e. sherehe, 30:29
  - f. wanadamu waliotakaswa, 66:17
3. שְׁתִּירָה, NOMINO, BDB 871, "kutengwa," "kuwekwa wakfu"
  - a. uzao mtakatifu, 6:13
  - b. mlima mtakatifu, 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
  - c. kutenga, 23:18
  - d. njia ya utakatifu, 35:8
  - e. madhabahu, 43:28; 62:9; 64:11
  - f. jiji takatifu, 48:2; 52:1
  - g. mtakatifu, 49:7
  - h. mkono mtakatifu, 52:10
  - i. siku takatifu, 58:13
  - j. watu watakatifu, 62:12
  - k. Roho Mtakatifu, 63:10,11
  - l. Kiti cha enzi cha Mungu, 63:15
  - m. mahali patakatifu, 63:18
  - n. majiji matakatifu, 64:10

Kurudiwa kwa mara tatu kunaashiria ULINGANIFU WA UTATU wa kiebrania (kama vile Yer. 7:4; Ezek. 21:27).

## MADA MAALUMU: MTAKATIFU

- . Agano la Kale (likielezwa kwa zaidi kutoka Isaya)
  - A. Asili ya neno *kadosh* (BDB 872, KB 1072) halina uhakika, pengine ni Ki-kanaani (yaani, lugha Magharibi mwa Syria). Inawezekana kwamba sehemu ya mzizi wa neno (yaani, *kd*) unamaanisha "kugawanya." Hiki ni chanzo cha ufanuzi unaofahamika wa neno "tengwa (kutoka kwenye utamaduni wa ki- Kanaani, kama vile Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19) kwa matumizi ya Mungu."
    - B. Inahusiana na uwepo wa Mungu ndani ya vitu, mahali, wakati, na watu. Halitumiki katika kitabu cha Mwanzo, bali linakuwa la kawaida katika vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu.
    - C. Katika fasihi ya Kinabii (hasa Isaya na Hosea) hali ya kibinadamu ilikuwepo hapo awali, lakini haikuhimizwa kwa ajili ya kutenda kazi (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu). Inakuwa njia ya kueleza asili ya Mungu.(kama vile Isa. 6:3). Mungu ni Mtakatifu. Jina Lake linalowakilisha sifa yake ni takatifu. Watu wake ndio wanaopaswa kuifunua sifa Yake kwa ulimwengu unaohitaji utakatifu (ikiwa watalitii agano katika imani).
      1. KIVUMISHI, BDB 872 תְּקִנֵּשׁ, "takatifu," "tukufu" linatumika juu ya
        - a. Mungu, Isa. 5:16; 6:3 (mara tatu); tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu
        - b. Jina Lake, Isa. 40:25; 49:7; 57:15
        - c. kukaa Kwake ndani, Isa. 57:15
        - d. Sabato, Isa. 58:13
      2. KITENZI, BDB 872 קַנֵּשׁ, "kutengwa mbali," "wekwa wakfu"

- a. sifa ya Mungu, Isa. 5:16; 29:23
- b. Mungu, Isa. 8:13; 65:5
- c. malaika wa Mungu, Isa. 13:3
- d. jina la Mungu, Isa. 29:23
- e. sherehe za kidini, Isa. 30:29
- f. wanadamu walioweka wakfu, Isa. 66:17
- 3. NOMINO, BDB 871 נַשׁ, "utengwaji," "uwekwaji wakfu"
  - a. uzao mtakatifu, Isa. 6:13
  - b. mlima mtakatifu, Isa. 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
  - c. kutengwa, Isa. 23:18
  - d. njia ya utakatifu, Isa. 35:8
  - e. mahali patakatifu, Isa. 43:28; 62:9; 64:11
  - f. mji mtakatifu, Isa. 48:2; 52:1
  - g. aliye Mtakatifu, Isa. 49:7 (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu)
  - h. mkono mtakatifu, Isa. 52:10
  - i. siku takatifu, Isa. 58:13
  - j. watu watakatifu, Isa. 62:12
  - k. Roha Mtakatifu, 63:10,11
  - l. Kiti cha enzi cha Mungu, Isa. 63:15
  - m. sehemu takatifu, Isa. 63:18
  - n. miji mitakatifu, Isa. 64:10
- D. Huruma ya Mungu na upendo havitenganishwi kutoka katika dhana ya theojia ya maagano, haki, na sifa ya muhimu. Humu ndani pana mvutano wa Mungu dhidi ya utu ulioanguka, usio mtakatifu, wenye kuasi. Kuna mada inayotia shauku sana kuhusiana na mahuhusiano kati ya Mungu kama "mwenye huruma" na Mungu kama "mtakatifu" katika kitabu cha Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 112-113.
- . Agano Jipy
  - A. Waandishi wa Agano Jipy (isipokuwa Luka) walikuwa Waebrania wenye fikra pana, lakini waliandika katika lugha ya kawaida ya Koine. Kanisa la Agano Jipy lilitumia fasiri ya Kiyunani kufasiri kitabu cha Agano la Kale. Ilikuwa ni tafasili ya Kiyunani ya Agano la Kale, sio fasihi ya Kiyunani cha daraja la juu, fikra, au dini, iliyodhibiti misamiati yao.
  - B. Yesu ni mtakatifu kwa kuwa Yeye ni wa Mungu na ni sawa na Mungu (kama vile Luka 1:35; 4:34; Matendo 3:14; 4:27,30; Ufu. 3:7). Yeye ni Mtakatifu na Mwenye Haki (kama vile Matendo 3:14; 22:14). Yesu ni mtakatifu kwa sababu hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; 2 Cor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).
  - C. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu (kama vile Yohana 17:11; 1 Pet. 1:156-16; Ufu. 4:8; 6:10), watoto Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Mat. 5:48; 1 Pet. 1:16). Kwa kuwa Yesu ni mtakatifu, wafuasi Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Cor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Wakristo wameokolewa ili kutumika katika ufanano wa Kristo (wenye utakatifu).

▣ “BWANA wa Majeshi” Hii kibayana ni “Kapteni wa majeshi ya mbinguni.” Angalia Mada Maalum katika 1:9.

▣ “dunia yote” Hii ni kumaanisha kuabudu Mungu mmoja. Mungu siku zote amekuwa Mungu wa wanadamu (kama vile Mwanzo 1:26,27; 3:15; 12:3; Kutoka. 19:5,6; Hes. 14:21; Zaburi. 2:8; 22:27-28; 59:13; 72:8,19; Isa. 45:21-22; 49:6; 52:10; Mika 5:4). Thiolojia ya Isaya ni ya kiulimwengu (yaani 12:5; 24:14-16; 42:10-12). Angalia Mada Maalum katika 2:2.

**6:4 “yake yeye aliyewaita”** Hii inaweza kurejerea sauti ya Mungu (kama vile mstari wa 8) au katika muktadha wa Maserafi (yaani “mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu” ya mstari wa 3).

■ “**alikuwa akijaza na moshi**” KITENZI (BDB 569, KB 583, *Niphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) inatumika pia katika Ezek. 10:4. Inaweza kuaksi Hes 14:21; Zab 72:19; na Hab. 2:14. Hii inarejerea aidha (1) kiwakilishi cha ishara ya Mungu; (2) rejea ya wingu la *Shekinah*, ambalo linawakilisha llakini linaficha uwepo wa Mungu (kama vile Kutoka 40:34); au (3) moshi kutoka katika uvumba wa madhabahu ili kwamba Mungu asiweze kuonekana.

**6:5 “ole wangu mimi, niliye mchafu”** Hiki KITENZI (BDB 198 II, KB 225, *Niphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) inaashiria uharibifu (yaani “kuwekwa kimya”) kwa mtu au kitu fulani.

1. ya majiji
  - a. ya Moabu, Isa. 15:1
  - b. kwa Philistia, Yer. 47:5
2. kwa watu
  - a. Israeli, Hosea 4:6
  - b. Yerusalem, Zef. 1:11
  - c. Edomu, Obadiah mstari wa 5
3. kwa wafalme
  - a. Israeli, Hosea 10:7,15
  - b. Misri, Ezek. 32:2
4. wanadamu chini ya sitiari ya wanyama, Zaburi 49:13,21
5. kwa Isaya, kwasababu alimuona YHWH, Isa. 6:5

Utakatifu wa Mungu ulimtaarifu Isaya juu ya upungufu wake wa haki ulioambatana na mwitikio unaotakiwa kibiblia juu ya hukumu! Neema ndio msingi, lakini utakatifu ndio lengo (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Kumb. 18:13; Mt. 5:48)! Mtu hawezi kubaki mtu wa aina ileile baada ya kukutana na Mungu, lakini hii ndio hakika watu wake walichokifanya.

■ “**mwenye midomo michafu**” Lugha ya mwanadamu huuaksi moyo wake (kama vile Mt. 15:18; Marko 7:20,23). Hii inaaksiwa katika Isa. 29:13 (Mt. 15:8-9) na Ezek. 33:30-32.

Isaya anatambua dhambi yake mwenyewe (yaani wajibu binafsi wa kiagano, kama vile Ezekiel 18 na 36) dhambi ya jamii (jukumu la kipamoja). Yote ni kweli na yana madhara na faida! Watu wa Mungu walitakiwa kuaksi tabia za YHWH kwa mataifa, lakini walikuwa washarubuniwa na kuharibiwa na mataifa. Yumkini “wasafi wa moyo watamwona Mungu” (kama vile Mt. 5:8),lakini Isaya alijua kwamba hakuwa mmoja wao, wala hakuwa mtu wa agano. Hii ni “ile” mvutano wa “maagano ya kimasharti” na tumaini kwa ajili ya “agano lisilo na masharti” ambalo litatoka katika watu wa Mungu (kama vile Ezek. 36:22-38).

■ “**macho yangu yamemwona Mfalme**” Angalia Kidokezo katika mstari wa 1.

■ “**Mfalme**” Wafalme wa Yuda waliwakilishwa na YHWH aliyekuwa mfalme wa kweli wa watu wa Agano (yaani Kutoka 15:18; Hesabu. 23:21; Waamuzi. 8:23; I Sam. 8:7; 12:12; I Wafalme. 22:19; Yer. 46:18; 48:15; 51:57).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:6-13**

<sup>6</sup> Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye aliquwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo aliquwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu; <sup>7</sup> akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa. <sup>8</sup> Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.

<sup>9</sup> Naye akaniambia, Enenda, ukawaambie watu hawa,

Fulizeni kusikia, lakini msifahamu; fulizeni kutazama, lakini msione.

<sup>10</sup> Uunoneshe moyo wa watu hawa,

ukayatie uzito masikio yao, ukayafumbe macho yao;

wasije wakaona kwa macho yao, na kusikia kwa masikio yao,

na kufahamu kwa miyo yao, na kurejea na kuponywa.

<sup>11</sup> Ndipo nilipouiza, Ee Bwana, hata lini? Naye akanijibu,

Hata miji itakapokuwa ukiwa, haina wenyeji,

**na nyumba zitakapokuwa hazina watu, na nchi hii itakapokuwa ganjo kabisa;**  
**<sup>12</sup> hata Bwana atakapowahamisha watu waende mbali sana,**  
**na mahame yatakapokuwa mengi ndani ya nchi.**  
**<sup>13</sup> Na ijapokuwa imebaki sehemu moja katika sehemu kumi ndani yake,**  
**italiwa hii nayo; kama mvinje na kama mwaloni,**  
**ambao shina lake limebak, ingawa imekatwa;**  
**kadhalika mbegu takatifu ndiyo shina lake.**

**6:6** Mstari huu unamaelezo sana ya taswira. Isaya alikuwa na maono ya hekalu la mbinguni, mahali akaapo Mungu. Siku zote ni ngumu kujua kile kilicho halisi na nini ni taswira! Tunalionia kuititia ukungu kutazama ulimwengu wa roho. Tumekusudiwa kukuza ufahamu wa maelezo ya kimbingu kutokana na maandiko kama haya. Nimtizamo wa jumla/ukweli ulio wa muhimu.

Kitu cha kushangaza ni kwamba Mungu ameanzisha Ufunuo pamoja na uanadamu ulioanguka. Anafunua (1) Yeye mwenyewe; (2) Mpango wake; na (3) mambo yajayo ya mbeleni, kukataa watu wake (kama vile 6:9-13). Yuda anakataa kusikia na kuona lakini Isaya anayekubali dhambi yake anatakaswa na anapatikana (kama vile mstari wa 8).

▣**“madhabahu”** Hii (BDB 258) inaonekana kumaanisha aidha (1) uvumba wa madhabahu kabla ya pazia au (2) madhabahu ya kudhabihu mbee ya mahali patakatifu. Kugusa kinywa cha Isaya kiliwakilisha ibada, kutakaswa kiibada.

**6:7 “akanigusa kinywa changu”** Mbinu hii ya utakaso na kuagizwa ni sawasawa na Yer. 1:9 na Dan. 10:16. Hatahivyo Ezekieli aliambiwa ale gombo (kama vile Ezek. 2:8-10; 3:3), ambayo ni sawasawa na Yer. 15:16 na Ufunuo 10:8-11. Vyote hivi ni sitiari kwa kuweka ndani neno la Kungu ili kuzungumza kwa ukweli kwa wengine.

▣**“na uovu wako umeondolewa”** KITENZI (BDB 693, KB 747, *Qal KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU*) ikimaanisha “kugeuza pembeni” au “kuondoa.” Hapa ni sambamba na “kusamehewa dhambi” (kifasihi. “kufunikwa,” “kulipiwa,” BDB 497, KB 493, *Pual KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, kama vile 22:14; 27:9; 28:18). Isaya amebadilishwa katika kuga’g’ania kwake na YHWH. Ya nyuma yameshashughulikiwa kiufanisi vizuri na yajayo yatakuwa tofauti. Hii inatangazwa na Maserafi, wazungumzao badala ya YHWH! Hiki ni kifungu cha kufurahisha sana juu ya Neema, zaidi kama Paulo alikwa njiani kwenda Dameski alipokutana na Yesu aliyefufuka (kama vile Mdo. 9).

Mbinu kwa ajili ya msamaha kamili na uliomaliziaka na kuondolewa dhambi hakutajwi kwa ufasaha katika hili andiko lakini kutoka 53:5-6 kazi ya msingi ya Masihi, Mtumwa Atesekaye “upatanisho, kulipiwa gharama kimbadala” kunafunuliwa (yaani Mwanzo 3:15; Marko 10:45; Rum. 5:12-21; II Kor. 5:21).

**6:8 “naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?”** Ile “yetu” inamaanisha wingi (kuna mahala pengi kadhaa katika Agano la Kale ambapo wingi unaonekana, kama vile Mwanzo 1:26; 9:6; Kumb. 6:4-5; Zab. 110, kama ilivyo kwa cheo chenye WINGI Elohim, Mwanzo 1:1; 5:1). Philo na Eben Ezra wanasema hii ni “wingi wa kiufalme”; wengine wanadai ni “baraza la mbinguni” (yaani Rashi, kama vile I Wafalme 22:19-23; Ayubu 1:6-12; 2:1-6). Inaweza kumaanisha kuaksi kujako kwa dhana ya ya Utatu.

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno “utatu,” kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

- A. Injili
  - 1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  - 2. Yohana 14:26
- B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
- C. Paulo
  - 1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10

2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
  3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
  4. Gal. 4:4-6
  5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
  6. 1 The. 1:2-5
  7. 2 The. 2:13
  8. Tit. 3:4-6
- D. Petro – 1 Pet. 1:2
- E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

- A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
  1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
- A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  4. Zakaria 3:1-2
- B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
- C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
- D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
- E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliyamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, amba ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho amba ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundi katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipyä linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

▣ “**Mimi hapa**” Hii ni nahau iliyozoleka ya kiebrania kwa upatikanaji (kama vile Mwanzo 22:1,7,11; 27:1; 31:11; 46:2; Kutoka 3:4; I Sam. 3:4,5,6,8,16; 22:12; II Sam. 1:7).

▣ “**nitume mimi**” KITENZI “kutuma” (BDB 1018, KB 1511) ni *Qal KAULI SHURUTISHI* iliyotumika kama maombi. Huu ni mwitikio wa Isaya kwa swali la YHWH. Linafunua kidhahiri upatikanaji wake.

Mtu anaweza kushangaa ni kwa kiasi gani dhana hii ya kiebrania juu ya “ye ye aliyetumwa kiungu” ni uanishi wa Yesu “aliyetumwa” katika Injili ya Yohana na waamini kama Wake “wale waliotumwa” ulimwenguni (kama vile Yohana 17:18; 20:21). Mungu anafikia uumbaji wake ulio wa kikaidi! Siku si nyingi nilisikia ushairi katika moja ya wimbo wa Kikristo “Mungu alimtuma mwanawewe, na bado anawatuma watoto wake.” Maneno yenye nguvu juu ya Mungu na juu ya watu wake!

**6:9-10** Kama vile YHWH anavyofunua kusudi lake kwenye huduma ya Isaya, Pia anafunua kwa Isaya muitikio wake wa ujumbe atakaokuwa nao kwa Yuda.

1. nenda, mstari wa 9, BDB 229, KB 246, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. waambie, mstari wa 9, BDB 55, KB 65, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
3. endelea kusikiliza, mstari wa 9, *Qal KAULI SHURUTISHI* na *Qal KITENZI JINA HALISI* cha BDB 1033, KB 1570
4. lakini hawaelewi, mstari wa 9, BDB 106, KB 122, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU* iliyotumika kama kwa namna ya HALI YA KUSIHI, kama vile 1:3; 5:21; 10:13; 29:14
5. endelea kutazama, mstari wa 9, *Qal KAULI SHURUTISHI* na *Qal KITENZI JINA HALISI* cha BDB 906, KB 1157
6. lakini hawaelewi, mstari wa 9, BDB 393, KB 380, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika katika HALI YA KUSIHI
7. Kufanya miyo ya watu hawa iwe isiosikia (kifasihi. "yenye mafuta"), mstari wa 10, BDB 1031, KB 1566, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
8. masikio yao viziwi, mstari wa 10, BDB 457, KB 455, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
9. na macho yao yasiyoona, mstari wa 10, BDB 1044, KB 1612, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*

Hizi KAULI SHURUTISHI zinafuatiwa na madhara (KAULI ZISIZO ZA WAKATI TIMILIFU tatu za VITENZI vilivyopita awali, "angalia," "kusikia," na "kuelewa"). Mungu anajua (aidha kwa maarifa yake ya mwanzoni au Kufanya kugumu kwa miyo yao iliokwisha kukengeuka) kwamba wataitikia na kuokolewa.

1. wasije wakatubu, BDB 996, KB 1427, *Qal KAULI TIMILIFU* iliyohasishwa
2. wasije wakaponywa, BDB 950, KB 1272, *Qal KAULI TIMILIFU* iliyohasishwa Isaya atahubiri Injili, wingi wa watu wake/jamii hawawezi (kama vile Rum. 1:24,26,28; Efe. 4:19) au hawawezi kuitikia (kama vile 29:9,10; Kumb. 29:4; Mt. 13:13; Rum. 11:8)!

Isaya sio mwinjilisti hapa lakini nabii wa agano la kutotii/madhara ya adhabu (kama vile Mt. 13:13; Marko 4:12; Luka 8:10). Ujumbe wake wa Matumaini ni kwa ajili ya siku zijazo, si siku yake!

**6:10 "yasiyoona"** Hii (BDB 1044, KB 1612) kibayana ni "kufunikwa kwa siri" (kama vile. 29:9; 32:3).

▣ "tubu" Katika misamiati ya Agano la Kale (BDB 996, KB 1427) ikimaanisha "kubadilika kwa tendo." Katika Agano Jipya toba humaanisha "kubadilisha ufahamu." Dhana zote mbili zinahuksika!

## MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)

Dhana hii ni ya muhimu sana lakini ni vigumu kuitolea ufanuzi. Wengi wetu tunao ufanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenye ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

- a. "kupunzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
- b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)
- c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
- d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahuksisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekeea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekeea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekeea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu

ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kuititia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipy inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham* linarejea juu ya hisia zenyenuguu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

**6:11 "hata lini?"** Hii inamaanisha kwa urefu wa muda wa ujumbe wa Mungu utakataliwa.

**6:12 "atakapotahamisha watu waende mbali sana"** Hii inamaanisha kuelekea uhamishoni lakini ikiwa Ashuru ikichukua khabila kaskazini au Babeli kuchukua makabila ya kusini haijulikani (yawezekana utata wa makusudi).

**6:13 "Na ijapokuwa imebaki sehemu moja katika sehemu kumi ndani yake, italiwa hii nayo"** Angalia Mada Maalum: Mabaki, Namna Tatu katika 1:9. Pia kumbuka (1) mwana wa Isaya, Shear-jashub, 7:3, ikimaanisha "mabaki yatarejeshwa" pia (2) kumbuka mjadala katika 10:20-22.

■ “**itatakiwa kuchomwa**” Mstari wa 13, ubeti wa b na c, ingeweza kueleweka katika namna mbili.

1. muktadha wa kifasihi – watu wa Mungu katika sitiari ya mti mkuu umekatwa na kuchomwa, lakini kuna maisha katika shina. Mbegu kitachomoza (yaani Masihi au jamii ya ki-Masihi, kama vile 4:2; 11:1; 53:2; Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12). Lakini matatizo ya wakati ujao (yaani kuchomeka).
2. Kihistoria, kidesturi – miungu ya uzao ya Wakanaani (yaani *Asherah*) yatachomwa kabisa kabisa. Watu wa Mungu watafunguliwa kutoka katika ibada za miungu siku moja!

■ “**ambao shina lake limebaki, ingawa imekatwa**” Mstari wa 13 una maneno mawili yanayotumika hapa tu katika Agano la Kale, maneno ya msingi!

1. “Limeanguka,” BDB 1021 I, mzizi huo huo uliotumika katika lango la hekalu (kama vile I Nyakati 26:16). Maana ya msingi ya mzizi “kutupa,” “kurusha,” au “kurusha.”
2. “hina,” BDB 663, mara kwa mara ikitumika juu ya nguzo ya mawe yaliyowekwa wakfu
  - a. kwa mababa wa imani na Musa
  - b. kwa waamini uzao wa kikanaani (yaani, *Baali*)

■ “**uzao mtakatifu ni shina lake**” Hii kama 4:2, una visawe vya kimasih. Angalia dokezo katika Isa. 11:1. Hii tungo inaachwa nje ya LXX.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini kifo cha Uzia kilimuathiri Isaya kwa ndani?
2. Isaya alimuona nani?
3. Kwa nini ujumbe wa Isaya ulikataliwa?
4. Siku za Isaya zinalinganishwaje na siku zetu?

## ISAYA 7

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Vita dhidi ya Yerusalem	Isaya anatumwa kwa mfalme Ahazi	Isaya na vita vya Waefrahimu wa Shamu (7:1:-8:15)	Ujumbe kwa mfalme Ahazi	Isaya anapatanisha
7:1-2	7:1-2	7:1-2	7:1	7:1-2
			7:2	
7:3-9	7:3-9 (7b-9)	7:3-9 (7b-9)	7:3-9 7:7-9a 7:9b	7:3-9 (7b-9)
Mtoto Immanueli	Unabii wa Immanueli	Ishara ya Immanueli	Ishara ya Immanueli	Isaya anapatanisha tena
7:10-17	7:10-17	7:10-17	7:10-11 7:12 7:13-16 7:17 7:18-19	7:10-12 (11) 7:12 (13b-17P) Unabii wa kushambuliwa 7:18-25 (18-25)
7:18-20	7:18-22 (18-19) (20)	7:18-19 7:20	7:18-19 7:20	7:18-25
7:21-22	(21-22)	7:21-22	7:21-22	
7:24-25	7:23-25 (23-24) (25)	7:23-25	7:23-25	

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)  
**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Sehemu hii ya fasihi (sura 7-12) mara nyingi huitwa” kitabu cha Immanueli”kwa sababu mara zote dhamira ni enzi mpya ambapo atazaliwa mwana wa ajabu ili awakomboe na kuwarejesha watu wa Mungu.
- B. mpangilio wa kifungu hiki cha maneno ni matukio ya kihistoria yanahusiana na vita ya Shamu waliopatana na Efraimu kati ya mwaka wa 735-733 K.K. Ashuru chini ya Tiglath-Pileser III alizivamia shamu na palestina (pia ilitwa *Pulu*, kama vile 2 Fal 15:19).
  - 1. Sura ya 7-10:4 mnamo mwaka wa 735 K.K. (siku za Tiglath-Pileser III, 745-729 K.K.)
  - 2. Sura ya 10:5-34 mnamo mwaka wa 701K.K. (siku za Senakarebu, 705-681 K.K.)
  - 3. Sura ya 11:1-12:26 ishara ya enzi ya masihi.
- C. Sehemu hii yote inahusiana na mwana kama ishara ya matukio ya kihistoria
  - 1. Mzaliwa wa kwanza wa Isaya (Shear-Jashubu), 7:3
  - 2. Mwana kama ishara kwa Ahazi, 7:14-16
  - 3. Mzaliwa wa pili wa Isaya (Maher-shalal-hash-bazi), 8:1,3
  - 4. Masihi kama mwana , 7:14; 9:6-7, 11:1-5
  - 5. Mwana wa enzi mpya, 11:6-9
- D. Soma matukio ya kihistoria yafuatayo yanayofanana na
  - 1. Sura ya 10:4 soma 2 Fal 16 na 2 Nya 28
  - 2. Sura ya 10:5-34 soma 2 Fal 18:17-20:11 na 2 Nyak. 32:9-24
- E. Kuna tofauti ya upungufu wa imani ulioonyeshwa na mfalme Ahazi na imani ilioonyeshwa na mwana wake , mfalme Hezekia ( kama vile . 37:14-20,30). Kumbuka mhusika mkuu kwenye haya maandiko ni Mungu! Anataka akae na watu wake (yaani ., Emmanueli) lakini imani yao /uaminifu ni muhimu sana !

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:1-2

<sup>1</sup>Hata ikawa katika siku za Ahazi, mwana wa Yothamu, mwana wa Uzia, mfalme wa Yuda, Resini, mfalme wa Shamu, na Peka, mwana wa Remalia, mfalme wa Israeli, wakapanda wakaenda Yerusalem ili kupigana nao, lakini hawakuweza kuushinda. <sup>2</sup>Kisha watu wa nyumba ya Daudi wakaambiwa kwamba Shamu wamefanya mapatano na Efraimu. Na moyo wake ukataharuki, na moyo wa watu wake, kama miti ya mwituni itikiswavyo na upepo.

**7:1 “katika siku za Ahazi”** Ahazi alitawala kutoka mwaka wa 735-715K.K. Mpangilio wa sura hii ni uvamizi wa Yuda uliofanywa na shamu na Israeli kwa sababu Yuda hakushirikiana na muungano wao a kijeshi dhidi ya Ashuru.

■“Peka” alijitwalia kitu cha enzi cha kifalme (yaani , kipindi cha utawala wake, kung’aa, 737-732; mdogo, 736-730; toleo la NIV Study Bible, 752-732) makabila kumi ya kusini. Tazama jedwari la “Wafalme wa utawala uliogawanyika” katika kiambatisho cha nne, #3.

**7:2 “*watu wa nyumba ya Daudi wakaambiwa*** Hii inamaanisha taarifa ilipelekwa kwenye familia nzima ya kifalme au taarifa ilitolewa kwa wazi mbele ya baraza.

□

NASB	“amefanya hema”
NKJV	“wamepelekwa katika”
NRSV	“amefanya mapatano na”
TEV	“walikuwa tayari ndani”
NJB	“amezuia”
LXX	“amekubaliana na”
Peshitta	“ameungana na”
REB	“amefanya ushirikiano na”

KITENZI (BDB 628, KB 679, *Qal KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU*) Chenye maana “pumzika.” Katika muktadha huu ina maana walipiga hema ya kudumu katikati. Hii inaonyesha Shamu ilikuwa imara ,kutawala muungano wa kisiasa.

Tambua hiki ni sawa na KITENZI kilichotumika kwenye mst wa 19 kuelezea jeshi kubwa la uvamizi.

□“**moyo wake na moyo wa water wake**” Hii inaweza kurejelea kwenye familia ya kifalme au wakazi wa Yerusalem ambaa waliisikia taarifa.

□“**ukataharuki kama miti ya mwituni itikiswavyo na upepo**”kuna urudiaji wa KITENZI “tikisika,” au “pepesuka” (BDB 631, KB 681, *Qal KAULI SHURUTISHI* na QaL KITENZI JINA CHENYE MUUNDO WA MANENO). Ni wazi mkazo huelezewa kwa KITENZI CHA KAULI ISIO TIMILIFU na KITENZI JINA HALISI, lakini hapa urudiaji wa KITENZI na KITENZI JINA katika muundo unaofanana.

Yuda na uongozi wake waliogopa. Hawakuwa na imani timilifu juu ya uwepo wa YHWH au ahadi zake!

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:3-9

<sup>3</sup>Basi Bwana akamwambia Isaya, Haya, toka, umlaki Ahazi, wewe na Shear-yashubu mwana wako, huko mwisho wa mfereji wa birika la juu, katika njia kuu ya uwanja wa dobi; <sup>4</sup>ukamwombie, Angalia, ukatulie; usiogope wala usife moyo, kwa sababu ya mikia hii miwili ya vinga hivi vitokavyo moshi; kwa sababu ya hasira kali ya Resini na Shamu, na mwana wa Remalia. <sup>5</sup>Kwa kuwa Shamu amekusudia mabaya juu yako, pamoja na Efraimu na mwana wa Remalia, wakisema, <sup>6</sup>Haya, na tupande ili kupigana na Yuda na kuwasumbua, tukabomoe mahali tupate kuingia, na kummilikisha mfalme ndani yake, huyo mwana wa Tabeeli.<sup>7</sup> Bwana MUNGU asema hivi, Neno hili halitasimama wala halitakuwa.<sup>8</sup>Kwa maana kichwa cha Shamu ni Dameski, na kichwa cha Dameski ni Resini; na katika muda wa miaka sitini na mitano Efraimu atavunjika vipande vipande, asiwe kabilia ya watu tena; <sup>9</sup>tena kichwa cha Efraimu ni Samaria, na kichwa cha Samaria ni mwana wa Remalia. Kwamba hamtaki kusadiki, bila shaka hamtathibitika.

**7:3 “Isaya”** Jina lake ni muunganiko wa NOMINO mbili , “wokovu” na “YHWH.” Kutetea ufahamu au kuonyesha maana, KITENZI ni lazima kisadiki, “YHWH ni wokovu,” “YHWH analeta wokovu,” nk.

□“**Shear-yashubu**” Huyu ni mzaliwa wa kwanza wa Isaya. Jina lake lina maana ya “mabaki yatarudi” wa sura ya 10:20-23. Ni jambo la maana kwamba Isaya aliambiwa amchukue mwana wake akampokee mfalme inaonyesha kwamba jina lake lina uhusiano na kusanyiko. Linaweza kuonyesha kuwa

1. Ni sehemu pekee ndogo ya jeshi lilioshambuliwa wanawenza kuokoka na kurudi nyumbani
2. Ni watu wachache wa Yuda wasiokuwa na imani watakaookoka. Isaya anatumia dhana ya “mabaki waaminifu” mara kwa mara. Tazama mada maalumu kwenye 1:9.

□“**huko mwisho wa mfereji wa birika la juu**” Hii inasimulia chemuchemu ya Gihoni ambayo ilisambaza maji katika mji wa Yerusalem wakati wa kuzingirwa na maadui. Chemuchemu hii pia ilitumika wakati wa kutawazwa

kwa wafalme wa Yuda. Ahazi alikuwa anakagua maandalio ya kuzingirwa kwao . alikuwa anakagua nyanzo vyake vya maji!

**7:4-9** Huu ni ujumbe wa YHWH kwa Ahazi kupitia kwa Isaya. Sehemu ya kwanza inamwelezea Ahazi.

1. angalia, BDB 1036, KB 1581, *Niphil KAULI SHURUTISHI*
2. ukatulie, BDB 1052, KB 1641, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
3. usiogope, BDB 431, KB 432, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya KITENZI AMRISHI
4. Wala usife moyo, BDB 939, KB 1236, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya KITENZI AMRISHI

Kilichosababisha hofu ya Ahazi ni mpango wa mashambulizi wa Shamu na Israeli (mst. 5).

YHWH anaainisha mawazo ya muungano ya Shamu waliopatana na Efraimu (mst. 6).

1. Tupande ili tupigane na Yuda, BDB 748, KB 828, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya HALI YA KUSIHI
2. kuwasumbua (pambizo za NASB), BDB 880, KB 1089, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya HALI YA KUSIHI
3. Tukabomoe kuta zake, BDB 131, KB 149, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana HALI YA KUSIHI
4. Tumweke mwana wa Tabeeli kama mfalme, BDB 573, KB 590, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana HALI YA KUSIHI

YHWH anaelezea mipango yake kwenye mst. 7.

1. halitasimama, BDB 877, KB 1086, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
2. Na wala halitapita , BDB 224, KB 243, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*

YHWH ndiye anaeongoza historia , sio majeshi ya wanadamu, kama Shamu/Israeli au Ashuru. Hata hivyo , kunahitajika uongozi wa YHWH badala ya uongozi wa Yuda —ni lazima waamini / kutumaini neno la YHWH (mst. 9)!

1. amini, BDB 52, KB 63, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, WINGI(baraza la kifalme na uongozi, kama vile.mistari ya 13,14)
2. halitadumu (lit. “thibitishwa”), BDB 52, KB 63, *Niphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* , WINGI

Hii ina maana הַיְהּ ni sawa na inayopatikana katika kitabu cha 2 Nya . 20:20. KITENZI hiki ni sawa na kilichotumika katika kitabu cha 2 Sam. 7:16 chenye uhusisno na ufalme wa kudumu wa kiti cha Daudi. Katika mahusiano wa agano YHWH huchagua sio katika matendo kama wafuasi wa agano wanavyokataa kumwamini /kumtumainia yeye (kamavile . 30:15). Tazama mada maalumu kwenye “Amini” 22:25.

▣“**mikia hii miwili ya vinga hivi vitokavyo moshi** ” wavamizi wawili wanaonyeshwa hivi punde “kutokuwa na umuhimu.” Shamu (yaani., Dameski) alianguka chini ya utawala wa Ashuru mwaka wa 732 K.K. Israeli (yaani , Samaria) ilianguka mwaka wa 722 K.K.namba (miaka 65) inaonekana kwenye mst 8 ni vigumu kupatanisha habari ya historia yetu ya sasa na juu ya wakati wa historia hii iliyopita.

## 7:6

<b>NASB</b>	“ <b>tuvunje kuta zake</b> ”
<b>NKJV</b>	“ <b>kutengeneza nafasi kwenye kuta zake</b> ”
<b>NRSV</b>	“ <b>kuitawala</b> ”
<b>NJB</b>	“ <b>kuiharibu</b> ”
<b>Peshitta</b>	“ <b>fanya tundu</b> ”
<b>REB</b>	“ <b>kumvunja moyo</b> ”

KITENZI hiki (BDB 131, KB 149, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* kimetumika kwenye maana HALI YA KUSIHI) kimsingi kina maana “tukabomoe” au “tukabomoe tupate pa kuinggia” (kama vile . 2 Fal. 3:26).

◻ Jina “Tabeeli” (BDB 370) ni jina la ki-ashuru. Kuna maana mbili zimetumika: (1) kacula la watu wakaao Gileadi au (2) jina la mfalme wa Troa (To-ba-il,toleo la LXX Tabeeli, pia linafahamika kwa Ethba’al); hata hivyo , andiko la Kimasoreti linaongeza irabu kwenye jina na kulibadilisha kuwa “Tabeal,” ambalo kwa kiebrania lina maanisha “kitu kisicho na thamani.” Ubadirishwaji wa majina katika Agano la kale ni jambo la kawaida ili kuonyesha mtazamo wa mwandishi juu ya tabia ya mtu. Ingawa , katika muktadha huu inarejerea mtoa msaada wa ki-Ashuru asiyefahamika ndani ya Yuda .

**7:7 “Bwana MUNGU asema hivi, Neno hili halitasimama wala halitakuwa ”** Hii ni moja kati ya aya nyingi kwenye huu muktadha ambaa unafundisha kwamba uongozi na utawala wa Mungu juu ya mataifa yote na historia yote (kama vile . mstr wa 17, 18 na 20). Pia muhtasri wa 8:10 and 28:18.

**7:8 “(na katika muda wa miaka sitini na mitano)”** Hii ni sehemu ya wakati ambaa ni vigumu sana kuutambua. Labda inasimulia kumalizika kufukuzwa kwa Esarhaddoni na kupanga upya makazi katika nchi ya Israeli (kama vile 2 Fal 17:24; Ezra 4:2). Huu unaweza kuwa mfano mzuri wa (1) utabiri wa unabii wenye utata katika Agano la kale; (2) baadae nakili za maandishi ya kale aya za Isaya kufanywa upya na mhariri, au (3) yote kwa pamoja. Toleo la NIV linaelezea neno la Isaya kama “Kwamba hamtaki kusadiki, bila shaka hamtathibitika..”

**7:9 “Kwamba hamtaki kusadiki ”** Angalia Mada Maalumu:Kusadiki , Kuamini,Imani,na Uaminifu katika Agano la kale 22:25.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 7:10-17

<sup>10</sup>Tena Bwana akasema na Ahazi akinena, <sup>11</sup>Jitakie ishara ya Bwana, Mungu wako; itake katika mahali palipo chini sana, au katika mahali palipo juu sana. <sup>12</sup>Lakini Ahazi akasema, Sitaitaka, wala sitamjaribu Bwana.

<sup>13</sup>Naye akasema, Sikilizeni sasa, enyi nyumba ya Daudi; Je! Ni neno dogo kwenu kuwachosha wanadamu, hata mkataka kumchosha Mungu wangu pia? <sup>14</sup>Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwitia jina lake Imanueli. <sup>15</sup>Siagi na asali atakula, wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema. <sup>16</sup>Kwa maana kabla mtoto huyo hajajua kuyakataa mabaya na kuyachagua mema, nchi ile, ambayo wewe unawachukia wafalme wake wawili, itaachwa ukiwa.

<sup>17</sup>Bwana ataleta juu yako, na juu ya watu wako, na juu ya nyumba ya baba yako, siku zisizokuja bado, tangu siku ile alioondoka Efraimu kutoka katika Yuda; yaani, mfalme wa Ashuru.

**7:11** kuna njia mbili za kuelewa aya ya kiebrania katika mst wa . 11.

1. KITENZI kimetumika mara mbili “jitakie” (BDB 981, KB 1371, *Qal KAULI SHURUTISHI*), kama vile toleo la . NKJV, Peshitta
2. KITENZI kimoja kimetumika (**שָׁלֵךְ**) na kimoja kimetumia neno Sheol(**שָׁלֹךְ**– BDB 982), kama vile toleo la. NASB, Vulgate, TEV, NJB, REB (toleo la LXX lina neno “mkazo”)

Mwanzoni wa toleo la UBS inatoa taarifa kwenye aya ya kiebrania inayotupatia neno “itake” mara mbili (KAULI SHURUTISHI itoayo alama “B” (pasipo mashaka). Zote zinafaa kwenye muktadha moja kwa moja. Hapa tena neno sahihi linakuwa sio sahihi, lakini maana halisi ya aya ni dhahili. Huu ni ukweli mkubwa zaidi wa aina hii ya makosa ya maandishi. Kumbuka, maana kuu ya wazo la ubeti (au kifungu), pasipo maelezo , ni ufunguo dhabitii wa kuelewa ufunuo wa Mungu kwetu. Tamani kujua zaidi, zaidi kuliko wengine, sio kutoka kwa Mungu!

Kwa mshangao, Mungu anatamani kumsaidia mtumishi wake mwoga aliamini neno lake. Watu wa Agano lake huwapa ishara (kama vile. 37:30; 38:7,8; 55:13). Aina hii ya uthibitisho wa kimaumbile haupatikani au kuahidiwa kwa wote waaminio (kama vile Mt. 12:38-39; 16:1,4; Marko 8:11-12; 13:4; Luka 11:16,29; Yoh 2:18; 4:48; 6:30; I Kor. 1:22). Ishara na /au miujiza mara nyingi inaweza kuwa ni hila za shetani (kama vile. Mt. 7:21-22; 24:24; Marko 13:22)!

◻“**kutoka kwa BWANA, Mungu wako**” nimuhtasari unaojitokeza kati ya “Mungu wako” na “Mungu wangu”. Hata hivyo , watu wengi wa imani wa Agano la kale walitumia neno “Mungu wako” kwenye mazungumzo na wengine. Ni lahaja isiyokuwa na dhamira ya thiolojia .

■ “**itake katika mahali palipo chini sana, au katika mahali palipo juu sana.**” Nabii anadai kwamba Ahazi anawenza kuuliza ishara yeote katika nchi, chini ya nchi, au juu mbinguni ili kuthibitisha uaminifu wa Mungu. Mungu alitamani hasa kudhihilisha uwepo wake kwa Ahazi. Kwa mjadala wa Sheol tazama Mada Maalumu: Wafu Wako Wapi? katika 5:14.

**7:12 “Lakini Ahazi akasema, Sitaitaka, wala sitamjaribu Bwana.**” Hili linasikika kama maelezo ya maana kwasababu watu wa Mungu wanaambiwa “usimjaribu” (BDB 650, KB 702) Mungu (kama vile Mwa. 17:2;7; Hes. 14:22; Kumb. 6:16; Zab. 78:18,41, 56; 95:9; 106:14). Hata hivyo, kusudi la mfalme huyu ni kwamba tayari alishafanya maamuzi ya kushauriana na Ashuru, sio na Mungu, kwa ajili ya msaada. Sio heshima kwa Mungu. Mungu mwenyewe aliupatia uzao wa kifalme wa Daudi nafasi hii ya kuthibitisha uaminifu wa neno lake, ulinzi, na masharti, lakini yeye Ahazi hakufanya hivyo!

**7:13 “Sikilizeni sasa”** KITENZI hiki (BDB 1033, KB 1570, *Qal KAULI SHURUTISHI, WINGI*) kinatumika mara kwa mara katika Isaya, lakini hapa pekee kwenye “kitabu cha Immanueli” (yaani ., Sura 7-12). Mungu anataka utii na kusikilizwa!

■ “**nyumba ya Daudi**” tungo hii katika muktadha huu , inaweza kuwa jina la shirika , inarejelea kwa Ahazi kama mwakilishi wa uzao wa kifalme wa Daudi (kama vile . 2 Samueli 7).

■ “**je! ni neno dogo**” Hii ni nahau ya kiebrania (BDB 589, kama vile Hes. 16:13; Yosh. 22:17; Ezek. 16:20; 34:18). Watu wanamtendea Mungu na yeye atajifunua ( sheria za Musa) kitu kidogo, kisichokuwa na maana.

■ “**jaribu kuwa na uvumilivu**” KITENZI hiki (BDB 521, KB 512) kimetumika mara mbili.

1. Mara moja kinarejelea mwanadamu (*Hiphil TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*)
2. Mara moja kinarejelea kwa Mungu (*Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*)

Ahazi hakutekeleza wajibu wake kama mwakilishi wa YHWH’ (kama vile ..2 Sam. 7) katikati ya watu!

**7:14 “Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara.”** Ishara hii (BDB 16) ni lazima isimuliwe kwanza katika siku za Ahazi (hasa mst . 15-16)

■ “**bikira**” Neno la kiebrania hapa *nialmah* (BDB 761). Neno hili limetumika kwa ajili ya binti mdogo aliyefikia umri wa kuolewa (kama vile Mwa. 43:24; Kut. 2:8; Mit. 30:19). Linakusudia kwa mwanamke ambaye amepevuka. Kuna neno lingine la kiebrania kwa ajili ya bikira , *bethulah* (BDB 143), ambalo limetumika kwenye Isaya 23:4, 12; 37:22; 47:1; 62:5. Katika tafasiri ya maandiko ya kale ya kiebrania inaitafasiri aya hii ikiwa na neno la Kiyunani “bikira”. Maneno haya yanapishana kielimu-maana na mabinti wadogo katika jamii ya Israel walipaswa kuwa mabikira. Hata hivyo, siwezi kuamini katika kuzaliwa bikira mara mbili, lakini mara moja. Kuna dhana ya kawaida katika siku za Ahazi kama ishara na (“yule” andiko la kimasoreti) ni mwanzo wa siku za Yesu (kama vile . Mat. 1:18-23; Luka 1:26-38). Huu ni utimilifu kamili wa unabii!

Nafikiri ndio sababu kwamba Agano jipyä halitilii mkazo zaidi ( linaonekana tu kwenye vyanzo viwili nya simulizi [ yaani., Mat. 1:23; Luka 1:31,34] na haliko kwenye mahubiri ya matendo au nyaraka za mtume yeote) ni kwasababu ya kutokufahamika kwa dini ya Wayunani-Warumi ambapo miungu na wanadamu ilifungamana, kukatokea uzao, ni wa kawaida.

Kujaribu kusimamia kwenye mafundisho ya dhambi kama inapelekwa kupitia mbegu za uzazi wa mwanaumme na, kwa hiyo inaonyesha kusudi la kuzaliwa na bikira, kwa mtazamo wangu, ni upumbavu! Ukweli ni kwamba inafanana na wanawake tasa wa mababa wa imani walipata mtoto kwa kuamuliwa na Mungu.Mungu ni mtawala wa masihi! Ni ukweli mkuu uliofunuliwa kwenye Agano jipyä ambapo masihi anaonekana kwa dhahili katika Uungu wenye umbo la kibinadamu (yaani ., Yoh 1:1; 5:18; 10:33; 14:9-11; Flp. 2:6)! Hivyo kuhitajika kuzaliwa na bikira!



<b>NASB</b>	<b>“atapata mtoto na kuzaa mwana”</b>
<b>NKJV, Peshitta</b>	<b>“atapata mimba na kuzaa mwana”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“ana mtoto na atazaa mwana”</b>
<b>TEV</b>	<b>“ana mimba atapata mwana”</b>
<b>NJB, REB</b>	<b>“ana mtoto na atamzaa mwana”</b>
<b>LXX</b>	<b>“atakuwa na mtoto na atazaa mwana”</b>

KIVUMISHI(BDB 248) mara kwa mara kinaonyesha mwanamke aliye tayari na mimba, lakini kuna baadhi ya utata, kama inavyoonekana kutoka kwenye tafasiri mbalimbali.

Hii inarejelea mwanamke Fulani wakati wa Isaya; kwa vyovvye alikuwa mke wa mfalme (yaani „kuzaliwa kwa Hezekia), mke wa nabii, au binti mdogo mwenye mashaka katika uwanja wa mahakama, lakini Hezekia (mwana wa Ahazi) ni bora zaidi anafaa kwa muktadha wa ufalme wa Daudi.

■“**Immanueli**” Jina hili (BDB 769) linamaanisha “Mungu pamoja nasi” ( kama vile 8:8,10). Katika nyakati za Isaya watoto wengi walipewa majina yaliyohusiana na Uungu. Jina la mtoto ni ishara, sio namna alivyoziiali! Watu hawa hawakutarajia mwujiza, amezaliwa na bikira, mwili wa binadamu wenye Uungu, mtoto wa mwujiza! Huu si ukweli wa Agano la kale, lakini ni kupiga hatua kwa Agano jipya lililofunua ukweli!

**7:15-16** Aya hizi zinafanana (VITENZI vitatu vimerudiwa). Usambamba huu ni mtindo wa tabia ya fasihi ya Kiebrania ( zote kwenye fasihi , na kwenye kifungu cha maneno na aina ya aya ).

**7:15 “Siagi na asali atakula,”** kuna nadharia mbili kama tungo hii inavyomaanisha: hii ina maana labda atakuja wakati wa utele mwangi (yaani., Kut. 3:8), au kinyume chake, kwamba atakuja wakati wa ukosefu mwangi (kama vile.mst. 21-22).

■“**wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema**” Hii inaonyesha inarejelea kwa

1. “umri wa kufikiria” (yaani ., matokeo ya mafunzo ya kidini)
2. Atakuwa mtoto mdogo ambae ataelewa ni nini kimezuiliwa au kimekubaliwa. Baadae katika maisha ya kiyahudi ilikuwa ni kuanzia umri wa miaka kumi na mitatu (yaani., *Bar-Mitzvah*). Hata hivyo , 8:4 inadokeza mapema zaidi!

**7:16 “nchi ile, ambayo wewe unawachukia wafalme wake wawili, itaachwa ukiwa ”** Hii inarejelea kushambuliwa na kupelekwa uhamishoni kwa Shamu ( kama vile . Amos 1:3-5) na Israeli ( kama vile 17:3) toka kwa Ashuru. Mji mkuu wa Israeli, Samaria, ulitekwa na Ashuru mwaka wa 722 K.K. baada ya kuzingirwa kwa muda mrefu. Jamii kubwa ya makabila haya kamwe hayakurudi katika nchi ya kanaani, lakini walimezwa na wingi wa watu huko walikopelekwa uhamishoni (yaani njia ya kufikisha ujumbe).

**7:17 “BWANA ataleta juu yako”** Huu ni mfano mzuri kwamba kila historia yenye matatizo makubwa katika nchi ya Israeli iliongozwu kwa makusudi ya YHWH .

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 7:18-19

<sup>18</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo Bwana atampigia kelele inzi aliye katika pande za mwisho za mito ya Misri, na nyuki aliye katika nchi ya Ashuru <sup>19</sup>Nao watakuja na kutulia katika mabonde yaliyo ukiwa, na katika pango za majabali, na juu ya michongoma yote, na juu ya malisho yote

**7:18 “tena itakuwa katika siku hiyo”**“Siku hiyo” ni siku ya BWANA kutimiza ahadi zake (kama vile mst. 18, 20,21, 23). Inaweza kurejelea wakati ujao ulio karibu sana ( kuangamizwa kwa Shamu na Israeli, kama vile mst 16) au wakati wa mwisho, mahala panapohusiana na hukumu , kifo, pepo (yaani enzi ya masihi, enzi ya mwanimifu wa

kweli aliyezaliwa na bikira).

▣ “**atampigia kelele**” Angalia muhtasari katika 5:26.

▣ “**Misri**” watu wa Mungu bado wameshikiliwa katika mapambano ya kupigania madaraka kati ya tawala zeny mafanikio na utawala wa mto Nile. Misri inarejelewa katika Hosea 7:11; 8:13; 9:3, 6; 11:5, 11; 12:1.

**7:19 “mabonde yaliyo ukiwa, na katika pango za majabali, na juu ya michongoma yote, na juu ya malisho yote”** Huu ni mfululizo wa sitiari kuelezea ukubwa wa jeshi la uvamizi litakavyomiliki hata na miji ya zamani ya nchi ya ahadi.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 7:20

**<sup>20</sup>Katika siku hiyo Bwana atanyoa kichwa na malaika ya miguuni, kwa wembe ulioajiriwa pande za ng'ambo ya Mto, yaani, kwa mfalme wa Ashuru, nao utazimaliza ndevu nazo.**

**7:20 “katika siku hiyo Bwana atanyoa kwa wembe”** Hii inaonekana inarejelea kwa Ahazi kutuma ushuru ili kuwakodi Waashuru ili kumsaidia kumwondo,2 Fal 16:7-9. Kunyolewa kichwa na ndevu ni ishara ya aibu na maombolezo (kama vile 2 Sam. 10:4-5; I Nya. 19:4; Yer. 48:37).

Tungo “nywele za miguuni” inaonekana kudokeza nywele ziotazo sehemu za siri za kijana wa kiume ( kama vile 6:2; Wam. 3:24; I Sam. 24:3), ambazo zinamaanisha aibu.

Neno la kiebrania “mguu” (BDB 919) katika maeneo mengi linaweza kumaanisha

1. Sehemu za kiume za uzazi, Kut. 4:25; Waam. 3:24; Ruth 3:4,7; I Sam. 24:3
2. Sehemu za kike za uzazi, Kumb. 28:57; Ezek. 16:25
3. Hata viumbe kama malaika , maserafi, Isa. 6:2; makerubi, Ezek. 1:23

Katika Isaya 36:12 mkojo unatajwa kama “maji yatokayo miguuni” (NIDOTTE, juzu 3, ukr. 1048).

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 7:21-22

**<sup>21</sup>Katika siku hiyo itakuwa ya kwamba mtu atalisha ng'ombe mke mchanga na kondoo wake wawili; <sup>22</sup>kisha itakuwa, kwa sababu wanyama hao watatoa maziwa mengi, atakula siagi; kwa maana kila mtu aliyesalia katika nchi hii atakula siagi na asali.**

**7:21** kuna mijadala minge ikiwa hili linarejerea kwenye mafanikio au uhaba kama inavyoonekana mst . 15

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 7:23-25

**<sup>23</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo kila mahali palipokuwa na mizabibu elfu, iliyopata fedha elfu, patakuwa mahali pa mbigili na miiba tu. <sup>24</sup>Mtu atakayekwenda huko atakwenda na mishale na upinde; kwa sababu nchi yote itakuwa ina mbigili na miiba. <sup>25</sup>Na vilima vyote vilivylimwa kwa jembe, hutafika huko kwa sababu ya kuiogopa mbigili na miiba, lakini hapo patakuwa mahali pa kupeleka ng'ombe, mahali pa kukanyagwa na kondoo.**

**7:24-25** Hii inarejelea kundi kubwa la wanyama wa mwituni ambao wataishi katika nchi ya ahadi kwa sababu ya kukosekana watu (wote wanaosimuliwa kwenye Agano la laana katika kitabu cha Kumb 28)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenywewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasir

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Wayahudi walitarajia masihi kuwa Mungu aliyedhihilishwa katika mwili?.
2. Katika Isaya 7:14 inatabiri bikira atazaa katika siku za Ahazi?
3. Kwa nini majina ya watoto yana umuhimu katika Sura hizi?

## ISAYA 8

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Dameski na Samaria	Ashuru Ataivamia Nchi	Ishara za Maher-shalal-hash -bazi	Mwana wa Isaya kama Ishara kwa Watu	Kuzaliwa kwa Mwana kwa Isaya
8:1-4	8:1-4	8:1-4	8:1-2 8:3	8:1-2 8:3-4
			Mfalme wa Ashuru Anakuja	Shilo na Mto
8:5-8	8:5-8	8:5-8	8:5-8a	8:5-10
(5b-8)				
Mabaki yenze Kuamini	(6-8)			
8:9-10	8: 9-10	8:9-10	8:9-10	
(9-10)	(9-10)	(9-10)		(9-10)
	Kumcha Mungu, Kulisikia Neno Lake	Ushuhuda na Mafundisho	BWANA Anamuonya Nabii	Maono ya Isaya
8:11-15	8:11-15	8:11-15	8: 11-15	8:11-20
(12-15)	( 12-15)		Onyo Dhidi ya Kuwatafuta Waliokufa	
8:16-18	8:16-18	8:16-22	8: 17-17	
	(16-18)			8:18
8:19-22	8:19-22		8:19	
			8:20	
			Wakati wa Maangamizi	Kutangatanga Gizani
			8:21-9-1a	8:21-13a

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama ukr. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **UTAMBUZI WA KIMUKTADHA**

- A. Sura hii inaeleza tatizo la kujaribu kueleza kwa muhtasari ushairi wa kinabii kwa kutumia beti. Hahuna uhakika wa namna beti hizi zilivoundwa. Pia hakuna uhakika wa wale wanaozungumziwa na beti hizi!
- B. Katika sura kama hizi hii inajaribu kutafuta ukweli ulio mkuu wa kila ubeti. Kisha angalia kama kuna maneno yo yote "ya msingi" au dhana iliyorudiwarudiwa. Iweni makini na ulazimishaji wa maelezo katika mifumo ya imani ama mifumo ya kithiolojia. Ushahiri wa Kiebrania unasifikasi kwa kuwa na utata. Angalia Kiambatisho cha Kwanza.
- C. Utata ni sifa bainishi ya Ushahiri wa Kiebrania na Unabii. Ufanuzi kiundani wa Maandiko ndiyo uuwao uhakisia wa Melezo ya maandiko (maneno ya kimzaha, ufanano) na mara nyingi hypoteza maana yake katika sehemu ndogo ndogo. Kiuhalisia mistari hii imejitenga. Iliwekwa katika muundo huo ili iweze kusikika! Hii ilimaanisha kuleta matokeo ya hisia za haraka! Ni kwa muda pekee, maombi, na ufunuo endelevu uifanyayo kweli kuwa sawa!.
- D. Sura za 6-8 zina VIWAKILISHI vingi vya UMOJA. YHWH anazungumza na nabii na mara nyingi anazungumza na makundi kama jamii moja.

### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 8:1-4**

<sup>1</sup>Bwana akaniambia, Ujipatie ubao mkubwa ukaandike juu yake kwa kalamu ya binadamu, Kwa Maher-shalal-hash-bazi; <sup>2</sup> nami nitajipatia mashahidi waaminifu ili kuandika habari, yaani, Uri, kuhani, na Zekaria, mwana wa Yeberekia. <sup>3</sup>Nami nikamwendea huyo nabii mke, naye akapata mimba, akazaa mtoto mwanamume. Kisha Bwana akaniambia, Mwite jina lake Maher-shalal-hash-bazi. <sup>4</sup>Kwa maana kabla mtoto huyo hajapata kujua kusema, Baba yangu, na Mama yangu, hazina za Dameski na mateka ya Samaria yatachukuliwa mbele ya mfalme wa Ashuru.

**8:1-4** Mwana wa pili walsaya (kama vile mst. 3) ni unabii uhusuo uharibifu wa mvamiaji mkuu wa Yuda (yaani, vita ya Washamu wenyewe asili ya Waefrahimu), Shamu (makao makuu ya Dameski). Dameski ilivamiawa na Ashuru mnamo 732 K.K. na wakazi wa nchi waliondolewa. Katika namna fulani mwana wa pili wa Isaya ana ufanano na mwana aliyejadiwa wa 7:14-16.

## **8:1 “Ujipatie ubao mkubwa ukaandike juu yake” YHWH anampa Isaya masharti mawili.**

1. “ujipatie,” BDB 542, KB 534, *Qal ya KAULILI SHURUTISHI*
2. “ukaandike,” BDB 507, KB 503, *Qal ya KAULI SHURUTISHI*, mara nyingi kitensi hiki kinatumika kumaanisha kifaa kilicho congwa, kama vile Kut.32:4,16

Tambua kwamba ufunuo wa mapenzi ya YHWH lazima uandikwe katika ustadi, pamoja na, na wasomaji na ya kwamba utachukua kipande “kikubwa” (BDB 152) cha nyenzo za kimaandishi ubao wa madini wa kuandikia au mhuri (kama vile 30:8). Neno la Kiebrania (BDB 163) halichagui aina gani ya nyenzo (elewa matumizi yake katika 3:23, ambapo ingeweza kurejelea ngozi yenye umbo silinda iliyokuwa imezunguka shingonikama vile tambibi ya JB, uk. 1155, na toleleo la IVP *Bible Background Commentary*, uk. 594). Jambo hili si dhahiri kutoka katika andiko ikiwa ujumbe ni mrefu au kwamba ni kifungu kilichoandikwa katika herufi kubwa!



NASB	<b>“kwa kalamu ya binadamu”</b>
NKJV, LXX	<b>“kwa kalamu ya mtu”</b>
NRSV, REB,	
JPSOA	<b>“katika aina ya kawaida”</b>
TEV	<b>“ktika herufi kubwa”</b>
NJB	<b>“mtindo wa kawaida”</b>
Peshitta	<b>“kwa namna nyepesi”</b>

Hiki ni kifungu chenye utata ulio dhahiri kwa sababu hii ndiyo ni sehemu pekee yenye neno hili “mwanadamu” (BDB60) lenye kutumika kwa kiumbe kisicho hai. YHWH hupenda ujumbe wake uchukuliwe kumbukumbu ili watu wake wote wawze kuuelewe ujumbe wake kwa urahisi.



NASB	<b>“uharaka ni hali ya umateka, harakisho ni ombi”</b>
NKJV, NRSV	<b>“Maher-shalal-hash-bazi”</b>
TEV	<b>“mali ya haraka, utekaji wa haraka”</b>
Peshitta	<b>“kuharakisha ukamataji, nukuu ya marupurupu”</b>
Tanbihi ya JB	<b>“marupurupu ya haraka-dhuruma ya haraka”</b>
Tanbihi ya toleo la REB	<b>“Harakisho la marupurupu, huarakisha dhuruma”</b>

Hili ni jina la mwana wa pili wa Isaya, “Maher-shalal-hash-bazi” (kama vile mst. 3). VITENZI viwili vile vile viko katika usemi wa kikejeli wa 5:19. Haya yanaweza kuwa mapambano ya YHWH juu yale majivuno ya Judea. Usemi huu ulikuwa na (kama yalivyo majina ya wana wote wa Isaya) maana ya kinabii kwa watu walioishi siku za unabii wake. Huu unaonekana kurejelea juu ya Ashuru kwa sababu ya kutoamini kwa Ahazi. Uvamizi huu uliimiliki Yuda pamoja na Shamu na Israeli.

Katika Hab. 1:6-8 VITENZI viwili vinavyofanana vinaeleza juu ya uvamizi wa Babeli ya Yuda.

## **8:2**

NASB	<b>“nitajipatia”</b>
NKJV	<b>“nitajitwalia”</b>
NRSV	<b>“nimejihakikishia”</b>
NJB	<b>“twaa”</b>
LXX	<b>“jifanya”</b>
Peshitta	<b>“nimejichukulia”</b>
JB	<b>“jikuta”</b>
REB	<b>“nimejihakikishia”</b>
JPSOA	<b>“ita”</b>

KITENZI kilicho ndani ya toleo la MT ni “dumisha ushahidi” (BDB 729, KB 795, *Hiphil* ya KAULI YA KITENZI CHENYE KUTIA MOYO). Magombo ya Bahari ya Chumvi, LXX, na Peshitta yanakibadili KITENZI kuwa KAULI SHURUTISHI na yanafuatiwa na matoleo ya NRSV, REB. Katika muktadha huu Mungu anawatafuta mashahidi wawili (kama vile Kumb. 4:26;30:19; 31:28) wenye kuukubali ujumbe wake (yaani, mbinguni na duniani, sangalia maelezo katika 1:2).

Shahidi wa kwanza aliyetajwa kwa jina, “Uria, kuhani,” huyu anatajwa katika II Fal. 16:10-16 (katika nuru ndogo zaidi). Shahidi mwiningine (Zekaria, mwana wa Yeberekia) hajulikani mpaka arejelee kwa Zekaria wa siku za Uzia kika II Mambo ya Nyakati 26.

Toleo la NIDOTTE, juzu. 3, uk. 336, linatoa mwelekeo wa fikra kuwa ni Isaiya mwenyewe ambaye anawahitaji mashahidi wawili kuwepo pale atakapokuwa anamtaja jina mwanae wa pili.

### 8:3

NASB           “nikamwendea”

NKJV, NRSV,

LXX           “nilikwenda”

NJB           “niliingiliana na”

REB           “niliweka”

Hiki KITENZI (BDB 897, KB 1132, *Qal* cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinadokeza mawasiliano ya kujamiiiana (kama vile Mwa. 20:4; Law. 18:6,14,19; Kumb. 22:14; Eze. 18:6).

Tena hili swalii la “nani” ni mimba iliyo ilijoitokeza katika 7:14. Kuna uwezekano mkuu wa aina mbili.

1. Mwana wa pekee anaakisi ufalme kamili wa Daudi na, hivyo, huenda ni Hezekia, mwana wa Ahazi
2. Isaya amekuwa akimhusianisha Ahazi, ikiwa ni hivyo, mwana wake pia angekuwa mfalme wa jamii ya Daudi. Makadilio ya 8:3 kwa 7:14 yanatengeneza uwezekano wa mwana wa pili wa Isaya “neno la karibu” kuwa na utimilifu.

▣“nabii mke” Hili ni rejeo lililo dhahiri kwa mke wa Isaya. Huyu alikuwa (1) nabii pia (BDB 612, UMOJA WA JINSIA YA KIKE) au (2) alikuwa ameolewa na nabii

## MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA BIBLIA

- I. Agano la Kale
  - A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
    1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
    2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
    3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
    4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
  - B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
    1. Mwanaume na mwanamke waliumbwu kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
    2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
    3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
    4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
    5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
    6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
    7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
    8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
    9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)
  - C. Wanawake katika dhima ya uongozi
    1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
    2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya

Vibanda(Kutoka 35:25-26)

3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vileWaamuzi. 4:4), alyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "Book of the Law" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipyta

- A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenyewe haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).
- B. Wanawake katika dhima ya uongozi
  1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
  2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
  3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
  4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
  5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
  6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
  7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
  8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
  9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

- A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?
  1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyeuvuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
  2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenyenye masharti na ya kihistoria yaliyovuviwa.
    - a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
    - b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
    - c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
      - 1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
      - 2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
      - 3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
      - 4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
      - 5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
      - 6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
  3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .
- B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama

viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuvia?

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunika, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenyе utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa viliviyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

#### C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi

1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
3. *Hard Sayings of the Bible* by Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667)

**8:4** Suala hili linaonekana kuwa na ufanano na sura na ujumbe wa wakati huo wa 7:15-16 (na mst. 4). Jina la mwana walsaya libatabiri juu ya tukio hili kupitia Ashuru (kama vile 10:5-7).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:5-8

<sup>5</sup>Kisha Bwana akasema nami mara ya pili, akaniambia,

<sup>6</sup>Kwa sababu watu hawa wameyakataa maji ya Shiloa yapitayo polepole,  
na kufurahi kwa ajili ya Resini na huyo mwana wa Remalia,

<sup>7</sup>basi sasa angalia; Bwana aleta juu yao maji ya huo Mto,  
yenye nguvu, mengi sana, nayo ni mfalme wa Ashuru na utukufu wake wote;  
naye atakuja, na kupita juu ya mifereji yake yote, atafurika juu ya kingo zake zote;

<sup>8</sup>naye atapita, atapita kwa kasi na kuingia Yuda;  
atafurika na kupita katikati, atafika hata shingoni;

**8:5-6** Mstari huu unaendeleza ujumbe wa hukumu ya YHWH juu ya Shamu na Israeli kupertia kwa Ashuru, lakini mstari huu unaongeza matokeo yenyne nguvu ambayo pia yatakuwa na madhara kwa Yuda (yaani, kuenea Yerusalem, kama vile mst. 8b). Huyu hataaribiwa, bali ataishi kwa nguvu.

**8:6 “watu hawa”** Je! Kifungu hiki kinamrejelea nani?

1. Israeli
2. Yuda

Jibu lake linapatikana katika mst. 6b. Yuda hakufurai katika Resini, bali Israeli (“mwana wa Remalia”) alifanya makubaliano ya kisiasa na kijeshi pamoja naye (kama vile 7:4-5,8,9). Hivyo, mst. 7 lazima urejelee juu ya uharibifu amba si juu ya Dameski pekee (kama vile 7:20), bali hata Samaria (yaani, Israeli). Inawezekana kwamba kifungu hiki kinalirejelea kundi lililo ndani ya Yuda ambaye alitaka kuungana katika umoja huo.

Motyer, katika Tyndale Old Testament Commentary Series (uk. 81), anaeleza kwamba hiki kifungu “watu hawa” kinaweza kurejeleajuu ya

1. Yuda, 28:14
2. utwala wa sasa, 23:13
3. Israeli, 9:16 (na hapa)

▣ **“maji ya Shiloa yapitayo polepole”** Hili ilikuwa korongo dogo lililokuwa mashariki mwa Yerusalem ambalo lilikusanya maji kutoka chemchemi ya Gihoni iliyokuwa katika mji huo (kama vile II Fal. 20:20; II Nya. 32:30). Hii ni ishara ya (1) YHWH kuyakataa matendo aua maneno (kama vile 5:24; 30:12) au (2) majaliwa ya YHWH juu ya Yerusalem, nyumba ya Daudi, Yuda, wakati wa vipingamizi.

▣ **“na kufurahi kwa ajili ya Resini na huyo mwana wa Remalia,”** Shamu ilikuwa sehemu ya mpango wa kukipindua kitu cha enzi cha Daudi (kama vile 7:6). Israelilikuwa ameweka tumaini lake katika umoja wa kisiasa na kijeshi.

▣ **“furahi”** Neno hili (BDB 965) linamaanisha “kuchangamka” ama “kuwa na furaha,” ambayo haiendani na muktadha. Inawezekana kwamba neno hili lilichaguliwa ili kuendana na ushahiri wa mstari huu, si kamsi. VITENZI “wameyakataa,” mst. 6 na “kufurahi,” mst 6, vinasikika sawa kwa ufanano. Unabii huu ungeweza kusomwa kwa sauti. Kuna nadharia mbalimbali zinazohusu yule anayerejelewa.

1. furaha ya Dameski
2. kundi la watu wa Yudea waliokuwa wakipinga umoja wa Kiashuru ulioanzishwa na Ahazi
3. “kutoweka” katika hali ya woga, si kufurahi (marekebisho)
4. Furaha ya Yuda huko ashuru kwa kuivamia Shamu na Israeli

Kwa namna ilio dhahiri muktadha haujulikani ni nani aneye tolewa rejea.

**8:7 “Bwana aleta juu yao”** YHWH analinda historia (kama vile 5:26; 7:7,18; 10:5; 13:2-3). Historia si uholela holela, bali ni ya kithiologia. Ina mipaka yake. Historia huenda pamoja na matokeo ya dhambi ya mwanadamu na makusudi ya Mungu!

▣ **“maji ya huo Mto”** Huu ni moja ya mito mikuu ya Mesopotamia. Mto Hedekeli na Frati iliunda mzunguko wenye rutuba amba ulianzia Ghuba ya Uajemi hadi karibia na pwani ya Shamu humo Lebanon. Jangwa ndilo lililotenganisha himaya za Mesopotamia yaani, Ashuru na Babeli) kutoka Kanaani. Hivyo, majeshi yalifuata maji ya Mto na kuelekea chini mwa pwani ya nchi za Lebanon na Kanaani. Hii safari ya kijiografia ilikuwa chanzo cha taswira ya kibiblia ya “kaskazini” kama ulivyo mwelekeo wa uovu.

**8:8** Mstari huu unaonyesha matokeo yautekaji waAshuru juu ya nchi ya Kanaani. Yuda ataishi kama taifa, lakini kwa ugumu sana. Ahazi hakumsikiliza Isaiya, hakuamini katika ahadi za YHWH.

■ “**kuyanyosha mabawa yake kutaujaza upana wa nchi yako**” Matoleo ya NASB, NRSV, NJB, REB yanakiunganisha kifungu hiki na ule uharibifu uliosababishwa na Ashuru (neno “mabawa” linatumika kama stiari ya “mwisho,” kama vile NIDOTTE, juzu. 2, uk.670, ambapo linadokeza juu ya uvamizi juu ya nchi yote), bali matoleo ya TEV na JPSOA yanachukua mabadiliko ya stiari (yaani, kutokana na mafuriko ili kuanisha uvamizi wa Ashuru) hadi kuenea kwa ndege wenye mabawa (BDB 642 KUUNDA BDB 489, kama vile 8:8; Zab. 17:8; 36:7; 57:1; 61:1,4; 63:7; 91:1,4) ili kuhusianisha na ahadi ya Mungu ya mwana wa pekee wa 7:14; pia tambua mist. 9-10! Kwa kunukuu kwamba uhadi iliusiana na agano lenye masharti ambyo yalidai imani na utii.

Pasipo kuwa na imani, ulinzi wa kiungu wa Yerusalemungelituma ujumbe wenye makosa (ni swan a watu wa sasa wanaiona hali ya Israeli kama tendo la urejesho wa ki-Ungu, lakini tatizo ni kwamba taifa hili halijajikita katika imani au kuishi maisha kama watu wa agano)! Israeli ya sasa ni ya kidunia!

■ “**Ee Imanueli**” Hapa hili jina linaonekana kama renye kurejelea juu ya ufalme waDaudi kwa wakati huo (yaani, Ahazi). Huu unaweza kuwa ushahidi wa kimaandiko kwamba motto wa 7:14 alikuwa Hezekia. Hatimaye, linamrejere Yesu, lakini katika Isaya jina hili lilirejerea mtoto mwanamume aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa ajabu, wa siku za hivi karibuni, (yaani 7:15-16)

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8: 9-10

<sup>9</sup> Fanyeni ghasia, enyi kabila za watu, Nanyi mtavunjwa vipande vipande;

Tegeni masikio, ninyi nyote wa nchi zilizo mbali;

Jikazeni viuno, nanyi mtavunjwa vipande Vipande;

Jikazeni viuno, nanyi mtavunjwa vipande vipande.

<sup>10</sup> Fanyeni shauri pamoja, nalo litabatilika;

Semeni neno, lakini halitasimama;

Kwa maana Mungu yu pamoja nasi.

**8:9-10** Toleo la NASB la 1970 ingawa mistari ya 9-15 ilikuwa mshororo mmoja, lakini Mboresho ya toleo la NASB 1995 yanaifanya mist. ya 9-10 kuwa mstari uliojiteteng (Nafikiri hii iko sawa, kama vile NKJV, NRSV, Peshitta). YHWH anazungumzia jeshi vamizi lenye hila.

1. mtavunjwa, mst. 9, BDB 949, KB 1270, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. mtavunjwa vipande vipande, mst. 9, BDB 369, KB 365, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile. 7:8; 30:31; I Sam. 2:10; Yer.48:1,2; 49:37; 50:2; 51:56
3. tegeni masikio, mst. 9, BDB 24, KB 27, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
4. 4-5. ujipatie (mara mbili), mst. 9, BDB 25, KB 28, *Hithpael* YA KAULI SHURUTISHI
6. mtavunjwa vipande vipande, sawa na #2
7. fanyeni shauri, mst. 10, BDB 734, KB 801, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
8. semeni neno, mst. 10, BDB 180, KB 210, *Piel* ya KAULI SHURUTISHI

Kwa kila tendo la wavamizi kuna upinzani wa Mungu. Maovu yao yote yanakwenda kuwa si kitu. Na sasa kumbuka kiuhalisia Mungu aliwaita ili wavamie kwa sababu ya dhambi ya watu wake, lakini baada ya hukumu Mungu atawakomboa watu wake kuititia wao wenyewe. Angalia Mada Maalum katika 1:3.

**8:10“Fanyeni shauri”** Hili neno (BDB 734) linatumika juu ya mipango ya mwanadamu. Mara nyingi hii mipango ni tofauti, pia ina mkanganyiko, kwa mipango ya YHWH (kama vile 14:24-27; Mit. 19:21). Mungu ataikamilisha mipango yake (kama vile 46:10; 55:8-11; Zab. 33:11). Mungu haitaji kuwatafuta washauri (40:13). Mipango yake ni ya uhakika na ni ya milele! Yeye anao mpango wa milele kwa wanadamu wote (angalia Mada Maalum katika 1:3).

■ “**Kwa maana Mungu yu pamoja nasi**” kifungu hiki kinamaana ya njia “Immanueli” kutoka 7:14; 8:8. Katika muktadha huu jina hili linamrejelea Ahazi (wa Ufalme wa Daudi)

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:11-15

<sup>11</sup> Maana Bwana aliniambia hivi, kwa mkono hodari,

**akanifundisha nisiende katika njia ya watu hawa, akisema,**  
<sup>12</sup>**Msiseme, Ni fitina,**

**katika habari za mambo yote ambayo watu hawa watasema,  
Ni fitina; msihofu kwa hofu yao, wala msiogope.**

<sup>13</sup>**Bwana wa majeshi ndiye mtakayemtakasa;  
na awe ye ye hofu yenu, na awe ye ye utisho wenu.**

<sup>14</sup>**Naye atakuwa ni mahali patakatifu;  
bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili,  
na mtego na tanzi kwa wenyeji wa Yerusalem.**

<sup>15</sup>**Na wengi watajikwaa juu yake,  
na kuanguka na kuvunjika,  
na kunaswa na kukamatwa.**

**8:11-15 Mshororo huu ni ujumbe mwingine uliohusiana na**

1. hukumu ya YHWH juu ya watu wake wenye dhambi
2. nabii wa YHWH anafikiri na kuyasema mawazo yake, si wale marafiki zake au jamii yake.

Mshororo huu unauakisi ujumbe wenye kumlenga Ahazi katika 7:9, na sasa unakuwa na mapana katika jamii nzima. Huu ni ujumbe wa hukumu ambayo ingekuwa imani/tumaini!

**8:11**

**NASB            “kwa mkono hodari”**

**NKJV, LXX     “kwa mkono wenye nguvu”**

Neno “Mkono” (BDB 388) linatumika mara nyingi katika maana ya lugha ya kibinadamu (angalia Mada Maalum katika 6:1) kuyazungumzia matendo ya Mungu ulimwenguni.

1. Stiari ya kipekee ya ufunuo, Isa. 8:11; Yer. 15:17; Eze. 1:3; 3:14,22; 8:1; 33:22; 37:1; 40:1
2. stiari ya ukombozi kutoka Misri, Kut. 3:20; 6:1; 13:3; 14:31
3. stiari ya kiapo na /au hukumu
  - a. kuunyoosha mkono wake, 19:16; Zek. 2:9
  - b. kuuinua mkono wake, 26:11; 49:22; Kumb. 32:40; Eze. 20:5
  - c. kuuachilia mkono wake, 14:26-27; Kut. 7:5; Yer. 6:12
4. stiari ya uumbaji, 19:25; 45:11-12; 48:13; 60:21; 64:8

▣“nisiende katika njia ya watu hawa” Mstari wa 11 unamwelezea Isaya, lakini mst. 12 ni WINGI.

▣“Nisienende” ni stiari ya maisha (yaani, Zab. 1:6). Watu wa Mungu (wa agano la ahadi ya Ibrahim) hawakuwa watu wa Mungu (katika kilitii agano la Musa). Hawa walikuwa mashahidi wa watenda mabaya kwa mataifa (kama vile Eze. 36:22-38).

Katika siku hizi mpya, siku za mwana wa pekee, njia mpya itatengenezwa (kama vile 57:14; 62:10).

Yohana Mbatizaji dhana hii alionna kama huduma yake (yaani, kutengeneza njia, kama vile Isa. 40:3; Mt. 3:3; Marko 1:3; Luka 3:4-6).

**8:12** Kifungu hiki kinairejelea7:2. Walisikia kuhusu muungano wa Waashuru wenye aslili ya Waefrahimu na wakaona hofu! Pia inawezekana kwamba kifungu hiki kinaurejelea upinzani wa Isaya juu ya sera ya Ahazi ya muungano wa Ashuru. Nabii huyu angefikiriwa kama msababishaji wa vurugu au mwenye hofu, *mtawanyishaji!*

**8:13** Nini kiliwapasa kuwatia hofu/kuwaogofya, ni BWANA mtakatifu wa majeshi. Yeye ni nahodha wa kweli wa jeshi lenye nguvu (kama vile 41:10,13,14; 43:1,5;44:2; 54:4). Yeye kwa haki yuko katika kuiongoza historia ya matukio (kama vile 7:7,18,20). Hakuna KITENZI chenye

1. Atakuwa ye ye hofu yenu (BDB432, au “na awe...”)
2. Atakuwa ye ye utisho wenu (BDB791, au “Ina awe...”)

Kifungu hiki kinavitia uchochezi vifungu hivi. Kuna usahihi (kama vile Zab. 76:12; Mal. 2:5) Na hofu isiyo sahihi (kama vile Luka 12:4; Yohana 12:43)! Kumcha YHWH ni mwanzo wa hekima (kama vile Mit. 1:7) na uaminifu; kuihofu nguvu ya mwanadamu ni upungufu wa imani katika uwepo na ahadi za YHWH!

**8:14-15** YHWH anaeleza juu ya mapambano yake yaliyosababishwa na kukataliwa na watu wa agano lake kwa stiari mbili za hukumu.

1. utakatifu (kama vile Eze. 11:16) wenyе kujengwa kwa mawe (YHWH alikuwa amejitakatifuza, kama vile Eze. 11:16)

2. kifaa kitumikacho kunasa wanyama na mtego

Watu wake, Israeli ("nyumba zote za Israeli"), zitajikwaa juu ya (BDB 505, KB 502, *Qal* ya KAULI TIMILIFU) mawe ya utakatifu. Stiari hii baadaye inaboreshwа na kuwa katika usemi wa jiwe lililokataliwa (Masihi). Angalia Mada Maalum ifuatayo.

Watu wake walio wengi, Yuda, ataanguka juu ya (BDB 656, KB 709, *Qal* ya KAULI TIMILIFU) hili jiwe au katika mtego (yaani, shimo) au watanaswa katika kifaa cha kunasia (kama vile 28:13) na kupotea (kama vile 24:18)! Hata hivyo, wengine (yaani, mabaki ya uaminifu), watatumaini katika yeye (kama vile mst. 16-18).

## MADA MAALUM: JIWE KUU LA PEMBENI

### I. Matumizi ya Agano la Kale

- A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
- B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
- C. Neno "jiwe" au "mwamba" liliuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
- D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
  1. linalowekwa la kwanza, ambalo liliuwa linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa" jiwe kuu la pembeni"
  2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
  3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

### II. Matumizi ya Agano Jipya

- A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)
- B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)
- C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo
- D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.III. Kauli za Kithiolojia
- A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wanglitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!
- B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katika muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekiel 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale waliumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-

- 27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.
- C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).
  - D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).
  - E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:16-18**

<sup>16</sup>Ufunge huo ushuhuda, ukaitie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu. <sup>17</sup>Nami nitamngojea Bwana, awafichaye uso wake nyumba ya Yakobo, nami nitamtazamia. <sup>18</sup>Angalieni, mimi na watoto hawa niliopewa na Bwana tu ishara na ajabu katika Israeli, zitokazo kwa Bwana wa majeshi, yeye akaaye katika mlima Sayuni.

**8:16-18** Mshororo huunaunganisha mwanzo wa sura (kama vile mst. 1-2). Hizini jumbe za kinabii ni kwa ajili ya uaminifu wa wanafunzi wa YHWH (katika kila zama). Kumekuwa na kundi la wanafunzi wa uaminifu /mara kwa mara (BDB 541). Kwa upekee Isaya inatumia maana hii nyingine (yaani, wanafunzi) katika neno lake (kama vile. 8:16; 50:4 [mara mbili];

54:13), mara nyingi neno hili analitafsiri kama “kufundisha,” “kutoa mafunzo,” “kujifunza.”

Mist. 19-22 inamweleza nani? Hii inaweza kuwarejelea (1) Watu wa Yuda walio waaminifu (yaani, Ufalme wa Kusini) au (2) Waisraeli walio waaminifu (yaani, Ufalme wa Kaskazini).

#### **8:16 Ilimpasa Isaya kufanya yafuatayo**

1. kuwapa masharti, BDB 864, KB 1058, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. kutia mhuri, BDB 367, KB 364, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI (yaani, kutia mhuri wa nakshi juu ya pembe za nje)

Hizi ni stiari zenyenye kudokeza utunzaji na ulinzi!

**8:17** Isaya anazungumza kwa niaba ya mabaki ya uaminifu nyakati za adhabu yak i-Ungu. Hawa “watangoja” (BDB 314, KB 313, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), ambayo pia inaweza kumaanisha “tumaini,” “kungoja kwa unyenyekevu,” au “kwa kipindi kirefu,” mara nyingi linatumika kumaanisha kutumaini/kumgoja Mungu (8:17; 25:9; 26:8; 33:2; 40:31; 51:5; 60:9; 64:4; Zef. 3:8).

Imani inaelezwa kuititia unyenyekevu na tumaini kuititia majoribu na kupita kwa kipindi kirefu.

▣ “Bwana, awafichaye uso wake” Hii ni stiari izungumziao uhusiano uliovunjika (kama vile Kumb. 31:17- 18).

▣ “nitamtazamia” Hiki KITENZI (BDB 875, KB 1082, *Piel* cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU) chenyenye kudokeza makosa ya ndani.

1. kinatumika kumaanisha YHWH katika 5:2,7
2. kinatumika kumaanisha wanafunzi wake katika 25:9; 33:2; 60:9

Kifungu hiki kinatia mkazo juu ya kipengele cha imani baina ya watu. Hizi sai Baraka za Mungu, bali uwepo wake ambaao hatimaye waamini wake huwa na shauku nao! Hivi ndivyo jiana “Immanueli” linavyo maanisha.

**8:18 Kipengele hiki kinarejeleakatika muktadha wa** Isaya katika karne ya nane, lakini hatimaye kinamrejelea zaidi Yesu (kama vile Ebr.2:13).

▣ “**yeye akaaye katika mlima Sayuni**” Katika uhalisia HWH anaishi mbinguni, lakini Sanduku la Agano lilikuwa mwimo wake (yaani, kama vile I Nya. 28:2; Zab. 99:5;132:7, mahali ambapo mbingu na nchi hukutana).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 8:19-22**

<sup>19</sup>Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenyepopo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! Haiwapi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? <sup>20</sup>Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi. <sup>21</sup>Nao watapita katikati yake, wamedhikika sana na kuwa na njaa; na itakuwa watakapoona njaa, watalalamika na kuapa kwa mfalme wao, na kwa Mungu wao, na kuelekeza nyuso zao juu; <sup>22</sup>nao wataiangalia nchi, na, tazama, shida na giza; hapana changamko kwa sababu ya dhiki; nao watafukuzwa na kuingia katika giza kubwa.

**8:19-22** Hii aya kimaandiko inatofautisha imani ya uongo inayohusishwa katika kutafuta mbinu na wachawi pamoja na maisha ya imani ya kweli katika kumtafuta YHWH. Katazo dhidi ya mbinu hizi na wachawi zinapatikana katika Kumb. 18:9-11 na Law. 20:26, 31.

**8:19“Tafuta”** Hiki KITENZI (BDB 205, KB 233) kinatumika mara mbili katika mstari huu.

1. taka, tafuta, kuiomba miungu ya uongo (ya siri), *Qal* cha KAULI ISIO TIMILIFU
2. taka, tafuta, kumuomba YHWH, *Qal* cha KAULI ISIO TIMILIFU

Katika:10 KITENZI hiki hiki kinatumika kumaanisha mataifa yanayotokana na shina la Yesu (yaani, Masihi wa uzao wa Daudi).

Mkono wa YHWH ulikuwa juu ya Isaya katika 8:11, lakini manabii wa uongo wanazungumza kutokana na fikra zao wenyewe au kutokana na nguvu za kimapepo. Nini tofauti kati ya mzungumzaji wa kweli na wazungumzaji wa uongo. Bado, wanadamu walioanguka wanawasiliza walimu wa uongo!

▣ Tambua orodha ya matendo ya kuiabudu miungu ya siri ambayo watu wa Mungu wameiiga kutoka kwa mataifa yaliyozunguka.

1. Mbinu za uaguzi, KAULI YA WAKATI ENDELEVU (BDB 981, KB 1371) ambayo maana yake ya msingi ni “kuuliza” au “kuomba.”

Hapa ni kuomba katika ulimwengu wa roho (mf. YHWH, Yoshua. 9:14 au miungu, Hosea 4:12).

NOMINO ya kwanza, “miungu iliyo sirini” (BDB 15) ni neno gumu kulitolea ufanuzi. Wengine wanalionna neno hili kama lenye kutumika katika Law. 19:31; 20:6,27 kama (1) shimo ama kaburi ambapo roho zinatawala, (2) muundo wa “baba” ambao unairejelea ibada ya kuabudu mizimu. Hii inatafsiriwa katika LXX katika Isa. 8:19 kama “sauti zenye mwangwi.”

Kwa sababu ya nomino hii na Isa. 29:4 wengine wanafikiri kwamba hii inamaanisha “kutetema” au “kunong’oneza.” Hii ingemaanisha “kutoa sauti kwa namna mbalimbali.” Hata hivyo, kutokana na I Sam. 28:7-9, hii iliusiana na uwezo wa kuita au kuzungumza na mtu kutoka ardhini au kuwasiliana na walikufa au roho za walio kuzimu, yaani, ufundi wa kuwasiliana na mizimu.

Hii NOMINO ya pili, “mtu wa rohoni” (BDB 396) ulikuwa muundo wa neno la Kiebrania wa neno “kujua” (BDB 395). Hili linamrejelea mtu mwenye maarifa ya mambo ya ulimwengu wa roho au mtu mwenye mawasiliano na wale walio katika ulimwengu wa roho wenyewaarifa (kama vile. Isa. 8:19; 19:3).

2. wachawi, Hili (BDB 396) ni neno lenye kueleza wanaume wenyepopo ukaribu hizi roho, wale wenyewewe kuwasiliana na waliokwisha kufa (kama vile 19:3; Law. 19:31; 20:6,27; Kumb. 18:11; I Sam. 28:3,9; II Fal. 21:6; 23:24
  - a. wanawong’ona, BDB 861, KB 1050, *Pilpel* ya KAULI ENDELEVU, kama vile. 29:4
  - b. wanarusia sauti zilizokwisha kutamkwa, BDB 211, KB 237, *Hiphil* ya KAULI ENDELEVU

**8:20 “kwa sheria na ushuhuda”** Tafsiori za NRSV na REB zinakiangalia kifungu hiki kama sentensi inayoanza katika mst. 19. Yawapasa watu wa Mungu kumtafuta yeye (yaani, 19:3; 31:1) na Neno lake, si watu waliokufa, kwa ajili ya kweli na uhai!

Lakini wanenaji wa uongo hawawezi kuijua kweli kwa sababu hawana nurut (“kuzimu,” kama vile. 47:12-13). Mungu amewatoa manabii wake, Ujumbe wake, kumbukumbu yake ilioandikwa (kama vile 8:1,2,16).

**8:21 “Nao”** Kiuhalisia VITENZIvyote vilivyo katika mist. 21 na 22 ni umoja, kama vile NJB. Kifungu hiki kinawarejelea watu wa agano. Hawa wanatafuta maarifa katika dini za uongo na shangaa kwa nini miungu yao haiwezi kuachilia utajiri. Utajiri ni moja ya agano la ahadi za Kumbukumbu la Torati 27-28, lakini kwa namna ya kipekee huu uhahusika na uaminifu wa agano!

Mwishowe (yaani, matokeo ya hukumu ya kilimo, kama vile mst. 22; 5:13-17) watauzungumzia uovu wa wakuu wao na miungu yao ya uongo (kama vile NRSV na REB, ambazo zinafuatisha LXX).

Inawezekana kwamba kuzungumzia uovu ni dokezo la Kut. 22:28 na Law. 24:15-16. Ikiwa ni hivyo, kisha huu ni mfano mwengine wa ukiukaji waagano. Kwangu mimi muktadha wa mist. 19-20 unakiusianisha kifungu hiki na miungu ya uongo.

**8:22** Mistari hii inaendana sura ya 9. Muktadha huu ni mzaha kati ya huzuni/giza na nuru.Utambua ufanano ulio katika 5:30. Huu ulikuwa ukinyume wa makusudi asilia ya YHWH ya uumbaji (kama vile Yer. 4:23-26,27-28)

## ISAYA 9

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuzaliwa na Kutawala mfalme Wa amani	Utawala wa mwana wa ahadi	Aya za muda kitambo	Wakati wa dhiki (8:21-9:1)	Ukombozi (8:23b-10:4)
9:1-7	9:1-7 (1-2)	9:1	9:1a	9:1-2 (1-2)
		Ufalme wa Masihi 9:1b-7	Mfalme ajae	
(2-7)		9:2-7 (2-7)	(2-7)	
	(3-5)			9:3 (3)
				9:4 (4)
				9:5-6 (5-6)
	(6-7)		BWANA ataidhibu Israeli	Amri kwa ufalme wa kaskazini (9:7-10:4)
Hasira za mungu Juu ya upumbavu Wa Israeli	Samaria inaadhibiwa	Hukumu ya efrahimu kwa ajili ya Yuda (9:8-10:4)		9:7-11 (7-11)
9:8-12 (8-12)	9:8-12 (8-12) (12b)	9:8-12 (8-12)	9:8-10	
			9:11-12	
9:13-17 (13-17)	9:13-17 (13-17)	9:13-17 (13-17)	9:13-17	9:12-16 (12-16)
				9:17-20 (17-20)
9:18-21 (18-21)	9:18-21 (18-21a)	9:18-21 (18-21)	9:18-10:4	
	(21b)			

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

## KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Sura ya 9 ni yenyeye utofauti mkubwa , lakini inahusiana na Sura ya 8:19-22 kwa kuyachezea maneno (yaani giza la utusitusi dhidi ya Mwanga).
- B. Tambua maneno haya yanayochezewa
  5. giza (BDB 365), 5:20; 8:22; 9:2; 29:18; 42:7; 45:3,7,19; 47:5; 49:9; 58:10; 59:9; 60:2
  6. utusitusi (BDB 734), 8:22; 9:1
  7. giza nene (BDB 66), 8:22; 58:10; 59:9
  8. atafanya utukufu (BDB 457, KB 455, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), 9:1
  9. “nuru kuu” (BDB 21, KIVUMISHI, 152), 9:2 (mara mbili)
  10. “giza nene” (BDB 853), 9:2; Ayubu mara nyingi; Zab. 23:4; 44:19; 107:10,14; Yer.2:6; 13:16; Amosi 5:8
  11. nuru itawangaza (BDB 618, KB 667, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), 9:2

Hizi ni sitiari zenyeye nguvu za hukumu na urejesho. Mungu ni nuru (kama vile I Yoh 1:5,7; 2:8,9,10; Ufu. 21:22-25)!

- C. Sura hii ina VITENZI TIMILIFU vingi ambavyo vinaonyesha kumalizika kwa jambo. Vinaweza kurejelea tukio lililopita au tukio lisilo la kawaida la wakati ujao. Kusudi la utata linafaa utimilizaji wa nabii mbalimbali. Haya ni matukio ya sasa na matukio ya wakati ujao; unabii wa sasa unatazamisha na unabii wa wakati ujao unatalenga (yaani , 7:14)
- D. ni kawaida katika sehemu za mwisho za fasihi ya kinabii kutilia mkazo kutoka kwenye
  1. hukumu hadi matumaini
  2. giza nene hadi nuru

Neno la Mungu lina faida na umuhimu. Kuwa makini na pale unapotazamisha juu ya mojawapo!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 9:1-9

<sup>1</sup>Lakini yeye aliyekuwa katika dhiki hatakosa changamko. Hapo kwanza aliiingiza nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali katika hali ya kudharauliwa, lakini zamani za mwisho ameifanya kuwa tukufu, karibu na njia ya bahari; ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa.

<sup>2</sup>Watu wale waliokwenda katika giza

Wameona nuru kuu;

Wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti,

Nuru imewaangaza.

<sup>3</sup>Umeliongeza taifa,  
umezidisha furaha yao;  
Wanafurahi mbele zako,  
Kama furaha ya wakati wa mavuno,  
Kama watu wafurahivyo wagawanyapo nyara.

<sup>4</sup>Kwa maana umeivunja nira ya mzigo wake, na gongo la bega lake,  
na fimbo yake yeye aliyemwonea, kama katika siku ya Midiani.

<sup>5</sup>Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo,  
na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kuteketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni.

<sup>6</sup>Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume;  
Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake;  
Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu,  
Baba wa milele, Mfalme wa amani.

<sup>7</sup>Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe,  
Katika kitu cha enzi cha Daudi na ufalme wake;  
Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki,  
Tangu sasa na hata milele.

Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo.

**9:1 “hakuna giza tena”** Katika andiko la kimasoreti lina aya ishirini na tatu katika Sura ya 8, lakini toleo la LXX lina mst. 23 Sura 9 aya 1.

Neno “giza” (BDB 734) limejitokeza katika 8:22 na 8:23 (9:1) pekee. Linaunganisha muktadha huu pamoja. Ni vigumu kutambua ni wapi unabii unaanza na kuishia. Kuwa makini sana na Sura za kisasa, aya, zilizoandikwa kwa herufi kubwa, na kifungu cha aya kwasababu unaweza ukakosa dhamira husika. Mhariri (au Isaya mwenyewe au mmojawapo wa wanafunzi wake) alikubaliana na mahubiri yake, mafunuo, mashairi yaliyowekwa pamoja. Mara nydingi yanahusiana na mchezo wa maneno, maeneo ya kihistoria, au muktadha wa theolojia ya kifo, hukumu, jehanamu na pepo.

Neno “hapana” linaweza kufahamika (1) katika maana hasi (ikiwa kama, aya hii inahitimisha muktadha uliopital) au (2) ikiwa mtu ataongeza “zaidi” (NASB), itakuwa na maana na itaanza na muktadha unaofuata.

▣“lakini yeye aliyeokuwa katika dhiki” KIWAKILISHI NOMINO cha neno “yeye” yumkini kinarejelea “nchi” (BDB 75, γρα). kwasbabu makabila mawili kusini mwa Israeli yametajwa wazi, hii ni lazima itaonyesha (1) makabila ya kusini au (2) kama watu wote wa Agano.

**9:1,3 “YEYE. . .YEYE. . .WEWE. . .WEWE”** wafasiri wa toleo la NASB wameandika kwa herufi kubwa hivi VIWAKILISSHI NOMINO kwa sababu waliona wao kama vinarejelea matendo ya Mungu.

▣“nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali” huu ni muunganiko imara kati ya 8:19-22 na 9:1na kuendelea. Inavyoonekana, haya makabila yaliyogawanywa mawili ya kusini yalisambuliwa vikali katika mwaka wa 732 K.K. chini ya Tiglath Pileser III (yaani., *Pul*, kama vile 2 Fal. 15:29). Hakuna hata mmoja aliyefikilia kwamba jambo jema laweza kutoka katika mji huu. Huu ni mwanzo wa hatua za kukamilishwa siku za Yesu katika huduma yake huko Galilaya (“lakini mwishowe waliona utukufu” kama vile Mt. 4:12-17).

Kwa sababu ya jangwa kati ya Mesopotamia na kanaani, jeshi lilifuata chanzo cha mto Hedekeli na kutelemkia uwanda wa pwani. Hii ni kwamba walishambulia kutoka kaskazini. Zabuloni na Naftali (sambamba na mji wa Dani) itakuwa ya kwanza kuteswa.

▣ “**Galilaya ya mataifa**” hii maana iliyio wazi ni “mataifa yaliyozunguka” (BDB 165 II MUUNDO WA MANENO BDB 156). Ashuru waliwapa makazi mapya wengi wa watu waliowashinda katika eneo hili. Neno kwa ajili ya mataifa ni neno la kawaida kwa ajili ya mataifa , *goy* (BDB 156,kama vile . 9:3). Wakati mwingine hutumika kwa ajili ya Israeli yenyewe (kama vile Mwa. 12:2; 18:18; Kumb. 19:6; Isa. 1:4).

Wakati wa Yesu inarejelea (1)wayahudi wa Galilaya au (2) mataifa , ambayo yalionyesha asili ya ulimwengu unaokuja wa huduma ya masihi, ambao unatiliwa mkazo na Isaya kuhusiana na mataifa.

**9:2 “wameona nuru kuu”** Neno nuru ni sitiari ya uwepo kwa ajili ya YHWH’ ( kama vile. Kumb. 33:2; Hab. 3:3; Ufu. 21:22-24). Hapa, nuru (BDB 21) ni sitiari ya injili (kama vile. Isa. 42:6; 49:6; 51:4; 60:1,3). Hakuna aliyetarajia Masihi kuwashudumia Wagalilaya wasiokubalika. Hii aya ni unabii unaoshangaza wa mahali pekee pa huduma ya Yesu! Hakuna aliyetarajia “Galilaya ya mataifa ” itakuwa sehemu ya kwanza kutoa “habari njema”!

**9:3 “umeliongeza taifa”** hiki ( KITENZI, BDB 915, KB 1176, *Hiphil KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU*) huenda inarejelea ahadi kamili za YHWH’ kwa mababa wa imani ili kuongeza uzao wa Ibrahimu.

1. Nyota za mbinguni (kama vile Mwa. 15:5; 26:4; Kumb. 10:22; 28:62)
2. Mchanga wa bahari (kama vile Mwa. 22:17; 32:12)
3. Mavumbi ya nchi (kama vile Mwa. 13:16; 28:14; Hes. 23:10)

▣ “**umezidisha furaha yao**” andiko la kimasoreti la kiebrania (Kethiv) lina neno “siyo” (BDB 518), lakini toleo la NASB linatafasiri hilo neno kama “wao.” Wahariri wa toleo la kimasoreti wanashauri kwenye pambizo (Qere) libadilishwe kuwa “yeye” (pia wamefanya hivyo mara kumi na nne katika sehemu zingine ).Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania pia lina neno “yeye.”

NOMINO “furaha” (BDB 970) limejitokeza mara mbili kwenye aya hii (labda pia kwenye mst. 17), kama kinavyosimuliwa KITENZI “furahi” (BDB 162, KB 189, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* ). Muundo wa KITENZI cha “furaha” (BDB 970, KB 1333, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) umejitokeza kwenye aya. Ni wazi Isaya alikuwa anakazia huu muktadha!

Walikuwa na furaha kwa sababu ya uwepo wa YHWH. Agano la Mungu ni pamoja na watu wake (yaani , Immanueli). Furaha yao inafafanuliwa katika sitiari mbili halisi

1. Mavuno
2. Kugawana mateka/mali

**9:4-5 kwasababuya uwepo wa YHWH** (mst. 3), atapigana kwa niaba yao (yaani vita vya BWANA).

1. Umeivunja nira ya mzigo wake (yaani kuwatoa katika utawala wa kigeni, kama vile. Yer. 28:2; Ezek. 34:27)
2. Kuvunja gongo juu ya mabega yao
3. Kuvunja fimbo ya waonezi wao ( gongo na fimbo ni alama ya wafalme wa kigeni na utawala wao,kama vile . 10:27)

KITENZI hikihiki, “kuvunja”, kimetumika mara tatu, BDB 369, KB 365, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile. 7:8; 8:9 (mara tatu).

Kama vile uwakilishi wa nguvu za Mungu (yaani., Gideoni) aliwashinda Wamidiani,sasa ni chombo kilichoteuliwa na Mungu,Babeli,atamharibu Ashuru na kuitawala Kanaani. Mungu ni mtawala wa historia ya ulimwengu na makusudi hasa ya Kanaani kwa sababu ya uzao wa Ibrahimu (yaani.,masihi ajae).

▣ “**kama katika siku ya Midiani**” angalia 10:26 na Amu. 6-8.

**9:5** maadui wa watu wa Agano watashindwa na mavazi yao (yaani., viatu na majoho) yatatumika kama mafuta kwenye moto. Hii ni sitiari ya ushindi kamili. Maandiko mengi yanazungumza juu ya kushindwa kwa silaha za jeshi la kigeni kwa sababu imani ya watu wake na ulinzi utakuwa katika Yeye na ahadi ya agano lake, sio katika nyara za kijeshi walizoteka (kama vile Zab. 46:9; 76:3; Hos. 2:18).

Mpiganaji wa Kimungu aliyemshindi anapigana tena kwa ajili ya watu wake. Aya ya 4 ni mfano kamili!

**9:6-7** toleo la NKJV linatia alama kwenye aya hizi mbili kama vifungu tofauti.

Aya ya 6 inaelezea mwana maalumu, Immanueli.

1. Uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; mwana wa pekee, tumaini la haki la uzao wa Daudi (kama vile. 2 Sam. 7) rudi katika mtazamo
2. Jina lake ( tabia za Mungu wake)
  - a. mshauri wa ajabu, hii inonyesha mpango wa kiroho, kama vile . 14:26,27; 19:17
  - b. Mungu menye nguvu, kama vile . 10:21
  - c. Baba wa milele
  - d. Mfalme wa amani, Mik. 5:5

Jina la kwanza laweza kuwa na vyeo viwili tofauti, lakini majina mengine matatu yana maneno yaliyohusiana. Majina matano huenda yanaakisi desturi ya Misri, ambapo Farao mpya alipewa taji mpya yenyenye majina matano wakati wa kutawazwa kwake.

Kuna majina manne yamechanganywa. Yumkini huenda haya ni majina ya mwana mpya anapotawazwa kuwa mfalme. Neno Immanueli kwenye 7:14 na 8:8-10, kama vile neno “Mungu mwenye nguvu” kwenye 9:6, halikusudii kuoodoa Uungu, lakini linaakisi mfalme bora. Majina yanaakisi tabia ya Mungu ambayo ni matarajio yanayoelezea sifa ya mfalme wa uzao wa Daudi. Ni lazima ikumbukwe kwamba haya majina yanahusika na (1) sehemu ya utawala , (2) nguvu za kijeshi, (3) mchungaji, na (4) utawala bora. Uungu wa masihi pia undokezwa, ingawa si kwa namna ya pekee, kwenye Dan. 7:14; Yer. 32:18.na itakumbukwa kwamba wayahudi hawakumtarajia masihi atakuja katika mwili wa YHWH kwa sababu mkazo pekee kwa Waisraeli ni kwamba kuna Mungu mmoja tu! Uungu wa Yesu na tabia ya kiroho yalikuwa ni matatizo halisi kwa walioamini kuna Mungu mmoja tu (yaani ., Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 4:35,39; Isa. 40:18,25; 46:5). “ufunuo ujao” pekee unatufundisha ukweli huu (kama vile Yoh 1:1-14; Phil. 2:6; Ebr. 1:2-3). Kama Agano jipya ni kweli basi waaminio wa Agano la Kale kuhusu imani ya Mungu mmoja lazima wanatofautiana kidogo (yaani ., nafsi moja ya kiroho yenyenye umilele imejifunua binafsi mara tatu). Ukosoaji wa lugha ya Agano la kale uko wazi lakini utimilifu dhahiri wa unabii wa Agano la kale juu ya jiografia na taifa la Israeli umefanywa kiulimwengu ukihuisha “mataifa.” Tazama Mada Maalumu katika 1:3.Kut 3:15 imetambulika na kufafanuliwa kwenye Yoh 3:16; 4:42; 1 Tim. 2:4; Tit 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yoh 2:1; 4:14).

Aya ya 7 inaelezea utawala wake.

1. Milele na utawala wa ulimwengu (kama vile. Mika. 5:4)
2. Milele na amani ya ulimwengu (kama vile . Mika. 5:5a)
3. Kutawala katika kitu cha enzi cha mfalme Daudi (kama vile. 16:5; 2 Samuel 7)
4. Kutimiza sheria na haki milele ( NOMINO hizi mbili mara nyingi zimetumika pamoja , kama vile . 32:16; 33:5; 59:14)
5. Shauku ya YHWH ni kukuhakikishia ukweli wake

Aya ya 7 bila shaka inafanana na utawala wa milele (kama vile Dan. 2:44; 4:3,34; 6:26; 7:13-14,27; Ezek. 37:25; Mika. 4:7; 5:4; 2 Pet. 1:11), utawala wa millennia usiokuwa na mwisho (tazama muhtasari wangu katika ufunuo wa fasiri “utangulizi muhimu” na utangulizi katika Sura ya 20 kwenye [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) ). Ahadi hii ya milele ni dhana ya enzi mpya ya Roho! Kumalizika kwa matatizo na kuangamia daima . Kurudisha nafasi bora zaidi ya Mungu (yaani.,ushirika katika bustani ya Edeni).

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 9:8-12

<sup>8</sup>Bwana alimpelekea Yakobo neno,  
likamfikilia Israeli.

<sup>9</sup>Nao watu wote watajua,  
yaani, Efraimu na ye ye akaaye Samaria,  
wasemao kwa kiburi na kwa kujisifu nafsi zao,

<sup>10</sup>Matofali yameanguka, lakini sisi tutajenga kwa mawe yaliyochongwa;  
mikuyu imekatwa lakini sisi tutaweka mierezi badala yake.

<sup>11</sup>Kwa sababu hiyo Bwana atawainua adui wa Resini juu yake,  
naye atawachochea adui zake;

<sup>12</sup>Waashuri upande wa mbele, na Wafilisti upande wa nyuma,  
nao watamla Israeli kwa kinywa kilicho wazi.  
Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali,  
lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa.

**9:8-12** Mungu alituma ujumbe wa wazi kwa makabila ya kaskazini. Waliusikia na wakauelewa (kama vile mst 9a), bado hawakuukubali .

1. Walijionyesha wana kiburi (BDB 144) na kujisifu (BDB 152)
  - a. watajenga baada ya hukumu Mungu, hata bora zaidi, mst. 10
  - b. watapanda tena baada ya hukumu ya Mungu, hata bora zaidi, mst. 10
2. YHWH atainua (BDB 960, KB 1305, *Piel KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) na kuwatikisa (BDB 1127, *Pilpel KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, hapa pekee na labda katika 19:2)
  - a. Shamu
  - b. Palestina
3. bado YHWH anaendelea kutikisa (kama vile. mst. 12,17,21)
  - a. hasira yake haikugeukia mbali
  - b. mkono wake umenyoshwa hata sasa

**9:8-9 “Israeli. . .Efraimu. . .Samaria”** haya majina yalionyesha makabila kumi ya kaskazini baada ya kutawanyika katika mwaka wa 922 K.K.

**ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) 9:13-17**

<sup>13</sup>Lakini watu hao hawakumwelekeea ye ye aliywapiga,  
wala kumtafuta Bwana wa majeshi.  
<sup>14</sup>Kwa sababu hiyo Bwana atakata katika Israeli kichwa na mkia,  
kuti na nyasi, katika siku moja.  
<sup>15</sup>Mzee mwenye kuheshimiwa ndiye kichwa,  
na nabii afundishaye uongo ndiye mkia.  
<sup>16</sup>Kwa maana wawaongozao watu hawa ndio wawakoseshao,  
na hao walioongozwa na watu hao wameangamia.  
<sup>17</sup>Kwa sababu hiyo Bwana hatawafurahia vijana wao,  
wala hatawahurumia yatima zao wala wajane wao;  
maana kila mtu ni mnajisi, dhalimu,  
na kila ulimi hunena upumbavu.  
Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali,  
lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa.

**9:13-17** sababu ya hasira ya YHWH kuendelea kuwepo ni kutojali kwa wana Israeli.

1. Hawakumwelekeea (yaani., kutubu, kifasihi “kugeuka,” BDB 996, KB 1427, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*)
2. hawakumtafuta (BDB 205, KB 233, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) BWANA wa majeshi hata hivyo, wamemalizwa kabisa (kichwa [“wazee”] na mkia [manabii] watakawta) kuangamizwa! Waliwaongoza watu upotevuni (BDB 1073, KB 1766, *Hiphil KAULI ENDELEVU*) hivyo wamechanganyikiwa (hasa “wameangamia,” BDB 118, KB 134, *Pual KAULI ENDELEVU*). Kiongozi wa aina hii anarejelewa Yesu katika kitabu cha Mt. 15:14; 23:16,24. Nuru yako inapokuwa giza , ni kwa jinsi gani giza linakuwa kuu! Hawezi kuwahuhurumia (NRSV,MT, “hatawafurahia”)
  1. vijana (mst. 17)
  2. yatima (mst. 17)
  3. wajane (mst. 17)

Kwa kawaida hawa walilindwa na YHWH (yaani Kumb. 10:18), lakini hapa wanahukumiwa na wale wote waasi watu wa Mungu!

kwa sababu wote

1. hawana Mungu (BDB 338)
2. Watenda maovu (BDB 949, KB 1269, *Hiphil KAULI ENDELEVU*)
3. Hunena upumbavu (BDB 615)

Aya ya 8-12 ni tungo inayojirudia mara kwa mara ikiwa imeunganishwa pamoja (“mkono wake umenyoshwa hata sasa”) katika mstari wa 12c,d; 17e,f; na 21c,d. tambua pia huenda muktadha unaenda haraka kupitia 10:4, ambapo tungo inajirudia tena. Kuwa makini sana unapotegemea Sura na mgawanyo wa aya. Sio zenye uhalisia, na hazina uvuvio!

**9:16**

**NASB** “*ilileta kuchanganyikiwa*”

**NKJV** “*wakaangamizwa*”

**NRSV** “*wakaachwa wamechanganyikiwa*”

**TEV** “*walichanganyikiwa kabisa*”

**NJB** “*wakaangamizwa*”

**LXX** “*wakashikwa na wasiwasi*”

**Peshitta** “*wakadidimia chini*”

**REB** “*wakamezwa*”

Asili ya kiebrania (BDB 118, KB 134) kimsingi inamaanisha “kushushwa chini,” “kupotezwa” (kama vile .

25:7,8; 28:4; 49:19), lakini inawezekana kuna asili nyingine

1. kutangaza (KB 135 II, kama vile Mith. 19:28)

2. Kuwachanganya (KB 135 III, kama vile 3:12; 19:3; 28:7) kwa mvinyo mwangi (NASB)

“kuchanganyikiwa” linafaa zaidi kwenye nadharia ya ufanano! Kumbuka , muktadha, muktadha unaamua maana , sio msamiati!

**9:17** “**wala hatawahurumia yatima zao wala wajane wao**” haya ni maamuzi ya mwisho ya Mungu kugeukia mbali. Ni kuachana kabisa na ahadi za Mungu katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 9:18-21**

<sup>18</sup>**Kwa maana uovu huteketeza kama moto;**

*huila mibigili na miiba,  
naam, huwaka katika vichaka vy a mwitu,  
nao hupaa juu katika mawingu mazito ya moshi.*

<sup>19</sup>**Kwa sababu ya hasira ya Bwana wa majeshi nchi hii inateketetea kabisa;**

*watu hawa nao ni kama kuni zitiwazo motoni;  
hapana mtu amhurumiaye ndugu yake.*

<sup>20</sup>**Hupokonya upande wa mkono wa kuume, nao huona njaa!**

*Hula upande wa mkono wa kushoto, wala hawashibi!  
Watakula kila mtu nyama ya mkono wake mwenyewe.*

<sup>21</sup>**Manase anamla Efraimu, naye Efraimu anamla Manase;**

*nao wawili pamoja watakuwa juu ya Yuda.  
Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali,  
lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa*

**9:18-21** Aya hizi zinazeleza hukumu ya Mungu kwa makabila ya kaskazini. Hukumu inajulikana kama moto unaoteketeza nchi. Angalia Mada Maalumu: Moto katika 1:31.hata watu ni mafuta kwa ajili ya moto!

    uovu wa watu unaelezewa kama

1. Wa mtu kutohurumiana nduguye

2. Kuiba lakini njaa kubaki pale pale
  3. Hula lakini hawashibi (hata miili yao wenyewe, kama vile. Yer. 19:9; toleo la Targums linaitafasiri kama “ndugu” na hivyo toleo la JPSOA hutafasiri “ndugu yake”)
- Watu wa Agano la Mungu wanapingana wenyewe kwa wenyewe!

**9:18 “Kwa maana uovu huteketeza kama moto”** inatia shauku kwamba moto unaweza kuwa na msaada au madhara.

1. Hapa, madhara (uovu)
2. 62:1, msaada (wokovu)

Muktadha , muktadha, muktadha unamua maana. Kuwa makini na ufanuzi wa leo wa maneno ya kibiblia!

## ISAYA 10

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ashuru ni chombo Cha Mungu 10:1-4 (1-4)	Adhabu ya Samaria (9:8-10:4) 10:1-4 (1-4)	Hukumu ya Efraimu ni fundisho kwa Yuda (9:8-10:4) 10:1-4 (1-4)	Bwana ataiadhibu Israeli (9:8-10:4) 10:1-4	Mateso ya ufalme wa Kaskazini 9:7-10:4 10:1-4
	Kiburi cha Ashuru Pia kinahukumiwa	Ole, Ashuru	Mfalme mkuu kama chombo cha Mungu	Kinyume na mfalme wa Ashuru
10:5-11 (5-11)	10:5-11 (5-11)	10:5-11 (5-11)	10:5-6	10:5-11 (5-11)
10:12-14 (13-14)	10:12-14 (13-14)	10:12-14 (13-14)	10:12 10:13-14	10:12-14 (13-14)
10:15-19 (15-19)	10:15-19 (15-19)	10:15-19 (15-19)	10:15	10:15-19 (15-19)
Mabaki watarudi	Kurudi kwa mabaki Ya Israeli	Mabaki tu ndio watakorudi	Wachache ndio watakorudi	Mabaki kidogo
10:20-23	10:20-23 (20-23)	10:20-23	10:20-23	10:20-23 (20-23)
		Ahadi ya unabii	Bwana atamwadhibu Ashuru	Imani katika Mungu
10:24-27	10:24-27 (27)	10:24-27a Mtazamo wa Watu Wa Ashuru 10:27b-32 (27b-32)	10:24-27	20:24-27 (24b-27)
			Wavamizi wavamia	Uvamizi
10:28-32 (28-32)	10:28-32 (28-32)	Bwana, bwana misitu atamkatilia mbali Ashuru	10:28-32	10:28-34 (28-34)
10:33-34 (33-34)	10:33-34 (33-34)	10:33-34 (33-34)	10:33-34	

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa XVI katika kipengele cha utangulizi)**

**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkaao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:1-4

<sup>1</sup> Ole wao wawekao amri zisizo za haki,  
na waandishi waandikao maneno ya ushupavu;  
<sup>2</sup> ili kumpotosha mhitaji asipate haki yake,  
na kuwanyang'anya maskini wa watu wangu haki yao;  
ili wajane wawe mateka yao,  
na kuwafanya yatima waliofiwa na baba zao kuwa mawindo yao!  
<sup>3</sup> Nanyi mtafanya nini siku ya kujiliwa,  
na wakati wa uangamivu, utakaokuja kutoka mbali sana?  
Je! Mtamkimbilia nani mpate msaada?  
Na utukufu wenu mtauacha wapi?  
<sup>4</sup> Watainama chini ya wafungwa tu,  
wataanguka chini yao waliouawa.  
Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali,  
lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa.

**10:1 "Ole"** Hiki KIHISISHI (BDB 222) kinatumika mara nyingi katika kitabu cha Isaya (na Yeremia). kinatafasiliwa (NASB 1995 lililoboreshwa)

1. "pia," 1:4; 17:12
2. "kwa hiyo," 1:24
3. "ole," 5:8,11,18,20,21,22; 10:1,5; 18:1; 28:1; 29:1,5; 30:1; 31:1; 33:1; 45:9,10; 55:1 (yaani., ole waaguzi)
4. "haya," 55:1; pia yumkini 10:5

Inaonyesha kuwepo na uchungu na maumivu au kuitwa shaulini (yaani., #4 hapo juu). Kuna KIHISISHI kingine (BDB 17), ambacho mara nyingi hutafasiriwa kama "ole," yenye kuelezea huzuni na kukata tamaa (kama vile 3:9,11; 6:5; 24:16 na mara 8 katika Yeremia).

◻ Ufanano wa mst. 1a na b unaunganisha viongozi wa kiraia (yaani., wale wote wanaoruhusu sheria za kiovu) na kuamua (ambao mara zote huweka kumbukumbu za maamuzi yasio haki, kama vile 5:23). Uongozi wa Israeli kwa makusudi wamevunja msisitizo wa agano la Musa juu ya uangalizi kwa ajili ya maskini, jamii kwa kutowapenda, watu wasio na uwezo kwenye jamii (kama vile mst. 2; 1:17,23; 3:14,15; 11:4; Kumb. 16:19; 24:17; 27:19; Mith. 17:23; 18:5; Amosi 4:1; 5:12).

**10:2** Mambo yamekwenda visivyo kuwa Yule ambaye YHWH anamtafuta kumlinda (yaani., wajane na yatima) wamekuja kuwa wenye kuharibu na kunyang'anya!

**10:3** Mlolongo wa maswali unaleta hatma ya hawa wanyonyaji! Siku moja ikiwa ni kwa muda au kwenye matukio ya siku za mwisho, muumba ataita viumbe wake, aliyewaumba kwa sura na mfano wake, kutoa hesabu ya utumishi wa karama ya maisha (mst. 4). YHWH NI Mungu mwadilifu, mwenye rehema na anazihitaji kuziona hizi

tabia kwa watu wake ili kwamba "mataifa" yapatae kumjua na kuja kwake!! Israeli ilikuwa ikitoa ujumbe usio wa kweli!

**10:4 "lakini mkono wake umenyooshwa hata sasa"** Hiki ni kifungu kinachojirudia katika sehemu hii ya fasihi (kama vile 9:12,17,21). Ni namna ya lugha ya mwanadamu (angalia Mada Maalum katika 6:1) kuielezea hukumu ya Mungu isiotegemewa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:5-11**

<sup>5</sup> Ole wake Ashuru! Fimbo ya hasira yangu,

ambaye gongo lililo mkononi mwake ni ghadhabu yangu!

<sup>6</sup> Nitamtuma juu ya taifa lenye kukufuru,

nitampa maagizo juu ya watu wa ghadhabu yangu,

ateke nyara, na kuchukua mateka,

na kuwakanyaga kama matope ya njiani.

<sup>7</sup> Lakini hivyo sivyo akusudiavyo mwenyewe,

wala sivyo moyo wake uwazavyo;

maana katika moyo wake akusudia kuharibu,

na kukatilia mbali mataifa, wala si mataifa machache.

<sup>8</sup> Maana asema, Je!

Wakuu wangu si wote wafalme?

<sup>9</sup> Je! Kalno si kama Karkemishi?

Hamathi si kama Arpad?

Samaria si kama Dameski?

<sup>10</sup> Kama vile mkono wangu ulivyofikilia falme za sanamu,

ambazo sanamu zao za kuchongwa zilikuwa bora kuliko sanamu za Yerusalem na za Samaria;

<sup>11</sup> je! Sitaautenda Yerusalem na sanamu zake vile vile kama nilivoutenda Samaria na sanamu zake?

**10:5-19** Hii ni sehemu ya fasihi juu ya kazi ya Mungu katika taifa la Ashuru. Ulikuwa ni utawala dhalimu wa Mashariki Karibu ya mbali. Ulikuwa ni ukatili juu ya kundi la watu waliotekwa. YHWH atatumia mataifa ya watu wapagani ili kulitimiza kusudi lake (kama vile mistari ya. 5b; 6b; kama Hab. 1:12-17 akamwomba Mungu kuhusu kuwatumia mateka wa Babeli). Mungu hutumia waovu ili kuyatenda mapenzi yake! Hawafanyi wao (yaani., Shetani, mapepo, malaika walioasi, himaya zilizo ovu), bali huwaongoza kwa ajili ya mema mengi (kama vile Ayubu 12:23; Zab.47:7-8; 66:7; Dan. 2:21; Mdo. 17:26, yaani., mpango wake wa ukombozi wa wote, angalia Mada Maalum katika 1:3). Hata hivyo, waovu huvuna madhara ya kile walichopanda katika matendo yao. Siku moja wao, hata sisi, tutahukumiwa (kama vile Kumb. 32:34-43; Isa. 14:24-27; 30:27-33; 31:5-9). Kile ambacho Ashuru alifanya kwa wenza, Babeli (kama vile 13:5) pia atawafanya wao!

**10:5 "Ole kwa Ashuru, Fimbo ya hasira Yangu"** Chombo cha Mungu kwa ajili ya kuuadhibu uasi wa watu wake kilikuwa ni taifa dhalimu la Ashuru (kama vile 7:17; 8:7). Hata hivyo, walipaswa kuwajibika kwa ajili ya matendo yao (kama vile 10:24-27). Majivuno ya Ashuru yanaonekana katika mistari ya 8-11,12.

**10:6 "taifa lenye kukufuru. . .watu wa ghadhabu yangu"** Hili linarejerea kwenye taifa la Israeli (kama vile 9:17,19)! Hiki kifungu mfanano kimetumika kwa Israeli katika 19:17; 32:6. Ni kejeli kiasi gani, watu wa agano kuitwa "kufuru" na kuwafanya kiuadilifu kuwa sawa na Ashuru "iliyokufuru"!

▣“ateke nyara, na kuchukua mateka” Kama ilivyo mst. 21, “mabaki yatarudi,” unaaksi kwenye jina la mwana wa kwanza wa Isaya (kama vile 7:3), hili linaaksi maana ya jina la mtoto wa pili (kama vile 8:1,3).

**10:7 "Lakini hivyo sivyo akusudiavyo mwenyewe,wala sivyo moyo wake uwazavyo"** Ashuru haikujua kuwa YHWH alikuwa akielekeza matendo kwa ajili ya kusudi lake. Ashuru zaidi zaidi ilikuwa tu kwa ajili ya kuharibu.

Kusudi la YHWH kwa ajili ya mfalme wa Ashuru linadhihirishwa katika orodha ya Qa/ KITENZIJINA CHA MIUNDO YA MANENO (mst. 6) dhidi ya Israeli.

1. Kuteka nyara (BDB 1021, KB 1531)
2. Kuchukua mateka (BDB 102, KB 117)
3. Kuwakanyaga kama matope (KIMANENO BDB 962, KB 1321, NOMINO BDB 942)

Kusudi la mfalme wa Ashuru linaelezewa katika maneno mawili ya *Hiphil* KITENZIJINA CHA MIUNDO YA MANENO katika mst. 7c,d.

1. kuharibu (BDB 1029, KB 1552)
2. kukatilia mbali (BDB 503, KB 500)

**10:8-11** Fikra za mfalme wa Ashuru (yaani., “majivuno,” TEV) yanadhihirishwa katika mstari huu

1. makamanda wake wote wa kijeshi ni wafalme (NRSV, TEV, NJB, REB, Peshitta), mst. 8
2. jeshi lake (Tiglath-Pileser III au yumkini Senakeribu in 701 k.k.) limeyashinda mataifa mengine mbalimbali na miji ya ng’ambo ya Eufrati, pamoja na miungu yao, mst. 9
  - a. Calno (au Calneh), mji ulioko Kaskazini mwa Shamu (kama vile Amosi 6:2) ulioanguka mwaka 742 K.K. (tarehe hizi zote ni za kukadilia tu)
  - b. Karkemish, Mji mkuu wa Wahiti karibu na chanzo cha Mto Hedekeli, ikiungana na muungano wa Waashuru mwaka wa 738 K.K
  - c. Arpad, mji ulioko Kaskazini mwa Shamu ulioshindwa mwaka wa 741 K.K
  - d. Samaria (mji mkuu wa Israeli) ulioshindwa mwaka wa 722 K.K kwa Sargon II
  - e. Dameski (mji mkuu wa Shamu) ulioshindwa mwaka wa 732 K.K
3. Alihatarisha kuuangamiza Yerusalemu na “ibada zao za sanamu” kama ilivyokuwa Samaria, mst. 11. Hakuwa na maarifa ya kutofautisha kati ya “ibada ya sanamu” (kama vile 2:8) na ibada ya kweli ya YHWH. Neno kuhusu uvamizi wa Waashuru ndiyo lililoelezewa. Majina ya mahali yanafuatisha uvamizi wa kidesturi wa barabara zielekeazo kwenye himaya za Mashariki Karibu ya Kale itokayo Mesopotamia. Kwa Sababu ya jangwa, iliwapasa kufuata Mto Hedekeli kuelekea kwenye chanzo chake na baadaye kuelekea Kusini wakiambaa kwenye uwanda wa Pwani. Tatizo la kutambua ni yupi aliwavamia Waashuru ni ngumu kwa sababu Senakeribu, ambaye aliikabiri na kuizingira Yerusalemu, kiuhalisia alitokea sehemu za kusini mwa mji katika mwaka wa 701 K.K. kuanguka kwa mji iliyotajwa kulitokea chini ya Tiglath-Pileser III (yaani., Puli). Kwa hiyo, nafikiria njia ilikuwa “ikifikiliwa” kama mvamizi wa Kaskazini.

**10:11 “sanamu”** Hili ni neno la kufurahisha (BDB 47). Maana yake ya msingi haijulikani, lakini maana yake inafanana na jina Elohim, ambalo linasababisha wanazuoni kudhani kuwa linarejerea sanamu zisizoishi (kama vile NIDOTTE, juzu. 1, uk. 411). Imani ya Mungu mmoja ni ya kipekee katika imani ya Waisraeli. Kuna uwepo wa viumbe vingine vya kiroho, lakini kuna Mungu mmoja tu aliye wa kweli (kama vile Kumb. 4:35,39; 6:8; 32:39; Isa. 43:9-11; 45:21-22; Yer. 2:11; 5:7,10; Rum. 3:30; I Kor. 8:4,6; I Tim. 2:5; Yakobo 2:19). Sanamu haziwasilishi kitu chochote, bali ni hofu na kuwa na tumaini la uongo (ushirikina) kwa mwanadamu aliyeanguka akitambua kuwa kuna ukweli zaidi ya ule anaouona, lakini akashindwa kukabiliana na ukweli wa kiroho (yaani., ufunuo)

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:12-14

<sup>12</sup> Basi, itakuwa, Bwana atakapokuwa ameitimiza kazi yake yote juu ya mlima Sayuni na juu ya Yerusalemu, nitayaadhibu matunda ya kiburi cha moyo wake mfalme wa Ashuru, na majivuno ya macho yake. <sup>13</sup> Kwa maana amesema, Kwa nguvu za mkono wangu nimetenda jambo hili, na kwa hekima yangu; maana mimi nina busara; nami nimeiondoa mipaka ya watu, nikaziteka akiba zao, nikawaangusha waketio juu ya viti vya enzi kama afanyavyo shujaa. <sup>14</sup> Na mkono wangu umezitoa mali za mataifa kama katika kioto cha ndege; na kama vile watu wakusanyavyo mayai yaliyoachwa, ndivyo nilivyokusanya dunia yote; wala hapana aliyetikisa bawa, wala kufumbua kinywa, wala kulia.

**10:12-14** YHWH anatetea udhibiti wake juu ya Ashuru na ushindi wake, atamwadhibu mfalme wa Ashuru (mst. 12) kwa ajili ya

1. Kiburi cha moyo wake

2. Majivuno ya macho yake

Kiburi cha mfalme wa Ashuru kimeonyeshwa katika orodha ya sifa zake binafsi (kur. 12-14), ambazo zinasikika vizuri kama nyaraka za Waashuru za zama hizo (angalia *The IVP Bible Background Commentary OT*, uk. 599)

1. Kwa nguvu ya mkono wangu

2. Kwa hekima yangu

Alipora taifa toka sehemu za Magharibi mwa kingo za Mto Eufrati kama mtu aporavyo kiota cha ndege!

**10:13**

**NASB** “**kama afanyavyo shujaa”**

**NKJV** “**kama afanyavyo mtu jasiri”**

**NRSV, TEV,**

**REB** “**kama jasiri”**

**NJB** “**kama shujaa”**

Maana ya msingi ya KIVUMISHI (BDB 7) , “mwenye nguvu,” chawea kurejerea kwa

1. Mtu jasiri/shujaa, Ayubu 24:22; 34:20; Yer. 46:15; Wimbo. 1:15
2. Moyo shupavu, Isa. 46:12
3. malaika, Zab. 78:25
4. wanyama
  - a. majasiri, Isa. 10:13 laweza kurejerea kwa sababu mafahari ya ng’ombe yaliyokuwa na mbawa yaliyokuwa alama ya Ashuru (yaani., juu ya pande za malango ya Ishtar, kama vile Zab. 22:13; 68:30; Isa. 34:7)
  - b. farasi, Amu. 5:22; Yer. 8:16; 47:3; 50:11

**10:14** Biblia mara nyingi hutumia stiari ya ndege kuuelezea uangalizi na ulinzi wa Mungu (kama vile Kut. 19:4; Kumb. 32:11; Ruth 2:12; Isa. 31:5; Mt. 23:37; Luka 13:34), lakini hapa stiari imekuwa kinyume! Mungu ameuondoa ulinzi wake!

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 10:15-19**

<sup>15</sup> Je! Shoka lijisifu juu yake alitumiaye? Je! Msumeno ujitujuu yake auvutaye? Ingekuwa kana kwamba bakora ingewatikisa waiinua, au fimo ingemwinua yeye ambaye si mti. <sup>16</sup> Kwa hiyo Bwana, Bwana wa majeshi, atawapelekea kukonda watu wake walionona; na badala ya utukufu wake kutawashwa kuteketea kama kuteketea kwa moto. <sup>17</sup> Na mwanga wa Israeli utakuwa ni moto, na Mtakatifu wake atakuwa mwali wa moto; nao utateketeza na kula mbigili zake na miiba yake katika siku moja. <sup>18</sup> Naye atauteketeza utukufu wa msitu wake, na wa shamba lake linalositawi, tangu nafsi hata nyama ya mwili, itakuwa kama vile afapo mtu aliye mgonjwa. <sup>19</sup> Na miti ya msitu wake itakayosalia itakuwa michache, hata mtoto atawea kuihesabu.

**10:15-19** YHWH anajibu majigambo ya mfalme wa Ashuru kwa kuuliza.

1. Shoka ujisifu juu yake alitumiaye?
2. Msumeno ujitujuu yake auvutaye?
3. Rungu lijisifu juu ya Yule alizungushaye?
4. Fimo ya kifalme ijivune juu ya Yule aiinuaye?

YHWH atamhukumu yeye na jeshi lake siku moja (mst. 17). Hili linarejerea kwa (1) Tiglath-Pileser III au (2) hasa kwa Senakerib (701 K.K.), aliyeandikwa katika Isaya 36-38; II Falm. 18:17-21:11; II Nya. 32:9-24, ambapo wanajishi 185,000 walikufa mbele ya ukuta wa Yerusalem wakiwajibika kwenye kiburi cha mfalme wa Ashuru na viongozi wake wa kijeshi (#2 unafaa zaidi, lakini haikutokea mpaka kipindi cha miaka kumi baada ya Tiglath-Pileser III kuichukua Samaria). Kuna tofauti kati ya Mungu wa Israeli na sanamu za mataifa!

**10:16** YHWH yuko katika udhibiti wa historia. Hii ni kauli yenye nadhalia ya uwepo wa Mungu mmoja ikihsiana na uhusika wa Mungu. Yeye yupo na yu katika utendaji wa uumbaji wake. Katika agano la kale sababu zote

zilitambulika mbele ya YHWH (kama vile Kumb. 32:29; Ayubu 5:18; Isa. 45:7; Hos. 6:1; Amosi 3:6). Ilikuwa ni namna ya kuithibitisha nadharia ya uwepo wa Mungu mmoja. Kiukweli namna gani,lini, wapi alitenda hili haijulikani, bali kuna

1. Mpango wa ukombozi wa milele
2. Watu wa agano
3. Ujio wa Masihi
4. Moyo kwa ajili ya "mataifa"

Historia sio kitu cha kujirudia bali ni imani kuwa viumbe vyote viliumbwa na Mungu kwa kusudi maalumu!

**10:17** Nuru (angalia kumbukumbu katika 9:2) na moto ni alama ya uungu (kama vile 9:19; 29:6; 30:27; 31:9; 33:11-12,14). Angalia Mada Maalum: Moto katika 1:31.

**10:18** "tangu nafsi hata nyama ya mwili" Mwanadamu ana vyote sehemu ya mwili na nguvu ya maisha. Sisi kama wanadamu tumeandaliwa kwa ajili ya maisha kwenye sayari hii na kwa ajili ya ushirika na Mungu asiye wa kimwili! Tunashiriki maisha ya duniani pamoja na wanyama, lakini sisi ni viumbe wa milele!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 10:20-23

<sup>20</sup> Tena itakuwa katika siku hiyo mabaki ya Israeli, na hao waliopona wa nyumba ya Yakobo, hawatamtegemea tena ye ye aliywapiga, bali watamtegemea Bwana, Mtakatifu wa Israeli, kwa kweli. <sup>21</sup> Mabaki, nao ni mabaki ya Yakobo, watamrudia Mungu, aliye mwenye nguvu. <sup>22</sup> Maana watu wako, Ee Israeli, wajapokuwa wengi kama mchanga wa pwani, ni mabaki tu watakaorudi; kuangamiza kumekusudiwa, kunakofurika kwa haki. <sup>23</sup> Kwa maana Bwana, Bwana wa majeshi, atayatimiza maangamizo yaliyokusudiwa katika nchi yote.

**10:20-23** kifungu hiki kinatazamisha juu ya kweli mbili za kithiolojia.

1. YHWH atawalida na kuwarejesha mabaki wote kwa uaminifu ("wale wanaomtegemea Bwana kwa ukweli," BDB 1043, KB 1612, *Niphil KAULI TIMILIFU*) kulikamilisha kusudi lake na uzao wa Ibrahimu.
2. "katika siku hizo" inarejea kwenye siku ya ukombozi. Mtu kamwe hana uhakika ikiwa hii ahadi itatimilizwa huko Uajemi au kwa watu wa Maccabe au siku ya mwisho. Kitabu ambacho kimenisaidia mimi kuelewa uwasilishaji wa unabii na matukio ya siku ya mwisho ni cha D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*.

**10:20** "hawatamtegemea tena ye ye aliywapiga" Ahazi aliamini/kutegemea juu ya Ashuru kwa ajili ya msaada badala ya YHWH, lakini si hivyo siku za usoni watamtegemea (yaani., watu wa Mungu) YHWH pekee!

**10:21** "mabaki watamrudia Mungu" Mabaki wameelezewa kama wale watokao kwa Yakobo na Israeli. Katika muktadha huu lazima kurejea kwenye makabila kumi ya Kaskazini yaliyogawanyika mwaka 922 K.K. na kutekwa na Ashuru mwaka 722 K.K. Wachache kati yao ndio waliorudi Yerusalem pamoja na Zerubabeli na Yoshua baada ya tamko la Koreshi katika mwaka 538 K.K. kuwaruhusu makundi ya watu waliotekwa kurudi kwenye nchi zao za asili. Angalia Mada Maalum: Mabaki, maana tatu katika 1:9. Kifungu kinatafasiri jina la kwanza la mtoto wa Isaya (Shear-jashub) aliyeambatana na babaye kumkabiri mfalme Ahazi (kama vile 7:1-3).

▣ "aliye mwenye nguvu" Hiki ni cheo cha aina ile ile kilichotumika kwa Masihi katika 9:6. Kinapatika katika sehemu hizi mbili tu.

**10:22** "wajapokuwa wengi kama mchanga wa bahari" Hili ni rejeo kwenye ahadi ya vizazi vingi, ambayo ilikuwa ni sehemu muhimu ya agano la Ibrahimu (kama vile Mwa. 22:17; 32:12). Ni utofauti wa namna gani wa kusikitisha unaoonekana pale ahadi ya YHWH kwa wazee wa imani wa vizazi vingi kuwa

1. Kama nyota za angani
2. Kama mavumbi

### 3. Kama mchanga wa bahari

Ilipunguzwa kuitia ukaidi wa agano na ukosefu wa imani binafsi (kama vile mst. 20) kwa wachache kuweza kurudi (kama vile mistari ya 21-22). Hapa ni mfululizo wa Baraka zaa Mungu alizokusudia na uwezo wa mwanadamu aliyeanguka!

#### ▣“kuangamiza kumekusudiwa, kunakofurika kwa haki” Hukumu ya Israeli imekuwa

1. Ikiamuriwa na YHWH, mst. 22
2. Ikitamkwa na YHWH, mst. 23

Haya maneno yote (NASB 1995) yanatafasiri KITENZI kile kile (BDB 358, KB 356, kama vile 28:22; Dan. 9:26,27; 11:36). Mungu atawahukumu watu wake (mst. 22). Mistari wa 23 (1) unafanana na huu au (2) YHWH atahukumu dunia nzima (LXX, Peshitta, NRSV. Paulo anarejea tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania katika Rum. 9:27-28). Muktadha unaendana vizuri na #1. YHWH alisema atafanya; na kweli alifanya!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 10:24-27

<sup>24</sup> Kwa hiyo Bwana, Bwana wa majeshi, asema hivi, Enyi watu wangu mkaao katika Sayuni, msiogope Ashuru, ingawa akupiga kwa fimbo, na kuliinua gongo lake juu yako, kwa namna ya Kimisri. <sup>25</sup> Maana bado kitambo kidogo tu ghadhabu itakoma, na hasira yangu itageukia kuwaangamiza. <sup>26</sup> Na Bwana wa majeshi ataamsha mjeledi juu yake, kama vile alivyopiga Midiani karibu na jabali la Orebu; na fimbo yake itakuwa juu ya bahari, naye ataiinua kwa namna ya Kimisri. <sup>27</sup> Tena itakuwa katika siku hiyo mzigo wake utaondoka begani mwako, na nira yake shingoni mwako, nayo nira itaharibiwa, kwa sababu ya kutiwa mafuta.

**10:24-27** Aya inaongeza msukumo wa haki adilifu ya YHWH ambayo inaaksi kwenye hukumu juu ya uovu.

1. Israeli ilishuhudia hasira ya haki ya YHWH (kama vile mst. 22)
2. Ashuru (kama vile Isa. 37:26-28)
3. Kama ghadhabu yake huko Misri kipindi cha wana wa Israeli kuondoka Misri (kama vile Kut. 14:16,27)
4. Kama Gidioni dhidi ya Wamidiani (Waamuzi 6-8)

Matendo ya YHWH, yaliyopita na yajayo, yaliyoelezewa katika mst. 27, yanafanan na kitendo chake (kama vile 14:25) kuitia kwa Masihi katika 9:4, ambacho pia kinataja vita dhidi ya Wamidiani (ni lahaja ya ushindi kamili wa YHWH juu ya adui, kama vile 9:4; Zab. 83:9-11).

**10:24 “msiogope Ashuru”** KITENZI hiki (BDB 431, KB 432, Qal KAULI ISIOTIMILIFU) kinatumika kama KAULI AMRISHI. Dokezo hapa ni “mwogopeni Mungu awezae kuleta hukumu juu yenu” (mistari ya 25-27).

**10:26 “jabari la Orebu”** Gidioni akawaita watu wa Efraimu ili kumsaidia kuyaondoa mabaki ya watu wa Midiani. Viongozi wawili kati yao walikamatwa na kuuwawa (kama vile Amu. 7:24-25). Mahali pale ambapo hili lilitokea paliwekwa majina ya viongozi wa Wamidiani, Orebu na Gebu. Mahali halisi hapajulikani.

#### 10:27

NASB	“nayo nira itakatika kwa sababu ya kuwa na mafuta”
NKJV	“nayo nira itaharibiwa kwa sababu ya kutiwa mafuta”
LXX, REB	“nayo nira itaharibiwa toka mabegani mwako”
Peshitta	“naya nira itaharibiwa toka shingoni mwako kwa sababu ya nguvu zako”

Kutokana na tafasiri hizi unaweza kupata chaguo moja.

1. Achana na kifungu “kwa sababu ya kutiwa mafuta,” LXX, REB
2. Kinarejerea kwa Masihi, NKJV (yaani., Mtiwa mafuta)
3. Toleo la Peshitta linaliangalia kama rejeo la uimalifu na ukuaji (kama vile Kumb. 32:15), ambalo laweza kukinzana na mst.16.

Kwa vile sura ya 7-12 inavyoelezea juu ya mtoto maalumu wa kizazi kipy, akijumuishwa na Masihi, naupenda uelewa wa toleo la NKJV kama moja lenye kuleta maana kubwa katika sehemu hii ya fasihi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:28-32**

<sup>28</sup> Amefika Ayathi; amepita kati ya Migroni; ameweka mizigo yake huko Mikmashi; <sup>29</sup> wamevuka kivuko; wamekwenda kulala katika Geba; Rama unatetemeka; Gibea wa Sauli umekimbia. <sup>30</sup> Piga kelele sana, Ee binti Galimu; sikiliza, Ee Laisha; ole wako, maskini Anathothi! <sup>31</sup> Madmena ni mkimbizi; wenyeji wa Gebimu wamejikusanya wakimbie; <sup>32</sup> siku hii ya leo atasimama huko Nobu; anatikisa mkono wake juu ya mlima wa binti Sayuni, mlima wa Yerusalem.

**10:28-32** H. C. Leupold, *Exposition of Isaiah*, juzu ya 1, uk. 40, inaelezea huu mstari (ubeti) kama “Mkakati wa Waashuru kusonga mbele ambao kiwastani uliuchukua Sayuni iliyoelezewa kwa namna ya taarifa rasmi ya habari toka mstari wa mbele.”

Sehemu nyingi za kijiografia zimetajwa na kile kilichokuwa kikitokea sehemu hizo kama Waashuru kwa namna jeshi la kukodiwa lilivyosogea.

▣ “**Aiath**” Huu mji wa Ai uko karibu na Yeriko. Mahali palipotajwa panaonyesha kundi la Waashuru dhidi ya Yerusalem tokea Kaskazini.

**10:30 “piga kelele sana. . .sikiliza”** Hizi zote ni KAULI SHURUTISHI.

1. BDB 843, KB 1007, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. BDB 904, KB 1151, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

Hili linakigawa kipengere cha mistari ya 28-32. Ikiwa aya hii ni “taarifa toka walioko mstari wa mbele,” hivyo mst. 30 ni maoni toka kwa nabii, na sio mjumbe wa Waashuru.



NASB	“fukara Anathothi”
NKJV	“maskini Anathothi”
NRSV	“umjibu, O Anathothi”
TEV	“jibuni, enyi watu wa Anathothi”
NJB, REB	“Anathothi atawasikiliza”
Peshitta	“nijibu, O Anathothi”

Hili pia ni kutoka

1. KITENZI “jibu,” BDB 772, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. KIVUMISHI “masikini,” BDB 776

Yote yana konsonanti zinazofanana. Mpango wa andiko la Kiebrania la toleo la UBS linatoa alama C kwenye mstari wa 2a “C” (pasipo mashaka). Hakika ni kweli kuwa neno “masikini” na “Anathothi” ni maneno yenye masihala yanayosikika sana (*NASB Study Bible*, uk. 974).

**10:32** Mstari wa pili wa ushairi unaelezea juu ya chuki ya Waashuru kwa ajili ya Mungu wa Yuda na hekalu lake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:33-34**

<sup>33</sup> Angalia, Bwana, Bwana wa majeshi, atayakata matawi kwa nguvu za kutisha; nao walio warefu wa kimo watakatwa; na hao walioinuka wataangushwa chini; <sup>34</sup> naye atavikata vichaka vyaa msitu kwa chuma; na Lebanoni utaanguka kwa mkono wake aliye mwenye uweza.

**10:33-34** Mistari ya 33-34 ni migumu kuielezea ni kwa yupi “imeondolewa.” inaonekana kuwa ni kiunganishi cha kifasihi kati ya mistari ya 16-19 na 11:1. Isaya mara nyingi hutumia matumizi ya tamathari za semi za elimu ya misitu. Yeyote aliyetunga gombo la Isaya alitumia uchezeshaji wa maneno na dhamira kama njia ya kuunganisha

pamoja jumbe za kinabii za Isaya zilizoandikwa. Kumbuka kuwa ukweli mkuu wa sehemu ya fasihi na aya ni za muhimu kuliko

1. maelezo
2. muundo wenyewe wa kihistoria wa kila fasihi

Upendo wetu kwa ajili ya Biblia na shauku ya kujua zaidi umetusababishia kuifanya Biblia kama isiwe ya kimuktadha, namna ya wazi, ambavyo huharibu asili ya fasihi ya maandiko na hasa unabii!

Nafikiria haya ni maelezo ya kina ya mistari ya 16-19. Sanamu ni uharibifu wa misitu, ambao humaanisha jeshi la Ashuru na uongozi wake.

**10:33** Nusu ya pili ya huu mstari una maneno mengi yanayopatikana hapa tu katika Agano la Kale. Hii ndio sababu kiini cha ukweli wa aya hii (lugha ya mjazo) au ubeti (ushairi) ni wa muhimu. Kweli kuu au pitcha ni suluhisho, na sio kila kitu na kila maelezo

#### **10:34**

**NASB, NKJV** “na aliye mwenye uweza”

**NRSV** “miti iliyo mirefu”

**TEV** “miti mirefu”

**NJB** “mwenye nguvu”

**LXX** “miti iliyo mirefu”

**REB** “miti iliyo mizuri”

Hili linarejerea kwa

1. Mungu (kama vile mst. 33a; mst. 34a)
2. miti mirefu ya Lebanoni (kama vile mst. 33b,c; LXX)

# ISAYA 11

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA				
NASB	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Utarwala wa haki Tawi 11:1-9 (1-9)	Utarwala wa uzao wa Yesse 11:1-5 (1-5)	Mfalme wa Ki-Masihi 11:1-3a (1-3a)	Ufalme wa Amani 11:1 11:1-5 (2-5) 11:3b (3b) 11:4-9 (4-9)	Uzao wa Daudi 11:1-4 (1-4) 11:5 (5) 11:6-9 (6-9) Zama za Ki-Masihi 11:6-9 (6-9)
Mabaki Yakirejeshwa 11:10-16 (10-16)		Watu wa uhamishoni Watarejeshwa 11:10 11:10-16		Kurudi kwa waliotawanyika 11:10-16 (10-16)
	11:10 (10)		11:11-16	
	11:11 (11)			
	11:12-16 (12-16)		(12-16)	

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. wa xvi katika sehemu ya utangulizi)

### KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### KUJIFUNZA HISTORIA YA NYUMA

- A. Sura ya 11 ni ulinganifu mkali wa sura ya 10, mistari ya 33-34, ambayo inaelezea kuanguka kwa Ashuru (kama vile 10:15-19).
- B. Kama Ashuru inavyokatwa chini kama msitu mkubwa, ndivyo Masihi atakavyoinuka kutoka katika shina la Yesse. Isaya mara kwa mara anatumia taswira ya miti.
- C. Isaya 11 ina aksi ahadi ya uzao wa Daudi inayopatikana katika II Samueli 7.

- D. Kipindi hiki kizuri cha matukio ya siku za mwisho pia kinaelezewa katika 2:2-4; 9:1-7. Sura ya 11, mistari wa 10 unaweza kwenda pamoja na 1-9 au 11:16 kwa kutegemea na jinsi mtu anavyotazama utawala wa kiasihi (yaani Nchi ya Ahadi inarejeshwa au dunia nzima).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 11:1-5

<sup>1</sup> Basi litatoka chipukizi katika shina la Yeso,  
na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda.  
<sup>2</sup> Na roho ya Bwana atakaa juu yake,  
roho ya hekima na ufahamu,  
roho ya shauri na uweza,  
roho ya maarifa na ya kumcha Bwana;  
<sup>3</sup> na furaha yake itakuwa katika kumcha Bwana;  
wala hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake,  
wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake;  
<sup>4</sup> bali kwa haki atawahukumu maskini,  
naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili;  
naye ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake,  
na kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya.  
<sup>5</sup> Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake,  
na uaminifu mshipi wa kujifungia.

**11:1 “chipukizi”** Neno hili nadra linapatikana tu hapa katika Agano la Kale, (“shina,” “chipukizi,” au “chipukizi” inafasiriwa “fimbo” katika Mithali. 14:3, BDB 310, KB 307) kidhahiri inamaanisha uzao wa kimungu wa Daudi (kama vile 6:13; II Samueli 7; Ufunuo 22:16) ikitokea kwa kinachoonekana shina lililokufa (yaani Yuda iliyo uhamishoni) patatokea mfalme! Taswira hii (lakini neno la Kiebrania tofauti) inaonekana tena katika Wimbo wa Mtumwa Atesekaye wa Isaya 52:13-53:12 (yaani mstari wa 2).

Toleo la Jewish Study Bible (ukurasa wa 807) inaongeza maoni ya kufurahisha “shina.”

“Ikiwa fasiri ya ‘shina’ ni sahihi, hivyo kifungu cha habari kinawenza kuashiria kwamba Ufalme wa Daudi uta (au ume) umefikia mwisho; sura hii ingeweza kutoka kando kidogo kimuhimu kutoka katika wazo la Isaya kwa wafalme wa Daudi watatawala milele (kama vile II Sam. 7:8-16; Ps. 89:20-37). Lakini Kiebrania ‘geza’ inamaanisha sit u kwa shina la mti ambalo limekatwa na kuanguka chini lakini shina la mti unaoishi.” Siwezi kuthibitisha maana hii ya “chipukizi” mpaka iwe ni 40:24.

▣“**kutoka katika shina la Yesse**” Yesse alikuwa baba wa Daudi. Uzao huu wa baadaye unatajwa katika mstari wa 10; 9:7; 16:5.

Agano la Kale inatoa uzao Ajaye wa pekee, mpakwa mafuta.

1. kutoka katika kabilia la Yuda, Mwanzo 49:8-12, hasa mstari wa 10 na Ufunuo 5:5
2. kutoka katika Familia ya Yesse, II Samueli 7

Mtoto maalum wa zama mpya sasa ametambuliwa kama mtawala maalum. Tabia yake itakuwa ya kizazi kipyta (kama vile Yer. 23:5).

▣“**na tawi litakalotoka katika mizizi yake**” Nomino “tawi,” “ikichipuka,” au “chipukizi” (BDB 666, kama vile 14:19; 60:21; Dan. 11:7) ni sambamba na “tawi” au “kuchipua” (BDB 855, kama vile 4:2; 61:11). Ukuaji mpya utakuja! Angalia Mada Maalum katika 4:2.

▣ “**litazaa matunda**” Toleo la MT lina KITENZI “kuzaa matunda” (קְרָפַ, BDB 826, KB 963, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU*, Magombo ya Bahari ya Chumvi, NASB), lakini zaidi ya kale na matoleo mapya yakidhaniwa kuwa na KITENZI kinachofanana, כְּרָפָ (BDB 827).

1. NKJV, NRSV, Peshitta, “litakua”
2. NJB, “litakua”
3. LXX, Targums, “litatokeza”
4. REB, “litachipuka kutoka”
5. JPSOA, “litachipua”

Mbadala wa pili unashabihiana na usambamba zaidi!

**11:2 “na Roho”** Wengi wamejaribu kuhusianishwa kifungu hiki kuwa na fungu saba za roho wa Ufunuo 1:4. Hii inanitia mashaka mimi. Toleo la MT linataja sifa sita, lakini toleo la LXX linaongeza ya saba, “wema,” katika nafasi ya “hofu” katika mstari wa 2, lakini baadaye linaongeza “hofu” kutoka katika mstari wa 3. Hatahivyo hii inao uhusiano na vyeo vya Isa. 9:6 na vinaelezea mfalme akiwezesha kikamilifu na Mungu katika hekima na maarifa, utawala, na wema. Roho wa Bwana anakaa juu yake kama alivyokaa kwa Daudi (kama vile I Sam. 16:13).

Ule unafsi “Roho” haufunuliwi kikamilifu katika Agano la Kale. Katika Agano la Kale Roho ni ushawishi binafsi wa YHWH katika kutekeleza makusudi yake zaidi sawasawa na “Malaika wa BWANA.” Haifanyiki mpaka Agano Jipyambayo u-nafsi wake kamili na uungu unafunuliwa. Angalia Mada Maalum: Utatu katika 6:8. Angalia Mada Maalum: U-nafsi wa Roho katika 32:15 20.

Tatizo jingine lililo katika neno (BDB 924) ni kwamba inaweza kumaanisha tabia za kibinadamu au matendo ya kiungu.

▣ “**atakaa juu yake**” KITENZI (BDB 628, KB 679) ni *Qal KAULI TIMILIFU* ikiashiria hali iliyotulia. Itakaa na kuendelea kubaki. Ukweli huu huu unatajwa katika njia mbali mbali katika 42:1; 59:21; 61:1; Mt. 3:16; Luka 4:18.

▣ “**roho wa . . .**” Kimsingi kuna makundi matatu ya karama.

1. ya akili
  - a. hekima, BDB 315 (kinyume cha 10:13)
  - b. ufahamu, BDB 108 (angalia jozi ya kwanza katika Kumb. 4:6)
2. utawala wenye ufanisi (kama vile 9:6-7)
  - a. ushauri, BDB 420
  - b. nguvu, BDB 150 (kutawala kwa amani kupitia nguvu ya kijeshi kama vile II Wafalme. 18:20)
3. hofu binafsi
  - a. maarifa ya Bwana, BDB 395
  - b. hofu ya Bwana, BDB 432 (kama vile mstari wa 3)

Aina hii hii ya maelezo inapatikana katika 2:2-4; 9:6-7; 42:1-4. Itakuwa muda wa haki ya kisheria, haki ya krisro na amani.

**11:3 “na furaha yake”** Hii kifasihi inamaanisha “kupumua hewa ndani” (BDB 926, KB 1195, *Hiphil KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO*). Hii inatumika katika namna ya harufu ipendezayo ya dhabihu au uvumba unaopanda kwa Mungu (yaani Mwanzo 8:21).

▣ “**itakuwa katika kumcha BWANA**” Neno hili “hofu” (BDB 432) Inaashiria heshima kwa uzuri wa Mungu. Ilmaanishwa kutunza watu wa agano mbali na kutenda dhambi (kama vile Kutoka 20:20; Kumb. 4:10; 6:24). Mfalme wa Daudi alikuwa akimuhofu YHWH (kama vile II Sam. 23:3). Masihi huyu, Daudi Mpya kiukamilifu anaaksi heshima hii kama mfano wa kuigwa wa “Mu-Israeli wa kweli.” Kumbuka namna inavyotengenezwa utangulizi wa Mithali (kama vile 1:7; pia kumbuka 2:5; 14:26,27)!

■ “**hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake**” Kwasababu ya karama za Roho kwa huyu mtawala wa Daudi maalum atakuwa na uwezo wa kuutambua ukweli na kutodanganywa na ushuhuda wa uongo. Atakuwa hakimu afaaaye wa haki. Mfalme wa Israeli alifanya kazi lama msuluhishi wa mwisho wa haki.

**11:4** Je inashangaza kwako kwamba umaskini na unyanya saji utaendelea katika zama mpya? Aina hii ya ubayana ambayo inasababisha mkanganyiko. Kusudi la mstari huu ni tabia ya Mtawala, sio maelezo ya jamii ya kimelenia! Ilikusudiwa kuonesha kwamba ataleta ufananishao wa uzuri wa agano lililofunuliwa na Mungu. Ataaksi tabia ya YHWH mwenyewe character kuashiria hii katika uhusiano wa kibinadamu!

■ “**haki**” Angalia Mada Maalum katika 1:4.

■ “**kwa fimbo ya kinywa chake,**” Hii inaonekana kuwa sawasawa na tungo iliyotumika katika Ufunuo 1:16; 2:16, ambayo inazungumzia nguvu ya neno la kutamkwa (kama vile Mwanzo 1; Yohana 1) katika tungo “upanga wa kinywa.” Mistari miwili ya ushairi unazungumza wa (kama vile mstari wa 2c).

**11:5** Kuvalishwa nguo ni sitiari inayotumika kuelezea sifa ya kuja kwa haki mtawala wa Daudi. Baadaye Paulo atatumia hii kuelezea utoshelevu wa mwamini kwa ajili ya mgogoro wa kiroho (kama vile Efe. 6:14).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11:6-9**

<sup>6</sup> Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo,  
na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi;  
ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja,  
na mtoto mdogo atawaongoza.  
<sup>7</sup> Ng'ombe na dubu watalisha pamoja;  
watoto wao watalala pamoja;  
na simba atakula majani kama ng'ombe.  
<sup>8</sup> Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka,  
na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira.  
<sup>9</sup> Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu;  
maana dunia itajawa na kumjua Bwana,  
kama vile maji yanavyoifunika bahari.

**11:6-9** Hii ni taswira ya kipindi cha Kimasihi, kilichoelezwa katika mtindo wa Mwanzo1 na kutumiwa katika Ufunuo wa Yoana 22. Asili imekuwa ikiathiriwa na dhambi ya wanadamu, Mwanzo 3. Hii pia itaathiriwa na wokovu wa Masihi (kama vile Rum. 8:19-25). Kwa mara nyingine utambue msistizo unaomzungumzia mtoto wa zama mpya.

Uhusiano kati ya wanadamu na wanyama unaikisi Bustani ya Edeni. Wanadamu wana mazoea sana na wanyama kutohuna na kuutawala uso wa syari hii. Hawa pia waliumbwu katika ushirika wa Mungu (kama vile Ayubu 38:39; 40:34) apamoja nasi! Biblia inaanza na Mungu, wanadamu, na wanyama katika mazingira ya bustani (Mwanzo 1-2) na inahitimisha na Mungu, wanadamu, na kwa vifungu hivi vilivyo ndani ya Isaya, wanyama (kama vile Isa. 65:15; Hosea 2:18; Ufunuo wa Yohana 21-22). Mimi binafsi sifikiri kwamba ushirika wetu pamoja na wanyama utakuwambinguni, bali nafikiri kwamba wanyama watawekwa kando dhidi ya umilele! Hawa wapo kwa ajili ya kuongeza utajiri wa ajabu katika maisha. Baada ya Anguko wanyama hawa walibadilika kuwa katika matumizi ya chakula na kutengeneza mavazi!

Hoja nyingine inayohusu utata wa sili iliyohujumuishwa katika maandiko yaliyohusiana na unaohusu mambo yatakayotukia siku za mwisho ni umri wa watu waliotajwa. Kifungu cha watoto (mst. 6) na watoto wanyonyao (mst. 7) kinamaanisha kwamba uzao wa kimwili unaendelea. Hili linafikiri juu ya ufanano wa mpangilio wa kidunia kwa ujumla kwa maisha ya sasa (kama vile Mt. 24:38; Luka 17:27). Hata hivyo, Yesu anadai kwamba hapatakuwa na tendo la kujamiihana kipindi cha zama mpya (kama vile Mt. 22:29-30). Je! Katika siku ya wanadamu wote watakuwa katika zama tofauti? Je! watazeeka? Hya ni maswali ambayo yamewasababisha watoa maoni kudhani juu ya kipindi cha kidunia kilichowekewa mipaka ya urejesho wa haki (yaani, miaka elfu) na utawala uso na dosari. Wengine pia wamedhani juu ya kuwepo mgawanyiko kati ya kundi la mbinguni na kundi la duniani. Napendelea hii

iliyo moja, Ujio wa Mra ya pili unaoonekana na ushirika na Mungu wa haraka ulio kamili. Ikiwa jambo hili ni la kweli, mambo yaliyo mengi ya Agano la Kale na Agano Jipya yanatakiwa kutazaimwa kama malazi yanayohusiana na Ufalme wa Mungu wa kiroho. Tafadhari fuatilia maoni yangu yahusuyo Ufunuo wa Yohana, Daniel, Zechariah mtandaoni bure katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

Hii siku mpya ya amani ya kiulmwengu inaelezwa katika namna isiyofahamika, upana wa eneo, maneno yenye kuhusishwa kwa makusudi. Je! ni lini zama hizi mpya zitajidhihirsha zenyewe?

1. kurudi kutoka uhamishoni chini ya Zerubabeli na Yoshua (yaani, Ezra na Nehemia)
2. kipindi cha Kimakabayo (kipindi cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya)
3. kuhimarishwa kwa Ufalme wa Mungu katika nyakati za Yesu (Injili)
4. kipindi cha mika elfu (Ufu. 20:1-10 pekee)
5. ufalme wa milele (kama vile Dan. 7:14)

Kila kipengele kinatazamwa kama fursa mpya, lakini chenye kukumbwa na matatizo (#1-4). Hapa ndipo mifumo mbalimbali ya kithiolojia (madhehebu) inapoweka utata wa marejeo na kuweka katika "upinzani wa kithiolojia" kuititia kutoa maoni ya Maandiko yote. Ahadi ni za uhakika! Bali kipindi maalumu na maelezo kamili ndiyo hayana uhakika.

Swali moja la msingi ambalo lihahusika na jambo hili ni "Uwazi wa namna gani kurejeshwa kwa bustani ya dunia (yaani, Edeni) ikichukuliwa (Mwanzo 1-3 na Ufunuo 21-22)"? Je! (1) sayari hii ndiyo inayotazamiwa; (2) ulimwengu huu ndiyo unaootazamiwa; au (3) ulimwengu wa roho zaidi ya wakati- ulimwengu, huenda huu ni uana mwagine wa ukweli huu (kama vile Yohana 4:21-24; 18:36)?

## 11:6

NASB, NKJV

NRSV                    "na kinono"

REV, REB                "watakula pamoja"

NJB                      "mbwa mwitu"

Matoleo ya LXX na Peshitta yanaongeza "ox" na pia yanaongeza KITENZI "kula pamoja." Toleo la MT lina kifungu "pasipo dosari," lakini hakina KITENZI. Kwa marekebisho "na pasipo dosari" (ימרר) kifungu hiki kinawenza kubadilishwa na kuwa "watalishwa" (וּמְרִיא). Toleo la UBS Hebrew Text Project linakipa KITENZI daraja "C" (mashaka yenye kufikirika). Kwa ufanano wa mistari ya ushairi miwili ya mwanzo na ule wa nne wenye VITENZI, mtu anaweza kutarajia mstari wa tatu kuwa na KTENZI kimoja pia. Magombo ya Isaya ya Baharia ya Chumvi na Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrani kuna KITENZI "lishwa".

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11:10

<sup>10</sup>Na itakuwa katika siku hiyo,  
shina la Yeso  
lisimamalo kuwa ishara kwa kabilia za watu,  
yeye ndiye ambaye mataifa watamtafuta; na mahali pake pa kupumzikia patakuwa na utukufu

**11:10** Mistari kama ya 4, 9, na 10 inaweza kuelewaka katika namna moja kati ya mbili.

1. YHWH atawarejesha watu wake huki Kanaani na ulimwengu utawapokea.
2. Msistizo wa utawala wa ulimwengu wote uzao wa Daudi unakamilisha ile ahadi ya Mwa. 3:15 ya urejesho wa sura na ufanano wa Mungu ndani ya wanadamu wote, ambao waliathiriwa na Anguko.

Je! Haya maandiko ya Isaya kwa haima yake yanahu Isreali pekee au yanauhusu ulumwengu? Je! Yana usahihi, ni ya kiishara, au yana utimilifu mbalimbali? Hapa ndipo mtazamo wa mtu wa moja kwa moja kuhusu Maandiko unapoanza kuumbika (kwa uzuri au kwa ubaya) kuhusu maandiko. Nina upendeleo kama kila mtu alivyo! Nimejaribu kuchimbua katika Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjili wa Bob. Unaweza kuisoma hii katika 1:3. Ni vugumu kuwa mwaminifu katika maandiko na katika muktadha na katika maandiko yote kwa wakati huo huo! Hakuna anayelitenda hili kwa ukamilifu!

## ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11:11-16

- <sup>11</sup> Na itakuwa katika siku hiyo, Bwana atapeleka mkono wake  
mara ya pili, ili ajipatie watu wake watakaosalia, kutoka Ashuru,  
na kutoka Misri, na kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu,  
na kutoka Shinari, na kutoka Hamathi,  
na kutoka visiwa vya bahari.
- <sup>12</sup> Naye atawatwekea mataifa bendera,  
atawakutanisha watu wa Israeli waliotupwa,  
atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia.
- <sup>13</sup> Na wivu wa Efraimu utaondoka, na wale wanaomwudhi Yuda watakatiliwa mbali;  
Efraimu hatamhusudu Yuda, wala Yuda hatamwudhi Efraimu.
- <sup>14</sup> Nao watashuka, watalirukia bega la Wafilisti upande wa magharibi;  
nao pamoja watawateka wana wa mashariki;  
watanyosha mkono juu ya Edomu na Moabu; na wana wa Amoni watawatii.
- <sup>15</sup> Na Bwana atauangamiza kabisa ulimi wa bahari ya Misri;  
na kwa upepo wake uteketezao atatikisa mkono wake juu ya Mto,  
naye ataupiga, uwe vijito saba,  
na kuwavusha watu wenye viatu vikavu.
- <sup>16</sup> Itakuwako njia kuu kwa mabaki ya watu wake watakaobaki, watokao Ashuru,  
kama vile ilivyokuwako kwa Israeli,  
katika siku ile walijotoka katika nchi ya Misri.

**11:11** Mstari huu unazungumziauangamivu wa hali ya nchi utakaofanywa na Mungu (kama vile 2:2,11,12,20; 3:7,18; 4:1,2; 7:17,18,20; 9:14; 10:3,17,20,27). Hapa panamaanisha siku ya urejesho! Watu wa agano (yaani, katika hali hii Makabila Kumi ya Kaskazini), yaliyotawanyika kupitia Mashariki ya Kale ya Karibu, yatarudi nyumbani (ishara ya kuirudia imani katika YHWH).

Hata hivyo, umoja sahihi uliobaki (sura 7-12) una msingi wa kiulimwengu (kama vile 2:2-4; 9:1-7)!

▣ “mkono wake” Hii ni nahau ya lugha ya kibinadamu ya tendo la ki-Ungu ndani ya historia. Katika Mwanzo 1 Mungu anazungumza na mambo yanatokea, lakini hapa anaunyoosha mkono wake (kama vile mst. 15; 1:25; 5:25; 8:11; 9:12,17,21; 10:4, n.k.).

**11:12 “ncha nne za dunia”** Nne ni tarakimu ya kiishara kwa dunia nzima.

## MADA MAALUM: UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO

- A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.
  1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
  2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchinne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
  3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
  4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
    - a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
    - b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
    - c. makanisa saba, Ufu. 1:20
    - d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
    - e. taa saba, Ufu. 4:5
    - f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
    - g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
    - h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1

- i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
  - j. ngurumo saba, Ufu. 10:3,4
  - k. elfu saba, Ufu. 11:13
  - l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
  - m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
  - n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
  - o. wafalme saba, Ufu. 17:10
5. Kumi– ukamilifu
- a. matumizi katika Injili
    - 1) Mt. 20:24; 25:1,28
    - 2) Marko 10:41
    - 3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
  - b. matumizi katika Ufunuo
    - 1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
    - 2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
    - 3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
  - c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
    - 1)  $144,000 = 12 \times 12 \times 1000$ , kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
    - 2)  $1,000 = 10 \times 10 \times 10$ , kama vile Ufu. 20:2,3,6
6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
- a. Wana kumi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumi na mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
  - b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
  - c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
  - d. mikate kumi na miwili, ju ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
  - e. Watu kumi na wawili, Kumb. 1:23;
  - f. mawe kumi na mawili, Yos. 4:2,3,4,8,9,20
  - g. miktume kumi na wawili, Mt. 10:1

matumizi katika Ufunuo

- 1) makakabila kumi na mbili elfu walioitiwa muhuri, Ufu. 7:5-8
  - 2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
  - 3) milango kumi na mikwili, malaika kumi na wawili, makabila kumi na mawili, Ufu. 21:12
  - 4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
  - 5) Yerusalemu mpya ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufu. 21:16
  - 6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
  - 7) mti wa uzima uzaao matunda, aina kumi na mbili, Ufu. 22:2
7. Arobaini –namba za nyakati
- a. wakati mwengine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
  - b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
    - 1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
    - 2) Musa juu ya Mt. Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
    - 3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
      - a) miaka arobaini ndani ya Misri
      - b) miaka arobaini jangwani
      - c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
    - 4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
  - c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Biblia!
8. Sabini – namba ya jumla ya watu

- a. Israeli, Kut. 1:5
  - b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
  - c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
  - d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
  - e. msamaha (70x7), Mt. 18:22
- A. Marejeo mazuri
1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
- D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

### **11:13 “Efraimu hatamhusudu Yuda, wala Yuda**

**hatamwudhi Efraimu**” Tambua kataka nyakati mpyaumoja ndiyo utakaokuwa kiini, si mgawanyiko ambao ndiyo tabia waliyokuwa nayo watu wa Mungu katika wakati uliopita.

**11:14** Mstari huu unastaajabisha! Je! Unabii aliyoutoa Isaya uliumiza Israeli au inapaswa kutazamwa kwa namna ya ufuno kwa “mataifa” ili kumjia YHWH katika hali ya amani (kama vile 2:2-4)?

▣“**wana wa mashariki**” Kifungu hiki kinaweza kurejelea makundi kadhaa tofauti tofauti, kutegemana na mukadha (kama vile Mwa. 29:1; Amu. 6:3,33; 7:12; 8:10; I Fal. 4:30; Ayubu 1:3; Isa. 11:14; Yer. 49:28; Eze. 25:4,10).

**11:15** Utamaduni wa maadui wa watu wa Mungu waaganoutaondolewa moja kwa ujumla.

▣

**NASB, NKJV,**

**NRSV**                  “*itaharibiwa kabisa*”

**TEV, NJB**                  “*itakauka*”

**LXX**                  “*itakuwa ukiwa*”

**Peshitta**                  “*itakauka kabisa kabisa*”

**REB**                  “*itagawanyika*”

Toleo la NASB linalifuatisha toleo la MT (וְהַרְמָם, BDB 355, KB 353, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), ambapo toleo la UBS Hebrew Text Project linatoa daraja “B” (kuna mashaka fulani). Leo mengine ni (וְהַרְבִּיב, BDB 351, KB 349). Leo la NEB na REB unakisia mzizi uliopendekezwa (חֲרָמָם, KB 354 II, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), ambao unamaanisha “tenga” au “gawanya” (kama vile Kut. 14:16). Hili ni dokezo la uhamisho mpya (kama vile mst. 11)!

**11:16 “njia kuu”** Angalia maelezo kamili katika 19:23.

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Majina ya watoto yaliyotumika katika sura ya 9 na 11 ni daia la Uungu wake?
2. Eleza mrejeo wa kihistoria wa sura za 7 kuitia 10:4 na 10:4 kuitia 34.
3. Je! Asili itakuwa sehemu ya mbingu?

## ISAYA 12

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Maelezo ya shukrani	Nyimbo za kusifu	Nyimbo mbili	Nyimbo za shukrani	Zaburi
12:1-6 (1-6)	12:1-2 (1-2)	12:1-2 (1-2)	12:1-3 (1-3)	12:1-2 (1-2)
	12:3 (3)	12:3-4 (3b-4)		12:3-6 (3-6)
	12:4-6 (4b-6)		12:4-6 (4b-6)	
		12:5-6 (5-6)		

### **MZUNGUKO WA TATU WAUSOMAJI (angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Hii (au hizi) nyimbo za kusifu ndizo za kufungia katika "kitabu cha Immanueli" (yaani , Sura ya 7-12).
- B. kwa sababu ya kifungu cha utangulizi , "katika siku hiyo" kimerudiwa katika mst. 4, baadhi ya matoleo ya (JB, NASB Study Bible) yanafikilia kuwepo na nyimbo za kusifu mbili.
  1. mist. 1-3, kama vile Kut. 15:1-17; Zab 118
  2. mist. 4-6, kama vile Zab. 165:1; 148:13
- C. Unafanana na ule wa kitabu cha Kut. 15 (wimbo wa Musa) na Zab 118. Mara nyingi wakati wa ushindi mkuu au ukombozi, Israeli waliimba nyimbo za kumsifu Mungu wao.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 12:1-6

<sup>1</sup>Na katika siku hiyo utasema,  
Ee Bwana, nitakushukuru wewe;  
Kwa kuwa ijapokuwa ulinikasirikia,  
Hasira yako imegeukia mbali,  
Nawe unanifariji moyo.

<sup>2</sup>Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu;  
Nitatumaini wala sitaogopa;  
Maana Bwana YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu;  
Naye amekuwa wokovu wangu.

<sup>3</sup>Basi, kwa furaha mtateka maji  
katika visima vyta wokovu.

<sup>4</sup>Na katika siku hiyo mtasema,  
Mshukuruni Bwana, liitieni jina lake;  
Yatangazeni matendo yake kati ya mataifa,  
Litajeni jina lake kuwa limetukuka.

<sup>5</sup>Mwimbieni Bwana; kwa kuwa ametenda makuu;  
Na yajulikane haya katika dunia yote.

<sup>6</sup>Paza sauti, piga kelele, mwenyeji wa Sayuni;  
Maana Mtakatifu wa Israeli ni mkuu kati yako.

**12:1 “utasema”** KITENZI (BDB 55, KB 65, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kinadokeza namna ya ukaaji wa Mwisraeli mmoja mmoja (UMOJA). Ni kwa namna ya wimbo wa ushindi unaopatikana kwenye Kut. 15:1-17. Huu pia ni wimbo wa kumsifu YHWH kwa ajili ya ukombozi. Mtu mmoja anaongea kwa niaba ya jamii nzima ya watu wa Agano. Shairi hili fupi limewekwa hapa kwa sababu ya kule kurudi kwao toka uhamishoni kunakotajwa kwenye 11:11-16. Pia lina uhusiano wa makusudi wa kitheolojia wa mataifa kumtambua na kumkaribia YHWH (kama vile. 2:2-4; 11:10; 12:4-6).

▣“**katika siku hiyo**” Hii ni lahaja kwa ajili ya matendo ya YHWH kwenye historia, huenda ni ya muda mfupi au matukio ya siku ile ya hukumu ijayo. Kuna siku ile ya kusaga meno inakuja. Kwa baadhi, ni wakati wa furaha na ushindi,kwa wengine ni wakati wa hukumu na kukataliwa! Kutokutii Agano kunaathiri wakati na umilele! kwasababu kifungu hiki kinajitokeza pote kwenye mst.1 na mst. 4 inawezekana kwamba hii Sura ni nyimbo mbili za kusifu (kama vile toleo la JB).

▣“**nitakushukuru wewe**” KITENZI hiki (BDB 392, KB 389 II, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* kimetumika kwenye maana ya HALI YA KUSIHI) kimsingi kina maana ya “kutupwa” au “kukatiliwa mbali.” Hata hivyo , hasa katika Zaburi, katika shina la neno *Hiphil* linadokeza “kukiri” au kusifu.” Linapatikana katika Isaya 12:1,4; 25:1; 38:18,19.

▣“**Ee BWANA**” Angalia Mada Maalumu : Majina ya Uungu katika 1:1

▣“**ijapokuwa ulinikasirikia**” Hii inaanishi mwitikio wa YHWH kwa watu wake awapendao wavunja sheria mara kwa mara (kama vile . 40:1-2; 54:8; na wengine wengi). Ghadhabu ya Mungu ni ngumu kueleweka kwa wasomaji wengi wa bibilia. Kwangu mimi ulinganifu wa Kumb. 5:9 kwa 5:10 na 7:9 unasaidia. Hasira ya Mungu inafahamika vizuri kama mzazi amutiavyo nidhamu mwanae (kama vile Ebr. 12:5-13).

▣“**Hasira yako imegeukia mbali,**” KITENZI hiki (BDB 996, KB 1427, *Qal KITENZI AMRISHI*) mara nyingi kimetafasiriwa kama “kutubu,” kinapotumiwa kuwahuusu wanadamu. Katika maana ya YHWH kutubu (yaani.,kubadili fikra na matendo ) kuwaelekea watu wake wa Agano (yaani , Hos. 11:8-9). Katika Agano la kale

mara nyingi haswa inahusiana na toba yao. Hata hivyo , katika Agano jipya ( na agano jipya , Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) inasababishwa na Neema na rehema yake, mbali na uwezo wa mwanadamu aliyeanguka kuweza kutenda/kutii/kubadili

▣ “**Nawe unanifariji moyo**” KITENZI hiki (BDB 636, KB 688, *Piel KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kinamaanisha “kufariji,” au “kuliwaza” (kama vile. 22:4; 40:1; 51:3,12,19; 61:2; 66:13). Baada ya hukumu huja faraja; baada ya nidhamu ushirika hurejeshwa! Kuna tumaini kwa ajili ya waasi na watenda dhambi katika rehema za tabia Zisizobadilika za YHWH (kama vile Mal. 3:6).

**12:2 “Mungu ndiye wokovu wangu”** Hakuna KITENZI katika mstari wa shairi hili, ambacho kinatilia mkazo kwenye kifungu. Kwa ajili ya neno “wokovu” (BDB 447) angalia Mada Maalumu katika 33:2.

▣ “**Nitatumain**” KITENZI hiki (BDB 105, KB 120, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kinaonyesha kile kilicho imara (yaani.,kutegemewa) au “kuanguka kifudifudi mbele zake.” KITENZI hiki kinaelezea matumaini thabitu juu ya Mungu (kama vile 26:3,4; Zab.78:22).

▣ “**wala sitaogopa**” KITENZI hiki (BDB 808, KB 922, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) ni kinyume cha kuamini (kama vile. Kut. 28:66; Isa. 44:8,11). kwa sababu wanamwamini YHWH, hakuna haja ya kuhofu ghadhabu yake, lakini wakitumai juu ya pendo lake la agano na ahadi yake (kama vile 1 Yoh 4:17-18)!

▣ “**BWANA YEHOVA**” hivi ni vyeo viwili vya Uungu vinavyohusiana.

1. יה, BDB 219 kifupi cha YHWH (kama vile Kut. 17:16; Zab. 118:14; Isa. 26:4; 38:11)
2. יהו, BDB 217 (YHWH)

Kwa ajili ya mjadala zaidi wa nadharia zenyet kuhusiana na jina la agano la Mungu kutoka kwenye KITENZI “kuwa,” angalia Mada Maalumu katika 1:1.

▣ “**nguvu zangu na wimbo wangu**” Kama ilivyo 12:2a, hakuna KITENZI kwenye hizi NOMINO mbili, kilicholengwa wazi na wanazuoni wa kimasoreti.

1. nguvu, BDB 738, inaelezea neno “mtumishi” katika 49:5 na sifa za Israeli katika Zab. 81:1
2. wimbo, BDB 274 I; NOMINO hizi mbili zinapatikana katika wimbo wa Musa wa ushindi kwenye Kut. 15:2, pia katika Zab. 118:14

Maana ya NOMINO ya pili, זמרה haijulikani (BDB 275 II).

1. wimbo, toleo la NASB, NKJV, NJB, Peshitta (BDB 274 I, KB 274 I)
2. Mwenye uweza, toleo la NRSV, TEV, JPSOA (KB 274 II)
3. Toleo la LXX lina kifungu “utukufu wangu na sifa zangu”
4. Toleo la REB lina kifungu “kimbilio langu na ulinzi”
5. Muundo ulio sawa (זמרת) kama ulivyojitokeza hapa katika Mwa. 43:11, ambapo imetafasiriwa kama “mavuno bora ya nchi”)

▣ inashangaza kwamba mstari wa 1 unaonyesha kuthibitisha kitu Fulani kuwa mstari wa 4 unaonekana kama endelevu. Mashairi ya kiebrania ni tatanishi. Angalia makala ya utangulizi kwenye mashairi ya Kiebrania.

**12:3** KITENZI hiki kina sitiari mbili.

1. Zawadi ya Mungu ya maji yatoayo uzima , hivyo ni ya muhimu kwao wale ambao hutegemea kilimo na ufugaji. maji mazuri yalionekana kama Baraka kutoka kwa Mungu (kama vile . Kumb 27-29)
2. Wokovu/ukombozi unaelezwa kuwa ni chanzo cha utele wa zawadi ya Mungu (kama vile . 48:18;Zab. 36:9; Yer.2:13; 17:13).

▣ “**wewe**” HALI YA UMOJA wa mistari ya 1-2 inabadilika kwenda kwenye WINGI wa furaha ya ujumla (kama vile. mist. 4-6).

**12:4-6** Aya hizi zinataja vitu avifurahiavyo Mungu, watu muhimu (kama vile.mst. 6b) wanapaswa kuvifanya na kwa nini (mst. 5b; 6b)

1. mshukuruni, BDB 392, KB 389, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*,kama vile .mst. 1 (yaani., muundo wa kumwabudu)
2. Liitieni jina lake, BDB 894, KB 1128, *Qal KAULI SHURUTISHI* (yaani., muundo wa kumwabudu)
3. Yatangazeni matendo yake kati ya watu, BDB 393, KB 390, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
4. Litajeni jina lake kuwa limetukuka , BDB 269, KB 269, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
5. Mwimbieni Bwana kupitia nyimbo, BDB 274 I, KB 273, *Piel KAULI SHURUTISHI*(yaani., muundo wa kumwabudu)
6. Na yajulikane haya katika dunia yote, *Kethiv* (yameandikwa) BDB 393, KB 390, *Pual KAULI ENDELEVU;Qere* (yamesomwa) BDB 393, KB 390, *Hophal KAULI ENDELEVU*(Owens, *Analytical Key* kina neno *Hiphil KAULI ENDELEVU*)
7. Paza sauti, BDB 843, KB 1007, *Qal KAULI SHURUTISHI*, kama vile., 54:1
8. piga kelele, BDB 943, KB 1247, *Qal KAULI SHURUTISHI*, kama vile 54:1

Tena tambua mamlaka ya umisionari (kama vile . 2:2-4; 51:4-5).

**12:4 “Liitieni jina lake”** Aya hii inadokeza na kusaidia namna ya kuabudu (kama vile Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5-7; Rum. 10:9-13). Jina linawakilisha mtu binafsi,tabia yake! Kwa kumuuta yeze tunafahamu mahitaji yetu kwake na shauku yetu tufanane nae na tumfurahie yeze.Aya hii inadokeza shauku kwa ajili ya ushirika (kama vile. Isa. 43:1; 45:3,4)!

Toleo la NIDOTTE, juzu. 4, uk. 150, lina orodha nzuri inayosimulia majina ya YHWH.

1. laweza kusifiwa, Yoeli 2:26	6. laweza kutangazwa, Isa. 12:4
2. laweza kupendwa, Zab. 5:11	7. yawezekana kuliende, Mik. 4:5
3. laweza kutamkwa, Zab. 22:22	8. yawezekana kulikufuru, Isa. 52:5
4. laweza kuogopewa, Mal. 4:2	9. laweza kuchafuliwa, Yer. 34:6
5. laweza kusubiriwa, Zab. 52:9	10. yawezekana wamekufuru, Ezek. 36:21-23

Watu wa Mungu wanaweza kumtafakali waziwazi au kinyume, lakini tunamtafakali yeze (kama vile. Mat. 5:13-16)!

**12:5 “Na yajulikane haya katika dunia yote”** Mpango wa YHWH ni kwamba wanadamu wote walioumbwa kwa Sura na mfanano wake (kama vile Mwa. 1:26, 27); walioumbwa wakiwa na ushirika na Yeye Mwenyewe (kama vile . Mwa 3:8), kurudisha ukaribu wa ndani, kuwepo na ushirika wa imani ya kila siku na muumba wao! Hili ndilo lengo la ufunuo (kama vile. Isa. 2:2-4; 25:6-9; 42:6-12; 45:22-23; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:23; Zab. 22:27; 66:24; 86:8-10; Mik. 4:1-4; Mal. 1:11; Yn 3:16; 4:42; 1 Tim. 2:4; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:1; 4:14).

**12:6** Aya hii ni sehemu katika hekalu lililoko Yerusalem. Nafasi iliyopo kati ya mbawa za makerubi wawili juu ya sanduku la Agano inaonekana ni kama mahali pa kuweka miguu pa YHWH, mahali ambapo mbingu na ardhi hukutana. Haya maelezo yanafanana na jina la mtoto , “Immanueli,” ambalo lina maanisha “Mungu pamoja nasi.” Hakuna Baraka kubwa zaidi kama uwepo wa YHWH na ushirika binafsi naye!

▣“mtakatifu wa Israeli” tazama muhtasari katika 1:11,24.

## ISAYA 13

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Unabii juu ya Bbeli	Mbinu dhidi ya Babeli	Miungu dhidi ya Mataifa ya Kigeni (13:1-23:18)	Mungu Ataiadhibu Babeli	Dhidi ya Babeli
13:1-5	13:1	13:1	13:1	13:1
(2-5)	13:2-3 (2-3)	13:2-3	13:2-3 (2-5)	13:2-22 (2-22)
Hukumu ya Siku Ya Bwana	13:4-5 (4-5)	13:4-5 (4-5)	13:4-5	
13:6-16 (6:16)	13:6-10 (6:10)	13:6-22 (6:22)	13:6-10	
	13:11-16 (11-16)		13:11-13	
Babeli Itaangukia Mikononi mwa Wamedi			13:14-16	
13:17-22 (17:22)	13:17-22 (17-22)		13:17-22	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Sura ya 13 inatengeneza mgawanyo mpya katika kitabu cha Isaya ambacho kinatengeneza upanuzi kuitia 21:17na pia 23:1-8. Kipengele cha Isaya kinashughulika na hukumu kwa mataifa yaliyozunguka eneo hili. Hii ni ya aina hii na ya namna yake. Sura hii inafanana sana na Yeremia 46-51; Ezekiel 25-32; Amosi 1-2; Obadia, Nahumu, na Sefania 2.

B. YHWH anayaambia mataifa yaliyozunguka, yote yaliyo makubwa kwa madogo, kupertia kwa nabii wake; kuhusu habari ambazo hawataziskia kamwe au kutoziitikia hata kidogo. Jambo hili linamaanisha ukuu wake kwa ulimwengu (kama vile 2:1-4; 9:7; 11:9)! Yeye ni Mfalme wa dunia ; Bwana wa uumbaji (kama vile LXX Kut. 32:8)!

C. Mataifa yanayoambiwa ni

1. Babeli (ama Ashuru kwa kutumia jina la kitu cha enzi cha Babeli "Mfalme wa Babeli"), 13:1-14:23
2. Ashuru, 14:24-27
3. Filistia, 14:28-32
4. Moabu, 15:1-16:14
5. Shamu, 17:1-3
6. Israeli, 17:4-14
7. Ethiopia (Kushi), 18:1-7; 20:1-6
8. Misri, 19:1-25; 20:1-6
9. Babeli, 21:1-10
10. Edomu, 21:11-12
11. Arabuni, 21:13-17
12. Yerusalem, 22:1-25
13. Tiro, 23:1-18

Utatambua kwamba Ashuru inaonekana kutoendelea katika andiko la sura ya 14:24-27. Inashangaza kwamba

1. Babeli inaambiwa kwanza wakati tataizo lililokuwepo katika siku za Isaya lilipokuwa Ashuru.
2. Babeli inaambiwa tena katika 21:1-10.
3. Kwa haraka Ashuru inatajwa kwa ufupi tu katika 14:24-27 pasipo kichwa cha habari kipyä (yaani, "uaguzi")

Njia moja ya kushughulikia matatatizo haya ni kutoa maoni juu ya 13:1-14:27 kama ilivyoelekezwa juu ya ashuru. Kwa ujumla Ashuru iliiteka na kishambulia Babeli mnamo 689 K. K. na wafalme wake walijichukulia jina la "mfalme wa Babeli" (kama vile 14:4). Ikiwa jambo hili ni sahihi kisha hii si Babeli mpya (yaani, Nebukadreza), bali ni Babeli ya (Mer odach-baladan) ambayo aliangukia mikononi mwa Ashuru katika 729 K.K. na makao mkuu ya Babeli yaliharibiwa na kuondolewa mnamo 689 K.K. Toleo la NASB Study Bible uk.976) linaeleza kwamba hakuna kichwa cha habari kipyä chenye kichwa cha habari "utabiri" katika 14:24, ambacho kinamaanisha muungano mmoja wa kimaandishi kutoka 13:1-14:32.

Tatizo moja la mtazamo huuu ni kwamba "Wamedi," walioiharibu Babeli Mpya mnamo 539 K.K., wanatajwa katika mst. wa 17. Hata hivyo, kwa kuishinda Ashuru mnamo 660, Midiani na Babeli waliungana kwa ajili ya kufanya uasi dhidi ya himaya iliyoanguka chini ya utawala wa Asur-bani-pali (IVP Bible Background Commentary, uk. 601). Makao makuu ya Ashuru yалиshindikana kutokana na jeshi la Kimidiani la Babeli lililoungana mnamo 612 K.K

D. Hii ni sehemu mzuri ya kuonyesha namna vipengele vya kiushairi vinavyobadilika kutoka mtu wa kwanza (nabii anayezungumza kwa niaba ya Mungu) hadi kwa mtu wa tatu (nabii anayemzungumzia Mungu).

1. Mistari ya 1-3, mtu wa kwanza
2. Mistari ya 4-10, mtu wa tatu
3. Mistari ya 11-16, mtu wa kwanza
4. Mistari ya 17-18, mtu wa kwanza
5. Mistari ya 19-22, mtu wa kwanza

Lakini mist. ya 13 na 19 inaonyesha namna ilivyo vigumu kuufuatisha muundo huu. Katika ukweli analazimisha kurudi nyuma kwa hiari na yule wa nne kwa ajili ya kuufunua ujumbe "kiushairi (namna ya kucheza na maneno, mapigo ya mistari, maneno adimu, mabadiliko ya mtu).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 13:1-16

- <sup>1</sup>Ufunuo juu ya Babeli; maono aliyoaona Isaya, mwana wa Amozi.
- <sup>2</sup>Haya! Juu ya mlima usio na miti inueni bendera,  
wapazieni sauti zenu, wapungieni mkono, kwamba waingie katika malango ya wakuu.
- <sup>3</sup>Mimi mwenyewe nimewaamuru watu wangu waliowekwa wakfu kwangu,  
naam, nimewaita watu wangu walio hodari kwa ajili ya hasira yangu,  
watu wangu wenye kutakabari.
- <sup>4</sup>Kelele milimani kama kelele za watu wengi sana;  
kelele za falme za mataifa waliokutana pamoja; Bwana wa majeshi anapanga jeshi kwa vita;
- <sup>5</sup>watu waliotoka katika nchi iliyo mbali,  
tokea upande wa mwisho wa mbingu;  
naam, Bwana na silaha za ghadhabu yake, ili aiangamize nchi yote.
- <sup>6</sup>Pigeni kelele za hofu; maana siku ya Bwana i karibu;  
itanyesha kama maangamizi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu.
- <sup>7</sup>Kwa sababu hiyo mikono yote italegea,  
na moyo wa kila mtu utayeyuka.
- <sup>8</sup>Nao watafadhaika;  
watashikwa na utungu na maumivu;  
watakuwa na utungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa;  
watakodoleana macho; nyuso zao zitakuwa ni nyuso za moto.
- <sup>9</sup>Tazama, siku ya Bwana inakuja,  
siku kali, ya hasira na ghadhabu kuu, ili iifanye nchi kuwa ukiwa,  
na kuwaharibu watu wake, wenye dhambi, wasikae ndani yake.
- <sup>10</sup>Maana nyota za mbinguni na matangamano havitatoa nuru yake;  
jua litatiwa giza wakati wa kucha kwake,  
na mwezi utaacha nuru yake isiangaze.
- <sup>11</sup>Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake,  
na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao;  
nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi; nami nitayaangusha chini majivuno yao walio wakali;
- <sup>12</sup>nitafanya wanadamu kuadimika kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya Ofiri.
- <sup>13</sup>Kwa hiyo nitazitetemesha mbingu,  
na dunia itatikiswa itoke katika mahali pake,  
kwa sababu ya ghadhabu ya Bwana wa majeshi,  
na kwa sababu ya siku ya hasira yake kali.
- <sup>14</sup>Basi, itakuwa kama vile paa aliyetishwa, na kama kondoo wasio na mtu wa kuwakusanya;  
kila mtu atageukia watu wake; nao watakimbia,  
kila mtu aende nchi yake mwenyewe.
- <sup>15</sup>Kila mtu atakayeonekana atatumbuliwa,  
na kila mtu atakayepatikana ataanguka kwa upanga.
- <sup>16</sup>Na watoto wao wachanga watavunjwa-vunjwa mbele ya macho yao,  
nyumba zao zitatekwa nyara, na wake zao watatendwa jeuri.

13:1

NASB, NRSV,

REB “madhabahu”

NKJV “mzigo”

TEV “ujumbe”

NJB “mbiu”

LXX	“maono”
Peshitta	“unabii”

Hili neno (BDB 672, KB 639) linaweza kumaanisha “mzigo” au “furushi.” Hili (BDB 672 III) linatumika mara kumi na moja katika kipengele hiki (sura za 13-23) cha Isaya ili kueleza juu ya maono ya hatma ya baadaye ya mataifa yaliyozunguka Israeli. Hili neno kimsingi linaweza kudokeza

1. sauti iliyopazwa kwa ajili ya kuufikisha ujumbe
2. ujumbe uliobebwa na mtu hadi kumwelekea mpokeaji
3. mbingu zinazohusiana na maono ya hukumu.

▣ **“Babeli”** Hii ilikuwa himaya ya Mashariki ya Kati ambayo iliwaletea watu wa Mungu madhara. Hii nguvu kuu ya kwanza ya ulimwengu ya Mashariki ya Kati kuletea madhara Israeli ilikuwa Ashuru, na baadaye Babeli Mpya, kisha Iran. Babeli inatumika katika Biblia kama ishara ya unyanyasaji na ukatili (kama vile I Pet. 5:13; Ufu. 14:8;16:19; 17:5). Kuanguka kwa Babeli kunafunuliwa katika 13:1-14:23 (Babeli ya kale) na 21:1-10 (Babeli mpya). Angalia katika Tambuzi za Kimuktadha, C, aya ya pili.

▣ **“aliyoyaona Isaya, mwana wa Amozi”** Adui wa papo kwa papo wa Israeli na Yuda katika siku za ya alikuwa Ashuru. Lakini nabii wa Mungu alionyeshwa (“aliona,” BDB 302, KB 301, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 1:1; 2:1; 13:1; Amosi 1:1; Mik. 1:1; Hab. 1:1) kifo cha baadaye cha Babeli, Ashuru, Babeli Mpya, na kuinuka kwa Koreshi Mkuu (kama vile mst. 17; 44:28-45:1). Wale wote walioukataa unabii uliotabiriwa watakumbana na kotoridhika hali inayoathiri tafsiri zote za tafsiri zao! Angalia Tambuzi za Kimuktadha, C, aya ya pili.

Unabii wa Unabii wa awali ndio ushahidi mkuu wa nguvu ya kipekee ya Biblia iliyovuviwa. Angalia mahubiri “Tumaini la Agano la Kale” na “Tumaini la Agano Jipy” mtandaoni katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) katika kipengele cha “Mahubiri ya Video” chini ya Lakeside Baptist church.

**13:2** Kifungu hiki kinatoa ufanuzi wa jeshi lenye nguvu(kama vile mst. 9). Kutokana na mst. 17 tunajifunza kwamba hili ni jeshi la (1) Ashuru au (2) Irani chini ya Koreshi II yaliyokusanya na Mungu kwa ajili ya kuwashinda aidha yale “ya kale” au “mapya” Babeli (kama vile 44:28; 45:1).

▣ **“wapazieni sauti zenu”** Kifungu kinafanua namna maaduiwa kale walivyofanya mawasiliano.

1. viashiria, bendera karika maeneo yanayoonekana, kama vile 5:26; 31:9; Yer. 51:12
2. kelele (muunzi, kama vile 5:26)
3. kutikisa mikono, kama vile 10:32; 19:16

Kuna mitiririko ya KAULI SHURUTISHI yenye kudokeza mapenzi ya YHWHLI.

1. pazeni, BDB 669, KB 724, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. inueni, BDB 926, KB 1202, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
3. wapungieni, BDB 631, KB 682, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile. 10:32; 11:15; 19:16
4. waingie, BDB 97, KB 112, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, lakini inatumika katika namna ya KAULI YENYE MASHARTI (Toleo la NEB linabadili irabu na lina “toeni silaha zenu, enyi wenyewe mamlaka”)

**13:3“nimewaamuru watu wangu waliowekwa wakfu”** Mungu anaendelea kuitawa historia! Hwa wanajeshi wakuu hawakuwakifishwa katika maadili au maana ya kidini. Kwa sehemu kubwa hawawatambui watumishi wa Mungu “waliotengwa” (“uweki wakfu,” BDB 872, KB 1073, *Pual* ya KAULI ENDELEVU) kwa ajili ya kuyatenda maagizo yake. Hii dhana inaweza kuonekana katika kifungu cha Koreshi kuitwa “Mchungaji wangu” katika 44:28; “ampakwa mafuta” katika 45:1.

Tambihi ya toleo la Jewish Study Bible inatotokana na toleo la JPSOA inakiona kifungu hiki kama “Wawafikishwaji wangu” (yaani, “Aliyetakaswa”) kama rejeo la karamu ya dhabihu ambapo wageni wanaambiwa kuandaa chakula wao wenyewe (uk. 809).

Uchaguzi mwingine ni kuona shairi hili kama istilahi lenye kueleza “Vita Takatifu” na kama ni hivyo, kisha haya yangweza kuwarejelea malaika (kama vile Yoshua. 5:13-15).

**13:4** Kifungu hiki kinafafanua sauti za mapambano ushindi!

**13:5** YHWH nayaachilia majeshi katili kutoka Mashariki ya Kati ili kuwaadhibu watu wake humo KAnaan (kama vile. 5:26; 7:18).



<b>NASB</b>	“nchi iliyo mbali”
<b>NKJV, Peshitta</b>	“mwisho wa mbinguni”
<b>NRSV</b>	“mwisho wa mbingu”
<b>TEV</b>	“miisho ya dunia”
<b>NJB</b>	“nchi ya mbali”
<b>LXX</b>	“kutoka msingi mkuu wa mbingu”

Toleo la NRSV ndilo shihi zaidi. Hili linadokeza mahali ambapo juu huchomoza, hivyo, kwa upande wa mashariki, kuna uelekeo mkuu wa hii kuwa nguvu ya nchi ya nyumbani ya Mesopotamia.

**13:6** “*Pigeni kelele*” Hili neno (BDB 410, KB 413, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI) linarejelea juu ya kupiga vigelegele, kupiga kelele. Hawa wabobeaji wa kelele hizi wanabebwa sana na hisia katika kuomboleza kuliko wenyeji wa mashariki. Neno hili linatumika katika Isaya (kama vile 13:6; 14:31; 15:2,3; 16:7 [mara mbili]; 23:1,6,14; 52:5; 65:14) na pia katika Yeremia (kama vile. 4:8; 25:34; 47:2; 48:20,31,39; 49:3; 51:8).

▣ “**maana siku ya Bwana i karibu**” Mungu muumbaji ni mmwaminifu, Mungu mwenye mwenye mwenendo mwema. Yeye huuchukulia uumbaji na viumbe wake katika nuru ya sifa yake. Wakati mwingine anachukua ukaribu kutokana na ukubalifu na baraka, lakini kwa wakati mwingine (kama ilivyo hapa) anweka ukaribu kutokana na hukumu (kama vile Kumbukumbu 27-29). Viumbe vyote vyenye kuenenda vema lazima vitoa hesabu zote kwa muda tu na katika siku ya mwisho (kama vile Mt. 25:31-46; Ufu. 20:11-15) kwa yule aliywapa uhai!

▣ “**Mwenyezi**” Huu ni wadhifa wa Kiebrania *Shaddai*. Hili lilikuwa jina la ubaba la YHWH (kama vile Kut. 6:3). Angalia Mada Maalum: Mjina ya Uungu katika 1:1. Hapa kuna mzaha wa sauti (BDB 994) kati ya “uharibifu” (כָּשֵׁר, BDB 994) na “Mwenyeji” (מְשִׁיר, BDB 994). Tambua uhusiano wa Yoeli 1:15.13:7-8 Ukaribu wa YHWH utasababisha mwitikio fulani wa woga.

1. “kelele,” mst. 6
2. “mikono yote itaangukia patupu” mst. 7, kama vile Eze. 7:17; 21:7
3. “kila moyo wa mwanadamu utayeyuka,” mst. 7, kama vile 19:1; Nah. 2:10
4. “watafadhaika,” mst. 8
5. “watashikwa na utungu na maumivu,” mst. 8
6. “utungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa,” mst. 8, kama vile 21:3; 26:17; 66:7
7. “watakodoleana macho,” mst. 8
8. “nyuso zao zitakuwa ni nyuso za moto,” mst. 8

**13:9** Mstari huu uinafafanua siku ya Bwana kama inavyohusiana na wenye dhambi (kama vile mst. 10). Nchi iliyotelekezwa na isiyokaliwa na watu hakika ni kinyume cha mapenzi ya Mungu kwa uumbaji wake (kama vile Mwanzo 1-2).

**13:10** Ukaribu wa YHWH kwa uumbaji wake wa kimwili ulisababisha asili ya mapambano. Haya mapambano mara nyangi yanarejelewa kama kipindi cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipy, lakini katika uhalisia wake haya ni ya kistiari za mabii wa Agano la Kale katika kipindi cha uwazi wa Agano la Kale na Agano Jipy.

1. nyota na mikusanyiko yenye nkustisha mng’ao (watu wa kale walifikiri kuwa hawa walikuwa hawa walikuwa miungu watawalao maisha), mst. 10
2. juu na mwezi vilikuwa hafufu, mst. 10
3. mbingu zitatikiswa, mst. 13

4. dunia zitatetemeka, mst. 13

Mbingu, makao ya Mungu, yalifunkwana giza na kuogofya (kama vile Eze. 32:7; Yoeli 2:10,31; 3:15; Mt. 24:29; Ufu. 6:12-13). Lakini kuna nuru mpya inayokuja (kama vile 2:5; 9:2; 60:1-3,19-20).

**13:11 “ulimwengu”** Hii (BDB 385) ni kisawe cha kiushairi kwa יְהוָה! (yaani, “nchi,” “dunia,” kama vile 14:21; 24:4; 34:1). Ni dhahiri kuwa huu ni uchochezi (au isiwe hivyo, kama vile 24:4; 34:1), lakini kifungu hiki hakielezi dhana ya kithiolojia ya YHWH muumbaji na mtawala wa sayari hii! Tambaua namna wanadamu wanavyobainishwa.

1. uovu
2. walivyodhoofika kwa sababu ya ukosaji wao
3. kiburi cha majivuno
4. kiburi cha ukatili wao

Hizi tabia zinazofanana ziafanua juu ya watu wa agano katika 2:9,11,17; 5:15!

Viungo vya wafu (yaani, ubinafsi, dhambi) wa Anguko viko kila mahali (pia elewa Mwa. 6:5,11; 8:21)!

**13:12 “Ofiri”** Jina hili linarejea eneo la kijiografia ka kusini mwa Aramu. Dokezo hili ni kwamba kila mwana damu aliye hai ataadika sana katika siku hiyo ya hukumu.

**13:14-16** Huu ni ufanuzi halisi wa wavamizi wenye kutia hofu.

1. paa aliyetishwa
2. kondoo wasio na mtu wa kuwakusanya
3. kila mtu atageukia watu wake
4. kila mtu aende nchi yake mwenyewe
5. ataanguka kwa upanga
6. watoto wao wachanga watavunjwa-vunjwa mbele ya macho yao, kama vile 18; II Fal. 8:12; 15:16; Hos. 13:16; Nah. 3:10
7. nyumba zao zitatekwa nyara
8. wake zao watatendwa jeuri (NASB), kama vile Kumb. 28:30.

Hukumu itokanayo na uvamizi lilikuwa tendo la kutisha. Hivi vita ya mataifa ya kutisha ilitoa tiba na kuipokea tiba hii (kama vile Zab. 137:8-9)! Mdhali mu wa haya majeshi yenye ghasia alikuwa Ashuru.

**13:16** Hii tambihi ya toleo la MT inapendekeza kwamba KITENZI “kushinda” (BDB 993, KB 1415, *NiphalyaKAULI YA ISIYO TIMILIFU*, kama vile Kumb. 28:30; Yer. 3:2; Zek. 14:2) kinasomwa (*Qere*) kama “kuzungukwa na” (BDB 1011, KB 1486, *Niphalya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*. LXX; Mambo ya Walawi 15,20; Kumbukumbu la Torati 22,27; Mik. 7:5).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 13:17-22

<sup>17</sup>Tazama, nitawaamsha Wamedi juu yao,

ambao hawaoni fedha kuwa kitu, wala hawafurahii dhahabu.

<sup>18</sup>Na nyuta zao zitawaangusha vijana; wala hawatahurumia mazao ya tumbo;  
jicho lao halitawahurumia watoto.

<sup>19</sup>Na Babeli, huo utukufu wa falme, uzuri wa kiburi cha Wakaldayo,  
utakuwa kama Sodoma na Gomora hapo Mungu alipoiangamiza.

<sup>20</sup>Hautakaliwa na watu tena kabisa, wala watu hawatakaa ndani yake tangu kizazi hata kizazi.  
Mwarabu hatapiga hema yake huko,  
wala wachungaji hawatalaza makundi yao huko.

<sup>21</sup>Lakini huko watalala hayawani wakali wa nyikani;  
na nyumba zao zitajaa bundi; mbuni watakaa huko; na majini watacheza huko.

<sup>22</sup>Na mbwa-mwitu watalia ndani ya ngome zake;  
na mbweha ndani ya majumba ya anasa; na wakati wake u karibu kufika,  
na siku zake hazitaongezeka.

**13:17 “Wamedi”** Hii ni nguvu nyingine ya Mashariki ya Kati ya kaskazini mashariki mwa Ashuru. Kwa mara ya kwanza walihusiana na Babeli ya “kale”, lakini hawakuwa na uhusiano na Uajemi iliyokuwa chini ya Koreshi II (kama vile 44:28; 45:1; Yer. 51:11).

▣ **“ambao hawaoni fedha kuwa kitu, wala hawafurahii dhahabu”** Hili jeshi litakuwa lenye makusudi mengi ya kulipiza kisasi, hapatakuwa na uwezekano wakuzinunua tena!

**13:18 “hawatahurumia mazao ya tumbo”** Kifungu hiki kiawarejelea watoto ambao hawajazaliwa na mama zao au watoto wadogo.

▣ **“jicho”** Neno hili linatumika kuwakilisha mitazamo/matendo ya mtu (kama vile Kumb. 7:16; 13:8; 19:13; Eze.7:4; 16:5; 20:17). Hapa ni kudokeza kwamba wavamizi hawatakuwa na uchungu juu nya watoto wao. Huu mstari wa ushahiri una ufanano na mstari wa hapo juu! Majeshi ya Wamidiani hayakuwa na mapatano wala huruma (kama vile Yer. 6:23; 21:7;50:42).

**13:19** Utamaduni wa uremboBabeli na weledi ulijulikana vema (yaani, Danieli 4 wa Babeli Mpya), lakini wotw huwo utwpotezwa na kuharibiwa! Hata hivyo, jambo hili linairejelea Babeli wakati wa kipindi cha Ashuru, kwa ujulma uliharibiwa mnamo 689 K.K. na Senakaribu.<sup>158</sup>

▣ **“Wakaldayo”** Hili lilikuwa jina la kabile la kusini mwa Babeli na mara nyingi lilitumika kama kisawe cha mataifa yajayo ya Babeli Mpya (yaani, Nebukadreza). Kwa maana nyingine ya neno hili angalia Dan. 1:24.

▣ **“Sodoma na Gomora”** Hii ni miji ya udhalimu mkuu, ambayo Mungu aliiteketeza kwa moto na nguzo ya chumvi (kama vile Mwa. 19:24-28;Kumb. 29:23).

**13:20-22** Hii ni lugha yenyе kutia uchochezi (kama vile maombolezo juu ya Uri na maono ya Nefatiti juu ya Himaya ya kale ya Misri). Mji ulishindwa katika siku za Merodach-baladani kwa Ashuru kwa maangamizi ya moja kwa moja. Mjiulishindwa kutokana na jeshi la Umedi-Uajemi mnamo 539 K.K. pasipokuwa na kuenea kwa uharibifu.

Kitabu ambacho hakika kimenisaidia, kama mtu wa mashriki ya sasa, kuuelewa unabii wa mashariki na fasihi ya kipindi cha utulivu wa Agano la Kale na Agano Jipyä ni chake D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*.

**13:20** Angamizo lilikamilika sana kwamba

1. halikuwa la kurithiwa na vizazi
2. Waaramu hawakuweka makao yao mahali pale
3. hakuna mifugo iliyofugwa mahali pale
4. majengo yaliyobaki yalitumiwa na wanyama mwitu pekee (huenda mapepo , kama vile mist. 21-22; 34:13-15; Ufu. 18:2)
5. hapakuwa na utambulisho wa taifa tena

Kifungu hiki kinaendana na Babeli ya” kale” kuliko Babeli “mpya”. Wamedi waliuvunja umoja wao na Merodach-baladani na kuungana na Ashuru katika kuuharibu mji wa Babeli mnamo 689 K.K.

## ISAYA 14

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kudhihakiwa kwa Israeli	Rehema juu ya Yakobo	Kurudi toka uhamishoni	Kurudi toka uhamishoni	Mwisho wa Uhamisho
14:1-2	14:1-2	14:1-2	14:1-2	14:1-2
	Kuanguka kwa Mfalme wa Babeli	Namna wenyewe nguvu walivyoanguka	Mfalme wa Babeli katika ulimwengu wa wafu	Kifo cha mfalme wa Babeli
14:3-23 (3-21)	14:3-4a	14:3-11	14:3-4a	14:3-8
	14:4b-8 (4b-8)	(4b-11)	14:4b-8	(4b-8)
	14:9-11 (9-11)		14:9-11	14:9-15 (9-15)
	Kuanguka kwa Ibilisi			
	14:12-15 (12-15)	14:12-20a (12-20a)	14:12-15	
	14:16-17 (16-17)		14:16-17	14:16-21 (16-21)
	14:18-21 (18-21)		14:18-21	
	Babeli inaangamizwa	14:20b-21 (20b-21)	Mungu ataiangamiza Babeli	
	14:22-23 (22-23)	14:22-23	14:22-23	14:22-23
Hukumu juu ya Ashuru	Ashuru inaangamizwa	dhidi ya Ashuru	Mungu atawaangamiza	Dhidi ya Ashuru
14:24-27	14:24-27 (24-27)	14:24-27 (24-27)	14:24-27	14:24 (24)
				14:24 (24)
				14:25 (25)
				14:26 (26)
				14:27

	Ufilisti inaangamizwa	Dhidi ya Ufilisti	Mungu atawaangamiza Wafilisti	(27) Dhidi ya Wafilisti
14:28	14:28-31	14:28-31	14:28	14:28
Hukumu juu ya Ufilisti				
14:29-32			14:29-30	14:29 (29) 14:30-31 (30-31)
			14:31	
14:32 (32)	14:32 (32)	14:32	14:32	14:32

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

A. Pamekuwepo na mijadala mingi juu ya uhusiano wa 14:12-21 na shetani. Inanionyesha kuwa lazima tuuchukulie kwa uzingativu mkubwa muktadha wa kihistoria na maelezo muhimu ya fasihi ya Isaya na kusisitiza kuwa mwanzoni hili lilirejerea kwa mfalme wa Babeli (au wafalme wa Ashuru baada ya mfalme Ashurbanipal). Hata hivyo, tatizo la mfalme wa Babeli, kama vilivyo viumbe vingine vyenye kutambulika, lilikuwa ni kiburi. Tukirudi kwenye Mwa. 3:5, tanaiona shauku hii kuwa kama Mungu. Sio tu kwamba dhambi iliathiri ulimwengu wa kimalaika, lakini pia anasa za kidunia (kama vile Danieli 4; 11:36; Ezek. 28:13na kuendelea; II The.2:4). Inanionyesha kuwa “Babeli” katika Biblia ni aina ya serikali ya mwanadamu asiye mjua Mungu (kama vile Ufu. 14:8; 16:19; 17:5; 18:2,10,21). Mfalme ni aina ya uongozi ulio dharimu. Kufuatia uovu wa viongozi wa kidunia katika Agano la Kale kunasimama miungu ya mataifa yao (kama vile Dan. 10:13,20). Kutoka kwenye agano Jipyta tunaelewa nguvu binafsi ya uovu ijulikanayo kama shetani. Ustawi kamili wa utambulisho katika aya hii kama shetani alivyokuwa yumkini alishawishiwa na

1. Jerome’s Vulgate akiutafasiri mst. 12 kama “Ibilisi”
2. Tertulian na Gregory the Great akihusianisha kifungu hiki na Luka 10:18
3. kifungu hiki kikitumika kama mazingira kote kwa Dante’s *Inferno* and Milton’s *Paradise Lost*

B. Angalia Mada Maalum ifuatayo

## MADA MAALUM: SHETANI

Hili ni suala gumu sana kutokana na sababu kadhaa.

1. Kitabu cha Agano la Kale hakimfunui adui mkuu apingaye mema, bali mtumishi wa YHWH (angalia. B. Davidson, *OT Theology*, kur. 300-306), ambaye anampa mwanadamu uchaguzi wa bure na pia kumlaumu mwanadamu juu ya kutokuwa kwake mwenye haki. Kuna Mungu mmoja pekee (angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu mmoja), nguvu moja, sababu moja iliyo ndani ya Agano la Kale—YHWH (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6).
2. Hii dhana ya huyu adui mkuu wa Mungu ilianza katika kipindi cha mwisho wa uandishi wa agano la kale na mwanzo wa uandishi wa agano jipya (pasipo sheria za kikanisa) chini ya ushawishi wa pande mbili za dini za Kiajemi (Dhana ya Zoroaster). Hii, katika kurudia, kwa kiwango kikubwa hizi ziliwashawishi viongozi wa dini za Kiyahudi na jamii ya Essene (yaani, Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi).
3. Kitabu cha Agano Jipya kiliikuza dhana ya Agano la Kale katika namna ya ugumu wa kushangaza, lakini wa kipekee, wa aina nyingi.

Ikiwa moja ya mitazamo ya somo la uovu kutokana na kipengele cha thiolojia ya kibiblia (kila kitabu au mwandishi au aina ya somo lililofundishwa na maeleo ya kimuhtasari yaliotengwa), tena ni mawazo tofauti sana ya uovu unaofunuliwa. Ikiwa, kwa vyo vyote, moja ya mitazamo ya somo la uovu kutoka kwenye mtazamo usio wa kibiblia au mtazamo wa ziada wa kibiblia wa dini za ulimwengu au dini za mashariki, tena maendeleo mengi ya kitabu cha Agano Jipya yanatabiriwa katika ule muunganiko wa Waajemi na dhana ya kiroho ya utawala wa Wagiriki-Waroma.

Ikiwa wazo la awali lilijikita juu ya Andiko la mamlaka ya Kiungu (kama Mimi Niko!), kisha ukuaji wa kitabu cha Agano Jipya lazima uonekane kama ufunuo endelevu. Yawapasa Wakristo kujilinda dhidi ya kuyaruhusu mafunzo ya mila na desturi za Kiyahudi au fasihi ya mashariki (Dante, Milton) kwa ajili ya ushawishi wa dhana ya baadaye. Kuna siri fulani na utata katika eneo hili la ufunuo. Mungu amechagua kutovifunua vipengele vyote vya uovu, chimbuko lake (angalia Mada Maalum: Ibilisi), uendelevu wake, sababu yake, lakini Yeye amelifunua ondoleo lake!

Katika neno la Agano la Kale neno "shetani" au "mshtaki" (BDB 966, KB 1317) linaweza kuhusiana na makundi matatu yaliyojitenga.

1. washtaki wa mwanadamu (kama vile 1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14,23,25; Zab. 109:6)
2. washtaki wa kimalaika (kama vile Hes. 22:22-23; Ayubu 1-2; Zek. 3:1)
3. washtaki wa kimapepo (kama vile 1 Nyak. 21:1; 1 Fal. 22:21; Zek. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha ukimya wa Agano la Kale na Agano Jipya ndipo yule joka wa Mwanzo 3 alipotambujishwa kama Shetani (kama vile Kitabu cha Hekima 2.23-24; II Enoch 31:3), na baadaye hili liliuja kuwa uchaguzi wa sheria za Kiyahudi. Sot 9b na Sanh. 29a). Wale "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 walikuja kuwa malaika katika I Enoch 54:6. Nalitaja hili, si usahihi wa kithiolojia, bali hili linaonyesha maendeleo yake. Katika Agano Jipya kazi hizi za Agano la Kale zilitambuliwa kuwa ni za kimalaika, uovu wa kibinadamu (kama vile 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9). Chimbuko la uovu wa kibinadamu ni gumi au haliwezekani (linategemeana na hoja ya mtazamo wako) kuibainisha kutokana na Agano la Kale. Moja ya sababu ya hili ni kuwepo kwa imani ya Mungu mmoja mwenye nguvu kwa Israeli (angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu Mmoja;pia nukuu 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Usababishi wote (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6) alipewa YHWH ili kuonyesha upkee na ubora Wake (kama vile Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Chimbuko la uhakika wa habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo Shetani ni mmoja wa "wana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14 na Ezekiel 28, ambapo wafalme wenyewe majivuno waliokuwa karibu na mashariki (Babeli na Tiro) kwa hakika wanatumika kueleza juu ya majivuno ya Shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganywa kihisia kuhusu mtazamo huu. Ezekieli anatumia stiari za Bustani ya Edeni, si kwa mfalme wa Tiro pekee kama Shetani (kama vile Eze. 28:12-16), bali pia kwa mfalme wa Misri kama Mt. wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (Ezekiel 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa mist. ya. 12-14, inaonekana kuufafanua uasi wa kimalaika kupitia majivuno. Ikiwa Mungu alitaka kuifunua kwetu ile asili ya kipekee na chimbuko la Shetani, hii ni njia isiyo ya wazi na ni sehemu ya

kulifanya hili. Yatupasa kujilinda dhidi ya uelekeo wa theolojia yenyewe mfululizo wa kuchukulia mambo madogo madogo, sehemu za utata wa semi mbalimbali, waandishi, vitabu, aina na kuziunganisha kama vipande vya mafumbo ya Uungu.

Nakubaliana na Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzu. 2, viambaisho XIII [kr. 748-763] na XVI [kr. 770-776]) kwamba Sheria za Dini ya Kiyahudi kwa kiasi kikubwa zimepewa ushawishi na zile pande mbili za Kiajemi na kisio la kimapepo. Hawa Walimu wa sheria za Kiyahudi si chimbuko zuri la ukweli ndani ya eneo hili. Kimsingi Yesu anaachana na mafundisho ya Masinagogi ndani ya eneo hili. Nafikiri kwamba ile dhana ya adui wa YHWH aliyejikuwa katika umbo la kimalaika iliendelezwa kutokana na miungu mikuu miwili ya pande mbili za ki-Irani, Ahkiman na Ormaza, ambapo iliendelezwa tena na Walimu wa Sheria katika pande mbili za YHWH na Shetani.

Kuna uhakika wa ufunuo endelevu katika kitabu cha Agano Jipywa kama uainishaji wa uovo, lakini si kama wanavyoeleza Walimu wa Sheria za Kiyahudi. Mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita ya mbinguni." Anguko la Shetani kimantiki lina umuhimu, lakini maelezo yake hayakutolewa (angalia Mada Maalum: Anguko la Shetani na Malaika Zake). Hata kile kilichotolewa kinafunkwa katika aina ya kiyama (kama vile Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa Shetani anaondolea kwa Yesu na kutupwa duniani, bado anafanya kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Katika eneo hili yatupasa kuzuia udadisi wetu. Kuna nguvu binafsi ya ushawishi na uovo, lakini bado kuna Mungu mmoja pekee na bado tunawajibika kwa ajili ya chaguzi zetu. Kuna mapambano ya kiroho, wakati wote kabla na baada ya wokovu. Ushindi unaweza kuja tu na kubaki pale pale kupitia Mungu wa Utatu. Uovo emeshindwa na utaondoshwa kama vile Ufu. 20:10)!

- C. Binafsi sijisikii kuitumia Isaya 14 na Ezekiel 28 kama maandiko ya Biblia kwa ajili ya asili na mwisho wa mjaribu wa kimalaika. Nafikiri udadisi wetu unatupeleka kutumia muktadha huu isivyostahili. Biblia imenyamaza juu ya mambo mengi ambayo tunataka kuyajua. Thiolojia iliyopangiliwa lazima ianze na ufanuzi! Kwa namna mbalimbali ulimwengu wa kiroho kwa makusudi kabisa umezingirwa.
- D. Kwa ajili ya muktadha wenge kufanana angalia Ezekiel 28 kwenye mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org), "Old Testament Studies," fasihi zilizoandikwa.
- E. The Jewish Study Bible (uk. 812) inazungumzia juu ya shairi "linaelezea kifo cha aibu cha mtawala wa Ashuru kipindi cha Isaya, yumkini Sargon II, ambaye aliuawa kwenye vita katika mwaka wa 705. Iliku baadaye kutafasiliwa upya kama utabiri wa kifo cha utawala wa Babeli." Nafikiria Isaya (au mwanafunzi wake) angweza kutumia shairi la mwanzo, au kwa wastani mchoro, kuelezea majisifu ya wafalme wa Mashariki amba waliangamizwa na YHWH.
- F. Haiwezekani kuendana pamoja madokezo yote ya kihistoria katika unabii huu. Kumbuka unabii wa Kiebrania ni "kielekezi" cha kihistoria, na sio mwongozo wenge maelezo ya kina. Watu wa Magharibi wanaelewa visivyo juu ya mchoro, utata, na utiaji chumvi! Angalia D. Brent Sandy, Plowshares and Pruning Hooks: *Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:1-2

<sup>1</sup> Maana Bwana atamhurumia Yakobo, atamchagua Israeli tena, naye atawaweka katika nchi yao wenyewe; na mgeni atajiunga nao, nao wataambatana na nyumba ya Yakobo. <sup>2</sup> Na hao mataifa watawatwaa na kuwaleta mpaka mahali pao wenyewe, na nyumba ya Israeli watawamiliki, na kuwafanya watumishi na wajakazi katika nchi ya Bwana; nao watawachukua hali ya kufungwa watu wale waliowafunga wao, nao watawamiliki watu wale waliowaonea.

**14:1 "Bwana atawahurumia"** KITENZI hiki (BDB 933, KB 1216, *Piel KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU*, kama vile 49:13, 15; 54:7-8) kinaonyesha uhusiano maalumu wa YHWH na watu wake wa agano (kama vile Hosea 1-2), kama

lifanyavyo neno “chagua” (BDB 103, KB 119, Qal KAULI TIMILIFU kama vile 41:8,9; 44:1; 49:7). katika 9:17 Mungu wa Israeli hataona huruma juu ya watu wake wa agano (kama vile Hosea 1-3;) na katika 13:18 Wamedi hawatakuwa na huruma juu ya Babeli, lakini YHWH tena ataurejesha uhusiano wake wa kipekee na uzao wa Ibrahim! Baada ya YHWH kutumia nguvu ya Mesopotamia kuwaadhibu watu wake wa agano kwa kutokutii, ataanzisha “safari mpya” na “ushindi mpya”!

▣“**Yacob. . .Israeli**” Maneno haya mawili yangaliweza kutumika kwa ajili ya makabila kumi ya Kaskazini na makabila mawili ya kusini yakionyesha kuungana tena.

**14:1-2 “na mgeni atajiunga nao, nao wataambatana na nyumba ya Yakobo”** Kuna namna mbili ya kuitafasiri mistari ya 1-2: (1) ikiwa mstari wa 1 na 2 vinaendana na kuelezea kikundi kile kile (yaani., wageni. . . watu) au (2) mstari wa 1 unaelezea Baraka za wasio Wayahudi (yaani., wageni) na mst. 2 unaelezea maadui wa Israeli walioshindwa kuwa wapagazi wao. Ni vigumu katika Isaya na Mika kuweka ulinganifu wa matendo na mtazamo wa YHWH kwa mataifa.

1. Anawapenda na kuwajumuisha ndani ya watu wa Agano (kama vile 2:2-4; 11:10, angalia Mada Maalum katika 1:3)
2. Huwahukumu na kuwaweka katika utumwa (yaani., 60:10; 61:5)

Kwa kiasi fulani yote ni kweli! Nabii anarudi nyuma na kwenda mbele, mara nyingi katika muktadha ule ule, kati ya hizi ncha mbili. Chaguo #1 linaaksi Mwanzo 1-3; 12, wakati chaguo #2 linaaksi historia ya Israeli huko Kanaani.

Katika Isaya tunayaona mataifa yakiwarejesha watu wa agano katika nchi zao (yaani., Kanaani) na kuwa wamoja katika kumwabudu YHWH (kama vile 49:22; 60:4-9,10-14; 66:20). Hili laweza kuaksi “safari mpya ya kuhama.” Wengi wa wageni waliondoka Misri wakiwa na Waisraeli na wengi wakaungana nao njiani (kipindi cha kutangatanga nyikani na ushindi). Yawezekana picha ya mst. 2 inaliaksi hili. Kama ndivyo, ingalitatta tatizo la #2 hapo juu.

**14:3** Kuna “dhima ilioikinyume” kati ya mst. 2 (utumwa wa maadui wa Israeli) na mst. 3 (utumwa wa Israeli, ambao sasa umekwisha). Mkakati wa “dhima iliyokinyume” ni wa kawaida katika Agano la Kale. YHWH anatenda kwa namna isiotarajiwa kuthibitisha chaguo la uzao wa Ibrahim (kama vile Mwanzo 12, 15, 17). Kusudi la uangalizi wake maalumu sio la kiupendeleo, bali mpango wake wa ukombozi wa milele (kama vile Mwa. 3:15; 12:3) kwa wanadamu wote walioumbwa kwa mfano wake (kama vile Mwa. 1:26-27).

Kama ilivyo mara nyingi katika Isaya, kuna mtazamo wa muda mfupi na mtazamo wa muda mrefu. Nabii anayagawa haya katika Nyanja mbili. Mfano mzuri wawezakuwa katika sura ya 13, ambapo hukumu ya Babeli na Babeli ya kale imegawanywa

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:3-27

<sup>3</sup> Tena itakuwa katika siku ile, ambayo Bwana atakupa raha baada ya huzuni yako, na baada ya taabu yako, na baada ya utumishi ule mgumu uliotumikishwa;

<sup>4</sup> utatunga mithali hii juu ya mfalme wa Babeli, na kusema,

Jinsi alivyokoma mwenye kuonea;

Jinsi alivyokoma mji ule wenye jeuri!

<sup>5</sup> Bwana amelivunja gongo la wabaya,

Fimbo ya enzi yao wenye kutawala.

<sup>6</sup> Yeye aliywapiga mataifa kwa ghadhabu,

Kwa mapigo yasiyokoma; Aliywatawala mataifa kwa hasira,

Ameadhibiwa asizue mtu.

<sup>7</sup> Dunia yote inastarehe na kutulia;

Hata huanzilisha kuimba.

<sup>8</sup> Naam, misunobari inakufurahia,

Na mierezi ya Lebanon, ikisema,

Tokea wakati ulipolazwa chini wewe,

Hapana mkata miti aliyetujia.

<sup>9</sup> Kuzimu chini kumetaharuki kwa ajili yako,

Ili kukulaki utakapokuja;

Huwaamsha waliokufa kwa ajili yako,

Naam, walio wakuu wote wa dunia;

Huwainua wafalme wote wa mataifa,

Watoke katika viti vyao nya enzi.

<sup>10</sup> Hao wote watajibu na kukuambia,

Je! Wewe nawe umekuwa dhaifu kama sisi!

Wewe nawe umekuwa kama sisi!

<sup>11</sup> Fahari yako imeshushwa hata kuzimu,

Na sauti ya vinanda vyako; Funza wametandazwa chini yako,

Na vidudu vinakufunika.

<sup>12</sup> Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni,

Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi!

Jinsi ulivyokatwa kabisa,

Ewe uliyewaangusha mataifa!

<sup>13</sup> Nawe ulisema moyoni mwako,

Nitapanda mpaka mbinguni,

Nitakiinua kitu changu juu kuliko nyota za Mungu;

Nami nitaketi juu ya mlima wa mikutano,

Katika pande za mwisho za kaskazini.

<sup>14</sup> Nitapaa kupita vimo nya mawingu,

Nitafanana na ye ye Aliye juu.

<sup>15</sup> Lakini utashushwa mpaka kuzimu;

Mpaka pande za mwisho za shimo.

<sup>16</sup> Wao wakuonao watakukazia macho,

Watakuangalia sana, wakisema, Je!

Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia,

Huyu ndiye aliyetikisa falme;

<sup>17</sup> Aliyeufanya ulimwengu ukiwa,

akaipindua miji yake;

Asiyewafungua wafungwa wake waende kwao?

<sup>18</sup> Wafalme wote wa mataifa wamezikwa wote kwa heshima,

Kila mmoja ndani ya nyumba yake mwenyewe;

<sup>19</sup> Bali wewe umetupwa mbali na kaburi lako,

Kama chipukizi lililochukiza kabisa;

Kama vazi la wale waliouawa,

Wale waliochomwa kwa upanga,

Wale washukao mpaka misingi ya shimo;

Kama mzoga uliokanyagwa chini ya miguu.

<sup>20</sup> Hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi,

Kwa maana umeiharibu nchi yako,

Umewaua watu wako;

Kizazi chao watendao uovu hakitatajwa milele:

<sup>21</sup> Fanyeni tayari machinjo kwa watoto wake.

Kwa sababu ya uovu wa baba zao;

Wasije wakainuka na kuitamalaki nchi,

Na kuujaza miji uso wa ulimwengu.

<sup>22</sup> Nami nitainuka, nishindane nao; asema Bwana wa majeshi; na katika Babeli nitang'oa jina na mabaki,

mwana na mjukuu; asema Bwana. <sup>23</sup> Tena nitaifanya hiyo nchi kuwa makao ya nungu, na maziwa ya maji;

nami nitaifagilia mbali kwa ufagio wa uharibifu; asema Bwana wa majeshi. <sup>24</sup> Bwana wa majeshi ameapa,

akisema, Hakika yangu kama vile vilivyoazimia, ndivyo itakavyokuwa; na kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyotokea;<sup>25</sup> kwamba nitamvunja huyo Mwashuri vipande vipande katika nchi yangu, na juu ya mlima wangu nitamkanya chini ya miguu yangu; ndipo nira yake ilio juu yao itakapoondoka, na mzigo wake utatoka mabegani mwao.<sup>26</sup> Hilo ndilo kusudi liliokusudiwa duniani mwote, na huo ndio mkono ulionyoshwa juu ya mataifa yote.<sup>27</sup> Maana Bwana wa majeshi amekusudia, naye ni nani atakayelibatili? Na mkono wake ulionyoshwa, ni nani atakayeugeuza nyuma?

**14:4 “mithali”** Hili ni neno la hekima la Kiebrania *mashal* (BDB 605), ambalo mara kwa mara linatafasiliwa kwa maana ya “mithali.” Hata hivyo, muundo wa kishairi wa mistari ya 3-21 upo katika kiashirio cha nyimbo za huzuni (yaani., sura 47 na maombolezo).

▣ **“dhidi ya mfalme wa Babeli”** Sura ya cheo hiki haijilikani. Tafadhari soma “tambuzi za kimuktadha,” C, aya ya pili sura ya 13. Tambua namna katika sura ya 14:24, pasipo kanuni yeyote ya “ufunuo”, Ashuru inaelezewa moja kwa moja. Baada ya kuanguka kwa mji wa Babeli mikononi mwa Ashuru katika mwaka wa 689 K.K, wafalme wa Ashuru walichukua vyeo vingine vya ukuu wa “mfalme wa Babeli.”

▣	
NASB	“hasira yake ilivyokoma”
NKJV	“mji wenye jeuri ulivyokoma”
NRSV	“jinsi jeuri yake ilivyokoma”
NJB	“namna majivuno yake yaliviyokoma”
LXX	“ubwana wako utakoma”

Andiko la Kimasoreti lina neno מִדְבָּר, lakini hili linatumika hapa tu katika Agano la Kale. Kama herufi ת (d) itabadilika kuwa ג (r), kama hati ya Isaya katika magombo ya Bahari ya Chumvi, hivyo מִרְחַבָּה (BDB 923) linakuwa ni “kiburi” au “jeuri.” Andiko la Kiebrania la toleo la UBS linaupatia usomaji huu alama “C” (yaani pasipo shaka).

Toleo la NKJV linafuatisha uwezekano wa mzizi wa neno la Kiarama ambao unarejerea kwenye dhahabu. Hakuna tafasiri nyingine iliyo kuu iliyo fuatisha mwongozo wake.

**14:5 “Bwana amelivunja”** YHWH ni mdhibiti nyuma ya historia ya mwanadamu (kama vile mst. 22-23,24). Anawezakuwa haonekani kwa wale wasio na imani, lakini anaelekeza habari kwa ajili ya ujio wa Masihi (ujio wa mara ya kwanza) na utimilizaji wa zama za haki (ujio wa mara ya pili). Angalia Mada Maalum katika 1:3.

▣ Gongo (BDB 641) na fimbo ya kifalme (BDB 986) zilikuwa ni ishara za uweza wa kifalme (kama vile mst. 6). Zilitumika kwa matumizi ya YHWH juu ya Ashuru katika 10:5.

**14:7 “Dunia yote itastarehe na kutulia”** Neno “kutulia” (BDB 628, KB 679, *Qal KAULI TIMILIFU*) linarejerea kipindi cha utulivu tokea kuvamiwa. KITENZI kile kile kinatumika katika mst. 3 (*Hiphil KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO*) kurejerea kwenye utulivu/amani ya watu wa agano. Hapa kinarejerea Mashariki karibu ya Kale yote (yaani., “dunia nzima”).

Kuanguka kwa tawala za Mesopotamia kulisababisha pumziko, utulivu, na furaha Mashariki karibu ya Kale yote. Mnyanyasaji ameangushwa (kama vile mst. 8).

▣ **“walipiga kelele za shangwe kwa kuimba”** Isaya anaongelea mara nyingi juu ya furaha ya kukombolewa (kama vile 44:23; 49:13; 52:9; 54:1). Hapa, ina viashiria vya furaha ya matukio siku ya hukumu (yaani., “dunia yote”). Mapenzi ya YHWH kwa mwanadamu yalikuwa ni pumziko, amani, utele, na furaha (kama vile Mwanzo 1-2)!

**14:8 “hakuna mkata miti aliyetujia”** Hili laweza kumaanisha vitu vitatu.

1. Babeli waliagiza miti mingi kwa ajili ya miradi yao ya ujenzi (maana iliyo wazi)
2. Adui hatakata miti kwa ajili ya kuzingira vifaa vyao (maana iliyo wazi)
3. Nchi itastawi kwa amani (kiashirio)

**14:9 “Kuzimu”** Kuzimu kunaainishwa kama sehemu ya maandalizi kwa ajili ya wafalme walio angushwa. Inarejere (BDB 982) sehemu inayowatunza waliokufa. Katika agano la Kale maisha baada ya kufa yameelezewa kama kuishi nafsini, lakini pasipo na furaha; watu wanakuwa kivuri tu cha uhalisia wao wakilazimika kuwa sawa katika utulivu (kama vile mistari ya. 10-11, Ayubu 3:17-19; 10:21-22; 21:23-26). Angalia Mada Maalum: Wafu Wako Wapi? Katika

5:14.



<b>NASB</b>	<b>“roho za waliokufa”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“waliokufa”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“vivuli vya waliokufa”</b>
<b>TEV, NJB</b>	<b>“roho”</b>
<b>LXX</b>	<b>“mwenye uwezo”</b>
<b>REB</b>	<b>“waliokufa kale”</b>

Neno (BDB 952 I, kama vile 26:19) linatumika kwa namna ya ushairi kwa ajili ya

1. Wafalme waliokufa, TEV, NJB
2. Wapiganaji waliokufa, LXX
3. Mababu waliokufa, REB
4. Wafu wote kwa ujumla, NASB, NKJV

Katika maandiko ya kihistoria yanarejere kwa Rephaim, kundi la binadamu lenye kuhusiana na majitu.

## **MADA MAALUM: MANENO YALIYOTUMIKA KWA MASHUJAA WENYE NGUVU AU MAKUNDI YA WATU**

Watu hawa wakubwa/warefu/wenye nguvu wanaitwa kwa majina mbali mbali

1. *Wanefili* (majitu, BDB 658, KB 709) - Mwa. 6:4; (angalia Mada Maalum: Wana wa Mungu katika Mwanzo 6; Hes. 13:33)
2. *Warefai* (huenda BDB 952 II, KB 1274) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:11,20; 3:11,13; Yosh. 12:4; 13:12; II Sam. 21:16,18,20,22; I Nya. 20:4,6,8
3. *Wazuzi* (BDB 273), *Wazuzi* (BDB 265) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:20
4. *Waemi* (BDB 34) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:10-11
5. *Wana wa Anaki* (wana wa Anaki, BDB 778 I) - Hes. 13:33; Kumb. 1:28; 2:10-11,21; 9:2; Yosh. 11:21-22; 14:12,15; 15:14; Amu. 1:20

Angalia namna Mwanzo 14:5 ilivyotaja wanaume watatu wakubwa wa haya makundi (kama vile LXX, Vulgate).

Neno *Warefai* pia linatumika kwa viumbe walioko kule kwenye shimo *sheol* (kama vile Ayubu 26:5; Zab. 88:10-11; Isa. 26:14,19).



<b>NASB, NRSV</b>	<b>“wakuu wote wa dunia”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“mtemi wa dunia”</b>
<b>TEV</b>	<b>“wale wote wenye nguvu”</b>
<b>NJB</b>	<b>“watawala wa dunia”</b>

Kwa maana iliyo wazi ni “kondoo dume” (BDB 800, kama vile Ezek. 34:17). Linarejere kiongozi wa kundi na kiistiani kwenye jamii ya watu.

**14:11** mistari miwili ya kwanzainaonyesha utele na maisha ya uharibifu ya wafalme wa Mashariki. Walijilaza juu ya mito na kulala kwenye vitanda laini.

Mistari miwili ya mwisho inaelezea kitanda kipyä cha wafalme huko kuzimu/kaburini (yaani funza). Hata watawala walijiona wao kama miungu mtu, siku moja watalala katika kitannda funza! Kifo ni mlinganganishaji wa wanadamu wote (kama vile 5:14). Ni utofauti ulioje!

▣ “**funza**” Hapa kwa maana iliyo wazi inatumika kama lahaja kwa ajili ya kifo na kiistiai hofu ya kifo na maisha ya muda tu ya mwanadamu.

**14:12 “jinsi ulivyoanguka toka mbinguni”** Kitenzi (BDB 656, KB 709, *Qal KAULI TIMILIFU*) kinaonyesha hali ya kutulia. Swali ni kwamba, “ni maana ya wazi au isio ya wazi?” KITENZI kinatumika kwa ajili ya kifo cha vurugu (BDB 657, mst. 2a). Isaya anakitumia katika 3:8; 8:15 kwa ajili ya kuuangamiza mji. Lakini kifungu kilichoongeza, “toka mbinguni,” ni kile kinachosababisha watoa maoni kudai kuwa ni viumbe wa kimalaika, vile vile maneno yenye kufanana na ya Yesu katika Luka 10:18.

▣	
NASB	“nyota ya alfajiri”
NKJV, Vulgate	“Ibilisi”
NRSV	“nyota ya adhuhuri”
TEV	“nyota ing’ayo asubuhi”
NJB, LXX	“nyota ya adhuhuri”
REB	“nyota ing’ayo asubuhi”

Neno la Kiebrania KIIMA JINSI YA KIUME ni הילל (BDB 237, KB 245). Muundo huu unapatikana hapa tu katika agano la Kale. Mzizi wa KIMANENO, הַלְלָה wawezza kumaanisha

1. “kung’aa,” yumkini ikirejerea kwenye mwandamo wa mwezi
2. “kujisifu” au “kusifu,” ambapo tunapata maombi ya kiliturujia (yaani., zaburi ya kusifu

Toleo la KB linataja chaguzi mbali mbali kama ilivyo mwanzo wa mzizi wa neno.

1. Kutokana na mzizi wa lugha ya Ugariti, *hll*
2. Kutokana na mzizi wa Kiarabu, hilali ya mwezi mwandamo
3. Kutokana na mzizi wa Kiebrania, haijulikani, lakini yumkini inarejerea nyota ya alfajiri (“mwana wa machweo”)
4. Kutokana na Kilatini, Ibilisi anarejerewa kama nyota ya alfajiri (yaani., hasa “mtoa nuru”)

Hoja nzima ya jina ni kuwa huu mwanga wa mbinguni kwa haraka unafunikwa na mwanga wa asubuhi. Mwangaza wake unakuwa wa muda mfupi! Kuna mwanga bora, mpya, na wa kung’aa unakuja!

▣ “**wewe**” Mistari miwili inayofuata baada ya mst. 12 dhahili unarejerea kwa mfalme wa kidunia wa Ashuru au Babeli (kama vile mistari ya 16-17). Picha ya shairi (mistari ya 4-21) imechukuliwa toka kwa hadithi za kubuni za Wakanaani (hasa. Mistari ya 13-14), zinazojulikana kwenye mabamba ya Ras Shamra yakiandikwa tokea karne ya kumi na tano yaliyopatikana katika mji wa Ugariti.

Neno “nyota ya alfajiri” (*Hehal*) na “machweo” (*Shabar*) yote ni majina ya miungu katika hadithi za kubuni za Wakanaani, kama ilivyo milima ya miungu huko kaskazini (Mlima Zaphon, kama vile Zab. 48:2). Pia cheo cha uungu, “Yeye aliye Juu,” ni cha kawaida katika shairi za lugha za Ugariti na inarejerea kwa *Ba’al Shamim* (“Bwana wa mbingu”). Ushairi wa kubuniwa wa Wakanaani juu ya nyota ya alfajiri, mungu mdogo, anajaribu kujimilikisha mamlaka, lakini alishindwa. Hili ni kinyume cha picha aliyonayo

Isaya juu ya jeuri za watawala wa Mashariki.

Maelezo haya kuhusu kiburi, majivuno ya mfalme wa Mashariki ya karibu yanaendelezwa toka mistari ya 8-11. Mst. wa 12, uliochukuliwa kwa maana iliyo wazi kufuatana na toleo la Vulgate, ukosefu wa maarifa ya fasifi ya Ugariti yaweza kuutumia huu muktadha kama wenye kurejerea uasi wa kiongozi wa kimalaika. Angalia Tambuzi za Muktadha, B.

**14:13-14** Aya hizi mbili zinaonyesha majivuno na kiburi cha wafalme wa Mashariki Karibu ya mbali.

1. “Nitapanda mpaka. . .,” BDB 748, KB 828, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU*
2. “nitakiinua kiti changu. . .,” BDB 926, KB 1202, *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU*
3. “nitaketi juu ya. . .,” BDB 442, KB 444, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU*
4. “nitapaa mpaka...,” KITENZI kile kile kama cha #1
5. “nitafanana na aliye. . .,” BDB 197, KB 225, *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU*

Majivuno na kiburi ndicho kiini cha roho ya mwanadamu aliyeanguka. YHWH kipekee kabisa anawahukumu binadamu wenyewe kujifanya miungu!

**14:13 “nyota za Mungu”** Cheo kwa ajili ya Uungu ni *EI, לְא* (BDB 42), ambacho kilikuwa ni cha kawaida kwenye usanifishaji wa uungu kote Mashariki Karibu ya Kale. Hili, pia, lingaliweza kuaksi hadithi za kubuniwa za Wakanaani Toka Ugariti. Nyota zilikuwa zikitazamwa kama malaika/miungu waliodhibiti hatma ya mwanadamu (yaani., kuabudu nyota kwa Wababeli toka Ziggurats). Huyu mtu alitaka kuwa na mamlaka juu ya dunia nzima.

▣“**Nami nitaketi juu ya mlima wa mukutano, Katika pande za mwisho za kaskazini**” Hii ni alama ya makazi ya Mungu (kama vile Zab. 48:2; Ezek. 28:14). Kitu cha kushangaza ni mahali penyewe “katika mwisho wa pande za kaskazini.” Mlima huu wa miungu huko pande za kaskazini ulikuwa ni sehemu ya hadithi za kubuni za Wakanaani, wenyewe kufanana na Mlima Olympus wa Wayunani.

**14:14 “yeye aliyejuu”** Cheo *Elyon, עליון* (BDB 751 II), kilitumiwa na Balaam katika kitabu cha Hes. 24:16 na kinafanana na *Shaddai* (yaani., Mwenyezi Mungu, BDB 994). Kilitumiwa na Musa katika wimbo wake kabla ya kufa katika Kumb.32:8, vile vile pia kama Daudi katika II Sam. 22:14 na Zaburi mbali mbali.

Pia kilitumika kwa bamba za Ras Shamra kwa ajili ya mungu wa Wakanaani.

**14:15** Badala ya kwenda mlimani pande za mwisho (BDB 438) za kaskazini, atakwenda chini (BDB 438), *kuzimu*. Neno *kuzimu* (BDB 982, angalia Mada Maalum katika 5:14) linafanana na neno “shimon” (BDB 92, kama vile Ezek.31:16), ambalo ni jina lingine kwa ajili ya kaburi (kama vile Mith. 28:17). Neno lile lile limetumika katika mst. 19 na linafanana na neno kaburi/mazikoni (kama vile mst. 18).

**14:16-19** Huu ni ubeti wa nne; unarejerea kwenye mshangao wa mashahidi huko *kuzimu* juu ya mwili wa mfalme wa Babeli aliyeureka. Unafanana na mistari ya 9-11.

**14:17** Hii aya inaonyesha kitendo cha kuwafukuza watu wajeuri wote wa Ashuru na Babeli. Hii namna ya udhibiti wa wingi wa watu uligeuzwa na Koreshi II (Umedi-Uajemi) katika mwaka wa 538 K.K.

**14:19 “kama chipukizi lililochukiza”** Hili neno lenye kufanana (BDB 666) limetumika katika 6:13 juu ya “mbegu takatifu ndiyo shina lake” na katika 11:1 ya shina la Yesu, ambayo yote yanarejerea kwa Masihi, mfalme wa kweli. Wafalme wa Mashariki Karibu ya Kale ni “tawi lililokataliwa”!

▣“**kama mzoga uliokanyagwa chini ya miguu**” Hili linazungumza kuhusu aibu ya maziko yasiyo sawa (yumkini rejeo kwa Sargon II). Sio tu kwamba mfalme alikosa kufanyiwa msiba wa kifalme, pia alikosa maziko vile vile! Neno “kukanyagwa” (BDB 100, KB 115, *Hophal HALI YA KUENDELEA*) pia limetumika katika mst. 25 (*Qal KAULI ISIO TIMILIFU*). Ilikuwa ni stiari ya hukumu ya YHWH (kama vile 63:6, *Qal KAULI ISIYO TIMILIFU* na 63:18, *Polel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*). Kitabu cha zaburi kinalitumia mara kwa mara kwa ajili ya ushindi wa watu wa agano juu ya adui kuititia uwezo na uwepo wa YHWH (kama vile Zab. 44:5; 60:12; 108:13). Watu wa agano wasiotii hukanyaga nchi ya Mungu (kama vile Yer. 12:10; *Polel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*).

**14:20** Sio tu mfalme jeuri atanyimwa maziko yaliyo mazuri, bali pia hata familia yake haitafanikiwa. Familia yake itakatiliwa mbali. Na hata nchi yake haitamkumbuka!

**14:21** Warithi wa mfalme watauawa kwa ajili ya dhambi za baba yao. Hii inaaksi Kut. 20:5. Mfalme na taifa lake lililo ovu hawataruhusiwa kustawi. YHWH anahitaji dunia ijazwe, lakini sio na watu wasio haki.

**14:22-23** Hili linaunda hitimisho ya lugha ya mjazo. Inanionyesha kwamba mst. 23 unashabihiana na 13:21-22, amba ni stiari kuelezea ukiwa wa hili taifa, mfalme, na mji wake.

**14:22 “mwana na mjukuu”** Haya maneno mawili (BDB 630 and 645) yanarejerea kwenye warithi.

1. kwanza, watoto waliopo
2. Pili , ukoo

Kupotea kwa warithi kulionekana kama aibu kubwa na laana (kama vile 47:9). Yaweza hata kufikirika kuathiri maisha ya mtu hata baada ya kufa.

**14:23 “name nitaifagilia mbali kwa ufagio wa uharibifu”** YHWH anafafanuliwa kama mwanamke/mtoto mwenye kuisafisha nyumba yake kwa kuifagia (BDB 370, KB 367, *Pilpel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*). Uchafu wote umeondolewa. Ni aina gani ya familia, lakini stiari ya familia yenye nguvu (ya kipekee kwa Isaya).

**14:24-27** Nyingi za tafasiri za Kiingereza zinatengeneza mabadiliko ya aya hapa. Lakini tambua hakuna watia alama za“ufunuo”, ambapo inadokeza kuwa sura ya 13:1-14:27 ni moja ya sehemu ya fasihi inayoshughulika na kuiangamiza Ashuru. Angalia Tambuzi za Kimuktadha, C.

**14:24** Aya hii inadai kuwa mapenzi ya Mungu yatatimia. Neno lake ni kweli (kama vile 46:11; 55:8-9; Ayubu 23:13; Zab. 33:9; Mdo. 4:28).

▣“**Bwana wa Majeshi ameapa**” Kwa uweza na mamlaka yake mwenyewe, YHWH anaelezea mipango na makusudi yake (kama vile 14:24; 45:23; 62:8; Kumb. 1:8,35; 2:14; 4:31; 6:10,18,23; Yer. 51:14; Amos 4:2; 8:7).

**14:25 “nitamvunja Mwashuru vipande vipande”**Hili laweza kurejerea tauni iliyoangamiza vikosi 185,000 vya Sennacherib katika usiku mmoja mbele ya malango ya Yerusalemu katika siku za Hezekia (kama vile II Fal. 18:13-19:37, hasa.19:35-37; II Mambo ya Nyakati 32).

▣“**ndipo nira yake iliyo juu yao itakapoondolewa**” Hili ni wazo lenye kujirudia (kama vile 9:4; 10:27). Nira, kama ilivyo “fimbo” au “ufito,” ilikuwa ni alama ya umiliki wa kigeni.

**14:26-27** Huyu mfalme wa Ashuru alikuwa na mpango wa kuitawala dunia (mst. 26), lakini YHWH alikuwa na mpango mwengine (kama vile 8:10), mpango wa kuukomboa ulimwengu (mst. 27)! Ashuru, Babeli, na Uajemi vilikuwa ni vyombo katika mpango wa YHWH na hakuna mtu awezae kuhimili mkono wake (yaani., mamlaka)

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:28-32**

<sup>28</sup> Ufunuo huu ulikuja mwaka ule alipokufa mfalme Ahazi.

<sup>29</sup> Usifurahi, Ee Ufilisti, pia wote,

Kwa sababu fimbo ile iliyokupiga imevunjika;

Maana katika shina la nyoka atatoka fira,

Na uzao wake ni joka la moto arukaye

<sup>30</sup> Nao walio maskini kabisa watakula,

Na wahitaji watajilaza salama;

Nami nitatia shina lako kwa njaa,

Na mabaki yako watauawa.

<sup>31</sup> Piga yowe, Ee lango; lia, Ee mji;

Ee Ufilisti, pia wote, umeyeyuka kabisa;

Maana moshi unakuja toka kaskazini,

Wala hakuna atakayechelewa katika majeshi yake.

<sup>32</sup> Wajumbe wa taifa hilo waletewe jibu gani?

Ya kuwa Bwana ameiweka misingi ya Sayuni,  
na ndani yake wale walioonewa katika watu wake wataona kimbilio.

**14:28** Tambua kuna “mafunuo” yalijotajwa katika 14:28-32 ambayo yanashughulika na hukumu ya YHWH juu ya Ufilisti (yaani., Wafilisti), lakini hili halihusiani na sehemu ya wimbo wenye kuelezea watu wa Ashuru katika mistari ya 24-27.

▣“mwaka ule alipokufa mfalme Ahazi” Katika orodha yangu ya Agano la Kale, “ya wafalme wa tawala zilizogawanyika” (kiambatisho cha nne, #3), wanazuoni watatu wanatoa mapendelekezo yao juu ya tarehe kwa ajili ya Ahazi.

1. John Bright, 735 - 715 K.K.
2. E. J. Young, 736 - 728 K.K.
3. R. K Harrison, 732/732 - 716/715 K.K.

Tarehe hizi (kutawala na kutawala kwa pamoja, sio muhimu kwa mauti yake) yangalifaa kwa ajili ya Wafalme wakorofsi wa Ashuru.

1. Tiglath-Pileser III, 745 – 727 K.K.
2. Shalmaneser V, 727 – 722 K.K.
3. Sargon II, 722 – 705 K.K.
4. Sennacherib, 705 – 681 K.K. (wapiganaji 185,000 waliuawa mbele ya ukuta wa Yerusalemu katika mwaka 701 K.K, kama vile Isaya 36-39; II Wafalme 18-19).

Namba 3, Sargon II, alikufa vitani mbali na nyumbani na hakushiriki katika kamjeni za kijeshi dhidi ya Ufilisti.

**14:29** Ufilisti inaanuriwa kutoshangilia (BDB 970, KB 1333, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa namna ya maana AMRISHI) kwa sababu ufalme wa uovu umeangushwa. Ukombozi wao wa muda mfupi hautadumu!

▣ Mistari miwili ya mwisho chini ya mst. 29 ni yenye utata na isiojulikana. Inaonekana kumaanisha kuwa mambo yataenda visivyo kutoka kwenye ubaya na kuwa mabaya zaidi. kifungu “joka arukaye” ni NOMINO ya neno “joka” (BDB 977 I, kama vile 30:6; Hes. 21:6) ukiongeza KAULI YENYE HALI YA KUENDELEA “arukaye” (BDB 733, KB 800, *Polel* KAULI YA HALI YA KUENDELEA), ambayo inaonyesha makuzi ya haraka (yaani., kugonga, kuteleza, kimbia kwa haraka).

**14:30** Mistari miwili ya kwanza inarejerea uangalizi wa Mungu kwa ajili ya

1. Watu wake wa agano (kama vile mst. 32) au
2. Wahitaji wa jamii ya Wafilisti

**14:31 “piga yowe, Ee lango; I;ia, Ewe mji”** Hizi KAULI SHURUTISHI mbili zina maneno

1. Piga yowe, BDB 410, KB 413, *Hiphil*
2. Iia, BDB 277, KB 277, *Qal*

Yakielezea juu ya kupigwa kwa miji mitano ya Wafilisti, kila moja ya mji ukiwa na mfalme wake.

▣“Umeyeyuka kabisa, Ewe Ufilisti, pia wote” KITENZI (BDB 556, KB 555, *Niphil* KITENZIJINA HALISI) kinaelezea juu ya hofu yenye kuogofya ambayo imeukamata umati wote (kama vile Kut. 15:15; Yosh. 2:9,24; I Sam. 14:16). Kumbuka kifungu hiki kinarejerea juu ya maangamizi ya jamii nzima (kama vile Yeremia 47 na Amos 1:6-8).

**14:31 “wala hakuna atakayechelewa katika majeshi yake”** Hii inaelezea juu ya uvamizi wa Mesopotamia mpya. Mmoja ameisha ondoka (kama vile mst. 29), lakini mwengine, Yule mbaya kuliko wote (kama vile mst. 29c,d), anakuja!

“**maana moshi unakuja toka Kaskazini**” Falme zenyе kustawi ziko Mashariki mwa Kanaani, lakini kwa sababu ya kuwepo jangwa kati yao na maadui zao, walitakiwa kuifuata njia itokayo kwenye vyanzo vya mto Frati na baadaye kuambaa na uwanda wa Pwani. Kwa hiyo, “kaskazini” pakajakuwa ni lahaja ya uvamizi, uovu, na maangamizi.

1. Hapa inarejerea Ashuru
2. Katika Yer. 4:6; 6:1,22; 10:22; 13:20; 15:12; 46:20,24; Ezek. 26:7 inarejerea Babeli Mpya

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je sura ya 13-14 inarejerea kwa Babeli au Ashuru?
2. Je sura za 13 na 14 zinazungumzia kuhusu mfalme Fulani wa kihistoria au cheo kilichotumika kama alama ya serikali wa watu wasiomjua Mungu?
3. Je sura ya 14 ni rejeo kwa shetani?
4. Je sura hii inataja mapepo au wanyama katika 13:21-22; 14:23?
5. Hitimisha ukweli wa kithiolojia kwa sentensi moja.
6. Ni kwa namna gani unabii umetumika katika Agano Jipya?

## ISAYA 15

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hukumu juu ya Moabu	Tangazo dhidi ya Moabu	Dhidi ya Moabu ( 15:1-16:14)	Mungu ataiharibu	Juu ya Moabu
15:1-9 (1-9)	15:1-4 (1-4)	15:1-9 (1-9)	15:1-9	15:1 (1)
15:2a-d				(2a-d)
				15:2e-3 (2e-3)
				15:4-5c (4-5c)
15:5-9 (5-9)				15:5d-f (5d-f)
				15:6 (6)
				15:7 ( 7)
				15:8 (8)
				15:9 (9)

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. xvi katika kipengele cha utangulizi)  
KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja na somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

Maeneo yaliyotajwa katika Sura ya 15-16

Isaya aliyafahamu sana maeneo ya kijiografia ya Kupitia Yordani (mashariki mwa Yordani)

A. Miji

1. Ari mst. wa 1
2. Kiri, mst. wa 1 (Kir-Haresethi, 16:7, 11)
3. Diboni mst. wa 2,9
4. Nebo, mst. wa 2
5. Medeba, mst. 2
6. Heshboni mst. 4; 16:9
7. Eleale, mst. wa 4; 16:4
8. Yahasa, mst. wa 4
9. Soari, mst. 5
10. Eglath-shelishia, mst. 5 (kifasihi. "Eglath ya Tatu," kama vile Yer. 48:24)
11. Luhithi, mst. 5
12. Horonaimu, mst. 5
13. Eglaimu, mst. 8
14. Beer-Elimu, mst. 8
15. Dimoni (DSS, "Diboni"), mst. 9
16. Sela 16:1
17. Kir-Heresethi, 16:7,11
18. Sibma, 16:8,9
19. Yezeri, 16:8,9
20. Adma (REB 15:9)?

B. vyanzo vya Maji

1. maji ya Nimrimu
2. kijito chenye mierebi (huenda ni "korongo lenye mipopula"), mst. 7
3. maji ya Dimoni, mst. 9
4. vivuko vya Arnoni, 16:2

C. Huku kuorodhesha miji hii iliyo mingi na vyanzo vya maji ni kwa ajili ya kutoa msistizo juu ya uharibifu.  
Kuna msafara wa wafanya biashara upande wa kusini au kuelekea Yuda (kama vile 16:1-4).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 15:1-9

<sup>1</sup> Ufunuo juu ya Moabu.

Maana katika usiku mmoja Ari wa Moabu umeharibiwa kabisa na kuangamizwa;  
maana katika usiku mmoja Kiri wa Moabu umeharibiwa kabisa na kuangamizwa.

<sup>2</sup> Wanapanda juu hata Bayithi na Diboni, mpaka mahali palipo juu ili walie;  
juu ya Nebo na juu ya Medeba Wamoabi wanalia;  
Wana upaa juu ya vichwa vyao vyote; kila ndevu zimenyolewa.

<sup>3</sup> Wanajivika nguo za magunia

katika njia kuu zao; juu ya dari zao, na katika mitaa yao,  
kila mtu analia, anamwaga machozi.

<sup>4</sup> Heshboni analia na Eleale;

mpaka Yahasa sauti ya kulia kwao inasikiwa;  
 hata watu wa Moabu waliovaa silaha wanapiga kelele sana kwa sababu hiyo;  
 nafsi yake inatetemeka ndani yake.  
<sup>5</sup> Moyo wangu unamlilia Moabu;  
 wakuu wake wanakimbilia Soari kama ndama wa miaka mitatu;  
 kwa maana wanapanda mbavu za Luhithi wakilia;  
 maana katika njia iendayo hata Horonaimu wanapaliza sauti ya kukata tamaa.  
<sup>6</sup> Kwa maana maji ya Nimrimu yamekuwa mahali palipoharibika,  
 kwa kuwa majani yamekauka, miche imenyauka, majani mabichi yamekoma.  
<sup>7</sup> Kwa hiyo vitu walivyojipatia tele, na akiba yao,  
 wanavichukua hata kijito cha mierebi.  
<sup>8</sup> Maana kilio hicho kimezunguka mipaka ya Moabu,  
 malalamiko yao yamefika hata Eglaimu, na malalamiko yao hata Beer-Elimu.  
<sup>9</sup> Maana maji ya Dimoni yamejaa damu;  
 maana ninaweka tayari msiba mpya juu ya Dimoni,  
 simba juu ya watu wa Moabu waliokimbia, na juu ya mabaki yao.

**15:1** Tambuaalama ya kimuktadha ya kifungu kipyta cha ono la Isaya “utabiri” (BDB 672 III) inayoonekana katika mst. wa 1. Agalia maelezo katika 13:1 (kama vile 14:28; 17:1; 19:1; 21:1,11,13; 22:1; 23:1; 30:6). Neno hili linadokeza ufunuo wa ki-Ungu.

▣ “Moabu” Huyu ni mmoja wa jamaa za Israeli na Lutu na mmoja wa binti zake wawili baada ya safari ya kutoka Sodoma (kama vile Mwanzo 19). Moabu, Amoni, na Edomu (yaani, mataifa ya ng'ambo ya Yordani) yanatajwa kwanza kama yenye kutoka kwa Yuda katika 11:14. Sura 15-16 zinaunda umaja wa kifasihi unaoshughulika na hukumu ya Moabu (kama vile Yeremia 48; Eze. 25:8-11; Amosi 2:1-3; Zef. 2:8-11). Moabu inatajwa mara nydingi katika Tarakimu kwa sababu ilimpasa Israeli kusafiri kupitia nchi yao ili aipate Kanaani. Musa alizikwa mahari pale (kama vile Kumbukumbu la Torati 34).

▣ “katika usiku mmoja” Kifungu hiki kinarudiwa mara mbili na kinatia mkazo juu ya uharaka na utimilifu wa ukumu ya miji ya Wamoabu inayokuja. VITENZI viwili “umeharibiwa” (BDB 994, KB 1418) na “kuangamizwa” (kifasihi, “kundoa,” BDB 198, KB 225) vyote ni vya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, pia ni vyenye kudokeza utimilifu wa uharibifu. Isaya alitumia KITENZI “kuangamizwa” ili kujieleza katika 6:5. Majeshi ya Ashuru yaliivamia Kanaani/Palestina mara kadhaa.

1. Sargoni wa II mnamo 71 K.K
2. Sargoni wa II mnamo 711 K.K
3. Senakeribu mnamo 701 K.

▣ “Ari” Hili neno (BDB 786 I) linaweza kurejelea mji (hili ni jina la jumla la mji katika lugha ya Moabu) ama eneo (yaani, Kumb. 2:9,29). Kwa kuwa jina Kiri (BDB 885 II) pia inamaanisha “ukuta” (kama vile LXX, yaani, mji uliozungushiwa ukuta) katika lugha ya Kiebrania, inawezekana kwamba miji ya Ari na Kiri inayarejelea makazi ya Moabu katika ufanano na mistarai ya kiushairi.

**15:2 “Diboni. . . Nebo. . . Medeba”** Pia kuna miji iliyoorodheshwa katika njia ya tarakimu katika uhusiano na Kipindi cha Kutanganga Nyikani kama ambavyo mwishoni Israeli alivyofika Kanaani kutoka upande wa mashariki mwa Bonde la ufa la mto Yordani.

**15:2-3 “analia. . . upaa. . . ndevu zimenyolewa. . . mwaga machozi. . . magunia. . . analia”** Haya yote yanarejelea taratibu za maombolezo za Mashariki ya Kale ya Karibu (kama vile 22:12; Ezra 9:3; Ayubu 1:20; Yer. 7:29; 16:6; 41:5; 47:5; 48:37; Eze. 7:18; 27:31; Mika 1:16). Watu wengi wanajaribu kuirudia miungu yao (kama vile mst. 2); wanajaribu kutubu na kuomba msaada, lakini hakuna msaada unaotolewa na sanamu hizi zisizo hai!

## MADA MAALUMU : IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvalaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19; Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Eze. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza , 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa), Yer. 48:37
13. Kunyoa ndevu, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani.

**15:4“Heshboni. . .Eleale. . .Yezeri”** Pia mijiiiliyo upande wa mashariki mwa Yordani, iliyokuwa karibu na ilitambulishwa na Moabu (ua Amoni, yaani, Mesha Stone, karne ya 9 K.K.).

▣**“analia”** Hiki ni KITENZI(BDB 277, KB 277, *Qal* cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ambacho kilitumika katika *Qal* muundo wa KAULI SHURUTISHI katika 14:31 (Filistia). Hapa kitenzi hiki kinachodokeza Moabu katika mst. 5 kinamdokeza YHWH au Isaya. Tambua matumizi yake katika Yer. 48:20,31.



**NASB** “*waliovaa silaha*”

**NKJV, Peshitta** “*wanajeshi wenye siraha*”

**NRSV, LXX,**

**JB** “*simba*”

**NJB** “*wapiganaji*”

**REB** “*wapiganaji shujaa*”

Tofauti kati ya wanajeshi na samba katika lugha ya Kiebrania ni matumizi ya msamiati, si mabadiliko ya kikonsonanti.

▣ **“nafsi yake inatetemeka ndani yake”** Hiki KITENZI (BDB 438, KB 440, *Qal* ya KAULI TIMILIFU) kinaonekana hapa. Kuna maneno kadhaa ya Kiebrania yaliyotafsiriwa “inatetemeka.” Haya yanadokeza kuogopa na kukosa ujasiri katika kuikabili hukumu ya Mungu. Haya yanabainisha “vita takatifu.” Moja linaweza kuchaguliwa kwa sababu za kiushairi ili lisikike kama KITENZI “kulia sana.”

**15:5-9** Toleo la Jewish Study Bible linaiona mistari hii kama yenye kuwarejelea Wamoabu wanoondoka Edomu (uk. 815). Hili linawezekana kwa sababu eneo hii miji linalotajwa hajulikani, japokuwa maeneo yote yako mashariki au mashariki mwa Mto Yordani.

**15:5“Moyo wangu unamlilia Moabu”** Hili neno “wangu” katika muktadha lazima linamrejelea YHWH Mwenyewe (kama vile mst. wa 9). Japokuwa inaweza kuwa nabii mwenyewe, kama vile 16:9,11. YHWH anavisikia vilio vya watu wa Moabu na kusimka. Bado wanaendelea kuipokea hukumu, lakini si kutoka kwa Mungu asieme waza, asijejali! Pia wamepewa msaada/ hifadhi ya bure katika 16:1-4. Ni jinsi andiko hili linastaajabisha! Toleo la Maandiko ya Kale ya Kiebrania linabadili marejeo haya kuwa “moyo wa eneo la Moabu unamlilia” (kama vile NJB).

□

NASB, NRSV,

TEV, NJB,

REB “Eglath-shelishia”

NKJV, LXX,

Peshitta “kama ng’ombe wa miaka mitatu ambaye hajazaaa”

Huu unaweza kuwa mji au kifungu (kama vile Yer. 48:34).

□“**wakimbizi wake**” Toleo la MT lina kifungu “ngozo zake” (BDB 138, בָּרִיחָה kutoka בְּרִיחָה), lakini tafsri zinabadili matamshi ya maneno kuwa “wakuu wake” kutoka מַבְרָה (BDB 138).

**15:6** Katika Agano la Kale Mungu anaitawala hali nya hewa (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-29). Anawajalia utele kwa sababu ya utii wa agano, lakini kwa kudumisha kilimo cha uzalishaji katika sura ya uovu, udharimu, na uasi. Moabu na vyote kuingiliwa na watu (kama vile mst. wa 9a) na upungufu wa chakula.

**15:7** Mji wa Moabu ulikuwa katika eneo kuu la misafara ya biashara kutoka Misri hadi Shamua. Mji huu ulilipwa kodi kutoka kwa makundi yote ya wafanya biashara na kuwa mji tajiri.

**15:9 “simba”** Huyu angeweza kuwa

1. sahihi, Mungu aliwatumia wanyama wa mwituni kutoa hukumu (yaani, I Fal. 13:24-28; II Fal. 17:25)
2. kama alama ya jeshi la Ashuru (kama vile 5:29; Yer. 50:17)
3. tamathali au ujio wa kutoka Yuda (kama vile 11:14, simba [mtawala] wa Yuda).

Toleo la JPSOA kwa maana iliyo dhahiri linaibadili tafsri ya mstari huu (hasa mistari 2-4) ili kuufanya kuwa himara (kama vile mst. ya 5, “wangu”).

“Kwa maana namimima nyongeza (maji) juu ya Dimoni.

Naigharikisha – kwa ajili ya wakimbizi wa Moabu – kwa mavumbi (tambibi, ‘machozi) kwa mabaki yake”

Toleo la LXX la mst. wa 9, mistari ya 2-4, pia ni tofauti sana, lakini kwa ujumla ni hasi.

“Kwa maana niwataleta Warabu juu ya Remnoni, na nitawaondoa watoto wa Moabu na Arieli na mabaki ya Adama.”

# ISAYA 16

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA				
NASB	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Unabii juu wa Kuharibiwa kwa Moabu 16:1-5 (1-5)	Moabu ikiharibiwa 16:1-5 (1-2) 16:3-5	Dhidi ya Moabu 16:1-4b (1-4b)	kupoteza tumaini kwa Moabu 16:1-2 16:3-4b 16:3-5 16:4c-5 4c-5	Ombi la Wamoabi 16:1-2 (1-2) (3-5)
16:6-12	16:6-7	16:6-7	16:6 16:7-12	16:6 (6) Maombolezo ya Moabu 16:7-12 (7-12)
	16:8-9 (8-9)	16:8-11 (8-11)		
	16:10-11 (10-11)			
	16:12 (12)	16:12		
16:13-14	16:13-14	16:13-14	16:13-14	16:13-14

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr.wa xvi katika sehemu ya utangulizi)

### KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 16:1-5

- <sup>1</sup> Pelekeni wana-kondoo, kodi yake aitawalaye nchi  
toka Sela kuelekea jangwani, mpaka mlima wa binti Sayuni.  
<sup>2</sup> Na binti za Moabu watakuwa kama ndege warukao huko na huko,  
kama kioto cha ndege walioitiwa hofu, kwenye vivuko vya Arnoni.  
<sup>3</sup> Lete shauri; kata neno;  
fanya kivuli chako kuwa kama usiku kati ya mchana;  
wafiche waliofukuzwa; usiwachongee walipotea.

<sup>4</sup> Watu wangu waliofukuzwa waache wakae pamoja nawe;  
katika habari za Moabu, uwe sitara kwake mbele ya uso wake anayeharibu;  
maana yeye atozaye kwa nguvu amekoma; afanyaye ukiwa ametoweka;  
waliokanya wa watu wametoka katika nchi.

<sup>5</sup> Na kiti cha enzi kitafanywa imara kwa rehemaa;  
na mmoja ataketi juu yake katika kweli,  
katika hema ya Daudi; akifanya hukumu,  
akitaka sana yaliyo haki, mwepesi wa kutenda haki.

## 16:1 Kuelekezwa kwa nani na kutoka kwa nani na kwanini maswali ya kimuktadha.

1. Wamoabu waliokimbia wanatuma zawadi ya kidhabihu kwa mtawala wa Kifalme wa Daudi katika Yerusalem ili kulinda msaada wake, TEV, NRSV
2. Ni rejea kwa Masihi, kama vile mstari wa 5; Peshitta, Vulgate
3. ujumbe wa hukumu inayoendelea na uharibifu hata kwa waliosalimika wa Moabu, kama vile mstari wa 1

▣ “**kutuma**” KITENZI (BDB 1018, KB 1511) ni *Qal KAULI SHURUTISHI*. Inaashiria kitendo cha kuweweseka na wasiwasi.

▣ “**kodi ya wana-kondoo**” Toleo la MT lina “wanakondoo” tu (BDB 503 III, WINGI, na kutaja “kama kodi”). Toleo la tu NASB ndilo linaloongeza KIVUMISHI kwenye tafsiri yake. Kama kwa ajili ya WINGI dhidi ya UMOJA:

1. WINGI, NRSV, REB, JB
2. UMOJA, MT, NJB, NASB, NKJV, TEV

Moabu ilikuwa inajulikana kwa kondoo wake (kama vile II Wafalme. 3:4).

Toleo la Kale lina fasiri tofauti tofauti.

1. LXX, “nitatuma kama vile wanyama watambaa juu ya ardhi!”
2. Peshitta, “ Nitatuma mwana wa mtawala wa ardhi.”
3. JPSOA, “Kumtoa mjumbe wa mtawala wa nchi.”

▣ “**Kutoka Sela**” Maana ya msingi ya neno (BDB 700) ni “jabali,” “jabali” (kama vile Yer. 51:25), lakini ilikuja kuashiria mji huko Edomu, Sela, au Petra (BDB 701 II, kama vile II Wafalme 14:7; Isa. 42:11). Hatahivyo, mji wa Sela haishabihiani na muktadha sawa sawa hivyo inaweza kuwa sifa zingine za mwamba karibu na mpaka wa Yudea. Inawezekana pia kuashiria njia ya kusini.

Ambapo sio muhimu kujua inatoka kwa nani na kuelekea kwa nani na kwa nini.

▣ “**kwenye mlima wa binti za Sayuni**” Hii ni njia yamafumbo ya kumaanisha hekelu la YHWH huko Yerusalem. Hii inamaanisha kwamba wanakondoo walitolewa dhabihu kwa YHWH (kama vile Ezra 7:17)

## 16:2 Moabu inaelezewa kama

1. ndege wapao, BDB 622 I, KB 672, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*
2. viota viliviyotawanywa, BDB 1018, KB 1511, *Pua/ ENDELEVU*

Anaendelea kutambuliwa kama “mabinti za Moabu,” lakini hii kama mstari wa 14, inamaanisha kwa wakazi wote wa nchi waliosalia hai.

▣ “**kwenye vivuko vya Arnoni**” Mto wa Arnoni (wadi El-Mujib) unatiririka katikati ya Bahari ya chumvi kuelekea upande wa Mashariki. Ulikuwa mpaka wa kijiografia kati ya mto Ammon upande wa kaskazini na Moab upande wa kusini (ukirefushwa zaidi kuelekea Zered Brook [yawezekana wadi El-Hesa]).

Inashangaza kwamba mawe haya ya kukanyagia (katika kivuko cha maji machache) hayako karibu ya mipaka ya Yuda, lakini karibu na Bahari ya chumvi. Yawezekana jeshi la Yudea lilikuwa limesogea kupitia Ammon kuelekea katika sehemu hizi za mawe ya kuvukia. Pia inawezekana kwamba tungo inaashiria kutoka upande wa kusini kwa mvamizi wa kaskazini.

**16:3-4** Mistari hii inatoa (1) ujumbe (KAULI SHURUTISHI inayotimika kama ombi) ambayo inafuatia na wanakondoo au (2) Maonyo ya Isaya kwa Wayudea kuwakubali Wamoabi. Nafikiria mbadala wa #1 ni bora zaidi.

1. “toa ushauri,” BDB 97, KB 112, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*, ikiandikwa kama WINGI WA JINSI YA KIUME, lakini ikitakiwa kusomwa kama UMOJA JINSI YA KIKE kukubaliana na “ushauri” (BDB 420), ambayo ni ya KIKE
2. “fanya uamuzi,” BDB 793, KB 889, *Qal KAULI SHURUTISHI*
3. “tupa kivuli chako,” BDB 1011, KB 1483, *Qal KAULI SHURUTISHI* (kama vile 25:4; 32:2; Zaburi 91:1)
4. “kuwaficha wageni wasiotakiwa,” BDB 711, KB 771, *Piel KAULI SHURUTISHI*
5. “usisaliti wakimbizi,” BDB 162, KB 191, *Piel KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika kama namna ya HALI YA KUSIHI
6. “waache wageni wakae pamoja na wewe,” BDB 157, KB 184, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU* ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI
7. “kuwa sehemu ya makimbilio kwa ajli yao,” BDB 217, KB 241, *Qal KAULI SHURUTISHI*

Ingawa Moabu alikuwa adui wa kijadi, kulikuwa na muunganiko wa karibu kwa nyumba ya Daudi (yaani Ruth; Sam. 22:3-5).

**16:3 “fanya kivuli chako kuwa kama usiku kati ya mchana”** Hii ni lugha ya kisitiari kwa ajili ya ulinzi. Inaweza kuwa rejea bayana kwa *Shekinah* wingu la utukufu ambalo liliwafuata waisraeli katika nchi hii hii wakati wa kipindi cha kutangatanga Jangwani. Ilikuwa ni kivuli cha wingu (kivuli na utulivu)wakati wa mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku. Iliwakilisha utoshelevu, ulinzi na uwepo binafsi wa YHWH.

**16:4** Kuna mfuatano wa masharti ya muda yanayohusiana na uvamizi wa Moabu baada ya mamlaka ya kiserikali ya Yudea yangepanuliwa katika eneo lote (kama vile mstari wa 5).

Haya hapa ni masharti .

1. mkandamizaji (BDB 568) amefikia mwisho wake (BDB 67, KB 79, *Qal KAULI ILIYO TIMILIFU*)
2. uharibifu (BDB 994, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*) umekoma (BDB 477 I, KB 476, *Qal KAULI TIMILIFU*)
3. wakandamizaji (BDB 942, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*) wamepotea kabisa juu ya nchi (BDB 1070, KB 1752, *Qal KAULI TIMILIFU*)

**16:5** Mstari huu unaelezea serikali ijayo kutokea Yudea (kama vile 9:6-7; 11:3-5).

1. enzi itaanishwa (KAULI TIMILIFU) katika wema (BDB 338, angalia Mada Maalum inayofuata
2. hakimu atakaa (KAULI TIMILIFU) juu yake katika uaminifu (BDB 54) katika hema ya Daudi
3. ataitafta haki ya kisheria (BDB 1048, kama vile 11:3,4)
4. ataiharakisha katika haki (“haki ya kimungu,” BDB 841, kama vile 11:4,5, angalia Mada Maalum katika 1:4; “kuharakisha,” BDB 555, siku zote ikimaanisha kuwa na ujuzi katika jambo fulani, hivyo kuwa na uwezo wa kulifanya kwa haraka. Hapa inashiria mtawala wa ufalme wa Daudi ambaye kwa haraka atatenda katika haki)

Huu mstari ni vile matoleo ya Peshitta na Vulgate yanautazama kama muktadha wa Kimasihi.

## MADA MAALUMU: WEMA (*HESED*)

Neno hili (BDB 338 I, KB 336 II) lina maeneo mapana ya maana.

- A. Lilitumika katika kuwaunganisha wanadamu
  1. Wema kwa wenzetu (mf. 1 Sam. 20:14; 2 Sam. 16:17; 2 Nya. 24:22; Ayubu 6:14; Zab. 141:5; Mit. 19:22; 20:6)
  2. wema kwa maskini na wahitaji (mf. Mika 6:8)
  3. upendo wa Israeli kumuelekea HWH (kama vile Yer. 2:2; Hos. 6:4,6)
  4. uzuri wa maua ya kondeni (kama vile Isa. 40:6)
- B. Lilitumika katika uungaishaji na Mungu
  1. uaminifu wa agano na upendo
    - a. “ ukombozi kutoka katika maadui na taabu” (mf. Mwa. 19:19; 39:21; Kut. 15:13; Zab. 31:16; 32:10; 33:18,22; 36:7,10; 42:8; 44:26; 66:20; 85:7; 90:14; 94:18; 107:8,15,21,31; 109:21-22; 143:8,12; Yer. 31:3; Ezr. 7:28; 9:9)

- b. "katika ulinzi wa maisha kutokka katika kifo" (mf. Ayubu 10:12; Zab. 6:4-5; 86:13)
  - c. "katika wepesi wa maisha ya kiroho" (mf. Zab. 119:41,76,88,124,149,159)
  - d. "katika ukombozi wa kutoka dhambini" (kama vile Zab. 25:7; 51:1; 130:7-8)
  - e. "katika kutunza maagano" (mf. Kum. 7:9,12; 2 Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4; Mik. 7:20)
2. kuzielezea sifa za Mungu (mf. Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona 4:2; Mika 7:20)
  3. wema wa Mungu
    - a. "utele" (mf. Hes.14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:5; 103:8; 145:8; Yoeli 2:13; Yer. 4:2)
    - b. "ukuu katika kiwango chake" (mf. Kut. 20:6; Kum. 5:10; 7:9)
    - c. "umilele" (mf. 1 Nya. 16:34,41; 2 Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136:1-26; 138:8; Yer. 33:11)
    - d. nguvu zilizo sawa (mf. Zab. 59:17)
    - e. iliusiana na nguvu za Mungu (mf. Zab. 62:11c-12a)
  4. matendo ya wema (mf. 2 Nya. 6:42; Zab. 89:2; Isa. 55:3; 63:7; Omb. 3:22)

Neno hili linatafsiriwa kwa njia mbalimbali katika tafsiri za Kiingereza. Nafikiri maelezo bora yaliyo katiaka ufupisho yangeliwuwa "hakuna kamba iliyounganisha utii wa agano la Kimungu" neno hili ni sambamba na neno la Agano Jipya "upendo" (agapaō). Munguni mwaminifu na mwenye upendo kwa sababu ya Yeye

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 16:6-12**

<sup>6</sup>Tumesikia habari za kiburi cha Moabu, ya kwamba ni mwenye kiburi kingi;  
habari za majivuno yake, na kiburi chake, na ghadhabu yake;  
majivuno yake si kitu.

<sup>7</sup>Kwa sababu hiyo Moabu atalia kwa ajili ya Moabu, kila mmoja atalia,  
maana mtaiomboleza mikate ya zabibu ya Kir-Haresethi, mkipigwa sana.

<sup>8</sup>Maana makonde ya Heshboni yamenyauka, na mzabibu wa Sibma;  
mabwana wa mataifa wameyavunja matawi yake mateule;  
yamefika hata Yazeri, yalitanga-tanga hata nyikani;  
matawi yake yalitapakaa, yaliivuka bahari.

<sup>9</sup>Basi, naililia mizabibu ya Sibma kwa kilio cha Yazeri,  
nitawanyeshea machozi yangu, Ee Heshboni na Eleale,  
kwa kuwa kelele za vita zimeyaangukia mavuno ya matunda yako,  
na mavuno ya mizabibu yako.

<sup>10</sup>Na furaha imeondolewa, na shangwe toka mashamba yaliyozaa sana;  
hapana kuimba katika mashamba ya mizabibu, wala sauti za furaha;  
akanyagaye hakanyagi divai katika mashinikizo; nimeikomesha sauti ya furaha yake akanyagaye.

<sup>11</sup>Kwa sababu hiyo mtima wangu unamlilia Moabu kama kinubi,  
na matumbo yangu kwa ajili ya Kir-Heresi. <sup>12</sup>Tena itakuwa,  
Moabu akionekana, na kujichosha kwa kulia juu ya mahali pa juu,  
na kuingia katika patakatifu pake aombe, hatapata kushinda.

**16:6** Huu unaanza ubeti mpya. Mistari ya 1-5 ni kile ambacho YHWH alitumaini kingetokea, lakini mstari wa 6 unaeleza kwanini hakikutokea (linganisha na Yer. 48:29).

1. kiburi cha Moabu
2. kiburi kilichozidi
3. majivuno
4. kiburi
5. hasira (BDB 720, "kutoheshimu")
6. uongo, majivuno ya bure (BDB 95 III, kujifanya majivuno ya bure, kama vile Ayubu 11:3; Yer. 48:30)

Jina la Kiebrania “kiburi” (BDB 144) linarudiwa mara nne katika njia tofauti tofauti. Moabu kama miungu yake inadai zaidi, inaongea zaidi lakini haiwezi kufanya chochote!

**16:7-10 “Hivyo”** Haya hapa ni madhara yake.

1. Moabu ataomboleza kwasababu ya kuabudu kwake Baali (yaani “mikate ya zabibu kavu”), mistari ya 7,12 (inawezekana kwamba hii ni nahau nyine kwa ajili ya kushindwa kwa kilimo)
2. kunyauka kwa mashamba na kutokuwa na mavuno, mistari ya 8-10 (kama vile 15:6)

Inawezekana kwamba “mikate ya zabibu kavu” katika muktadha huu inamaanisha maisha ya anasa.

**16:10 “mvinyo”** Angalia Mada maalum katika 1:22.

▣**“Nimefanya na furaha imeondolewa”** Hii inamaanisha kwa watumwa wavamizi wa YHWH walioharibu mavuno na sherehe zake za mwishoni mwa mwaka.

Dhana ya kuondolewa kwa “furaha” inajirudia katika mstari huu.

1. furaha kuondolewa, BDB 62, KB 74, *Niphil KAULI TIMILIFU*
2. furaha ikichukuliwa (ikichukua KITENZI KILEKILE sawa sawa na #1)
3. bila vilio (au nyimbo) za furaha, BDB 943, KB 1247, *Pual KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
4. bila kupiga kelele za furaha, BDB 929, KB 1206, *Pola KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
5. kukoma kwa kupiga kelele, BDB 991, KB 1407, *Hiphil KAULI TIMILIFU*

**16:11 Swalli ni nani anayezungumza.**

1. Mungu (מְנֻגָּה, BDB 588, yaani 63:15; Yer. 31:20)
2. nabii
3. Moabu akinafsishwa

Kwasababu ya mstari wa 12, Moabu (#3) haiwezi ikawa sawa. Kwasababu ya mstari wa 13 inawezekana kuwa #2, nabii Isaya, lakini kwasababu ya 15:5,9, kama pia maana ya kimasih ya mstari wa 5, Nafikiri ni Mungu anayehuzuni juu ya “kitu gani kinge kwa kimefanyika” Mungu anawapenda wanadamu aliowafanya kwa sura na mfano wake, aliowafanya kwa ajili ya ushirika, lakini bado wanageukia miungu ya uongo, matumaini ya uongo!



**NASB, REB**                    “Kir-Haresethi”

**NKJV, NRSV**

**TEV, NJB**                    “Kir-Hares”

Toleo la MT linaaksiwa katika NKJV, lakini ni muundo uliofupishwa wa NASB (kama vile mstari wa 7; jiji lilikuwa linamaanisha kwa “Kir” katika 15:1).

**16:12** Mstari huu unaweza kueleweka kwa namna mbili.

1. Moabu wanaleta sadaka (mstari wa 1) kuelekeea Yerusalem (mstari wa 5), lakini kwa ajili ya kiburi chake hukataa kumsikiliza YHWH (mstari wa 6). YHWH anawajali wao sana (15:5; 16:11).
2. Moabu wakitafta msaada kutoka kwa miungu wake wengine (15:2; 16:12), lakini wanashindwa kuitikia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 16:13-14**

<sup>13</sup>Hilo ndilo neno lile alilolisema Bwana juu ya Moabu zamani. <sup>14</sup>Lakini sasa Bwana asema hivi, Katika muda wa miaka mitatu, kama miaka ya mtu wa mshahara, utukufu wa Moabu utadharauliwa, pamoja na wingi wake wote; mabaki yake yatakuwa machache sana, kama si kitu kabisa.

**16:14** Hii inaelezea dhahili (miaka 3) hatma ya kiburi ya Moabu! Badala ya watu tele, utajiri, ushawishi na mazao Moabu atakuwa “mdogo sana na asiyekuwa na uwezo”! Kurudishwa nyuma kihistoria kunashangaza na kunaelekeza kwenye ubinadamu ulioanguka kuelekeea katika ahadi na shauku ya ustahimilivu na amani inayopatikana tu katika Mungu wa Israeli!

## ISAYA 17

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Unabii juu ya Dameski	Tangazo dhidi ya shamu na Israeli	Dhidi ya muungano mwefraimu mwenye Asili ya shamu	Mungu ataadhibu shamu na Israel	Dhidi ya Dameski na Israeli
17:1-3 (1-3)	17:1-3 (1-3)	17:1-3 (1-3)	17:1-3	17:1-3 (1-3)
17:4-11 (4-11)	17:4-8 (4-8)	17:4-6 (4-6)	17:4-6	17:4-6 (4-6)
		17:7-8 17:9 (9)	17:7-8 17:9	17:7-8 17:9-11 (9-11)
	17:10-11 (10-11)	17:10-11 (10-11)	17:10-11	Mataifa maadui yanapigwa
17:12-14 (12-14)	17:12-14 (12-14)	17:12-14 (12-14)	17:12-14	17:12-14 (12-14)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 17:1-3**

<sup>1</sup> Ufunuo juu ya Dameski.

Tazama, Dameski umeondolewa usiwe mji,  
nao utakuwa chungu ya magofu.

<sup>2</sup>Miji ya Aroeri imeachwa;  
itakuwa kwa makundi ya kondoo,  
nao watajilaza huko wala hapana atakayewatia hofu.

<sup>3</sup>Na ngome ya Efraimu itakomeshwa,  
na ufalme wa Dameski,  
na mabaki ya Shamu;

watakuwa kama utukufu wa wana wa Israeli,  
asema Bwana wa majeshi.

**17:1** “Dameski” huu ni mji kuu wa Aram/Shamu. Kushambuliwa na kuharibiwa kwa Shamu kunatajwa kutokea mapema katika 7:16; 8:4; 10:9. Ni mji wa kale sana (kama vile. Kut. 14:15; 15:2) na ni mji muhimu ulioko kaskazini na kusini mashariki mwa njia kuu za kibiashara .

◻ Tambua usambamba wa mstari wa 2 na 3 ina maana sawa. Tiglath-pileser III kwa sehemu aliuharibu mji wa Dameski katika mwaka wa 732 K.K. na ukajengwa tena kama mji mkuu wa Ashuru. Kumbuka unabii wote unakosoa (tazama D. Brent Sandy, *Plowshares na Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*).

**17:2** “Miji ya Aroeri” Tungo hii inachanganya.

1. Hili ni jina la mji, sio jimbo.
2. Kuna miji mingi ambayo inaitwa kwa jina hili (BDB 792,a,mbalo labda linarejelea “mti” au “kilele cha mlima” AB, juzuuy a 1, ukr. 399). Miji mitatu kati ya minne inawezekana iko kusini mwa himaya ya Shamu
3. Toleo la LXX limeacha jina la mahali (kama liliovskyofanya toleo la REB).
4. Toleo la Peshitta linataja Aroeri.

Inaonekana kwamba kwenye Sura hii Shamu na Israeli wameungana pamoja. Wakatengeneza muundo wa kisiasa/kijeshi pamoja dhidi ya Asuru na wakajaribu kumsih Yuda ajiunge nao. Muungano huu ulisababisha vita vya Waefrahimu wenyen asili ya Shamu ambapo makabila haya mawili ya kaskazini kuivamia Yuda (kama vile. 7:16; 8:4; 10:9).

Marejeo mengi ni katika makabila kumi ya kaskazini yaliyoitwa Israeli/Yakobo (mst. 4); Samaria au Efrahimu (mst. 3). Shamu ilikuwa chini ya utawala wa Israeli kipindi cha muungano wa kifalme.

Aroeri labda inadokeza ngome iliyokuwa katika mto Arnoni.

◻ mstari wa 2 na 3 unaelezea uharibifu wa jumla na kupungua kwa idadi ya watu mahali hapo.

**17:3** miji yenye ngome za ukuta ya Shamu na Efrahimu itaangamia (BDB 991, KB 1407, *Niphil KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU*). Toleo la JPSOA lina tanbihi inayounga mkono kwamba andiko limerekebishiwa kutoka “Efrahimu” (BDB 68) אֶרְםָאַקְוֵנְדָה! “Aramu” (BDB 78), ambalo linaweza kuwa ni ukweli ulio sambamba. Lakini kama sehemu ya kwanza ya shairi ni juu ya vita vya Waefrahimu wenyen asili ya Shamu, hivyo basi tayari usambamba uko hapo. Nafikiri mst. 3 una AB, BA mtindo fulani wa mashairi (chiasim), kama ilivyo katika Andiko la kimasoreti.

◻ “mabaki ya Shamu” Tungo hii inaweza kurejelea kwenye

1. Mji mkuu kama sehemu pekee iliyobakia chini ya utawala wa Shamu ( na utaangamizwa, mst. 6)
2. Mji mkuu utakapo angamizwa hata na wakimbizi hawataokolewa.

◻ ingawa mistari miwili ya mwisho ya mst. 3 inajitokeza kuwa endelevu, haiwezi kuwa hivyo. Efrahimu itaangamizwa katika 3a, na sasa Shamu inashiriki maangamizi yake (dhihaka, “utukufu,” kama vile mst.. 4). “utukufu” inaweza kurejelea mji mkuu wa Israeli, “Samaria,” ambao uliangamizwa baada ya kuzingirwa kwa muda mrefu na Waashuru chini ya Sargon II katika mwaka wa 722 K.K .

◻ “**Asema BWANA wa majeshi**” YHWH ni mtawala wa historia, hasa kwa yale matukio yanayo athiri watu wake wa Agano. Kwa ajili ya cheo “BWANA wa majeshi” tazama mada maalumu:Majina kwa ajili ya Uungu katika 1:1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 17:4-11**

<sup>4</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo, utukufu wa Yakobo utapungua-pungua,  
na kunona kwa mwili wake kutakonda.

<sup>5</sup>Tena itakuwa kama hapo avunaye ashikapo mabua ya ngano,

na mkono wake ukatapo masuke;

tena itakuwa kama hapo mtu aokotapo masuke

katika bonde la Warefai.

<sup>6</sup>Lakini kilichosazwa na mvunaji kitakuwa ndani yake, kama vile wakati wa kupiga mizeituni, matunda mawili matatu yaliyo juu sana; matunda manne matano katika matawi, matawi ya mti wa matunda, asema Bwana, Mungu wa Israeli.

<sup>7</sup>Katika siku hiyo mwanadamu atamwangalia Muumba wake, na macho yake yatamtazama Mtakatifu wa Israeli.

<sup>8</sup>Wala hataziangalia madhabahu, kazi ya mikono yake; wala hatavitazama viliyofanyika kwa vidole vyake, maashera na sanamu za jua.

<sup>9</sup>Katika siku hiyo miji yake yenye maboma itakuwa kama mahali palipoachwa ndani ya mwitu, na juu ya kilele cha mlima, palipoachwa mbele ya wana wa Israeli; napo patakuwa ganjo.

<sup>10</sup>Maana umemsahau Mungu wa wokovu wako, wala hukuukumbuka mwamba wa ngome yako; kwa sababu hiyo ulipanda mashamba yapendezayo, na kutia ndani yake mizabibu migeni.

<sup>11</sup>Katika siku ile ulipopanda, ulifanya kitalu, na wakati wa asubuhi ulizimeesha mbegu zako, lakini mavuno yatatoweke siku ya huzuni, na ya sikitiko la moyo lifishalo.

**17:4 “katika siku hiyo”** Inatia mashaka ni kwa jinsi gani andiko lifuatalo linagawanywa katika sehemu ya ubeti wa shairi. Tungo hii inaweza kudokeza mwanzo wa shairi jingine (kama vile .mst. 4, mst. 7, mst. 9, mst. 11). Ni vigumu kutambuwa tofauti iliyopo kati ya mashairi na andiko lisilo la kishairi (muhtasari wa mgawanyo wa aya na mistari ya kishairi katika tofauti ya tafsiri ya mwanzo wa Sura).



NASB        “kufifia”

NKJV        “kufifia”

NRSV        “kushushwa”

TEV        “kumalizwa”

NJB        “kuishiria”

KITENZI hiki (BDB 195, KB 223, *Niphal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) Kwanza inarejelea matunda yaliyoning’inia au matawi,lakini *Niphal* tawi linadokeza kwamba ni ambalo limeletwa chini au kulazwa chini (kama vile Waam. 6:6). The *Qal* tawi limetumika katika 19:6 na 38:14.

Hii ni moja kati ya semi nyingi zisizo na maana zinazoelezea Israeli.

1. Utukufu . . .utafifia,mst. 4
2. Kunona kwa mwili wake kutakonda mst. 4
3. Israeli itaangamizwa chini, mst. 5
4. Mizabibu michache itaachwa imesimama, mst. 6

**17:5 “katika bonde la Warefai ”** Hii inarejelea bonde lenye rutuba kusini magharibi mwa Yerusalem ambalo limetajwa mara nyingi katika Agano la kale (kama vile 2 Sam. 5:18,22; 23:13; 1 Nya. 11:15; 14:9; na hapa). Ni lazima itumike kwanza kama taswira ya matunda yasiyotarajiwa ya Isaya (kama vile . mst. 4). Ndio sababu alitumia eneo katika Yuda , sio Israeli, hii inatia mashaka.

**17:6** mavunoyamwanzo ya mti wa mzeituni ilikuwa ni kwa kutikiswa au kuushambulia mti (kama vile. 24:13; Kumb. 24:20). Kulikuwa na mizeituni michache ambayo daima iliachwa bila kuangushwa. Hii kwa kawaida iliachwa kwa ajili ya maskini (yaani , wavunaji). Isaya aliwatumia kama alama kwa ajili ya mabaki waliookoka.

▣“**mawili au matatu . . .manne au matano**” huu ni mfano wa nahau ya kiebrania kwa ajili ya idadi isiyo na mwisho.

**17:7-8** Ayahizi zina muundo tofauti. Aya ya 7 inadokeza toba , aya ya 8 wamegeuka kutoka kwenye nini (yaani.,kuabudu sanamu). Swalni kwa akina nani amabo aya hizi mbili zinalekezwa.

1. Israeli
2. Israeli na Shamu
3. Israeli, Shamu, na Ashuru
4. Tamaduni zote Mashariki ya Karibu ya Kale (yaani “wanaume,” המְבוּאַת).

Hii ina maana kuwa sambamba na Sura ya 7, 9, na 11? Pia tambua ahadi ya ushindi kwa watu wa Agano wa Mungu katika mist. 12-14 (na hasa mst wa. 14b)!

**17:7** usambamba wa aya hizi una muunganiko “muumbaji” (yaani.,muumbaji wa mbingu na nchi au muumbaji wa Israeli, kama vile. 51:13) na “mtakatifu wa Israeli” (cheo kilichotumiwa na Isaya ni cha pekee sana ). Hii ni taswira ya kumwabudu Mungu mmoja pekee!

**17:8** badala ya Mungu kuwa “muumbaji” walijitengenezea miungu yao (yaani.,Baali na Maashera, mstri 3; 2:8,20; 30:22; 31:7)

## **MADA MAALUMU: IBADA YA USTAWI WA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE**

### I. Sababu ya

- A. Wanadamu wa kale walianza kama wawindaji walioishi sehemu moja, lakini maisha ya kuhamahama yaliimarika, hitaji kwa ajili ya mazao na mifugo.
- B. Wakazi wa Mashariki ya Karibu ya kale walikuwa hatarini kukabiliana na nguvu ya asili. Kadiri ustaarabu ulivyokua kuzunguka maeneo ya vyanzo vikubwa vya maji safi, walikuwa wategemezi kwa utaratibu wa kila siku wa majira.
- C. Nguvu za asili ikawa miungu iliyotakiwa kujazwa na kuongozwa/kuendeshwa.

### II. Wapi na kwanini

- A. Dini za kuabudu kuzaa ilikua katika
  1. Misri (Nile)
  2. Mesopotamia (Hedekeli na Frati)
  3. Kanaani (Yordani)
- B. Kuna ufanano wa msingi kati ya dini za uzao za Mashariki ya Karibu ya kale.
- C. Majira yanayobadilika na yasiyofikirika na hali ya hewa ilisababisha ukuaji wa hadithi za kishujaa kwa kutumia analogia ya kibinadamu /kiungu kama msingi wa maisha katika ulimwengu war oho na duniani.

### III. Nani na namna gani

- A. Nani (miungu ya kiume na kike)
  1. Misri
    - a. Isis (wa kike)
    - b. Osiris (wa kiume)
  2. Mesopotamia
    - a. Ishtar/Inanna (wa kike)
    - b. Tammuz/Dumuzi (wa kiume)
  3. Kanaani
    - a. Ba'al (wa kiume)
    - b. Ashera, Astarte, Anathi (wa kike)

- B. Kila moja ya jozi hizi zilikuwa hadithi za kimiujiza katika namna inayofanana
    - 1. Mmoja anafariki
    - 2. mwingine anarejesha
    - 3. Utaratibu wa kufa na kuinuka kwa miungu kunaiga mzunguko wa kila mwaka wa asili
  - C. Uigaji wa kimiujiza uliona muunganiko wa ujamiihana wa kibinadamu (yaani ndoa za miungu) kama njia ya kuhakikisha ustawi wa mazao, mifugo na watu.
- IV. Waisraeli
- A. Watu wa YHWH walionywa (yaani Mambo ya Walawi na Kumbukumbu la Torati) kukwepa ibada za ustawi (haswa za Kanaani).
  - B. Dini/ibada hizi zilikuwa maarufu kwasababu ya uchawi wa wanadamu na chagizo la nyongeza la tendo la ndoa
  - C. Ibada ya sanamu ilishirikisha Baraka ya uzima kutaftwa katika njia za ishetani badala ya imani binafsi na tumaini kwa YHWH.
- V. Masomo yanayopendekezwa
- A. W. F. Albright, *Archaeology and the Religion of Israel*
  - B. J. H. Breasted, *Development of Religion and Thought in Ancient Egypt*
  - C. James G. Frazer
    - 1. *Adonis, Attis, Osiris*
    - 2. *Folklore in the Old Testament*
    - 3. *The Worship of Nature*
  - D. C. H. Gordon, *Before the Bible*
- S. N. Kramer, *Mythologies of the Ancient World*

▣ “sanamu za juu” neno hili (BDB 329 linaitwa “nguzo za juu,” lakini KB 329 inaitwa ya kuchukulika “madhabahu”) mara zote inatumika katika maana ya muktadha wa waabudu sanamu (kama vile Law. 26:30; 2 Nya.14:5; 34:4,7; Isa. 17:8; 27:9; Ezek. 6:4,6).

**17:9** huu unaonekana ni mwanzo wa umoja mpya. Inaelezea kuja kwa hukumu katika sitiari za kilimo za kiuchochazi (MT)

1. Kama mahali palipoachwa mwituni
2. Kama matawi ambayo yameachwa
3. Nchi itaachwa ukiwa

Aya hizi zinatafsiriwa tofauti na tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania na tafsiri yake inafuatiwa na matoleo ya JB, NRSV, na REB (na toleo la JPSOA inaonekana ni uhalali wa ufahamu katika tanbihi hii). Tungo inadokeza (1) kutoka upesi Misri ambapo visivyo na maana viliachwa au (2) makundi ya watu yalitawaliwa na Israeli wakati wa uvamizi (yaani., waamori na wahiti).

**17:10** Hii ni aya ya pekee inayoelezea sababu ya kuja kwa hukumu juu ya Israeli kwa agano la uungu wao.

1. Kumsahau Mungu wa wokovu wako (yaani., Zab. 78:11,42)
2. Hukumkumbuka mwamba wa ngome yako (yaani., Zab. 18:1-3; 78:35)
3. Ulipanda mashamba mazuri kwa ajili ya heshima ya miungu ya kigeni (kama vile. 1:29-30; 65:3; 66:17, yaani , bustani takatifu au miti. Labda inarejelea Adonisi/Tammuzi, mungu wa mazao ambaye katika yeeye mazao yalipandwa mwanzoni mwa majira ya kuchipua, kama vile. AB, juzu. 6, ukr. 318)

▣ “mungu wa wokovu wako” haya ni maelezo yaliyorudiwa mara kwa mara kumhusu Mungu wa Israeli (kama vile . 12:2; 17:10; 33:2; 45:17; 61:16; 62:10; Zab. 65:5; 68:19; 85:4). Wokovu unamaanisha kukombolewa kutoka nguvu yejote au ukandamizaji unaokana au kukataa Agano la YHWH analotamani kwa ajili ya watu wake .dhambi za Israeli pekee ndizo zinaweza kuzuia shauku yake juu yao na bado, Yeye anabaki kuwa “Mungu wa wokovu wako” (kama vile . Mika 7:7; Hab. 3:13,18).

**17:11** hii inarejelea bustani takatifu namba 3 kwenye mst wa. 10 juu.

1. Walipanda kwa makini
2. Waliweka uzie
3. Wakatia na mbolea

Itakuwa haraka na kutoa matunda ya kushangaza, lakini matokeo yake yatakuwa ni

1. Mavuno yatakuwa kidogo
2. Huzuni kuu
3. Maumivu makali (kama vile. Ayu 34:6; Yer. 15:18; 17:9; 30:12,15; Mika 1:9)

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 17: 12-14**

<sup>12</sup>Aha! Uvumi wa watu wengi!

Wanavuma kama uvumi wa bahari;  
 Aha! Ngurumo ya mataifa!  
 Wananguruma kama ngurumo ya maji mengi;  
<sup>13</sup>Mataifa wananguruma kama ngurumo ya maji mengi;  
 Lakini atawakemea, nao watakimbia mbali sana,  
 Watafukuzwa kama makapi milimani mbele ya upepo,  
 Na kama mavumbi vurvuru mbele ya tufani.

<sup>14</sup>Wakati wa jioni, tazama, kuna hofu;  
 Na kabla ya mapambazuko hawako;  
 Hilo ndilo fungu lao watutekao,  
 Na ajali yao wanaotunyang'anya mali zetu.

**17:12-14** Huu ni ubeti wa mwisho wa Sura ya 17.inabainishwa kwa mfanano na kurudiwa kutumika kwenye asili mbili.

1. BDB 242, KB 250, “uvumi,” “kukua,” “ngurumo,” au “kuwa na kelele”
  - a. NOMINO, mst. 12
  - b. *Qal* TUNGO YA KITENZI JINA HALISI, mst. 12
  - c. *Qal* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 12
2. BDB 980, KB 1367, “ngurumo,” “wanavuma,” “uvumi,” au “tufani”
  - a. NOMINO(BDB 981),mst. 12
  - b. NOMINO(BDB 981), mst. 12
  - c. *Niphal* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 12
  - d. NOMINO(BDB 981), mst. 13
  - e. *Niphal* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 13
3. Mfanano wa sura, mst. 13
  - a. kama makapi, mst. 13
  - b. kama mavumbi, mst. 13

Muungurumo wa YHWH ni mkubwa zaidi ya makelele ya mataifa na matokeo yake watashindwa! Atayashinda machafuko ya maji tena ,kama katika uumbaji (kama vile. Zab 29).

4. Kinyume chake
  - a. wakati wa jioni, tazama kuna hofu
  - b. kabla ya mapambazuko hawako
  - c. kisawe, mst. 14
    - a. watekao, BDB 1042, KB 1367, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU
    - b. vaporaji, BDB 102, KB 117, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU

**17:14 “Na kabla ya mapambazuko hawako”** kifungu hiki hakina KITENZI,kitakacho onyesha mkazo.

mstari huu unatupatia muktadha wa urejesho wa mistari ya 12-14. Ubeti huu ni mfanano na mawazo ya Zaburi 2. YHWH anatuma mataifa (yaani., kuwaadhibu watu wake kwa kutokutii Agano na upungufu wa imani kwake), lakini anayahukumu mataifa mengine. Watu wake ni salama kwake! Kuwageukia huku ni sawa sawa katika 10:33-34.

Mara nyingi katika Isaya ukombozi wa Mungu ni kuwaunganisha Nuru ijayo (kama vile. 8:22-9:2; 17:14; 29:18; 30:26; 33:2; 42:16; 49:9-10; 58:8,10; 60:1-3,19-20).

▣“fungu” Neno hili (BDB 324) linadokeza mapenzi ya Mungu katika sura ya kiroho. Haina maana kwamba ni hatima isiyo na misingi kamili au uhakika, lakini matukio yapo katika uweza wa Mungu (kama vile. Yer. 13:25)

## ISAYA 18

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ujumbe kwa Ethiopia	Tangazo la vita dhidi Ethiopia	Kuhusiana na Ethiopia	Mungu ataiadhibu Ethiopia	Dhidi ya kushi
18:1-7 (1-7)	18:1-2 (1-2)	18:1-2 (1-2)	18:1-2	18:1-6 (1-6)
	18:3	18:3-6	18:3-6	
	(3)	(3-6)		
	18:4-6 (4-6)			
	18:7	18:7	18:7	18:7

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasi.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.K

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 18:1-7**

<sup>1</sup> Ole wa nchi ya uvumi wa mabawa,

Iliyoko mbali kupita mito ya Kushi;

<sup>2</sup> Ipelekayo wajumbe wake kwa njia ya bahari,

Na katika vyombo vya manyasi juu ya maji.

Nendeni, wajumbe wepesi,kwa watu warefu,laini;

Watu watishao tangu mwanzo wao hata sasa;

Taifa la wenye nguvu,wakanyagao watu,

Ambao mito inakata nchi yao.

<sup>3</sup> Enyi watu mkaao katika ulimwengu wote,

na wenyeji wa dunia, bendera ikiinuliwa milimani, angalieni;

na wakipiga tarumbeta, sikieni.

<sup>4</sup> Maana Bwana ameniambia hivi,

Mimi nitatulia, na kuangalia katika makazi yangu,

kama wakati wa mwangaza mweupe wa juu kali,  
mfano wa wingu la umande katika hari ya mavuno.

<sup>5</sup>Maana kabla ya mavuno, maua yaangukapo,  
na maua yakawa zabibu zianzazo kuiva,  
ndipo atakapoyakata matawi kwa miundu,  
na kuviondoa vitawi vilivyopanuka na kuvikata.

<sup>6</sup>Wote pamoja wataachiwa ndege wakali wa milimani,  
na hayawani wa nchi;  
ndege wakali watacaa juu yao wakati wa juu,  
na hayawani wote wa nchi watacaa juu yao wakati wa baridi.

<sup>7</sup>Wakati huo Bwana wa majeshi ataletewa hedaya  
na watu warefu, laini;

Watu watishao tangu mwanzo wao hata sasa;

Taifa la wenyewe nguvu, wakanyagao watu,

Ambao mito inakata nchi yao;

mpaka mahali pa jina la Bwana wa majeshi, mlima Sayuni.

#### 18:1

NASB                  “Ole”

NKJV, Peshitta      “Ole”

NRSV, JPSOA        “Ole”

KIHISISHI hiki (BDB 222) kinatumika mara kwa mara na manabii (kama vile. 1:4,24; 5:8,11,18,20,21,22; 10:1,5; 17:12; 18:1; 28:1; 29:1,15; 30:1; 31:1; 33:1; 45:9; 55:1). mara nyingi huelezea juu ya mwitikio ulio kinyume kwenye ujio wa maumivu ya hukumu ya Kiungu. Hata hivyo, baadhi ya muktadha huonyesha huruma au rehema , kama katika 18:1; 55:1; Yer. 47:6.



NASB, NRSV        “nchi ya uvumi wa mabawa”

NKJV                “nchi ya uvuli wa mvumo wa mabawa”

TEV                 “nchi ambayo sauti ya mabawa inasikika”

NJB                 “nchi ya uvumi wa nzige”

LXX                 “mabawa ya nchi ya merikebu”

Peshitta            “nchi ya uvuli wa mabawa”

REB                 “nchi yenye merikebu” (kutoka kiarabu na kiaramu , Targums, na toleo la LXX)

JPSOA              “nchi ya uvuli mkuu wa mabawa”

Huu mzizi (צְלָל, BDB 852) yawezekana una maana kadhaa

1. 821 I Uvumi, mvumo kama mabawa za wadudu
2. 852 II, mvumo wa mkuki kwenye vita (kama vile. Job 40:7)
3. KONSONANTI ZILE ZILE, lakini zikiwa na IRABU tofauti, mvumo wa nzige (kama vile. Kumb. 28:42)
4. WINGI, midundo ya ara ya muziki (kama vile 2 Sam. 6:5; 1 Nya. 13:8; Zab. 150:5).
5. KITENZI chenye kuhusiana (צְלָל, BDB 852), au msisimko (kama vile 1 Sam. 3:11; 2 Fal. 21:12; Yer. 19:3) tetemeka (kama vile Hab. 3:16)
6. 853 II, zama (kama vile Kut. 15:10)
7. 853 III, kuwa giza (kama vile Neh. 13:19; Ezek. 31:3)
8. NOMINO yenye kuhusiana, צְלָל, kivuli (kama vile Isa. 4:6; 16:3; 25:4,5; 30:2,3; 32:2; 34:15; 38:8; 49:2; 51:16 ( hivi ndivyo toleo la JPSOA linavyokitafasiri kifungu)



NASB, MT,

NJB, REB	"kushi"
NKJV, LXX,	
Peshitta	"Ethiopia"

NRSV tanbihi "Nubi"

Hii inarejelea eneo la nchi kusini mwa maporomoko ya mwanzo ya mto Nile. Ilifahamika katika kitabu cha Mwanzo kama "Kushi" (BDB 468, kama vile Mwa. 2:13; 10:6,7,8). Kipindi cha Uyunani liliitwa "Ethiopia." Leo inaweza kuhusishwa Sudani na sehemu za Ethiopia ya sasa (toleo la TEV tanbihi, ukr. 625).

Katika muktadha huu (yaani ,Sura ya 19), yaweza kurejelea kwenye watawala wa Wanubi wa karne ya 25<sup>th</sup> huko Misri (yaani , Pianchia, Shabaka). Hata hivyo, tambua ya kwamba watu wanaoelezewa ni wale walioko "ng'ambo ya mito ya Kushi". Labda Misri yenyelewa ilikuwa ikitafuta maaskari wa kukodi!

**18:2 "vyombo vya manyasi juu ya maji "** Kwa mara ya kwanza mtu angaliweza kufikilia hili lazima linarejelea merikebu zisafirizo kwenye mto Nile, lakini aina hizi za merikebu pia zilitumika kwenye mito ya Hedekeli na Frati (kama vile James M. Freeman, *Manners naCustoms of the Bible*, ukr. 2560

▣ "nendeni" Hii ni *Qal KAULI SHURUTISHI*. Hii inaelezewa kwa akina nani?

1. Wajumbe kutoka Kushi e
2. Wajumbe kutoka Misri
3. Wajumbe kutoka makundi ya kukodiwa kusini mwa Kushi
4. Wajumbe kutoka Ashuru
5. Majeshi ya wanadamu yanampinga YHWH na watu wake wa Agano

Mara kwa mara Isaya anaelezea muundo wa kihistoria au tukio la muundo wa siku za mwisho. Matukio na vilio vya kipindi chake yanaonyesha kivuli cha matukio ya hitimisho la historia. Hii sintofahamu ni ngumu kuifunga kwenye kumbukumbu ya kihistoria (nyakati, mahali, watu). Matokeo ya kiulimwengu na makusudi yako kazini nyuma ya matukio ya kimaisha.

▣ Mstari huu unaelezea sifa za taifa.

1. Watu wa baharini (yaani., merikebu za mafujo ya Mto Nile, BDB 479 MUUNDO WA MANENO BDB 167)
2. Watu warefu (BDB 604, KB 645, *Pual KAULI ENDELEVU*, hasa "kurefusha")
3. Watu laini, BDB 598, KB 634, *Pual KAULI ENDELEVU*(imetumika kwa vichwa venye upara, lakini pia upanga ung'ao na ngozi ya watu: [1] hakuna doa, toleo la REB, TEV, "ngozi laini" [2] rangi thabiti, "liobadilika rangi", toleo la NJB; au [3]lioniyelewa vizuri, hakuna nywele za uso)
4. Watu watishao tokea mwanzo na wenyewe nguvu
5. Taifa lenye nguvu (Ebrania haijulkani, lakini inawezekana ni nahau kwa ajili ya "lugha ya kigeni")
6. Taifa dhalimu (Ebrania haijulkani)
7. Mito inagawa nchi (Ebrania haijulkani, KITENZI hiki, BDB 102, KB 107, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, inajitokeza mara mbili pekee kwenye sura hii. Tafasiri ya "kugawa" ni msingi wa asili ya lugha ya kiarama. Toleo la REB lina neno "tesa," likirejelea kwenye mafuriko ya kila mwaka, hata hivyo, linawezza kurejelea kwenye Mto Hedekeli na Frati)

Namba 2-6 imerudiwa kwenye mst. 7. Maelezo haya yanawafaa watu wa kusini mwa maporomoko ya mwanzo ya Mto Nile, warefu, weusi, kundi la watu wapenda vita.

Hata hivyo, muktadha huu unaweza kuelewaka kama Misri akitafuta ushirikiano wa kijeshi dhidi ya Ashuru. Neno lililotafasiriwa "warefu" kamwe halikutafasiriwa kwa njia hii sehemu yeyote ile. Mzunguko wa kidunia katika mst. 3 unaweza kubadili shairi hili kuwa ujumbe toka kwa YHWH kwamba hakuna yeyote anayeweza kuokoa taifa kutoka kwenye hukumu yake. Misri mwenyewe, wala watu wapiganaji maarufu wowote, wanaweza kumsaidia Yuda (kama vile Sura ya 7), YHWH pekee.

Kimuktadha swali ni

1. je Sura ya 18 ni shairi linalojitegemea?
2. je Sura ya 18 inahusiana na Sura ya 17?

3. je Sura ya 18 inahusiana na Sura ya 19?



NASB	“taifa lenye nguvu na dhalimu”
NKJV	“taifa lenye nguvu na kandamizi”
NRSV	“taifa kuu na lenye ushindi”
TEV	“imara na taifa lenye nguvu”
JPSOA	“taifa lenye maneno na kujitapa”

Toleo la LXX na Peshitta yanatafasiri andiko hili kama mwenye kulielezea taifa lililoshindwa,lakini hii haifuatiwi na tafasiri za kisasa.

Kuna NOMINO mbili zilizotumika kuwaelezea watu hawa.

1. Neno “mwenye nguvu”(BDB 876) liko mara mbili. Hii inaweza kulifanya neno kuwa imara (yaani., kishindo cha mwendo wa kijeshi, IVP Bible Background Commentary, uk. 608) au, kama toleo la JPSOA,hubadilika kwenda kwenye maelezo ya lugha zao.
2. Neno la pili (BDB 101) kwa maana ilio wazi ni “kukanyaga” toleo la (NKJV)katika maana ya sitiari ya kushinda.

**18:3 “Enyi watu mkaao katika ulimwengu wote na wenyeji wa dunia”** Isaya amelielezea hili kundi kubwa mara kadhaa (kama vile. 2:2-4; 9:7; 11:10,11-12; 12:4-6; 17:7-8; 26:9). Kile kinachotokea kwa watu wa Agano la YHWH kitaathiri mataifa yote. Neno linaweza kurejelea wokovu wa ulimwengu au hukumu (kama. 13:11; 24:4; 34:1).kwa maana , utumiaji wa neno “dunia” (BDB 385) unaonyesha umuhimu wa YHWH ulimwenguni, nguvu, na uwepo, kama kipengele cha fasihi ya hukumu kwa mataifa yaliyozunguka. Matendo ya YHWH huathiri ulimwengu mzima .Yeye ni Bwana wa uumbaji!

Nani aliyetuma ujumbe wa mst. 3 na ni nani anaelezewa?

1. Kushi kwenda Ashuru
2. Muungano ulio kinyume na Ashuru kwenda Kushi (NRSV tanbihi)
3. Ujumbe wa wa muungano ulio kinyume na Ashuru wakiangalia uwezekano wa kushikiana na Shamu na Israeli (REB tanbihi)
4. Kushi anajibu ujumbe kutoka Yuda kwa ajili ya msaada (tanbihi toka toleo la Jewish Study Bible)
5. Tanbihi toka toleo la JB linasema kwamba ujumbe huu wote unarejelea kwa Misri kwa sababu kipindi hicho Farao alikuwa Mnubi. Hivyo basi Ingaliwa ni sehemu ya fasihi katika Sura ya 19, na sio Sura ya 17!
6. Ashuru kwenda ulimwenguni
7. YHWH kwenda kwa maadui wa wanadamu ambao wako kinyume na makusudi na watu wake (kama vile. Zab 2)

Hivyo tena tunaona utata uliopo, hata hivyo ni yenye nguvu, ile sura ya ushairi wa kiebrania.

□ Hizi zilikuwa ni njia za mawasiliano kwenye vita (yaani wakiinua bendera na kupiga tarumbeta). Alama hizi zinaweza kuwa kwa ajili ya

1. hukumu (kama vile mist. 5-6)
2. wokovu (kama vile mst. 7)

Ni mshangao ulioje kwa ushairi mdogo kuonyesha machafuko ya dunia dhidi ya utulivu wa mbinguni, vile vile pia kile kinachoonekana kama hukumu kuwa mwaliko (yaani 2:2-4; 11:10; 49:6; 51:4-8)

**18:4 “Maana Bwana ameniambia hivi”** Hili ni rejeo maalum la madai ya Isaya la kutiwa moyo. Ujumbe wake haukuwa wake pekee, lakini wa YHWH! Hili ni jambo la mamlaka ya kibiblia! Je Mungu alizungumza? Tunaweza kuelewa? Tunaweza kutumaini? Haya ni maswali ya kimsingi yanayopaswa kujibowi na kila mtu na kila mmoja ahusianapo na Biblia. Angalia mahubiri “uaminifu katika agano la kale” na “uaminifu katika agano jipya” kwenye mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) katika “utafasiri wa Biblia,” somo la pili.

▣ Mistari ya 2-4 inaelezea ujumbe wa Mungu kwenda kwa Kushi au kwenda kwa Ashuru. Anazungumzia kiusalama zaidi (HALI ZA KUSIHI mbili ) kutoka (1) Mlima Moria, katika hekalu ambapo alikaa katikati ya mbawa za makerubi juu ya sanduku la Agano au (2) inarejelea mbinguni (kama vile 1 Fal. 8:39,43,49). Uwepo wake ni furaha!

Katika kitabu cha Isaya Yerusalemu kamwe haitachukuliwa. Aya hii yaweza kuakisi theolojia. Ulimwengu huu wawezakuwa katika vita (mst. 3), lakini Yuda itakuwa salama katika ulinzi wa YHWH (yaani, 7:4; 8:8). Yuda haiitaji muundo wa muungano na Shamu/Israeli au Misri. Ashuru itaangamizwa kabisa.

Ulinzi,utulivu na amani ya YHWH' juu mbinguni ni kinyume cha machafuko duniani. Hili linafanana na muundo wa fasihi wa kitabu cha Ufunuo katika Agano jipya, ambapo machafuko katika dunia yameelezwa kwenye Sura ya 2-3, lakini nafasi ya kiti cha enzi cha mbinguni pako kimya na amani kwenye Sura ya 4-5! Historia sio mtiririko wa mbadiliko, lakini ni namna ya mpangilio wa kilele cha kithiolojia na kupangiliwa na Mungu!

**18:5** Ujumbe wahukumu ya YHWH hutolewa kwa namna ya sitiari ya kilimo, ambapo ni wa kawaida katika Isaya. Mavuno yaliyopotea huharibu mazao ya chakula cha mwaka kwa wale ambao walikitegemea.

Hii ni sitiari ya hukumu ya haraka sana (kama vile. 17:14).

**18:6** wingi wa vifo vyta wanadamu utakuwa ni karamu kwa ajili ya mawindo ya ndege na wanyama wa mwituni.

**18:7** wakati unakuja ambapo mabaki ya wanadamu (au yumkini ulimwengu mzima) watatumiwa ujumbe mwingine, lakini wakati huu hauna kitisho (kama vile mst. 3),bali ni matoleo kwa YHWH huko Yerusalemu (kama vile mst. 7, mstari 6). Zawadi itakuwa alama ya kitamaduni/ kidini wakikubaliana na ubwana na utawala wa YHWH. Maadui wa mst . 1-2 sasa waamini! Huu ni utimilisho wa Mwa. 3:15 (angalia Mada Maalumu: Upendeleo wa Bob wa Kiinjili katika 1:3). Ukombozi ni kusudi kubwa zaidi ya uzao wa kimwili wa Ibrahimu. Hii inajumuisha uzao wake wa kiroho (kama vile. Rum. 2:28-29)!

□

**NASB, NKJV,**

**NRSV, REB,**

**LXX**

**"kutoka"**

**NJB**

**"badala ya"**

Andiko la kimasoreti lina NOMINO "watu" (BDB 766 I), lakini hakuna KIHUSISHI. Inawezekana watu wenywewe walikuwa ni sadaka ya kuteketezwa. Matoleo ya DSS na tafasiri ya maandiko ya kale ya kiebrania na Vulgate yana KIHUSISHI "kutoka".

## ISAYA 19

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ujumbe kwa Misri	Mbinu dhidi ya Misri	Dhidi ya Misri	Mungu Ataidhibu Misri	Dhidi ya Misri
19:1-4 (1-4)	19:1 (1)	19:1-4 (1-4)	19:1-4	19:1-4 (1-4)
19:5-10 (5-10)	19:5-10 (5-10)	19:5-10 (5-10)	19:5-10	19:5-15 (5-15)
19:11-15 (11-15)	19:11-15 (11-15)	19:11-15 (11-15)	19:11-15	
		Kuongoka kwa Misri na Ashuru	Misri Itamwabudu BWANA	Kuongoka kwa Misri
19:16-17	19:16-17	19:16-17	19:16-17	19:16-23
		Misri, Ashuru na Iliyobarikiwa Israeli		
19:18	19:18	19:18	19:18	
19:19-22	19:19-22	19:19-22	19:19-22	
19:23	19:23	19:23	19:23-25	
19:24-25	19:24-25		19:24-25	19:24-2

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyouvumiwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 19:1-4

<sup>1</sup>Ufunuo juu ya Misri.

Tazama, Bwana amepanda juu ya wingu jepesi, anafika Misri;  
na sanamu za Misri zinatikisika mbele zake,  
na moyo wa Misri unayeyuka ndani yake.

<sup>2</sup>Nami nitawaamsha Wamisri juu ya Wamisri;

nao watapigana, kila mtu na ndugu yake, na kila mtu na jirani yake,  
mji juu ya mji, na ufalme juu ya ufalme.

<sup>3</sup>Na roho ya Misri itamwagika kabisa katikati yake,

nami nitayabatilisha mashauri yake, nao watakwenda kwa sanamu zao,  
na kwa waganga, na kwa wapiga ramli, na kwa wachawi.

<sup>4</sup>Nami nitawatoa hao Wamisri na kuwatia katika mikono ya bwana mgumu;

na mfalme mkali atawatawala; asema Bwana, Bwana wa majeshi.

**19:1 “Bwana amepanda juu ya wingu jepesi”** Hii ni lugha ya kistiari inayomweleza YHWH kama

1. mtawala wa ile asili
2. mwongozaji wa ile asili ya uweza
3. wepesi katika kuja kwake

Angalia Zab. 18:10; 104:3. Kifungu hiki kina uhusiano wa ki-Masihi katika Dan.7:13 na Mt. 26:64; Marko 14:62.

Kama vifubgu vingi vya Agano la Kale vinavyomfafanua YHWH tunatambua kwamba vile vinavyo fanana vinatumika kwa miungu wa kipagani au zile sheria za Mashariki ya Kale ya Karibu. Neno amepanda mawinguni linatumika kwa Baali katika mashairi ya ki-Ugaritiki. Kadri watu wa Mungu walivyokumbana na semi /madai ya kiuchochazi ya mataifa yaliyozunguka, ndivyo yeye alivyowafahamisha kwa Mungu wake, Mungu wa pekee, yule ambaye wangeupata utimilifu wao katika njia ya kweli. Hiki ni kifungu cha kweli kama “Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana” na majina mengine ya YHWH yanayofahamika sana.

▣ “**anafika Misri**” Uwepo wa YHWH wa mara nyingine ni hukumu zote (mist. 1-15) na wokovu (mist. 16-23). Hizi ni maana mbili ambayo zinaboreshwu kuitia unabii wa Kiebrania. Mbinu ya kifasihi inayojulikana kama “urejeshi” ndio inayoitwala sana aina hii ya ushahiri. Hii ni sawa na ufanano kinzani uliochukuliwa kutoka katika kipande kukubwa cha maandiko (kama fumbo). Misri atahukumiwa kuwa mwenye kutakaswa na kuandaliwa kwa ajili ya kumwabudu YHWH. Yeye atakuja kwake katika namna ya ukombozi kama alivyofanya juu ya Yuda. Moyo wa YHWH unawaelekewa wanadamu waliumbwu kwa mfano wake (kama vile Mwa. 1:26-27), si kwa kundi la wanadamu fulani waliochaguliwa (yaani, Israeli). Yeye anautumia uzao wa Ibrahim ili kulikamilisha kusudi lake kuu (kama viel Mwa. 3:15)!

▣ “**sanamu za Misri**” Misri ilikuwa na miungu mingi (Kut. 12:12; Hes. 33:4). Sanamu za ibada za Heri zinafafanuliwa katika mst. 3.

1. sanamu (BDB 47)
2. roho za wafu (BDB 31, zinazopatikana hapa)
3. wachawi (BDB 15, “warozi,” kama vile Kumb. 18:11)
4. wapiga ramri (BDB 396, “wachawi,” “wapandisha pepo,” kama vile Kumb.18:11)

Angalia Maelezo katika 8:19. Yale maradhi ya kitabu cha Kutoka yalitabiriwa kwa makusudi juu ya mingu ya Kimisri kwa makusudi ya kuhimarisha imani katika mataifa yote ya Waisraeli na Wamisri (yaani “umati wenye mchanganyiko,” kama vile Kut. 12:38). Katika muktadha huu watu walidai kuwa na uweza au uhusiano wa kiroho (yaani, wapandisha pepo) kwa ajili ya kuwasiliana na wafu (kama vile Law. 19:31; 20:6,27; Nya. 18:11; I Sam. 28:8; II Fal. 21:6; II Nya. 33:6; Isa. 8:19; 19:3). Hawa walikuwa wakitafuta ujumbe uliohusu maisha yao na ulinzi wa ubaadae wao, tofauti na YHWH. Jambo hili linasababishwa na

1. asili ya utu ulioanguka
2. makuhanii /manabii wenye ulaghai

3. tendo la kimapepo
4. kuitafuta nguvu ya kimiungu juu ya maisha yetu na maisha ya wengine

▣ Mistari miwili ya mwisho ya mst. wa 1 inafanana.

1. miungu ya Misri itatetemeka, BDB 631, KB 681, *Qal* ya WAKATI TIMILIFU, kama vile 6:4; 7:2 (mara mbili); 19:1; 24:20 (mara mbili); 29:9; 37:22
2. roho ya Wamisri itayeyuka pamoja nao, BDB 587, KB 606, *Niphal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 13:7; Yos. 2:11; 5:1; 7:5 (yaani, “vita takatifu” istilahi)

**19:2** Mtu anastaajabu kama hili linahusiana na

1. ujuzi wa kijeshi wa viongozi wa Nubia dhidi ya Wamisri wenyeji wa eneo la Delta
2. migogoro kati ya miji tofauti ya Misri, kila sehemu ikiwa na miungu wake

Hii migogoro ya ndani kwa ndani kati ya watu wale wale na maadui zao ni mfano mwagine wa “vita takatifu” (yaani, Amu. 7:22; I Sam. 14:20; II Nya. 20:23).

▣“nita. . .” Isaya anazunguza moja kwa moja kumhusu YHWH (mist. 2,3,4). YHWH husababisha

1. vita ya wenye kwa wenye kwa wenye, mst. 2
2. kukatiana tamaa,mst. 3a
3. ushauri wenye/ mipango yenyenye mkanganyiko, mst. 3b
4. utegemeki juu ya miungu ya uongo, mst. 3,c,d
5. kuja kwa kiongozi katili, mfalme mwenye nguvu, mst. 4

○

**NASB, REB**      “Nitamimina”

**NKJV**            “Nitaweka”

**NRSV, TEV,**

**NJB, LXX,**

**Peshitta**        “Nitachanganya”

Hiki KITENZI (BDB 696 I au BDB 1127) kinatumika mara mbili katika shina la *Pilpel* (Isa. 9:11 na hapa). Katika muktadha huu hiki kinaonekana kumaanisha

1. kuchanganya
2. kukaripia
3. kumimina (mzizi wa lugha ya ki-Ethiopia)

Mzizi wa lugha ya Kiarabu unamanisha “kunuka” (kama vile NIDOTTE, juzu. 3, uk. 233).

**19:3“nitayabatilisha”** Huu ni mzizi wa Kiebrania (BDB 118 I) mara nyingi unamaanisha “kuppotea.” Wasomi wengi wanadhani hii ni maana ya pili ya mzizi ule ule, “nitayabatilisha” au “kanganya” (BDB 118 III, kama vile 3:12; 9:15; 28:7).

**19:4** Katika muktadha huu (kama vile 20:4) neno hili lingeweza kurejelea juu ya (1) Ashuru (kama vile sura 20) au (2) wavamizi wa Nubi (kama vile sura ya 18). Istilahi ile ile inatumika juu ya Babeli katika Yer. 46:26; Eze. 29:19. YHWH anaziongoza himaya za ulimwengu kwa makusudi yake.Yakupasa kufanya uamuzi kama hii inafanana na uchochezi wa kiuaminifu wa, ni kawaida sana katika ulimwengu wa kale, ama ukwelii(yaani, mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia). Waandishi waliovuviwa wanaichukua istilahi ya Mashariki ya Karibu ya Kale na kuitumia kwa YHWH.

Tofauti yake I katika suala la imani! Je? Biblia ndiyo ya kipekee, iliyovuviwa, yenyenye kujifunua kwa ufunuo wa Mungu mmoja? Hili ni jambo! Angalia mahubiri yangu katika “Kwa nini Naliyamini Agano la Kale” na “Kwa nini Naliyamini Agano Jipy” mtandaoni katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) katika kipengele cha “Semina ya Ukalimani wa Kibiblia” (video ya Semina ya iliyoboreshwa 2009, Somo la 3).

“nitawatoa” Hiki KITENZI (BDB 698, KB 755, *Piel* cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kuabidhi kwa” (kama vile Targums, LXX, Peshitta). Hii *Piel* inaonekana hapa tu. Hiki KITENZI Hakioneekani katika *Niphil* iliyo katika Mwa 8:2 na Zab. 63:12, ambapo hiki kinamaanisha “kustishwa.” Hii maana nyingine ya *Piel* inatokana na mzizi wa Kiaramu cha kale. Hivyo, huenda kuna mizizi ya Kiebrania iliyojitenga.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:5-10**

<sup>5</sup>Na maji ya baharini yatapunguka,  
na huo mto utakauka na kuwa pakavu.  
<sup>6</sup>Na vijito vya mto vitatoa uvundo,  
na mifereji ya Misri itakuwa haina maji mengi, itakauka;  
na mianzi itanyauka.  
<sup>7</sup>Vitu vimeavyo karibu na Nile,  
katika ukingo wa Nile, na vyote vilivyopandwa karibu na Nile vitakauka  
na kuondolewa na kutoweka.  
<sup>8</sup>Na wavuvi wataugua, na wote wavuao kwa ndoana watahuzunika,  
nao watandao jarife juu ya maji watazimia.  
<sup>9</sup>Tena wao wafanyao kazi ya kuchana kitani watafadhaika,  
na hao pia wafumao bafta.  
<sup>10</sup>Na nguzo za nchi zitavunjika vipande vipande,  
wote wafanyao kazi ya mshahara watahuzunika nafsini mwao.

**19:5-10** Huu ubeti unaeleza juu ya hukumu ya YHWH juu ya Misri.

1. maji yao mengi yatokayo Nile yanakauka.
2. kwa madhara yake mimea ya mto inakauka.
3. kwa madhara yake mazao yanayomwagiliwa yanakauka.
4. kwa madhara yake kiwanda cha samaki kitanung’unka na kudhoofika.
5. Kwa madhara yake kiwanda cha kutengeneza mavazi kiestisha.
6. jamii ya Kimisri ilikuwa katika unyanyasikaji, usagaji wa nafaka ilistishwa.
7. Watenda kazi wote watahuzunika.

Kuna VITENZI vitatu vyenye uhusiano ambavyo vinadokeza juu ya upotetu wa maji.

1. “yatapunguka,” BDB 677, KB 732, *Nipha* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, mst. 5; 41:17;
2. “utakauka,” BDB 351, KB 349, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, mist. 5,6; 11:15; 37:25; 44:27; 50:2; 51:10
3. “itakauka,” BDB 386, KB 384, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, mist. 5,7; 15:6; 27:11; 40:7,8,24; 42:15 (mara mbili); 44:27

Uwezo wa Mungu wa kuyatawala maji (nyenzo pekee za vitu ambavyo Mungu hakuviumba kwa kutamka katika Mwanzo 1) unarudiwa rudiwa katika Agano la Kale.

1. maji yaliyotengwa juu ya maji ya chini, Mwa. 1:7
2. maji yaliyokusanyika ili kwamba nchi kavu ioneckane, Mwa. 1:9-10
3. mafuriko yaliyotumwa, Mwa. 7:4,7
4. mafuriko yaliyokauka, Mwa. 8:2-3
5. maji ya chemchemi aliyopewa Hajiri, Mwa. 21:19
6. kuigawanya na kuirejesha Bahari ya Reeds, Kut. 14:16,27
7. kuyatakasa maji huko Mara, Kut. 15:22-25
8. kutoa maji kutoka mwambani katika kati ya jangwa, Hes. 20:8,11
9. wingi wa mazao uliohaidiwa kama wangel agano, Kumbukumbu la Torati 27-28
10. kuugawa mto Yordani, Yos. 3:14-17; 4:23-24
11. kukauka kwa mto Nile na vijito vyake, Isa. 19:5
12. kukauka kwa mto Frati, Uf. 16:12
13. maji kutiririka kutoka katika hekalu jipya (Eze. 47:1) kutoka Yerusalem (Zek. 14:8) na katika mji mpya wa mbinguni, Ufu. 22:1

Kwa watu wa jangwani hakika hii ilikuwa miujiza mikubwa na uhakikisho wa nguvu za Mungu kwa sababu maji yalikuwa ishara ya uhai. Kumbuka, mto Nile ultazamiwa kama moja ya miungu uya Misri (kama alivyokuwa Re, mungu juu, kama vile mst. 18).

**19:6“vitatoa uvundo”** Hiki KITENZI (BDB 276 II, KB 276, *Hiphil* cha KAULI YA WAKTI TIMILIFU) kinajitokeza hapa pekee. Hiki kinaonekana kuakisi mzizi wa Kiaramu. Mazao mengi yalianza kuoza!

**19:9**

NASB, NJB	“nguzo za nchi”
NKJV	“kanzu nzuri”
NRSV, REB	“yatabadili rangi”
LXX	“mavazi”
JPSOA	“yenye kuchukiza”

Toleo la MT lina kifungu חָרְרִי, “nguo nyeupe” (kwa ufanano wa Kiaramu angalia Dan. 7:9), lakini ufanano zaidi unaendana na חָרְרִי (, “kubadili rangi” (kama vile Isa. 29:22 na DSS ya andiko hili). Ni dhairi kuwa kuna mzaha uliokusaudiwa kuhusu “nyeupe” (חָרְרִי, BDB 301).

**19:10**

NASB	“nguzo”
NKJV, JPSOA	“misingi yake”
NRSV, TEV,	
NJB	“wachanaji wake”

Toleo la MT (BDB 1011, hapa pekee) lina kifungu “msingi” au “pumziko” (la jamii), ambacho kingerejelea juu ya watawala wa tabaka la juu. Neno “Wafumaji” linatokana na wale wanaotazamia ufanano linganifu wa neno “wafanyakazi wa mshahara” (DSS, Targums kutoka mzizi wa Kiaramu, “wachanaji”) katika mstari wa pili. Swalii ni hili, “Jel! ufanano huu ni wa visawe (wachanaji) au ni wa kiupinzani (tabaka la juu ya tabaka la chuini)?” Hili andiko la Kiebrania linabaki kuwa la kitata (kama vile LXX na Peshitta).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:11-15

<sup>11</sup>Wakuu wa Soani wamekuwa wapumbavu kabisa;  
washauri wenyewe hekima wa Farao, shauri lao limepumbazika;

mwawezaje kumwambia Farao, Mimi ni mwana wa wenyewe hekima, ni mwana wa wafalme wa zamani?

<sup>12</sup>Wako wapi, basi, watu wako wenyewe hekima?

Na wakuambie sasa;

na wajue mambo aliyokusudia Bwana wa majeshi juu ya Misri.

<sup>13</sup>Wakuu wa Soani wamekuwa wapumbavu,

wakuu wa Nofu wamedanganyika;

na hao walio mawe ya pembeni ya kabilia zake wameikosesha Misri.

<sup>14</sup>Yeye Bwana ametia roho ya ushupavu katika moyo wa Misri,

nao wameikosesha Misri katika matendo yake yote, kama mlevi aendavyo huko na huko akitapika.

<sup>15</sup>Wala haitakuwako kazi yo yote katika Misri iwezayo kufanywa,

ya kichwa au ya mkia, ya tawi au ya nyasi.

**19:11-15** Ubeti huu ni ufanuzi wa mst. 3.

1. mst. 11, “wakuu wa Soani” (Tanisi, makao ya eneo la Delta) kwa ujumla ni wapumbavu (BDB 17, hili linatumika kumaanisha Yuda katika Yer. 4:22)
2. mst. 11, “washauri wenyewe hekima wa Farao wamepumbazika” (kifasihi. “ukatili,” BDB 129 II, KB 146, *Niphil* ya KAULI ENDELEVU, kama vile Yer. 10:14,21; 51:17)

3. mst. 13, "wakuu wa Soani wamekuwa wapumbavu" (BDB 383, KB 381, *Niphil ya KAULI ENDELEVU*, kama vile Yer. 5:4; 50:36)
4. mst. 13, "wakuu wa Memfisi (Nofu, makazi mengine ya Misri) wamedanganyika Misri" (BDB 674, KB 728, *Niphil ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU; Hiphil YA WAKATI TIMILIFU* inatumika katika Mwa. 3:13)
5. mst. 13, "wameikosesha Misri" (BDB 1073, KB 1766, *Hiphil ya KAULI TIMILIFU*, kama vile mst. 14; 3:12; 9:16; Yer. 23:13,32; Hos. 4:12; Mika 3:5)
6. mst. 14, "wameikosesha . . matendo" (KITENZI kile kile kama #5, hapa kinadokeza juu ya giza)

**19:11** Mstari wa4 ni wa kinahau wa kwa lile kundi la wenyeh hekima, sawasawa kile alichokoshiriki Danieli ndani ya Babeli. Hili neno "mwana" linatenda kazi kama "mmoja wa kundi hili."

**19:12** YHWH anawauliza swali kimzaha lenye kufahamika kwa majibu yake. Hili linafuatiwa na KAULI mbili za WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 616, KB615, na BDB 393, KB 390) linatumika katika maana ya KAULI AMRISHI (yaani, "na wa . . .").

Walidai kuwa wenyeh hekima (mst. 11d; I Fal. 4:30; Matendo 7:22). Walidai kuwa na mipango (mst. 3b), lakini hekima na mipango yao haikubaliwi katika makusudi ya YHWH (v. 12a).

**19:13** "hao walio mawe ya pembedi" Hapa kifungu "mawe ya pembedi" (BDB 819) kinadokeza juu ya watawala (kama vile Amu. 20:2; I Sam. 14:38).

#### **19:14**

NASB, LXX	"ametia"
NKJV, Peshitta	"amehusianisha"
NRSV, JB	"amemimina"
REB, NJB	"amejaza"

Toleo la MT lina KITENZI "ametia" (אַמְתִּיא, BDB 587, KB 605, *Qal cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), ambacho kinadokeza kinywaji kikali (kama vile 5:22). Hata hivyo, kwa sababu ya Isa. 29:10 huenda KITENZI lazima kiwe לְבָשׂ ("kumimina," BDB 650, KB 703, *Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), ambayo inapatikana katika DSS. Aidha katika hali hii kiini ni giza kama stiari ya mkanganyiko na ukosefu wa amani.

**19:15** Mstari wa pili una nahau mbili ambazo zinadokezaviwango vyote vya jamii (kama vile 9:14-15).

1. kichwa – mkia
2. tawi – nyasi

Kutakuwa na jambo litalotumwa toka kwa Mungu (kama vile mst. 14a) kukosa uwezo mja kwa moja! Wale waliodai kuwa wenyeh hekima (kama vile mst. 11d, 12a,13c) wamehakikishwa kuwa wapumbavu kwa sababu wanaamini katika (1) miungu ya uongo; (2) dini za uogo; na (3) mipango iliyo miovu (kama vile mst. 3)! Uhusiano wote wa Misri (kama vile mst. 11-12), ya kiutawala na kidini, iko nje ya utendaji, ni kama wafanyakazi wake wote (kama vile mist. 8-10).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:16-17**

<sup>16</sup> Katika siku hiyo Misri itakuwa kama wanawake; itatetemeka na kuogopa kwa sababu ya kutikiswa kwa mkono wa Bwana wa majeshi, autikisao juu yake. <sup>17</sup> Na nchi ya Yuda itakuwa sababu ya utisho kwa Misri; kila mtu atakayeambiwa habari zake ataingiwa na woga, kwa sababu ya kusudi la Bwana wa majeshi, analolikusudia juu yake.

**19:16-17** Kifungu hiki kinaeleza matendo ya YHWH (yaani, "kutikiswa kwa mkono wa Bwana wa majeshi") atakayoyoatenda, makusudi yake (mst. 17b, BDB 420).

1. Wamisri watakuwa kama wanawake, mst. 16
2. itatetemeka, mst. 16 (BDB 353, KB 350, *Qal ya KAULI TIMILIFU*)
3. watakuwa katika woga, mst. 16 (BDB 808, KB 922, *Qal ya KAULI TIMILIFU*)

4. Yuda atakuwa utisho kwa Misri, mst. 17 (KITENZI, *Qal* chakauli timilifu, NOMINO, “utisho,” BDB 291, lakini kinapatikana hapa pekee)
5. Watakuwa katika woga, mst. 17 (BDB 808, KB 922, *Qal* ya KAULI TIMILIFU, angalia #3)

**19:16“Bwana wa majeshi”** Kamakifungu“katika siku hiyo” kianavyounganisha mistari hii mitano ya beti tano (kama vile mist. 16, 18, 19, 23, 24), ndivyo jina hili la YHWH la mara kwa mara (kama vile mist. 16, 17, 18, 20, 25 na BWANA lilivyo pekee katka mist. 19, 20, 21, 22). Mungu wa agano ni mtendaji katika hizi beti za ukombozi zenye kustaajabisha kwa mataifa!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:18**

<sup>18</sup> Katika siku hiyo itakuwako miji mitano katika nchi ya Misri itumiayo lugha ya Kanaani, na kumwapia Bwana wa majeshi; mji mmoja utaitwa Mji wa uharibifu.

**19:18** Hii ni aya iliyojitenga. Inadokeza wongofu kutoka kuabudu sana hadi kumwabudu YWHH.

Hii “lugha ya Kanaani” ingeweza kudokeza Kiebrania (BDB 488 I). Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 6:5 au hata Mwa. 11:1.

Hiki kifungu “kumwapia” (BDB 989, KB 1396, *Niphah* ya KAULI ENDELEVU) kinadokeza uhusiano wa Mungu wa Yuda (kama vile mist. 19-22, 23, 24-25). Mara kwa mara hii imekuwa sababu ya hukumu yak i-Ungu!

▣“Katika siku hiyo” Kielewe hiki kifungu cha mara kwa mara, “katka siku hiyo,” mist. 16, 18, 19, 23, 24. Hiki kinagusia moja kwa moja ubaadaye wa kipekee wa siku zijazo.

1. hukumu mja katika woga, mist. 16-17
2. hukumu moja katika wongofu (mist. 18, 19-22) na ibada za ulimwengu mzima (mist. 23, 24-25)

Tena, majanga ya sasa (kama vile mst. 20) katika ANE yanadokeza tukio la siku za mwisho. Hukumu ina mpango wa ukombozi (kama vile mst. 22). Uovu, uasi, na ujinga ndilo litakalokuwa neno la mwisho! YHWH anao mpango wa milele wa ukombozi kwa ulimwengu mzima (kama vile mst. 24b).

▣“miji mitano” Sababu ya namba hii ya kipekee haijulikanai. Kifungu hiki kinadokeza wongofu, lakini si wogofu (yaani, nusu ya kumi, angalia Mada Maalumu: Ishara na Tarakimu katika Maandiko katika 11:12) kamili.

Swali linabaki, “Kifungu hiki kinamrejelea nani?”

1. miji ya wakolono wa Kiyahudi
2. miji ya miungu ya Kimisri

Kwa sababu ya mist. 19-22, 23, 24-25 Nachagua uchaguzi #2. Muktadha huu hauwazungumzii Wayahudi, bali Wamisri.



**NASB, NKJV      “Mji wa uharibifu”**

**NRSV, TEV,**

**NJB                “Mji wa Jua”**

Neno la toleo la MT lenye kuzungumzia “uharibifu”( BDB 249) linaonekana hapa pekee. KITENZI cha mzizi ule ule (BDB 248) kinamaanisha “kuangusha,” “kustisha,” au “kumimina chini.” Hiki kinaweza kuwa neno la kimasihara lenye kuzungumzia mji wa Misri ambaulikuwa ukimwabudu mungu “Jua” (katika Heliopolis).

1. סְרָה, mji wa Jua (BDB 357, kama vile DSS, Targums, Vulgate)
2. סְרָה, mji wa uharibifu. Maana yake ni kwamba yale mahekalu ya Re (mungu Jua) yamebomolewa.

Neno la Kiebrania “jua” lina konsonanti kamas “ban” (yaani, yenye shauku ya uharibifu). Kunaweza kuwa na neno la kimasihara mara mbili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:19-22**

<sup>19</sup> Katika siku hiyo itakuwako madhabahu katika nchi ya Misri kwa Bwana, na nguzo mpakani mwake kwa

**Bwana.**<sup>20</sup> Nayo itakuwa ishara na ushuhuda kwa Bwana wa majeshi katika nchi ya Misri; kwa maana watamlilia Bwana kwa sababu ya watu wawaoneao, naye atawapelekea mwokozi mwenye kuwatetea, naye atawaokoa.  
**21** Na Bwana atajulikana na Misri, na Wamisri watamjua Bwana katika siku hiyo; naam watamtumikia kwa dhabihu na matoleo, nao watamwekeea Bwana nadhiri, na kuzitekeleza.<sup>22</sup> Naye Bwana atapiga Misri, akipiga na kuponya; nao wakirudi kwa Bwana, atakubali maombi yao na kuwaponya.

**19:19**

**NASB, NKJV,**

**Peshitta** “kati ya nchi ya Misri”

**NRSV, NJB** “katikati ya nchi ya Misri”

**REB** “ndani ya moyo wa Misri”

**LXX** “katika mipaka yake”

Matumizi ya neno hili (BDB 1063) katika Yushaua. 3:17; 4:3,9,10,18 lazima yaelewaka kama “mpakani,” si “katikati.” Hii ndiyo asili ya kifungu “kwa mipaka yake” katka LXX. Je! Tukio hili lilitukia lini?

1. Hekalu dogo la Kiyahudi lilijengwa na jeshi ka Kiyahudi katika kisiwa kilicho katika mto Nile (Elephantine, Aswani ya sasa, katika maporomoko ya kwanza ya mto Nile), wakati mwingine kabla ya 525 K.K
2. Hili hekalu la Kiyahudi (liliboreshw baada ya kujengwa kwa hekalu humo Yerusalem) lilijengwa huko Leontopolis na Onias IV, kuhani mkuu Myahudi wa kigeni kutoka Yerusalem, mnamo 160 K.K. (kama vile Josephus, Antiq.12.9.7;13.3.3)
3. Tukio la siku za mwisho 19:19-20

**19:19-20** Tazama namna inavyoshangaza, lakini tukio la kustaajabisha kwamba uwepo wa YHWH wa kimwonekano utaimarishwa katika Misri.

**19:20** Kitendo hiki kinalinganishwa na namnaHWH alivyoshughulikia na Israeli katika kitabu cha Waamuzi. Hukumu kali ya uvamizi na umilikaji (kama vile mst. 4) inasababisha toba na imani katika Mungu na katika uwezo wake na mapenzi yake katika kufanya jambo la ukombozi. Misri imekuwa katika hali hiyo na YHWH anakubali. Ushahidi mkuu wa muktadha huu unahu tabia ya Mungu wa Israeli. Yeye asamehe kwa hiari na kwa ukamilifu anawakubali maadui wa watu wake wa agano. Hakika yeye ndiye Mungu wa mataifa, Mkombozi wa ulimwengu (kama vile Yohana 3:16; Tito 1:3; 2:10; 3:4).

▣“mwokozi na mshindi” Katika muktadha huu kifungu hiki kinarejelea ju ya yule ambaye alimshinda bwana katili na mwenye nguvu wa mst. 4, lakini pia kina maana za ki-Masihi. Katika neno hili “Mwokozi” huyu ni YHWH mwenyewe na si mwingine (kama vile 43:3,11; 45:15,21), lakini kutokana na Agano Jipya huyu alikuwa Masihi aliyekuwa akitenda kazi kama mwakilishi wa YHWH (yaani, Isa. 28:16; Rum. 9:30-33; 10:9-13; I Pet. 2:6-10).

1. Mwokozi, BDB 446, KB 448, *Hiphi* ya KAULI ENDELEVU
2. mtetezi, BDB 936, KB 1224, *Qal* ya KAULI ENDELEVU
3. mkombozi, BDB 664, KB 717, *Hiphil* ya KAULI TIMILIFU

**19:21** “Bwana atajulikana na Misri, na Wamisri watamjua Bwana katika siku hiyo” Hili neno la kimasihara la neno la Kiebrania “kujuwa” (BDB 393, KB 390), ambalo linadokeza maarifa yote na uhusiano binafsi pamoja naye.

### **MADA MAALUM: AKAMJUA (kama ilivyoelezewa kutoka Kumbukumbu la Torati)**

Neno la Kiebrania “kujuwa”(yada, BDB 393, KB 390) lina maana kadhaa (mazingira ya kimaana) katika shina la neno *Qal*.

1. Kuelewa mema na mabaya - Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yona 4:11
2. Kujuwa kwa kuelewa - Kumb. 9:2,3,6; 18:21

3. Kujua kupitia mazoea - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Yos. 23:14
4. Kufikiri - Kumb. 4:39; 11:2; 29:16
5. kujua kibinafsi
  - a. Mtu - Mwa. 29:5; Kut. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9, Yer. 1:5
  - b. mungu -Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
  - c. YHWH - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
  - d. Kujamiiana - Mwa. 4:1,17,25; 24:16; 38:26
6. ujuzi wa kujifunza - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. Kuwa mwenye hekima - Kumb. 29:4; Mit. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. maarifa ya Mungu
  - a. kwa Musa - Kumb. 34:10
  - b. kwa Israeli- Kumb. 31:21

kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya kibiblia ni ushirika wa ndani, wa kila siku, unaokua pamoja na Mungu (angalia Mada Maalum: *Koinōnia*). Sio sheria pekee au maisha ya kiadilifu pekee. Ni imani binafsi ya kiushirika. Hii ndio sababu Paulo alitumia nyumba ya mshirika katika Efe.5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa.

▣“kuabudu” Tambua viashiria vya kuabudu (BDB 712, KB 773, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) iliyotajwa.

1. dhabihu, BDB 257
2. sadaka, BDB 585
3. kiapo, BDB 623, KB 674, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Hawatafanya taratibu za ibada tu, bali wataziacha (BDB 1022, KB 1532, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, lit.“kamilisha”) taratibu hizo (yaani, viapo).

**19:22** Matendo yaYHWH juu ya Misri kuyaiga matendo yake juu ya watu wake wa agano.

1. anawashambulia (mara mbili, BDB 619, KB 669)
2. wanamlilia, mst. 20
3. anawaponya (mara mbili, BDB 950, KB 1272)
4. wanamrudia (BDB 996, KB 1427,hili ni neno la Kiebrania lenye kumaanisha toba)
5. anawasikiliza (BDB 801 I, KB 905, *Niphal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, angalia KAULI YA WAKATI TIMILIFU katika Mwa. 25:21; II Nya. 33:13; Ezra 8:23. YHWH husikia na kujibu ombi la toba).

Hakikisha unatambua kwamba hukumu (yaani, ishara) ilikuwa kwa ajili ya kusudi la kuhimarisha (au kwa ajili ya Israeli, kurejesha) uhusiano na YHWH.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:23

<sup>23</sup> Katika siku hiyo itakuwako njia kuu itokayo Misri na kufika hata Ashuru; Mwashuri atafika Misri, na Mmisri atafika Ashuru, na Wamisri wataabudu pamoja na Waashuri.

**19:23** Kutakuwa na mwingiliano huru kati ya mataifa kwa kusudi la kumwabudu YHWH.

Mataifa yatakuja!

Inatia hamasa namna Isaya alivyotumia tamathali za hii njia kuu.

1. njia kuu kwa kurudi kwa Wayahudi toka uhamishoni, 11:16; 57:14
2. njia kuu kwa Mataifa ya waabuduo kurudi, 19:23
3. njia kuu ya utakatifu, 26:7; 35:8; 43:19; 49:11; 51:10
4. njia kuu ya Kimsahi, 40:3; 42:16

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 19:24-25**

<sup>24</sup>Katika siku hiyo Israeli atakuwa wa tatu pamoja na Misri na Ashuru, watakuwa baraka kati ya dunia;  
<sup>25</sup>kwa kuwa Bwana wa majeshi amewabariki, akisema, **Wabarikiwe watu wangu Misri; na wewe Ashuru, kazi ya mikono yangu; na wewe Israeli, urithi wangu.**

**19:25** Hivi ni vifungu vya kimaagano ambavyo sasa vinatumika kwa Wamisri na Waashuru waliochukiwa. Linganisha na 45:14-17. Ni tofauti iliyo je. Ni vigumu sna kuviweka hivi kwa pamoja (yaani, mataifa yaliyopendwa, mataifa yaliyohukumiwa). Nachagua mst. 22! Nachagua mst. 20!

## ISAYA 20

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Unabii kuhusu Misri Na Kushi	Ishara dhidi ya Misri na Kushi	Dhidi ya Misri	Ishara ya nabii aliyejkuwa utupu	Kuhusiana na kukamatwa kwa Ashdodi
20:1-6	20:1-6	20:1-6	20:1-6	20:1-6

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-a ya kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 20:1-6**

<sup>1</sup> Katika mwaka ule jemadari Yule alipofika Ashdodi, alipotumwa na Sargoni mfalme wa Ashuru; naye alipigana na Ashdodi akautwaa. <sup>2</sup> wakati huo Bwana alinena kwa kinywa cha Isaya, mwana wa Amozi, akisema, Haya, uvue nguo ya magunia viunoni mwako, na viatu vyako miguuni mwako. <sup>3</sup> Naye akafanya hivyo akaenda uchi, miguu yake haina viatu. Bwana akasema, Kama vile mtumishi wangu Isaya anavyokwenda uchi, hana viatu, awe ishara na ajabu kwa muda wa miaka mitatu juu ya Misri na juu ya Kushi; <sup>4</sup> vivyo hivyo mfalme wa Ashuru atawachukua uchi, wafungwa wa Misri, na watu wa Kushi waliohamishwa, watoto kwa wazee, hawana viatu, matako yao wazi, Misri iaibishwe. <sup>5</sup> Nao watafadhaika, na kuona haya kwa ajili ya Kushi, matumaini yao, na Misri, utukufu wao. <sup>6</sup> Na mwenyeji wa nchi ya pwani atasema katika siku hiyo, Angalia, haya ndiyo yaliyowapata watu wale tuliovatumaini, ambao tuliwakimbilia watuokoe na mfalme wa Ashuru; na sisi je! Twawezaje kupona?

**20:1** Aya hii inawapa wasomaji wa leo muundo kamili wa kihistoria ya hukumu ya YHWH juu ya Wafilisti kwa maelezo ya kuanguka kwa Ashdodi (moja ya miji mitano mikubwa ya nchi ya Ufilisti-Ashdodi, Ashkeloni, Gaza, Gathi, Ekonni). Kuanguka kwa mji mmoja kulimaanisha ni anguko la miji yote (angalia Mshauri wa mwanzo katika 14:28-32). Waliangamizwa mara mbili (1) na Sargon II (aliyetajwa hasa katika Agano la Kale hapa tu, alitawala toka mwaka 722-705 K.K.), mfalme wa Ashuru. Katika mwaka 713 K.K. mfalme wa Ashdodi, Azuri, aliasi na katika mwaka 711 K.K. jeshi la Sargon II lilikuja na kuuzuia uasi na (2) na Senakarebu katika 705-701 K.K.

Hata hivyo, sura hii haitengenezi ushauri mpya kuhusu kuangamizwa kwa Ufilisti (au “uwanda wa Pwani,” kama vile mst. 6), lakini mwendelezo wa hukumu juu ya Kushi/Misri, ulioelezewa katika sura ya 18. Udhaliilishaji wa

Ashdodi ulikuwa ni kivuri cha aibu, wenyе kufedhehesha mateka wa Misri na majeshi ya Ashuru juu ya matukio tofauti mbalimbali ya kihistoria. Sehemu za jeshi la Kimisri walikamatwa na kuchukuliwa mateka.

■“**Jemedali**” Neno (BDB 1077) linamaanisha kamanda wa vita (kama vile. II Fal. 18:17 na pia kumbuka Isa. 36:2, ambapo jina la jenerali katika II Wafalme 18 linatokea, lakini sio cheo chake).

**20:2** Isaya anaambiwa kuelezea (au kutoeleza) njia Fulani kuonyesha kanuni za kuomboleza za kitamaduni zilizopo (angalia Mada Maalum katika 15:2-3), lakini pia kuonyesha aibu, juu ya kushindwa kwa Ashuru na mateka wa mataifa mbalimbali.

1. Ashdod (Filistia)
2. Misri
3. Kushi au ufanano wa Misri wa tawala 25 za koo ambazo ziliwu za Wanubi.

Kile kilichotokea kwa Ashdodi kwa miaka mitatu kingalitokea kwa Misri (kama vile mst. 3).



**NASB, NRSV,**

Peshitta	“ <b>kuvua nguo za magunia</b> ”
NKJV	“ <b>uvue nguo ya magunia</b> ”
TEV, LXX	“ <b>vua. . .nguo za magunia</b> ”
REB	“ <b>vua</b> ”

KITENZI kilichozoleka (BDB 834, KB 986, *Piel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kimsingi kinamaanisha “kuweka wazi.” Kwa hiyo swali ni, “je inamaanisha ‘kulegeza’ (majonzi) au ‘kuvua’ (aibu)?”

1. “ondoa,” NIV, Zab. 30:11; toleo la NASB lina neno “legeza,” lakini likimaanisha “kuvua” katika Isa. 52:2; Yer. 40:4
2. “kulegeza,” Isa. 5:27

Kwa kawaida kuva “nguo za magunia” (BDB 974) kungalimaanisha hali ya kuomboleza, kama ambavyo ungalikwenda pasipo viatu (kama vile Mika 1:8), lakini yawezekana kuwa Isaya aliondoa alama ya utambulisho wake wa kinabii (“vazi lenye usinga,” BDB 12 MUUNDO WA MANENO, BDB 972, kama vile Mt. 3:4). Kama hili ni sahihi hivyo basi andiko haliongelei kuhusu kubaki uchi (lakini “kubaki uchi,” BDB 736 katika mistari ya 2,3,4 inawezekana, kama vile Mwa. 2:25). Hata hivyo, wengi wanaolitumia neno “kwenda uchi” humaanisha kwa namna Fulani ni kutokuwa na nguo (kama vile 47:1-3; I Sam. 19:24; II Sam. 6:14,20; Amosi 2:16; Mika 1:8; Yn 19:23; 21:7).

**20:3 “iwe ishara” NOMINO ,“ishara” (BDB 16), linatumika**

1. Kama alama ya muda, Mwa. 1:14
2. Kama alama ya mtu, Mwa. 4:15
3. Kama alama ya agano, Mwa. 9:12,13,17; 17:11
4. Kama alama ya imani juu ya ahadi, Kut. 3:12
5. Kama muujiza wa kuwadhihirisha wawakilishi wa Mungu (yaani Musa), Kut. 4:8 (mara mbili), 9,17,28,30; 7:3;8:23, n.k.
6. Kipimo cha makabila, Hes. 2:2; Zab. 74:4
7. Kama onyo, Hes. 16:38; 17:10

Mara nydingi limetumika katika kitabu cha Isaya.

1. Uzao wa kipekee, 7:14
2. Wana wa Isaya, 8:18
3. Madhabahu na nguzo huko Misri, 19:20
4. Vazi la Isaya, 20:3
5. mavuno, 37:30
6. kuitahadharisha Yerusalem juu ya Ashuru, 38:7
7. uponyaji wa Hezekia, 38:22

8. ishara za uongo, 44:25
9. Baraka za mashambani, 55:13
10. Kufanya umisheni kwa mataifa, 66:19

◎

<b>NASB</b>	“alama”
<b>NKJV, Peshitta</b>	“ajabu”
<b>NRSV, REB,</b>	
<b>NJB, LXX</b>	“ishara”

Neno “ajabu,” “ishara,” “alama” (BDB 68) ni visawe vya neno “chapa,” “nembo” (BDB 16). Linatumika mara nydingi katika kitabu cha Kutoka na Kumbukumbu la Torati, lakini mara mbili tu katika kitabu cha Isaya (yaani., 8:18 na 20:3).

BDB ina matumizi mawili makuu.

1. Udhahirisho maalumu wa nguvu za Mungu
2. Alama ya matukio ya mbeleni au ishara ya kitendo kinachomaanisha matukio ya mbele (kama vile Zak. 3:8).

#### **20:4** Hii aya inaelezea juu ya mateka.

1. Vijana na wazee kuchukuliwa (lahaja kwa ajili ya jamii nzima ya watu)
2. Kwenda uchi (BDB 736, lahaja kwa ajili ya fedheha, na bado alivaa nguo za ndani zenye kubana)
3. Kwenda pasipo viatu (BDB 405, lahaja kwa ajili ya kuomboleza)
4. Matako yaliyowazi (BDB 1059, hapa tu na II Sam. 10:4, lahaja ya fedheha)
5. aibu/kubaki uchi (BDB 788, angalia picha za ukutani za Waashuru)

Aya inaweka wazi kuwa Isaya alishangaa kuona jamii yake ikienda nusu uchi kwa muda wa mika mitatu ili kuelezea ukweli wa kithiolojia/unabii. Kutembea uchi ilikuwa ni sehemu ya laana kwenye Kumbukumbu la torati (kama vile 28:48), ambayo ilimaanisha mateka.

#### **20:5** Kwa sababu ya imani ya Kushi/Misri kwao wenywewe (yaani., jeshi, hekima, mali, dini) watakuwa

1. wakishangaa, BDB 369, KB 365, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 7:8; 8:9 (mara tatu); 9:4; 20:5; 30:31; 31:4,9;37:27; 51:6,7
2. wataaibishwa, BDB 101, KB 116, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 1:29; 19:9; 20:5; 24:23; 26:11; 29:22; 30:5; 37:27; 41:11; 44:9,11 (mara mbili); 45:16,17,24; 49:23; 50:7; 54:4; 65:13; 66:5

Dhahiri kuna maneno mawili ambayo ni sehemu muhimu ya ujumbe wa Isaya, yote hasi na chanya!

**20:6** Aya hii inamuunganisha Ashdodi (mst. 1) na wakazi wote waishio katika uwanda wa Pwani ya Palestina. Inavyoonekana Wamisri waliahidiwa msaada wa kijeshi, kama Waashuru watawavamia, lakini hawakufanya (kama vile 30:7; 31:3). Hapakuwepo na mtu wa kuwaokoa (kama vile 10:3). Hakika, aya hii inaunga mkono ujumbe wa Isaya kwa Hezekia alishirikiana na wa Misri (kama vile 30:1-5; 31:1-3).

## ISAYA 21

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mungu anaamuru Babeli kuchukuliwa	Anguko la Babeli linatangazwa	Dhidi ya Babeli	Maono juu ya anguko la Babeli	Anguko la Babeli
21:1-10 (1-5)	21:1-2 (1b-2)	21:1-10	21:1-2a 21:2b 21:3-4	21:1-5 (1-5)
(6-7) (8-10)	21:3-5 (3-5)		21:5	
	21:6-9 (6-9)		21:6-7	21:6-10 (6-10)
	21:10 (10)		21:8 21:9	
Ufunuo kuhusu Edomu na Arabuni	Tamko dhidi ya Edomu	Kuhusu Edomu	Ujumbe kuhusu Edomu	Juu ya Edomu
21:11-12 (11-12)	21:11-12 (11-12)	21:11-12 (11b-12)	21:11 21:12	21:11 21:12
21:13-15 (13-15)	Tamko dhidi ya Arabuni 21:13-15 (13-15)	Kuhusiana na Arabuni 21:13-15 (13-15)	Ujumbe kuhusu Arabuni 21:13-15	Dhidi ya Arabuni 21:13a 21:13b-15 (13b-15)
21:16-17	21:16-17	21:16-17	21:16-17	21:16-17

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Aya hii inaorodhesha mataifa mbalimbali yaliyozungumziwa na YHWH kuitia manabii wake, yote yakinambulishwa na alama ya fasihi, "ufunuo wenyewe kuyahusu."

B. Nimekwisha kutaja mapema kuwa nafikiri ufunuo uliomzungumzia "mfalme wa Babeli" kiukweli unashughulika na Ashuru (yaani., 13:1-14:27). Sura hii (yaani., mistari ya. 1-10) inaihusu Babeli.

Hii sio ile Babeli ya kale ya Nabonidus na Nebukadneza, lakini watu wa Ukaldayo walipitia kwenye chanzo cha Mto Tigris na Eufrati. Mji wao mkuu ungalikuwa ni Babeli na mfalme wao Merodach-baladan, aliyeasi katika mwaka wa 720 K.K, lakini alikuja kushindwa na Sargon II na kutorokea kwenye mabwawa na kukimbia huko Elam katika mwaka 710 K.K. (IVP Bible Background Commentary, uk.611). Mji wa Babeli uliangamizwa na Waashuru katika mwaka wa 703 K.K. na mfalme wa Ashuru akachukua mamlaka ya kuwa "mfalme wa Babeli."

C. Sura hii pia inazungumzia

1. Edomu, mistari ya 11-12
2. Arabuni, mistari ya 13-17

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21:1-10

<sup>1</sup> Ufunuo juu ya bara ya bahari.

Kama tufani za Negebu zikaribiavyo kwa kasi,  
inakuja kutoka bara, toka nchi itishayo.

<sup>2</sup> Nimeonyeshwa maono magumu;

atendaye hila anatenda hila,  
mharibu anaharibu.

Panda juu, Ee Elamu; husuru, Ee Umedi;

mimi ninakomesha maombolezo yake yote.

<sup>3</sup> Kwa sababu hiyo viuno vyangu vimejaa maumivu,

utungu umenishika, kama utungu wa mwanamke azaaye;

ninaumwa sana, nisiweze kusikia;

nimefadhaishwa wa hofu, nisiweze kuona.

<sup>4</sup> Moyo wangu unapiga-piga, utisho umenitaabisha,

gizagiza la jioni nilipendalo limegeuka likanitetemesha.

<sup>5</sup> Wanaandika meza, wanaweka ulinzi, wanakula, wanakunya.

Simameni, enyi wakuu, itieni ngao mafuta.

<sup>6</sup> Maana Bwana ameniambia hivi, Enenda, weka mlinzi;

aonayo na ayatangaze.

<sup>7</sup> Naye akiona kundi la wapanda farasi, wakienda wawili wawili,

na kundi la punda, na kundi la ngamia;

asikilize sana, akijitahidi kusikiliza.

<sup>8</sup> Ndipo akalia kama simba,

Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana,

na kila usiku ninakaa katika zamu ya ulinzi wangu.

<sup>9</sup> Na, tazama, linakuja kundi la watu, wapanda farasi, wakienda wawili wawili.

Akajibu na kusema, Babeli umeanguka, umeanguka;

na sanamu zote za miungu yake zimevunjwa chini.

<sup>10</sup> Ewe niliyekufikicha, na nafaka ya sakafu yangu;

Hayo niliyoyasikia kwa Bwana wa majeshi,

Mungu wa Israeli, nimewapasha habari zake.

**21:1 “bara ya Bahari”** Hili laweza kuwa jaribio la kutafasiri (1) jina la Kiashuru kwa ajili ya Babeli (*Mat + Amil*, kama vile tanbihi kwenye toleo la JB) au (2) cheo cha lugha ya Akadi “Eneo la Bahari (*Mat tam-tim*), lakini sasa uliangamizwa, kwa hiyo, “nchi” ilibadilika kuwa “jangwa.” Toleo la Peshitta linautafasiri kama “jangwa la Baharini,” yumkini linarejerea kwenye bwawa lenye matope karibu na chanzo cha Mito Hedekeli na Frati. Toleo la TEV lina neno “Babeli.” Neno “nyikani” (BDB 184) linaashiria sehemu kubwa ya nchi isiokaliwa na watu.

**21:1-2a** Isaya anajaribu kuelezea msukumo wake wa ndani pale alipopata ufunuo huu.

1. Kama tufani za Negebu, mst. 1
2. Toka nyikani, uk. 1
3. Toka katika nchi iogopewayo (BDB 431, KB 432, *Niphil KAULI ENDELEVU*), uk. 1
4. Maono machungu (BDB 904), uk. 2a

**21:2b** Hii inazungumzia juu ya wavamizi wa Babeli (yaani, Ashuru, . mst. 9).

1. Yule atendaye hila atatenda hila, hushiriki juu ya BDB 93, KB 108, maneno mawili ya *Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA*, 24:16; 33:1; Yer. 3:20; 5:11 (inawezekana kuwa tafasiri ya NIV ya neno “msaliti,” REB, “msaliti,” au NRSV, “msaliti” kihistoria linamfaa Merodach-baladan, mfalme wa Babeli, vizuri)
2. Aharibuye ataharibu, hushiriki juu ya BDB 994, KB 1418, maneno mawili ya *Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA*, 16:4; 33:1; Jer. 6:26

**21:2c** Mungu anaziamuru mamlaka mbili Kaskazini mwa Mesopotamia kuivamia Babeli.

1. “panda juu” (BDB 748, KB 828, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU*) Elamu (BDB 743). Hili linashangaza tangu mwanzo pale Elamu alipoamua kuisaidia Babeli kuuondoa utawala wa Waashuru.
2. “husuru” (BDB 848, KB 1015, *Qa/KAULI ISIOTIMILIFU*) Umedi (BDB 552). Hili lilikuwa ni kundi jingine la kikabila huko Kaskazini mwa eneo la Eufrati.

Inawezekana kuwa hivi ni vilio vya vita vya wale wasio muungano na Waashuru (yaani., Elamu, Umedi, ndivyo asemavyo mto maoni wa Kiyahudi Ibn Ezra). Hii ingalifanya maana zaidi kama Babeli ya wakati wa Isaya itaelezewa.

**21:2d** Toleo la NASB lina kifungu “nimekwisha weka mwisho wa maumivu yote aliyokwisha sababisha.” Toleo la maandiko ya Kimasoreti lina kifungu “maumivu yote nimeyakomesha” (BDB 991, KB 1407, *Hiphil KAULI TIMILIFU*). Kifungu, “amesababisha,” kwenye toleo la NASB, hakipo katika toleo la andiko la Kimasoreti. Kama ndivyo inavyodhaniwa, lazima lielezewe kuwa huu mstari wa ushairi unafaa vizuri kwenye Babeli mpya. Hii himaya ya baadaye ilikuwa na eneo kubwa la ushawishi (yaani., Nebukadneza, kama vile Danieli 4).

Tena, baadhi (ukijumuisha na mimi) tunauangalia huu mstari wa mwisho kama maelezo toka kwa mfalme wa Babeli (Merodachbaladani) au miungu yake (Marduk) yakielekeza kwenye “kushindwa” kwa Ashuru/Nineva. Kuna wazungumzaji wengi kwenye sura hii ambavyo ni vigumu kujua haswa mzungumzwaji mlengwa (nabii, YHWH, mfalme wa Babeli, waangalizi mbali mbali, sauti zisizojulikana).

**21:3-4** Nabii anajaribu kuelezea madhara ya ujumbe alionao juu yake binafsi. Pia Danieli aliyatitia maumivu ya mwili wakati wa mafunuo ya YHWH (kama vile Dan. 7:15,28; 8:27; 10:16-17).

1. Viuno vyangu vimejaa maumivu
2. Utungu umenishika kama utungu wa mwanamke azaaye, kama vile 13:8; 26:17
3. Ninaumwa sana, nisiweze hata kusikia, kama vile. 19:14 (yaani., ni lahaja ya mtu aliyelewa)
4. Nimefadhaishwa nisiweze kuona
5. Moyo wangu unapigapiga
6. Utisho umenitaabisha
7. Gzagiza la jioni nilipendalo limegeuka likanitetemesha (“gzagiza” yumkini kushindwa kwa Babeli kulimaanisha Ashuru yenye nguvu, iliyojitanua)

Hivi VITENZI vyote viko katika KAULI YA WAKATI TIMILIFU, vyene kuonyesha hali timilifu. Kwa nini alikuwa amefadhaika hivyo? Hapana yeote wa kuweza kumzuiya Ashuru sasa! anakuja!

**21:4** Hii aya inaendelea mpaka kwenye mstari wa 2a (“maono ya kutaabisha”). Inaelezea majibu ya Isaya kwenye ufunuo huu.

1. Moyo wangu unapigapiga, BDB 1073, KB 1766, *Qal KAULI TIMILIFU*
2. Utisho umenitaabisha, BDB 129, KB 147, *Piel KAULI TIMILIFU*
3. Gizagiza la jioni nilipendalo limegeuka likanitetemesha, BDB 962, KB 1321, *Qal KAULI TIMILIFU*

Swali ni kuwa, “kwa nini Isaya hakufurahi kwenye anguko la Babeli?” yumkini kwa sababu ya

1. Ugomvi mkubwa aliquingilia
2. Babeli anaiweka Ashuru katika uthabiti. Sasa Ashuru inakuwa huru kupanua eneo lake (angalia *Exposition Bible Commentary*, juzu ya 6, uk. 134).

**21:5** Hii aya ina mfululizo wa VITENZIJINA HALISI vine vya neno *Qal* (vikitenda kazi kama vyene KUSHURUTISHA) na baadaye viwili vya neno *Qal KAULI SHURUTISHI*.

1. Waandaa meza
2. Wanaweka walinzi (angalia kumbukumbu ifuatayo)
3. Wanakula
4. Wanakunywa

Hii ingalimaanisha wingi wa chakula. Baadhi ya watoa maoni wanalionia hili likirejerea kwa Danieli 5. Kama ndivyo, hivyo basi sura hii inarejerea kwenye Babeli ya kale ya muda kitambo (yaani., Nebukadneza). Katikati ya sherehe mjumbe akawasili na kuitisha maandalizi ya kijeshi (“makaptaini,” BDB 978).

1. Simameni, BDB 877, KB 1086, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. Itieni ngao mafuta, BDB 602, KB 643, *Qal KAULI SHURUTISHI*.

Wapiganaji wa kale walizifunika ngao zao kwa ngozi ili kwamba mishare yeny moto iweze kupenya kwenye ngozi laini na kuzima, kama vile II Sam. 1:21.



**NASB, NJB**                   “**walifunika juu yake kwa nguo**”

**NKJV, Peshitta**               “**kuweka mlinzi katika mnara**”

**NRSV, TEV,**

**REB**                           “**waliweka mazulia**”

**JB**                           “**walifunika kwa nguo**”

Kifungu hiki kimetengenezwa kwa NOMINO na asili ile ile yeny MANENO.

1. NOMINO, צפית (BDB 860 II) inapatikana hapa tu, baadhi ya wanazuoni wanaliangalia hili kama “zulia,” wengine kama “mlinzi” (BDB 859, מצלפה)
2. KITENDO, צפה (BDB 860 II, KITENZIJINA HALISI), kinamaanisha “tandika” au “weka juu ya”

Kwa vile watu wa Mashariki Karibu ya Kale walikula wakiwa wamekalia mito kwenye sakafu, hili lingalirejerea kwenye aina hii ya maandalizi ya ukaaji/ulaji (yaani., “andaa mito,” kama vile toleo la NIDOTTE, juzu ya 3, uk. 832).

**21:6** Tambua nabii anategemea maneno ya YHWH.

1. Enenda, BDB 229, KB 246, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. Weka mlinzi, BDB 763, KB 840, *Hiphil KAULI SHURUTISHI* (“mlinzi,” hasa. “Yule aonaye,” BDB 859, KB 1044, *Piel KAULI ENDELEVU*)
3. ayatangaze, BDB 616, KB 665, *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI

**21:7** Ameelekezwa kuangalia aina yeote maalum ya muundo wa kijeshi.

1. Wapanda farasi waendao wawili wawili

2. Kundi la punda
3. Kundi la ngamia

Neno “wapanda farasi” (BDB 935) laweza kufahamika kama gari la kukokotwa na farasi wawili ( toleo la NKJV, Peshitta). Kwa ajili ya #2 na #3, yaweza kuelekezwa kwa wapanda farasi (kama vile toleo la NRSV, LXX).

Katika mtazamo wa aina hii ya vifaa vya kijeshi na maandalizi yake, anatakiwa atangaze haraka (matumizi mara mbili ya neno “kuweka tahaadhari,” BDB 904). Ashuru inakuja!

**21:8** Hii ni aina mojawapo ya njia ya kijeshi ya kutangaza kwa sauti (yaani., kama simba) na mlinzi aliye juu ya ukuta. Mpaka sasa hajaona kitu.

Andiko la Kimasoreti ni gumu na machapisho ya Kiebrania toka toleo la DSS yanaonyesha mwito wa mlinzi kuwa kama wa simba, ambao ndiyo uchaguzi mzuri kwa ajili ya kulielewa andiko tatanishi la Kiebrania.

Hata hivyo, inawezekana kuliangalia neno “simba,” אֲרִיָה (BDB 71) kama kosa la mnakilishaji wa neno “angalia,” רָאֵה (BDB 906), hatimaye ikasababisha matokeo ya utafasiri wa kifungu cha maneno, “hivyo Yule aangaliaye kama mlinzi” (yaani mlinzi) hupiga kelele.

**21:9** Ghafla maandalizi ya kijeshi na vifaa vinachunguzwa! Uwepo wake huko Palestina unaonyesha anguko lake la nyuma la mji wa Babeli. Hili anguko limeelezewa kwa KITENZI kukiongeza mara mbili (BDB 656, KB 709, *Qal KAULI TIMILIFU*), ambacho ni kitu cha kawaida katika Isaya. Mji wa Babeli ulianguka mara kadhaa mikononi mwa wafalme wa Ashuru.

Mwisho wake umekamilika kama ulivyoelezewa kwa kuharibu (BDB 990, KB 1402, *Piel KAULI TIMILIFU*) sanamu zake (kama vile sura ya 46-47). Kwa kushindwa kwake Babeli miji ya Elamu na Umedi haikutumika tena kwa muda, Ashuru yaweza kuanza kusudi lake la upanuzi!

**21:10** Nabii anawaambia watu wa agano walioonewa kuwa Mungu wao (yaani., “Bwana wa Majeshi,” “Mungu wa Israeli”) amekwisha kutenda, lakini kwa namna gani?

1. Kuanguka kwa Babeli haukuwa ushindi kwa ajili yao, lakini ahadi ya uhakika kuwa Ashuru atarudi.
2. Swali linabaki ni Babeli ipi ambayo nabii anairejerea kwayo?
  - a. Babeli ya Merodach-baladan ya kipindi cha Isaya
  - b. Babeli ya kale ya Nebuchadneza ya kipindi cha Ezekiel na Yeremia

Suala sio moja ya ukweli wa unabii uliotabiliwa, lakini ni ule muundo wa kihistoria!

Kitu kama kumbukumbu kuhusu namna tofauti ya kuitafasiri aya hii. Yawezekana kuwa Yule anayeelezewa ni Wbabeli ambao Ashuru atawaangamiza. YHWH mapema kabisa amekwisha sikia kuanguka kwa Moabu (kama vile 15:5; 16:11) na maombi ya Wamisri wanaokandamizwa (kama vile 19:20).

▣“niliyekuficha na nafaka ya sakafu yangu” Hii ni lahaja ya Kiebrania “mwana wa sakafu yangu.” Neno la Kiebrania “mwana” lina matumizi ya elimu-maana mbalimbali katika Isaya.

1. Mwana wa kuzaa sana, 5:1
2. mwana wa asubuhi, 14:12
3. Mwana wa wenye hekima, 19:11
4. Mwana wa Adamu, 56:2
5. Mwana wa wageni, 56:6

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 21:11-12

<sup>11</sup> Ufunuo juu ya Duma.

Mtu ananililia toka Seiri,  
Ee mlinzi, habari gani za usiku?  
Ee mlinzi, habari gani za usiku?

<sup>12</sup> Mlinzi akasema,  
Mchana unakuja na usiku pia;  
mkitaka kuuliza, ulizeni; njoni tena.

**21:11** Ujumbe mpya unaanza (yaani., utumiaji wa alama za kifasihi, “ufunuo”). Andiko la Kimasoreti lina neno “duma” (BDB 189). Ni masihala juu ya neno la Kiebrania “kunyamaza” (BDB 189). Edomu atanyamazishwa. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yana neno “duma.” Edomu ilikuwa ni sehemu ya ushirika wa walio kinyume na Ashuru, kama ilivyokuwa Ufilisti. Wote waliangushwa katika mwaka wa 711 K.K.na jeshi la Sargon II.

▣“Seiri” Hii (BDB 973) inaweza kurejerewa kwenye nchi ya Edomu (kama vile Mwa. 32:3; 36:30; Hes. 24:18; Kumb. 2:4,8, 12,22,29; Amu. 5:4).

**21:11c-12** Huu ni ubeti wenye fumbo ukiwa na KAULI SHURUTISHI. Mlinzi juu ya ukuta, kama ulivyo mist. 6 na 8, inaelezewa na sauti isiojulikana ambayo inauliza kuhusu muda wa usiku (mara mbili). Jibu pia ni la ajabu.

1. Mchana unakuja
2. Usiku pia
3. Mkitaka kuuliza
4. Ulizeni

Yumkini inamaanisha, “ni wakati gani haya yote yatatendeka?”

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 21:13-15

<sup>13</sup> Ufunuo juu ya Arabuni.

Ndani ya msitu wa Arabuni mtalala,  
Enyi misafara ya Wadedani.

<sup>14</sup> Waleteeni wenye kiu maji,

Enyi wenyiji wa nchi ya Tema;  
Nendeni kuwalaki wakimbiao na chakula chao.

<sup>15</sup> Kwa maana wanakimbia mbele ya panga,

Upanga uliofutwa, na upinde uliopindwa,  
Na mbele ya ukali wa vita.

**21:13** Ujumbe mpya (utumiuaaji wa alama mpito za fasihi, “ufunuo”) unaelezewa kwa Arabuni. Haifahamiki mpinzani ni nani.

1. Ashuru (uvamizi)
2. Kedari (vita vya jamii)

Inafurahisha kwamba “Duma” (mst. 11) na Seiri (mst. 11) pia ni majina ya sehemu zilizomo, au karibu na, Arabuni.

▣“msitu” Isaya anatumia taswira ya “msitu” mara nyingi. Neno hili (BDB 420) laweza kumaanisha

1. Msitu
2. Vichaka

Kwa vile Arabuni ni jangwa, hoja namba mbili itafaa sana. Ingaliweza kumaanisha bonde jembamba lenye uwoto wa vichaka vinene, mahali ambapo wanyama hujificha. Sasa wakimbizi, na misafara ya ngamia (yaani., Wadedani walikuwa ni watu wa Bedou waliohusiana na Sheba) walijificha huko kuepuka uvamizi wa kijeshi (kama vile mst. 15). Hawakuweza kutumia njia za kawaida au zile sehemu za mapumziko.

**21:14** Waarabu waliamriwa (BDB 87, KB 102, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI) kuleta maji na chakula kwa ajili yao.

▣“Tema” Huu ulikuwa mji maarufu pande za Kaskazini, nyumbani mwa waabuduo mungu mwezi. Angalia Mada Maalum: Kuuabudu Mwezi katika 3:18.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 21:16-17

<sup>16</sup> Kwa sababu Bwana ameniambia hivi, Katika muda wa mwaka, kama miaka ya mtu mwenye kuajiriwa, utaangamia utukufu wote wa Kedari. <sup>17</sup> Na mabaki ya hesabu ya wavuta pinde, hao mashujaa wa Kedari watakuwa wachache; maana Bwana, Mungu wa Israeli, amenena neno hili.

**21:16 “katika muda wa mwaka,kama miaka mtu mwenye kuajiriwa”** Lahaja yenyewe kufanana ya muda sahihi inapatikana mwanzoni katika Isa. 16:14.

▣“**Kedari**” Huu ni mji mwingine maarufu wa Arabuni. Kwa maana ya jeshi lote la Arabuni, watashindwa. Sargon II alivamia hili eneo mwaka wa 715 K.K. Tena kifungu cha kithiolojia “kwa vile Mungu wa Israeli amesema.” Haikuwa nguvu ya majeshi ya kale ambayo yalielekeza matukio ya Mashariki Karibu ya Kale, bali ni Mungu wa Israeli! Haya ni madai ya wale wenye imani ya Mungu mmoja.

## ISAYA 22

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Bonde la maono	Tangazo dhidi ya Yerusalem	Onyo la kushambuliwa kwa Yerusalem	Ujumbe juu ya Yerusalem	Dhidi ya furaha ya Yerusalem
22:11 (1-11)	22:1-7 (1b-4)	22:1a 22:1b-4 (1b-4)	22:1a 22:1b-2a 22:2b-5	22:1-4 (1-4)
		22:5-8a (5-7)		22:5-11 (5-11)
	22:8-11 (8-11)	22:8b-11	22:8b-11	
22:12-14 (12-14)	22:12-14 (12) (13) (14)	22:12-14 (12-14)	22:12-14	22:12-14 (12-14)
			22:14	
22:15-25 (15-23)	Hukumu juu ya Shebna 22:15-19 (15b-19) 22:20-25 (20-23)	22:15-19 22:20-25	Onyo juu ya Shebna 22:15-19 22:20-23 22:24-25	Dhidi ya Shebna 22:15-23 (15-23) 22:24-25

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi wa kipengele cha ufunguzi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kii ni cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 22:1-11**

<sup>1</sup> Ufunuo juu ya bonde la maono.

Sasa una nini, wewe, Hata umepanda pia juu ya dari za nyumba?

<sup>2</sup>Ewe ulijeaa makelele,

Mji wa ghasia, mji wenyе furaha;  
 Watu wako waliouawa hawakuuawa kwa upanga,  
 Wala hawakufa vitani.

<sup>3</sup>Wakuu wako wote wamekimbia pamoja,  
 Wamefungwa wasiutumie upinde.  
 Wote walioonekana wamefungwa pamoja,  
 Wamekimbia mbali sana.

<sup>4</sup>Kwa sababu hiyo nasema, Geuza uso wako usinitazame,  
 nipaye kulia kwa uchungu;  
 usijishughulishe kunifariji, kwa ajili ya kuharibika kwake binti ya watu wangu.

<sup>5</sup>Kwa maana siku ya kutaabika, siku ya kukanyagwa, siku ya fujo inakuja, itokayo kwa Bwana, Bwana wa majeshi,  
 katika bonde la Maono;  
 inabomoa kuta;  
 na kuililia milima.

<sup>6</sup>Na Elamu wameshika podo,  
 pamoja na magari ya vita, na watu wenyе kupanda farasi;  
 na Kiri wameifunua ngao.

<sup>7</sup>Hata ikawa mabonde yako mateule yamejaa magari ya vita,  
 nao wapandao farasi wamejipanga wakielekeea malango.

<sup>8</sup>Kisha alikiondoa kifunko cha Yuda,  
 naye siku hiyo ulivitazama vyombo vy'a vita katika nyumba ya mwituni.

<sup>9</sup>Nanyi mlipaona mahali palipobomoka  
 katika mji wa Daudi ya kuwa ni pengi,  
 nanyi mliyakusanya maji ya birika la chini.

<sup>10</sup>Nanyi mlizihesabu nyumba za Yerusalem,  
 mkazibomoa nyumba ili kuutia nguvu ukuta.

<sup>11</sup>Nanyi mlifanya birika la maji katikati ya kuta mbili,  
 la kuwekea maji ya birika la kale;  
 lakini hamkumwangalia yeye aliyeyafanya hayo,  
 wala kumjali yeye aliyeyatengeneza zamani.

**22:1 “ufunuo”** Andiko hili ni ishara mpya ya ujumbe kutoka kwa YHWH na kwenda kwa taifa/tamaduni fulani. Inashangaza katikati ya hukumu ya YHWH juu ya mataifa yaliyoizunguka, anaielezea Yuda, inawezekana kwa sababu ya dhambi zake, yeye ni taifa lingine *goim*.

Ni hakika inawezekana kwamba ujumbe huu unasilulia kwa bayana historia ya mashambulizi. Kwa miaka tofauti, majeshi mbalimbali na mataifa yaliathirika .lakini sio dhahiri shairi la kiebrania kwamba mahali pa historia halisi ni vigumu kupatambua. Inawezekana baadae ujumbe wa Isaya ulifanyiwa marekebisho kutohuna na msingi wa kweli wa neno husika au aina ya maneno, sio matukio ya kihistoria (yaani., shairi liko nje ya utaratibu wa miaka na matukio).

Kumbuka kuwa jambo la muhimu kwa ufunuo wote na ukweli muhimu wa kila ubeti ni njia ya kumkaribia nabii (yaani., YHWH')maana , sio uangalifu mkuu wa kila kitu na maneno yasiyo ya kawaida.

▣“bonde la maono” kwa sababu ya kutumika kwa tungo hii kwenye mst. 5b,ni lazima irejelee “siku ya kutaabika” iliyoitumwa na BWANA wa majeshi (muhtasari Yoeli 3:14).

Cha kushangaza toleo la JB limebadilisha “maono” kwenda “Hinnom” (kama vile. Yer. 7:31-34). Toleo la LXX lina “bonde la Sayuni.”

**22:1b-2b** hayanimaelezo ya wakati wa kushangilia katika Yerusalem.

1. Juu ya dari za nyumba

2. Wewe uliyejaa makelele
3. Wewe mji wa ghasia
4. Mji wenye furaha

Toleo la JB (tanbihi) linasadiki kuwa linamsimulia ushindi wa kwanza wa Hezekia juu ya Ashuru katika mwaka wa 705K.K. au 713 K.K. (Jewish Study Bible).

**22:2c-3d** inaonekana ni baadhi ya mji (yaani, viongozi na askari) walikimbia kabla ya kuvamiwa.

1. Walitekwa , lakini sio vitani
2. Viongozi wao walikimbia pia, na wao pia walitekwa
3. Wote waliokimbia walichukuliwa uhamishoni

Kwa sababu ya mistari nhii ya shairi wengi wanaamini kwamba Sura hii inarejelea kuzingirwa na Nebukadnezza katika mwaka wa 586 K.K, ambapo Zedekia aliukimbia mji na kutekwa (kama vile. 2 Fal. 25:4-6), lakini nafikiri inarejelea uvamizi wa Ashuru kwa sababu moja ifuatayo:

1. Tiglath-pileser III (Isaya 7-12)
2. Shalmanesa V (kama vile. 2 Fal 17)
3. Sargon II (kutekwa kwa Samaria katika mwaka wa 722 K.K., kama vile. 28:1-6)
4. Senakeribu (705 na 701 K.K., Isaya 36-39; 2 Fal 18-19)

Sura hii inaonekana inasimulia dhahili utawala wa Hezekia mwaka wa (715-687 K.K.). lakini kama ilivyotokea mara kwa mara kwa Isaya, mashambulizi haya yanamaanisha kama kuchanganyikiwa. Isaya alikuwa wa kwanza kuhusika na teolojia ; kihistoria ni mtumishi anaonyesha ukweli juu ya Mungu, ubinadamu, Dhambi, na Wokovu.

**22:4** Nabii anaongea juu yake mwenyewe, kama alivyofanya katika 21:3-4

1. Geuza uso wako usinitazame, BDB 1043, KB 1609, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. Nipate kulia kwa uchungu, BDB 600, KB 638, *Piel KAULI ISIO TIMILIFU iliotumika kwa namna ya HALI YA KUSIHI*
3. Usijaribu kunifariji, BDB 21, KB 23, *Hiphil KAULI WA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika katika maana KITENZI AMRISHI* (“kufariji,” BDB 636, KB 688, *Piel TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*)

Nabii alitaka awe peke yake kama kuipitia huzuni yake binafsi.

▣“**binti ya watu wangu**” Hii ni Tungo ya Nahau kwa ajili ya watu au tamaduni ya kundi (kama vile. 1:8; 10:30, 32; 16:1; 23:10-12; 37:22; 47:1,5; 52:5; 62:11). Hapa inarejelea watu wa Agano wa Yuda (yaani , “Binti wa Sayuni”).

**22:5** Aya hii zinaelezea “siku ya kutaabika ” ya YHWH. Ni kinyume na mistri ya . 1-2.

1. Kutaabika , BDB 223, kama vile. Kumb. 28:20
2. Kutiisha , BDB 101, imetumika mara mbili pekee, kama vile. 18:2,7
3. mchafuko, BDB 100, imetumika mara mbili pekee, kama vile. Mika 7:4
4. kubomoa kuta , בְּרִכָּה, BDB 903 II, KB 1148, *Pilpel KAULI ENDELEVU* (hana pekee; baadhi ya wanazuoni wanafikiri asili yake ni Kiarabu au asili ya Ugaritiki lenye maana ya , “piga kelele,” “toa sauti,” au “fanya kelele” (KB 1128 I, בְּרִכָּה)
5. kuililia milima (hakuna KITENZI)

▣“**milima**” NOMINO hii (BDB 249) ni UMOJA na labda inarejelea kukua kwa hekalu (yaani , kumlilia YHWH).

**22:6-7** Aya hizi zinaelezea kipengele cha kushambuliwa kwa jeshi. Elamu na Kiri (inawezekana kwa wastani, kama vile. 21:2; 2 Fal. 16:9) Eneo la kaskazini mwa Mesopotamia. Walikuwa ni Askari wa kukodiwa katika jeshi la Ashuru ili kuwalinda na mashambulizi.

**22:6**

**NASB**      “askari wa miguu”

NKJV	“wanaume”
REB	“Aramu”

Toleo la Andiko la Kimasoreti lina “wanaume” (וָנוֹם, BDB 9, tazama 31:8, ambapo “adamu” imetumika kwa maana ya jeshi), lakini kwa ajili ya mfanano baadhi wamebadilisha kwenda “Aramu,” אַרְם. Hii ችልት dhidi ya ነገር kwa Kiebrania inachanganya.

**22:8 “Kisha alikiondoa kifuniko cha Yuda,”** “kifuniko” katika Aya hii inamaanisha “kufunikwa” (BDB 697). Hawakuwa na Imani nae (kama vile.mst. 11c,d) hivyo basi akaondoa uwepo wake wa ulinzi juu yao (yaani., wingu kama vile. 4:5; Zab. 105:39). Hili lilikuwa ni tatizo katika historia yote ya Israeli. Na kuna madhara kwa watu wa Mungu kushindwa kumtii na kumwamini!. Baraka na laana kutoka katika kitabu cha Kumb. 27-29 ziliwaonyesha wazi .

“kifuniko” labda kwa wazi kilirejelea ngome ya Azeka (Jewish Study Bible, tanbihi, ukr.825).

▣“**siku hiyo**” hii ni Nahau ya kawaida katika Unabii kwa ajili ya siku ya kutembelewa na Mungu (yaani 19:16,18, 19,21,23,24).

□

NASB	“wewe ulivitazama”
NKJV, NRSV	“wewe ultazama”
NJB	“umegeuka na kutazama”

KITENZI (BDB 613, KB 661, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) Inadokeza kwamba walizitumainia silaha zao, na sio YHWH.

▣“**katika nyumba ya mwituni**” Hili lilikuwa ni jina la Ghala la siraha katika Yerusalem (kama vile. 1 Fal. 7:2; 10:17).

**22:9** Muundo wa kihistoria unajitokeza wakati wa Hezekia. Alijenga (2 Fal. 20:20) Birika kwa ajili ya kukusanya maji wakati wa kuzingirwa (kama vile. mst. 11; 7:3; Neh. 3:16). Ni wazi kuwa Hezekia alifanya maandalizi ya vitu kwa ajili ya kuilinda Yerusalem kabla ya kushambuliwa na Senakeribu mwaka wa 701 K.K., lakini sio mpango huo uliouokoa mji wa Yerusalem; Ni YHWH na makusudi yake makuu (mst. 11).

**22:10** Aya hii inaonekana inaelezea Ukuta wa Yerusalem kama kuta mbili (ambapo hakuna uthibitisho wa mambo ya kale). Watu wengi waliamhia ndani ya mji kwa ajili ya usalama na kujenga nyumba za muda katika nafasi ya kuta mbili. Lakini nyumba hizi ziliondolewa (tazama IVP, Bible Background Commentary, ukr. 614).

Njia nyininge ya kulifahamu andiko hili inawezekana kwamba baadhi ya nyumba ziliharibiwa ili kuziba nafasi kati ya kuta hizi mbili. Hii ilikuwa ngumu sana kwa vifaa viliviyotumika kutobolea ukuta kufanikiwa.

Baadhi ya sehemu zilijazwa maji kama maeneo muhimu (kama vile.mst. 11). Hii ilitumika kama

1. kizuizi kwa wale waliotaka kutoboa ukuta wa nje
2. maji ya ziada yaliyosambazwa katika mji ambaa ulikuwa umejaa wakimbizi

**22:11 “lakini hamkumwangalia yeye aliyeyafanya hayo”** hii ni aina ya thiolojia katika muktadha. Baadhi ya KITENZI kwenye mst. 8b kimerudiwa (hana *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kifasihi. “hamkumwangalia”). Walitumaini katika kuimarisha na mahitaji muhimu kwa ajili ya vita, sio katika Agano lao na Mungu!

▣“**wala kumjali yeye aliyeyatengeneza zamani.**” KITENZI hiki (BDB 906, KB 1157) ni *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*. Watu wa Mungu waliiacha Ahadi ya kulindwa ambayo Mungu aliifanya kwa ajili yao. Isaya anatilia mkazo Ahadi hizi na anatetea mara nyingi kwamba Yerusalem haita angamizwa.

Sababu ya kutoangamizwa kwa mji huu ni Mungu kutimiza kusudi lake (yaani ., “mpango,” lit. “muundo” BDB 427, KB 428, *Qal KAULI ENDELEVU*, kama vile. 37:26; 46:11; Yer. 18:11) kwa ajili ya watu wake.

1. Kuujulisha ulimwengu juu ya YHWH
2. Aina ya jamii ya kiungu
3. Kuwa chombo kwa ajili ya kuja kwa Masihi

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 22:12-14**

<sup>12</sup>**Siku hiyo Bwana, Bwana wa majeshi, akawaita watu walie na kuomboleza,**

**na kung'oa nywele zao, na kucaa nguo za magunia;**

<sup>13</sup>**na kumbe! Furaha, na kucheklea,**

**na kuchinja ng'ombe, na kuchinja kondoo,**

**na kula nyama, na kunywa mvinyo;**

**“tule, tunywe, kwa maana kesho tutakufa”.**

<sup>14</sup>**Na ye ye Bwana wa majeshi akafunua haya masikioni mwangu,**

**“Ni kweli, uovu huu hautatakaswa wala kuwatokeni hata mfe;”**

**asema Bwana, Bwana wa majeshi.**

**22:12-14** Huu ni ubeti mwingine unaoanza na “Siku hiyo”.

Aya ya 12 inataja maana ya maombolezo (tazama mada maalumu katika 15:2-3) kwamba inabainishwa Yerusalem.

1. kulia, BDB 113 (hakuna KITENZI)

2. kuomboleza, BDB 704 (hakuna KITENZI)

3. kung'oa nywele kichwani, BDB 901 (hakuna KITENZI, upara unawenza kuwa kwa kunyoa nywele au kunyonyoa, kama vile. Ezra 9:3; Ayubu 1:20; Yer. 7:29; 16:6; 41:5; 48:37; Mika. 1:16)

4. kucaa nguo za magunia, BDB 291, KB 291, *Qal TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*

Aya ya 13 inaelezea badala yake kile ambacho Yerusalem ilifanya. Walipaswa kumtafuta YHWH katika toba na maombi, lakini walinaswa katika

1. furaha, BDB 965

2. kucheklea, BDB 970

3. kuchinja kama kawaida , mbili *Qa KITENZI JINA HALISI* (BDB 246, BDB 133)

4. kula nyama zilizochinjwa, BDB 37, *Qal KITENZI JINA HALISI*

5. kunywa mvinyo, BDB 1059 I, *Qal KITENZI JINA HALISI*

**22:13d** Mtazamo juu ya maisha yao unaelezewa katika mstari wa shairi hili. Ni sawa na karamu ya Belshaza kwenye kitabu cha Danieli 5.

Mtazamo huu uliakisi upungufu wao wa ufahamu juu ya mipango (BDB 427, KB 428, *Qal KAULI ENDELEVU*, kama vile. 11d) ya YHWH kwa ajili ya Yerusalem na watu wake (kama vile. 5:11-12). Badala ya kushirikiana kwa mikakati na tumaini, walipigana mara moja kwa ubinafsi mmoja mmoja bila kuungana ili kupata ushindi, Na hili kweli ndilo neno ambalo kanisa pia linahitaji!!

**22:14** Upungufu wa imani wa Yuda ndio matokeo ya kifo chake. Hukumu ilikuja juu ya Yuda. Yerusalem itakuwa salama peke yake, lakini Yuda itaharibiwa.

Yuda haikuja majira ya kutembelewa na YHWH (kwa ajili ya ukombozi), Na ni kwa jinsi gani angetambua majira ya kuangamizwa kwake!

▣**“Ni kweli, uovu huu hautatakaswa”** Uovu gani? Nafikiri ni uovu wa kutokuwa na tumaini na imani katika Mungu uliotajwa katika mst. 11c,d.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 22:15-25**

<sup>15</sup>**Bwana, Bwana wa majeshi, asema hivi,**

**Haya! Enenda kwa huyu mtunza hazina,**

**yaani, Shebna, aliye juu ya nyumba, ukamwambie,**

- <sup>16</sup>Unafanyaje hapa?  
 Nawe una nani hapa?  
 Hata ukachimba kaburi hapa;  
 ukamchimbia kaburi huko juu,  
 na kumchongea makao katika jabali!
- <sup>17</sup>Tazama, Bwana atakutupa kwa nguvu, kama mtu mwenye nguvu;  
 naam, atakuzonga-zonga.
- <sup>18</sup>Hakika atakukunja na kukutupa kama mpira,  
 mpaka nchi iliyo mbali; huko utakufa,  
 na magari ya utukufu wako yatakuwa kuko huko,  
 ewe uliye aibu ya nyumba ya bwana wako.
- <sup>19</sup>Nami nitakusukuma na kukutoa katika mahali pako,  
 naye atakushusha uteke hapa usimamapo.
- <sup>20</sup>Na itakuwa katika siku ile  
 nitamwita mtumishi wangu Eliakimu, mwana wa Hilkia;
- <sup>21</sup>nami nitamvika vazi lako,  
 nitamtia nguvu kwa mshipi wako,  
 nami nitamkabidhi ye ye mamlaka yako;  
 naye atakuwa baba kwa wenyeji wa Yerusalem, na kwa nyumba ya Yuda.
- <sup>22</sup>Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani mwake;  
 ye ye atafunga wala hapana atakayefunga;  
 naye atafunga wala hapana atakayefunga.
- <sup>23</sup>Nami nitamkaza kama msumari mahali palipo imara;  
 naye atakuwa kiti cha utukufu kwa nyumba ya baba yake.
- <sup>24</sup>Nao wataangika juu yake utukufu wote wa nyumba ya baba yake; wazao wake na watoto wao, kila chombo kidogo tangu vyombo vya vikombe hata vyombo vya makopo vyote pia.
- <sup>25</sup>Katika siku ile, asema Bwana wa majeshi, ule msumari uliokazwa katika mahali palipo imara utalegea; nao utakatwa na kuanguka chini, na ule mzigo uliokuwa juu yake utakatiliwa mbali; maana Bwana amesema haya.

**22:15-19** Hii inaelezewa hukumu ya YHWH juu ya Shebna, msimamizi wa Mfalme Hezekia. Kwa sababu Shebna' alilazimisha kuchukua nafasi ya Eliakimu (kama vile.mist. 20-25) kwa mashaka , lakini lazima ilikuwa baya zaidi na katika muktadha, labda "roho ya kujitegemea."

Shebna dhahili ni "Shebna" wa 2 Fal. 18:18, aliyekuwa mwandishi wa Eliakimu.

**22:16** Hapa ni mfuatano wa maswali kuujaribu utumishi wa Shebna.

**22:17-19** Uovu una matokeo. Viongozi waliwajibika haswa. YHWH anaelezewa kama mpatanishi binafsi wa hukumu.

1. atakutupa, mst. 17, BDB 376, KB 373, *Pipe/ KAULI ENDELEVU*;na inahusiana na NOMINO(BDB 376), "atakutupa kwa nguvu"
2. Atakushika kwa nguvu, mst. 17, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU* na *Qal KITENZI JINA HALISI* chaf BDB 742 II, KB 814 II
3. "atakukunja na kukutupa kama mpira,"mst. 18, *Qal KITENZI JINA HALISI* na *Qal KITENZI CHA KAULI ISIO TIMILIFU* kama vile NOMINO,kama asili sawa (BDB 857, KB 1039)
4. Mpaka nchi ya mbali huko utakufa,mst. 18c,d
5. "kukutoa katika mahali pako," mst. 19, BDB 213, KB 239, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
6. "naye atakushusha," mst. 19, BDB 248, KB 256, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*

Kuna nadharia ya msamiati unaotia shauku unaohusiana na namba 2. NIDOTTE, juzu. 3, krs. 380-381, inashauri kwamba asili hii inamaanisha "ondolewa," kama sitiari kwa ajili ya kutimia kwa mashambulizi (kama vile. Yer. 43:12).

**22:20-25** Aya hizi zinaeleza kwamba YHWH atamfanyia heshima Eliakim, mrithi wa Shebna (kama vile II Wafalme. 18:18, 26,37; 19:2; Isa. 22:20; 36:3,11,22; 37:2).

1. YHWH atamuita , kifasihi. "ita," BDB 894, KB 1128, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
2. YHWH atamvika vazi refu,mst. 21, BDB 527, KB 519, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
3. YHWH atamtia nguvu kwa mshipi mst. 21,KITENZI kutoka namba 2 kinadokeza
4. YHWH atamkabidhi yeye mamlaka yako, mst. 21, BDB 304, KB 302, *Piel KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
5. YHWH atauweka ufunguo wa nyumba ya Daudi mabegani mwake, mst. 22, BDB 678, KB 733, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
6. YHWH atamkaza kama msumari mahali palipo imara, mst. 23, BDB 1075, KB 1787, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*

**22:21-23** Aya hizi zinaelezea ni nini atafanya.

1. Atakuwa baba wa wenyiji wa Yerusalem
2. Naye atafunga wala hapana atakayefunga, atafunga na hapana atakayefungua, mst. 22
3. Naye atakuwa kiti cha utukufu kwa nyumba ya baba yake, mst. 23 (kama vile. mst. 24)

Kwa maana nyingine Aya hizi zinamwonyesha Eliakimu kama alama au kivuli kijacho cha Masihi. Kivuli hiki ni sawa na kile kinachoonekana katika kitabu cha Zekaria pamoja na Zerubabeli na Yoshua (kama vile. Zek. 3-4).

**22:23** "imara" tazama mada maalum inayofuata, hasa II., A., 1., b., (2)

## MADA MAALUM: KUAMINI, TUMAINI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (עֲמָלֵם)

### I. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoolezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

- A. Watu binafsi na jamii
- B. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

- A. Ibrahim na uzao wake
- B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majoribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

### II. Asili kuu iliyotumika

- A. עַמְלֵם (BDB 52, KB 63)
  1. KITENZI
    - a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
    - b. Shina la neno *niphil*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
      - 1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
      - 2) Kwa vitu, Isa. 22:23
      - 3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
    - c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
      - 1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
      - 2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (iliikanushwa katika Kumb. 1:32)

- 3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
- 4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
- 5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
- 6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.
- B. אַמְנוֹן (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
  2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
  3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16
- C. אַמְנוֹנָה (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
1. Katika mikono, Kut. 17:12
  2. Katika muda, Isa. 33:6
  3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
  4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138
- III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale
- A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).
- B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katikaaya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (אַמְנוֹן).
1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
  2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pemberi kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
    - a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
    - b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
  3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)
- IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale
- A. Petro anaunganisha
1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
  2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pemberi)
  3. Zab. 118:22 – 1 Pet. 2:7 (jiwe lililokataliwa)
- B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliilezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
  2. Isa. 61:6; 66:21
  3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1 Petro. 2:5,9)

1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii
  - A. Utumiaji wake

Neno “akaamini” linatokana na neno la Kiyunani *pisteuō* ambalo pia laweza kutafasiliwa “kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato

wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. *eis inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu*
  - a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
  - b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
  - c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
  - d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
  - e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
  - f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
  - g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mk 1:15; Mdo 5:14*
3. *epi ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6*
4. *uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10*
5. *hoti, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa*
  - a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
  - b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
  - c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
  - d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
  - e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
  - f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
  - g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
  - h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
  - i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
  - j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
  - k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

V. Hitimisho

- A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
  1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
  2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
  3. Utii
  4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)
- B. Imani ya Kibiblia ni
  1. Uhusiano binafsi (iman ya awali)
  2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (iman katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
  3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwaa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya” inayotuwezesha kuititia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!

Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa

maana ya Wayunani na Waebrania)

Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipy), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipy katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, ilioonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

**22:25** Hata Eliakimu naye (yaani.,msumari uliokazwa utalegea ),yote kwa msaada wa YHWH, haiwezi kuzuia hukumu ijao.

1. Msumari utalegea (BDB 559 I, KB 561, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
2. Utakatwa hata chini (BDB 154, KB 180, *Niphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
3. Utaanguka chini (BDB 656, KB 709, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
4. Utakatiliwa mbali (BDB 503, KB 500, *Niphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)

Hukumu inakuja, anasema YHWH (BDB 180, KB 210, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU).

**22:25 “msumari”** huu (BDB 450) labda inarejelea

1. Shebna
2. Eliakim
3. Yuda
4. Yerusalem
5. Masihi

Katika muktadha wa namba 1 au namba 2 ni bora zaidi, lakini wengine wanaelezea ni mipango ijayo ya YHWH (kama vile . mst. 11).

## ISAYA 23

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuanguka kwa Tiro 23:1-7 (1-7)	Tamko dhidi ya Tiro 23:1-7 (1) (2-3) (4-5) (6-7)	Unabii juu ya Sidoni 23:1-7 (1-7)	Ujumbe juu ya Foenike 23:1-3 23:4 23:5 23:6-9	Dhidi ya Tiro 23:1-14 (1b-4)  (7-14)
23:8-11 (8-11)	23:18-14 (8-9) (10-12)		(8-12)	
23:12 (12)				
23:13-18 (14) (16)	(13) (14) 23:15-18 (16)	23:13-18 (14) (16)	23:14 23:15 23:16 (16) 23:17-18	23:15 23:16 (16) 23:17-18

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukr. xvi na kipengele cha utangulizi) KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kushutumiwa huku kwa Foenike ni sambamba katika Ezekiel 26-28; Amosi 1:9-10. Tiro (mji mkuu wa Foenike) lilikuwa taifa lenye nguvu na lenye utajiri wa bahari, jambo lililosababisha kuwa wenyе viburi na kujitegemea.
- B. Kwasababu ilikuwa falme iliyoneea sana kiasi hicho mataifa kadhaa na maeneo ya kijiografia yaliomboleza kwasababu ya kupoteza biashara.
  1. Meli ya Tarshishi (yaani, eneo la masharibi ya Shamu), mistari ya 1,6,14
  2. ardhi yote ya pwani, mistari ya 2,6
  3. wafanya biashara ya Sidoni (yaani, jiji kubwa la pili la kifoenike), mistari wa 2

4. Misri, mistari ya 3,5
5. Kanaani, mstari wa 11
6. Kipro, mistari ya 12

C. Tazama hesabu ya KAULI SHURUTISHI zinazoelekezwa Tiro/Foenike.

1. omboleza, mstari wa 1, BDB 410, KB 413, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, kama vile 13:6;14:31; 15:2,3; 16:7 (mara mbili); 65:14
2. tulieni (kifasihi. "kuwa na utulivu"), mstari wa 2, BDB 198, KB 226, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. Kutahayari, mstari 4, BDB 101, KB 116, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile 1:29; 19:9; 20:5; 24:23; 26:11; 29:22; 30:5; 37:27; 41:11; 42:17; 44:9,11; 45:16,17,24; 49:23; 50:7; 54:4; 65:13; 66:5; Mika 3:7; 7:16
4. kupitisha, mstari wa 6, BDB 716, KB 778, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile 23:2
5. omboleza, mstari wa 6, sawa sawa na #1
6. kumiminika (kifasihi. "kupita kiasi"), mstari wa 10, sawasawa na #4
7. inuka, mstari wa 12, BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
8. kupita, mstari wa 12, sawasawa na #4,6
9. omboleza, mstari wa 14, sawasawa na #1,5
10. chukua kinubi chako, mstari wa 16, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI
11. kutembea katika jiji mstari wa 16, BDB 685, KB 738, *Qal* KAULI SHURUTISHI
12. kupiga nyuzi (kifasihi. "kucheza kwa ufundi"), mstari wa 16, BDB 405, KB 408, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, kama vile I Sam. 16:17; Zab. 33:3; Ezek. 33:32
13. imba nyimbo nyingi, mstari wa 16, BDB 915, KB 1176, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

D. Kama ilivyo siku zote kujaribu kufasiri mashairi ya Isaya, mazingira ya kihistoria yangesaidia katika kuelewa maelezo na ufanuzi, lakini mashairi haya yanaweza kushabihiana na uvamizi tofauti kadhaa. Kitabu cha Isaya ni mkusanyiko wa jumbe kutoka kila eneo la maisha yake yakiunganishwa kwa tarehe za baadaye. Zimetengenezwa kwa muundo kwa namna isiyofuata njia ya mtirikio zikijikita katika

1. maneno yanayofanana
2. maeneo ya kijiografia yanayofanana
3. sitiari za kimaneno
4. maudhui
5. na zaidi

Wa kisasa hawajui kwa namna gani, wakati gani au kwa nani vitabu vya Agano la Kale hatimaye zilikusanywa/kuhaririwa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 23:1-7**

<sup>1</sup> Ufunuo juu ya Tiro.

Toeni sauti za uchungu,  
enyi merikebu za Tarshishi,  
kwa maana umeharibika kabisa,  
hata hapana nyumba,  
hapana mahali pa kuingia;  
toka nchi ya Kitimu wamefunuliwa habari.

<sup>2</sup> Tulieni, enyi mkaao kisiwani;  
wewe ambaye wafanya biashara wa Sidoni,  
wavukao bahari, walikujaza.

<sup>3</sup> Vitu vilivyopandwa,  
vya Shihori, mavuno ya Nile,  
yaliyokuja juu ya maji mengi,  
ndiyo pato lake,

naye alikuwa soko la mataifa.

<sup>4</sup> Tahayari, Ee Sidoni;

kwa maana bahari imenena,  
hiyo ngome ya bahari ilisema,

Sikuona utungu,

wala sikuzaa, wala sikulea vijana, wala sikulea wanawali.

<sup>5</sup> Habari itakapofika Misri wataona uchungu sana kwa sababu ya habari ya Tiro.

<sup>6</sup> Piteni mpaka Tarshishi,

enyi mkaao kisiwani, toeni sauti ya uchungu.

**23:1 “ombolezeni, enyi merikebu za Tarshishi”** “omboleza” (עַלְיָה, BDB 410, KB 413, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*) ikiashiria kelele za sauti. Imetumika katika Isaya (kama vile 13:6; 14:31; 15:2,3; 16:7 [mara mbili]; 23:1,6,14; 52:5; 65:14 na neno linalohusiana [עַלְלָה] katika 15:8 [mara mbili]). Angalia Mada maalum: Ibada kwa wenyewe huzuni katika 15:2-3.

Angalia tungo hii hii inatokea katika mstari wa 14. Mara kwa mara tungo inayojirudia inaonesha kipengele cha kisarufi. Lakini hapa kwamba havishabihiani vizuri.

Meli za Tarshishi zilikuwa zikibeba mzigo mkubwa wa nafaka za kibiashara, mara nyingi kutoka Misri. Zilifanyika nahau (kama ilivyokuwa “Foenike” na “Wakanaani”) kwa ajili ya wafanya biashara.

▣ “**Tarshishi**” Hili jina la eneo (BDB 1077) lilimaanisha

1. jiji katika Uhispania katika upande wa bahari ya Atlantiki, ambalo lilikuwa koloni la Foenika (yaani, Tartessus, mstari wa 7)
2. kisiwa cha Sardinia (kama vile Mwanzo 10:4)
3. jiji katika kaskazini kwa pwani ya Afrika (Carthage lilikuwa Koloni la Foenike)
4. sitiari kwa bandari ya mbali
5. aina ya meli kubwa ya kibiashara iendayo baharini
6. taifa pinzani lililoko majini (kama vile I Wafalme 10:22)

▣ “**bila nyumba wala bandari**” Jiji la Tiro lilikuwa na mgawanyiko miwili.

1. nyumba nyingi na maduka yalikuwa katika pwani kuu (kama vile Yosh. 19:29; II Sam. 24:7)
2. jumba la kifalme, hekalu na ngome vilikuwa katika kisiwa (kwa asili visiwa vidogo viwili) vilivyo mbali na pwani (kama vile Ezek. 27:32)

Hii iliufanya usiwe katika hatari mpaka Iskanda Mkku mnamo 332 k.k. alipoharibu sehemu ya pwani na kutumia mabaki katika kujenga njia ya kuelekea katika ngome ya kisiwa (kama vile Ezek. 26:3-5).

Meli kutokea Tarshishi hazikuwa na sehemu ya kutua mizigo yao wala kupokea mizigo tofauti ya kurudi nayo nyumbani.

Kuna jambo la kimuktadha linalounganishwa na “bandari.” Kibayana “kuleta” (NJB, “kukosa njia ya kuingilia,” BDB 97, KB 112, *Qal TUNGO YA KITENZI JINA*), ambayo yaweza kuashiria bandari au sehemu ya kutulia mizigo. Ni sambamba na mstari wa 14, hivyo NRSV inafasiri mstari huu kama “kwa maana ngome yako imeharibiwa.”

▣ “**Kitimu**” Toleo la MT lina “Kittim” (BDB 508), yawezekana ikiwa imechukuliwa kutoka katika jina la mji wa Kirumi katika kisiwa cha Kitimu kiiwtacho “Citium,” ambacho kwa asili lilikuwa koloni la Foenike (kama vile mstari wa 7). Baadhi wanatambua wakaazi pamoja na mmoja wa wana wa Javan, Elishah (kama vile Mwanzo. 10:4; Ezek. 27:7).

**23:2 “Tulieni”** Hii *Qal KAULI SHURUTISHI* ni sawasawa na “kuomboleza” katika mstari wa 1 (BDB 198 I). Kuna madhanio yaliyojikita katika mzizi wa Ugaritiki ambayo inaaksi mzizi tofauti (BDB 199 II) “kuomboleza” (“kulia,” TEV; “kuomboleza,” REB).

▣ “**Sidoni**” Mji huu wa pwani (kama vile Mwanzo 10:19) ya Foenike kama maili ishirini na tano kusini mwa Tiro. Kiasili lilikuwa jiji kuu (kama vile Yosh. 13:4,6). Jina linaonekana kutokea kwa wana wakubwa wa Kanaani, mwana wa Ham (kama vile Mwanzo 10:15). Tiro na Sidoni mara kwa mara vinaunganishwa pamoja katika Agano Jipya katika rejea kwa taifa la Foenike (kama vile Mt. 11:21,22; 15:21; Mdo. 12:20).

□

**NASB, NRSV,**

**NJB** “**wajumbe wako walivuka bahari**”

**NKJV** “**ambao wale waliovuka bhari wamewajaza**

**TEV** “**ulituma mawakala**”

**JB** “**ambao bidhaa zao zilisafirishwa baharini**”

Toleo la NASB inafuata gombo la Isaya kutoka DSS. Leo la MT lina “kupitiwa katika bahari (BDB 569, KB 583, Piel KAULI ILIYOTIMILIFU) zitakujaza wewe.” Neno “wajumbe wako,” katika muundo wa kuaksiwa, ni sawasawa na kiebrania kwa kitenzi “kujaza.”

1. KITENZI (מלאון (“kujaza,” BDB 569, NKJV)
2. NOMINO, מלאבין (“mjumbe,” BDB 521, NASB)

### 23:3

**NASB, JB** “**nafaka ya Nile**”

**NKJV, NRSV**  
**REB,** “**nafaka ya Shihori**”

**NJB** “**nafaka ya Mfereji**”

**Peshitta** “**mavuno yam to**”

Toleo la MT lina “nafaka ya Shihor, mavuno ya Nile.” Shihor (BDB 1009) ikimaanisha “bwawa la Horus” (KB 1477). Ikierejerea

1. tawi la mashariki ya Nile (BDB 1009)
2. mfereji wa maji meusi (BDB 1007 I)
3. ziwa katika ukanda wa mashariki

Inatamkwa tofauti katika

1. Yosh. 13:13; I Nyakati 13:5, שיחור
2. Yer. 2:18, שחר
3. Isa. 23:3, שחר

Iakini vyote vinarejerea eneo lile lile katika Misri.

▣ “**alikuwa soko kwa mataifa**” Angalia Ezek. 27:3-23.

**23:4 “Tahayari”** KITENZI (BDB 101, KB 116, *Qal KAULI SHURUTISHI*) inatumika juu ya hukumu ya Mungu juu ya sanamu (kama vile Yer. 50:2). Hapa inaashiria aibu ya taifa lililoshindwa (kama vile 1:29; 19:9; 37:27; 41:11). Mataifa haya yanaweza kupata kujua msamaha na urejesho ikiwa watamgeukia YHWH (kama vile 49:23); hii pia ni kweli watu wake mwenyewe (kama vile 29:23; 45:17; 54:4).

▣ Sidoni inabinafsishwa. Leo la Tanbihi la NRSV linasema “Sidoni iliyoharibiwa ni tasa kama bahari bila mabaharia (yaani, vijana).”

**23:7** Hii inaelezea Tiro (kama vile mstari wa 5)

1. *Jiji* lenye furaha(yaani lenye kiburi na majivuno na kutafta maslahi yake binafsi, kama vile 22:2; 24:8; 32:13)
2. *jiji* la kale sana (yaani kiburi katika antiquity zao)
3. taifa linalotawala linguine kibabe (kiburi katika ushawishi wao wa kimataifa)

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 23:8-11**

<sup>8</sup> Ni nani aliyefanya shauri hili juu ya Tiro, uliotia watu taji,  
ambao wafanya biashara wake walikuwa wana wa wafalme,  
na wachuuzi wake ni watu wakuu wa dunia?

<sup>9</sup> Bwana wa majeshi ndiye aliyefanya shauri hili,  
ili kuharibu kiburi cha utukufu wote, na kuwaabisha watu wa duniani wote pia.

<sup>10</sup> Pita katika nchi yako, kama Nile, Ee binti wa Tarshishi, hapana tena mshipi wa kukuzuia.

<sup>11</sup> Amenyosha mkono wake juu ya bahari,  
amezitikisa falme; Bwana ametoa amri katika habari za Kanaani, kuziangamiza ngome zake.

**23:8-12** Ubeti huu unaunganishwa kwa matumizi ya KITENZI “kupanga” (kifasihi. “lioshauriwa” au “kufanyiwa makusudi,” BDB 419, KB 421, *Qal KAULI TIMILIFU*, kama vile mistari ya 8,9; 14:24, 26, 27; 19:12,17). Kuna nia nyuma ya historia—YHWH! Falme za ulimwengu huu unafanya mipango zake (mstari wa 8), lakini Mungu wa uumbaji pia anafanya ya kwake (mstari wa 9).

**23:8**

NASB, NRSV	“mtoaji wa mataji”
NKJV, Peshitta	“mji utoao mataji”
TEV	“mji wa kifalme”
NJB	“ye ye atumiaye mikono kuvika taji”
REB	“jiji lenye mataji katika karama zake”

KITENZI (BDB 742, KB 815, *Hiphil ENDELEVU*) ikimaanisha “kuwekea taji.” Inaweza kurejerea

1. mtoaji wa taji (NASB, NRSV, NJB, REB)
2. mvaaji wa taji (TEV, NKJV, Peshitta)

**23:10** Falme pinzani ya baharini ya Tarshishi inakaribishwa kupanua na kujieneza kwasababu ya uharibifu wa Foenike.

Uelewa mbadala wa tungo upo katika Tafsiri ya Agano la Kale, “Palilia ardhi yako; kwakuwa hakuna meli zaidi zitokazo toka katika Ghala yako.” Hii inafuatiwa na REB, “limeni mashamba yenu, enyi watu wa Tarshishi; kwakuwa umepoteza soko lako.” Siku zenu za biashara zimekwisha,tulieni na limeni ardhi yenu .

**23:11 “Amenyosha mkono wake juu ya bahari”** Angalia dokezo katika 14:26.

▣“amezitikisa falme” KITENZI (BDB 919, KB 1182, *Hiphil KAULI TIMILIFU*) kinatumika juu ya YHWH “kutikisa” vitu kadhaa.

1. milima, 5:25
2. mbingu, 13:13
3. kuzimu, 14:9
4. bahari, 23:11
5. YHWH mwenyewe, 28:21
6. wale wajisikiao salama, 32:10,11
7. mataifa, 64:2

na mara moja wakati Yuda alipopinga YHWH katika 37:29.

▣“Kanaani” Hii ingemaanisha Tiro kama ngome pekee/bandari katika pwani ya Wakanaani au Kanaani kama njia ya kumaanisha ufalme wa Foenike wa kibiashara.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 23:12**

<sup>12</sup> Naye akasema, Usizidi kufurahi, ewe bikira uliyeabishwa, binti wa Sidoni, haya, ondoka, uende hata Kitimu; huko nako hutapata raha.

**23:12** Katika sura hii Foenike (NIV) linaitwa kwa jina la mji wake mkuu wa zamani, "Sidoni," na mji wake mkuu mpya, "Tiro."

▣ "haya, ondoka, uende hata Kitimu; huko nako hutapata raha" Baadhi wanaona hii kama kumaanisha haswa kwa mfalme wa Sidoni, "Lulli," aliyekimbia kutoka kwa jeshi la Kiashuru kla Kitimu mnamo 701 k.k., ambapo aliuwawa (Tanbihi ya JB, ukurasa wa. 1177). Hii hakika inawezekana, lakini si ya uhakika. Ushairi wa Kiebrania una utata.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 23: 13-18**

<sup>13</sup> Tazama, nchi ya Wakaldayo; watu hao hawako tena; Mwashuri ameiweka tayari kwa hayawani wa jangwani; wamesimamisha buruji zao za vita, wameyaharibu majumba yake ya enzi, akaufanya kuwa uharibifu.

<sup>14</sup> Pigeni yowe, enyi merikebu za Tarshishi;

maana ngome yenu imefanywa ukiwa.

<sup>15</sup> Basi, itakuwa katika siku ile, Tiro utasahauliwa miaka sabini, kadiri ya siku za mfalme mmoja; hata mwisho wa miaka sabini, Tiro utakuwa kama vile ulivyo wimbo wa kahaba.

<sup>16</sup> Twaa kinubi, tembea mjini,

Ewe kahaba uliyesahauliwa;

Piga vizuri, imba nyimbo nyingi,

Upate kukumbukwa tena.

<sup>17</sup> Hata itakuwa mwisho wa miaka sabini, Bwana ataizuru nchi ya Tiro, naye atarudi apate ujira wake, atafanya ukahaba pamoja na falme zote za ulimwengu juu ya uso wa dunia.

<sup>18</sup> Na biashara yake na ujira wake utakuwa wakfu kwa Bwana, hautawekwa hazinani wala hautawekwa akiba; bali mapato ya biashara yake yatakuwa mali zao wakao mbele za Bwana, wapate kula na kushiba, na kuva mavazi ya fahari.

**23:13 nchi ya Wakaldayo**" Hii inaonekana kurejerea uharibifu wa Babeli (sio Babeli mpya) kwa Ashuru (kama vile Sura ya 13-14). Zipo mbili "Wababeli" iliyotajwa katika manabii.

1. Mji mdogo na wenye uhuru kidogo uliokaribu na lango la mito Frati na Hedekeli ambayo iliasi dhidi ya Ashuru na ilivamiwa na mji mkuu wao "Wakibabeli" uliharibiwa na Sargon II (722-705 k.k.), waliochukua enzi ya kiti cha jina la Babeli "Mfalme wa Babeli." Hivyo ingerejea wafalme wa kibabeli
  - a. Merodach-baladan, alitawala 721-710 na tena 703-702 k.k. (alituma wajumbe kwa Hezekia 712 k.k., kama vile II Wafalme. 20:12-21; Isaya 39)
  - b. Shamash-shum-ukim, mwana wa Esarhaddon, 681-669 k.k. na ndugu mpinzani wa Ashurbanipal [669-633 k.k.] aliyefanywa mfalme wa Ashuru
2. mpya (yaani "mpya") Babeli ilitokea katika matukio 626 k.k. pamoja na kuinuka kwa Nabopolassor (626-605 k.k), baba wa Nebukadneza II (605-562 k.k.). Nabopolassor alikuwa kisababishi katika kuanguka kwa Asshuru (mji mkuu mmoja wa kiashuru) katika 614 k.k. na Ninawi (mji mkuu wa Kiashuru) mnamo 612 k.k. (angalia juu ya "Brief Historical Survey of the Powers of Mesopotamia" katika kiambatisho cha tatu).

▣ "ume" Je hii inarejerea Mji mkuu wa Wakaldayo wa Babeli au Sidoni/Tiro? Katika muktadha inamaanisha kwa Babeli kuharibiwa na Sargon II mnamo 710 au Senakeribu mnamo 689 k.k. Tiro ingeonekana kama kama Babeli. Waashuru, Babeli Mpya, na Iskanderia Mkuu wanakuja!!!

▣ "kwa ajili ya viumbe vyta jangwani" Neno hili (BDB 850 II) linaashiria wanyama mwitu wa aina fulani. Lina visawe vyta nyongeza vyta kukaliwa na mashetani (kama vile NIDOTTE, vol. 3, ukurasa wa 79, na fasiri za NEB, REB).

**23:15 "kwa miaka sabini"** Maelezo ya muda yanaonekana hapa na katika mstari wa 17. Inaonekana kuelezea ukamilifu kamili wa muda (kutoka 7 x 10, angalia Mada Maalum: Uwakilishi wa namba katika maandiko 11:12). Angalia baadhi ya matumizi yake katika maandiko

1. Kulipa kisasi, Mwanzo. 4:24

2. miaka ya Tera wakati Ibrahimu alipozaliwa, Mwanzo. 11:26
3. sabini katika familia ya Yakobo walihamia Misri, Kutoka. 1:5
4. wazee sabini wakati wa kipindi cha Safari ya Jangwani, Kutoka. 24:1,9; Hesabu. 11:16,24,25 (pia Ezek. 8:11)
5. hesabu ya ndugu wa Abimeleki waliouwawa, Waamuzi. 9:56
6. umri wa maisha unaotegemewa, Zaburi. 90:10 (Baraka maalum za kutosha kutoka kwa Mungu, Ayubu 42:16)
7. mapigo yaYHWH yaliua 70,000, II Sam. 24:15; I Nyakati. 21:14
8. wana sabini wa Ahabu, II Wafalme. 10:1,6,7
9. hukumu ya miaka sabini
  - a. Yuda katika Babeli, Yer. 25:11; Dan. 9:2; Zek. 7:5
  - b. Tiro, Isa. 23:15
10. Yesu aliwatuma sabini, Luka 10:1,17
11. msamaha wa mara 70 mara 7, Mt. 18:22

**“Kama siku za mfalme mmoja”** Tingo hii inaelezea utawala utegemewao wa kifalme. Miaka sabini ulikuwa muda wa umri wa maisha ya kawaida, lakini hapa inarejerea utawala wa muda mrefu ambao yawezekana unaonesha asili ya uwakilishi wa namba inayokaribia

**23:17-18** Utajiri wa Foenike itatiririka kwa watu wa Mungu waliorejeshwa (tazama pia 18:7 na 45:14, ambalo inaashiria matendo yanayofanana). Foenike haitaitikia kwa ushuhuda wa Israeli lakini inaendelea kuwa ya kipagani (yaani waabudu Baali)

## ISAYA 24

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hukumu juu ya Dunia	Kuizua Hukumu juu ya Ulimwengu	Dhana ya "Isaya" ya Matukio ya siku za Mwisho (24-27)	Bwana Atihukumu Dunia	Hukumu ya Yahweh
		Hukumu ya Ulimwengu		
24:1-6	24:1-13 (1-3)  (4-6)	24:1-23 (1-3)  (4-13)	24:1-3	24:1-6 (1-6)  Wimbo Unaohusu Nchi Iliyo Angamizwa
24:7-23 (7-23)	(7-13)			24:7-16a (7-16a)
	24:14-20  (14-16)	24:14-16a  (14:16)		Mapigano ya Mwisho
			24:16b-20	24:16-23b (16-23b)
(17-18)	(17-20)  (19-20)			
	24:21-23 (21-23)	24:21-23 (21-23)		

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA HISTORIA YA NYUMA

- A. Isaya 24-27 anaunda umoja wa kifasihi unaohusiana na nyakati za mwisho (yaani, hukumu ya ulimwengu). Hii aina ya kipekee ilio ndani ya Isaya (inayounda hatua ya kifasihi kwa ajili ya mwendelezo wa aina ya matukio ya siku za mwisho) ni uumbaji wa muundo wa Baraka na hukumu ya siku za mwisho, hasa Kumbukumbu la Torati 27-28. Isaya 24 inazungumzia hukumu ya Mungu ya kiulimwengu juu ya dunia, ambapo sura ya 25 inazungumzia dunia nzima iliyobarikiwa kwa kurejeshwa Sayuni kama vile Isa. 2:2-24).
- B. Isaya 13-23 inaonyesha hukumu ya Mungu juu ya mataifa yaliyozunguka ambayo imewaathiri watu wa Mungu. Isaya 24-27 ni hitimisho sahihi kwa muungano huu wa kifasihi. Hii aina ya hitimisho inayofanana inaweza kuonekana katika sura za 24 na 35.
- C. Angalia Mada Maalum ifuatayo

### MADA MAALUM:FASIHI YA MATUKIO YA SIKU ZA MWISHO

Kitabu cha Ufunuo ni aina ya kipekee ya fasihi ya Kiyahudi, matukio ya siku za mwisho. Mara nyingi hii ilitumika katika nyakati zilizojaa mvutano ya kwamba Mungu alikuwa katika mamlaka ya historia na angeleta ukombozi kwa watu Wake. Hii aina ya fasihi inabainishwa na

1. maana nzito ya ukuu wa Mungu kiulimwengu (Mungu aliye mmoja na kuashiliwa)
2. mapambano kati ya wema na uovu, zama hizi na zama zijazo (dhana ya uwili)
3. matumizi ya mfumo wa maneno ya siri (mara nyingi kutoka Kitabu cha Agano la Kale au fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku za mwisho katika Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipy)
4. matumizi ya rangi, namba, wanyama, wakati mwagine wanyama/wanadamu
5. matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa maana ya maono na ndoto, lakini mara nyingi kupitia upatanisho wa kimalaika
6. mitazamo ya mwanzo juu ya nyakati za mwisho (zama mpya)
7. matumizi ya muonekano wa ishara, si ukweli, ili kupasha habari za nyakati za mwisho
8. Baadhi ya mifano ya hii aina hii ya fasihi ni
  - a. Agano la Kale
    - 1) Isaya 24-27, 56-66
    - 2) Ezekiel 37-48
    - 3) Danieli 7-12
    - 4) Yoeli 2:28-3:21
    - 5) Zekaria 1-6, 12-14
  - b. Agano Jipy
    - 1) Mathayo 24, Maro 13, Luka 21, na 1 Wakorinhto 15 (katika njia nyingine)
    - 2) Ufunuo (sura 4-22)
  - c. isiyo ya umbo- mwili (ilichukiliwa kutoka D. S. Russell, *The Method and Message of Jewish Apocalyptic*, kr. 37-38)
    - 1) I Enoch, II Enoch (the Secrets of Enoch)
    - 2) The Book of Jubilees
    - 3) The Sibylline Oracles III, IV, V
    - 4) The Testament of the Twelve Patriarchs
    - 5) The Psalms of Solomon
    - 6) The Assumption of Moses
    - 7) The Martyrdom of Isaiah
    - 8) The Apocalypse of Moses (maisha ya Adamu na Hawa)

- 9) The Apocalypse of Abraham
  - 10) The Testament of Abraham
  - 11) II Esdras (IV Esdras)
  - 12) Baruch II, III
9. Kuna maana ya uwili katika fasifi hii. Hii inauangalia ukweli kama mtiririko wa uwili, tofauti, au mvutano (ni kawaida sana katika maandiko ya Yohana) kati ya:
- a. mbingu – dunia
  - b. zama za uovu (wanadamu wa uovu na malaika wa uovu) – zama mpya za wenyewe haki (watu wa Mungu na malaika wa Mungu)
  - c. Kuwepo kwa sasa – kuwepo kwa baadaye

Hizi zote zinaelekeea utimilifu ulioletwa na Mungu kumhusu Mungu. Huu si ulimwengu alioukusudia Mungu kuwa, bali Yeye azidi kutenda kazi na kuonyesha mapenzi yake kwa ajili ya urejesho wa uhusiano wa karibu ulionzia ndani ya Bustani ya Edeni. Tukio la Kristo ni mpango wa Mungu wa umwagaji maji, lakini ujio mbili unasababisha uwili wa sasa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 24:1-6

<sup>1</sup>Tazama, Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, aifanya ukiwa, aipindua, na kuwatawanya wakao ndani yake. <sup>2</sup> Na itakuwa kama ilivyo hali ya watu, ndivyo itakavyokuwa hali ya kuhani; kama ilivyo hali ya mtumwa, ndivyo itakavyokuwa hali ya bwana wake; kama ilivyo hali ya mjakazi, ndivyo itakavyokuwa hali ya bibi yake; kama ilivyo hali yake anunuaye, ndivyo itakavyokuwa hali yake auzaye; kama ilivyo hali yake akopeshaye, ndivyo itakavyokuwa hali yake akopaye; kama ilivyo hali yake atwaaye faida, ndivyo itakavyokuwa hali yake ampaye faida. <sup>3</sup> Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; maana Bwana amenena neno hilo. <sup>4</sup> Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika. <sup>5</sup> Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. <sup>6</sup> Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea, watu waliosalia wakawa wachache tu.

**24:1 “Bwana ameifanya dunia kuwa tupu”** Mstari wa1 na 3 inatumia mfuatano wa VITENZI vyenye mkazo kueleza juu ya hukumu ya YHWH juu ya dunia (hapa si “nchi” kwa sababu ya ufanano na “ulimwengu” [BDB 385, kama vile 14:16-17;34:1; Yer. 10:12; 51:15], angalia Mada Maalum ifuatayo).

1. ameifanya. . .utupu, mst. 1, BDB 132, KB 150, *Qal* ya KAULI TENDAJI ENDELEVU, kama vile mst. 3; Nah. 2:2
2. ukiwa, mst. 1, BDB 118, KB 135, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU, kama vile Nah. 2:10
3. aipindua (kifasihi. “geuza,” kama vile NRSV), BDB 730, KB 796, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
4. kuwatawanya, mst. 1, BDB 806, KB 918, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATITIMILIFU
5. itafanywa tupu kabisa, mst. 3, BDB 132, KB 150, *Niphal* ya KITENZIJINA HALISI na KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi unaofanana unaodokeza nguvu.
6. kuharibiwa kabisa, mst. 3, BDB 102, KB 117, *Niphal* ya KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi unaofanana unaodokeza nguvu. YHWH anazirudisha karama zake, alizokuba amezitoa wakati wa uumbaji (kama vile mist. 5-6). Haya ni mapinduzi ya kusudi asilia la uumbaji, lakini mabaki ya uaminifu yataishi (kama vile mst. wa 6)!

Mistari ya 1 na 3 inafanana sana na hukumu ya Mungu juu ya dunia (የተኋኒ, BDB 75) katika siku za Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9; pia zitambue juhudii za kuiepuka hukumu ya Mungu katika 2:10,19,21). Utupu wa ulimwengu mzima ni upinzani halisi wa kusudi la uumbaji!

## MADA MAALUM: ARDHI, NCHI, DUNIA (*erets*)

Kama ilivyo mizizi ya Kiebrania, muktadha ni muhimu katika kutambua maana ya mizizi iliyokusudiwa na mwandishi wa asili. Idadiya mipaka ya mizizi ya Kiebrania (yaani, lugha ya Kisemiti ya kale) inasababishakila mzizi kufanya kazi katika maana tofauti na maana nyingine. Huu mzizi (BDB 75, KB 90) unaweza kumaanisha

1. Sayari nzima (ingwa wachambuuzi wa kale hawakubainisha kiwango na umbiile lake. Mara nydingi huu unatumika kumaanisha "ulimwengu usio julikana")
  - a. Mwanzo 1-2; 6-9; 10:32; 11:1,4,8,9; 14:19; 18:18,25; 22:18, n.k.
  - b. Kutoka 9:29; 19:5
  - c. Zaburi 8:1,9; 24:1; 47:2,7; Yer. 25:26,29,30
  - d. Mithali 8:31
  - e. Isaya 2:19,21; 6:3; 11:4,9,12; 12:5
2. Dunia katika kutofautisha na mbingu
  - a. Mwanzo 1:2
  - b. Kutoka 20:4
  - c. Kumbukumbu la Torati 5:8; 30:19
  - d. Isaya 37:16
3. sitiari kwa wakazi wanadamu wakaaoo juu ya sayari
  - a. Mwanzo 6:11; 11:1
  - b. 1 Wafalme 2:2; 10:24
  - c. Ayubu 37:12
  - d. Zaburi 33:8; 66:4
4. Nchi au himaya
  - a. Mwanzo 10:10,11; 11:28,31
  - b. hasa. Israeli (zawadi kutoka kwa YHWH, Yeye anaimiliki)
5. udongo, kama vile Yoshua 7:21
6. chini ya ulimwengu (KB 91)
  - a. Kutoka 15:12
  - b. Zaburi 22:29; 71:20; Yer. 17:13; Yona 2:6
7. ulimwengu mpya
  - a. Isaya 9:1-7; 65:17; 66:22
  - b. Angalia Agano Jipya, Rum. 8:19-22; Gal. 6:15; 2 Pet. 3:13; Ufu. 21:1,5

Kumbuka, muktadha, mukatadhi, mukaradha ni muhimu. Mara nydingi mzizi tambuzi inaweza kusaidia, lakini si mara kwa mara.

Kitabu amabacho kilinisaidia kuanza kufikiri kuhusua namana neno hili lianavyotumika katika mistarai tofauti ni Bernard Namm, *Christian View of Science and Scripture*. Yeye alinishawishi katika juu ya gharika lililowahi kutokea (yaani, Mwanzo 6-9). Iweni makini na matumizi ya thiolojia yako mwenyewe katika ufanuzi wa Maneno ya lugha ya Kiingereza!

❑“**aifanya ukiwa**” Aidha hii ingekuwa stiari ya hukumu uya Mungu juu ya dunia katika maneno ya kifizikia (kif. “geuza,” BDB 730, KB 796, *Piel ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) au inaweza kuwa stiari ya Mungu kuyafanya makazi ya dunia kuwa utupu kama mtu awezavyo kusafisha sehemu za jiko zilizo chafu.

❑“**na kuwatawanya wakaaoo ndani yake**” Kifungu hiki ni sawa na istilahi iliyotumika katika Mwanzo 10 cha mnara wa Babeli. Hapa kinadokeza uhamisho.

**24:2** Kipengele hiki kinaonyesha kwamba tofauti zote za kijamii zinaonolewa. Kila mtu anahukumiwa (kama vile mst. wa 4).

**24:3 “maana Bwana amenena neno hilo”** Kifungu hiki kinaonyesha uhakika wa tukio hili kwa sababu Mungu amelisema hili (BDB 180, KB 210, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 24:3; 25:8; 40:8; 55:10-11). Pia tambua tofauti iliyokusudiwa; neno la uumbaji lililozungumzwa sasa ni neno linazungunzwa kumaanisha hukumu.

**24:4** Elewa ufanuzi kuhusu dunia.

1. inaomboleza – (1) BDB 5 I, KB 6, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Yer. 23:10; kwa ajiliya ubainishaji wa dunia, pia pia elewa mst. wa 7, au (2) BDB 5 II unamaanisha “kunyamazisha” ambalo ni neno linaendana na ufanano wa mist. ya 4 na 7 zaidi (kama vile NRSV, REB)
2. inazimia – BDB 615, KB 663, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (mara mbili)
3. wanadhoofika – BDB 51, KB 63, *Pulal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 16:8; 33:9
4. unazimia – BDB 337, KB 335, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Tambua idadi ya VITENZI vya KAULI YA WAKATI TIMILIFU katika mist. 4 na 5 ambavyo vinadokeza tendo la kuhimarishwa, tendo kamili!

VITENZI vyote vinatamkwa kwa ufanano.

Mungu wa uumbaji anatenda kazi kama mkuu katika uumbaji wake. Hii ilifanywa ili kuwa hatua kwake na mwanadamu kuwa na uhusiano naye, lakini viumbe vyake vimeharibu na kuinajisi hatua hii kwa matendo yao. Hii iliumbwaa kwa ajili ya uzidisho, lakini sasa wameangukia katika kuhukumiwa na kutozalisha.

▣ **“ulimwengu”** Hili neno la Kiebrania (BDB 385) mara nyingi linatumika katika kiunganishi na “dunia” (BDB 75, kama vile Ayubu 37:12; Zab. 96:13; 98:9; Yer. 10:12; Omb. 4:12, angalia Mada Maalum katika mst. 1). Isaya analitumia neno hili zaidi kuliko manabii wengine (kama vile NIDOTTE, juzu. 4, uk. 273, kama vile 13:11; 24:4; 34:1).

▣ **“watu wakuu wa dunia wanadhoofika”** Toleo la tafsri ya RSV (kwa mabadiliko ya irabu tu) liamaanisha kwamba kifungu hiki kinahusiana na hukumu ya mbinguni na duniani (yaani, uumbaji wote), si kwa watu wa dunia (yaani, “urefu”) waliosoma.

**24:5 “dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa”** Asili inasumbuliwa kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu (kama vile 4:20; Mwa. 3:17-19; Hes. 35:33; Yer. 3:1-2,9; Rum. 8:18-25).

1. wameziasi sheria, BDB 716, KB 778, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. wameibadili amri, BDB 322, KB 321, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. wamelivunja agano la milele, BDB 830, KB 974, *Hiphil* ya WAKATI TIMILIFU

Kifungu hiki hakiirejelei sheria ya Musa, bali kwa vyo vyote (1) ni juu ya ufunuo wa asili unaopatikana katika Zab. 19:1-6 na Rum. 1:19, 20; 2:14-15 au (2) katika siku za Nuhu (kama vile Mwa. 6:5-7, 11-12, huenda katika hali ya upekee kwa 9:4-6).

Kifungu hiki hiki “agano la milele” kinajitokeza katika Mwa. 9:16. Hili agano la milele lingeweza kuhusiana na kuchukua mfano wa maisha ya mwanadamu (kama vile 26:21). Mauaji yana matokeo! Maisha ni ya Mungu. Yeye alimtaka mwanadamu azae matunda na kuijaza nchi, si kuana!

**24:6 “laana imeila dunia hii”** Utamkaji huu unafana sana na laana ya Mwa. 3:17-19. Kithiolojia hili linatenda kazi kma Rum. 1:18-3:20; wote wametenda dhambi (yaani, wamelivunja agano, kama vile mst. wa 5) na wanahitaji wokovu wa Mungu!



**NASB, NKJV,**

<b>JB</b>	“wameangamizwa”
<b>NRSV</b>	“wameanguka”
<b>REB</b>	“wamepunguziwa”
<b>Peshitta</b>	“wataadhibiwa”
<b>LXX</b>	“watakuwa maskini”

Toleo la MT lina neno “wameteketezwa” (BDB 359 I, au 351 I, *Qul ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*). Wasomi wamependekeza mzizi mwingine wa Kiarabu, “kupunguza” (KB 351 II), ambao unahusiana na kifungu kinachofuatia.

Huu ni mfano mwingine wa ugumu katika ushairi wa Kiebrania ulio katika utata. Muktadha wa mara kwa mara ndio ulinzi pekee wa mfasiri na hata, mizizi ingine na utambuzi mwingine unawezekana. Toleo la MT si andikola Kiebrania la kale.

■ **“watu waliosalia wakawa wachache tu”** Kimsingi hili ni wazo la Agano la Kalelamabaki ya uaminifu ya kwamba Mungu amewaweka akiba watu waliosali duniani. Kipengele hiki kinaendana sana na manaeno ya Yesu aliyojanena katika Mt. 7:14. Angalia Mada Maalum: Mabaki, Namna Tatu katika 1:9.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 24:7-23**

- <sup>7</sup>Divai mpya inaomboleza,  
    mzabibu umedhoofika,  
    ~~watu wote waliochangamka moyo wanaugua.~~
- <sup>8</sup>Sauti ya furaha ya matoazi inakoma; kelele yao wafurahio imekwisha;  
    furaha ya kinubi inakoma.
- <sup>9</sup>Hawatakunywa divai pamoja na nyimbo;  
    kileo kitakuwa uchungu kwao wakinywao.
- <sup>10</sup>Mji wa machafuko umebomolewa;  
    kila nyumba imefungwa, asipate kuingia mtu awaye yote.
- <sup>11</sup>Pana kilio katika njia kuu kwa sababu ya divai; furaha yote imetiwa giza,  
    na changamko la nchi limetoweza.
- <sup>12</sup>Ndani ya mji umebakia ukiwa,  
    na lango lake limepigwa kwa uharibifu.
- <sup>13</sup>Maana katikati ya dunia, katikati ya mataifa,  
    takuwa hivi; kama wakati utikiswapo mzeituni,  
    kama wakati waokotapo zabibu baada ya mavuno yake.
- <sup>14</sup>Hawa watainua sauti zao, watapiga kelele;  
    kwa sababu ya utukufu wa Bwana watapiga kelele toka baharini.
- <sup>15</sup>Basi, mtukuzeni Bwana katika mashariki,  
    litukuzeni jina la Bwana, Mungu wa Israeli, katika visiwa vya bahari.
- <sup>16</sup>Toka pande za mwisho wa dunia tumesikia nyimbo, Atukuzwe mwenye haki.  
    Ndipo niliposema, Kukonda kwangu!  
    Kukonda kwangu! Ole wangu! Watenda hila wametenda hila,  
    naam, watendao hila wametenda hila sana.
- <sup>17</sup>Hofu, na shimo, na mtego, vi juu yako,  
    Ee mwenye kukaa duniani.
- <sup>18</sup>Itakuwa kila akimbiaye sauti ya hofu ataanguka katika shimo;  
    na kila apandaye na kutoka shimonii atanasa na mtego;  
    kwa maana madirisha yaliyo juu yamewekwa wazi, na misingi ya dunia inatikisika.
- <sup>19</sup>Dunia kuvunjika, inavunjika sana;  
    dunia kupasuka, imepasuka sana;  
    dunia kutikisika, imetikisika sana.
- <sup>20</sup>Dunia inalewa-lewa kama mlevi, nayo inawayaya-waya kama machela;  
    na mzigoo wa dhambi zake utailemea; nayo itaanguka, wala haitainuka tena.
- <sup>21</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo,  
    Bwana ataliadhibu jeshi la mahali palipo juu katika mahali palipo juu,  
    na wafalme wa dunia katika dunia;

<sup>22</sup> nao watakusanya pamoja kama vile wakusanyawavo  
wafungwa katika shimo nao watafungwa katika gereza;  
na baada ya muda wa siku nyingi watajiliwa.

<sup>23</sup> Ndipo mwezi utatahayari, na jua litaona haya;  
kwa kuwa Bwana wa majeshi atatawala katika mlima wa Sayuni, na katika Yerusalem,  
na mbele ya wazee wake kwa utukufu.

**24:7-14** Huu ni mfuatano wa sitiari zinazohusu shughuli za kawaida za kijamii za jamii ya kilimo ambazo zinafikia mwisho kwa sababu ya hukumu ya Mungu.

**24:9 “divai . . kileo”** Angalia Mada maalum katika 1:22.

**24:10 “Mji wa machafuko umebomolewa”** Kuna mzaha kupitia muungano huu wakifasihi kuhusu “mji.” Kimahususi mji huu haubainishwina, hivyo, unaonekana kuwa ishara ya jamii yote ya mwanadamu inayotenda kinyume na Mungu (sawa na mji wa Mwanzo 11). Kistiari ni sawa na matumizi ya (1) “ulimwengu” katika I Yohana na (2) “ukahaba wa Babeli” katika Ufunuo wa Yohana 18 kama yenye kuwakilisha jamii yote ya mwanadamu aliyeanguka. Mji huu unaweza kuonekana katika Isa. 25:2,3,12. Hili dokezo la mji wa Mungu linapatikana katika Isa. 26:1-6 (kama vile Ebr. 11:10,16). Kifasihi, hili neno “machafuko” (BDB 1062) linamaanisha “utupu,” “majivuno,” “isiyo na mwonekano,” “ghasia,” au “kukosekana kwa ukweli” linatumika kueleza dunia katika Mwanzo 1:2 (“isiyo na mwonekano”). Mara nyingi neno hili linatumika katika Isaya (kama vile 24:10; 29:21; 34:11; 40:17,23; 41:29; 44:9; 45:18,19; 49:4; 59:4), lakini kwa wakati mwingine linatumika kwa Manabii wote (yaani, Yer. 4:23). Mungu alianza na uumbaji wake kwa Nuhu (Mwanzo 6-9), sasa atalifanya hili tena! Angalia Jedwali la Miji “Miwili” katika Utanguliziwa sura ya 26, D.

**24:12 “lango lake limepigwa kwa uharibifu”** Hiki KITENZI (BDB 510, KB 507, *Hophal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinadokeza kwamba “mji usiobainishwa” ni udhaifu, malango yake yako katika magamba! Nani aweza kusimama mbele ya YHWH?

**24:13 “Maana katikati ya dunia, katikati ya mataifa”** Kipengele hiki knawea kufasiriwa katika namna mbili: (1) kinaweza kuwarejelea watu wote wa duniani (kama vile mst. 1 na Isa. 11:10 ) au (2) kinaweza kuwarejelea Wayahudi walismabaa kwa sababu ya Uhamisho (kama vile 11:11 na 24:8). Ni vigumu kufanya uamuzi kuhusiana na hoja hii, lakini kwangu mimi inaonekana hivi kwa sababu ya mist. 14,16 na 25:6,7, hapa tunauzungumzia ulimwengu (yaani, uchaguzi #1) ulio kibainishi cha Isaya. Ulimwengu ni wa kipekee katika mwaliko wake, mataifa yote Misri na Ashuru kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu katika Isa. 19:18-25.

▣**“kama wakati utikiswapo mzeituni,**

**kama wakati waokotapo zabibu baada ya mavuno yake”** Hii ilikuwa stiari ya kilimo inayozungumzia uvunaji. Hii inadokeza dhamna kwamba kutakuwa na nwatu wachache watakao wabakizwa (kama vile mst. 6; Mik. 7:1). Mistari 14-16 ni muungano wa sifa zinazowarejelea wale wanaomtumainia YHWH. Hiii ni sifa bainishi ya umoja huu wa kifasihi nah ii ni aina ya kipekee katika Isaya ya kuahidi haki ya baraka katikati ya hukumu.

**24:14-15 “baharini . . mashariki”** Hili neno “mashariki” (BDB 410) kiuhalisia ni “baharini” na linarejelea Bahari ya Shamu. Neno “mashariki” (BDB 22) kiuhalisia ni “nuru” ambayo inarejelea mawio ya jua. Tena, haya maneno mawili yanairejelea Misri hadi magharibi na Ashuru hadi magharibi (kama vile 19:23-25).

**24:15** The Jewish Study Bible inadai kwamba baadhi ya makundi (Yuda au Mataifa yamekuwa yakimtumainia YHWH, mist. ya 15,16a; 25:3) yameanza kumshukuru Mungu katika sifa (mst.14) ya kwamba hukumu imefikia mwisho, lakini ghafla yalitambua kwamba sivyo (kama vile mist. ya 16b-23).

Kuutambua ukuu na utukufu wa YHWH ni ishara iliyo dhahiri ya uhusiano mpya pamoja naye (kama vile 12:5; 26:10). Wanadamu wachache (Myahudi na Mataifa), mabaki ya uaminifu (kama vile mst. 6; angalia Mada Maalum

katika 1:9) yapatikana katika uaminifu hata katkati ya hukumu (kama vile Hab. 2:4).

▣“**katika visiwa vya bahari**” Katika LXX kifungu hiki kinamaanisha “visiwa,” ambavyo mara kadhaa vimekuwa vikirejelewa na Isaya kwa Mataifa (kama vile 41:5; 42:4,10).

**24:16a** Hili ni rejeleo lingine la kipengele cha ulimwengu cha hitimisho la waamini wa Mataifa(kama vile 2:2-4).

▣“**mwenye haki**” Tafsri zamatoleo ya NASB na NRSV yanakigusia kifungu hiki kwa ajili ya kumdokeza Mungu wa Israeli.

Matoleo ya Peshitta, KJV, na ASV yana kifungu “haki,” ambacho ni kifungu kingine kwa mabaki ya mabaki ya waaminio ambao wataokolewa nje ya Israeli na watu wa duniani. Tafsri ya REB ina kifungu “taifa lenye haki,” kwa udhirisho hili wazo linalohusu taifa la Israeli.

**24:16b** Ni dhahiri kuwa hapa kuna pumziko ambalo halibainishwi vema na utamaduni wa migawanyo wa mstari. Kutokana na kipengele dhahiri cha sifa za mist. ya 14-16a, mst. 16b inaanza na maombolezo yanayohusiana na hukumu ya Mungu inayokuja (tambua “huzuni” [mara mbili, kif. “nitabakizwa au nitaachwa”] na “huzuni,” hiki ni KIHISISHI, BDB17). Uhusiano wake halisi wa muktadha huu ni kwa kiasi fulan haujulikani. Hili linaweza kuwa pendekezo binafsi la Isaya mwenyewe ambapo siku yake mwenyewe haiendani, mist. ya 14-16a. Kumekuwa na tafsri nydingi na tofauti tofauti za lugha za Kiingereza za kifungu hikie.

The AB Commentary (uk. 353) inaeleza kwamba kifungu hiki kinaondolewa na ile Tafsri ya Maadiko ya Agano la Kale la Kiebrania na mwandishi (Blenkinsop) anadhani kuwa huu ni mzizi wa Kiaramu wa neno “siri,” ambao unafuata matoleo ya utamaduni wa ufundishaji wa sheria za Kiyahudi na Peshitta na Vulgate.

**24:16c,d** Huu ni mzaha wa nguvu sana. Kuna matumizi kadhaa ya neno moja (BDB 93, KB 108), ambayo yana nguvu, yenye msistizo unaorudiwa rudiwa juu ya suala la uaminifu, watu walio matepeli. Tambua

1. Watenda hila, BDB 93, KB 108, *Qal* ya KAULI TENDAJI ENDELEVU
2. wametenda hila, BDB 93, KB 108, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. NOMINO, BDB 93 I (kama vile Yer. 12:1)
4. marudio ya #1
5. marudio ya #2

**24:17** “Hofu, na shimo, na mtego, vi juu yako”Huu muundo wa kucheza na sauti katika maneno yale yale. Maneno yote haya (BDB 808, 809, 809) yanatumika kumaanisha kuwanasa wanyama (kama vile Yer. 48:43,44).

<b>NKJV, Peshitta</b>	<b>“kelele za hofu”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“kele za mwenye hofu”</b>
<b>NJB</b>	<b>“kilio cha mwenye woga”</b>
<b>LXX</b>	<b>“mwoga”</b>
<b>REB</b>	<b>“kelele za hofu”</b>

Toleo la MT kifungu “katika sauti ya mwenye hofu (BDB 876 TUNGO BDB 808 ). Hili ni dokezo la (1) sauti ya mapambano (kama vile Isa. 29:6; Yer. 4:19,21; Eze. 1:24), (2) sauti ya Mungu (kama vile 30:30-31), au (3) dhana ya agano (kama vile Yer. 3:13,25; 7:23; 11:4,7; 26:13; 38:20).

▣“**na shimo . . . na mtego**” Hivi ni vidokezo kwa mwanadamu ambaye hunaswa kama wanyama (kama vile 8:15; 28:13). Wanadamu watajaribu kuikwepa hukumu ya Mungu ili ni kutafuta mitikisiko tu (kama vile 2:10,19-22).

**24:18c “maana madirisha yaliyo juu yamewekwa wazi ”** Hili ni dokezo lingine la maelezi ya gharika la Mwanzo (kama vile 7:11; 8:2). Kufungu amadirisha ya mbinguni yanaweza kuwa kwa ajili ya baraka (yaani, maji kwa ajili ya

kilimo na mifugo,kama vile II Fal. 7:2,19; Mal. 3:10) au hukumu (yaani, kuachilia maji mengi, kama vile Mwa. 7:11; 8:2; Isa. 24:18, au kutokuwa na maji).

**24:19** Tambaua ufanano unaotokana na KITENZI JINA HALISI na KITENZI kinachoendana.

1. inavunjika sana, BDB 949, KB 1270, *Qal ya KITENZI JINA HALISI na Hithpoel KAULI TIMILIFU*
2. imepasuka sana, BDB 830, KB 975, *Qal ya KITENZI JINA HALISI na Hithpoel ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
3. imetikisika sana, BDB 556, KB 555, *Qal ya KITENZI JINA HALISI na Hithpoel ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*

Huu muundo unaofanana (yaani, KITENZI JINA HALISI na muundo wa KITENZI kutokana na mzizi ule ule) unaendelea katika mst. wa 20, BDB 631, KB 681, *Qal ya KITENZI JINA HALISI na Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*. Dunia, iliumbwba kwa ajili ya Mungu na mwanadamu kukutana na kuwa na ushirika, iliumbwba kwa ajili ya utele na uzima, has become rimekuwa ya uovu na itaangamizwa

1. kwa maji, Mwanzo 6-9
2. kwa neno lililozungumzwa, Isa. 24:3
3. kwa taswira ya matukio ya siku za mwisho, Yer. 4:23-28
4. kwa moto, II Pet. 3:10-11

**24:20** Ulevi (yaani, kustaajabu, BDB 631, KB 681, KITENZI JINA HALISI na KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU cha mzizi ule ule) mara nyingi kinatumika kama ishara ya hukumu katika Agano la Kale (kama vile Isa. 19:14; 28:7,8; 29:9).

▣ “**nayo inawayaya-waya kama machela**” Hili ni dokezo linguine la kiutamaduni wa kutengeneza kibanda kidogo (BDB 434) ambacho kilijengwa uwanjani wakati wa mavuno kwa ajili ya makazi mtu ili mtu huyo aweze kulinda mazao (kama vile 1:8). Mistari ya 19-20 inaeleza juu ya dhambi iliyouelemea uumbaji wa kimwili (kama vile Rum. 8:18-22).

▣ “**wala haitainuka tena**” Huu ni usemi wa kiuchochazi wenye kuonyesha namna nguvu ya hukumu ya Mungu juu ya dunia iliyopotoka. Lakini kutokana na maandiko mengine, tufahamu kwa atakuwa na huruma juu yake na kuirejesha! Kwa matumizi ya lugha ya kiuchochazi na fasihi ya matukio ya siku za mwisho angalia D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic*.

**24:21 “katika siku hiyo”** Angalia maelezo katika 2:11. Hii dhana ya matukio ya siku za mwisho inarudiwa katika 25:9; 26:1,2,12.

▣ “**jeshi la mahali palipo juu katika mahali palipo juu**” Katika Agano la Kale kifungu hiki kinarejelea miungu ya akinajimu ya Babeli (kama vile 40:26; 45:12). Hata hivyo, katika muktadha huu kifungu hiki kinarejelea dhana ya Agano la Kale inayozungumzia malaika wa mataifa (kama vile Kumb. 32:8 katika LXX na Danieli 10). Mungu atawahukumu wote wanadamu walio mwasi au juu ya matendo ya kishetani (angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, uk. 179).

**24:22** Wafalme wote wa dunia walio na kiburi na majivuno (kama vile 10:12; 13:11) na malaika wa mataifa walio asi (kama vile LXX la Kumb. 32:8 na Dan. 10:10-13) watahukumiwa na kutiwa gerezani. Huu ni ufanano na II Pet. 2:4; Yuda, mst. wa 6; na Ufu. 20:1-3. Hili linaonekana kuwa dokezo la Sheol (Agano la Kale) au Tartarus (Agano Jipya). Angalia Mada Maalum katika 5:14.

Baadhi ya wasomi wamekuekuwa wakidai kwamba kifungu “baada ya siku nyingi” kinarejelea ile miaka elfu ya Ufu. 20:1-6. Hii ni miaka elefu inayo fanana ambayo wasomi hawa ambao kwa namna isiyo stahili wanautafuta ushahidi wa kibiblia kwa ajili ya wakati uliotajwa katika Ufunuo wa Yohana 20. Angalia maoni yangu yaliyoandikwa kuhusu Ufunuo wa Yohana 20 mtandaoni katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

▣ “**Wafungwa**” Muundo huu (BDB 64) unapatikana hapa tu nani ondoleo lalililo katika DSS, the LXX, na Targums ya Karamu.

**24:23 “mwezi utashushwa na juu kuaibishwa”** Lugha hii ya Kimatukio ya siku za mwisho yanayozungumzia matukio ya kimajanga ya asili kama Muumbaji anavyojongea. Uwepo wa Bwana Mwenyewe utafanyika nuru kwa mwanadamu (kama vile Isa. 30:26; 60:19, 20; Ufu. 21:23; 22:5).

▣ **“Bwana wa majeshi atatawala katika mlima wa Sayuni, na katika Yerusalem”** Hapa tena ni kipengele cha kiulimwengu kinachohusu ulimwengu kukusanya Yerusalem kwa ajili ya kumjua Mungu wa kweli (kama vile. Isa. 2:2-4; 24:23; 25:6-7; 27:6,13). Taswira hii imewekwa wazi kiulimwengu kuhusu utawala wa YHWH juu ya dunia yote katika Dan. 2:35,44-45!

▣ **“na mbele ya wazee wake kwa utukufu”** Hawa wazee (BDB 278) walikuwa wale wazee wa siku za Musa (yaani, Kut. 3:16,18; 4:29; 12:21, n.k.). Hili eneo lilitokeza wanaume wazee wa makabila tofauti. Dhana hii ilikuja kuwa msingi wa uongozi wote. Katika Isaya wazee hawana majukumu mengi (kama vile 3:2-3; 9:14-16), bali hapa katika siku za mwisho wataushikilia utakufu wa YHWH (dhahiri katika kusujudu na kuheshimisha, yaani, wazee waliolekwa). Robert Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament* (uk. 245) anasema kuwa hawa ni wawakilishi wa watu wa Mungu.

## MADA MAALUM : WAZEE

1. neno hili linatumika kumaanisha malaika wa Mungu wanaounda baraza la kimalaika (kama vile. Isa. 24:23). Istilahi zinazofanana zinatumika kwa viumbe wa kimalaika wa Ufunuo wa Yohana (kama vile. 4:4,10; 5:5,6,8,11,14; 7:11,13;11:16; 14:3; 19:4).
2. linatumika kumaanisha (*zaqen*) katiaka Agano la Kale (kama vile Kutoka 3:16; Hes. 11:16). Katika Agano Jipya baadaye neno hili lilitumika kwa kundi la viongozi toka Yerusalem amabao walioounda mahakama kuu ya Wayahudi, Wakuu wa Sinagogi (kama vile Mt. 21:23; 26:57). Katika siku za Yesu hiki chombo chenyе watu sabini kilitawaliwa na ukuhani uliopotaka.
3. Neno hili lilitumika kwa viongozi wa mahali wakanisa la Agano Jipya. Hili ni moja ya maneno ya visawe (mchungaji, mwaonaji, na mzee kama vile Tito: 1,5,7; Matendo ya Mitume 20:17,28). Petro na Yohana wanalitumia neno hili kujijumuisha katika kundi la uongozi (kama vile I Petro 5:1; II Yohana 1; III Yohana 1).
4. Neno hili lilitumika kwa wazee wa kanisa, neno hili si la muhimu katika sana katika uongozi (kama vile I Tim. 5:1; Tito 2:2).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini sura za 24-27 zinaitwa sura za matukio ya siku za mwisho?
2. Ni katika vifungu vipi vya Agano la Kale Isaya anatengeneza kielelezo cha taswira yake?
3. Ni kwa namna gani mji wa uaminifu wa 1:26 unahusiana na mji wenye machafuko katika 24:10?
4. Nani anayezungumza katika mist. ya 14-16a na nani aliye katka mst. wa 16b?
5. “jeshi la mbinguni” ni lipi (kif. “jeshi la juu mahali pa juu”)?

## ISAYA 25

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Wimbo wa sifa kwa Ajili ya msaada wa Mungu	Sifa kwa Mungu	Zaburi za shukrani	Nyimbo za sifa	Nyimbo za shukrani
25:1-5 (1-5)	25:1-5 (1-5)	25:1-5 (1-5)	25:1-5 (1-5)	25:1-5 (1-5)
		Kipengele cha tatu Chenye matukio ya Siku ya mwisho	Mungu anaandaa karamu	Karamu ya Kiungu
25:6-12 (6-12)	25:6-8 (6-8)	25:6-10a (6-10a)	25:6-8	25:6-12 (6-8)
	25:9-12 (9)		25:9	(9-12)
		Ufunuo wa hukumu	Mungu ataiadhibu	
		25:10b-12 (10b-12)	Moabu	
			25:10-12	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Ni sura ya ajabu kiasi gani kuhusu pendo la YHWH kwa ulimwengu
  - 1. mpango wa ukombozi wa Mungu, mst. 1d
  - 2. tabia ya upendo wa Mungu, mst. 4
- B. Hii sura ni mwanzo wa Agano la Kale la wingi wa
  - 1. Maelezo ya Yesu (yaani., Yn 5:28-29)
  - 2. Maelezo ya Paulo
    - a. katika I Wakorintho 15 juu ya ufufuo, mst. 54
    - b. kusudi la pazia katika II Kor. 3:15-16 na Efe. 4:18
  - 3. Matumizi ya Yohana ya sura ya Agano la Kale kwenye ufunuo

- a.wakafutwa machozi, Ufu. 7:17; 21:4
  - b.miji ya kidunia ikaangamizwa (yaani., Babeli, Ufu. 14:8; 16:19; 18:2)
  - c. karamu ya Kimasihi, Ufu. 19:9
4. Mpango wa ukombozi wa Luka ulioamriwa kabla katika Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; pia kumbuka Luka 22:22 (angalia Isa. 2:2-4; 9:6-7; 11:1-10)
- C. Hii ni moja ya mitazamo sahihi kati ya miingi ya ufufuo katika agano la kale
1. Isaya 26:19
  2. Ayubu 14:14; 19:25-27
  3. Ezekiel 37:12-14
  4. Danieli 12:2

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:1-5

<sup>1</sup> Ee Bwana, wewe u Mungu wangu;  
**Nitakutukuza na kulihimidi jina lako;**  
**Kwa kuwa umetenda mambo ya ajabu,**  
**Mashauri ya kale, kwa uaminifu na kweli.**  
<sup>2</sup> **Kwa sababu umefanya mji kuwa ni chungu;**  
**Mji wenyе boma kuwa ni magofu;**  
**Jumba la wageni kuwa si mji;**  
**Hautajengwa tena milele.**  
<sup>3</sup> **Kwa hiyo watu walio hodari watakutukuza,**  
**Mji wa mataifa watishao utakuogopa.**  
<sup>4</sup> **Maana umekuwa ngome ya maskini,**  
**Ngome ya mhitaji katika dhiki yake,**  
**Mahali pa kukimbilia wakati wa tufani,**  
**Kivuli wakati wa hari;**  
**Wakati uvumapo upepo wa watu watishao,**  
**Kama dhoruba ipigayo ukuta.**  
<sup>5</sup> **Kama vile hari katika mahali pakavu Utaushusha mshindo wa wageni;**  
**Kama ilivyo hari kwa kivuli cha wingu,**  
**Wimbo wa hao watishao utashushwa.**

**25:1 “Ee Bwana, wewe u Mungu wangu”** Kipengere hiki cha Isaya ni cha kibinasi (kama vile 61:10). Isaya anamjua YHWH (ni mwakilishi sahihi wa agano la kiroho) na kuomba kwake kama rafiki, Mwokozi, na Mwenye Enzi!

Tambua namna Isaya anavyomwelezea YHWH.

1. Nitalikuza, mst. 1, BDB 926, KB 1202, *Polel KAULI ISIOTIMILIFU* iliyotumika katika maana ya KUSIHI
2. Nitalihimidi jina lako, mst. 1, BDB 392, KB 389, *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU* ikitumika katika maana ya KUSIHI

Tambua namna anavyomwasilisha Mungu.

1. Wewe u Mungu wangu, mst. 1
2. Umetenda mambo ya ajabu, mst. 1
3. Mashauri ya kale yamekuwepo kwa uaminifu na kweli, mst. 1
4. Umefanya miji kuwa ni chungu, mst. 2
5. Watu walio hodari watatukuzwa, v. 3
6. Maana umekuwa ngome ya maskini, mst. 4
7. Mahari pa kukimbilia wakati wa tufani, mst. 5

Hii ni zaburi ya sifa, sio kama Zaburi ya 145. Hii ni kinyume cha kithiolojia cha hukumu ya ulimwengu ya sura ya 24.

NRSV	“mambo ya ajabu”
TEV	“mambo ya kushangaza”
NJB	“ajabu”

## MADA MAALUM: MAMBO YA AJABU (מַדָּאַלְעָם)

Neno (BDB 810, KB 927) linaonyesha kitendo ambacho wanadamu hawawezi kukitimiliza wao wenyewe au hata kukielezea, vitendo vyenye kusababisha maajabu na mshangao (kama vile Mwa. 18:14; Yer. 32:17,27; Zak. 8:6).

### KITENZI

1. Waisraeli kuondoka Misri, Kut. 3:20; 34:10; Mika. 7:15
2. mapigo, Kumb. 28:59
3. kuvuka Mto Yordani, Yos. 3:5
4. mambo ya Mungu yaliyopita, Amu. 6:13; 1 Nya. 16:9,12,24; Neh. 9:17
5. kuzaliwa kwa Samson, Amu. 13:19
6. upendo wa Daudi kwa Yonathani, 2 Sam. 1:26
7. mara nyingi kwa Ayubu, 5:9; 9:10; 10:16; 37:5,14; 42:3
8. mara therathini na mbili katika Zaburi
9. baraza la YHWH, Isa. 28:29
10. matendo ya YHWH, Isa. 29:14 (mara mbili); Yoeli 2:26

### NOMINO

1. kupewa ruhusa kwa Waisraeli ,Kut. 15:11; Zab. 77:11,14; 78:12
2. kuhusiana na wafu, Zab. 88:10,12
3. mbingu zinasifu matendo ya YHWH, Zab. 89:5
4. sheria za YHWH, Zab. 119:129
5. Masihi wa YHWH, Isa. 9:6
6. matendo ya YHWH, Isa. 25:1; 29:14
7. matukio ya siku ya mwisho, Dan. 12:6

Mungu anatenda kwa namna ya ukombozi wenye nguvu kujidhirisha Yeye Mwenyewe kwenye uumbaji wake (mwanaadamu). Anawahitaji waje kwake na kumwamini. Matendo yake ni ufunuo, uwekaji kumbukumbu wa matendo hayo ni uvuvio, na kuyaelewa matendo hayo ni nuru. YHWH anahitaji ulimwengu umujue Yeye! Angalia Mada Maalum zifuatazo.

1. Mada Maalum: Akamjua
2. Mada Maalum: Uvuvio
3. Mada Maalum: Nuru

▣ “**Mashauri ya kale, kwa uaminifu na kweli**” Mungu yupo katika udhibiti kamili wa historia. Hili ni somo lenye kujirudia katika agano la kale (yaani., Isa. 14:24,26-27; 23:8,9; 46:10-11). Historia sio kitu cha kujirudia, bali ni cha kithiolojia. Hapana KITENZI katika andiko la Kimasoreti (“kilichojitokeza”ni cha kusadikika). Maneno mawili ya Kiebrania yaliyotafasiliwa “kwa uaminifu na kweli” yanatoka katika asili moja.

1. la kwanza (אִמְוֹבֵה, BDB 53) linamaanisha “kuwa imara,” “ustahimilivu,” au “mwaminifu.” Ni NOMINO JINSI YA KIKE (kama vile Zab. 88:12; 89:1,2,5,8; Hosea 2:20).
2. Lile la pili (אִמְמָה, BDB 53) linamaanisha “kusadiki,” au “uaminifu.” Ni NOMINO JINSI YA KIUME (kama vile 26:2; Kumb. 32:20).

Kwa pamoja (jamii ya maneno yanayokubaliana) yanadokeza uaminifu kamili wa Mungu katika mipango yake, ahadi, na makusudio yake (yaani., Mwa.3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Isa. 2:2-4; 19:23-25, angalia Mada Maalum katika 1:3).

**25:2 “mji kuwa ni chungu”** Hapa tena pana mji unaowakilisha uasi wa mwanadamu (kama vile 24:10). Unasimama kwa ajili ya kila mji mkuu wa kila jamii ya mwanadamu anayejaribu kujitengenezea njia zake na kuyakabili mahitaji yake pasipo Mungu. Angalia kumbukumbu katika 24:10 na jedwali katika sura ya 26, utangulizi D.

Neno “chungu” (BDB 164) limetumika kama lundo la magofu baada ya mji kuangamizwa (kama vile 37:26; II Fal.19:25; Yer. 9:11; 51:37). Miji iliyoimarishwa ilikuwa na ulinzi imara, lakini sasa imerundikiwa mawe!

▣“**jumba la wageni**” Toleo la JPSOA limeliboresha hili kuwa “ngome ya watu wenye kiburi” (tanbihi), likifuatiwa na toleo la JB, *The Bible: An American Translation*, cha Smith and Goodspeed, na *A Translation of the Old Testament Scriptures From the Original Hebrew* cha Spurrell. Toleo la LXX lina “mji wa wasiomcha Mungu.”

Hili linajumuisha badiliko toka

1. Toleo la MT, זָרִים, BDB 266 I, KB 267, *Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA*, “mgeni”
2. . זָדִים, BDB 267, “jeuri,” “mwenye kiburi”

Huu ni mkanganyiko wa Kiebrania wa herufi “R” na “D,” ambazo zinaonekana kufanana.

**25:3 “watu walio hodari watakutukuza”** Hii yumkini inarejerea kwenye makundi mbalimbali ya watu wa mataifa.

1. 18:2,7 (Kushi)
2. 19:19-25 (Misri na Ashuru)
3. 24:14-15 (mataifa ya Magharibi na Mashariki [Pwani])

Neno “watu walio hodari” (BDB 766 & 738) linafanana na “mataifa jeuri” (BDB 156 & 792, mistari ya 4d,e na 5). Udhahirisho wa nguvu za YHWH (yaani., “mambo ya ajabu,” BDB 810, mst. 1) zikawashawishi kuwa Yeye ni Bwana wa ulmwengu.

▣“**mji wa mataifa watishao watakuogopa**” Hapa tena kuna mchezo juu ya neno “mji,” lakini dokezo linaonekana kuwa hata hizi miji zenye kuasi (yaani., 24:10; 25:2,3,12; 26:1-6) zinaelekea siku moja kumsifu na kumtumikia Mungu. Mshangao wa Isaya lakini wenye kujirudia kwa wote (yaani., 2:2-4; 19:23-25; 24:14-16a; 43:21) unaonekana tena (kumsifu Mungu!).

**25:4** Hili ni dokezo la wazi kwa Mungu kuwajali wale wote wasio kubalika kijamii na kidini (yaani., 4:5-6; 32:2). Mungu anawapenda masikini (kama vile 29:19). Tambua namna YHWH anavyotenda dhidi ya masikini, wasio na msaada na wale wasikubalika kijamii.

1. Mlinzi kwa wasio na msaada
2. Mlinzi kwa wahitaji walio katika dhiki
3. Kimbilio wakati wa tufani, kama vile 4:6; 32:2
4. Kivuli wakati wa hari

Hili ni tofauti toka kwenye neno “watishao” (BDB 792, kama vile 29:5,20). Hii ndiyo namna jamii ilitakiwa kuwa (yaani., Kutoka 20; Kumbukumbu la Torati 5).

Pia tambua kuwa hawa watu wenye uhitaji na masikini lazima watafute ukweli toka kwa YHWH na ahadi yake ya msaada. Mungu anatenda na wanadamu walioanguka katika ushirika wa agano. Mara zote anachukua fursa na kuweka masharti, lakini mwanadamu lazima aitikie (kama vile Zab. 50:15; 91:15; 107:6,13) kwenye zawadi yake ya toba, imani, utii, na ustahimilivu. Matoleo yote ya Agano la Kale na Agano Jipya yana faida na wajibu! Angalia Mada Maalum katika 1:3.



<b>NASB</b>	“kama dhoruba ipigayo ukuta”
<b>NKJV, Peshitta</b>	“kama dhoruba ipigayo ukuta”
<b>NRSV</b>	“kama mvua yenye dhoruba wakati wa baridi”
<b>TEV, NJB</b>	“kama dhoruba majira ya baridi”
<b>REB</b>	“kama dhoruba wakati wa theruji”

Toleo la MT lina neno “dhoruba” (BDB 281, kama vile 4:6; 28:2; 30:30; 32:2) na “ukuta” (קִרְבָּה, BDB 885, kama vile 22:5; 38:2; 59:10). Neno lenye kufanana na “baridi” (ברִידָה, NRSV, TEV, NJB, REB, NIDOTTE, juzu ya 3, kur.

994, 995, גֶּר linatoka kwenye גֶּר, BDB 903). Mpango wa andiko la Kiebrania la toleo la UBS linapatia neno "ukuta" alama A (iliwa na uwezekano mkubwa).

**25:5 "wimbo wa hao watishao"** Toleo la JPSOA linabadilisha andiko la Kiebrania toka kwenye neno "wimbo" kwenda kwenye neno "dhoruba" (kama vile mst. 4).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 25:6-12**

<sup>6</sup> Na katika mlima huu Bwana wa majeshi atawafanyia mataifa yote karamu ya vitu vinono,  
karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake,  
karamu ya vinono vilivyoja mafuta,  
karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake, iliyochujwa sana.  
<sup>7</sup> Naye katika mlima huu atauharibu uso wa sitara iliyowekwa juu ya watu wote,  
na utaji ule uliotandwa juu ya mataifa yote.  
<sup>8</sup> Amemeza mauti hata milele;  
na Bwana MUNGU atafuta machozi katika nyuso zote;  
na aibu ya watu wake ataiondoa katika ulimwengu wote;  
maana Bwana amenena hayo.  
<sup>9</sup> Katika siku hiyo watasema, Tazama,  
huyu ndiye Mungu wetu,  
Ndiye tuliyemngoja atusaidie;  
Huyu ndiye Bwana tuliyemngoja,  
Na tushangilie na kuufurahia wokovu wake.  
<sup>10</sup> Kwa maana mkono wa Bwana utatulia katika mlima huu,  
na Moabu atakanyagwa chini huko aliko,  
kama vile majani makavu yakanyagwavyo katika maji ya jaa.  
<sup>11</sup> Naye atanyosha mikono yake katikati yake,  
kama vile aogeleye anyoshavyo mikono yake ili aogelee,  
naye atashusha kiburi chake, pamoja na hila za mikono yake.  
<sup>12</sup> Na boma la ngome ya kuta zako ameliinamisha,  
na kulilaza chini, na kulitupa chini hata mavumbini.

**25:6 "Katika Mlima huu Bwana wa Majeshi atawafanyia mataifa yote karamu ya vitu vinono"** Hapa Mlima Sayuni unaonekana kuwa picha ya tendo la Mungu wakati wa tukio la mwisho (kama vile 2:2-4; Kut. 24:11; Mt. 8:11; Luka 14:15; 22:16; Ufu.19:9). Hii karamu ya Kimasihi ni kwa ajili ya watu wote (kama vile 27:13; 66:20). Mungu atatoa chakula kizuri (kama vile Isa. 55)!

▣ "katika Mlima huu" Hili linarejerea Mlima Sayuni uliofanywa upya (yaani., Yerusalem) au Mlima Moria (yaani., hekalu) katika Yuda (kama vile 24:23). Yerusalem, katika muktadha wa tukio la siku ya mwisho, ingalirejerea

1. Kwa maana ilio wazi kwenye mji wa Yuda
2. Kiishara kwenye nchi mpya (kama vile Ufu. 21:1-2)

▣ "mvinyo" Tambua aina tofauti tofauti.

1. Mvinyo wa muda mrefu, BDB 1038 II, hii inarejerea kwenye mvinyo uliokaa kwa muda
2. Mvinyo ilio bora, BDB 279, KB 279, *Pual HALI YA KUENDELEA*, hili linarejerea kwa mvinyo ilio safi baada ya kukaa kwa muda mrefu, kuifanya ionekane ya thamani.

Angalia Mada Maalum: Kilevi na Ulevi katika 1:22.

**25:7 "Naye katika mlima huu atauharibu uso wa sitara iliyowekwa juu ya watu wote,  
na utaji ule uliotandwa juu ya mataifa yote"** Hili ni la muhimu sana. Tambua tena kuwa Mungu anakwenda kuondoa kitu Fulani (kifashi "nyuso" [BDB 815], "uliotandwa" [BDB 532, KB 523, *Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA*], "uliotandwa" [BDB 532, KB 523, *Qal KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA*]; kifungu mfanano kwa

maana iliyowazi ni “utando” [BDB 697], “ambao hutanda” [BDB 651 II, KB 703, *Qal KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA*], au “kudaliziwa” [BDB 651 II, NASB kumbukumbu za kipambizo, NIDOTTE, juzu 3, uk. 253]) toka kwa watu wa mataifa (“juu ya watu wote” ikifanana na “juu ya mataifa yote,” hivi ni vifungu jumuishi, vyatatu watu wote) kwamba wapate kuja kwake. Pamekuwepo na nadharia mbalimbali kuhusu hili neno “kutanda.”

1. Kifo chenyewe (kama vile mst. 8, unakirudia KITENZI cha mst. 7)
2. ishara ya kuomboleza kwa ajili ya aliyekufa (cf. II Sam. 15:30)
3. ishara ya aibu (kama vile II Sam. 19:5; Yer. 14:3)
4. Upofu wa kiroho (kama vile II Kor. 3:15-16; Efe. 4:18)
5. Asili ya Kiebrania ya neno לֹט (BDB 532) hutoke aha tu. Linahusiana na וְ (BDB 532), ambalo humaanisha “siri” (kama vile Ruth 3:7; I Sam. 18:22; 24:4 na mara nydingi hurejerea kwenye ibada ya sanamu, kama vile Kut. 7:22; 8:7,18).

Neno “kutanda” laweza kurejerea kwenye dini za uongo ambazo zimepofusha macho ya mwanadamu aliyeanguka (kama vile Rum. 1:21-32).

**25:8 “amemeza mauti hata milele”** Ni maelezo ya kustaabisha kiasi gani! Mwonekano wa asili wa Edeni umerejeshwa (kama vile 65:19-20). Wanadamu waasi, wenyenye kutenda dhambi wanaweza kuokolewa moja kwa moja! Ufufuko hasa umetajwa katika 26:19 (kama vile Ayubu 14:14; 19:25-27; Ezek. 37:12-14; Dan. 12:2; I Wakorintho 15).

Mauti imetawala toka kwa Adamu mpaka kwa Kristot (kama vile Rum. 5:12-21), lakini kwa kufufuka kwake Yesu, kifo kimeshindwa (kama vile Hosea 13:14 ikinukuriwa katika I Kor. 15:55-57).

Katika Agano la Kale nafsi itendayo dhambi ndiyo itakayo kufa (kama vile Ezek. 18:4,20; Rum. 6:23). Agano la Musa lilikuwa ni agano liliogamia juu ya utendaji (kama vile Law. 18:5; Gal. 3:12), lakini kutohakana na angukol (kama vile Mwanzo 3) na udhaifu wa mwanadamu ikajakuwa ni laana, hukumu ya kifo (kama vile Gal. 3:13; 4:5). Yesu, Masihi, atatuakoa toka kwenye hukumu ya kifo (kama vile Kol. 2:14).

▣ **“Bwana Mungu atafuta machozi katika nyuso zote”** Tambua ni Mungu wa agano wa Israeli (kifasihi Adon YHWH) Yeye afutaye machozi (BDB 562, KB 567, *Qal KAULI ILIYO TIMILIFU*, kama vile 43:25; 44:22; Zab. 51:1,9). Pia kumbuka ni “nyuso zote” (BDB 481 na BDB 815)!

Hii mada ya majonzi, majuto (hukumu), na furaha (wokovu) iliyorejeshwa ni kitu kinachojirudia katika Isaya (kama vile 30:19; 35:10; 51:11; 65:19; pia kumbuka matumizi yake katika Agano Jipy, Ufu. 7:17; 21:4).

▣ **“na aibu ya watu wake ataiondoa katika ulimwengu wote”** Hili lawezakuwa na maana mbili.

1. linahusiana na agano jipy katika Ezek. 36:22-38 ambalo linarejesha sura ya Israeli kati ya mataifa
2. linahusiana na “watu wake” kwa watu wote (kama vile Rum. 2:28-29; Rum. 9:6; na 11:26; pia kumbuka Gal.6:16; I Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Aibu ni matokeo ya dhambi. Ondoleo lake ni tendo la msamaha na urejesho. Huu ni mpango wa Kiungu kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu wote (mst. 1)!

▣ **“maana Bwana amenena hayo”** Hapa tena ni kuwepo kwa uhakika wa matukio kwa sababu Mungu amelisema hilo (kama vile 24:3; 30-31; 40:8; 55:10-11).

**25:9 “katika siku hiyo watasema”** Hili linarejerea kwenye siku Mungu atakapopatiliza. Kwa baadhi ya watu itakuwa siku ya hukumu; kwa wengine itakuwa ni siku ya wokovu (kama vile 12:1-4; 26:1; 27:1-2). Angalia mhutasari katika 2:11.

▣ **“huyu ndiye Mungu wetu”** Hili lingalirejerea kwa (1) Mungu wa Israeli (yaani., Agano la Ibrahimu, Mwanzo 12,15,17) au (2) Mungu wa uumbaji ambaye aliahidi ukombozi kwa wanadamu wote aliowaumba kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26,27) katika Mwa. 3:15.

▣ **“ndiye tuliyemingoja”** Hiki KITENZI (BDB 875, KB 1082, *Piel KAULI TIMILIFU*) kinajitokeza mara mbili (kama vile 8:17; 26:8; 33:2; 40:31; 49:23; 51:5; 60:9). Ni kidokezo cha neno “kumtamani,” “kumwamini,” “wakimtarajia kwa

hamu”! mara nyingi linatumika katika Zaburi na Isaya.

▣“**tuliyemngonja atusaidie**” Mara zote katika Agano la Kale KITENZI hiki (BDB 446, KB 448, *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU*) kinamaanisha “kuokoa” (yaani., ukombozi wa mwili, Mwa. 12:12; Kut. 1:17-22; 14:30; Yakobo 5:20), lakini katika muktadha huu maana yake zaidi inaambatana na utumiaji wa Agano Jipywa neno “kuokoa” (yaani., Mt. 1:21; 18:11; I Kor. 1:21; 9:22; I Tim. 1:15; II Tim. 1:9). Hawa watu (Myahudi na Mtu wa mataifa) wataokolewa toka kwenye dhambi na mauti. Angalia Mada Maalum katika 33:2.

▣“**na tushangilie na kufurahia**” Hizi zote ziko katika HALI YA KUSIHI.

1. BDB 162, KB 189, *Qal HALI YA KUSIHI*
2. BDB 970, KB 1333, *Qal HALI YA KUSIHI*

Wokovu wake unaleta urejesho wa shangwe na furaha kwenye uumbaji wake (kama vile 35:1-2,10; 65:18; 66:10).

**25:10-11** Kuna mfuatano wa maneno yaliongezwa kwa ajili ya kusositiza.

1. Kukanyangwa chini, mst. 10, BDB 190, KB 218
  - a. *Niphal KAULI TIMILIFU*
  - b. *Niphal KITENZIJINZA CHA MUUNDO WA MANENO*
2. Atanyosha mikono yake, mst. 11, BDB 831, KB 975
  - a. *Piel KAULI TIMILIFU*
  - b. *Piel KAULI ISIOTIMILIFU*
3. Kama vile aogeleye, mst. 11, BDB 965, KB 1314
  - a. *Qal KAULI YA HALI YA KUENDELEA*
  - b. *Qal KITENZIJINZ CHA MUUNDO WA MANENO*

Moabu atajaribu kuogelea katika shimo la maji (mst. 10, huu ni uonekanaji pekee wa neno [גַּדְעֹן, BDB 199]).

Toleo la LXX na Peshitta halitofautishi hili andiko, lakini lina neno “kama wakanyagavyo majani makavu.” Leo la JPSOA linalisahihisha kwa kupaita jina “Madmena,” karibu na Yerusalem, kama vile 10:31.

**25:10-12** Hili linaonekana kurudi kwenye somo la hukumu juu ya mataifa yaliyoko jirani na hasa juu ya Moabu (toleo la JPSOA linashauri marekebisho kuwa ni “Ashuru”). Moabu ilikwisha hukumiwa kipindi cha nyuma katika Isaya 15-16. Hapa, Moabu (taifa pekee lililotajwa katika sura za 24-27) linaonekana kuwa alama ya wanadamu wote walioasi, wenyewe majivuno juu ya hali zao. Moabu, kijografia ukiwa juu ya miinuko na yenyewe utajiri kwa sababu ya biashara zake, ni uwakilishi wa mafanikio ya mwanadamu mbali na Mungu. Hili linaonekana kuwa usuli wa (1) “mji wa machafuko” katika Isa. 24:10 au (2) “mji usioshambulika” ultajwa katika Isa. 26:5.

**25:11 “Naye Bwana atashusha kiburi chake”** KITENZI (BDB 1050, KB 1631, *Hiphil KAULI TIMILIFU*, kama vile mst. 10) pia kimetumika mara mbili katika 26:5 kumrejerea YHWH kwa ajili ya kuushusha chini “mji” (kama vile 24:10; 25:2-3). Ni KITENZI kinachojirudia katika Isaya kuhusiana na YHWH akihukumu kiburi na majivuno (kama vile 2:9,11,12,17; 5:15 [mara mbili]; 10:33; 13:11; 25:11; 29:4; 40:4; kumbuka II Sam. 22:28; Ayubu 40:11; Zab. 18:27; Mith. 29:23).

Kiburi cha Moabu kilichopitiliza kilitajwa mapema katika 16:6 na uharibifu wake katika 16:14.



<b>NASB, NKJV</b>	“ <b>hila za mikono yake</b> ”
<b>NRSV</b>	“ <b>bidii ya mikono yake</b> ”
<b>TEV</b>	“ <b>mikono yake itazama pasipo na msaada</b> ”
<b>NJB</b>	“ <b>kile mikono yake yaweza kukifanya</b> ”
<b>JB</b>	“ <b>anyoshavyo mikono yake</b> ”
<b>Peshitta</b>	“ <b>uharibifu wa mikono yake</b> ”

Toleo la JPSOA linashauri urekebishaji wa kifungu “kukiwa na ishara ya nguvu zao,” ambacho chawenza kuhusiana na “kuimarisha mashambulizi,” kama vile mst. 12.

Tatizo ni neno "hila," ;ארבותה! (BDB 70), ambalo linapatikana hapa tu katika Agano la Kale, lakini aina ya neno lililoko karibu, "מְאָרָב" (BDB 70) linamaanisha "kuvamia" au "אַרְבָּה" (BDB 70) likimaanisha "kutegesha" au "vamia," lakini hili halistahilishi muktadha.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini tofauti kati ya neno "siku hiyo" katika 25:9 na 24:21?
2. Kwa nini Moabu imebaguliwa katika 25:10-12?

## ISAYA 26

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Wimbo wa Matumaini kwa ya Ulinzi wa Mungu	Wimbo wa Wokovu	Wimbo wa Ushindi	Mungu Atawapa Ushindi watu wake	Wimbo wa Shukrani
26:1-6 (1-6)	26:1-11 (1b-6)	26:1-6 (1-6)	26:1-19 (1-6)	26:1-6 (1-6)
Zaburi ya matukio ya siku za Mwisho				Zaburi
26:7-10 (7-10)		26:7-15 (7-15)		26:7-19 (7-11)
			(10-11)	
26:11-19 (11-19)				
	26:12-19 (12-15)	26:16-19		(12-15)
			(16-18)	(16-19)
				(16-19)
			(19)	
Kuomba Hifadhi kutohana na Hukumu Ijayo	Kipengele cha Nne Matukio ya Siku za Mwisho (26:20-27:1)		Hukumu na Urejesho	Hukumu ya BWANA
26:20-21 (20-21)	26:20-27:1 (20-21)	26:20-21 (20-21)	26:20-21	26:20-27:1 (20-21)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia ukr.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Yapaswa kukumbukwa kwamba Isaya 26 na 27 zinaunda umoja wa kifasihi ambao unaanza katika sura ya 24.
- B. Sura za 24-27 ni umoja wa kifasihi uliowekwa katika hitimisho la mfululizo wa maono ya hukumu dhidi ya mataifa yaliyozunguka yanayopatikana katika Isaya 13-23. Hukumu si neno lamwisho! Mungu wa neema na rehema anao umilele, ni mkamilifu, mpango wa ukombozi wa milele!
- C. Hiki kipengele kizima kinajikita katika miji miwili.
  - 1. miji iliyoundwa na watoto wa Kaini, mwanadamu aliyeanguka, ambao walikuwa wakijaribu kuyatafuta mahitaji yao kwa ukamilifu katika vyanzo vyao wenye (yaani, Mwanzo 10-11).
  - 2. mji wa Sayuni, ambapo Mungu hukaa (yaani, juu ya mabawa ya Kerubi lililo juu ya Sanduku la Agano katika patakatifu pa watakatifu pa hekalu katika Yerusalem) na ambapo watu wake (Myahudi na Mataifa) humjia na kumwabudu (kama vile 2:2-4; 19:18-25; Ebr. 11:10; 12:22; 13:14; Ufu. 21:1-2).
- D. Miji inayowakilisha makundi ya watu/mataifa.

### Miji ya Mwanadamu

1:7,8, aliteketeza miji ya Yuda  
1:21, mji umekuwa wa ukahaba  
6:11, miji ya Yuda imefadhaik  
14:17,21, miji yote imefadhabhika  
14:31 miji ya Filistia  
17:1-3,9, miji ya Shamu imekuwa ukiwa  
19:2, miji ya Misri itapigana  
22:2,9, mji uliyo jaa makelee, Yerusalem iliyoanguka  
23, Tiro inaharibiwa  
24:1-25:5, uharibifu wa miji kiulimwengu  
25:10-12, Moabu na mahali pake  
boma la ngome limeangushwa  
26:5, mji usiokataliwa, bila shaka Moabu  
27:10, mji uliozungushwa ngome umeangushwa  
29:1, "Arieli" (Yerusalem)  
33:2, 19, mji wa shangwe (Yerusalem)  
48:2,mji mtakatifu, lakini katika jina tu

### Mji wa Mungu

1:26, mji wa haki, mji wa uaminifu  
19:18-22, Miji ya Misri itamwabudu Mungu  
19:23-25, Misri na Ashuru zote zitakuwa  
miongoni mwa watu wa Mungu  
25:6-9, karamu juu ya mlima wa Mungu,  
miji unapiga tarumbeta  
(yaani, Yerusalem)  
26:1, mji wenye nguvu , Yerusalem,  
Uliorejeshwa  
45:13, Mji wangu (kama vile 44:23)  
52:1-6, mji mtakatifu  
60:14, mji wa BWANA  
62:12, mji usioachwa  
66:6, mji wa shangwe, kelele zitokazo hekaluni

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:1-6

<sup>1</sup>Siku ile wimbo huu utaimbwu katika nchi ya Yuda;

Sisi tunao mji ulio na nguvu;

Ataamuru wokovu kuwa kuta na maboma.

<sup>2</sup>Wekeni wazi malango yake,

Taifa lenye haki, lishikalo kweli, liingie.

<sup>3</sup> Utamlinda ye ye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu,  
kwa kuwa anakutumaini.

<sup>4</sup> Mtumainini Bwana siku zote Maana Bwana YEHOVA ni mwamba wa milele.

<sup>5</sup> Kwa kuwa amewashusha wakaao juu, Mji ule ulioinuka, aushusha,

Aushusha hata nchi, auleta hata mavumbini.

<sup>6</sup> Mguu utaukanyaga chini,

Naam, miguu yao walio maskini, Na hatua zao walio wahitaji.

**26:1 “Siku ile”** Kifungu kinalejelea juu ya ujio wa Mungu kuutembelea uumbaji wake. Hii inaweza kwa kwa ajili ya Baraka au kwa ajili ya hukumu. Angalia maelezo kamili katika 2:11.

❑“**wimbo**” Kuna nyimbo kadhaa katika mkusanyiko wa kifasihi (yaani, sura ya 24-27).

1. hukumu, 23:15-18

2. hukumu, 24:7-11

kuabudu, 24:14-16

3. shukrani na sifa, 25:1,3,6,9

4. kufurahia, 26:1,19

5. kufurahia, 27:2

Hii aina ya muziki/sifa kuja kwa YHWH katika hukumu au baraka (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-28).

❑“**tunao mji ulio na nguvu**” Mji uliorejelewa katika mst. 1-6, kwa kuuondoa mst. wa 5, ni mji wa Mungu, Yerusalemu iliyorejeshwa, ambayo ni ishara ya urejesho wa Mungu wa dunia yake yote. Angalia herufi D katika maelezo yalijotangulia hapo juu.

❑“**Ataamuru wokovu kuwa kuta na maboma**” Haya maboma zilikuwa kazi za mashariki ambazo zisingeruhusu vifaa vya kutobolea kuta kuzifikia kuta za kutobolea mji. Hiki KIWAKILISHI kinamrejelea YHWH.

Neno “ulinzi” kiuhalisia ni “wokovu” (BDB 446), angalia Mada Maalum katika 33:2. 26:2

❑“**Wekeni wazi malango yake, Taifa lenye haki, lishikalo kweli, liingie**” Kifungu hiki kinarejelea kuingia katika mji mtakatifu na hekaluni (ama vile 60:11,18; 62:10). Hili neno “taifa” (BDB 156) linatumika katika namna ya kuyashushia hadhi Mataifa, lakini hapa kuna maana nytingine ya chanya ya kuyarejelea mataifa ya Yuda. Kumbuka, muktadha, context, context!

❑“**yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu**” Mistari 2-4 inaonekana kuwa mzaha juu ya neno la Kiebrania “uaminifu” au “tumaini.” Angalia Mada Maalum katika 22:23. Mstari huu unassistiza juu ya mwendelezo wa imani kwa

1. ile *Qal* ya KAULI TENDAJI ENDELEVU ya “kutunza” (BDB 1036, KB 1581)

2. WINGI wa “imani” (BDB 53)

Tena, haijulikanai kama ni mtu anayerejelewa ama ni sura ya kitaifa (kama vile NRSV, JB, REB). Kwa kiasi fulani kuna ufanano wa tataizo lililo katika 24:13 (kama vile Isa. 30:15). Wazo hili la kuendelea kukaa katika uaminifu linawenza kuhusiana na dhana ya kumsubi Bwana (kama vile 25:9; 26:8). Katikati ya hukumu watu wa Mungu wa kweli bado wanaendelea kumtumainia

**26:3 “Utamlinda ye ye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu”** Kitambue kipegele cha kimaagano.

1. Akili ya yule aaminiye inaakaa kwa YHWH (BDB 701, KB 759, *Qal* ya KAULI TENDEWA ENDELEVU, lakini inatumika katika maana ya KAULI TENDAJI, kama vile I Nya. 29:18).
2. YHWH humtunza (BDB 665 I, KB 718, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, uhusiano wa kimaagano una washiriki wawili, angalia Mada Maalum katika 1:19).
3. “Amani kamili” ni uwili wa neno *shalom* (BDB 1022, kama vile DSS). Huku kuyaweka maneno katika mfumo wa uwili ni wa kawaida sana katika kipengele hiki cha Isaya.

▣ **“kwa kuwa anakutumaini”** Hili neno “anayekutumaini” (BDB 105, KB 120, *Qal* ya KAULI TENDEWA ENDELEVU) inamaanisha “kusadikt” katika YHWH (kama vile 12:2; 26:4; 36:15; 37:10; 50:10). Tambua kwamba mstari wa mwisho una neno lile lile una KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Hii ni dhana ya kithiolojia iliyo ya muhimu sana ya uhitaji binafsi na Mungu, si utii tu. Yote ni muhimu!

**26:4 “Mtumainini Bwana siku zote”** Kwa KITENZI (BDB 105, KB 120, *Qal* cha KAULI SHURUTISHI), angalia Mada Maalum katika 22:23.

Majina ya Uungu yaliyo katika mistari ya kwanza ya mstari wa 4 ni YHWH; katika mstari wa pili katika TUNGO Yah na YHWH, angalia Mada Maalum katika 1:1.

Hili neno “siku zote” (BDB 723 I), kwanza muundo wa UMOJA na muundo wa WINGI (TUNGO, kama vile 65:18; Zab. 83:18; 92:8). Utungaji huu, kandokando na neno “milele” (BDB 761), unatumika kwa YHWH, unamaanisha uhusiano binafsi ulio nyuma ya maisha haya (kama vile mist. 14,19; Zab. 23:6).

▣ **“ni mwamba wa milele”** Hili neno “mwamba” ni stiari ya tabia ya Mungu ya kutobadilikabadilika (kama vile Zab. 18:1, 2; Isa. 17:10; 30:29; 44:8).

**26:5 “Mji ule ulioinuka”** Kifungu hiki kinaweza kurejelea yale majivuno ya Moabu (kama vile 25:10-12), hasahasa mst. 12. Majivuno na kiburi cha mwanadamu mara nyingi ni matokeo Uungu.

**26:6** Hapa HWH anatenda kwa niaba ya watu wake. Hii dhana ya “kukanyaga” inakiunganisha kifungu hiki na 5:10, ambacho kinaeleza kuwa hukumu ya Mungu juu ya Moabu inayooonekana, katika muktadha huu, kuwa ishara ya wanadamu wote, mtenda dhambi, jamii ya uasi (sawa na matumizi ya Babeli katika katika Ufunuo wa Yohana).

Yatambue maneno tofauti ambayo yanahuksiana na chini.

1. KITENZI, “utaukanyaga” (BB 942, KB 1245, *Qal* ya KAULI ISIO TIMILIFU)
2. NOMINO, “chini” (BDB 919, UMOJA)
3. NOMINO, “chini” (BDB 919, WINGI)
4. NOMINO, “hatua” (BDB 821)

Sura hii ina maneno kadhaa yaliyojirudia rudia, ambayo ni kibainishi cha muktadha mpana.

1. amani, mst. wa 3
2. YHWH, mst.wa 4
3. chini, mst. wa 6

Kumbuka VITENZI vyote vimwejirudia rudia katika sura 24-27.

1. “utaukanyaga,” BDB 615, KB 663, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, 24:42.
2. “chini,” BDB 991, KB 1407, *Qal* ya KAULI TIMILIFU, 24:8
3. “kunywa,” BDB 1059, KB 1667, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU naENDELEVU, 24:9
4. “udanganyifu,” BDB 93, KB 108, *Qal* ya KAULI ENDELEVU na KAULI TIMILIFU (mara mbili), 24:16
5. “kanyagwa,” BDB 190, KB 218, *Niphil* ya KAULI TIMILIFU na KAULI YA KITENZI JINA, 25:10 257
6. “atashusha,” BDB 831, KB 975, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU NA USIO TIMILIFU, 25:11
7. “aogelee,” BDB 965, KB 1314, *Qal* ENDELEVU na MUUNDO WA KITENZI JINA, 25:11
8. “mahali pa kukimbilia,” BDB 105, KB 120, *Qal* ya KAULI TENDEWA YA WAKATI ENDELEVU na *Qal* ya KAULI SHURUTISHI 25:3,4
9. “aushusha,” BDB 1050, KB 1631, *Niphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (mara mbili), 26:5

10. "watauona," BDB 302, KB 301, *Qal ya KAULI TIMILIFU* (mara mbili), 26:11
11. "Umeliongeza," BDB 414, KB 418, *Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU* (mara mbili), 26:15
12. "afanye," BDB 793, KB 889, *Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU* iliyotumika katika maana AMRISHI (mara mbili), 27:5
13. "Amempiga," BDB 645, KB 697, *Hiphil ENDELEVU* na KAULI YA WAKATI TIMILIFU, 27:7

▣ “**miguu yao walio maskini**” Huyu ni YHWH anayekanyaga, lakini mara nyingi huwatumia wajumbe wake (yaani, Ashuru, Babeli). Hapa wanyonge na maskini ambao wamekuwa wakitukanwa, hawa watakuwa wajumbe wake (kama vile 3:14-15).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:7-10**

- <sup>7</sup>Njia yake mwenye haki ni unyofu;  
 Wewe uliye mnyofu wainyosha njia ya mwenye haki.  
<sup>8</sup>Naam, katika njia ya hukumu zako Sisi tumekungoja, Ee Bwana;  
 Shauku ya nafsi zetu inaelekea Jina lako na ukumbusho wako.  
<sup>9</sup>Kwa nafsi yangu nimekutamani wakati wa usiku;  
 Naam, kwa nafsi yangu ndani yangu nitakutafuta mapema;  
 Maana hukumu zako zikiwapo duniani, Watu wakaao duniani hujifunza haki.  
<sup>10</sup>Mtu mbaya ajapofadhiliwa, Hata hivyo hatajifunza haki;  
 Katika nchi ya unyofu atatenda udhalimu,  
 Wala hatauona utukufu wa Bwana.

**6:7“Njia. . . unyofu”** Huu ni mzaha wa dhana ya kuandaa mapitoa kwa ajili ya ujio wa kiuaminifu. Hii ilikuja kutumka kistari kwa ajili ya maandalizi ya kiroho kwaajili ya ujio wa Mungu. Hii ni dha ambayo Yohana Mbatizaji aliitumia kuelezea huduma yake mwenyewe (kama vile 40:3,4; 42:16; 45:13; Mt. 3:3; Marko 1:3; Luka 3:4-6; Yohana 1:25).

Usawa, njia ilisawazishwa inaweza kufikiriwa kama njia ambayo inadokeza maisha ya Uungu na utii wa agano. Mwamini mwaminifu anabainishwa na

1. moyo ulio kwa ajili ya Mungu (uhusianao binafasi, kama vile mst. wa 9)
2. maisha kwa ajili ya Mungu (utii, kama vile mst.wa 8)

Haya lazima yaende kwa pamoja! Hayawezi kutengana (kama vile Luka 6:46).



<b>NASB, NJB</b>	<b>“uliye mnyofu”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“mnyoofu zaidi”</b>
<b>NRSV, JPSOA</b>	<b>“uliye mionganoni mwao”</b>

Hii ndiyo sehemu pekee ndani ya Biblia ambapo sifa hii imetumika kwa minajiri ya Mungu. Wengine waiona sifa hii kama yenye kuhusiana na dhana ya “Mwenye haki” (kama vile 24:16), ambapo tafsri zengine zinalifanya hili kwa Mungu mara chache sana, ambapo wengine wanasema kuwa sifa hii inahusiana na wafuasi wa haki yake (LXX, Peshitta, JB, REB) wanaendenda kwa unyoofu kama walivyomrudia waliporejeshwa Yerusalem (kama vile 42:16).

**26:8 “Njia”** Tambua ni kwa namna gani (kif.mapito, BDB 73) linahusiana na “njia” la mst. wa 7.

1. mst wa 7, mapito sahihi
2. mst. wa 8, mtindo wa maisha

▣ “**tumekungoja**” Hiki KITENZI (BDB 875, KB 1082, *Piel ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kinatafsiriwa na toleo la NASB kwa kuongeza KIELEZI cha Kiingereza “tumekungoja” Tafsiri nyingine za Kiingereza hazina kielezi hiki. Kielezi hiki kinaakisi kutumaini kwa uvumilivu/kumsubiri Mungu katka kati ya mambo magumu (kama vile 8:17; 25:9; 33:2).

## **MADA MAALUM: Maneno ya Ufunuo wa Mungu (Kwa kutumia Kumbumbu la Torati na Zaburi)**

- I. "Maagizo," BDB 349, "sheria, kanuni, au masharti"
  - A. JINSI YA KIUME, נִיר (KB, 346) – Kumb. 4:1,5,6,8,14,40,45; 5:1; 6:1,24; 7:11; 11:32; 16:12; 17:19; 26:17; 27:10; Zaburi 2:7; 50:16; 81:4; 99:7; 105:10,45; 148:6
  - B. JINSI YA KIKE, נִיר (KB, 347) – Kumb. 6:2; 8:11; 10:13; 11:1; 28:15,45; 30:10,16; Ps. 89:31; 119:5,8,12,16,23,26,33,48, 54,64,68,71,80, 83,112,124,135, 145,155,171
- II. "Sheria" BDB 435, KB 1710, "agizo"
  - Kumb. 1:5; 4:44; 17:11,18,19; 27:3,8,26; 28:58,61; 29:21,29; 30:10; 31:9; Zab. 1:2; 19:7; 78:10; 94:12; 105:45; 119:1,18,29,34,44,51,53,55,61,70,72,
- 77,85,92,97,109,113,126,136,142,150,153,163,165,174
- III. "Shuhuda" BDB 730, KB 790, "sheria za ki-Ungu"
  - A. WINGI, עַתָּה – Kumb. 4:45; 6:17,20; Zab. 25:10; 78:56; 93:5; 99:7; 119:22,24,46,59,79,95,119,125,138,146,152,167,168
  - B. עַתִּית or עַתָּה – Zaburi 19:7; 78:5; 81:5; 119:2,14,31,36,88,99,111,129,144,157
- IV. "Maagizo" BDB 824, KB 959, "amri"
  - Zaburi 19:8; 103:18; 111:7;
- 119:4,15,27,40,45,56,63,69,78,87,93,94,100,104,110,128,134,141,159,168,173
- V. "Amri" BDB 846, KB 622
  - Kumb. 4:2,40; 5:29; 6:1,2,17,25; 8:1,2,11; 10:13; 11:13; 15:5; 26:13,17; 30:11,16; Zab. 19:8; 119:6,10,19,21,32,35,47,48, 60,66,73,86,96,98,115,127,131,143,151, 166,176
- VI. "Hukumu/sheria" BDB 1048, KB 651, "maamuzi" au "haki"
  - Kumb. 1:17; 4:1,5,8,14,45; 7:12; 16:18; 30:16; 33:10,21; Zaburi 10:5; 18:22; 19:9; 48:11; 89:30; 97:8; 105:5,7; 119:7,13,20,30,39,43,52,62, 75,84,102,106,120,137, 149,156,160,164; 147:19; 149:9
- VII. "Njia zake" BDB 202, KB 231, maongozo ya YHWH kwa maisha ya watu
  - Kumb. 8:6; 10:12; 11:22,28; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16; 32:4; Zab. 119:3, 5,37,59
- VIII. "Maneno yake"
  - A. BDB 182, KB 211 – Kumb. 4:10,12,36; 9:10; 10:4; 17:19; 18:19; Zab. 119:9,16,17,25,28,42,43,49,57,65,74, 81,89,101,105,107,114,130,139,147, 160,161,169
  - B. BDB 57, KB 67
    - 1. "neno" – Kumb. 33:9; Zab. 119:11,67,103,162,170,172
    - 2. "ahadi" – Zab. 119:38,41,50,58,76,82,116,133,140,148,154
    - 3. "utii" – Zaburi 119:158

Haya yote yanaurejelea ufunuo pekee wa Mungu mwenyewe kwa. Kimsingi haya ni visawe. Angalia Mada Maalum: Uvuvio.

▣ **"Jina lako na ukumbusho wako"** Hili ni nendo la mwamini kusubiri kwa muda binafsi kwa ajili ya Mungu (kama vile mst. wa 9; 25:9). Kifungu "Jina lako" kinawakilisha sifa ya Mungu (yaani, Kut. 3:15; Zab.135:13). Kifungu "ukumbusho wako" kinawakilisha matendo yake makuu yua ukombozi yaliyoeleza katika katika wimbo wa sifa.

**26:9** Mistari miwili ya kwanza ya mst. wa 9 inaimbika kama Zaburi. Kwa kina mwabudu anashauku ya kuwa na YHWH, si kwa kwa mawazo tu, bali yeye, Mwenyewe.

1. mapema, BDB 16, KB 20, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

2. tafuta, BDB 1007, KB 1465, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, Zab. 63:1; 78:34; Hos. 5:15

Hiki ni kipengele chenye nguvu, ni lugha binafsi. Hiki kinanikumbusha Zab. 42:1-2. Tumeumbwa ili tumjue yeye. Hatuwezi kuitafuta amani tofauti na yeye! Nyoyo zetu, ziuumbwu katika sura na mfano wake, mapema kwa ajili yake!

■ Mistari miwili ya pili na mst. wa 10 inazungumzia wale wadharimu ambao hawaelewi kuhusu uvumilivu wa Mungu na manufaa ya wema wake (kama vile Rum. 2:4-5). Sheria ya Mungu (yaani, hukumu) ilimaanisha kuyasaidi amataifa ili yamjue (kama vile mst. 11), lakini kutotii mkwa Israeli kulihitimisha ufunuo. Hata Waisraeli wenyewe walitafuta manufaa ya desturi za nyumba zao (yaani, ahadai kwa Ibrahimu).

Makao ya uaminifu wa nulimwengu ni kujifunza haki (mst. wa 9d), bali wadhalimu hawataweza (mst. wa 10b).

■ “**hukumu**” Angalia Mada Maalum: Toa hukumu, Hukumu, Haki katika Isaya katika 3:1.

**26:10 “ijapokuwa wadhalimu huonyeshwa fadhila”** Mstari huu unaliubainisha kusudi la ufunuo na matendo ya YHWH (yaani, kuwafikia wadhalimu ili kuwababilisha).

1. Aliwaonyesha fadhila (yaani, huruma), BDB 335, KB 334, *Hophal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

2. wanaruhusiwa kuishi “katika nchi ya wenye haki”

3. amewaonyesha ishara zake (yaani, ameounyoosha mkono wake), mst. wa 11

Mwitikio wa wadhalimu ni upi kwa YHWH kujifunua mwenyewe?

1. hawajifunzi haki, mst. wa 10

2. hawatendi haki, mst. wa 10

3. hawautambui utukufu wa Bwana, mst. wa 10

4. hawazioni wivu kwa watu wake, mst. wa 11

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 26:11-19

<sup>11</sup>Bwana, mkono wako umeinuliwa, lakini hawaoni;

lakini watauona wivu wako kwa ajili ya watu wako,  
nao watatahayari; naam, moto utawala adui zako.

<sup>12</sup>Bwana, utatuamuria amani;

maana ni wewe pia uliyetutendea kazi zetu zote.

<sup>13</sup>Ee Bwana, Mungu wetu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki;

lakini kwa msaada wako peke yako tutalitaja jina lako.

<sup>14</sup>Wao wamekufa, hawataishi; wamekwisha kufariki, hawatafufuka;

kwa sababu hiyo umewajilia, na kuwaangamiza, na kuupoteza ukumbusho wao.

<sup>15</sup>Umeliongeza hilo taifa, Bwana, umeliongeza taifa;

wewe umetukuzwa, umeipanua mipaka yote ya nchi hii.

<sup>16</sup>Bwana, katika taabu zao walikwenda kwako;

waliomba maombi mengi wakati adhabu yako ilipokuwa juu yao.

<sup>17</sup>Kama vile mwanamke mwenye mimba anayekaribia wakati wake wa kuzaa,

alivyo na utungu na kulia kwa sababu ya maumivu yake,

ndivyo tulivyokuwa sisi mbele zako, Ee Bwana.

<sup>18</sup>Tumekuwa na mimba, tumekuwa na utungu, tumekuwa kana kwamba tumezaa upepo;

hatukufanya wokovu wo wote duniani, wala hawakuanguka wakaao duniani.

<sup>19</sup>Wafu wako wataishi,

maiti zangu zitafufuka; amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini,

kwa maana umande wako ni kama umande wa mimea, nayo ardhi itawatoa waliokufa.

**26:11 “mkono wako umeinuliwa”** Hii ni nahau ya matendo ya YHWH, ya nyakati zote wakati uliopita na uliopo. Ni dhahiri, lakini maadui wa watu wake hawamwoni wala kumwelewa (kama vile mst. 10; 5:12,25; 8:11; 9:12; 10:4,10; 11:15; 13:2; 14:26-27; 23:11; 25:10; 28:2, n.k.).

▣ **“moto utawala adui zako”** Hii inaweza kuwa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika maana AMRISHI (yaani, “na moto uwalambe maadui zake”).

**26:12** Huu ni ukubalifu wa utukufu waYHWH wenye nguvu. Yeye anatenda badala ya Israeli (kama vile Eze.36:22-38) kwa ajili ya makusudi makuu ya ukombozi!

**26:13 “mabwana wengine”** Inawezekana kwamba kifungu hiki kinairejeleat miungu ya uongo ya 2:8; 27:9, lakini linaweza kuwa dokezo la maadui wa mataifa (Shamu, Ashuru, Babeli) ambayo Israeli iliwakabili.

▣ **“mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki;”** Hiki KITENZI (BDB 127, KB 142, *Qal* cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinaweza kumaanisha

1. kumiliki mke au suria, Mwa.20:3; Kut. 21:3,22; Kumb. 22:22; 24:1
2. kutawala, 26:13; I Ny. 4:22

Mstari huu unaweza kurejelea ibada ya sanamu, hasa ibada ya ustawi. YHWH ndiye “bwana”, “mume” wa kweli pekee (kama vile Hos. 2:14-20).



NASB	“tutalitaja jina lako”
NKJV	“tunatengeneza njia ya kulitaja”
NRSV	“tunalikiri jina lako”
NJB, REB	“tunalisifu jina lako”
LXX	“tunaliitia jina lako”

Hiki KITENZI (BDB 269II, KB 269, Hiphil cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha “kukumbuka” KB anasema kuwa kitenzi hiki kinamaanisha “kukiri katika sifa” (yaani, nyimbo za kumsifu Mungu). Hiki, hivyo, kinadokeza utaratibu wa kuabudu ambapo sifa na matendo ya Mungu wa yanaheshimiwa (kwa hali chanya, yaani, Zab. 71:14-16; na hali hasi, hakuna miungu wengine wanaotajwa ndani ya sifa, Kut. 23:13).

Tambua kuwa ni YHWH (yaani, “kupitia wewe”) ambaye watu wake wanao uwezo wa kumwabudu.

1. ukombozi wa mataifa (kama vile mst. wa 15, hekaluni)
2. ukombozi binafsi (kama vile mst. wa 16, kuwa na shauku ya kwenda mahali pale)

**26:14 “Wao wamekuwa, hawataishi; wamekwisha kufariki, hawatafufuka”** Kifungu hiki kinaonekana kuunganishwa na mst. wa 13, “mabwana wengine,” ambapo kifungu hiki kinawarejelea wafalme wa kigeni ambao hawataifadhaisha tena Israeli. Mstari huu haumaanishi kufundisha thiolojia inayohusu maisha baada ya kifo, hasa dhiki kuu ya wadhalimu. Kuna vifungu vingine vingi sana katika Biblia ambavyo vinafundisha juu ya ufufuo wa jumla (kama vile Dan. 12:2; Mt. 25:46; Yohana 5:28-29; Matendo 24:15). Mstari huu unasema kwamba hao wafalme, wanao ahukumiwa na kufa, hawataishi tena kibinafsi au kiishara, kwa wakati mwingine, kwa ajili ya kuwapa taabu watu wa Mungu.



NASB	“roho zilizokwisha ondoka”
NRSV, JPSOA	“vivuli”
TEV, JB	“roho”
NJB	“vivuli”

Neno la Kiebrania (BDB 952 I) linaonekana kuhusianishwa na wale waliodunishwa, wafu wasio na nguvu (kama vile Ayubu 26:5; Mit. 2:18; Isa. 14:9; katika 26:19); neno hili linatumika kwa wale wenye haki ambao watafufuliwa).

Mzizi kama huu (BDB 952 II) ulikuwa moja ya maneno yaliyotumika kuyafafanua majitu. Angalia Mada Maalum katika 14:9. Inawezekana kwamba Warefai ilikuija kuwa stiari iliyosanifishwa kwa mashujaa wakuu na kiishara kwa wafalme wa mataifa yenze nguvu.

**26:15** Hii ilikuwa sababu ya Mungu ya kimaagano kuuelekea vizazi vya Ibrahimu. Hii taswira inayofanana mara nyingi ilipanuliwa hadi kuzungumzia matikio ya siku za mwisho, ambapo mataifa yote yatakuja kumwabudu YHWH kuko Yerusalemu.

**26:16 “waliomba maombi mengi”** Waaminifu wa Mungu walikuwa wakiteseka chini ya hukumu ya Mungu juu ya watu wake kwa ujumla. Hawa walimtzama Mungu katika hali ya uhaba wa amani na walilindwa kwa maombi katikati ya mkono wa Mungu wenze nguvu.

Hili linaweza kuwa neno la kimzaha la kithiolojia.

1. waliomba kwa sauti ya chini (BDB 538 #3)
2. waliomba kwa sauti ya chini kama sehemu ya ibada kwa miungu ya Israeli (BDB 538 #1,2, kama vile 3:3,20)

Kumbuka , muktadha, muktadha, mukadha ndiyo utambulishao maana!

**26:17 “kama vile mwanamke mwenye mimba”** Mara nyingi katika Biblia, neno kuzaa linatumika kama stiari kwa ajili ya maumivu ya ghafla ya hukumu ya Mungu inayokuja. Baadhi wanaitafasiri mistari ya 17-18 kama uzao wa kimasihi (yaani., stiari ya maumivu ya uzao wa enzi mpya, kama vile Marko 13:8), lakini katika muktadha inaonekana kurejerea hukumu.

**26:18 “tumekuwa kana kwamba tumezaa upepo.**

**hatukufanya wokovu wowote duniani,**

**wala hawakuanguka wakao duniani**” Hapa hii ni rejea ya mamlaka ya wito wa Israeli kuwa ukuhani wa kifalme (kama vile Kut. 19:4-6). Alimaanisha kuwa nuru kwa mataifa (kama vile Isa.42:6; 49:6; 51:4). Hata hivyo, kwa sababu hakuzishika sheria za Mungu, watu wa dunia wakamtazamia YHWH katika hukumu. Hili halikuwa kusudi la Mungu (kama vile mst. 15); kwa hiyo, kusudi la Mungu (kama vile 25:1) kwa ajili ya Israeli na dunia lilizuiliwa.

Neno “upepo” (BDB 924) lina vidokezo mbalimbali katika Isaya.

1. Pumzi, 11:4; 25:4; 27:8; 30:28,33; 33:11; 59:19
2. Upepo, 7:2; 11:15; 17:13; 26:18; 32:2; 41:16,29; 57:13; 64:6
3. Roho
  - a. Roho wa Mungu, 11:2 (mara 4); 30:1; 32:15; 34:16; 40:13; 42:1; 44:3; 48:16; 59:21; 61:1; 63:10, 11,14
  - b. roho ya binadamu, 4:4; 19:3,14; 26:9; 28:6; 29:10,24; 31:3; 37:7; 38:16; 42:5; 54:6; 57:15(mara mbili), 16; 61:3; 65:14; 66:2

Hata hivyo katika vitabu vya Hekima neno lenyewe linamaanisha kutokuwa na maana, tupu/pasipo kitu (yaani., Mhu. 1:14,17;2:11,17,26; 4:4,6,16; 5:16; 6:9). Nafikiri matumizi ya Isaya katika 26:18 na 41:29 kwa uzuri kabisa yanafaa dokezo hili la pili. Uzao wa Ibrahimu haukuweza kuyaleta mataifa kwa YHWH kwa sababu ya

1. Anguko lao binafsi
2. anguko la mataifa

lakini YHWH anaweza (kama vile mst. 12)!

Neno “kuzaliwa” (BDB 656, KB 709, *Qal KAULI ISIOTIMILIFU*) katika mst. 18d kwa maana iliyo wazi linamaanisha “kushuka” au “kuanguka,” lakini linatumika kiistari kwa ajili ya kuzaa. Kwa asili ya Kiarabu neno linamaanisha kuzaa; kimsingi linatumika kwa wanyama (kama vile toleo la NIV).

**26:19 “wafu wako wataishi;**

**maiti zangu zitafufuka**” Aya ya 19 inatofautiana na mst. 14. Ndiyo maana mst. 14 hauwezi kuwa chanzo cha thiolojia. Aya ya 19 ina ufanano mwingu na 25:8. Swali tuliloliona katika 26:3

linashughulika na rejeo la utambulisho wa taifa au wa mtu binafsi. Neno “zako” katika mst. 19b kwa maana iliyo wazi ni “zangu” katika Kiebrania. Hapa tena linashiriki juu ya mtu binafsi dhidi ya watu wa taifa fulani. Huu ufufuko wa kitaifa wa Israeli unaendana na wa Ezekiel 37.

Kuna KAULI SHURUTISHI mbili katika aya hizi ambazo zinalezea kile wafu (“wewe unayelala mavumbini”) wanapaswa kukifanya.

1. inuka, BDB 884, KB 1098, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
2. Piga kelele, BDB 943, KB 1247, *Piel KAULI SHURUTISHI*

Ufufuko ni dhana iliyoonekana kuwa ya kawaida huko Mashariki Karibu ya Kale.

1. Ayubu (Edomu katika kipindi cha 2000 K.K), 14:13-15; 19:25-27
2. Utiaji maiti mumiani huko Misri (ulioanza mwaka  $3000 \pm$  K.K., na kukamilishwa na mtawala wa ishirini na moja
3. Lakini sio huko Mesopotamia

Ikiwa wanadamu waliumbwu kwa ajili ya ushirika na Mungu lakini dhambi zikasababisha mauti, hivyo kinyume kwa ajili ya uaminifu kinaonekana kuwa na mantiki. Walimu (yaani., Mafarisayo) waliyamini katika ufufuko (kama vile Mdo. 23:6; Ebr. 6:1-2). Yesu aliamini katika ufufuo (kama vile Mt. 22:23-33; Luka 14:14; Yn 11:24-25). Dhana ya mbinguni ni suala la ushirika. Gehenna ni sehemu ya utengano wa milele kwa wale walioikataa imani na ushirika! Taswira ya Biblia kwa ajili ya mambo yajayo imerejeshwa pale Edeni (kama vile Ufunuo 21-22).



NASB	“kama umande wa machweo”
NKJV	“kama umande wa mimea”
NRSV, NJB	“umande ung’ao”
TEV	“umande wenyewe kumelemeta”
REB	“umande wenyewe kung’aa”
Peshitta	“umande angazi”
JPSOA	“umande uanzao kudondoka”

Kwa maana iliyo wazi hii ni “kwa ajili ya umande angazi.” Neno “mwanga” (BDB 21) lina vidokezo viwili.

1. Mwanga wa uhai dhidi ya giza la mauti (WINGI, BDB 21 I, yumkini Esta 8:16)
2. Mmea (BDB 21 II, Mwa. 1:11,12)

Kuna vipindi viwili vya majira ya mvua huko Palestina. Kati ya nyakati hizi mbili mazao yaliweza kustahimili na kukua kwa kutegemea umande. Kwa hiyo, vyote “umande” na “mwanga” ni alama ya uhai na ukujai!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 26:20-21

<sup>20</sup> Njoni, watu wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako,  
ukafunge mlango nyuma yako ujifiche kitambo kidogo,  
mpaka ghadhabu hii itakapopita.  
<sup>21</sup> Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali pake,  
ili kuwaadhibu wakao duniani, kwa sababu ya uovu wao;  
ardhi nayo itafunua damu yake,  
wala haitawafunika tena watu wake waliouawa.

**26:20** Watu wa Mungu wametenda dhambi. Wana hatia. Hukumu inawajilia juu yao, lakini itapita. Kuna KAULI SHURUTISHI nne katika aya hii ambazo zinalezea wale waaminifu na namna watakavyo enenda wakati wa kipindi cha hukumu ya Mungu.

1. njoni, BDB 229, KB 246, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. ingia, BDB 97, KB 112, *Qal KAULI SHURUTISHI*
3. ukafunge, BDB 688, KB 742, *Qal KAULI SHURUTISHI*
4. ujifiche, BDB 285, KB 285, *Qal KAULI SHURUTISHI*

Zote zipo katika HALI YA UMOJA JINSI YA KIUME, lakini kwa pamoja zinarejerea kwenye uaminifu.

Hili ni dokezo kwenye kuilewaa Pasaka ya Wayahudi ya Kutoka 12.

1. fungeni mlango
2. KITENZI, “Pasaka” (BDB 716) hakifanani na KITENZI kilichotumika katika Kutoka 12 (BDB 820), lakini wazo ni lile lile

Walio waaminifu wataokolewa toka kwenye hukumu ya Mungu.

**26:21 “Bwana anakuja kutoka mahali pake”** Kifungu hiki kimetumika mahali hapa tu na Mika 1:3.  
kinaonekana kurejerea

1. Mbinguni (yaani., kwenye kiti cha Enzi cha Mungu)
2. Hekaluni (yaani., mahali pa Mungu kuweka miguu)

▣“duniani” Sura ya 24-27 inazungumzia juu ya hukumu ya ulimwengu wote!

## ISAYA 27

<b>MGAWANYO WA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ukombozi wa Israeli  27:1 (1)	Kuwaokoa Wakimbizi na Hukumu ijayo  (26:20-27:1)	Sehemu ya nne ya Nyakati za mwisho  (26:20-27:1)	Hukumu na urejesho  (26:20-27:13) 26:20-27:1	Hukumu ya BWANA  (26:20-27:1)
Urejesho wa Israeli  27:2-11 (2-11)	Shairi la nne la Ukombozi siku za mwisho  27:2-11 (2-5)	27:2-11 (2-5)	27:2-5	Shamba la Mizabibu la YHWH  27:2-5 (2-3) (4) (5)
			27:6	Msamaha na Adhabu  27:6-11 (6-11)
		27:7-9		
	Kuhusiana miungu Kuangamizwa na tarumbeta  27:12-13 (12) (13)	27:10-11		Israeli wanarudi  27:12-13 (12-13)
			27:12	
			27:13	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukur. wa xvi wa kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasi.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyouvuvia, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kia cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

- A. Huu ni mwisho wa Sura unaoanza kusimuliwa kuanzia Sura ya 24.
- B. Mistari miwili ya mwisho ni sitiari inayofaa kwa hitimisho la hukumu ya mwisho, inayoanza na uzao wa Ibrahim (kama vile Yer. 25:29; Amosi 3:2; 1 Pet. 4:17), Lakini inaenda zaidi kwa wanadamu wote.
- C. Aya ya mwisho, kama mst. 5, inaeleza zaidi matumaini kwa mataifa ya ulimwengu (kama vile 2:2-4; 19:18-23; 25:2-3).
- D. Hii ni Sura ya shairi la ajabu, lakini ni zuri kwa sababu ya utata na kuchanganya. Kumbuka, kutafuta maana ya ubeti, sio maelezo ya neno la shairi au dokezo la elimu ya visasili.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 27:1

<sup>1</sup> Katika siku hiyo Bwana, kwa upanga wake ulio mkali, ulio mkubwa, ulio na nguvu, atamwadhibu lewiathani, nyoka yule mwelesi,  
na lewiathani, nyoka yule mwenye kuzonga-zonga;  
naye atamwua yule joka aliye baharini.

27:1 “katika siku hiyo” Tazama muhtasari katika 2:11.

■“Lewiathani nyoka yule mwelesi” Lewiathani (BDB 531) inaonekana kuwa visasili Ugaritiki mnyama wa baharini (yaani., Ayubu 41:19-21) anatajwa katika Ayubu 3:8; Zab. 104:26; Amosi 9:3. Hata hivyo ,wakati mwingine anatumika kama Ishara ya taifa ovu (kama vile zab. 74:13-14,inawezekana kuwa ni Misri). Anafanana na mto uliopindapinda na kukatiza katika nchi. Wakati mwingine neno hili lina muunganiko hasa na “Rahabu,” ambayo ni njia ya kurejelea Misri (kama vile Zab. 87:4; 89:9-10; na Isa. 30:7). Kwangu inaonekana kwamba, katika muktadha, tunazungumzia mto kama alama ya taifa adui, Misri au Ashuru (kama vile . mst. 12). Sababu ya neno hili kutumika kama alama kwa urahisi ni kwamba limetumika wakati uliopita kwa baadhi ya fasihi za kitheolojia za kanaani (kama vile Zab. 74:12-17; tazama G. Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*,krs. 239-240).

Kuna mfanano kati ya

1. Nyoka yule mwelesi (BDB 638 I) au mnyama wa kutisha wa baharini (NASB tanbihi)
2. Nyoka mwenye kuzonga-zonga
3. Joka aliye baharini

Taswira hii inapatikana kwenye (1) mashairi ya Ugaritiki na (2) Isa. 51:9, anatumia “Rahabu,”ambaye anafahamika pia kwa neno kama “joka” (BDB 1072).

muunganiko wa wazi na wa pekee kati ya Aya hii na muktadha ni mstr ya . 11-12.

1. YHWH kama Muumbaji, mst. 11
2. Mito ya Frati na mto wa Misri katika mst. 12
3. Mwisho wa nyakati ni kama mwanzo wa nyakati (yaani.,Mwa 1-2; Ufu 21-22)

Ni dhahili mkusanyiko wa maandishi ya Isaya ulifanywa kwa miaka mingi na yalikusanywa katika msingi wa mchezo wa maneno au dhamira, sio historia.

■“joka” neno hili (BDB 1072) lina maana

1. nyoka, Kut. 7:9,10,12; Kumb. 32:33; Zab. 91:13
2. joka, Neh. 2:13; Yer. 51:34
3. mnyama wa baharini/mto, Mwa. 1:21; Ayub 7:12; Zab. 74:13; 148:7. Ina mfanano na Lewiathani (kama vile Zab 74:13-14). Imetumika kama sitiari kwa ajili ya Misri katika Isa. 27:1; 51:9,10; Ezek. 29:3; 32:2.

Mito miwili mikubwa ya mashariki ya kale ya karibu ilikuwa ni kitovu cha ustaarabu wa jamii (yaani., mto Nile na mto Hedekeli/Frati).

Tanin (BDB 1072) ni mfanano na

1. Lewiathani, Zab. 74:13-14; Isa. 27:1

2. Rahabu, Isa. 51:9
3. Bashani, Zab. 68:22; Amosi 9:3 (kama vile. NIDOTTE, juzu. 3, ukr. 87)

### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:2-6**

<sup>2</sup>Katika siku hiyo;  
**Shamba la mizabibu la mvinyo, liimbieni.**

<sup>3</sup>Mimi, Bwana, nalilinda,  
 Nitalitia maji kila dakika,  
 Asije mtu akaliharibu;  
**Usiku na mchana nitalilinda.**

<sup>4</sup>Hasira sinayo ndani yangu;  
**Kama mibigili na miiba ingekuwa mbele zangu, Ningepanga vita juu yake,**  
**Ningeiteketeza yote pamoja.**

<sup>5</sup>Au azishike nguvu zangu,  
 Afanye amani nami;  
**Naam, afanye amani nami.**

<sup>6</sup>Siku zijazo Yakobo atatia mizizi;  
**Israeli atatoa maua na kuchipuka;**  
**Nao watajaza uso wa ulimwengu matunda.**

#### **27:2**

<b>NASB</b>	“shamba la mizabibu la mvinyo”
<b>NKJV</b>	“shamba la mizabibu mwekundu”
<b>NRSV, TEV</b>	“shamba zuri la mizabibu”
<b>NJB, REB</b>	“shamba bora la mizabibu”
<b>LXX</b>	“shamba zuri la mizabibu”
<b>JPSOA</b>	“shamba la kupendeza la mizabibu”

Neno la kiebrania kwa ajili ya “liimbieni” ni לִימְבֵּן (BDB 326), ambalo katika Biblia Hebraica Stuttgartensia, lakini toleo la Andiko la Kimasoreti na toleo la DSS yana נָסַע sio תְּ. Neno la kiebrania kwa ajili ya “mvinyo” ni מִנְיָה (BDB 330). Alama ya silabi ni sawa kwa ajili ya maneno yote. Toleo la UBS Andiko la kiebrania linatupatia “liimbieni” “C” alama (mashaka makubwa).

Shamba la mizabibu ni alama ya taifa la Israeli (kama vile . 5:1-7; Peshitta), lakini hapa, kwa sababu ya asili ya ulimwengu kwenye Sura ya 24-27, huwenda ni kwa ulimwengu mzima (kama vile 26:21; toleo la JPSOA tanbihi).

▣“imba” Hii ni *Piel KAULI SHURUTISHI* (BDB 777, KB 854). Kuna “nyimbo” nyingi zimetajwa kwenye sehemu hii kwa uwazi . Tazama muhtasari katika 26:1b.

**27:3** YHWH ana uhusiano maalumu, uhusiano wa kiagano na uzao wa Ibrahimu. Ni wa pekee kwa watu wake. Hata hivyo, mst. 6 inaonyesha ana mpango na ulimwengu kwa ajili ya watu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5)

**27:4-5** Kuna HALI YA KUSHIHI na KITENZI AMRISHI vingi kwenye Aya hizi.

1. Nitasimama juu yao, BDB 832, KB 979, *Qal HALI YA KUSHIHI* (KITENZI kimepatikana hapa pekee kwenyw Agano la kale)
2. Nitawateketeza, BDB 428, KB 429, *Hiphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya HALI YA KUSHIHI
3. Acha atumaini katika ulinzi wangu, BDB 304, KB 302, *Hiphil KITENZI AMRISHI*
4. Acha afanye amani na mimi, BDB 793, KB 889, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* imetumika kwenye maana ya KITENZI AMRISHI,mara mbili.

Aya ya 3 inaelezea utunzaji na ulinzi wa YHWH kwa ajiri ya uzao wa Ibrahimu; Aya ya 4 inaelezea mapenzi yake ya kuwalinda na kuwaangamiza maadui wake; Aya ya 5 inatambulisha kumtumaini katika utunzaji na ulinzi; Aya ya 6 ni matokeo ya ya Baraka ambazo siku moja zitajazwa Duniani ( makusudi makuu ya Mungu katika Mwa 1).

**27:4**

NASB	“hasira”
NKJV	“ghadhabu”
TEV, JB	“hasira”
NJB, LXX	“ngome”
REB	“mvinyo”
Peshitta	“epuka”

Tambua uchaguzi uliopo.

1. הַשִּׁיר (BDB 404), “hasira,” ni la kawaida katika Isaya
2. המוֹר (BDB 327), “mibigli,” imetumika kwa uwazi na mara nyingi , kama vile. 2:15; 22:10,11; 25:12; 26:1
3. תְּמִימָה (BDB 330), “mvinyo,” ni mara chache, pekee kwenye 27:2 na Kumb. 32:14

Toleo la Andiko la mpango wa kiebrania UBS linatupatia neno “hasira” a “B” alama (baadhi ya mashaka ).

**27:5 “Au azishike nguvu zangu”** Hii inaonyesha kwamba mwanadamu (hata kwa maadui wa Mungu, kama vile. mst. 4) kuitikia kwake ni sehemu ya mpango wa Mungu (kama vile . Isa. 1:16-17,18-20). Kuna ukweli unaokinzana katika Biblia kati ya utawala wa Mungu katika historia na mapenzi ya Mungu ambayo kwayo wanadamu wanayapokea kwa imani. Tazama Mada Maalumu katika 1:3. Aya ya 5 ni msamaha unaotolewa na Mungu na Wokovu kwa wanadamu watakao mwamini yeye (kama vile. 2:2-4; 42:6; 45:22; 49:6).

▣ **“Afanye amani nami”** Tungo hii iko mara mbili, ambayo inaelezea sifa ya sehemu hii ya Isaya. Tazama muhtasari katika 26:6.

Amani ni kipengele cha muhimu sana cha mahusiano ya Imani na Mungu (kama vile. 26:12; 32:17; 52:7; 54:10; 55:12; 57:2,19; 60:17; 66:12; Fil. 4:7,9) na Masihi wake (kama vile. 9:6,7; 53:5; Rum. 5:1; Yoh. 14:27; 16:33; 20:19,21,26). Pia inahusiana na Amani kati Mataifa (kama vile. 2:4; 39:8), lakini hakuna amani kwa ajiri ya waovu (kama vile. 48:22; 57:1; 59:18).

Hapa inadokeza mkataba wa amani, unaotolewa kwanza na YHWH, lakini ni lazima ukubaliwe na waishi kwa imani.

**27:6 “Israeli atatoa maua na kuchipuka;**

**Nao watajaza uso wa ulimwengu matunda** Hapa tena ni taswira ya Hekalu la Sayuni ambalo litainuliwa juu ya milima yote na baadhi ya vizuizi vya Sura ya nchi vitaangamizwa na kwamba watu wote duniani wataenda Yerusalem kumwabudu Mungu (kama vile. 2:2-4; 24:23; 25:6,7; 27:13). Kuamini huku ni tofauti hasa na 26:18. Labda sehemu ya matunda ni “atakaye inuka” ya 26:19.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 27:7-11**

<sup>7</sup>Je! Amempiga kama hilo pigo la hao waliompiga,

au ameuawa kama walivyouawa wao waliouawa na yeye?

<sup>8</sup>Umemwadhibu kwa kiasi, ulipomfukuza;

ukampepete kwa upepo mkali katika siku ya upepo wa mashariki.

<sup>9</sup>Basi, uovu wa Yakobo utatakaswa hivyo,

na hayo ndio matunda yote ya kumwondolea dhambi yake;

afanyapo mawe yote ya madhabahu kuwa kama mawe ya chokaa yaliyopondwa,

hata maashera na sanamu za jua havitasimama tena.

<sup>10</sup>Kwa maana mji ulio na boma umekuwa peke yake,

makao yaliyoachwa na ukiwa kama jangwa;  
 huko ndiko atakakolisha ndama,  
 na huko ndiko atakakolala, na kuyala matawi yake.  
<sup>11</sup>Matawi yake yatakapokauka yatavunjwa;  
 wanawake watakuja na kuyachoma moto;  
 kwa maana hawa si watu wenye akili;  
 kwa sababu hiyo ye ye aliyewaumba hatawahurumia,  
 ye ye aliyewafanya hatawasamehe.

**27:7** Aya hii ni ngumu sana. Inaelezea kwamba hukumu ya Mungu inaenda kwa Mataifa yale ambayo Mungu aliyatumia kuwahukumia watu wake mwenyewe. (Kama vile. 47:6).

Kurudiwa kwa maneno na Tungo ni tabia ilio wazi kwenye Sura hii (tazama 26:6). NOMINO hapa, מבה (BDB 646, JINSI YA KIKE, mara kwa mara limetumika kwa YHWH kuleta hukumu kwa watu wake, kama vile. Law. 26:21; Kumb. 28:61; Yer. 30:12), “kupiga,” au “kuuawa” inafuatiwa na KITENZI kinachojirudia kinachosimulia, נכה (BDB 645, KB 697, *Hiphil KAULI ENDELEVU* na *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*). Wale wote ambao YHWH aliwatumia kuwaadhibu watu wake wataadhibiwa kwa ukali zaidi ya vile walivyo adhibiwa watu wa Mungu (NET Bible).

**27:8 “hao”** neno “hao” kwenye mst. 8 inarejelea taifa la Israeli lilitengwa (yaani, “muktadha,” BDB 936, KB 1224, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, kama vile. Hos. 2:2) na Mungu kwasababu alivunja Agano (kama vile. 50:1). Hivyo basi, Mungu aliwaleta watawala wageni ili kuwahukumu watu wake (kama vile. Kumb. 28:49-57; yaani., Ashuru, Isa. 10:5, na Babeli, Isaiah 14). Hata hivyo, Mungu atawahukumu na wao pia (kama vile. mst. 7; 47:6; 49:25).

▣	
NASB	“kwa kuwafukuza”
NKJV	“katika kupanga”
NRSV	“kwa kuwafukuza”
NJB	“kwa kuwaondosha”
LXX	“fukuza”
Peshitta	“kwa kipimo alichopimia”

Andiko la Kimasoreti lina בטהר (linapatikana hapa pekee), ambalo linafhamika kama

1. בטהר, “kipimo kwa kipimo” (BDB 684, KB 738, *Pipel TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*, Targums na Vulgate)

2. בטהר, kwa kumfukuza atoke (tazama kifungu kinachofatia)

Toleo la UBS Hebrew Text Project linatupatia namba 1 a “B” alama (baadhi ya shaka), inawezekana kwasababu maneno haya mawili na Tungo ni jambo la kawaida kwenye fasihi hii.

Neno lingine la kiebrania ni בטליה (BDB 1018, KB 1511, *Piel TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*, ambalo lina maana ya “kuwapeleka mbali utumwani.” Tafsiri nyigi hapo juu zimeacha KITENZI cha kwanza na kutafsiri KITENZI cha pili.

▣ “ulipomfukuza mbali” KITENZI cha kiebrani (BDB 212, KB 237, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) Inadokeza kusafisha kwa kuondoa uchafu (kusafisha Shaba, kama vile Mit. 25:4).

▣ “upepo wa mashariki” mara kwa mara hii inarejelea nguvu ya Mesopotamia (yaani, 46:11; Ezek. 17:10; Hos. 13:15) kwamba itavamia Palestina, lakini haiwezi kuwa na maana hapa kwa sababu ya mst wa . 7. Hivyo ni lazima iwe sitiari ya hukumu ya kiroho (kama vile. Kut. 10:13; Zab. 48:7; Yer. 18:17). Wakati mwengine upepo wa mashariki ni Baraka za matendo ya kiroho (kama vile. Kut. 14:21; 15:10; Hes. 11:31; tazama NIDOTTE, juzu. 3, krs. 871-873).

**27:9** Hapa tena wengi wanadai kwamba hii inaonyesha kwamba Israeli/Yuda zilisamehewa kwa sababu ya walikuwa na ufahamu wa hukumu kutoka kwa Mungu. Lakini subiri,lazima pia waharibu mabaki yote ya miungu ya uzao waliyo kuwa nayo (mistari ya 3, 4). Hata hivyo , hii ni lazima imeletwa na dhana ya mstari ya “mateso ya mtumishi” yanayopatikana katika Isa. 52:13-53:12. Tena, na sio /au mahali, lakini njia mbili tofauti za kuangalia matendo ya Mungu kwenye historia ya mwanadamu. Masihi ana maanisha wokovu, lakini watu ni lazima wampokee kwa imani na kumtumainia.

▣“**mawe ya madhabahu . .maashera**” Hizi ni ishara za miungu ya kiume na kike ya uzazi ya Wakanaani ambayo waliiharibu ili kumwabudu YHWH. Wataharibiwa! Tazama Mada Maalum katika 17:8.

▣“**mawe ya chokaa**” neno hili (BDB 162) inajitokeza hapa pekee kwenye Agano la kale. Inadokeza jiwe laini ambalo linaweza kusagwa kwa urahisi.

Neno linalofanana na hili linapatikana kwenye Dan. 5:5, lakini kwenye Lugha za kialama, na inarejelea kwenye mchanganyiko wa chokaa,mchanga na maji katika ukuta wa chumba cha kalamu kwenye jumba la kifalme la Belshaza,mwana wa Nebukadnezza .

**27:10 “Kwa maana mji ulio na boma umekuwa peke yake”** Huu ni mchezo wa neno “mji”. Tazama muhtasari katika 24:10 na jedwari katika Sura 26, utambulisho, D.

**27:11** Taswira ya malisho ya jangwa yanawakilisha uhamishoni, Uovu wa watu wa Mungu unaendelea kutoka mst 10 hadi mst. 11, mistari ya 1-2.

Uasi huu wa watu wa Agano unaelezea sifa ya:

1. Hawakuwa watu wenye utambuzi, kama vile. Hos. 4:14
2. Muumba wao (kama vile. 43:1,7; 44:2,21,24; Kumb. 32:18) hatawahurumia
3. Muumbaji wao hatawasamehe

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 27:12-13**

<sup>12</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo, Bwana atayapiga-piga matunda yake toka gharika ya Mto hata kijito cha Misri, nanyi mtakusanywa mmoja mmoja, enyi wana wa Israeli. <sup>13</sup>Tena itakuwa katika siku hiyo, tarumbeta kubwa itapigwa, nao waliokuwa karibu na kuangamia katika nchi ya Ashuru watakuja; na hao waliotupwa katika nchi ya Misri; nao watamsujudu Bwana katika mlima mtakatifu huko Yerusalemu

**27:12-13** Huu unaonekana ni muundo unanaohitimisha fashi ya maelezo. Aya ya 12 inaongelea Mungu anahusika na (yaani , “kupura,” BDB 286, KB 285, Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ambayo inadokeza mavuno ya nyakati za mwisho na kuwatenganisha wenye imani na wasio na imani,( kama vile Mt. 13:36-43; 24:31; 25:32) watu wake, anatumia taswira ya taifa. Inarejelea katika ukomo wa nchi wa nchi ya ahadi unaopatikana mara kwa mara kwenye Agano la kale (kama vile Kut. 15:18; 1 Fal.8:65; Ezek. 47:15-19). Aya 13 ni upeo wa ulimwengu; inahusika na yale mataifa yasiyoaminibali na watu wa Mungu ambaao pia wamekaribishwa kumpokea Mungu kwa Imani (yaani, 2:2-4; 19:18-25).

Aya hizi mbili zinaakisi Kumb. 30:1-10 katika taswira ya nyakati za mwisho (muhtasari Hos. 11:8-11).

**27:12 “toka gharika ya mto”** Nenohili (BDB 987) lina maana mbili.

1. Gharika ya mto, BDB 987 I, kama vile. Zab. 69:2,15
  2. Kukusanya nafaka, BDB 987 II,kama vile. 17:5; Mwa. 41:5,6,7,22,23,24,26,27; Ruth 2:2; Ayu 24:24
- Sura hii inatumia maana zote. Namba 1 dokezo hili linafaa kwenye mst wa . 1, lakini Namba 2 KITENZI kinafaa mara moja (kupura) na sitiari kwa ajiri ya hukumu (yaani,mavuno).

▣“**kijito cha Misri**” Hii inarejelea wadi El’arish, ambaao ni mpaka wa kusini mwa nchi ya Ahadi.

**27:13 “tena itakuwa katika siku hiyo tarumbeta kubwa itapigwa”** Hii ni kujirudirudia kwa dhana ya Nyakati za Mwisho ikitumia sitiari ya kuabudu au kijeshi ya tarumbeta kupigwa (aina mbili).

1. kuabudu, Kut. 19:16,19; Law. 25:9; Hes. 10:2,8,10; 1 Nya. 15:24
2. Jeshi, Hes. 10:9; Yoshua 6; Waamuzi. 3:27; 6:34; 7; 1 Sam. 13:3; 2 Sam. 2:28
3. Nyakati za Mwisho, inawezekana hapa katika kitabu cha Zek. 9:14; Mt. 24:31; 1 Nya. 15:52; 1 The. 4:16

## MADA MAALUM: PEMBE ZITUMIKAZO NA ISRAELI

Kuna maneno manne katika Kiebrania yahusianayo na pembe/tarumbeta.

1. “pembe ya mwana kondoo” (BDB 901) – ikigeuzwa kuwa chombo cha sauti, kama vile Yosh. 6:5. Neno hilihili linatumika kwa ajili ya mwanakondoo aliyenaswa na pembe zake ambaye Ibrahimu alimfanya mbadala wa Isaka katika Mwanzo 22:13.
2. “tarumbeta” (BDB 1051) – kutoka katika neno la kiashuru ikimaanisha kondoo wa porini (ibex). Hii ni pembe ambayo ilitumika katika Kutoka 19:16,19 katika Mlima Sinai/Horeb; #1 na #2 zina usambamba na Yosh. 6:5. Ilitumika kuwasiliana wakati wa ibada na wakati wa kupigana (yaani Yeriko ilikuwa vyote, kama vile Yosh. 6:4).
3. “pembe ya mwana kondoo” (BDB 385) – kutoka neno la kifoinike kwa ajili ya mwana kondoo (kama vile Yosh. 6:4,6,8,13). Ilisimama pia kwa ajili ya Mwaka wa Jubilei (kama vile Mambo ya Walawi 25:13,28,40,50,52,54; 27:17,18,23,24).  
(Zote za hizi tatu za kwanza zinaonekana kubadilishana bila kutenganishwa. Toleo Mishnah [RH 3.2] iliruhusu mnyama yoyote—kondoo, mbuzi au paa.)
4. “matarumbeta” (BDB 348) – yawezekana kutoka katika KITENZI VERB “kujinyoosha,” ikimaanisha mfupa ulionyooka (sio pembe ya mnyama iliyojikunja). Hizi zilikuwa zimefanywa kwa shaba (baada ya uumbo na muundo wa Misri).  
Hizi zinatumika
  - a. zikiwa na ibada za kuabudu (kama vile Hesabu. 10:2,8,10; Ezra 3:10; Neh. 12:35,41)
  - b. kwa makusudi ya kijeshi (kama vile Hesabu. 10:9; 31:6; Hosea 5:8)
  - c. kwa makusudi ya kifalme (kama vile II Wafalme. 11:14)

Moja ya hizi pembe za chuma zinachukuliwa na msaidizi wa Tito katika Rumi; pia Josephus akiwaelezea katika Antiq. 3.12.6.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Lewiathan ni nani na ni nini katika Isaya 27:1?
2. Je Isaya 27:5 ina mfanano gani na Isaya 1:16-17?
3. Kwanini Isaya 27:6 ni muhimu sana katika ufahamu wa mpango wa Mungu kwa Yerusalem?
4. Ni kwa namna gani Isaya 27:12 na 13 ni tabia ya kipengele hiki kizima cha kifasihi? (yaani mchezo kati ya utaifa na umataifa na ujumuishi na mmoja mmoja)

## ISAYA 28

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kutekwa kwa Efraimu 28:1-8 (1-8)	ole wa Efraimu na Yerusalem 28:1-4 (1-4) 28:55-8 (5-6) (7-8)	Ufunuo juu ya Yuda Na Efraimu (28:1-35:10) dhidi ya viongozi wa dini 28:1-13 (1-4) (5-8)	onyo kwa ufalme wa kaskazini 28:1-4 Isaya na manabii Walevi wa Yuda 28:5-6 28:7-8	dhidi ya Samaria 28:1-4 (1-4) dhidi ya Manabii wa uongo 28:5-6 (5-6) 28:7-13 (7-13)
28:9-13 (9-13)	28:9-10 (9-10) 28:11-13 (11-13)	(9-10) (11-13)	28:9-10 28:11-13	
Yuda anaonywa 28:14-22 (14-15)	Jiwe katika Sayuni 28:16-22 (16b-19)	dhidi ya viongozi wa Kiraia 28:14-22 (14-22)	jiwe la pembedi kwa Sayuni 28:14-17a	dhidi ya washauri waovu 28:14-17a (14-17a)
(16-22)	(20-22)		28:17b-21	28:17b-22 (17b-22)
Sikiliza mafundisho ya Mungu 28:23-29 (23-29)	mfano wa wakulima 28:23-29 (23-26) (27-29)	28:22 hekima ya Mungu	mfano 28:23-29 (23-29)	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia ukr. waxvi na kipengele cha utangulizi) KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Isaya 28:1-33:24 inaunda kipengele (matamko ya "ole" sita) ambayo inashughulika na muungano wa Yuda pamoja na Misri dhidi ya Ashuru katika utawala wa mfalme Hezekia wa Yuda (kwa ajili ya tarehe ya utawala wake angalia jedwali la "Wafalme wa Ufalme uliogawanyika" katika kiambatisho cha Nne, #3.) Natumia tarehe za wanataaluma hawa watatu: John Bright, 715-687; E. J. Young, 727-699; R. K. Harrison, 716/15- 687/86). Historia ya nyuma ya kihistoria iko dhahiri muda wa kuzunguka (yaani, 705-701 k.k.) kuvamiwa kwa ufalme wa Kishuru wa Senakarebu mnamo 701 k.k.
- B. Isaya 28:1-6 inahusu kuanguka kwa Israeli kuekekea Ashuru. Mji mkuu wa Israeli, Samaria, ulianguka mnamo 722 k.k. mpaka Sargon II baada ya uvamizi wa miaka mitatu.
- C. Sargon II inalikufa mnamo mwaka 705 k.k. (angalia jedwali la "A Brief Historical Survey of the Powers of Mesopotamia" katika kiambatisho cha tatu). Wengi wa mataifa ya majini yalichukua fursa ya kuasi dhidi ya Ashuru. Senakeribu, ufalme unaofuata wa kiashuru ulivamia Yuda mnamo mwaka 701 k.k. Tunajua kutoka katika nyaraka za kiashuru kwamba aliteka vijiji vyenye kuta arobaini na sita katika Yuda na kuzima mapinduzi
- D. Ainisho fupi la Sura hii
  1. ole wa walevi wa Efraimu, mistari ya 1-6
  2. ole kwa makuhani walevi na manabii wa Yuda, mistari ya 7-13
  3. ole wauongozi wa kiraia wa Yuda, mistari ya 14-22
  4. mithali kutoka katika kilimo, mistari ya 23-29

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28:1-8

<sup>1</sup> Ole wa taji ya kiburi ya walevi wa Efraimu,  
 na ua la uzuri wa fahari yake linalonyauka,  
 lililo kichwani mwa bonde linalositawi, la hao walioshindwa na divai!

<sup>2</sup> Tazama, Bwana ana mmoja aliye hodari,  
 mwenye nguvu; kama dhoruba ya mvua ya mawe,  
 tufani iharibuyo, kama dhoruba ya maji mengi yafurikayo,  
 ndivyo atakavyotupa chini kwa mkono.

<sup>3</sup> Taji ya kiburi ya walevi wa Efraimu itakanyagwa kwa miguu;

<sup>4</sup> na ua la uzuri wa fahari yake linalonyauka,  
 lililo kichwani mwa bonde linalositawi,  
 litakuwa kama tini iliayotangulia kuiva kabla ya wakati wa hari,  
 ambayo, aionapo ye ye aiangaliaye, huila mara anapoishika mkononi mwake.

<sup>5</sup> Katika siku ile Bwana wa majeshi atakuwa ni taji ya fahari,  
 na kilemba cha uzuri, kwa mabaki ya watu wake.

<sup>6</sup> Naye atakuwa roho ya hukumu kwake ye ye aketiye ili ahukumu;  
 naye atakuwa nguvu kwao wageuzao nyuma vita langoni.

<sup>7</sup> Lakini hawa nao wamekosa kwa divai, wamepotea kwa kileo;  
 kuhani na nabii wamekosa kwa kileo, wamemezwa kwa divai,  
 wamepotea kwa kileo; hukosa katika maono, hujikwaa katika hukumu.

<sup>8</sup> Maana meza zote zimejaa matapiko na uchafu, hapana mahali palipo safi.

**28:1 “Ole”** Hili neno (BDB 222) linaweka tabia ya kitabu kizima (“ole,” sita kama vile 28:1; 29:1,15; 30:1;31:1; 33:1, sawasawa na ole sita ya 5:8-22). Neno “ole” inaaksi uzani wa kimashairi juu ya msiba.

▣“**walevi wa Efraimu**” Misari ya 1-4 ni maneno ya nabii juu ya hukumu ya kidini na uongozi wa kisiasa wa Makabila kumi ya Kaskazini(kama vile mistari ya 1 (mara mbili), 3,7; Hos. 7:5). Utumiaji mbaya wa pombe mara kwa mara unatumika kama sitiari ya hukumu ya maskini ambayo inapelekea hukumu ya kimungu. Angalia Mada maalumu katika 1:22. Tokea mgwanyiko wa muungano wa kifalme (chini ya Daudi na Suleimani) katika nyakati wa Rehoboamu(yaani, 922 K.K), kikundi cha kaskazini kilikuwa kikijulikana kwa majina yao.

1. Israeli (cheo cha kijumla)
2. Efraimu (kabila kubwa kuliko yote)
3. Samaria (mji mkuu)

<b>NASB</b>	<b>“lililo kichwani mwa bonde linalositawi”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“lililo kichwani mwa bonde lililostawi”</b>
<b>NRSV, JPSOA</b>	<b>“lililo kichwani mwa wale waliochiba chakula tele”</b>
<b>NJB</b>	<b>“lililokaa katika kichwa cha bonde zuri”</b>
<b>Peshitta</b>	<b>“katika malango ya bonde lenye rutuba”</b>
<b>REB</b>	<b>“juu ya vichwa vya wale wamiminao kwa manukato”</b>

Tungo tata linawenza kumaaanisha

1. Samaria iliyo juu ya mlima mrefu
2. wakuu wa walevi

Toleo la REB linafuata maandiko ya DSS ya Isaya28:2 “Tazama, Bwana ana mmoja aliye hodari, mwenye nguvu;” Hii inamaanisha kwa ufalme wa kiashuru uliotumwa na YHWH(kama vile Isa. 8:7; 10:5-6) kuadhibu Israeli.Uharibifu wa Makabila kumi ya kaskazini ilihitimishwa katika anguko mji mkuuSamaria baada ya kuzungukwa kwa miaka mitatu na Sargon II mnamo 722 K.K (kama vile II Wafalme 17:6; 18:9-12). Watu wake wote walipelekwa uhamishoni kuelekea Media. Wengi wa watu hawakuwahi kurudi.

Tazama namna gani Hodari wa BWANA inawekwa kitabia.

1. Mwenye nguvu
2. Mwenye uweza
3. dhoruba ya barafu (kama vile 30:30)
4. dhoruba ya uharibifu
5. dhoruba ya maji yatiririkayo kwa uweza mwangi (kama vile 8:7-8)
6. “ameitupa chini duniani kwa mkono Wake” (yaani, YHWH ndiye aliyeituma)

**28:4** Hii ni sitiari ya kilimo inayohusiana mazao ya kwanza makubwa ya mtini (kama vile Hos. 9:10; Mik. 7:1). Matunda haya yaliliwa haraka haraka na kuondoka. Ndivyo hivyo pia ardhi yenye rutuba ya makabila Kumi ya Kaskazini inatekwa na kukaliwa na wageni

**28:5 “siku hiyo”** Angalia dokezo katika 2:11. Siku ya wokovu wa YHWH na kutembelewa.

▣“**taji zuri**” Hii kwa uhalisia kwa ulinganifu “taji ya wenye majivuno wa walevi la Efraimu”katika mstari wa 1. Katika 28:1Inamaanisha Samaria, hapa yawezekana ni Yerusalem iliyoreshewa pale ambapo Masihi anatawala (kama vile Mistari.16-17).

▣“**kilemba cha uzuri**” Hii ni NOMINO nadra (BDB 862) ambayo ina usambamba na “taji” (BDB 742), inalitumia mstari wa kifalme wa Samaria (kama vile mstari wa 1) na ya Yuda (62:3).Viongozi walioteuliwa na Mungu, hata familia ya Daudi, ilifeli. Yeye mwenyewe atakuwa mfalme wao kama inavyotakiwa (kama vile I Sam. 8:7; 10:19).

▣ “Mabaki ya watu Wake” Angalia Mada Maalum katika 1:9. Mstari huu bado upo katika ubeti ukiashiria Israeli. Hii inaweza kumaanisha kwa wale (wachache) wa makabila ya kaskazini ambao siku moja yatarudi Yerusalem.

**28:6** Mstari huu unaelezea kiongozi mpya wa nasaba ya Daudi aliyeulewa na Mungu (kama vile 9:1-7; 11:1-5,10).

1. roho ya haki (haswa. 11:2)
2. kukusanyika kwa walini wa mji (yaani, Yerusalem)

**28:7** Nakubaliana na JPSOA, TEV, na NJB kwamba kuvunjwa kwa aya kunatakiwa kutokea kati ya mstari wa 6 na mstari wa 7. Mistari ya 7 na 8 inaelezea uongozi wa ki-Yuda wa sasa (kama vile mstari 14; Yer. 13:12-14, saba za VITENZI niQal KAULI TIMILIFU, ambayo inashiria hali iliyowekwa sawa), sawasawa na mistari ya 1-4, ambayo inaelezea uongozi wa kilezi wa Israeli.

**NASB, NRSV,**

NJB                           “**kuchanganywa na divai**”

**NKJV, ASV**

LXX                           “**kumezwa na divai**”

**TEV**

“**katika mkanganyiko**”

**JB**

“**kuchanganywa na divai**”

**REB**

“**kuvurugwa na mvinyo**”

KITENZI katika BDB 118 (*Niphal KAULI TIMILIFU*) inamaanisha “kumeza” au “meza” (kama vile 25:8; Mwanzo 41:7,24; Kutoka. 7:12; 15:12; Hes. 16:30,32,34; 26:10; Kumb. 11:6; Yer. 51:34). Hatahivyo, NIDOTTE, vol. 1, kurasa za 666-668 na KB 135-136 inaorodhesha mizizi mitatu inayowezekana.

1. KB 135 I, meza, kuzungukwa
2. KB 136 II, kutangaza, kuwasiliana
3. KB 136 III, *Niphal* kuchanganya; *Piel* in 3:12; *Pual* katika 9:16

**28:8 “Meza”** Neno hili (BDB 1020) linaweza kumaanisha

1. meza ya mfalme, kama vile 21:5
2. meza ya mkuu, kama vile Neh. 5:17
3. sehemu binafsi
4. sadaka, kama vile Kutoka. 25:23; Mambo ya Walawi. 24:6; Hes. 3:31; 4:7 (katika hema)

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 28:9-22**

<sup>9</sup> Atamfundisha nani maarifa? Atamfahamisha nani habari hii? Je!

Ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini?

<sup>10</sup> Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo.

<sup>11</sup> La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa;

<sup>12</sup> ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia.

<sup>13</sup> Kwa sababu hiyo neno la Bwana kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.

<sup>14</sup> Basi, lisikieni neno la Bwana, enyi watu wenye dharau, mnaowatawala watu hawa walio ndani ya Yerusalem.

<sup>15</sup> Kwa sababu mmesema, Tumefanya agano na mauti, tumeplatana na kuzimu; pigo lifurikalo litakapopita, halitatufikia sisi; kwa maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu, tumejificha chini ya maneno yasiyo kweli;

<sup>16</sup> kwa ajili ya hayo Bwana, MUNGU, asema hivi,

Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi,  
jiwe liliojaribiwa, jiwe la pemberi lenye thamani, msingi ulio imara; ye ye aaminiye hatafanya haraka.

<sup>17</sup> Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni,  
na haki kuwa ndiyo timazi; na mvua ya mawe itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo,  
na maji yatapaghari kisha mahali pa kujisitiri.

<sup>18</sup> Na agano lenu mliloagana na mauti litabatilika,  
tena mapatano yenu mliyopatana na kuzimu hayatasimama;  
pigo lifurikalo litakapopita, ndipo ninyi mtakapokanyagwa nalo.

<sup>19</sup> Kila wakati litakapopita litawachukueni. Maana litapita asubuhi baada ya asubuhi, wakati wa mchana na  
wakati wa usiku; na kuifahamu habari ile kutakuwa kitisho tu.

<sup>20</sup> Maana kitanda kile ni kifupi asiweze mtu kujinyosha juu yake,  
na nguo ile ya kujifunika ni nyembamba asipate mtu kujizingisha.

<sup>21</sup> Maana Bwana ataondoka kama vile katika mlima Perasimu,  
ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni; apate kufanya kazi yake,  
kazi yake ya ajabu; na kulitimiza tendo lake, tendo lake la ajabu.

<sup>22</sup> Basi sasa msiwe watu wenyewe kudharau,  
vifungo vyenu msije vikakazwa; maana nimesikia kwa Bwana,  
Bwana wa majeshi, habari ya hukumu itakayotimizwa,  
nayo imekusudiwa, itakayoipata dunia yote pia.

**28:9-10** Maneno ya Isaya (au maneno ya YHWH kuitia ye ye) walivamiwa na(1) uongozi wa kidini au (2) Wale aliowahutubia katika mistari ya 7-8 (kama vile Yer. 26:9-15; Amosi 7:12; Mik. 2:6-11).

**28:10,13** Hii ilikuwa ni rejea iliyofichwa. Ilijumuishwa na marudio ya &7 (BDB 846, katika Hos. 5:11 inamaanisha “kuamuru”) na &8 (BDB 876 II, katika mstari wa 17 inamaanisha “mstari wa kupimia”). Walevi wa kidini walikuwa wanashutumu jumbe za Isaya kwa kuwa mtoto na mgumu wa kuelewa (KB 1081 I #2). Mstari wa 11ni mwitikio wa Mungu kwa mwitikio wao kwa jumbe za Isaya.

**28:11-13** Huu ni mwitikio wa Isaya kwa wasomi wa kidini na wenyewe majivuno wa siku zake katika Yerusalem.

**28:11** “**La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine**” Huu ni mwitikio wa Mungu kwa kukataliwa kwa kwa nabii Wake. Ukweli ni kwamba anasema, “Ikiwa una wakati mgumu kuelewa baadhi ya vitu vyake vya chini, subiri mpaka utakaposikia lugha ya kiashuru” (kama vile mstari wa 13; 33:19; Yer. 5:15). Paulo ananukuu mstari huu katika I Kor. 14:21 katika mjadala wake wa “kunena kwa lugha.” Angalia fasiri yangu juu ya I Wakorintho katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

**28:12** “**Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha ye ye aliyechoka**” YHWH alitaka watu wake wawe na “mapumziko” (BDB 629) na amani (kama vile 11:10; 30:15; 32:17,18). KITENZI (BDB 628, KB 679) ni*Hiphil KAULI SHURUTISHI*. Hii inarejerea jumbe za Isaya za matumaini na urejesho ikiwa tu watamgeukia YHWH, lakini wasingeweza (mstari wa 12b)! Yesu aliwapa wito huo huo katika Mt. 11:28-29.

**28:13** Ujumbe pekee wa kwa ulikuwa ujumbe wa YHWH ambao waliukataa kwa ajili ya uharibifu wao.

1. kurudi nyuma BDB 505, KB 502, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 3:8; 59:14
2. kukata tamaa, BDB 990, KB 1402, *Niphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 8:15
3. kutishwa, BDB 430, KB 432, *Niphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 8:15
4. kuchukuliwa mateka, BDB 539, KB 530, *Niphil KAULI TIMILIFU*, kama vile 8:15; 24:18

**28:14** “**sikia**” Hiki KITENZI (BDB 1033, KB 1570, *Qal KAULI SHURUTISHI*) kilikuwa vyote wito wa utii na na utangulizi wa hukumu. Wasingeweza kusikiliza (kama vile 28:12,14,22,23 [mara mbili]; 29:18; 30:9,19,21,30; 32:3, 9; 33:13,15,19; 34:1 [mara mbili]). Maudhui inayojirudia rudia kiasi gani—Mungu anajaribu kuelekeza lakini wanakataa kumsikiliza! “Sikia neno la BWANA” ni alama ya kifasihi ya “ufunuo wa hukumu.”

▣ “**enyi wenge dhara**” Hii ni TUNGO (“watu,” BDB 35 na “kubeza” BDB 539). Wanatajwa mara kwa mara katika Mithali (yaani., 1:22; 29:8). Ni kwa namna gani inashangaza kwamba hii inarejerea kwa viongozi wa Yuda na Yerusalem ambao walitakiwa kujua vyema na kutumaini zaidi! Mgogoro unafunua uongozi wa kweli au kukosekana kwake

**28:15 “tumefanya agano na mauti”** Isaya kwa kebehi anayapa tabia mawazo ya viongozi wa Yerusalem. Hii inamaanisha agano (yaani, “agano,” BDB 136, angalia mada maalum katika 1:19 na neno la nadra, “makubaliano,” BDB 302, kama vile mstari wa 18) ambayo Yuda alifanya na Wamisri (kama vile 30:1-7). Ni mbinu ya kithiolojia ya neno la Mungu kupitia Musa ya kuwahudumia watu Wake pamoja na uchaguzi wa mauti na uzima katika Kumb. 30:15-20 (angalia dokezo kutoka Kumb. mtandaoni [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)). Kwa namna hii, uchaguzi unaojumuishwa kuchagua ulinzi kutoka katika chanzo cha kijeshi cha duniani au kutumaini kwa Mungu. Walichagua kifo.

▣ “**Kuzimu**” Hii inamaanisha sehemu washikiliwayo wafu na inakuwa sawa sawa na “mautini/Jehanamu.” Angalia Mada Maalum katika 5:14.

NASB	“teso lizidilo”
NKJV, NRSV	“teso imfurikayo”
NJB	“gharika iumizayo”
JB	“pigo haribifu”
LXX	“dhoruba kali”
REB	“gharika kali”

Hili ni neno la kwanza la KAULI YA ENDELEVU (BDB 1009, KB 1474, *Qal* KAULI TENDAJI). Ni neno la pili ambalo linawasilisha mbadala (NIDOTTE, vol. 4, kurasa. 64-65)

1. ַעֲשׂ, BDB 1009, “kumiminika,” kama vile 8:8; 10:22 (yaani jeshi linalovamia)
2. מְוִיבָה, BDB 1002, “mwiba,” “piga,” kama vile I Wafalme 12:11,14

▣ “**halitatufikia**” Hiki KITENZI (BDB 716, KB 778) ni aidha *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (*qere*) au *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (*kethiv*, kama vile 26:20). KITENZI kinamaanisha “kupita juu ya,” “kupita katika kati,” au “kupita karibu ya.” Inatumika mara thelathini na nne katika Isaya katika kipengele hiki cha kifasihi (yaani, sura za 28-35, kama vile 28:15,18,19 [mara mbili]; 29:5; 31:9; 33:8,21; 34:10; 35:8).

▣ “**kwa maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu**” Bahati gani mbaya kwa watu wa Mungu: hali iliyojitengeneza yenyeewe ya kutumaini katika mkono wa mwili!

1. Uongo, BDB 469, kama vile mstari wa 17 (iliyozoleka katika Zaburi na Mithali) udanganyifu, BDB 1005, kama vile 9:15; 32:7; 44:20; 57:4; 59:3,13 (iliyozoleka katika Zaburi na Mithali, ikitumiwa mara kwa mara katika Yeremia) Muundo wa KITENZI wa “kimbilio” (BDB 340) ikiashiria kuweka ujasiri na tumaini katika kitu au mtu. Mara kwa mara ikitumika kukimbilia kwa YHWH.
2. YHWH kama mwamba, Kumb. 32:37; Zab. 18:2
3. YHWH kama mama, Ruth 2:12; Zab. 36:7; 57:1; 61:4; 91:4
4. YHWH kama ngao, II Sam. 22:3,31; Zab. 18:30; 144:2; Mithali. 30:5
5. Katika Yeye, Zab. 2:12; 5:11; 7:1; 11:1; 16:1; 25:20; 31:1,19; 34:8,22; 37:40; 57:1; 64:10; 71:1; 118:8,9; 141:8; Isa. 57:13; Nah. 1:7
6. Mkono wa kuume wa YHWH, Zab. 17:7
7. Sayuni, Isa. 14:32
8. Jina la YHWH, Zef. 3:12

**28:16** Mstari huu ni mabadiliko ya kushangaza, kugeuzwa kwa matumaini kwa kithiolojia katikati ya hukumu. Mpango wa ukombozi wa milele wa YHWH unajifunua wenyeewe tena. Masihi atakuja! Ni mstari mmoja tu! Huu ni mfululizo wa vyeo vyaa kimasihii kwa kutumia “ujenzi wa” sitiari.

1. Neno “jiwe” (BDB 6) mara kwa mara linatumwi na Mungu; hatahivyo “jiwe la pembedi” (BDB 819) lina muunganiko wa kipekee pamoja na Masihi (kama vile Masihi. 118:22; Mt. 21:42, 44; Luka 20:17; Mdo.4:11; Rum. 9:33; 10:11; Efe. 2:20; I Pet. 2:6-8).
2. Neno “kujaribiwu” (BDB 103) ni neno la Kimisri la kukopa kwa punje laini za mawe ya nafaka yafaayo kwa kuchonga. Hii inaonekana kumaanisha 16d. Ufunguo kwa wazo hili ni neno “aaminie” (kama vile Isa. 30:15 kwa msisitizo unaofanana juu ya “kutumaini”).
3. Neno “msingi” (BDB 414) inapatikana hapa tu na II Nyakati. 8:16, ambapo inarejerea Sulemani kujenga msingi wake wa hekalu. Tazama kwamba msingi huu ni “umewekwa imara sana” (pambizo za NASB, “iliyojengwa vizuri”). Kiebrania kina neno linguine linalokuja mara mbili. Hapa ndipo maelezo “kwa msingi” au “iliyowekwa vyema” inakuja kutoka. Angalia Mada Maalum: Jiwe la pembedikatika 8:14-15 na Mada Maalum: Amini, Kutumaini, Imani na Uaminifu katika 22:23.

**28:17 “haki ya kisheria”** Angalia Mada Maalum: Hakimu, Hukumu na Haki katika 3:1.

□“kuwa ndiyo kanuni. . .kanuni” Hizi zilikuwa njia za kupima unyoofu (kama vile II Wafalme. 21:13) za kupima ulali (BDB 876 II) na kipimo wima (BDB 1054).

□“haki” Angalia Mada Maalum: Haki katika 1:4.

□ Mstari wa c na d ni sitiari za maji (kama vile 27:12). Ille “kimbilio la uongo” na “sehemu ya siri” inaweza kurejerea tendo la kuabudu miungu mingine katika hema lenyewe (kama vile Ezekiel 8 na Kumb. 27:15). YHWH hafanyi kazi wala kuzungumza kwa siri, sehemu za giza, bali kwa uwazi katika nuru (kama vile 45:19; 48:16).

## 28:18

NASB           “kusitishwa”

NKJV, NRSV

JB             “kusitishwa”

TEV             “kukomeshwa”

NJB             “kuvunjwa”

LXX, Peshitta

REB            “haitadumu”

Hiki KITENZI cha kiebrania (BDB 877, KB 1086, QalKAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ikimaanisha “kuinuka,” “kusimama,” au “kusimama juu.” Ni kisitiari kwa hilo ambalo halitatokea (kama vile 7:7; 8:10; 28:18; Mithali. 15:22). Mapenzi ya Mungu na mpango utapita mipango ya wanadamu (kama vile 14:24-27; 40:8; 46:10; Zab. 35:10-11; Mithali. 19:21; Yer. 44:28)! Mstari huu unahusiana na “teso lililopitiliza” ya mstari wa 18. Ita (mvamizi, kama vile II Wafalme. 24:2) kuja tena na tena na kuleta hofu na mkanganyiko. Hawatakuwa na uwezo wa kuelewa kwanini (katika ulinganifu wa 50:4). Mithali hii inaaksi kukosekana kwa utshelevu wa mipango ya kibinadamu.

**28:21 “MlimaPerazim. . .bonde la Gibeoni”** Hizi zote mbili zinamaanisha msaada wa Mungu kwa Daudi katika vita dhidi ya Wafilsti; hatahivyo katika hali ya sasa Mungu hayuko upande wa Yuda, lakini upande wa Waashuru (kama vile II Sam. 5:17-21; I Nyakati. 14:13-17).

□“kuifanya kazi Yake, kazi Zake zisizo za kawaida,

**Na kuifanya kazi Yake, Kazi yake isiyokuwa ya kawaida**” Watu wengi wanarejerea hili jukumu lisilokuwa la kawaida kwa hukumu ya Mungu; hatahivyo, kwasababu ya muktadha, jukumu lisilokuwa la kawaida ni hukumu ya Mungu, lakini kwa kutumia Falme ya Kiashuru isiyo mcha mungu (kama vile Habakkuk, NIDOTTE, vol. 1, ukurasa wa 775).

## 28:22

NASB           “uharibifu mbaya”

NKJV	“uharibifu ulioamuliwa”
NRSV	“tangazo la uharibifu”
TEV	“uamuzi wa kuharibu”
NJB	“kuamuliwa bila kipingwa”
REB	“uharibifu ultamkwa”

KITENZI (BDB 358, KB 356, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) katika *Qal* shina huashiria “kukata,” “tangazo,” au “kuashiria.”

1. umri wa maisha wa binadamu, Ayubu 14:5
2. matukio ya siku zijazo, Isa. 10:22-23; Dan. 9:26-27

Historia haiongozwi; Ni imani kwamba viumbe vyote viliumbwu na Mungu. Lina mpango wa kimungu na kusudi (yaani ukombozi wa ubinadamu ulioanguka, kama vile Mwanzo. 3:15). Tazama kauli za

1. Luka 22:22
2. Mdo. 2:23
3. Mdo. 3:18
4. Mdo. 4:28
5. Mdo. 13:29

▣ “juu ya dunia yote” Hukumu ya kiulimwengu inaonekana katika sura za 24-27 inajirudia, lakini mshukuru Mungu, kutakuwa pia na ukombozi wa kiulimwengu (yaani, mstari wa 16)!

#### ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) 28:23-29

<sup>23</sup> Tegeni masikio, sikieni sauti yangu, sikilizeni mkasikie neno langu.

<sup>24</sup> Je! Mwenye kulima alima daima, ili apande?

Afunua daima madongoa ya nchi yake, na kuyavunja?

<sup>25</sup> Akiisha kuulainisha uso wa nchi yake, je!

Hamwagi huko na huko kunde, na kutupa-tupa jira, na kuitia ngano safu safu, na shayiri mahali pake palipochaguliwa,

na kusemethi karibu na mipaka yake?

<sup>26</sup> Kwa maana Mungu wake anamwagiza vizuri na kumfundisha.

<sup>27</sup> Kwa maana kunde zile hazipurwi kwa chombo kikali,

wala gurudumu la gari halipitishwi huko na huko juu ya jira ile,

bali kunde zile hupurwa kwa fimbo, na jira ile kwa ufito.

<sup>28</sup> Ngano ya mkate husagwa; kwa maana haipuri siku zote bila kukoma;

na ingawa gurudumu la gari lake na farasi wake huitawanya ngano ile, haisagi.

<sup>29</sup> Hayo nayo yatoka kwa Bwana wa majeshi,

mwenye shauri la ajabu, apitaye wote kwa hekima yake.

**28:23-29** Hii ni nahau kwa kutumia sitiari za kilimo juu ya nmna za kupanda na kuvuna mazao ya aina fuani. Hii inazungumzia ukweli kwamba Mungu anajua kile anachokifanya. Anafanya kazi na watu Wake kwa njia zilizosahihii zenye kusudi. Anao mpango wa ukombozi wa milele ambaa unafanya kazi wenyewe katika historia ya kibinadamu!

**28:23** Mstari huu ni mfuatano wa KAULI SHURUTISHIkutoka kwa Mungu (kama vile mstari wa 29) kupitia nabii Wake kwa Watu wake.

1. tega sikio, BDB 24, KB 27, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
2. sikia sauti yangu, BDB 1033, KB 1570, *Qal KAULI SHURUTISHI*, kama vile mistari 12,14,22
3. sikiliza, BDB 904, KB 1151, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
4. sikiliza maneno yangu, same as sawasawa kama #2

Lakini wasingeweza; wasingeefanya (kama vile 6:9-10)!

**28:28 “kwa maana haipuri siku zote bila kukoma”** Hiki ni KITENZI JINA HALISI na KITENZI cha WAKATI USIO TIMIIFUwa mzizi ule ule (BDB 190, KB 218) ikitumika kwa ajili ya msisitizo. YHWH anatoa haki kwa kiasi sawa cha hukumu, sio sana wala si kidogo!

**28:29** Tumaini, msaada na furaha huja kwa kusikia na kuheshimu Neno la Mungu!

## ISAYA 29

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Yerusalem Inaonywa	Ole kwa Yerusalem	Hatimaye Yuda inarejeshwa	Maangamizi ya Yerusalem	Juu ya Yerusalem
29:1-4 (1-4)	29:1-4 (1-4)	29:1-8 (1-4)	29:1-4	29:1-12 (1-4)
29:5-8 (5-8)	29:5-8 (5-8)	(5-8)	29:5-8	(5-8)
	Upofu wa Kutotii	Machafuko ya Kiroho	Maonyo Yasiyojaliwa	
29:9-12 (9-10)	29:9-10 (9-10)	29:9-10 (9-10)	29:9-12	(9-10)
	29:11-12	29:11-12		Unabii
29:13-14 (13-14)	29:13-14 (13-14)	29:13-21 (13-14)	29:13-14	29:13-14 (13-14)
			Tumaini la Nyakati Zijazo	Furaha ya Nuru
29:15-16 (15-16)	29:15-16 (15-16)	(15-16)	29:15-16	29:15-24 (15-24)
Baraka Baada ya Kutii	Urejeshaji hekima wa siku zijazo			
29:17-21 (17-21)	29:17-21 (17-21)	(17-21)	29:17	
29:18-21 (22-24)	29:22-24 (22b-24)	29:22-24 (22b-24)	29:22-24	29:22-24

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkaao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuvuwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Toleo la The Jewish Study Bible (uk. 839-840) linaainisha sura hii kamaushairi mashairi matatu yaliyojitetenga na yenye kujitegemea.
  1. mist. ya 1-8 (inaanza na "ole")
  2. mist. ya 9-12
  3. mist. ya 15-24 (inaanza na "ole")
- B. Maajabu ya YHWH kurejea katika matatizo ya watu wake ndiyo dhamira kuu.
  1. 3:25-5:6
  2. 8:6-8
  3. 8:22-9:1
- C. Mpangilio wa kihistoria wa surah ii unaweza kuonekana kwa uvamizi wa Senakaribu ndani ya Yuda mnamo 701 K.K. Yerusalemu inaepushwa (thiolojia ya Isaya), lakini Yuda inatishwa
  1. Isaya 36-39
  2. II Wafalme 18-19
  3. II Nyakati 32

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 29:1-4

<sup>1</sup>Ole wa Arieli, Arieli, mji ambaao Daudi alifanya kituo chake ndani yake;

ongezeni mwaka baada ya mwaka; sikuu na zirudi wakati wake,

<sup>2</sup>ndipo nitamwudhi Arieli;

kutakuwapo maombolezo na kilio;

naye atakuwa kwangu kama Arieli.

<sup>3</sup>Nami nitapiga kimo juu yako pande zote, nitakuhusuru kwa ngome,

nami nitajenga maboma yakuzunguke.

<sup>4</sup>Nawe utashushwa, nawe utanena toka chini ya nchi,

na maneno yako yatakuwa chini toka mavumbini;

na sauti yako itakuwa kama sauti ya mtu mwenye pepo,

ikitoka katika nchi, na matamko yako yatanong'ona toka mavumbini.

29:1 "Ole" Angalia maelezo katika 5:8.

▣ "Arieli" (mst. wa 1,2,7) Neno hili linaweza kumaanisha

1. mashujaa, kama vile II Sam. 23:20; I Ny. 11:22 (BDB72 I, #3)
2. "simba wa Mungu" (BDB 72 I #1)
3. "afya ya Mungu" (BDB 72 II)

Kwa sababu jina hili linatumika katika maana yaustawi wa kiadhabahu katika mst. wa 2, ambayo inafuata Eze. 43:15-16, Naamini hiki kinarejelea afaya ya Mungu, ambayo inaweza kuonekana dhahiri katika 31:9. Kwa sababu ya mst. wa 7, ni dhahiri kuwa hili ni dokezo la Yerusalemu. Ubeti wa kwanza (yaani, 29:1-4) unajihuisha na makazi ya Yuda, Yerusalemu, kama 28:1-4 inashughilika na makao ya Mkabila kumi ya Kaskazini, Samaria.

▣ “**ongezeni mwaka baada ya mwaka; sikukuu na zirudi wakati wake**” Huu ni ubti wa pili wa mst. wa1 unasistiza kwamba mist. ya1-4 inarejelea Yerusalem, sehemu ya sikukuu za Israeli (kama vile Kutoka 23; Kumbukumbu la Torati 16).

1. ongezeni, BDB 414, KB 418, *Qalya KAULI SHURUTISHI*
2. zirudi, BDB 668, KB 722, *Qalya KAULI YA WAKATI HSRUTISHI* inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI29:2-3

**29:2-3** Mistari hii inaeleza kile atakachokifanya YHWH juu ya maji wake uliochagauliwa (yaani, Yerusalem, mahali ambapo alilisababisha jina lake kujulikana kwa wingi, kama vile Kumb. 12:5,11,21; 14:23,24; 16:2,6,11; 26:2).

1. Nilateta dhiki, BDB 847, KB 1014, *Hiphilya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile mst. wa 7; 51:13 (mara mbili); Kumb. 28:53,55,57.
2. Naye atakuwa kama
  - a. maombolezo, BDB 58, kama vile 21:2; 35:10; 51:11
  - b. kuhuzunika, BDB 58 kuweka tunzi katika mfumo wa uwili ni tabia ya Isaya, pia elewa Omb. 2:5
  - c. kuwekwa nje ya ustawi, BDB 72, kama vile mist. 1,2,7
3. Nitajenga boma likuzunguke pande zote, BDB 333, KB 332, *Qalya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile Luka 19:43,44
4. Nitakomesha maombolezo yake yote, BDB 848 II; KB 1015, *Qalya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile 21:2
5. Nitainua minara ya mapambano, BDB 877, KB 1086, *Hiphil ya KAULI TIMILIFU*, Kama vile 23:13

**29:4** Mstari huu una mtiririko wa stiari zihuusizo mauti.

1. nawe utashushwa, BDB 1050, KB 1631, *Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
2. utanena toka chini, BDB 180, KB 210, *Piel ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
3. toka mavumbini, BDB 1005, KB 1458, *Niphal ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
4. sauti yako itakuwa kama sauti ya mtu mwenye pepo, BDB 224, KB 283, *Qal ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
5. matamko yako yatanong'ona toka mavumbini, BDB 861, KB 1050, *Pilpel ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*

Huu muktadha haujihusishi na maarifa yahusuyo mawasilianao na mizimu, kama Kumb. 18:9-12,14 ilivyo, bali lugha ya kistiari yenye kutoa ufanuzi juu ya Yerusalem, ukaribu wa maangamizi ya moja kwa moja, akimilia Mungu wake katika kwa sauti dhaifu huku akiwa amepiga magoti juu ya ardhi kabla ya kukumbwa na mauti.

#### ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) 29:5-8

<sup>5</sup>Lakini wingi wa adui zako utakuwa kama mavumbi membamba,  
na wingi wao watishao utakuwa kama makapi yapitayo;  
naam, itakuwa mara na kwa ghafula.

<sup>6</sup>Naye atajiliwa na Bwana wa majeshi kwa ngurumo, na tetemeko la nchi, na sauti kuu,  
na chamchela,

na tufani, na mwali wa moto uteketezao.

<sup>7</sup>Na wingi wa mataifa wapiganao na Arieli,  
wote wapiganao naye na ngome yake, nao wamwudhio,  
watakuwa kama ndoto, na maono ya usiku.

<sup>8</sup>Tena itakuwa kama mtu mwenye njaa aotapo, kumbe, anakula;  
lakini aamkapo, nafsi yake haina kitu; na kama mtu mwenye kiu aotapo, kumbe, anakunywa;  
lakini aamkapo, kumbe, anazimia, na nafsi yake inatamani;  
hivyo ndivyo utakavyokuwa huo wingi wa mataifa waletao vita juu ya mlima Sayuni.

**29:5-6** Hiki ndicho kitendo cha kuirudia maara kwa mara mistari hii miwili iliyo katika muktadha. Mungu ameahidi kuihukumu Yerusalem na sasa anaahidi kuiwakomboa Yerusalem kutokana na adui wa uvamizi wa Isaya 36-37.

Katika mst. wa6, kuna matumizi ya stiari ya kimbunga ili kutoa ufanuzi juu ya Mungu .Hii ni dhana ya mara kwa mara kwa Manabii wote. Hata matumizi ya nguvu ya stiari hii yanaweza kupatikana katika 30:27-33.

Tambua kileatakachokifanya YWHW (yaani,BWANA wa majeshi, mst. wa 6) kwa hawa wavamizi.

1. utakuwa kama mavumbi membamba
2. utakuwa kama makapi yapitayo
3. itakuwa mara na kwa ghafla (zote BDB 837, עַלְפָה, kama vile 30:13 נִחְמֹדֶת, kama vile 47:11; 48:3)
4. atajiliwa(kif. "atafikiwa na , " BDB 823, KB 955, *Niphal ya KAULI YA WAKATIUSIOTIMILIFU*) kwa ngurumo (BDB 947)
5. watajiliwa kwa tetemeko (BDB 950)
6. atajiliwa kwa sauti kuu (BDB 876, kifungu hiki kinatumika katika 33:3 kama ujumbe wa kinabii ambao unaweza kufanana na I The. 4:16)
7. atajiliwa kwa chamchela (BDB 693)
8. atajiliwa kwa tufani (BDB 704)
9. atajiliwa kwa mwali wa moto uteketezao (BDB 529 TUNGO BDB 77; KITENZI, BDB 37, KB 46, *Qal ya KAULI TENDAJI ENDELEVU*)

Haya yote yanaeleza juu ya kuja/kujiliwa naYWHW kwa ajili ya hukumu (kama vile 28:2). Hizi aina stiari za machafuko zilikuwa mwanzo wa asili ya lugha ya matukio ya siku za mwisho.

## 29:5

NASB, NJB,REB	"maadui"
NKJV, NRSV	"wapinzani"
NASB, NRSV (footnote)	"wageni"
TEV	"watu wa nje"
Peshitta	"watesao"

Toleo la MT lina kifungu "wageni wako" (וְגַנֵּן, BDB 266, KB 267, *Qal ya KAULI TENDAJI ENDELEVU*), lakini kuna uwezekano wa mkanganyiko "R" (ר) - "D" (ד). Kiebrania cha kifungu cha "maadui zako" (מְאֹדָעַ) kinatoka katikaTargums.

**29:7-8** Haya ni matumiziya stiari ya jinamizi(kif. "ndoto," BDB 321; "maono ya usiku,"BDB 302 TUNGO 538) kueleza matokeo ya tendo la Mungu sehemu zote YudanaAshuru. Katika mst. wa7, wavamizi wa ki-Ashuru watakuwa kama jinamizi lipitalo Yuda, katika mst. wa 8 jinamizi litajitokeza katika jeshi la Ashuru (kama vile II Fal. 19:35-37; II Nyakati 32; Isaya 36-37).

## 29:7

NASB, NRSV	"ngome yake"
NKJV	"boma lake"
NJB	"wigo"
REB	"kazi za kuzingira"

Tofauti kati ya hizi chaguzi mbili nimkanganyiko wa "R" and "D".

1. ngome, BDB 845 II, מְצֻדָּתָה
2. boma, BDB 849, וְמַצְרָתָה

Toleo la UBS Hebrew Text Project inaipa #1 daraja "C" (shaka lenye kufikirika).

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:9-12

<sup>9</sup>Ngojeni mstaajabu;

fanyeni anasa zenu na kuwa vipofu;

wamelewa wala si kwa mvinyo; wamewaya-wayaya wala si kwa sababu ya kileo.

<sup>10</sup>Kwa maana Bwana amewamwagieni roho ya usingizi, amefumba macho yenu, yaani, manabii;

**amefunika vichwa vyenu, yaani, waonaji.**

<sup>11</sup> Na maono yote yamekuwa kwenu kama maneno ya chuo kilichotiwa muhuri, ambacho watu humpa mtu aliye na maarifa, wakisema, Tafadhali ukisome hiki; akasema, Siwezi, kwa kuwa kimetiya muhuri;

<sup>12</sup> kisha chuo hiki apewa mtu asiye na maarifa, akaambiwa, Kisome hicho tafadhali, akasema, Sina maarifa mimi.

## **29:9“Ngojeni mstaajabu,**

**fanyeni anasa zenu na kuwa vipofu”** Mistari miwili ya kwanza ya ushairi ya mstarai huu inazo KAULI SHURUSHI nne.

1. ngojeni, BDB 554, KB 552, *Hithpalpel* ya KAULI SHURUTISHI, JINSIA YA KIUME WINGI
2. mstaajabu, BDB 1069, KB 1744, *Qalya* KAULI SHURUTISHI, JINSI YA KIUME WINGI; kif. “kushangazwa,” kama vile Hab. 1:5  
NASB“mstaajabu”  
NKJV“mkashangae”  
NRSV“kuwa katika bumbuazi”  
NJB“kuchangamka”  
LXX, Peshitta“kushangazwa”
3. fanyeni anasa zenu, BDB 1044 I, KB 1612, *Hithpalpelya* KAULI SHURUTISHI, JINSI YA KIUME WINGI
4. Kufanya kipofu, BDB 1044, KB 1612, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, JINSI YA KIUME WINGI, kama vile 6:9-10; Mika 3:6-7

Inawezekana kwamba #3 na #4 zinatokana na asili ya Kiebrania ya neno “kufurahia” (BDB 1044 II), ikiwa ni hivyo, kifungu hiki ni cha kimzaha.

Tambua ulinganifu kati ya uhuru wa mwanadamumu, mst. wa9 na enzi ya ki-Ungu, mst. wa10. Zote hizi ni za kweli! Angalia Mada Maalum katika 1:3.

▣“wamelewa wala si kwa mvinyo” Haya ni matumizi mengine ya neno ulevi (BDB 1016, KB 1500, *Qal* ya KAULI YA WAKATI ULIOPPO) yenyе kueleza uasi wa viongozi wa watu wa Mungu wa kidini na kisiasa (kama vile 28:1-4,7-8).

## **29:10-12**Elewa kazi za YHWH katika kuundoa ujumbe wake kutoka kwa watu wake (kama vile 6:9-10; Mik. 3:6-7).

1. Bwana amewamiminia (BDB 650, KB 703, *Qalya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) roho ya usingizi mzito (BDB TUNGO BDB 922)
2. Ameyafunga (BDB 783, KB 868, *Pielya* KAULI ISIO TIMILIFU) macho ya manabii wenu
3. Ameyafunika (BDB 491, KB 487, *Pielya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, TEV “vipofu vipofu waliofungamanishwa”) macho ya wote viongozi wa kidini na kisheria (kama vile mist. ya 11-12; 6:9-10; 8:16)

Mstari wa10 unanukuliwa na Paulo katika mjadala wa Israeli kushindwa kuamini/kutumaini katika Yesu Masihi katika Rum. 11:8.

**29:11 “kilichotiwa muhuri”**Hiki KITENZI (BDB 367, KB 364, *Qalya* KAULI TENDWA ENDELEVU) pia kinatumiwa nalsaya katika8:16, ambapo kinarejelea mafunjo ya kimafuno yaliyoandikwa na nabii kwa mwongozo wa Mungu. Kifungu “kilichotiwa mhuri”kinarejelewa kama namna ya

1. kuonyesha umiliki
2. kuhakikisha usalama

Tendo hili lilikamilishwa kwa

1. tone la nta (au iliyofinyangwa) juu ya kingo zilizojikunjwa lenye muhuri wa mviringo wa yule aliyetuma wenyе kugandamizwa.
2. matoneya nta (au iliyofinywangwa) yenyе muhuri kati yao na kukandamizwa kwa pete au isharana kukandamizwa kwa pete ya yule aliyetuma.

Kama Isaya alivyoambiwa kutia muhuri ule ujumbe katika 8:16, ndivyo ilivyo,kwa Danieli katika Dan. 12:4. Hata hivyo, katika 29:11 hii ni stiari ya kuhitimisha ufunuo wa Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 29:13-14**

<sup>13</sup>Bwana akanena,

Kwa kuwa watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao,  
bali miyo yao wamefarakana nami,  
na kicho chao walicho nacho kwangu ni maagizo ya wanadamu waliyofundishwa;

<sup>14</sup>kwa sababu hiyo mimi nitafanya tena kazi ya ajabu kati ya watu hawa,  
kazi ya ajabu na mwujiza;  
na akili za watu wao wenyewe akili zitapotea, na ufahamu wa wenyewe busara wao utafichwa.

**29:13“hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao”**Hili neno (BDB 620, KB 670, *Niphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) linazungumzia matendo ya kusanyiko la kuabudu ndani ya hekalu.Kwa uhalisia wake neno hili lilikuwa likitumiwa na makuhani (yaani, Kut. 19:22).

▣**“kicho chao walicho nacho kwangu ni maagizo ya wanadamu waliyofundishwa”**Huu ni ukweli wa kithiolojia ambao unaonyesha kanuni na litrujia, pasipokuwa na uhusiano binafsi, unaoambatana na maisha, upendo na maadili, yote haya ni kumkataa Mungu (kama vile 1:10-15;58:1-5; Yeremia 7; Amosi 5:21-24; Mika 6:6-8; Mt. 15:1-20; Marko 7:1-23; Kol. 2:16-23; II Tim. 3:5). Kanuni hazikuwa mbaya, I ni mtazamo wa mtu ambao unajaribu kuwa juu ya Mungu.

Mstari wa shairi la hapo juu unafanana na ule unaofuatia, “hawa hunikaribia kuniheshimu kwa vinywa vyao” (kama vile Yer. 12:2). Hawa wanaosema kitu kimoja, lakini wanaishi kivingine (kama vile Mt. 15:8-9; Marko 7:6-7, ambapo “maneno” na “vinywa” vinaelezwa kama “kuyakataa maagizo ya Mungu, mnawashikilia watu wadesturi,” kifungu kinachoelezwa katika Marko 7:3,5,9,13).

**29:14“mimi nitafanya tena kazi ya ajabu . . . ajabu na mwujiza”**Katika lugha ya Kiingereza vifungu hivi vinatamkika vema, lakini ni vya *Hiphil*TUNGO YA KITENZI; *Hiphilya* KITENZI JINA HALISI; na NOMINO zote za asili zinazofanana (BDB 810), ambazo zinadokeza

1. mapigo yasiyo ya kawaida katika Kutoka 3:20; Kumb. 28:59
2. ushauri usio wa kawaida ulio mkatika 9:6; 28:29
3. matendo ya kushangaza yaliyo katika Kut. 34:10; I Ny. 16:9,12,24; Isa. 25:1

Lazima muktadha utambulisse kama hukumu ni chanya au hasi. Hapa ni hukumu ya YHWH kwa watu wake ni hasi. Hii hukumu itakuwa kwamba viongozi wao wenyewe hekima watashindwa katika kazi yao (kama vile mist. ya 9-12).

Paulo ananukuu mstari huu katika INya. 1:19 katka mjadala wake wa upumbavu wa hekima ya mwanadamu hasa kama inavyojikita katika kuelewa kwa nini Masihiyampasa kuteswa na kufa (yaani, injili).

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 29:15-16**

<sup>15</sup>Ole wao wanaojitahidi kumficha Bwana mashauri yao,  
na matendo yao yamo gizani, nao husema, Ni nani atuonaye? Nani atujuaye?

<sup>16</sup>Ninyi mnapindua mambo; Je! Mfinyanzi ahesabiwe kuwa kama udongo;  
kitu kilichofinyangwa kimmene yeeye aliyekifinyanga, Hakunifinyangwa huyu;  
au kitu kilichoumbwa kimmene yeeye aliyekiumba, Yeeye hana ufahamu?

**29:15“kumficha Bwana mashauri yao”**Kipengeke hiki kinayarejelea mashauri ya uongozi wa Yuda kwa ajili ya muungano wa kisiasa pamoja na Misrikama vile 28:7-22; 30:1-5; 31:1-3) ili kujilinda dhidi ya Ashuru. Hawa wanaitumaini Misri, si YHWH!

▣**“Ni nani atuonaye?” “Nani atujuaye”**Kimsingi huku ni kuukataa uwepo binafsi wa Mungu. Mstari wa 16unaeleza mantiki na upumbavu wa semi hizi.

**29:16 “Mfinyanzi”** Mungu kama mfinyanzi ni stiari ya kibiblia ya kawaida (kama vile Isa. 45:9; 64:8; Yer. 18:4 na kuendelea; Ayubu 10:9). Kwa hali iliyo dhahiri kifungu hiki kiliboreshwu kutona na uumbaji asilia wa mwanadamu katika Mwa. 2:7. Paulo analigusia andiko hili katika Rum. 9:20. Warumi 9 ni ukubalifu wa enzi ya Mungu ya moja kwa moja na iliyo kamilika!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:17-21**

<sup>17</sup>Je! Si muda mdogo uliobaki,  
na Lebanoni itageuzwa kuwa shamba lizaalo sana,  
na lile shamba lizaalo sana litahesabiwa kuwa msitu?  
<sup>18</sup>Na katika siku hiyo viziwi wasasikia maneno ya hicho chuo,  
na macho ya vipofu yataona katika upofu na katika giza.  
<sup>19</sup>Wanyenyekevu nao wataongeza furaha yao katika Bwana,  
na maskini katika wanadamu watafurahi katika Mtakatifu wa Israeli.  
<sup>20</sup>Kwa maana mwenye kutisha ameangamizwa,  
naye mwenye dharau amekoma,  
nao wote watazamiao uovu wamekatiliwa mbali;  
<sup>21</sup>hao wamfanya mtu kuwa amekosa katika neno,  
na kumtegea mtego yeye aonyaye langoni,  
na kumgeuza mwenye haki kwa kitu kisichofaa.

**9:17-21** Hapa kipengele hiki kinaleza nyakati mpya za ki- Masihi ambazo zinakuja.

1. muda mdogo uliobaki, mst. wa 17a (kama vile 10:24-25)
2. Lebanoni itageuzwa kuwa shamba lizaalo sana, mst. wa 17b,c, kama vile 32:15; 35:1-2 (toleo la NASB Study Bible, uk. 996, linahusianisha kifungu hiki na Isa. 10:34 na kudai kwamba Lebanoniingeliweza kuwa njia ya kuirejelea Ashuru). Senakaribualijivunia unyonyaji wake juu ya msitu wa(kama vile 37:24; II Fal. 19:23).
3. viziwi wasasikia, mst wa 18a, kama vile 32:3; 35:5
4. vipofu yataona, mst. wa 18b, kama vile 32:3; 35:5
5. Wanyenyekevu nao wataongeza furaha yao katika Bwana, mst. wa 19a, kama vile 11:4; 61:1
6. na maskini katika wanadamu watafurahi katika Mtakatifu wa Israeli, mst. 19b, kama vile 3:14-15; 11:4; 14:30,32
7. naye mwenye dharau amekoma, mst. wa 20a
8. nao wote watazamiao uovu wamekatiliwa mbali, mst. wa 20a, kama vile 28:14
9. nao wote watazamiao uovu wamekatiliwa mbali, mst. wa 20b
10. mwenye haki kwa kitu kisichofaa, mst. wa 21, kama vile mst. wa 32:7

Kipengele hiki kina ufananowa kithiolojia na yale maelezo yanayostaajabisha ya sifa ya YHWH katika 25:4.

Hakikisha unanukuu kwamba #3 na #4 ni stiari za awali kwaajili ya kupokea na kuelewa ufunuo wa (kama vile Kumb. 29:4; Isa. 5:12,13; 6:9; 30:9).

**29:19“Mtakatifu”** Angalia Mada Maalum katika 6:3.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 29:22-24**

<sup>22</sup>Basi, Bwana aliyemkomboa Ibrahimu asema hivi,  
katika habari za nyumba ya Yakobo;  
Yakobo hatatahayarika sasa, wala uso wake hautabadilika rangi yake.  
<sup>23</sup>Bali atakapowaona watoto wake,  
walio kazi ya mikono yangu, katikati yake, wao watalitakasa jina langu;  
naam, watamtakasa Mtakatifu wa Yakobo, nao watamcha Mungu wa Israeli.  
<sup>24</sup>Hao nao wakosao rohoni mwao watapata kufahamu,  
na hao wanung'unikao watajifunza elimu.

**9:22-24** Kama mist. Ya 5-8 inavyoangukia katika muktadha wa hukumu juu ya Yerusalemupamoja na neno la matumaini, ndivyo ilivyo, mist. ya22-24. Hii tofauti ya haraka kati ya maono ya hukumu na maono ya ahadi ndiyo sifa bainishi ya Manabii. Mara nyangi hukumu ni kwa ajili ya urejesho! Ndiyo, Mungu atawahukumu watu wake pale wanapotenda dhambi na kulivunja agano lake, lakini anayo sababu kuu juu yao (yaani, mpango wa milele kwa wanadamu wote). Tambua vifungu na majina tofauti tofauti ambayo yanadokeza agano la Uungu.

1. Bwana aliyemkomboea Ibraimu, mst. wa 22
2. watoto wakewalio kazi ya mikono yangu, mst. wa 23
3. jina langu. . Mtakatifu wa Yakobo, mst. wa 23
4. Mungu wa Israeli, mst.wa 23, kama vile 1:4

**29:22** Nyumba Ibraimu iliyochaguliwailendelezwa na kuwa katika makabila ya wana wa Yakobo. YHWH anaahidi nyakati mpya wakati,kwa uweza na uwepo wa agano, hawa

1. hawatahaibishwa, BDB 101, KB 116, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, yenyenye kutumika mara kwa mara katika Zaburi, Isaya,na Yeremia
2. ama atastawi katika wingi wa nuru, BDB 301, KB 299, *Qalya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, hiki KITENZI kinajitokeza hapa tu.

VITENZI vyote vinazirejelea nahau za Kiebrania za kutokuwa na matumaini na hatia juu ya tabia ya kutotii. Mtenda dhambi hujisikia kutokumfurahia Mungu!

▣“aliyemkomboea Ibraimu”Hiki KITENZI (BDB 804, KB 911, *Qalya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, angalia Mada Maalum ifuatayo) hapa kiatumika kwa Ibraimu. Kifungu hiki kinaweza kumaanisha

1. kukombolewa kutoka nyumba yenyenye kuabudu miungu (kama vile Mwanzo 11)
2. watu wa Mungu waliochaguliwa kama watu wa agano kwa namna ya kipekee (yaani, Mwanzo 12, 15, 17)
3. tendo la ukombozi mahususi
  - a. kutoka kwa Farao (kama vile Mwa. 12:10-20)
  - b. kutoka kwa Abimeleki (kama vile Mwanzo 20)

YHWH anaitwa “Mkombozi wa Israeli” (kama vile 41:14; 43:14; 48:17; 49:7,26; 54:5,8). Ile dhana ya YHWH kama mkombozi wa pekee wa nyumba iliyochaguliwa inaweza kuwa ukweli wa kithiolojia wa mist.ya 22-23.

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

- . AGANO LA KALE
  - A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
    1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyangi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruth 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
    2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
      - a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
      - b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
      - c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)
  - B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
    1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
      - a. Kimaumbile
      - b. Kijamii

- c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
- 2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
  - a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
  - b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
- 3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (yaani., *go'el*, BDB 145).
- 4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
  - a. Baba
  - b. Mme
  - c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupertia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

#### AGANO JIPYA

- A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
  - 1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusiowandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.
  - 2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenyewe dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamilii, ukubalifu, na upenyo!
  - 3. *Luō*, "kuweka huru"
    - a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulmwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
    - b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
      - 1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
      - 2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
      - 3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
    - c. *Lutrōsis*, "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
      - 1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
      - 2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
      - 3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
  - 4. *Apolytrōsis*
    - a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
      - 1) Luka 21:28
      - 2) Warumi 8:23
      - 3) Waefeso 1:14; 4:30
      - 4) Waebrania 9:15
    - b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
      - 1) Warumi 3:24
      - 2) 1 Wakorintho 1:30
      - 3) Waefeso 1:7
      - 4) Wakolosai 1:14
  - 5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliywafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.

1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kat), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

**29:24** Mstari huu ni kinyume cha mistari ya 9-12,14. Ufunuo na uelewa utarudi kwa watu wa Mungu kuitia uongozi wake ulioitwa, zote za kiraia na kidini! Huku ni kuinuliwa kwa vipofu na viziwi 6:9-10!

□  
**NASB**            “ufahamu”  
**NKJV, NRSV**  
**LXX, Peshitta**    “ufahamu”

Neno la Kiebrania *ruah* (BDB 924), lililotumika kwa namna ya shughuli ya kiakili (kama vile Kutoka 28:3; Kumb.34:9; I Nyakati. 28:12; Ayubu 20:3; Ezek. 20:32). Kumbuka, muktadha, muktadha, muktadha huamua juu ya maana ya neno

## ISAYA 30

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Yuda anaonywa juu Ya ushirikiano na Misri	matumaini yasiyo na faida toka Misri	kutuma wajumbe Misri	makubaliano na Misri yasiyo na maana	dhidi ya wajumbe wa Misri
30:1-5 (1-5)	30:1-5 (1-5)	30:1-7 (1-5)	30:1-5	30:1-5 (1-5)
Unabii juu ya				wajumbe
30:6-17 (6-11)	30:6-7 (6-7)	(6-7)	30:6-7	30:6-7
	Watu waasi	mapatano ya sira kati Yuda na Misri	watu wasio tii	maagano
	30:8-11 (8-11)	30:8-17 (8-14)	30:8-11	30:8-17 (8-11)
(12b-14)	30:12-17 (12b-14)		30:12-14	(12-14)
(15b-17)	(15b-17)	(15-17)	30:15-18	(15-17)
Mungu ni wa rehema na haki	Mungu atawarehemu	Matumaini kwa wale wanaoteseka	Mungu atasamehe	
30:18 (18)	30:18-22 (18)	30:18 (18)	Mungu atabariki watu wake	30:18 (18)
30:19-22		30:19-22	30:19-26	30:19-26 (19-22)
30:23-33 (27-33)	30:23-26 (23-26)	30:23-26		
	Hukumu juu ya Ashuru	Ufunuo dhidi ya Ashuru	Mungu ataadhibu Ashuru	Dhidi ya Ashuru
(27-28)	30:27-33 (27-28)	30:27-33	30:27-33 (27-33)	30:27-33
		30:29-33		
	(29-33)		30:30-33	

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. xvi kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk

## **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Muktadha huu unarejelea maasi mengi dhidi ya Ashuru baada ya kifo cha Sargon IImwaka wa 705 K.K. Maasi haya yalipelekea vibaraka wengi wa serikali kuwekwa chini ya Dola mpya ya mfalme Senakeribu.
- B. Misri ambayo Hezekia aliomba msaada wa ushirikiano kisiasa/kijeshi alikuwa mtawala wa Ishirini na tano. Iliongozwa na Mkushi/mfalme Mnubi, Shabaka, aliyekuwa jeuri na alijaribu kuyaunganisha mataifa yote madogo, kutoka mwanzo wa mto Frati hadi mipaka ya Misri, dhidi ya Ashuru.
- C. Kuna ole sita zaufunuo kwenye sehemu hii ya Fasihi (yaani.,Sura ya 28-33).
  1. Ole kwa makabila ya kaskazini na kusini mwa Israeli, Sura 28
  2. Ole kwa Yerusalem, 29:1-14
  3. Ole kwa wale wanaotafuta msaada muungano wa kisiasa na sio kwa YHWH, 29:15-24
  4. Ole kwa wanaotafuta msaada kutoka Misri, Sura ya ya 30
  5. Ole kwa wanaotafuta msaada kutoka Misri, Sura ya 31-32
  6. Ole kwa Ashuru, Sura ya 33

## **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 30:1-5**

<sup>1</sup> Ole wa watoto waasi; asema Bwana;  
watakao mashauri lakini hawayataki kwangu mimi;  
wajifunikao kifuniko lakini si cha roho yangu;  
wapate kuongeza dhambi juu ya dhambi;

<sup>2</sup>waendao kutelemkia Misri  
wala hawakuuliza kinywani mwangu;  
ili wajitie nguvu kwa nguvu za Farao,  
na kutumainia kivuli cha Misri.

<sup>3</sup>Basi, nguvu za Farao zitakuwa aibu yenu,  
na kutumainia kivuli cha Misri kutakuwa kufadhaika kwenu.

<sup>4</sup>Kwa maana wakuu wake wako Soani,  
na wajumbe wake wamefika Hanesi.

<sup>5</sup>Wote watawaonea haya watu wasioweza kuwafaidia,  
wasio na msaada wala faida, bali ni aibu na sababu ya kushutumiwa.

30:1 “Ole” Angalia muhtasari katika 18:1.

▣ “**watoto waasi**” Jina hili linaonyeshwa mara mbili.

1. Walikuwa ni “watoto” (yaani ., Uzao wa Ibrahim, warithi wa Ahadi, kama vile Rum. 9:4-5)
2. Matendo yao “waasi” (BDB 710, KB 770, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*, kama vile 1:23), ambapo linatafsiriwa “Uasi”, pia muhtasari katika 65:2. Msingi wa maana wa asili ni “ukaidi” (kama vile . Hos. 4:16). Katika Zab. 78:8 neno hili na kisawechake (BDB 598) vinafanana (kama vile. Kumb. 1:26,43; 9:7,23,24; 21:18,20; 31:27). Hii inajitokeza kuelezea tabia ya watu wa Mungu wa Nyakati za kale.

Ni sehemu ya kuongezeka kwa laana!

Tambua kwamba Isaya alifanya jambo la maana sana kuwapa jina la “**watoto waasi**” kwa kile walichokifanya.

1. Walibuni mipango yao wenyewe ili kujilinda wao dhidi ya Ashuru (kama vile. 29:15)
2. Walifanya ushirikiano wa kisiasa (tazama muhtasari chini) na Misri (kama vile. 20:5; 31:3; 36:9), lakini wakamkataa Roho wa YHWH(uwepo wake, Ahadi, na ulinzi, kama vile . 28:14-22; 29:15-16)

▣

**NASB, NRSV** “**fanya ushirikiano**”

**NASB margin** “**wakimimina kinywaji cha sadaka**”

**NKJV** “**mipango ya kubuni**”

**TEV** “**wakaweka makubaliano**”

**NJB** “**wakafanya ushirikiano**”

**REB** “**wakafanya mipango**”

**LXX** “**wakafanya makubaliano**”

**Peshitta** “**wakatoa sadaka za mvinyo**”

Asili hii ya Kiebrania ina maana nyingi.

1. ΤΟΙ, KITENZI, BDB 650 I katika *Qal shina*
  - a. wakamimina, sitiari, Isa. 29:10
  - b. wakamimina, Fasihi, Isa. 30:1; Hos. 9:4
  - c. Wakatupa sanamu za dhahabu, Isa. 40:19; 44:10
2. ΤΟΙ KITENZI , BDB 651 II kina maana “wakafanya” Isa. 25:7, REB

Ingawa sadaka ya kinywaji (Kumb. 32:38) haikuwa sehemu ya utaratibu wa makubaliano, yalifanyika labda ni kwa sababu ya tabia za kidini za makubaliano ya watu wa kale (kama vile. Isa. 57:6).

**30:2 “wajitie nguvu kwa nguvu za Farao na kutumainia kivuli cha”** Hii inaa kisi Maneno mawili (BDB 731, KB 797 na BDB 340, KB 337,yote kwa pamoja Qa TUNGO YA KITENZIJINA HALISI) kwa kawaida hutumika kwa YHWH, lakini hapa wametumia kuelezea Misri.

### **MADA MAALUM: KIVULI (kwa kutumia tungo kadhaa zinazofanana)**

Hii ni Nahau ya Kiebrania kwa ajili ya

1. “**kivuli**” kama ulinzi
  - a. wa YHWH – Isa. 16:3-4
  - b. wa Misri – Isa. 30:2-3
  - c. wa Masihi wa YHWH – Omb. 4:20
2. “**kivuli cha mkono**,” pia ni ulinzi wa YHWH – Zab. 121:5; Isa. 49:2; 51:16;pia muhtasari Kut. 33:22)
3. “**kivuli cha juu yangu**,” Nahau nyingine kwa ajili ya ulinzi – Mwa. 19:8
4. “**kivuli cha YHWH wingu maalum wakati wa nyikani kipindi cha kuzunguka**” (yaani., wingu mchana , usiku Nuru kuwalinda wao) – Kut. 13:21-22; 14:19,20,24; Isa. 4:6; 25:4-5; 32:1-2
5. “**kivuli cha mbawa**” – Nahau ya Kiebrania ya Mungu kama Ndege mwenye kifaranga – Zab. 17:8; 36:7; 57:1; 61:4; 91:1,4; Isa. 31:5 (sawa na taswira katika Kumb. 32:10-11; Ruth 2:12; Mt. 23:37; Luka 13:34)
6. “**kivuli cha mti**”

- a. mfano wa uhusiano na Abimeleki – Amu. 9:15
- b. mfano wa Tai na Mzabibu – Ezek. 17:23
- c. mfano wa Misri – Ezek. 31:6,17
- d. ndoto ya Nebukadnezza – Dan. 4:12
- e. taswira ya kutekwa Israeli – Hosea 14:7

kivuli kina nguvu, kuokoa - maisha sitiari kwa ajili wa watu wa jangwani.

▣ “**wala hawakuuliza kinywani mwangu**” Hawa watu wa Yuda ni dhahili walitaka shauri kwa mizimu (kama vile. 8:19), lakini sio kwa manabii wa YHWH (Kifashihi. “hakuuliza kinywani mwangu,” kama vile. Kut.4:16; Yosh. 9:14).

**30:3** Hakunatumaini tena katika Misri (kama vilemist. 3,5,7; 20:5-6; 36:6). Cha kushangaza Yuda akamwacha Mungu wao wa agano kwa ajiri ya ulinzi ambaeo Bwana aliwapa hapo kabla! Yuda atafanya hivyo tena Siku za Yeremia (kama vileYer. 2:13; 42:18- 22)!

**30:4 “wajumbe wao”** Toleo la MT lina neno “yake”, ambalo linafuatwa na tafsiri nyingi za Kiingereza. Toleo la NASB labda linatetea kwamba hawa “wajumbe” wanarejerewa Viongozi wa Farao (kama vile . 19:11), lakini katika muktadha inarejelea Wawalikishi wa Hezekia waliokuwa wakita futa ushirikiano wa kisiasa/kijeshi na Misri.

▣ “**Soani. . .Hanesi**” Hii ilikuwa miji miwili ambayo punde ilikimbia toka kwenye utawala wa Ishirini na tano. Ilitumika kuonyesha nguvu za jeshi la Misri.

Miji miwili hii iliyotajwa ina uhusiano na eneo la Mto Nile.

- 1. Soani pia inajulikana kama Tanisiau Avarisi (kama vile. Hes. 13:22; Zab. 78:12,43; Isa. 19:11).
- 2. Hanesi haifahamiki (toleo la LXX limeacha), lakini inawezekana kuna uhusiano na Tahpanhes (kama vile. Yer. 2:16; 43:7,8,9; 44:1; 46:14), Ngome iliyokuweko karibu. Baadhi ya wanazuoni wanasimulia hili jina na Heracleopolis Magna kwasababu ni mji mkuu wa Nyakati za nasaba ya Nubi.

**30:5**

**NASB, NKJV**     “haya”

**NRSV**           “aibu”

**TEV**             “majuto”

**NJB**             “sikitishwa”

Tafsiri zote hizi za Kiingereza zimechagua chaguo la neno *Qere* (yaani, maelezo ya nyongeza) ya wanazuoni wa Kimasoreti (בְּבֵשׁ BDB 101, KB 116, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, NOMINO [BDB 102] Imetumika baadee kwenye mstari huu). Toleo la MT (*Kethib*) lina kifungu “sababisha harufu mbaya” (הַבָּאֵשׁ, BDB 92, KB 107, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*; KITENZI kimetumika katika 50:2 na NOMINO kwenye 34:3).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:6-17**

<sup>6</sup>Ufunuo juu ya hayawani wa Negebu.

Katikati ya nchi ya taabu na dhiki,

Ambayo hutoka huko simba jike na simba, Nyoka na joka la moto arukaye,

Huchukua malii zao mabegani mwa punda wachanga,

Na hazina zao juu ya nundu za ngamia Waende

kwa watu ambaeo hawatawafaa kitu.

<sup>7</sup>Kwa maana Misri huwasaidia bure, bila faida;

Kwa hiyo nimemwita,

Rahabu aketiye kimya.

<sup>8</sup>Haya, enenda sasa, andika neno hili katika kibao mbele ya macho yao,  
lichore katika kitabu ili liwe  
kwa ajili ya majira yatakayokuja,  
kwa ushuhuda hata milele.

<sup>9</sup>Kwa maana watu hawa ni watu waasi, watoto wasemao uongo,  
watoto wasiotaka kuisikia sheria ya Bwana;

<sup>10</sup>wawaambiao waonaji, Msione;  
na manabii, Msitoe unabii wa mambo ya haki,  
tuambieni maneno laini,  
hubirini maneno yadanganyayo;

<sup>11</sup>tokeni katika njia, geukeni mtoke katika mapito;  
mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu.

<sup>12</sup>Basi kwa ajili ya hayo Mtakatifu wa Israeli asema hivi,  
Kwa sababu mwalidharau neno hili,  
na kutumainia jeuri na ukaidi, na kuyategemea hayo;

<sup>13</sup>basi, uovu huu utakuwa kwenu kama mahali palipobomoka,  
palipo tayari kuanguka patokezapo katika ukuta mrefu,  
ambapo kuvunjika kwake huja ghafula kwa mara moja.

<sup>14</sup>Naye atapavunja kama chombo cha mfinyanzi kivunjwavyo,  
akikivunja-vunja asiache kukivunja,  
hata hakipatikani katika vipande vyake  
kigae kitoshacho kutwaa moto jikoni,  
au kuteka maji kisimani.

<sup>15</sup>Kwa maana Bwana MUNGU, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi,  
Kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa;  
nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini;  
lakini hamkukubali.

<sup>16</sup>Bali ninyi mlisema, La! Maana tutakimbia juu ya farasi;  
basi, ni kweli, mtakimbia;  
tena, Sisi tutakimbia juu ya wanyama waendao upesi;  
basi, wale watakaowafuati watakuwa wepesi.

<sup>17</sup>Elfu moja watakimbia kwa kukemewa na mtu mmoja;  
kwa kukemewa na watano mtakimbia;  
hata mtakapoachwa kama mlingoti juu ya kilele cha mlima,  
na kama bendera juu ya kilima.

**30:6-7** Hii inaelezea msafara wa Yuda uliotumwa kupitia jangwa hatari la Yuda na Misri (yaani .,mst. 6b,c), aina ya zawadi (mst. 6d,e) katika jaribio la kujaribu kuunda muundo wa ushirikiano wa kisiasa na Misri (yaani., Rahabu, BDB 923, tazama muhtasri katika 27:1).

Toleo la NASB Study Bible linatoa hoja kuwa labda msafara huo ulipitia barabara ya kuelekea Misri kwasababu jeshi la Ashuru lilimiliki njia kuu ya msafara (ukr. 997,pia IVP *BibleBackground Commentary*, ukr. 621).

Toleo la NIDOTTE,juzuu. 3,uk. 87, linatoa hoja kuwa labda inawakilisha namna ya kurudi kwao.Lakini nafikilia uchaguzi wa muktadha Namba 1 (yaani ,ushirikiano wa kisiasa) unafaa zaidi. Nimeorodhesha baadhi ya chaguzi za tafsiriili kuelezea kwa mifano.

1. Kwa namna gani shairi la Kiebrania linaweza kuwa tatanishi
2. Ni vidokezo gani tofauti vinawenza kuonekana nyuma ya maneno na tungo
3. Kukazia tena umuhimu wa kutafuta maana kuu ya ubeti na uhusiano wake wa muktadha mkubwa na usiwe na msingi mmoja wa theologia unaoelekeza kuelezea maelezo ya shairi la Kiebrania

**30:6** fahamu “wanyama” (BDB 96) wa Negebu (BDB 616) walijotajwa.

1. Simba jike, BDB 522
2. Simba, BDB 539 I
3. Nyoka, BDB 821
4. Joka arukaye, BDB 977 I kukiwa na *Polel KAULI ENDELEVU* “arukaye” (BDB 733, KB 800), tazama muhtasari katika 14:29
5. Punda, BDB 747
6. Ngamia, BDB 168

Namba 1-4 inaongelea safari ya hatari, ambapo 5-6 inaongelea wanyama wabebao mizigo kwamba walibeba mizigo ya kibashara.

**30:7**

<b>NASB</b>	<b>“Rahabu aketiye kimya”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“Rahabu-Hem-Shebeth” (“Rahabu ameketi ametulia” tanbihi)</b>
<b>NRSV</b>	<b>“Rahabu bado ameketi”</b>
<b>TEV</b>	<b>“Misri nimempa jina, “Joka lisilo na madhara”</b>
<b>NJB</b>	<b>“na nitamuita yeye ‘Rahabu aliye vunjika’”</b>

Toleo la MT lina neno “Rahabu ambaye bado ameketi.” Rahabu inarejelea Misri. Tazama muhtasari kamili katika 51:9). Andiko la Kiebrania la UBS linalipatia Andiko la Kimasoreti la neno “wao (kuwa) wameachwa alama “B” (pasipo mashaka). Kusudi kuu ni kwamba Misri haiwezi kusimama au hata kama itasaidiwa na Ashuru kuivamia Palestina. Joka (Rahabu, BDB 923, KB 1193) hana meno!

**30:8** kuna sababu mbili kwa ajili ya uwekaji wa kumbukumbu (1) Mungu alitaka ushahidi ulioandikwa wa Uasi wa watu wake atakapo waleta katika hukumu, ushahidi uko wazi (kama vile. 8:1; Hab. 2:2) na (2) kuonyesha anavyoitawala historia, hivyo kujithibitisha Yeye Mwenyewe na manabii wake kwamba vizazi vinavyofutia labda wataamini neno lake.

Kuna Amri nyingi katika Aya hii.

1. enenda, BDB 97, KB 112, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. Andika , BDB 507, KB 503, *Qal KAULI SHURUTISHI*
3. lichore, BDB 349, KB 347, *Qal KAULI SHURUTISHI*
4. uwe ushuhuda hata milele, BDB 224, KB 243, *Qal KITENZI AMRISHI*

Toleo la MT lina neno “shahidi” (BDB 723 I), “milele” (BDB 761, kama viletoleo la NKJV, NJB, LXX, Peshitta), lakini asili ,<sup>תְּעִ</sup>, kwa kawaida lina maana ya “kudumu” (yaani., “kipengele cha muda” sambamba na ‘olam). Mara kwa mara inawezekana tafsiri za Kiingereza hazina ishara za kutosha za maneno mbalimbali ya Kiebrania. Ndiyo maana kulinganisha natafsiri za Kiingereza kunasaidia.

**30:9 “Kwa maana watu hawa ni watu waasi,**

**watoto wasemao uongo,**

**watoto wasiotaka kuisikia sheria ya Bwana”**

Angalia mst. 1; 1:2-3; 6:9-10; 29:9-12.

KITENZI “kuisikia” (BDB 1033, KB 1570, *Qal TUNGO YA KITENZIJINA HALISI*) kinaelezea “kutenda kama ulivyosikia” (yaani ,Kumb. 4:1; 6:4). Dhana hii ya mwitikio wa mtindo wa maisha kwenye ufunuo wa kiroho ni kiini cha imani ya Agano la Kale( kama vile Kumb. 29:4). Kama Aya hii inavyoonyesha wazi, Utiini tatizo linalojirudia kwa ajiri ya anguko la mwanadamu. Udhafiu wa Agano la kale sio ufunuo wake, bali ni wahusika wa agano la mwanadamu(kama vile Galatia 3). Hapa linahitajika “Agano jipya” (kama vileYer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38). Agano jipya,kama lile la kwanza, lilifanywa ili kujenga ushirika kati ya Mungu na Mwanadamu na kuifunua tabia ya Mungu kwa ulimwengu ulioanguka. Utiifu ni jambo la muhimu sana kwa wote (kama vile Mt. 11:29; Luka 6:46).

**30:10-11** Watu wa Yuda sio tu kwamba hawakutaka kumfuata YHWH, hawakutakata hata kusikia kutoka kwa wajumbe wake!

1. Kwa waonaji, msione,
  - a. waonaji, BDB 906, KB 1157, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*
  - b. msione, BDB 906, KB 1157, kanusha *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
2. Kwa manabii, msitoe unabii
  - a. manabii, BDB 302
  - b. msitoe unabii, BDB 302, KB 301, kanusha *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
3. Tuambieni maneno laini, BDB 180, KB 210, *Piel KAULI SHURUTISHI*
4. Hubirini maneno yadanganyayo, BDB 302, KB 301, *Qal KAULI SHURUTISHI*. "madanganyo" (BDB 1122) kunapatikana hapa pekee. Walihitaji ujumbe wowote lakini hasa ujumbe wa YHWH!
5. Tokeni katika njia (kifasihi. "geukeni mtoke katika mapito"), BDB 693, KB 747, *Qal KAULI SHURUTISHI*
6. Geukeni mtoke katika mapito, BDB 639, KB 692, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*
7. Komesheni mtakatifu walsraeli mbele yetu (Kifasihi. "mwondoe mbele zetu"), BDB 991, KB 1407, *Hiphil KAULI SHURUTISHI*

Haya ni maelezo ya kutisha. Isaya alitumia maonyo kwa nguvu ili kufanikisha mtizamo wake. Watu hawa ni kwa jina la YHWH pekee!

**30:10 "waonaji"** Neno hili (BDB 909) ni wazi linasimulia KITENZI cha kawaida cha neno "kuona" (BDB 906).

## MADA MAALUM: MANENO TOFAUTI YA KIEBRANIA KWA AJILI YA NABII

Maneno ya Kibiblia

1. *ro'eh* = "mwonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Sam. 9:9. Hii rejea inaonyesha kubadilika kwenda neno *nabi*, ambalo lina maanisha "nabii" na linatokana na asili, "kuita". *Ro'eh* ni kutoka jumla ya neno la Kiebrania "kuona". Mtu huyu anafahamu njia za Mungu na Mipango na Mshauri wa Mungu kuhakikisha Mapenzi yake yanafuatwa.
2. *hozeh* = "mwonaji" (BDB 302, KB 301), 2 Sam. 24:11; Amosi 7:12. Kimsingi ni kisawe cha *ro'eh*. Linatoka kwenye neno zuri la Kiebrania "kuona maono". KAULI ENDELEVU hii ni muundo ulitumika mara nydingi kurejelea manabii.
3. *nabi'* = "nabii" (BDB 611, KB 661), KITENZI *nabu*=hiki chenye asili moja ya Akkadian "kuita" na kwa Kiarabu *naba'a* = "tangaza." Hili ni neno la kawaida kwenye Agano la kale la kumdhahirisha nabii. Limetumiwa zaidi ya mara 300. Kwa kweli elimu ya asili na historia ya maneno haijulikani, lakini "kuita" kwa wakati huu inaonekana ni chaguo bora zaidi. Inawezekana ufahamu bora zaidi unatokana na maelezo ya YHWH kwa Musa juu ya mahusiano na Farao kupitia kwa Haruni (kama vile Kut. 4:10-16; 7:1; Kumb. 5:5). Nabii ni mtu yule anaeongea na Mungu kwa ajili ya watu wake (kama vile Amosi 3:8; Yer. 1:7,17; Ezek. 3:4).
4. Maneno yote matatu yametumika katika sehemu ya kazi ya nabii kwenye 1 Nya. 29:29; Samueli – *Ro'eh*; Nathani – *Nabi'*; na Gadi – *Hozehe*.
5. Tungo hii *'ish ha – 'elohim*, "mtu wa Mungu," na pia kwa ujumla ni jina kwa ajiri ya anaeongea kwa ajili ya Mungu. Baadhi imetumika mara 76 katika Agano la kale kwa maana ya "nabii".
6. Katika Agano jipya neno "nabii" lina asili ya Ugiriki. linatokana na
  - a. *pro*, linalomaanisha "kabla" au "kwa ajili"
  - b. *phemi*, linalomaanisha "kuongea."

**30:12 "na kutumainia"** KITENZI hiki (BDB 105, KB 120, *Qal KAULI WAKATI USIO TIMILIFU*) kimetumika mara kwa mara katika Isaya.

1. Kumwamini Mungu, kama vile. 12:2; 26:3,4; 36:7,15; 37:10; 50:10 (kwa jina la BWANA)
2. Kuamini katika vitu
  - a. 30:12, ukandamizaji na hila
  - b. 31:1, jeshi la Misri

- c. 36:6,9, Misri
  - d.42:17, Sanamu
  - e. 47:10, Uovu
  - f. 59:4, ghasia
3. Kumwamini mtu, 36:5,6,9

▣ “**kutumaini**” KITENZI hiki (BDB 1043, KB 1612, *Niphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kinafanana na neno “kuamini” (kama vile. 2 Nya. 13:18;14:11; 16:7,8). Kinapatikana hapa pekee katika shina la neno *Niphil* na kimetumika mara kwa mara katika Isaya (kama vile. 10:20 [mara mbili]; 31:1; 50:10). Kwa kawaida kinamaanisha “kutegemea” au “kumtegemea” (kama vileMwa. 18:4).

**30:13-14** Hizi sitiari mbili zimetumika kwa ajili ya maangamizi yajayo: (1) anguko la wazi la ukuta na (2) kuvunjika kabisa kwa chombo cha mfinyanzi.

**30:15** Fahamu majina ya Mungu wa Yuda.

- 1. Adonai YHWH (Bwana Mungu)
- 2. Mtakatifu wa Israeli, kama vileMistr. 11,12

Hiki ni Cheo cha maagano! (Angalia Mada Maalum katika 1:1.) Hii itakuwa kwa watu wa maagano!

▣ “**Kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa**” Ayaya 15-17 inaelezea majibu mawili ya ahadi za Mungu. Aya ya 15 inaelezea Imani ya kweli (kama vileZab. 118:6-9), ambapo mistari ya 16-17 inaelezea Imani ya uongo. Wokovu (BDB 446, KB 448, *Niphil KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) unaelezewa na NOMINO mbili.

- 1. Kurudi (Kifasihi. “kurudi nyuma”), BDB 1000, KB 1435; hili ni neno adimu linalopatikana hapa pekee. baadhi ya wanazuoni wanadokeza kuwa na uhusiano na Mika 2:8, lakinihili halijulikani. Msingi asilia wa neno, שׁוּב, unamaanisha “kurudi” na linafaa katika muktadha.
- 2. kustarehe, BDB 629 I, KB 692 II, linamaanisha “utulivu,” “uvumilivu,” “amani”
  - a. Ayub 17:16; Mhu. 6:5, kustarehe katika kifo
  - b. Mit. 29:9, hakuna kustarehe kwa ajiri ya mpumbavu
  - c. Isa. 30:15, inawezekana kustarehe kutoka katika vita, msingi wake unafanana na Mika 2:8, Namba 1 hapo juu.

Uinjilisti ndani yangu unataka kubadili maneno haya muhimu “kuokolewa” “kurudi” na “kustarehe”, kwenda ujumbe wa Injili, lakini hili sio Agano jipya! Huu ni ubeti juu ya Yuda akitafuta ushirikiano wa kijeshi na Misri. Amegeukia mbali na Mungu wake na hajastarehe ndani yake (kama vile. 15d).

▣ “**nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini**” Mstari huu unafanana na mstari hapo juu, hivyo kuna maneno manne YHWH ametumia kuwaelezea wao.

- 1. kurudi, angalia hapo juu
- 2. kustarehe, angalia hapo juu
- 3. kutulia, BDB 1052, KB 1641, *Hiphil KITENZIJINA HALISI*, kama vile. 7:4; 32:17
- 4. kutumaini, BDB 105, kama vile. 32:17

Kumbuka huu ni mfanano wa kithiolojia wa wito wa Isaya kwa ajili ya ahazi “kuwa mwangalifu, tulia, usiwe na hofu na usiwe na woga” katika 7:4. Na sasa YHWH anamwelezea Hezekiakwa ujumbe unaofanana! Nitumaini mimi!

**30:16 “basi, wale watakaowafuatia watakuwa wepesi”** Yuda walikuwa wakiamini kwenye uwezo wa kijeshi walioupanga kuupata toka Misri(kama vile. 2:6-7; 31:1). Hata hivyo,kama alivyowatumainia wepesi wa kikosi cha kukodi cha magari ya farasi, Mungu anatangaza wepesi wa jeshi mbadala la Ashuru.

**30:17 “Elfu moja watakimbia kwa kukemewa na mtu mmoja”** Huu ni msamiati wa vita takatifu (kama vile Law. 26:8; Kumb. 32:30; Yoshua. 23:10). Umechukuliwa toka katika kitabu cha Kutoka na ushindi waPalestina. Hata hivyo, mambo yamebadilika na Mungu yuko upande wa Ashuru.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 30:18**

<sup>18</sup>Kwa ajili ya hayo Bwana atangoja,  
ili awaonee huruma, na kwa ajili ya hayo atatukuzwa,  
ili awarehemu; kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu;  
heri wote wamngojao

**30:18 “Kwa ajili ya hayo Bwana atangoja, ili awaonee huruma”** Aya hii ni ya ajabu sana (na ya kuogofya inayoturudisha nyuma) kwamba inafunua tabia ya YHWH.

1. Atangoja ili awaonee huruma
  - a. atangoja (Kifasihi. “kungoja”), BDB 314, KB 313, *Piel KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
  - b. huruma, BDB 335, KB 334, *Qal TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*
2. Wamngojao ili awaonee huruma
  - a. wamngojao (Kifasihi. “yuko juu”), BDB 926, KB 1202, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
  - b. huruma, BDB 933, KB 1216, *Piel TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*

Mwanadamu ni lazima atumaini katika tabia ya Mungu. Anatamani kubariki (BDB 80) wale wote wamngojao (Kifasihi. “wamngojao,” KITENZI sawa kama namba 1 hapo juu, lakini hapa *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*, kama vile. 25:9; 26:8; 33:2; Zab. 33:20) kwa ajili yake.

Hivyo “kungoja” huku kunaelezea kutumaini, utulivu wa mtazamo wa dunia juu ya uwepo wa YHWH, Ahadi, na makusudi (kama vile. 48:9-11; Hos. 11:8-11), hata wakati wa machafuko na mashaka.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 30:19-22**

<sup>19</sup>Kwa maana watu watakaa katika Sayuni huko Yerusalem; wewe hutalia tena; hakika yake atakuonea rehema nyingi kwa sauti ya kilio chako; asikiapo ndipo atakapokujibu. <sup>20</sup>Na ingawa Bwana atawapeni chakula cha shida na maji ya msiba, lakini waalimu wako hawatafichwa tena, ila macho yako yatawaona waalimu wako;

<sup>21</sup>na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto. <sup>22</sup>Nanyi mtakitia najisi kifuniko cha sanamu zenu za fedha zilizochongwa, na mabamba ya sanamu zenu za dhahabu zilizoyeyushwa; utazitupilia mbali kama kitu kilicho najisi; utasema, Haya, toka hapa.

**30:19-22** Tambua kile ambacho YHWH atafanya katika Yuda kwa kutubu na kuwa waaminifu siku zijazo.

1. Hawatalia tena – huu ni mkazo wa *Qal KITENZI JINA HALISI* na *Qal KITENZI CHA KAULI ISIO TIMILIFU* cha asili moja (BDB 113, KB 129). Siku hii mpya pia inatajwa katika 25:8; 60:20; 61:1-3.
2. Hakika atakuonea rehema – hii inafanya kutilia mkazo kwa kutumia *Qal KITENZI JINA HALISI* na *Qal KITENZI CHA KAULI ISIO TIMILIFU* cha asili moja (BDB 335, KB 334; tazama muhtasari katika mst. 18).
3. Asikiapo sauti ya kilio chao – BDB 1033, KB 1570, *Qal TUNGO YA KITENZI JINA HALISI*.
4. Ndipo atakapokujibu – BDB 772, KB 851, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile. 58:9; 65:24 (yaani, agano lina nguvu na ni imara)
5. Hatajificha tena – BDB 489, KB 486, *Niphah KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*. Hili ni neno adimu lilnalopatikana hapa pekee. Kwa kawaida lina maanisha “sukumia kwenye kona” (NKJV). Toleo la NASBLina neno “ficha” kutoka asili ya kiarabu, “kuzunguka” au “kulinda.”
6. Macho yako yatawaona waalimu wako – BDB 906, KB 1157, *Qal KAULI TENDAJI ENDELEVU*.
7. Masikio yako yatasikia neno nyuma yako – BDB 1033, KB 1570, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*. Hii ni kurudishwa nyuma katika 6:9-10 na nafasi yake katika Kumb. 29:4. Hili “neno” (BDB 182) ambalo watalisikia ni kituo cha aya, ambalo ni sitiari ya mtindo wa maisha ya imani.
  - a. njia, BDB 202 (yaani maagano hai, kama vile 35:8-9; 42:16; Zab. 25:8-9)
  - b. ifuate, BDB 229, KB 246, *Qal KAULI SHURUTISHI* (kama vile. Law. 26:3; Kumb. 8:6; 10:12; 11:22);

28:9; 1 Fal. 6:12; 8:36,61; 2 Nya. 6:16,27; Neh. 10:29; Isa. 2:3; Yer. 6:16; 44:10,23;  
Ezek. 5:6-7; 11:20; 18:17; 20:13,16,19,21; 33:15; 37:24; Dan. 9:10; Mika 4:2  
c. mgeukapo mkono wa kulia au mkono wa kushoto (ni nahau nyingine inayosimulia kubaki katika njia)

8. Utazitupilia mbali sanamu zako
  - a. mtakitia najisi, BDB 379, KB 375, *Piel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
  - b. Utazitupilia mbali, BDB 279, KB 280, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
  - c. utasema haya "toka hapa" BDB 422, KB 425, *Qal KAULI SHURUTISHI*

Isaya alikuwa na ufumbuzi wa pekee wa kutetea kwamba Yerusalemukamwe haiwezi kuangamizwa, lakini Yeremia anadai kwamba itaangamizwa. Wote kwa pamoja wanadai kwamba itarejeshwa kama tu watageuka na kumrudia YHWH!

### 30:20 katika Aya hii kuna watu wengi wametajwa.

1. "BWANA" – Adonai
2. "waalimu wako" (mara mbili)
3. "wewe" (yaani, Wayuda, WINGI)  
Huyu "mwalimu" anaweza kurejelea
  1. YHWH (WINGI WA UKUU, toleo la TEV, kama vile. 45:15, "wewe ni Mungu unayejficha," lakini KITENZI tofauti)
  2. Masihi (mwakilishi wa YHWH)
  3. Manabii/makuhani (yaani, urejesho wa ufunuo mpya, kama vile. Zab. 74:9)  
Neno "mwalimu" (מָלִיכְךָ בְּדֶבֶר BDB 435) inafahamika kama
    1. UMOJA, John J. Owens, *Analytical Key to the OT*, juzu 4, ukr. 90, tazama toleo la NASB, JPSOA, NRSV, ASV
    2. WINGI, Benjamin Davidson, *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon*, ukr. 475, tazama toleo la NKJV, REB

Muundo unaweza kuakisi mojawapo (NIDOTTE, juzu 2, ukr. 538).

### 30:22

NASB	"kitu najisi"
NKJV	"kitu kichafu"
NRSV	"kama kitambaa najisi"
NJB	"kama vitu vilivyochafuka"
Peshitta	"majji machafu kama hedhi ya mwanamke"

Hili nineno (BDB 188) ambalo linaonyesha vitambaa vilivyotumika wakati wa kipindi cha hedhi ya mwanamke (kama vile. Law. 15:33; 20:18). Hii inaweza kuwa ni nahau ya kufuata utatibu wa kiibada wa tamaduni imara ambapo kitu kilichoonekana kuwa najisi kiwekwe mbali (kama vile. 64:6).

Toleola LXX (REB) linachukua neno lifuatalo "amekwisha kwenda" (BDB 422, KB 425) kama neno linalofanana, "kinyesi," ambalo linaweza kuwa ni nahau nyingine ya utamaduni ya kuchafua utaratibu maalum na hasa wa kiibada.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 30:23-26

<sup>23</sup> Naye atatoa mvua juu ya mbegu zako, upate kuipanda nchi hii; na mkate wa mazao ya nchi, nayo itasitawi na kuzaa tele; katika siku hiyo ng'ombe zako watakula katika malisho mapana. <sup>24</sup> Ng'ombe pia na wana-punda wailimao nchi watakula chakula kilichokolea, kilichopepetwa kwa ungo na kwa pepeo. <sup>25</sup> Na juu ya kila mlima mrefu, na juu ya kila kilima kilichoinuka, itakuwapo mito na vijito vya maji, katika siku ya machinjo makuu itakapoanguka minara. <sup>26</sup> Na tena nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itaongezeka mara saba, kama nuru ya siku saba, katika siku ile Bwana atakapofunga mapigo ya watu wake, na kuliponya pigo la jeraha yao.

**30:23-26** Hii inaelezea Baraka za kilimo na ufgaji ambazo ziliahidiwa kwa uzao wa Ibrahimu kama watatembea katika Agano la YHWH (kama vile. Law 26 na Kumb 27-28).

1. Mvua kwa majira yake, mstr. 23,25, kama vile. 35:6,7; 41:18; 43:19,20
2. Mazao bora ,mstr. 23
  - a. yatastawi (BDB 206)
  - b. kuzaa tele (BDB 1032)
3. Malisho kwa ajiri ya wanyama, mst. 23, kama vile. 32:20
4. Chakula kwa ajiri ya wanyama wailimao nchi, mstr. 24 (neno BDB 330 linapatikana hapa pekee)
5. Kupigwa kwa maadui, mstr. 25 ("juu ya kila mlima." Hii ni sawa na Nahau iliyotumika kwa waabudu *Ba'al* katika Hosea)
6. Wingi wa nuru kwa ajili ya Afya na usitawi, mst. 26, kama vile. 60:20-21 (saba ni ishara ya ukamilifu na Nuru ni ishara ya uwepo wa Mungu, yaani ., jina lake, mstr. 27)

**30:26** Baraka hizi za urejesho (kama vile 11:6-9; Rum. 8:18-22) ni baada ya

1. Siku ya machinjo makuu itakapoanguka minara, mst. 25
2. Siku ile Bwana atakapofunga mapigo ya watu wake, mst. 26
3. Siku ile Bwana atakapoponya pigo la jeraha yao, mst. 26

■“kuliponya pigo la jeraha yao” Tingo hii na nydinge kama hii (yaani., Kumb. 32:39; 1 Sam 2:6; 2 Fal. 5:7; Ayubu 5:18; Isa. 45:7; Yer. 1:10; 24:6; 31:28; Hos. 6:1; Amosi 3:6) imesababisha siku hizi kuuliza tabia na rehema ya Mungu. Hizi zote ni njia za nahau wanazotetea waamini wa Mungu mmoja (yaani.,mmoja na peke yake anasababisha). Watu wa sasa wa magharibi wana uhakika kwamba kuna visababishi vingi sana kwenye uzoefu wao na historia zao. Biblia inatetea utawala wa Mungu katika maeneo yote katika uhalisia. Mungu yupo na ni mtendaji!

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 30:27-33

- <sup>27</sup>Tazama, jina la Bwana linakuja kutoka mbali sana,  
linawaka kwa hasira yake, kwa moshi mwangi sana unaopaa juu;  
midomo yake imejaa ghadhabu,  
na ulimi wake ni moto ulao;
- <sup>28</sup>na pumzi yake ni kijito kifurikacho,  
kifikacho hata shingoni,  
kupepete mataifa kwa ungo wa ubatili;  
na lijamu ikoseshayo itakuwa katika taya za watu.
- <sup>29</sup>Mtakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku, ishikwapo sikukuu takatifu,  
mtakuwa na furaha ya moyo kama vile mtu aendapo na filimbi katika  
mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli.
- <sup>30</sup>Naye Bwana atawasikizisha watu sauti yake ya utukufu,  
naye atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira yake,  
na mwako wa moto ulao,  
pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu.
- <sup>31</sup>Maana kwa sauti ya Bwana, Mwashuri atavunjika-vunjika,  
yeye apigaye kwa bakora.
- <sup>32</sup>Na kila pigo la fimbo ilioamriwa,  
ambayo Bwana ataliweka juu yake,  
litakuwa pamoja na matari na vinanda,  
na kwa mapigano yenye kutikisa atapigana nao.
- <sup>33</sup>Maana Tofethi imewekwa tayari tokea zamani,  
naam, imewekwa tayari kwa mfalme huyo;  
ameifanya kubwa, inakwenda chini sana;  
tanuru yake ni moto na kuni nyingi;

**pumzi ya Bwana, kama mto wa kiberiti, huiwasha.**

**30:27-33** Ubei huu unaakisi hukumu ya Mungu juu ya Ashuru katika nahau ya Mungu kudhihilika katika mwili kama kimbunga kinachokaribia (kama vile. Kut. 19:16na kuendelea; Amu. 5:4-5; Zab. 18:7na kuendelea; 50:3-5; Hab. 3:3-4).

1. Msingi wa Tofethi –mist. 27, 30a-c, 33e
2. Msingi wa dhoruba –mist. 28, 30d
3. Msingi wa urejesho – mst. 29
4. Msingi wa hukumu – Ashuru, mistr. 31-33

**30:27**

<b>NASB</b>	<b>“moshi mwingi”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“mzigo wake ni mzito”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“katika midomo yake unafuka moshi”</b>
<b>NJB</b>	<b>“utisho wake mkuu”</b>

toleo la MT lina כבד, BDB 457, KB 451, MUUNDO WA MANENO BDB 673, “kufuka moshi.” Neno la kwanza linaweza kumaanisha

1. Uzito
2. ukubwa
3. mzigo
4. heshima

Neno la pili (שׁאַהֲנָה, BDB 673, KB 640) linapatikana hapa pekee kwenye Agano la kale . Toleo la BDB linasema neno linamaanisha “lililoinuliwa” (wingu). Toleo la KB inasema neno linamaanisha “kuinuliwa juu,” lakini pia linatajwa katika Amu. 20:38-40 kama mfanano ambapo משאת, mst. 38, linadokeza kufuka moshi kutoka katika mji unaoungua. Muktadha wa 30:27 ni moja ya udhihilisho Mungu katika mwili na hukumu, hivyo yote yanafaa.

1. Furaha , inadokeza wingu (yaani., *Shekinah*)
2. Moshi mwingi

**30:28 “kifikacho hata shingoni”** hiini sawa na Nahau iliyotumika kwenye uvamizi wa Ashuru katika 8:8. Hapa Nahau imegeuzwana YHWH anapigana upande wa Yuda dhidi ya Ashuru.

**30:29 “mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli.”** Hizi niNahau kwa ajiri ya hekalu huko Yerusalem kwa sababu ya dhana ya kufanana. Mara kwa mara neno “mwamba” linarejelea kwa YHWH peke yake (kama vile. 17:10; Kumb.32:4,18,30; 1 Sam. 2:2; Zab. 18:2,31,46; 28:1; 31:3; 42:9).

**30:30 “sauti yake”** kwamaana ilio wazi, neno linamaanisha “ukuu wa (BDB 217) sauti yake.” Mapenzi ya Mungu yatakamilishwa kwa kuongea (yaani ., uumbaji, Mwanzo 1). Sauti yake inaathiri (kama vile Isa. 45:23; 55:11; Mt. 24:35).Taswira ya Yesu yenye upanga ukatakao kuwili (kama vile. Ebr. 4:12) utokao kinywani mwake (kama vile. Isa. 49:2; Ufu. 1:16; 2:12,16; 19:15) ni ufanano wa kithiolojia, kama ilivyo “fimbo ya kinywa chake” katika Isa. 11:4.

▣**“mawe ya barafu”** Mungu aliyatumia katika Yosh. 10:11 kama njia ya kuwapiga Wakanaani na kuwapatia ushindi Israeli (kama vileYosh. 10:14,42; 23:3,10).

**30:31**

<b>NASB, TEV,</b>	
<b>NJB</b>	<b>“ataogopeshwa”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“ataangushwa chini”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“ataingwa na huzuni kuu”</b>

KITENZI hiki (BDB 369, KB 365, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kwa maana iliyo wazi kinamaanisha “kuharibiwa,” kikionesha ushindi kamili katika vita kunakotanguliwa na hofu iliyowadhoofisha na maangamizi yajayo (kama vile. 7:8; 8:9 [mara mbili]; 9:4; 20:5; 30:31; 31:4,9; 37:27; 51:6,7). YHWH anapigana upande wa watu wake dhidi ya Ashuru. Hofu na mashaka na kupoteza matumaini kwa Israeli na Yuda ndiyo sasa kunapitiwa na Ashuru (fimbo ya hasira ya YHWH, kama vile. 10:5).

▣“**apigaye kwa bakora**” katika Isaya 10:5, Waashuru waliita “fimbo ya hasira ya Mungu” lakini hapamsingi wake umerudishwa nyuma na Mungu amewarudia watu wake .

**30:32** Hukumu ya Bwana inaelezewa kwa Nahau ya kupiga kwa fimbo. Inawezekana kwamba mistari miwili inayofuatia (mst. 32c,d) inaonyesha kwa picha

1. Pigo linatolewa katika mdundo wa muziki wa furaha
2. Kwamba Yuda anafurahia baada ya Ashuru kuangamizwa naYHWH (kama vile. mst. 32d).

**30:33 “Tofethi”** Hilini neno la Kiebrania kwa ajili ya “tanuru ya moto” (BDB 1075). Mara nyingi limetumika katika kuhusisha nawale wenyewe kuabudu mungu Molech. Hapa katika muktadha inaweza kudokeza

1. Sehemu ya kuteketezea sadaka kwa YHWH palipoandaliwa na Mfalme kwa watu wake waliorejeshwa
2. Sehemu aliyoandaa YHWH kwa ajiri ya mazishi ya mfalme wa Ashuru (kama vile. 31:9)
3. “mfalme” anaye rejelewa kwa *Molech*, mungu ndege atoaye moto (kama vile Law. 18:21)

Katika muktadha Namba 2 unafaa zaidi.

# ISAYA 31

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Msaada haukutoka Misri bali kwa Mungu	Upuuzi wa kutokumwamini Mungu	Dhidi ya Misri	Mungu atailinda Yerusalem	Dhidi ya ushirikiano na Wamisri
31:1-3 (1-3)	31:1-3 (1-3)	31:1-3 (1-3)	31:1-3	31:1-3 (1-3)
	Mungu ataiokoa Yerusalem		Dhidi ya Senakeribu	Dhidi ya Ashuru
31:4-5 (4-5)	312:4-5 (4-5)	31:4-9 (4-5)	31:4-5	31:4-9 (4-9)
31:6-9 (6-9)	31:6-9 (6-9)		31:6-9	

## **MZUNGUKO WA TATU WAUSOMAJI (angalia ukur. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Sura za 31-32 ni sehemu ya fasihi inayoshughulika na matukio ya kihistoria yaliyo sawa 29:15-30:33. Hezekia alijaribu kutafuta ushirikiano na Misri ili kujilinda wao wenyewe na fujo za Waashuru, lakini mnamo mwaka wa 701 K.K Senakeribu akaivamia Yuda na kuangamiza miji 46 yenye boma, ingawa Yerusalem yenyewe iliachwa.
- B. The Anchor Bible ina jedwali lenye kufurahisha ambalo linaonyesha tabia za kinabii zenye kwenda mbele na nyuma kati ya hukumu na tumaini(uk. 426).

<b>vitisho</b>	<b>Ahadı</b>
28:14-15	28:16-17
29:1-4	29:5-8
29:15-16	29:17-21

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 31:1-3

<sup>1</sup> Ole wao watelemkao kwenda Misri wapate msaada, na kutegemea farasi; watumainio magari kwa kuwa ni mengi, na wapanda farasi kwa kuwa ni hodari sana; lakini hawamwangalii Mtakatifu wa Israeli, wala hawamtafuti Bwana! <sup>2</sup>Lakini ye ye naye ana akili, naye ataleta uovu, wala hatayatangua maneno yake; bali ataondoka juu ya nyumba yao watendao mabaya, na juu ya msaada wa hao watendao maovu. <sup>3</sup>Basi Wamisri ni wanadamu wala si Mungu, na farasi zao ni nyama wala si roho; na Bwana atakaponyosha mkono wake, ye ye asaidiaye atajikwaa, na ye ye asaidiwaye ataanguka, nao wote pamoja watakoma.

**31:1 “Ole”** Hii ni ya hamsini katika mfululizo wa “ole” ambazo zinaanzia katika 28:1; 29:1,15; 30:1; 31:1; 33:1. Neno linaanzisha kipimo cha mashairi ya uombolezaji wa kwenye msiba. Angalia muhtasari katika 5:8.

▣“wateremkao kwenda Misri wapate msaada” Watu wa Mungu walikuwa wakijaribiwa kwenye imani (BDB 105, KB 120, angalia Mada Maalum katika 22:23) katika ushirikiano wa kisiasa badala ya nguvu, uwepo na ahadi za YHWH kwa ajili ya msaada wao (kama vilesura ya 28-34).

▣“farasi. . .magari. . .na wapanda farasi” Waashuru walijulikana kutokana na kuwa na kikosi kikubwa cha askari wa farasi. Misri ilijulikana kwa ajili ya vikosi vyao vya magari ya kukokotwa. Yuda ilikuwa ikiwaogopa Waashuru na walikuwa wakiiamini Misri badala ya Mungu. Mwanadamu wa lika lote lazima awe mwangalifu katika kuamini hatua iliyopo ya teknolojia badala ya Mungu aliye waumba na rehema.

▣“magari” Misri iliwaazia nchi majirani zake magari ya kukokotwa (kama vile I Fal. 10:29), lakini yangeweza kufanikiwa tu kwenye eneo tambarare, na sio nchi ya milima kama Yuda.

▣“Mtakatifu wa Israeli” Haya maneno mawili yanatumika kwa Mungu wa agano (kama vile 1:4). La kwanza linarejerea kwenye asili yake kama mwenye haki, lakini bado akiwaita wanadamu wenye dhambi kuwa wana wake. Neno la pili ni jina la agano la Mungu, “YHWH” (kama vile Kut. 3:14). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:1.

▣“hawamwangalii. . .hawamtafuti” VITENZI vyote ni vyenye KUKANUSHAQal KITENZI KILICHO TIMILIFUambacho kinaonyesha hali ya utulivu .

1. tazama (kifasihi “kuangalia kwa uangalifu”), BDB 1043, KB 1609, kama vile 17:7,8
2. tafuteni, BDB 205, KB 233, kama vile 9:13; 55:6; 58:2; 65:10

VITENZI vinaonyesha kipengele binafsi chenyе nguvu (kama vile Dan. 9:13).

**31:2 “naye ana akili, naye ataleta ukaribisho”** Toleo la NET Bible inalionia hili kama hoja yenye kejeli kuhusu washauri wa Yuda ambao wanatafuta msaada toka Misri. Hata hivyo, aya nzima, sio tu ile mistari miwili ya mwisho, inazungumza juu ya YHWH.

▣“wala hatayatangua maneno yake” Wakati Mungu akiongea, maneno yake yanaweza kutumainiwa kwayo (kama vile Isa. 45:23; 55:11; Yer. 44:29).

▣“ataondoka” KITENZI hiki (BDB 877, KB 1086, Qal CHA WAKATI TIMILIFU) kinatumika kwa namna ya lugha ya kibinadamu kumuhusu YHWH akiinuka toka katika kitie chake cha enzi ili kupigana kwa ajili ya watu wake (kama vile 14:22) au dhidi ya watu wake (kama vile Amos7:9). Angalia Mada Maalum: Lugha ya mwanadamu iliyyotumika

kumwelezea Mungu katika 6:1.

▣ “nyumba yao watendao mabaya . . juu ya hao watendao uovu” Hivi vifungu viwili vinarejerea kwa Yuda (yaani., “yeye asaidiwaye,” mst. 3e) na ushirikiano wake wa kisiasa (yaani., Misri, “yeye amsaidiaye,” mst. 3d).

**31:3** Huu ni ulinganisho kati ya udhaifu wa mwanadamu na umilele wa Mungu (*EI*). Hasa hapa unaweza kurejerea kwenye Kut. 14:26-31a. Pia aya hii kwa uwazi inamtofautisha Mungu (*EI*) na mwili. Mungu ni “roho” (kama vile Yn 4:24). Anaweza kuchukua umbo la kibinadamu (kufanyika mwili), lakini Yeye ni roho na anaishi tokea uumbaji wake wote (kama vile I Fal. 8:27; Yer. 23:24). Huchagua kuwa na ushirika na mwamini mnyenyekevu, mwenye kutubu (yaani., Isa. 66:1-2).

▣ “na Bwana ataunyosha mkono wake” Hii ni lahaja ya lugha ya kibinadamu kuyaelezea matendo ya Mungu. Angalia Mada Maalumu katika 6:1.

▣ “yeye asaidiwaye ataanguka” KITENZI hiki (BDB 477, KB 476, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU*) chenye kuonyesha utimilifu wa jambo na mwisho wake (kama vile 1:28; 16:4; 29:20). Kile chenye kuonyesha uwezo na kudumu muda mrefu hakipo! Hiki kinafanana na mithali ya kawaida kuhusu kunyauka kwa mwanadamu kama majani (kama vile Isa. 40:6-8; Zab. 90:5-6; 103:15; 104:14; Yakobo 1:10-11; I Pet. 1:24)

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:45

<sup>4</sup>Maana Bwana aniambia hivi, Kama vile ilivyo simba angurumapo na mwana-simba juu ya mawindo yake, wachungaji wengi wakiitwa ili kumpiga, lakini hatiwi hofu na sauti zao, wala kufanya woga kwa sababu ya mshindo wao; <sup>5</sup>ndivyo Bwana wa majeshi atakavyoshuka ili kufanya vita juu ya mlima Sayuni, na juu ya kilima chake. <sup>5</sup>Kama ndege warukao, Bwana wa majeshi ataulinda Yerusalem; ataulinda na kuuokoa, atapita juu yake na kuuhifadhi.

**31:4 “simba”** Hii stiari inaonekana kumwelezea Mungu kama mwenye uweza na thabiti juu ya mahali pake mwenyewe (yaani., hekalu). Kama ndivyo, ni mbadala wa ubeti wa kwanza (31:1-3).

▣ “Bwana wa majeshi atashuka” KITENZI (BDB 432, KB 434, *Qal KAULI ISIO TIMILIFU*) kinamaanisha “kushuka chini,” “kuja chini,” “kuteremka chini.” Kinatumika mara nyingi kuhusu Mungu kuacha makao yake huko mbinguni na kuja duniani

1. Kuangalia na kupokea matendo ya mwanadamu, Mwa. 11:5,7; 18:21
2. Kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu, Kut. 3:8; 19:11,18,20; Hes. 11:17,25; 12:5 (sehemu mbili maalumu ambapo tabia zake zimeorodheshwa ni Kut. 34:5,6-7; Neh. 9:13,17)
3. Kumwainisha YWWH katika zaburi mbalimbali, II Sam. 22:10; Zab. 18:9; 144:5
4. Kwa ajili ya hukumu, Mika 1:3 (kama #1)

KITENZI hiki ni maalum (yaani., chini), lakini kinakuwa cha kiistiani iwapo kinarejerea kwenye uhusiano kati ya mbingu na nchi (kama vile Mdo. 1:2,9). Yuda ilishuka Misri (mst. 1, KITENZI kile kile), YHWH alishuka kuitetea Yerusalem hata katikati ya kutoamini kwao. Isaya kipekee kabisa anadai uwakfishaji wa mji wa Yerusalem! Hata hivyo, manabii waliokuja baadaye wanagawanyika juu ya msimamo wake juu ya uwezo wa Yuda kutubu na kumwamini YHWH (kama vile Yer. 26:18; Mika 3:11-12; 5:5b-6,7-8).

**31:5 “kama ndege warukao”** Hili linamrejerea Mungu kama mwenye upendo na mwaminifu kama ndege aatamiavyo wanawe (“atawalinda,” BDB 170, KB 199, zote *Hiphil KAULI ISIOTIMILIFU* na *Qal KITENZIJINA HALISI* vya asili ile ile kuonyesha uimalifu). Mara nyingi katika Biblia, Mungu anaelezewa kwa stiari ya jinsi ya kiume (kama vile Mwa. 1:2; Kumb. 32:11; Isa. 40:31; Hos. 11:4; Mt. 23:37; Luka 13:24).

Tambua vile vitu YHWH atafanya kwa ajili ya watu wake katika mst. 5.

1. ataulinda, BDB 170, KB 199 *Hiphil KAULI ISIO TIMILIFU*
2. Ataulinda, BDB 170, KB 199, *Qal KITENZIJINA HALISI*

3. atauokoa, BDB 664, KB 717, *Hiphil KAULI TIMILIFU*
4. Atapita juu yake, BDB 820, KB 947, *Qal KITENZIJINA HALISI*
5. atauhifadhi, BDB 572, KB 589, *Hiphil KAULI TIMILIFU*

▣ “Atapita juu yake” KITENZI hiki (BDB 820, KB 947, *Qal KITENZIJINA HALISI*, kama vile Kut. 12:11-27) kinaurejerea ulinzi wa Mungu dhidi ya maadui wa mwanadamu. Panaonekana kuwepo na dokezo kwenye tukio la pasaka kwenye kitabu cha Kutoka ambapo Mungu, dhidi ya nafasi ya mwanadamu, kuwalinda na kuwaokoa watu wake.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 31:6-9**

<sup>6</sup>Mwelekeeni yeye mliyemwasi sana, enyi wana wa Israeli.<sup>7</sup>Maana katika siku hiyo kila mtu atatupa sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, ambazo mikono yenu imezifanya, zikawa dhambi kwenu.<sup>8</sup> Ndipo huyo Mwashuri ataanguka kwa upanga ambaao si wa mtu; na upanga usio upanga wa mtu utamla; naye ataukimbia upanga, na vijana wake watatoa kodi.<sup>9</sup> Na mwamba wake utatoweka kwa sababu ya hofu, nao wakuu wake wataionea bendera hofu kuu, asema Bwana, ambaye moto wake u katika Sayuni, na tanuru yake katika Yerusalemu.

**31:6 “mwelekeeni Yeye” KITENZIshub** (BDB 996, KB 1427, *Qal KAULI SHURUTISHI*), ambacho kimsingi kinamaanisha “kumgeukia” au “kumrudia.” Chaweza kutumika juu ya

1. Kurudi nyuma, Hes. 14:43; Yosh. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; I Sam. 15:11; I Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. Kumwelekeea Mungu, I Fal. 8:33,48; II Nya. 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yer. 3:7,12,14,22; 4:1; 5:3; Hos. 3:5; 5:4; 6:1; 7:10,16; 11:5; 14:1,2; Amosi 4:6,8,9,10,11 (kumbukumbu hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH mwanzoni akamwambia Isaya kuwa Yuda asingalitubu (kama vile 6:10), lakini sio kwa mara ya kwanza katika kitabu anawaita wapate kumrudia.

Toba sio kitu cha hisia kamaulivyo msukumo wa kumwelekeea Mungu. Ni namna ya kujirudi katika mwelekeo wa maisha toka kwako kumwelekeea Yeye. Inaonyesha utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Sio ukomo kamili wa dhambi, bali hali ya kila siku ya kuacha uasi! Ni lile tatizo la matokeo ya ubinaksi ya anguko la Mwanzo 3. Inaonyesha kuwa sura na mfanano wa Mungu(Mwa. 1:26-27), ingawa imeharibiwa, lakini imerejeshwa! Ushirika na Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka unawezekana tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi ilimaanisha “mabadiliko ya tabia,” wakati “toba” katika Agano Jipyä kimsingi ilimaanisha “badiliko la fikra.” Yote kati ya haya ni ya muhimu kwa ajili toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kuwa toba ni tendo la awali na mchakato endelevu. Kitendo cha awali kinaweza kuonekana katika Mark 1:15; Mdo.3:16 and 19; 20:21, wakati ule mchakato endelevu unaweza kuonekana katika I Yn. 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba sio suala la uchaguzi (kama vile Luka 13:3)! Angalia Mada Maalum: Toba Katika Agano la Kale katika 6:10.

▣ “Yeye mliyemuasi” Hili linazungumzia juu ya uasi wa Yuda dhidi ya YHWH.

1. “kwa ndani,” BDB 770, KB 847, *Hiphil KAULI TIMILIFU*, hili neno lilikuwa likitumika katika 30:33 kuelezea kimbwi la msiba wa mfalme wa Ashuru. Vile vile laweza kuelezea dhambi, kama ilivyofanyika hapa na Hosea 5:2;9:9. Hasa laweza kurejerea kwenye “siri” ya Yuda ya kupanga kupata msaada toka Misri (kama vile 29:15).
2. “kumuasi,” BDB 694, hapa linarejerea uasi, kama vile Kumb. 13:5; Isa. 1:5; 31:6; Yer. 28:16; 29:32

▣ “Enyi wana wa Israeli” Katika Biblia neno “Israeli” laweza kurejerea kwenye vitu vingi: (1) laweza kurejerea kwa mzee wa imani Yakobo na wanawe, (2) laweza kurejerea kwenye makabila kumi ya Kaskazini —pia yaitwayo Samaria na Ephraimu, au (3) laweza kurejerea kwa Yuda. Katika muktadha huu ni #3.

**31:7** Israeliimekuja kuwa huru katika imani yake na kujaribu kuwashirikisha taratibu za ibada za Wakaanani (angalia Mada Maalum katika 17:8) zikiendana na ibada ya YHWH. Hii siku zoteni msiba.

**31:8 “ndipo Mwashuru ataanguka”** Ashuru kilikuwa nichombo cha Mungu kilichotumika kuyahukumu makabila kumi ya Kaskazini (kama vile Isa. 10:5), lakini Mungu atashughulika kwa haki na taifa la miungu ya Ashuru (kama vile 10:12; 14:15; 30:31-33; 37:7). Nineva, mji mku wa Ashuru, ukaangukia kwa Babeli mpya mnamo mwaka wa 612 K.K.

▣**“kwa upanga amba si wa mtu”** Soma sura ya 36 na 37 ya Isaya, ambayo inaelezea uvamizi na kuizingira Yerusalem chini ya Senakeribu. Tambua ukombozi wa kimiujiza wa Mungu (sio kwa upanga wa mtu) katika 37:36.

▣**“watumwa wa kushurutishwa”** Majeshi yaliyookoka kwenye vita

1. Waliwandikisha kama mamluki kwenye jeshi la ushindi
2. Waliuzwa kama watumwa
3. Walitumikishwa kama wapagazi kulitumikia jeshi

Wakazi wengine wote walilazimishwa kuwa watumwa (kama vile Wimb. 1:1). Utumwa ulikuwa ni wa kawaida katika ulimwengu wa kale kwa ajili ya wadaiwa au wale wote walioshindwa vita.

**31:9 “mwamba wake. . .wakuu wake”** Haya yako katika uhusiano wenye kufanana wa Kiebrania, kwa hiyo, neno “mwamba” linarejerea kwa mfalme wa Ashuru (au moja ya miungu wake, kama vile Kumb. 32:31,37) na majemedari wake wa vita (yaani., mwana wa mfalme”) wakaogopeshwa na kiwango cha YHWH (BDB 651, kama vile Isa. 13:2; Yer. 50:2; 51:12,27) juu ya Yerusalem

▣**“ambaye moto wake”** Hili linarejerea, sio kwenye moto ule baada ya hukumu (ingawa yawezekana ni kwenye dokezo la 30:33), wala moto wenye nuru, bali ni mahali pa Mungu penye moto (kama vile “Arieli,” 29:1,2,7, lenye kurejerea Yerusalem).

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani sura ya 31 inahusiana na hali yetu ya sasa ya kulisaidia tukio?
2. Je teknolojia nzuri na utawala mzuri unatuhakikishia ulinzi wa taifa?
3. Kwa nini YHWH aelezewe kwa maneno ya jinsi ya kiume?
4. Elezea toba. Ni kitendo cha kufanya mara moja pasipo kurudia tena au ni tendo endelevu la kila mara? Kimsingi ni muonekano au ni badiliko la matendo?
5. Elezea ni kwa namna gani Ashuru ilianguishwa kwa namna isio ya kibinadamu.

## ISAYA 32

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Nyakati zijazo za Utukufu	Utawala wa haki	Kuja kwa Nyakati za haki	Mfalme Mwaminifu	Mfalme Mwema
32:1-8 (1-8)	32:1-8 (1-4)  (5-8)	32:1-8 (1-8)	32:1-8	32:1-5 (1-5)
			Bahiri na mwadilifu	
	Matokeo ya kuridhika	Dhidi ya wanawake wa Yuda walioridhika	Hukumu na Urejesho	32:6-8 ( 6-8)
				Dhidi ya wanawake wa Yerusalem
32:9-20 (9-20)	32:9-15 (9-11)  (12-15)	32:9-14 (12-15)	32:9-14 (9-14)  (10) (11) (12-13) (14)	32:9-14 (9)  (10) (11) (12-13) (14)
		Nyakati za Roho Zitayaona Mabadiliko ya Uumbaji Wote		Kumiminiwa yule Roho
	Amani ya Utawala wa Mungu	32:15-20 (15-20)	32:15-20	32:15-20 (15-17)
	32:16-20 (16-19)  (20)			(18-20)

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. xvi na kipengele cha utangulizi)**  
**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.  
 Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Sura za 31-32 ni ole tano kati ya ole sita (28:1; 29:1,15; 30:1; 31:1;33:1) ambazo zinahusika na juhudzi za Hezekia za kuunda umoja wa jeshi la kisiasa pamoja na Farao wa Nubia ya Himaya ya Misri ya Karne ya Ishirini na Tano.
- B. Yuda ilitumaini katika Misri, lakini si YHWH, kwa ajili ya ulinzi. Isaya alilionia suala hili kama ukiukaji wa tumaini/imani katika agano la ahadi na uwepo wake.
- C. Sura hii inaangalia juu ya selikali ya nyakati zijazo za Mfalme mewenye Haki katika Yerusalem (kama vile mst. wa 1; 9:6-7; 11:1-5; Mika 5:2-5a). Hivi ndivyo ilivyompoasa Hezekia kuwa. Yeye alimkaribia katika imani yake, suala hili linaonekana katika 37:14-20,30.

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 32:1-8

<sup>1</sup>Tazama, mfalme atamiliiki kwa haki,  
na wakuu watatawala kwa hukumu.  
<sup>2</sup>Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo,  
na mahali pa kujisitiri na dhoruba;  
kama mito ya maji mahali pakavu,  
kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.  
<sup>3</sup>Tena macho yao waonao hayatakuwa na kiwi,  
na masikio yao wasikiao yatasikiliza.  
<sup>4</sup>Tena moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu maarifa,  
na ndimi zao wenye kigugumizi zitakuwa tayari kunena sawasawa.  
<sup>5</sup>Mpumbavu hataitwa tena mwungwana,  
wala ayari hatasemwa kwamba ni karimu.  
<sup>6</sup>Maana mpumbavu atanena yaliyo upumbavu,  
na moyo wake utafanya maovu,  
ili kutenda hila na kusema yasiyo kweli juu ya Bwana,  
ili kuziacha nafsi za watu wenye njaa hazina kitu,  
na kukikomesha kinywaji chake mwenye kiu.  
<sup>7</sup>Tena vyombo vyake ayari ni vibaya;  
hutunga hila mbaya, ili kuwaangamiza wanyonge kwa maneno ya uongo,  
mtu mhitaji ajaposema maneno yenye haki.  
<sup>8</sup>Bali mwungwana huwaza mambo ya kiungwana,  
naye hushika sana mambo ya kiungwana.

**32:1“mfalme. . .malkia”** Mistari ya 1-8 inaakisi utawala wa mfalme anayemcha Mungu na Serikali yake (kama vile 9:6-7;11:1-5; 16:5; Mika 5:2-5a). Inaonekana kuwepo utata uliokusudiwa ili Hezekia (utimilifu wa haraka wa 7:14-15) na Masihi ajae (utimilifu wa mwishokama vile 7:14, kama vile Mt.1:23) wote waweze kuakisiwa katika kifungu hiki.

**32:2**Huu ni mstari unatoa ufanuzi katika stiari za “jangwa” juu ya utawala wa kiongozi huyu mcha Mungu na umoja wake.

1. kimbilio (BDB 285, kif. “eneo la kujificha,”muundo huu unapatikana hapa pekee) kutokana na upepo
2. makazi (BDB 712) kutokana na dhoruba (inafanana na #1)
3. chemchemi za maji katika nchi yenyeye uchovu
4. kivuli (BDB 853) cha mwamba mkubwa katika nchi yenyeye jangwa

Stiari zinazofanana zinatumika kwaYHWH katika 25:4. Na sasa zinatumika kutoa ufanuzi wa watu wa Mungu au utawala kwa kiasi fulani (yaani, “watawala,” KITENZI,BDB 979, KB 1362, Qalya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU).

Hiki KITENZI “mwanadamu” (BDB 224, KB 243 Qalya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kingeweza kumrejelea “mfalme”wa mst. 1 au watu wa“agano jipya” wanaoleezwa katika Yer. 31:31-34.

**32:3-4** Kipengele hiki kinaleza hali ya kiroho ya watu wa agano walioreheshwa kama yenyeye kutofautishwa na 6:9-10 (kama vile Kumb. 29:4).

1. hayatakuwa na kiwi
2. yatasikiliza
3. utafahamu maarifa
4. yenyeye kigugumizi zitakuwa tayari kunena sawasawa(“wenye kigugumizi,” BDB 748, neno hili linajitokeza hapa tu)

**32:5-8“Mpumbavu . . . mwungwana”**Makundi haya mawili yataendelea kuwemo ndni ya jamii, lakini yataonekana kwa namna yalivyo (mst. 6-7). Mstari wa 6-7 unaonekana kueleza watu wawili walio dharimu, ambapo mst. wa 8 unaeleza juu ya mkuu wa “kweli”

1. “mpumbavu” (BDB 614) anayeelezwa katika mst. wa 6
  - a. moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu maarifa
  - b. moyo wake utafanya maovu
    - 1) anatenda yasiyo ya Mungu
    - 2) ili kutenda hila na kusema yasiyo kweli juu ya Bwana
    - c. kuziacha nafsi za watu yenyeye njaa hazina kitu
    - d. kukikomesha kinywaji chake mwenye kiu.kuziacha nafsi za watu yenyeye njaa hazina kitu
2. neno“ayari” (BDB 647, linalojitokeza hapa pekee, mara mbili) linaleezwa kataika mst. wa 7
  - a. vyombo vyake ayari ni vibaya
  - b. hutunga hila mbaya
  - c. ili kuwaangamiza wanyonge kwa maneno ya uongo
  - d. mtu mhitaji ajaposema maneno yenyeye haki
3. mwungwana(BDB 622), mst. wa 8
  - a. mwungwana huwaza mambo ya kiungwana(au “mkarimu”) hupanga tofauti na wale waliotajwa katika mist. ya 6 na 7
  - b. naye hushika sana mambo ya kiungwana

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 32:9-20

<sup>9</sup>Inukeni, enyi wanawake yenyeye raha,

isikieni sauti yangu;

enyi binti za watu msiokuwa na uangalifu,

tegeni masikio yenu msikie matamko yangu.

<sup>10</sup>Maana mtataabishwa siku kadha wa kadha zaidi ya mwaka,

enyi wanawake mlajikinai;

kwa sababu mavuno ya mizabibu yatakoma,

wakati wa kuvuna vitu vya mashamba hautakuja.

<sup>11</sup>Tetemekeni, enyi wanawake yenyeye raha;

**taabikeni, enyi msiokuwa na uangalifu;**

**jivueni, jivueni nguo zenu kabisa, jivikeni viuno nguo za magunia.**

**<sup>12</sup>Watajipiga vifua kwa ajili ya mashamba mazuri, kwa ajili ya mzabibu uliozaa sana.**

**<sup>13</sup>Juu ya nchi ya watu wangu itamea michongoma na mibigili;**

**naam, juu ya nyumba za furaha katika mji ulio na shangwe;**

**<sup>14</sup>maana jumba la mfalme litaachwa; mji uliokuwa na watu wengi utakuwa hauna mtu;**

**kilima na mnara utakuwa makao ya wanyama milele,**

**furaha ya punda-mwitu, malisho ya makundi ya kondoo;**

**<sup>15</sup>hata roho itakapomwagwa juu yetu kutoka juu; hata jangwa litakapokuwa shamba lizaalo sana;**

**nalo shamba lizaalo sana litakapohesabiwa kuwa msitu.**

**<sup>16</sup>Ndipo hukumu itakaa katika jangwa, na haki itakaa katika shamba lizaalo sana.**

**<sup>17</sup>Na kazi ya haki itakuwa amani;**

**na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima.**

**<sup>18</sup>Na watu wangu watacaa katika kao la amani;**

**na katika maskani zilizo salama, na katika mahali pa kupumzikia penye utulivu.**

**<sup>19</sup>Lakini mvua ya mawe itakunya, wakati wa kuangushwa miti ya msituni;**

**na huo mji utadhilika.**

**<sup>20</sup>Heri ninyi mpandao mbegu kando ya maji yote,**

**na kuiacha miguu ya ng'ombe na punda waende ko kote.**

**32:9-12** Huu ubeti unawazungumzia matajiri, jamii wanawake wa Yerusalem waliyo na mali (kama vile 3:16-4:1). Angalia namna wanavyoelezwa.

1. Inukeni, enyi wanawake wenye raha, mst. wa9, BDB 877, KB 1086, *Qalya KAULI YENYE MASHARTI*. KITENZI kinachofanana kimetumika kataika msari uliotangulia katika maana ya "simameni" au "ngogeni," bali hapa mstari huu unamaanisha "simameni" wakati Bwana (aunabii wake) anapozungumza nanyi.
2. isikieni sauti yangu, mst. wa 9, BDB 1033, KB 1570, *Qalya KAULI SHURUTISHI*
3. tegeeni masikio yenu msikie matamko yangu, mst wa 9, BDB 24, KB 27, *Hiphilya KAULI SHURUTISHI* (kama vile 28:23). Angalia namna VITENZI vya tatu nan ne vinavyofanana, kama vifungu vibainishi "enyi wanawake wenye raha,"(kama vile mst. wa 11) na "enyi binti za watu msiokuwa na uangalifu," na tena katika mist. ya10,11.
4. mtataabishwa, mst. wa10, BDB 919, KB 1182, *Qalya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*. Neno hili linadokeza "hofu," "kutetemeka," "kuwa na mashaka." Angalia umuhimu wa"wakati" katika mst. wa10.
  - a. siku kadha wa kadha
  - b. zaidi ya mwaka
  - c. mavuno ya mizabibu yatakoma
5. taabikeni, mst. wa11, BDB 353, KB 350, *Qalya KAULI SHURUTISHI*, kama vile 10:29; 19:16; 41:5. Kifungu hiki kinafanana na "mnataabishwa"katika mst. wa10 (kwa mshangao KAULI SHURUTISHI zote za mst. wa 11 ni JINSI YA KIUME, lakini zinatoa mawaiza kwa wanawake).
6. taabikeni, mst. wa11, BDB 919, KB 1182, *Qalya KAULI SHURUTISHI*, ina KITENZI kinachofanana na mst. wa 10
7. tetemekeni, mst. wa11, BDB 832 II, KB 980, *Qalya KAULI SHURUTISHI*. Hii inaweza kuwa ishara ya (1) kuomboleza (kama vile Eze. 26:16) or (2) unyanyasaji (kama vile Hos. 2:5).
8. jivueni, mst. wa 11, BDB 792, KB 889, *Qalya KAULI SHURUTISHI*
9. , jivikeni viuno nguo za magunia,mst. wa11, BDB 291, KB 291, *Qalya KAULI SHURUTISHI*, pia hii ni ishara ya kuomboleza. Angalia Mada Maalum katika 15:2-3.
10. Watajipiga vifua, mst. wa12, BDB 704, KB 763, *Qalya KAULI TENDAJI ENDELEVU*, hii ni alama nyingine ya kuomboleza , Luka 18:13; 23:48.

Vifungu hivi vyote vinahusiana na kipindi cha uvamizi wa Senakaribu juu ya Yerusalem mnamo 701 K.K.. Wavamizi walikuwa wamebobe katika ukatili wa maangamizi na maradhi.

### 32:9,10,11

NASB, NKJV,

NRSV	“wanawake mliorizika”
NJB	“wanawake mnaojiamini sana”
REB	“wanawake msiojali”
LXX	“wanawake wenye matumaini”
JPSOA	“binti wenye ujasiri”

Hili neno la Kiebrania (BDB 105, KB 120) mara nyigi linamaanisha “ulinzi” au “ujasiri,” kuitia kwa baadhi ya wasomi angalia asili nyingine (BDB 105 II, KB 121) yenye maan ya “kusujudu” (NIDOTTE, juzu. 1, uk. 649).

Hili neno pia linajitokeza katika 32:17 na linatafsiriwa kama “ujasiri” ama “ulinzi” (pambizo za toleo la NASB). Hawa wanawake wenye mali, wasomi walikuwa wanajiamini sana (NJB).

**32:10“zaidi ya mwaka”**Huu ni wakati unaorejelewa kwa upekee sana (huenda unahusishwa na msimu wa mavuno) na uanaonekana kuhusiana na kuja kwa Senakaribu mnamo 701 K.K.

**32:12“Pigeni vifua vyenu”**Kuna njia mbili za kushughulika na kifungu hiki.

1. jivikeni viuno nguo za magunia mst. wa 11
2. badili neno la Kiebrania “kifua”(neno hadimu la kiushairi, BDB 994, תְשׁוּ) katika “mashamba” (BDB 961, יָדֵשׁ, kama vile 56:9), kama vile Toleo la JPSOA linavyoorodhesha katika tambihi. Ikiwa uchaguzi #2 unafuatawa, kisha “mashamba,” “mashamba yafuraha,” na “mzabibu wenye kuzaa matunda” huu unakuwa ufanano wa kupoteza manufaa ya kilimo.
3. Kione kifungu hiki kama nahau ya kuomboleza kwa vyo vyote kwa wanaume au wanawake (Peshitta)

**32:13“ nyumba za furaha”**Hili neno “furaha” linalofanana (BDB 965) linatumika katika mst. wa 14 kwa kifungu “furaha ya punda-mwitu” Isaya anatumia

1. uwili
2. mizaha
3. stiari ziliyorudiwa ili kufikisha jumbe zake. Andiko la Kiebrania lalsaya linabadilika zaidi na linaumbwa katika kutafsiri. Alikuwa bwana wa shairit. Mtu anashangaa ikiwa YHWH anaweza kuzifikisha jumbe zake katika ushairi aulsaya aliumba. Kwa kuwa mafunuo yote ya YHWH hayapo katika sanaa ya mashairi, inaonekana huu ulikuwa ustadi wa Isaya. Uchaguzi wa maneno yaliyo mengi katika Isaya yaangukia katika mashairi ya kuimbika kuliko maana ya uumbaji wa maneno. Maneno hadimu yanatumika, kama maana za kipekee katika maneno ya kawaida. Hapa ndipo utata unapoanzia kwa wafasiri!

▣“mji ulio na shangwe”Angalia maelezo katika 24:10 na jedwali katika utangulizi wa sura ya 26, D. Mungu alitaka nkuwabariki watu wa agano kwa Baraka za kipekee ili kuyavutia “mataifa,” lakini kwa sababu yauasi wa Israeli na Yuda, badala ya utulivu na amani ilitokea miiba na mbigili (kama vile 5:6; 7:23-25; 9:18; 10:17; 27:4; Mwa. 3:18).

**32:14** Huu mstarai unaeleza juu ya maangamizi ya Yerusalem (kama vile 6:11; 64:10), ambayo si nya kawaida kwa Isaya ambaye mara nyigi mji huu unaona ukombozi (kama vile 1:8-9; 8:8; 29:1-8; 37:36-37). Isaya anaueleza utakaso wa Yerusalem kwa sababu ya uwepo wa YHWH mahali pale (yaani, hekalu), lakini baadaye Yeremiakwa usahihi anaongeza jambo hili la kithiolojia kwa kutazamia asili ya hali ya ahadi za YHWH kwa watu wake wa agano (yaani, Kumbukumbu 27-28). Isaya analitumaini neno la Mungu, lakini ahadi zake zinahusianishwa na imani sahihi ya mtu na utii. Agano ni maneno mawili ya mtaa! Tazama namna maangamizi yanavyonyumbuliwa.

1. jumba la mfalme litaachwa (yaani, uzao wa Daudi umetelekezwa)
2. mji uliokuwa na watu wengi utakuwa hauna mtu(yaani, uzao wa he Ibrahim) umetelekezwa)
3. NASB, “kilima”

NJB "Ofeli" (BDB 779), ni eneo la kingo za kusini mwa Yerusalemu ya kale (austiasi ya mji mzima, sawasawa na "Sayuni"). Kifungu hiki kinatajwa katikali Nya. 27:3;33:14; Neh. 3:26-27; 11:21

4. #3inafana na "mnara wa ulinzi"; haya yote yanaweza kudokeza majanga ya Yerusalemu kuharibiwa
5. mahali pa punda- mwitu
6. malisho kwa ajili ya mifugo, zote #5 na #6 zinadokeza sehemu iliyona jangwa, mji ulioharibiwa, eneo linaokaliwa na wanyama tu (kama vile 13:21; 34:13)

Kuna VITENZI vyenye ufanano wa aina mbili.

1. litaachwa, BDB 643, KB 695, *Pual* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, hili neno *Pual* linajitokeza hapa tu
- 2.imeachwa, BDB 736, KB 806, *Qal* ya KAULI TENDAJI(*auPual*) YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Yer. 49:25

◎

<b>NASB</b>	"mapango"
<b>NKJV</b>	"mashimo"
<b>NRSV</b>	"matundu"
<b>NJB</b>	"maandaki"

Hili neno (BDB 792) linamaanisha "pango," lakini katika muktadha huu, "ni mashimo ya wanyama." Inawezekana kwamba Isaya alilichagua neno hili kwa sababu sauti yake inafanana na

1. "andaki" (mzizi wa Kiarabu), עַד (muktadha wa kifo na maangamizi)
2. "jivueni," עָרֵן, KITENZI hadimu kinachotumika katika mst. wa 11
3. "shamba lizaalo," שְׁמַעַתְּקֹוֹתָאָה asili ya Kiarabu (NIDOTTE, juzu 2, uk. 1034)

▣ "milele" Huu ni uhusiano wa matumizi ya neno la Kiebrania 'olam. Hili neno lina matumizi mapana ya kimaana na lazima lifasiriwe katika muktadha.

## MADA MAALUMU: MILELE ('OLAM)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, סִלְעָה (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzu 3, uk. 345). Haya yanatumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na muktadha). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
  - a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
  - b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
  - c. Mungu, Zab. 93:2; Mit. 8:23; Isa. 63:16
  - d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
  - e. muda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. muda/ wakati ujao
  - a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
  - b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
  - c. uwepo endelevu
    - 1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
    - 2) mbinguni, Zab. 148:5
  - d. uwepo wa Mungu
    - 1) Mwa. 21:33
    - 2) Kut. 15:18
    - 3) Kumb. 32:40
    - 4) Zab. 93:2
    - 5) Isa. 40:28
    - 6) Yer. 10:10
    - 7) Dan. 12:7

- e. agano
  - 1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
  - 2) Kut. 31:16
  - 3) Ufu. 24:8
  - 4) Hes. 18:19
  - 5) II Sam. 23:5
  - 6) Zab. 105:10
  - 7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
  - 8) Yer. 32:40; 50:5
- f. Agano maalumu na Daudi
  - 1) II Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
  - 2) I Fal. 2:33,45; 9:5
  - 3) II Nya. 13:5
  - 4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
  - 5) Isa. 9:7; 55:3
- g. Masihi wa Mungu
  - 1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
  - 2) Isa. 9:6
- h. Sheria za Mungu
  - 1) Kut. 29:28; 30:21
  - 2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
  - 3) Hes. 18:8,11,19
  - 4) Zab. 119:89,160
- i. ahadi za Mungu
  - 1) II Sam. 7:13,16,25; 22:51
  - 2) I Fal. 9:5
  - 3) Zab. 18:50
  - 4) Isa. 40:8
- j. Uzao wa Ibrahamu na nchi ya ahadi
  - 1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
  - 2) Kut. 32:13
  - 3) I Nya. 16:17
- k. Sikukuu za ahadi
  - 1) Kut. 12:14,17,24
  - 2) Ufu. 23:14,21,41
  - 3) Hes. 10:8
- l. umilele, kudumu milele
  - 1) I Fal. 8:13
  - 2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
  - 3) Isa. 26:4; 45:17
  - 4) Dan. 9:24
- m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
  - 1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
  - 2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
  - 3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
  - 4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
  - 5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
  - 6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
  - 7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
  - 8) baliki jina lake, Zab. 145:1

3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
  - a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
  - b. Zab. 90:2 (Mungu Mwenyewe)
  - c. Zab. 103:17 (huruma za Bwana)

Kumbuka, mktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka, sisi pia, agano jipya linajumuisha ahadi za agano la kale (angalia mada maalum: unabii wa agano la Kale ya mambo yajayo dhidi ya unabii wa Agano jipya).

**32:15-20** Huu ubeti unaeleza nyakati mpya, nyakati mpya kwa Yerusalem.

1. Roho amamiminwa kutoka kwa Mungu. Uhusiano kamili kati ya YHWH na "Roho" katika Agano la Kale ni mgumu kuhusianisha na mafunuo kamili ya kipekee ya Agano Jipya. Mara nyingi Roho anahusianishwa na uumbaji (kama vile Mwa. 1:2; Ayubu 26:13; Zab. 104:29-30; 147:14-18). Kwa uumb! Kwa habari zako, Nimeujumuisha mstari huu katika Mada Maalum yangu ya Agano Jipya inahu "Utu wa Roho."

## MADA MAALUM: UTU WA ROHO

Katika kitabu cha Agano la Kale "Roho wa Mungu" (yaani, *ruach*) ilikuwa nguvu ambayo ilikamilishwa kwa kusudi la YHWH, lakini kulikuwa na dokezo chache kwamba nguvu hii ilikuwa ya kibinagsi (yaani, Mungu mmoja wa Agano la Kale, tazama Mada Maalum: Mungu mmoja). Hata hivyo, katika Agano Jipya nafsi kamili na utu wa Roho unafunuliwa:

1. Anayeweza kukufuliwa (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Anayefundisha (kama vile Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Anayeweza kubeba ushuhuda (kama vile Yohana 15:26)
4. Anaye weza kuhakikisha, huogoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa "aliye" (yaani, *hos*, kama vile Efe. 1:14)
6. Anayeweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anayeweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anayeweza kumpingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Ni msaidizi kwa waamini (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Anamtukiza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya Utatu (hapa kuna matatu kati ya mengi, angalia Mada Maalum: Utatu) pia yanazungumza juu ya nafsi tatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Japokuwa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni TASA, linamrejelea Roho, kitabu cha Agano Jipya mara nyingi kinatumia KIVUMISHI ONYESHI JINSI YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho ameungamanishwa na matendo ya mwanadamu.

Matendo 15:28

1. Rum. 8:26
2. Kor. 12:11
3. Efe. 4:30

Mwanzoni sana mwa kitabu cha Matendo, kazi ya Roho inasistizwa (kma katika Injili ya Yohana). Siku ya Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho, buli sura mpya. Yesu alikuwa na Roho mara kwa mara. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa Roho, bali sura mpya. Roho ni maana kamili ya kusudi la Baba kwa ajili wa wanadamu wote walioumbwa kwa sura na mfano wake (tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele)!

2. Jangwa linafanyika shamba lizaalo sana . . . msitu, mst. 15. Huu ni mrejeo wa mist. ya12-13. Angalia stiari zinazofanana za rutuba katika 29:17.
3. Hukumu. . .haki itadumu, mst. 16
4. utulivu na matumaini daima, mst. 17. Kifungu hiki kinamaanisha ujio (kama vile mst. 18).
5. Mstari wa 19 linaweza kurejea utangulizi waAshuru.
6. Mstari wa 20 ni baraka nyingine, lakini kwa kiasi fulani kifungu hiki ni cha utata.

### 32:15

NASB, NKJV,

NIV "roho itakapomwagwa juu yetu kutoka juu"

NRSV, JPSOA "mpaka roho kutoka juu itakapomiminwa juu yetu"

TEV "Mungu atatupelekea roho wake"

NJB "hadi roho atakapomiminwa toka juu yetu"

REB "hadi roho atakapomiminwa juu yetu"

Andiko la Kiebrania halinaKIBAINISHI,KIWAKILISHI,au kifungu bainishi (yaani, "ya Bwana" kama katika 11:2 au "Wangu," 44:3; 59:21; Yoeli2:28) linalohusianishwa na NOMINO "roho" (BDB 924). Swali ni nkwamba kifungu hiki kinamrejelea nani.

1. Roho wa nyakati mpya
2. Roho Mtakatifu
3. Roho wa toba na tumaini toka kwa Mungu

Sarufi inapendekeza #1 au #3, lakini muktadha unapendekeza #2.

Huu ni mgawanyiko wa mara kwa mara katika muktadha. Hivi ni vifungu vinavyofanana vinavyozungumza juu

Roho wa Mungu ni Isa. 44:3;

Eze. 39:29; Yoeli 2:28-29; Zek. 12:10; Acts 2:1-21.KITENZI hiki hiki kinatumika katika maana ya dhabihu ya Masihi katika Isa. 53:12.Kuna mfuatano wa Baraka saba ambazo zitatokea kwa sababu ya kuwepo kwa Roho: (1) rutuba, (2)hukumu, (3)haki,(4) amani, (5) utulivu, (6) ujasiri, na (7) maskani za salama.

▣“**kutoka juu**”Hii ni nahau ya neno “mbinguni,” mahali pa maskani ya YHWH (kama vile Ayubu 16:19; 31:2; Isa.33:5).

**32:16“hukumu. . .haki”** Hizi ni jozi za kawaida katika Agano la Kale (kama vile II Sam. 8:15; I Fal. 10:9; I Nya.18:14; II Nyak.9:8; Zab. 99:4; Isa. 9:7; 32:16; 33:5; 59:14; Yer. 4:2; 9:24; 22:3,15; 23:5; 33:15; Eze.18:5,19, 21,27; 33:14,16,19; 45:9; Amosi. 5:7,24). Hizi zinadokeza aina ya jamii (kama vile mist.ya 17-18) ambapo watu wote wanaleshimiwa na kuchukuliwa kwa usawa kama washirika wa agano. Kisha kifungu hiki kinabainisha uwepo wa Mungu wa kipekee kati watu wake.

**32:17“amanī”**Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM : AMANI (*SHALOM*)

Neno la Kiebrania *shalom* (BDB 1022, KB 1532) ni la kawaida katika asili ya Kisemiti.

- A. Lugha ya Akkadia
  - 1. Kutokudhurika
  - 2. Kuishi vizuri
  - 3. Kuwa katika hali nzuri
- B. Ugariti (Wakaanani)
  - 1. Kutohdhurika
  - 2. Kuwa mzima
- C. Kiarabu
  - 1. Kuwa mwenye afya
  - 2. Kuwa katika hali ya amani
- D. Kiarama
  - 1. Kuwa mkamilifu
  - 2. Kufikia mwisho/kuhitimisha
  - 3. Kuhitmisha amani
  - 4. Kubaki pasipo kudhuriwa
- E. Vidokezo vya Kiebrania
  - 1. Kuwa mtimilifu
  - 2. Mwenye kusikika
  - 3. Kustawi
  - 4. amani

siku hizi neno *shalom* ni neno la salamu na maelezo ya kutakiana heri. Bado linamaanisha kukosekana kwa uovu na uwepo wa mema(yaani., kutosheka na maisha). Inamaanisha hali ya akili ya usalama na utosherevu. Tambua namna Agano la Kale linavyozungumzia juu ya "agano la amani" (kama vile Hes. 25:12; Ezek. 34:25; 37:26; pia kumbuka Mwa. 26:29,31; Yos. 9:15). Lazima litendeke (kama vile Zab. 34:14; Rum. 14:19). AB, juzu. 5, uk. 206, inasema, "amani," "ukweli," na "haki" zinafanana na dhana ya Kiebrania (kama vile Zak. 8:16-19). YHWH anaitwa "Bwana wa amani" (kama vile Amu. 6:24; Rum. 16:20; 2 Kor. 13:11; Fil. 4:9; 1 The. 5:23). Masihi ataitwa "Mfalme wa Amani" (kama vile Isa. 9:5). Siku mpya wakati amani, ukweli, na haki itakuwa wazi kwa uzoefu wa mwanadamu (kama vile Isa. 60:17; 66:12,22). "uzuri" wa Mwanzo 1:31 tena ni uwezekana, ahadi (yaani., "mbingu mpya na nchi mpya").

▣ "mahali pa kupumzikia penye utulivu." Haya maneno mawili (BDB 1052 na BDB 105) pia yanajitokeza katika 30:15, sura ambayo inatoa sifa bainishi za nyakati mpya za hukumu, haki, na utulivu (kama vile mist.ya 1,16).

**32:19** Huu ni mstarai mgumu sana ambao unaonekana kuwa nje ya eneo. Huu unaweza kuirejelea Ashuru. Hiki kifungu "msitu" kinatumika Ashuru katika 10:18-19,33,34. Hikikifungu "mji" kinatumika kumaanisha Ashuru katika 24:10; 25:2,3;

26:5.

▣	
NASB	"itakunya"
NKJV	"japo inakunya"
NRSV	"haitaonekana hata kidogo"
TEV	"(lakini mvua itanyesha. . .)"
NJB	"itaangamizwa kwa ujumla"
LXX	"ikirashia"

Peshitta	“mvua itanyesha”
REB	“itakuwa tuli juu ya miinuko”
JPSOA	“itazama na kudidimia”

Matoleo ya kale yanaliona toleo la MT (mfumo usiojulikana) kama בְּרֵד, BDB 135, “mvua,” kama vile nomino katika 28:2,17.

Toleo la REB linakiona kifungu hiki kama chenye kutokana na asili ya inayofanana katika maana ya Kiaramu “kuwa tulivu” (BDB 135).

Toleo la NJB na JPSOA yanayaona maneno ya kwanza ya toleo la MT kama mwanzo unaotokana na asili ya KITENZI kinachofanana, תִּנְזִי,

1. *Qalya KAULI YA WAKTI TIMILIFU*
2. *Qalya TUNGO YA KITENZI JINA*

yenye kudokezautimilifu wa maangamizi ya moja kwa moja (“mashambulizi”).

**32:20** Huu mstari pia ni mgumu sanakuhuusianisha na muktadha. Hata hivyo, pumziko linonekana kuwepo katika siku za baraka za Mungu, mazao yatakuwa mengi ambapo mifugo itazunguka kwa uhuru na kila pasipo kuyazuru mazao.

## ISAYA 33

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hukumu ya Mungu 33:1-12 (1-12)	Maombi kwa ajili ya Mateso ya Kina 33:1-4 (1)  (2-4)  33:5-9 (5-6)  (7-9)	Litrujia ya Kinabii 33:1-24 (1)  (2-6)	Maombi kwa ajili ya hitaji la Msaada 33:1  33:2-4  33:5-6  33:7-9  (6)	Ukombozi Uliotarajiwa 33:1-16 (1-5)  Mungu Anawaonya Maadui zake  33:10-13 (10-13)  33:14-16 (14-16)  Nchi ya Mfalme Mkuu  33:17-24 (17-24)
33:13-16 (13-16)		(13-16)		
			33:10-13  33:14-16  Wakati wa Utukufu Ujao  33:17-24  (21-24)	Kurudi Yerusalem  33:17-24 (17-20)
			(23a)  (23b-24)	
		(23b-24)		

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi na kipengele cha utangulizi)  
KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibilia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

2. Ayaya kwanza
3. Ayayapili
4. Aya ya tatu
5. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ugawaji katika haya ni wa kiutata (kwa sababu ya asili ya mchanganyiko wa mashairi haya) katika sura hii. Makundi kadhaa na tofauti tofauati yanaainishwa.

1. Ashuru, mst. wa 1
2. watu wa agano, mst. wa 2
3. mashujaa wanaolia nje, mst. wa 7
4. wajumbe wa amanini nwanaolia kwa uchungu, mst. wa 7
5. msafiri, mst. wa 8
6. watu, mst. wa 12
7. ninyi mlion mbali, mst. wa 13
8. ninyi nmlio karibu,mst. wa 13
9. wenye dhambi walio katika Sayuni, mst. wa 14
10. ni yeye atendaye kwa haki, mst. wa 15
11. Huyu . .yake, mst. wa 16
12. Moyo wako, mist. ya 18-20
13. Kamba zako, mst. wa 23
14. wenyeji. . .watu, mst. wa 24

Ni vigumu kutambua ni makundi gani ambapo kila moja linahusika.

B. Tambua namna majina mengi / nyadhifa na sifa bainishi za Uungu zinavyotajwa katika sura hii.

1. Bwana,mst. wa 2
2. Bwanaanajiinua, mist. ya 5,10
3. Yeye atakuwa imara (kif. "mwaminifu"), mst. wa 6
4. Nyakati za wokovu, hekima, na maarifa, mst. wa 6
5. kumcha Bwana, mst. wa 6
6. Mfalme katika uzuri wake, mst. wa 17
7. Mwenye adhama, v. 21
8. mwingi, "Bwana ni. . .," mst. wa 22

C. Iawezekana kwamba kipengele cha kwanza cha Isaya kinahitimisha sura hii kwa sababu katika Mafunjo ya DSS ya Isaya nafasi zilizo mara bili ziznjitokeza baada ya sura hii, lakini si baada ya sura ya 39.

D. "Inawezekana" muhtasari wa mtiririko/mpangilio wa ushairi huu

1. Mungu aliyeihukumu ashuru ndiye aliyetumika kuihukumu Yuda, mst. wa 1
2. Yuda analia kwa ajili ya msaada, mst. wa 2
3. Mugu anajibu, mist. ya 3-6,10-12
4. Hali ya sasa ya Yuda, mist. ya 7-9
5. Wacha Mungu wanaokolewa, mist. ya 13-16
6. ufupisho wa kipindi cha Ashuru, mist ya 17-20
7. utawala wa mfalme mwenye haki, mist. ya 21-2

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 33:1-12**

<sup>1</sup>Ole wako uharibuye ila hukuharibiwa,  
utendaye hila wala hukutendwa hila!  
Utakapokwisha kuharibu, utaharibiwa wewe; na utakapokwisha kutenda kwa hila,  
wao watakutenda hila wewe.  
<sup>2</sup>Ee Bwana, uturehemu; tumekungoja wewe;  
uwe wewe mkono wetu kila asubuhi, na wokovu wetu pia wakati wa taabu.  
<sup>3</sup>Kabila za watu wamekimbia wakisikia kelele za fujo; mataifa wametawanyika ulipojiinua nafsi yako.  
<sup>4</sup>Na mateka yako yatakumbwa  
kama wadudu wakumbavyo, wataruka juu yake kama arukavyo nzige.  
<sup>5</sup>Bwana ametukuka; kwa maana anakaa juu;  
amejaza Sayuni hukumu na haki.  
<sup>6</sup>Nyakati zako zitakuwa nyakati za kukaa imara;  
za wokovu tele na hekima na maarifa;  
kumcha Bwana ni hazina yake ya akiba.  
<sup>7</sup>Angalia, mashujaa wao wanalia nje,  
wajumbe wa amani wanalia kwa uchungu.  
<sup>8</sup>Njia kuu zimeachwa, msafiri amekoma;  
ameyavunja maagano, ameidharau miji, hamjali mtu,  
<sup>9</sup>Nchi inaomboleza, na kulegea;  
Lebanoni imetahayarika na kunyauka;  
Sharoni imekuwa kama jangwa;  
Bashani na Karmeli zimepukutika majani.  
<sup>10</sup>Basi, sasa nitasimama; asema Bwana;  
sasa nitajiinua, sasa nitajitukuza.  
<sup>11</sup>Ninyi mtachukua mimba ya makapi, mtazaa majani makavu;  
pumzi yenu ni moto utakaowateketeza wenyewe.  
<sup>12</sup>Nao mataifa watakuwa kama kuchoma chokaa,  
kama miiba iliyokatika, iteketezwayo motoni.

**33:1** “Ole” Sura za 8-33 zinaunda umoja ambao mara nyingi uanaitwa “Umoja wa Maangamizi” kwa sababau ya matumizi ya mara kwa mara ya neno “ole,” (kama vile 28:1; 29:1,15; 30:1; 31:1; 33:1). Angalia maelezo yanayohusu “Ole” katika 5:8.

■“uharibuye” Mstari 1 unaizungumzi Ashurua, kama mist. ya3,4,7-9,11-12,17-19,23; hata mist. ya21 inaweza kuirejelea miji iliyo katika Mito ya Hedekelina Frati. Sura hii inaufuata mpangilio wa dhana ya kawaida ya Isaya.

1. hali ya uhasi wa mara kwa mara wa watu wa Mungu
2. hukumu ya Mungu kwa nguvu za kigeni
3. hukumu ya Mungu juu ya nguvu hizi za kigeni (hapa ni Ashuru)
4. hali ya watu wake ya utakufu ujao kupitia mfalme mwenye haki (kama vile 32:1)  
Maneno yote ya “waliaharibu” (BDB 994, KB 1418 mara mbili, *Qal ya KAULI TENDAJI ENDELEVU, YENYE KUKANUSA Qal ya KAULI TENDEWA ENDELEVU*) na “wasio waaminifu” (kif. “kutotenda kwa uaminifu,” BDB 93, KB 108 mara mbili, *Qalya KAULI TENDAJI ENDELEVU, YENYE KUKANUSA Qalya WAKATI TIMILIFU*) pia yanatumika katika 21:2 kuhusu kuanguka kwa Babeli. Katika maana ya kithiolojia utata wa Isaya ni wa kukusudiwa. Kwa makusudi anatengeneza uambulisho wa washambulaiji wa Israeli/Yuda wasiojulikana ili mashairi yake yaweze kutenda kazi kamaunabii “utimilifu mara difu”. Maadui wanakuja na kuondolewa kwa mkono na makusudi ya YHWH, lakini YHWH mwenyewe na makusudi yake ya ukombozi wa milele, kuutumia uzao wa Ibrahimu, si hivyo!

**33:2** Mudhui ya maombi ya Yuda yanaorodheshwa.

1. uwe mwenye huruma kwetu, BDB 335, KB 334, *Qalya KAULI SHURUTISHI*, kama vile 30:18,19

2. tunakungoja wewe, BDB 875 I, KB 1082, *Pielya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile . 8:17; 25:9; 26:8; 40:31;49:23; 51:5; 60:9
3. uwe nguvu yetu (kif. "mkono") kila asubuhi, BDB 224, KB 243, *Qalya KAULI SHURUTISHI*
4. uwe wokovu wetu katika nyakati za taabu (KITENZI "kuwa" chenye kudhaniwa)YHWH ndiye tumaini pekee la Yuda (kama vile 59:16; 63:1,5), si Ashuru (muungano) na si Misri (muungano), ni YHWH pekee. Wanadamu huelekea kufadhaika na kupoteza tumaini katika nyakati za ghasia na zisizo na uhakika. Hawa wanajaribu kujiokoa wenyewe kwa kutumia nyenzo zao za wanadamu wengine, kunufaika!

▣“nguvu”Kiuhalisia kifungu hiki kinamaanisha “mkono” (BDB 283).Hii ni stiarai ya lugha ya kibiblia yenyе kueleza majibu ya Mungu na uweza katika matukio ya kila siku.

▣“wokovu”Neno hili (BDB 447)linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya ukombozi wa kimwili (kamavile 12:2 [mara mbili], 3;25:9; 26:1,18; 33:6).

### **MADA MAALUM : WOKOVU (Neno la Agano la Kale)**

Neno hili (BDB 447, KB 446, ni la jinsi zote JINSI YA KIUME na NOMINO YA JINSI YA KIKE), ambazo kimsingi linamaanisha "kuwa pana na wazi" au "kuwa huru," lina maana kadhaa.

1. usalama, 2 Sam. 22:3; Ayubu 5:11; Zab. 12:5
2. heshima, mafanikio, Ayubu 30:15
3. wokovu wa ki-Ungu ambaa unahusisha ukombozi wa namna zote, wa kimwili na kiroho
  - a. Mwa. 49:18
  - b. Kumb. 32:15
  - c. 2 Sam. 23:5
  - d. Zab. 3:2,8; 22:1; 35:3; 62:2; 69:29; 70:5; 78:22; 80:3; 89:26; 91:16; 106:4; 140:7
  - e. Isa. 12:2; 33:2; 51:6,8; 52:7,10; 56:1; 59:11; 60:18; 62:1,11
4. hili wazo la ukombozi wa namna zote , namna ya kimwili na kiroho linawasilishwa vema katika Yohana 2:9-10
5. ushindi, Kut. 14:30; 15:2; 1 Sam. 14:45; Zab. 20:6; 21:5; 44:4-5; 68:19-20; 118:14,15,21; Isa. 12:2; Hab. 3:8
6. mara nyingi neno "kufurahi" linahusiana na wokovu wa YHWH, 1 Sam. 2:1; Isa. 25:9; 26:1; Zab. 9:14; 13:5; 21:1; 35:9; 118:15,21

Wokovu unahusisha utekelezaji wa ushirika asilia ulio kusudiwa na YHWH na jamii yenyе viumbe vya kibinadamu. Hii inahusisha mtu binafsi na jamii mzima!

**33:4** Katika mstari huu neno “mateka”(BDB 1021) ni stiari ambayo inadokeza uharibifu wa maadui wa YHWH. Hiki KITENZI “yatakumbukwa” (BDB 62, KB 74, *Pualya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) pia kinatumika katika 32:10 kutoa ufanuzi wa hukumu juu ya Yerusalem. Pia kitenzi hiki kinatumika katika 24:22 (shina linalofanana) kudokeza hukumu ya siku za mwisho kwa ulimwengu mzima. Wanadamu “wanakumbukwa” kwa ajili yao wenyewe,uchoyo, na nguvu, bali Mungu anawakumbuka kwa ajili ya hukumu. Agano Jipyä linaeleza kukumbukwa kwa nyakati za mwisho juu ya

1. kukombolewa, Mt. 13:48; 24:31
2. wadhalimu, Mt. 13:40-41

▣“wadudu”Umamizi wa wadudu ulikuwa wa kawaida katika ANE. Mara nyingi walilinganishwa na jeshi lililofanya uvamizi (kama vile Kut. 28:38,42; Yoeli 1:4; 2:25; Amosi 7:1-2). Mungu anayaongoza majeshi kama anavyoviongoza vitu vyote! Hawa wadudu waliwazunguka mateka wote wa Ashuru.

Kuna maneno kadhaa ya Kisemiti yenyeye kuzungumzia wadudu hawa, maneno ambayoao kwa udhahiri wake yanadokeza (1) viumbe tofautitofauti au (2) hatua mbalimbali za ukuaji.

**33:5“maana anakaa juu”** Kifungu hiki ni stiari ya kimbingu (kama vile 32:15; Job 16:19; 31:2). ANE Iliitazama mbingu kama sehemu ya juu. Kwa Waisraeli moshi uliotoka katika shabihu zao walizoziteketeza ulipaa hadi kwa Mungu, hivyo, Huyu lazima awe juu. Pia kulikuwa na ntonofauti ya kithiolojia ya neno “chini” kama stiarai ya kifo. Kuzimu ilikuwa chini, bali mbingu ilikuwa juu. Katika kipindi chetu cha sasa hizi stiari maalum zinaonekana kutokuwa sahihi, lakini kumbuka hizi ni stiari za kale ambazo kamwe haikukusudia kubeba uhalisia. Lugha ya Agano la Kale nila kifenomenolojia, ambapo inaamaanisha lugha ya ubainishaji kwa kutumia milango mitano ya fahamu ya mwanadamu. Biblia haiku kinyume na Sayansi, ilikuwepo kabla ya sayansi! Kuzichukua stiari za kale kifasihi si ishara ya kiutamaduni, bali ni kuikosa maana halisi ya mpangilio wa kihistoria wa waandishinwalio vuviva iliokusudiwa.

▣“**hukumu na haki**” Angalia maelezo katika 32:16.

### 33:6

**NASB, NKJV,**

**NRSV**           “**atakuwa utuluvu wa nyakati zenu**”

**NJB**           “**mnahesabu siku zenu zote katika hili**”

**Peshitta**       “**imani itakuwa utulivu wa nyakati zenu**”

**REB**           “**nguvu zake zitakuwa katika utulivu usiobadilika**”

YHWH huteta “utulivu,” kif. “uaminifu,” BDB 53, kama vile 25:1. Tumaini na utulivu wa Yuda ndiyo sifa ya Mungu wake (kama vile Kumb. 32:4; Zab. 36:5; 89:1-2,5,24,33,49; 88:11; 92:2; 143:1). Hili ni jibu la maombi ya mst. wa2. Kwa sababu ya sifa yake ya uaminifu yeye huwapa watu wake walio wakaidi

1. wingi (BDB 340) wa
  - a. wokovu (BDB 447)
  - b. hekima (BDB 315 pamoja na mabadiliko ya kudumu kutoka **ن** na kuelekean kama vile 11:2)
  - c. maarifa (BDB 395, kama vile 11:2)
2. uchaji (BDB 432, katika maana ya kuheshimishasana. 11:2; Mit. 1:7,29; 2:5) wa YHWH ndiyo hazina yake (BDB 69, katika maana ya ghara, kama vile I Nya. 27:27-28; II Nya. 11:11)

**33:7-9** Kifungu hiki kinadokeza hali ya huzuni ya wavamizi kwa sababu makubalianao yao yameshidwa (kama vile II Fal.18:13-16).

**33:7**Hii mistari miwili ya kiushairi si ya maana zinazokaribiana. Wasomi wa kibiblia wakuwa wakishawishiwa na by Robert Lowth, ambaye alijaribu kuhusianisha ufanano wa Kiebrania katika vipengele vitatu au vinne. Katika halia ya sasa wasomi wanalewa ufananoa mwingi wa kiushairi. Kwa sasa ni bora kusema kwamba mstari wa pili “unaongeza” au “unaenda zaidi” (Adele Berlin, *The Dynamics of Biblical Parallelism: Revised and Expanded*, uk. 64).

Makundi mawili tofautitofauti yanaeleza

1. mstari wa kwanza – wanajeshi wa Yerusalem
2. mstari wa pili – mjambe wa amani aliyetumwa na Hezekia huko Misri (kama vile mst . wa 8)

Hii inatenda kazi sawasawa/mambo yanayofanana

–“lieni,” BDB 858

–“ombolezeni,” BDB 113

Ufanano ni moja ya misingi mikuu katika kuufasiri ushairi wa Kiebrania,lakini yatupasa kutambua kuwa huu unatumika katika mifumo mingi na katika viwango vingi.

**33:7“watu mashujaa”** Kwa hakika kipengele hiki kinahusiana na mziziariel, (NJB, kama vile 29:1,2,7; 31:9).

**33:8**

**NASB, NKJV, Peshitta “miji”**

**NRSV, DSS** “viapo”

**NJB, RSV** “mashahidi”

**REB** “mikataba”

**TEV** “makubaliano”

Toleo la MT lina kifungu “miji” (מִיְרָע, BDB 746), lakini kwa bababu ya ufanano, neno “mashahidi” (מִשְׁחָהִידִי, BDB729) linaendana sana. Huu unaweza kuwa mkanganyiko mwingine wa “R” – “D”. Toleo la UBS Hebrew Text Project linalipa neno “ushahidi” daraja C (yaani, wasiwasi wenye kufikirika).

**33:9** Mstari huu unatumia stiari ya kilimo kueleza matatizo yaliyowakumbawamizi wa ki-Ashuru juu ya Yerusalem mnamo 701 K.K..Hizi aina za stiari za kilimo ni za kawaida katika Isaya (kama vile 16:8; 24:4,7).

YHWH huitawala hali ya hewa kwa makusudi yake (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-28). Hakuna tofauti kati ya neno “asili” na “nguvu ya asili” katika Biblia,kama ilivyo katika Mashariki ya Karibu ya Kale. Uungu umehusishwa kwa ukaribu sana katika uumbaji wake. Iweni makini na usasa wenu, mtazamo wa ulimwengu wa kisayansi wa thiolojia ya kimtandao kuhusiana na Maandiko!

**33:10-12** Kwa namna iliyo dhahiri kipengele hiki kinahusianisha Ashuru kama katika mst. wa 1.

**33:11-12** Taswira ya neno “makapi” na “moto” ni ya kawaida katika Isaya (kama vile 1:7;5:24; 9:18-19; 10:16-19;26:11; 29:6; 30:27-28; 33:11-14; 47:14, pia Yoeli 2:3). Angalia Mada Maalum :Moto katika 1:31.Isaya anatumia taswira kutokana na uzalishaji wa mwanadamu.

1. hapa, mwanzo, BDB 247 I, KB 255, *Qalya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, 8:3; 26:18; 59:4,13
2. kuzaa, 9:6; 13:8; 21:3; 23:4;26:17,18; 39:7; 51:18; 54:1; 59:4; 66:7,9}

▣“**pumzi yenu** ”Hili ni nenoruah(BDB 924) linalotumika kama stiari ya lugha ya kibinadamu kumaanisha upepo wa hukumu kutokana na matundu ya pumzi ya YHWH (angalia Mada Maalum katika 6:1). Kwa mtazamo ulio dhahiri hii ni stiari ya ushiriki binafsi wa YHWH(kama vile Kutoka 15:18; II Sam. 22:16; Zab. 18:15) katika hukumu (kama vile 11:4; 30:28; 40:7).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:13-16**

<sup>13</sup>Sikieni, ninyi mlion mbali, niliyoyatenda;

na ninyi mlion karibu, kirini uweza wangu.

<sup>14</sup>Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa;

tetemeko limewashika wasiomcha Mungu;

Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao;

ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele?

<sup>15</sup>Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili;

ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma;

akung'utaye mikono yake asipokee rushwa;

azibaye masikio yake asisikie habari za damu;

afumbaye macho yake asitazame uovu.

<sup>16</sup>Huyu ndiye atakayekaa juu; majabali ni ngome yake;

atapewa chakula chake;

maji yake hayatakoma.

**33:13“ninyi mlion mbali . . . ninyi mlion karibu”** Katika muktadha, kipengele hiki kinawarejelea watu wa Mungu waliohamishiwa Ashuru na watu wa Mungu ambaa bado wapo katika Yuda (kama vile Dan. 9:7). Hata hivyo,

jambo hili linaonekana katika muktadha mpana wa zama mpya, hili linaweza kuhusiana na Mataifa na watu wa Kiyahudi (kama vile 49:1; hii ni nahau ya wote, kama vile Yer. 25:26).

**33:14 “Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa”** Tena ukweli kuhusu mchanganyiko wa waaminifu na watenda dhambi mionganoni mwa watu wa Mungu unatambuliwa. Wenye dhambi

1. wanaogopa, BDB 808, KB 922, *Qal ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile NOMINO- 2:10,19,21; 24:17,18; KITENZI 12:2;19:16,17; 44:8,11; 51:13
2. tetemeko limewashika wasiomcha Mungu, BDB 28, KB 31, *Qal ya KAULI ISIYO TIMILIFU*, kama vile 13:8; 21:3

Hawa “wasiomcha Mungu” (BDB 338) wanaelezwa katka 32:6 kama wale wanaotenda matendo yasiyo ya ki - Mungu na wanazungumza mabaya dhidi ya Bwana (kama vile 9:17; 10:6).

□“**kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao  
ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele”**

Kifungu hiki kinaurejelea utakatifu wa Mungu kama inavyoonekana katika stiari ya moto iliyounganishwa na haki na hukumu zake (kama vile Kumb. 4:24; 5:24; Isa.30:27,30).Kwa neno “kukaa” (kif. “milele”) anagalia Mada Maalum katika 32:14.

**33:15** Kipengele hiki kinaakisi tabia yaYHWH kama inavyoonekana ndani ya watu wake.

1. aendao kwa haki
2. anenaye maneno ya adili
3. ni yeye anayedharau
4. asipokee rushwa
5. asisikie habari za damu (yaani, kumwaga damu)
6. asitazame uovu

**33:16** Mtu anayeishi maisha kama haya anaelezwa katika mst. wa15

1. atakayekaa juu
2. majabali ni ngome yake
3. atapewa chakula chake
4. maji yake hayatakoma

Kipengele hiki kinamfafanua mtu wa zama mpya. Ukweli wa Kumbukumbu la Torati unathibitika!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 33:17-24**

<sup>17</sup> Macho yako yatamwona mfalme katika uzuri wake,  
yataona nchi iliyoenea sana.

<sup>18</sup> Moyo wako utatafakari hofu ile;  
Yuko wapi yeye aliyehesabu? Yuko wapi yeye aliyeupima ushuru?

Yuko wapi yeye aliyeihesabu minara?

<sup>19</sup> Hutawaona watu wale wakali;  
watu wa maneno magumu usiyoweza kuyafahamu;  
wenye lugha ya kigeni usiyoweza kuelewa nayo.

<sup>20</sup> Angalia Sayuni, mji wa sikukuu zetu;  
macho yako yatauona Yerusalemu umekuwa kao la raha;  
hema isiyotanga-tanga; vizingi vyake havitang'olewa, wala kamba zake hazitakatika.

<sup>21</sup> Bali huko Bwana atakuwa pamoja nasi, mwenye adhama;  
mahali penye mito mipana na vijito, pasipopita mashua na makasia yake;  
wala hapana merikebu ya vita itakayopita hapo.

<sup>22</sup> Kwa maana Bwana ndiye mwamuzi wetu;  
Bwana ndiye mfanya sheria wetu; Bwana ndiye mfalme wetu;  
ndiye atakayetuokoa.

<sup>23</sup>Kamba zako zimelegea;  
 hawakuweza kukaza sana shina la mlingoti wao;  
 hawakuweza kulikunjua tanga;  
 ndipo mapato ya mateka yaligawanywa, hata wachechemeao walipata mateka.  
<sup>24</sup>Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa;  
 watu wakaao humo watasamehewa uovu wao.

**33:17**“**Macho yako yatamwona**”Hiki KITENZI (BDB 302, KB 301) mara nyingi kinatumika kurejelea utambuzi wa kiroho (kama vile 26:11; 33:17,20; 48:6; Ayubu 23:8-9; Zab. 46:8; 63:2). Wanadamu Waliombwa kutenda kazi katika falme mbili.

1. ufalme unaonekana (yaani, *nephesh*, sayari hii)
2. ufalme wa kiroho (yaani, *ruah*, ushirika na Mungu)

Anguko la Mwanzo 3 limeharibiwa katika vipengele vya falme zote!

▣“**mfalme katika uzuri wake**”Huu ni utata uliokusudiwa, mwingi kama 32:1, ambapo muktadha unaendana na nyakati zote, nyakati za Hezekia na kuja kwa Masihi wa 7:14.

**33:18**“**Yuko wapi yeye aliyehesabu**”Kipengele hiki kinairejeleawakaidi waAshuruwaliokuwa wakiipeleleza Yerusalem kwa ajili ya ujio wa wavamizi.

**33:19**“**watu wa maneno magumu**”Kifungu hiki kinairejelea lugha ya Ashuru (kama vile 28:11).

**33:20** Hii ni thiolojia ya Isaya kwamba kamwe Yerusalem haitaanguka (kama vile Isaya 36-37). Kwa mjadala kamili kuhusu mji” angalia maelezo katika 24:10 na jedwali katika Utangulizi wa sura ya 26, D. Huu unabii lazima ueleweka katika muktadha kwa sababu nyakati za Yeremia, Mungu uliwapa unabii kinzani hasa.Taswira ya “hema” ni dokezo lililopitwa na wakati lenye kurudia maandiko ya kitabu cha Kutoka.Pia kifungu hiki kinaweza kudokeza “kibanda” kilichojengwa kwa hema rahisi. Hili dokezo linalofanana (yaani, hema) linatumika katika 54:2 kwa ajili ya upana ya kiulimwengu.

**33:21** Hii stiari ya neno “mitona merikebu” inaonekana kuwa masihara juu ya umoja wao na Misri (kama vile mst. wa 23). Badala ya Misri, YHWH (Mwnye Adhama) atakuwa mtoaji na mlinzi (kama vile mst. wa 22).

**33:22** Yerusalem (kama vile mst. wa 20) kwa mara nyingine ni mji wa Mfalme Mkuu (YHWH Mwenyewe) kama alivyowasilisha katika ondoleo lake la haki (Masihi wa uzao wa Daudi).

**33:23**Huu ushahiri ni wa kiutata. Kipengele hiki kinaweza kurejelea

1. maangamizi ya Ashuru
2. kuiwezesha Yerusalem
3. au vyote

Katika mst. wa17, vifungu “macho yako” na “yataona” vyote vya utangulizi. Msrtari wa18 unaonekana kuirejelea Ashuru ambayo ilikuwa inaikagua Yerusalem kwa ajili ya uvamizi na upinzani. Mstari wa19 unaonekana kudokeza sauti za lugha ya wavamizi wa Ashuru. Bado katika mst. wa20 tendo linabadilika na kuwa Yerusalem isiyo na maangamizi. Hivyo, mist.ya 21na 22 ingeweza kuirejelea Yerusalem, kwa namna iliyo dhahiri mst.24 unafanya hivyo. Wengine wanaona tendo la “utekaji nyara” (BDB 1021) katika mst. 23 kama lenye kuhusiana na vitu ambavyo Ashuru ilivisambaratisha kabla ya kuta za Yerusalem mnamo 701 K.K. na si gunia la Ninewi yenyewe, mnamo612 K.K.

**33:24** YHWH anabainishwa kama msikilizaji. Hili ni dokezo la sura ya 1 ambapo watu wa Mungu wanachorwa kama wagonjwa (kama vile mst. wa 1:5-6). Ugonjwa ni stiari ya “dhambi” na “uasi” (kama vile Zab. 41:4; 103:3; Isa.53:5). Agano Jipyaa linaendeleza dhana ya Kiyahudi ya ugonjwa kwa kuhusianisha na dhambi(kama vile Yohana

5:14; Yamkobo 5:14-15). Hili neno “okoa” katika Agano la Kale linadokeza ukombozi wa kimwili (angalia Mada Maalum katika 33:2).

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana..

1. Ni kwa namna gani sura za 32 na 33zinahusiana na 28-31?
2. Je! Hizi sura mbili ni za ki-Masihi au ni za kihistoria?
3. Orodhesha baraka za Roho zinazoelezwa katika 32:15-18.
4. Toa muktadha wa kihistoria wa 33:7-9

## ISAYA 34

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ghadhabu ya Mungu dhidi ya Mataifa	Hukumu juu ya Mataifa	Mwisho wa Kutisha wa Maadui wa Mungu	Mungu Atawaadhibu Maadui zake	Hukumu juu ya Moabu
34:1-15 (1-4)	34:1-4 (1-4)	34:1-17 (1-4)	34:1-4	34:1-17 (1-4)
	34:5-7 (5-7)	(5:7)	34:5-8	(5-8)
34:8-15	(8:12)	(8-12)		
34:9-15	(9-11) (13-15)			
34:16-17 (16a-17)	34:16-17 (16 -17)		34:16-17	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufutilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

- 3. Aya ya kwanza
- 4. Aya ya pili
- 5. Aya tatu
- 6. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Isaya 34 na 35 zinafanana sana na sura ya 24-27. Zote hizi ni mchanganyiko wa vipengele vya hukumu na baraka ambavyo ni hitimisho kwa muungano wa kifasihi ulio mrefu.
  - 1. Isaya 34 inazungumzia hukumu ya ulimwengu katika maneno ya kitakwimu.
  - 2. Isaya 35 inazungumzia urejesho wa kiulimwengu katika namna iliyorembeshwa, katika maneno ya kimafumbo.
- B. Kwa sababu kuna nafasi zilizojirudia mara mbili kati ya sura ya 33 na sura ya 34 katika Magombo ya kale ya Nahari ya Chumvi ya nakala zalsaya, inawezekana kwamba huu muungano wa kifasihi (sura za 34-35 na 38-39) lazima ziendane na 66 (kama ulivyo muktadha wa kifasihi). Sura ya 35 ni

mjadala wa zama mpya, siku ya urejesho. Hizi zinaelezea kile ambacho YHWHalikusudia kufanya na mwanadamu kabla ya Anguko la mwanzo 3 na kutotii kwa uzao wa Ibrahimu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 34:1-15

- <sup>1</sup> Karibuni, enyi mataifa, mpate kusikia; sikilizeni, enyi kabilia za watu; dunia na isikie, nacho kijazacho, ulimwengu na vitu vyote viutokavyo.
- <sup>2</sup> Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote, hasira kali juu ya jeshi lao lote; amewaaangamiza kabisa, amewataoa waende kuchinjwa.
- <sup>3</sup> Watu wao waliouawa watatupwa nje, na uvundo wa maiti zao utapaa juu, na milima itayeyushwa kwa damu yao.
- <sup>4</sup> Na jeshi lote la mbinguni litafumuliwa, na mbingu zitakunjwa kama karatasi, na jeshi lao lote litanyauka kama vile jani la mzabibu linyaukavyo na kupukutika, na kama jani la mtini linyaukavyo na kupukutika.
- <sup>5</sup> Maana upanga wangu umekunywa na kushiba mbinguni; tazama, utashukia Edomu, na juu ya watu wa laana yangu, ili kuwahukumu.
- <sup>6</sup> Upanga wa Bwana umeshiba damu, umenona kwa unono, kwa damu ya wana-kondoo na mbuzi, kwa mafuta ya figo za kondoo waume; maana Bwana ana dhabihu huko Bozra, machinjo makubwa katika nchi ya Edomu.
- <sup>7</sup> Na nyati watatelemka pamoja nao, na mahasai, na nchi yao italewa kwa damu, na mavumbi yake yatanoneshwia kwa shahamu.
- <sup>8</sup> Maana ni siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, ili kushindania Sayuni.
- <sup>9</sup> Na vijito vyake vitageuzwa kuwa lami, na mavumbi yake yatageuzwa kuwa kiberiti, na ardhi yake itakuwa lami iwakayo.
- <sup>10</sup> Haitazimwa mchana wala usiku, moshi wake utapaa milele; tangu kizazi hata kizazi itakuwa ukiwa; hapana mtu atakayepita kati yake milele na milele.
- <sup>11</sup> Kaati na nungu wataimiliki, bundi na kunguru watakaa huko, naye atanyosha juu yake kamba ya ukiwa na timazi ya utupu.
- <sup>12</sup> Watawaitia wakuu wake ufalme, lakini hawatakuwapo; wakuu wake wote wamekuwa si kitu.
- <sup>13</sup> Miiba itamea majumbani mwake, upupu na mbigili ndani ya maboma yake; nayo itakuwa kao la mbweha, na ua la mbuni.
- <sup>14</sup> Na hayawani wa nyikani watakutana na mbwa-mwitu, na beberu anamwita mwenziwe; naam, babewatoto anakaa huko na kujipatia raha.
- <sup>15</sup> Huko pili atafanya kioto chake na kuzaa na kuotamia, na kukusanya watoto wake katika kivuli chake; naam, huko watakusanyika tai, kila mmoja na mwenzake.

**34:1** Katika mstari huu kuna masharti kadhaa.

1. karibu, BDB 897 I, KB 1132, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. kusikia, BDB 904, KB 1151, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
3. sikilizeni, BDB 1033, KB 1570, *Qalya* KAULI AMRISHI

Ukuu wa ulimwengu unaeleza uumbaji wake na kutangaza hukumu yake.

1. “enyi mataifa,” BDB 156, kama vile mst. 2; 43:9
2. enyi kabilia za watu, BDB 522, kama vile 17:12; 43:9

3. dunia, BDB 75, kama vile 37:16,20; Mwa. 18:18; 22:18; Mika 1:2
4. mataifa yote, BDB 571, kama vile 6:3
5. ulimwengu, BDB 385, kama vile 13:11; 24:4
6. vitu vyote viutokavyo, BDB 481 TUNGO BDB 425

Kwa uwazi kipengele hiki kinarejelea juu ya ulimwengu ule wa siku za Isaya unaojulikana,lakini lugha ni ya kiulimwengu.

**34:2 “Maana Bwana ana ghadhabu juu ya mataifa yote. . . amewaangamiza kabisa”** Hili wazo la “amewaangamiza kabisa” (BDB 355 I, KB 353, *Hiphil yaKAULI YA WAKATI TIMILIFU*) linairejelea dhana ya “vita takatifu.”

Katika kitabu cha Yoshua dhana hii yenye uhusiano na Yeriko inatafsiriwa kama “chini ya kizuizi” (yaani, iliyoelekezwa kwa YHWH kumaanisha maangamizi, kama vie Yoshua. 6:17,18 [mara tatu]; 7:1 [mara mbili], 12 [mara mbili], 13 [mara mbili], 15).

**34:3** Mstari huuinapanua wazo la mst. 2, kupitia stiari za kitakwimu za vita ya wenyewe kwa wenyewe.

1. wao waliouawa watatupwa nje, BDB 1020, KB 1527, *Hophal ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*
2. na uvundo wa maiti zao (kifasihi. “kupanda”) utapaa juu, BDB 748, KB 828, *Qal ya KAULI ISIYO TIMILIFU*, kama vile Amosi 4:10
3. na milima itayeyushwa (kifasihi. “itatoweka”) kwa damu zao, BDB 587, KB 606, *Niphalya WAKATI TIMILIFU*

Kipengele hiki kinaakisi tendo la mapigano ambapo miili ya wafu imekaa kwa muda mrefu.

Katika ANE maziko ya mfalme yalikuwa ya kutisha na hayakuwa ya hadhi na yangeweza kumwathiri mtu mwingine baadaya kuondoka duniani.Hii ilimaanisha kushindwa moja kwa moja, kimwili na kiroho.

**34:4** Lugha hii ya kiuchochesi yenye kuhusiana na mzunguko wa jua na mwezi ndiyo dhana ya sasa katika Biblia.

1. Isaya 13:13; 34:4; 51:6
2. Ezekiel 32:7,8
3. Yoeli 2:31
4. Mathayo 24:29
5. II Petro 3:10
6. Ufunuo wa Yohana 6:12-14; 20:11

Hiki kifungu “jeshi la mbinguni” kinaweza kujrejelea juu ya

1. miungu ya kinajimu (jua, mwezi, nyota, sayari, vimondo,n.k.)mara nyingi ilihusiana na Babeli
2. jeshi la kimalaika (kama vile 24:21-22; Yoshua. 5:14-15, lilijikita katika Kumb. 32:8 katika LXX na linalelezwa katika Danieli 10)

Katika muktadha huu hii inarejelea vitu Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.

▣“**zitakunjwa kama karatasi**” Taswira hii inatumwa na Yohana katika Ufu. 6:14. Katika Mashariki ya Karibu ya Kaleanga lilifikiliwa kuwa kama(1) ngozi iliyokunjwa na kugandamizwa juu ya dunia kama bakuli (kama vile Isa. 40:22) au (2) hema lililosimikwa (kama vile Zab. 104:2). Ule mpangilio wa kale uliondolewa na ule mpya (kama vile Ufu. 21:1).



<b>NASB, NRSV</b>	“ <b>mzabibu</b> ”
<b>NKJV, TEV</b>	“ <b>anguka</b> ”

KITENZI hiki (BDB 615, KB 663) kimejitokeza mara tatu ndani ya mstari huu.

1. *Qal* cha KAULI ISIYO TIMILIFU
2. *Qal* cha TUNGO YA KITENZI JINA
3. *Qal* cha KAULI TENDAJI ENDELEVU

Pia kitenzi hiki kinajitokeza katika ufanano wa muungano wa kifasihi katika sura 24-27 (kama vile 24:4 [marfa mbili]). Pia uzalishaji wa mazao utatikiswa katika siku hii ya kuja kwa muumbaji! Tunaweza kusema mbingu nan chi vyote vitakuwa pembani wakati Muumbaji atakapokuwa anatekeleza amri /Hukumu kwa sababu hivyo,navyo, vimeathiriwa na dhambi ya mwanadamu (kama vile Mwa. 3:17-19; Rum. 8:19-22).

**34:5 “utashukia Edomu”** Edomu ndiyo iayotajwa tu kwaajili ya hukumu katika mchanganyiko huu wa kifasihi kama Moabu ilivyotajwa pekee katika Isa. 25:10-12. Hapa Edomu (kama Moabuhapo awali) ni ishara ya mataifa yote yaliyo na chapa ya majivuno dhidi ya Mung.

**34:6-7** Mistari hii inatumia stiari za dhabihu(kama vile BDB 830, kama vile Yer. 50:27; 51:40; Eze. 39:17-20) kueleza juu ya hukumu ya YHWH

1. damu ya wana-kondoo na mbuzi, mst. 6
2. mafuta ya figo za kondoo waume, mst. 6
3. mahasai,mst. 7

Sio tu wanyama wafugwao pekee wanapaswa kutolewa dhabihu, bali hata wanyama wa mwituni (BDB 910). Taswira ya upanga waYHWH pia inapatikana katika Kumb. 32:41-42 na Eze. 21:28-32.



**NASB**           “yatanoneshwā kwa shahamū”

**NKJV**           “yanayotiririka mafuta”

**NRSV, REB,**

**LXX**           “yenye kuenea mafuta”

**NJB**           “yalijaa mafuta”

KITENZI hiki (BDB 206, KB 234, *Hothpaēl* cha KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinapataikana hapa pekee katika shina hili adimu. Hiki kinadokeza dhana yenye kubadilika, “upanga waYHWHumejilisha wenyewe.” Hii *Pual* ya KAULI ISOO TIMILIFU ya KITENZI kile kileinapatikana katika mst. 7, “yatanoneshwā kwa shahamū.” Vyote vinazungumza juu ya idadi kubwa ya waathiriwa wa upanga wa dhabihu (stiari ya jeshi la maadui waliokufa). Mafuta ya viumbe wadogo yalikuwa sehemu ya mnyama juu ya madhabahu.

**34:8** Sisi kama wafasiri yatupasa kukumbuka asili ya ushahiri wa Kiebrania ni

1. ni muundo uliofupishwa
2. utamkaji wa suti
3. ufanano wake

Wanamagharibi wanaelekeea kuwa wanafikra wa Kigiriki, wanafasihi wa kimantiki! Hata hivyo, hii ni fasihi ya ushairi wa kale wa mashariki. Angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura ya5, “Hebrew Idiom and Hebrew Thought,” kr. 107-117. Pia hii ni kweli ya Mwanzo 1-2. Angalia John L. Walton, *The Lost World of Genesis 1*.

Mstari huu ni mfano mzuri sana, “siku,” mstariwa 1 unafanana na neno “mwaka,”mstari wa 2. Hii haimaanishi kuwa ya muda mfupi, maoni ya kihistoria, bali utambuzi ambao wakati wa hukumu na uwajibikaji kwa Mungu unakuja! Ni kwa muda kipindi kitachukua muda hili si tatizo.

**34:9 “lami. . . kiberiti. . . kiberiti”** Hivi (BDB 278, 172, 278/128) ni vidokezo vyta maangamizi ya Sodoma Gomora katika Mwa. 19:24. Pia, angalia ufanano wa muhimu katika Yer. 49:17-18.

Sodomana Gomora ziko katika eneo la kaskazini mwa Edomu (yaani, kusini mwa ukingo wa Bhari ya Chumvi).

**34:10** Hii ni lugha ya kimubaraghya ambayo inadokeza maangamizi kamili ambayo yanaendelea katikaubaadaye usio na kikomo (kama vile 1:31; 13:20; 66:24).

Kuna maneno mawili ya neno “milele” lilitotumka.

1. mstariwa 2, עולם (BDB 761, angalia Mada Maalum katika 32:14)
2. mstari wa 4, בָּצָח (BDB 664, kama vile II Sam. 2:26; Isa. 13:20; 25:8; 28:28; 33:20; 57:16)

Hiki kifungu "moshi wake utapaa milele" unatumika katika Ufu. 14:11na 19:3. Inaonekana kwamba huenda (1) "Moabu" katika 25:10-12; (2) Edomu katika muktadha huu; na(3) "Babeli" katika Ufunuo wa Yohana yote haya yanasisimama kumaanisha "jamii ya mwanadamu iliyokusanyika na yanayotenda kazi mbali na Mungu auhata katika uasi dhidi ya Mungu."

Kwa mjadala ulio mzuri wa matumizi ya kibibliawa neno "milele" angalia D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*, kr. 98-101.

**34:11-15** Kuna wanyama wengi(hasa wamyama) walijotajwa katika kipengele hiki. Hawa wote si safi kulingana na Mambo ya Walawi 11. Hawa wanyama wa aina moja wasio fanana wanaonekana katika magamba ya mji wa Babeli (kama vile 13:19-22). Kuna fasiri mbili za kipengele hiki: (1) haya magamba ni ishara za juhudzi za mwanadamu aliyehu na kuangamizwa na Mungu ili pasiwepo kitu bali wanyama walioishi hapa au (2) miji hii sasa ni ilimilikiwa na mapepo (kama vile Mt. 12:43). Tafsri za kisasa kama NEB limeonyesha ushahidi dhahiri wa matukio ya kale ambao unaweza kuwarejelea mapepo (kama vile hasa mst. 14).

- |         |                   |
|---------|-------------------|
| 1. NASB | "mwenye manyoya"  |
| NKJV    | "mbuzi-mwitu"     |
| NRSV    | "mbuzi wa kipepo" |
| TEV     | "pepo"            |
| NJB     | "zimwi"           |
| REB     | "beberu"          |

Hili neno (BDB 972 III) linarejelea

- a. sanamu (kama vile II Nya. 11:15)
- b. mapepo (kama vile Law. 17:7)
- c. wanyama wa mwituni (kama vile Isa. 13:21)

- |              |                    |
|--------------|--------------------|
| 2. NASB, TEV | "jitu jeusi"       |
| NKJV         | "kiumbe cha usiku" |
| NRSV, NJB    | "jitu la usiku"    |
| REB          | "kapu la usiku"    |

Katika dini ya Kiyahudi iliyofuatia (BDB 535) hili neno lilibadilika kuwa jina la wale wawashawishio wanaume usiku wa manane. Asili ya neno hili na dhana hii inaweza kuwa pepo watatu wa usiku wa manane wenye asili ya ki-Akkadia (KB 528). Toleo la Peshitta linalitambua hili kama "kelele za bundi" Usiku wa manane na mambo yake yote "asili ya sauti" viliwaogofya watu.

## MADA MAALUM: PEPO WABAYA KATIKA AGANO LA KALE

- A. Uhusiano kamili kati ya malaika walioanguka na pepo wabaya haujulikana. I Enoch anadai kwamba *Nephilim* ya kitabu cha Mwanzo 6:1-8 ndicho nchanzo cha uovu (walimu wengi wa Kiyunani pia wanajikita katika Mwanzo 6 na si Mwanzo 3). I Enoch anasema kwamba hawa nusu malaika/nusu viumbi vya kibinadamu waliuwawa kwa gharika (pia anadai kwamba kifo chao kilikuwa sababu ya gharika), na sasa roho zao zisizoonekana zinatafuta mwili wa kuishi. Kifungu kinatia shauku, lakini si cha kiufunuo (yaani, hakijavuviwa).
- B. Kuna roho zinazopingana au pepo nzilizotajwa katika Agano la Kale.
1. *Satyrs* au "wenye manyoya," huenda ni pepo wenye kuonekana katika umbo la mbuzi (BDB 972 III, KB 1341 III) – Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14
  2. *Shedim* (BDB 993, KB 1417) – Kumb. 32:17; Zab. 106:37, kiuembe ambaye sadaka zilitolewa kwa ajili yake (ni sawa na Molech)
  3. *Lilith*, pepo la kiume la usiku (BDB 539, KB 528) – Isa. 34:14 (sehemu ya hadithi za Babeli na Ugariti)
  4. *Azazel*, pepo la madai (jina la pepo mkuu katika I Enoch, kama vile 8:1; 9:6; 10:4-8; 13:1-2; 54:5;

- 55:4; 69:2) – Law. 16:8,10,26 (BDB 736, KB 806)
5. Zaburi 91:5-6 ni viashiria vya mapigo (kama vile Zab. 91:10), Sisi viumbe vya kiroho (kama vile Wimbo Ulio Bora 3:8)
  6. Isaya 13:21 na 34:14 inaorodhesha wanyama wa jangwani kama njia ya kuonyesha huzuni ya mahali palipoangamizwa. Wengine wanadai kwamba hii orodha inahusisha pepo wabaya ili kutoa kielezo cha maeneo haya yaliyoangamizwa kuwa pia ni maeneo yanayokaliwa na viumbe vingine (kama vile Mt. 12:43; Luka 11:24; Ufu. 18:2)
- C. Imani ya Agano la Kale inayohusu Mungu mmoja (angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu mmoja) ilinyamazisha na kuboresha ngano za mataifa ya kipagani, lakini mara nyingine majina na nyadhifa za ushirikina wao zinarejelewa (hasa maandiko ya kiushairi). Ukweli wa hizi roho za uovu ni sehemu ya uhusiano endelevu na sehemu hii inaendelea katika Agano Jipyä kupewa uhusika kama mtu /malaika wa Shetani (angalia Mada Maalum: Shetani) na wafiasi wa roho yake (yaani, pepo wabaya)

**34:11** Hili neno lilitotfsriwa kama “huzuni” (BDB 1062, kama vile 24:10) na “utupu” (BDB 96) yote yanatumika katika Mw. 1:2 kueleza juu ya machafuko ya awali ya sari hii. Edomu (yaani, mataifa yote ya uasi) itapunguzwa hadi kuondolewa katika uhalisia wa machafuko(yaani, 13:9-11; Yer. 4:23-26).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 34:16-17**

- <sup>16</sup>Tafuteni katika kitabu cha Bwana mkasome;  
 hapana katika hao wote atakayekosa kuwapo,  
 hapana mmoja atakayemkosa mwenzake;  
 kwa maana kinywa changu kimeamuru, na roho yake imewakusanya.  
<sup>17</sup>Naye amewapiglia kura, na mkono wake umewagawanya kwa kamba;  
 wataimiliki hata milele,  
 watakaa ndani yake kizazi hata kizazi.

**34:16** “Tafuteni katika kitabu cha Bwana mkasome” Isipokuwa mst. 1, hakuna KAULI SHURUTISHI katika sura hii kabla ya mstari huu. Wito wa YHWH wa kuwaita ili wamkaribie na kumsikiliza katika mst. 1 (KAULI SHURUTISHI mbili) unahusianishwa kwa KALI SHURUTISHI mbili ambazo zinafunga sura hii (mbinu ya kawaida ya fashihi y ki-Semiti).

1. tafuteni, BDB 205, KB 233, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
2. mkasome, BDB 894, KB 1128, *Qalya* KAULI SHURUTISHI

Mataifa yameondoa ule mamlaka aliopewa mwanadamu katika Mwanzo 2, hivyo kiUungu wanyama wameteuliwa kwa ajiliya nchi!

Kumekuwa na maoni mengi kuhusu kitabu hiki (BDB 706). Wengine wanaonakuwa hii ni kumbukumbu ya hukumu (kama vile 29:11,12; 30:8). Wengine wanaona uwa hili ni dokezo la vile vitabu viwili vilivyotajwa katika Dan. 7:10; 12:1 na Ufu.20:4-15, ambavyo viko katika namna ya kistiari kwa ajili ya kumbukumbu ya Mungu.

1. “kitabu cha uzima”
  - a. Kut. 32:32
  - b. Zab. 69:28
  - c. Isa. 4:3
  - d. Dan. 7:10; 12:1  
 Luka 10:20
  - e. Flp. 4:3
  - f. Ebr. 12:23
  - g. Ufu. 3:5; 13:8; 17:8; 20:12,15; 21:27
2. Kitabu cha sheria/kumbukumbu
  - a. Zab. 56:8; 139:16
  - b. Isa. 65:6
  - c. Dan. 7:10

- d. Mal. 3:16
- e. Ufu. 20:12-13

■“**hapana katika hao wote atakayekosa kuwapo;**

**hapana mmoja atakayemkosa mwenzake.**

**kwa maana kinywa changu kimeamuru**” Hapa tunazo sitiari mbili ambazo zinairejelea nguvu ya upanga wa Mungu. Ya kwanza ni sitiari ya kijeshi, ambapo ya pili ni ya nyumbani. Mungu anapozungumza, iinaweza kujumuishwa (kama vile 24:3; 25:8; 55:10-11).

■“**roho yake imewakusanya**” Angalia maelezo na Mada Maalum katika 11:2; 32:15-20. Mungu huwakusanya wanyama/mapepo waliorodheshwa katika mist. 11-15.

**34:17** Hili ni dokezo la ule ugawaji wa ardhi kwa usawa (yaani, Urimuna Thummim)katika Yoshua 12-19. Hii ni njia ya kale ya kueleza kwamba agano limerudishwa upya na limedumishwa!

## ISAYA 35

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Furaha ijaو ya Sayuni	Utukufu ujaو wa Sayuni	urejesho wa Sayuni	Njia ya Utakatifu	Shangwe ya Yerusalem
35:1-10 (1-10)	35:1-7 (1-2) (3-4) (5-7)	35:1-10 (1-2) (3-4) (5-7)	35:1-10 (1-2) (3-4) (5-7)	35:1-10 (1-7)
	35:8-10 (8-10)	(8-10)	(8-10)	(8-10)

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuvia, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

7. Aya ya kwanza
8. Aya ya pili
9. Aya ya tatu
10. Nk

### **UTAMBUZI WA KIMUKTADHA**

- A. Sura hii kwa wazi ni marudio ya Sura ya 34.
- B. Swali ni kwamba anaelezewa nani na lini.
  1. Je hii inarejelea uzuri wa kilimo katika nchi ya ahadi Nyakati za mwisho (yaani., waamini waminifu wa Kiyahudi na watu wa mataifa?)
  2. Je hii inarejelea kurudi kwa mateka wa Kiashuru Palestina (yaani ., Israeli)?
  3. Je hii inarejelea amri iliyotolewa na Koreshi ya kurudi kwa mateka kutoka uhamishoni Babeli (yaani ., Yuda)?
  4. Je hii inarejelea jangwa lililoko kati ya Mesopotamia na Palestina lililogeuzwa kuwa njia kwa ajili ya watu wa Mungu kurudi Palestina?

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 35:1-10**

<sup>1</sup> Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi;

jangwa litashangilia na kuchanua maua  
kama waridi.

<sup>2</sup>Litachanua maua mengi,  
na kufurahi, naam, kwa shangwe na kuimba;  
litapewa uzuri wa Lebanoni,

utukufu wa Karmeli na Sharoni;

watauona utukufu wa Bwana,

ukuu wa Mungu wetu.

<sup>3</sup> Itieni nguvu mikono iliyio dhaifu, yafanyeni imara magoti yaliyolegea.

<sup>4</sup> Waambieni walio na moyo wa hofu,

Jipeni moyo, msiogope;

tazama, Mungu wenu atakuja na kisasi,

na malipo ya Mungu;

atakuja na kuwaokoa ninyi.

<sup>5</sup> Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa,

na masikio ya viziwi yatazibuliwa.

<sup>6</sup> Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu,

na ulimi wake aliye bubu utaimba;

maana katika nyika maji yatabubujika;

na vijito jangwani.

<sup>7</sup> Na mchanga ung'aao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji,

na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji;

katika makao ya mbweha, walipokuwa wamelala,

patakuwa na majani, pamoja na mianzi na manyasi.

<sup>8</sup> Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia,

nayo itaitwa, Njia ya utakatifu;

wasio safi hawatapita juu yake;

bali itakuwa kwa ajili ya watu hao; wasafirio,

wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.

<sup>9</sup> Hapo hapatakuwa na simba,

wala mnyama mkali hatapanda juu yake;

hawataonekana hapo;

bali waliokombolewa watakwenda katika njia hiyo.

<sup>10</sup> Na hao waliokombolewa na Bwana watarudi,

watafika Sayuni wakiimba;

na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao;

nao watapata kicheko na furaha,

huzuni na kuugua zitakimbia.

35:1 “nyika” Neno hili linarejelea makazi yaliyoachwa (BDB 184, kama vile Yoeli 1:19-20).

▣“mahali palipo ukiwa” Neno hili (BDB 851) linarejelea ukame, nchi kame (kama vile 41:18; 53:2; Yoel 2:20). Tambua kwamba “nyika” inahusiana na “jangwa” na ina mfanano na “jangwa la Araba”.

▣“Jangwa” Neno hili (BDB 787) linarejelea jangwa la Yordani kusini mwa bahari ya chumvi (kama vile. 33:9).

▣“litashangilia na kuchanua maua kama waridi ”VITENZI viwili nya mwanzo katika mst. 1 pia vinafanana nausafishaji wa mimea.

1. watafurahia, BDB 965, KB 1314, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TMILIF*(inawezekana kuna maana katika KITENZI AMRISHI), KITENZI hiki kimetumika mara Nane katika Sura ya 61-66

2. watashangilia, BDB 162, KB 189, *Qal KITENZI AMRISHI*, kama vilemst. 2; 25:9; KITENZI hiki kimetumika mara nne katika Sura ya 61-66, kama vile. Yoel 2:21,23

KITENZI cha tatu “chipukizi” (BDB 897, KB 965, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kinaonyesha ni kwa jinsi ganimmea (yaani., usafishaji) unafurahia. Mara kwa mara Isaya alitumia taswira ya vitu nya asili (kama vile. 33:9; 44:23; 55:12, kama viletleo la NASB Study Bible, ukr 1004). Mazingira ya bustani ya Edeni (Mwa 1-2) yametunzwa; Enzi mpya inakuja!

Aya ya 10 inajirudia katika 51:11. Hii ni ishara ya Enzi mpya ya urejesho (kama vile 7:21-25; 27:6; 32:15; 41:8-19; 55:12-13).



**NASB, NRSV,**

**Peshitta** “waridi”

**NKJV, JPSOA** “waridi”

**NJB, REB** “kondeni”

**JB** “waridi”

**LXX** “yungiyungi”

Ni vigumu sana kutambulisha sawa sawa (toleo la TEV “mimea”) mimea yote ya nchi na mkusanyiko wa wanyama katika mazingira Fulani ndani ya Biblia. Waalimu wa sheria za kiyahudi wanasema hii (BDB 287) inarejelea maua ya waridi, ambapo wafuasi wa Luther na wafuasi wa Calvin wanasema inarejelea yungi yungi. Kila mtu anakisia na bado wanaendeleakukisia! Chanzo kizuri juu ya jambo hili ni mwendelezo wa “msaada wa wafasiri”, *Fauna and Flora of the Bible*, UBS.

**35:2 “Lebanoni . . Karmeli na Sharoni”** Sehemu hizi tatu zilikuwa maarufu kwa ajiri ya majani yake kustawi kwa haraka. Tungo “litachanua maua mengi” ni *Qal* KITENZIJINA HALISI na *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ni ya asili moja (BDB 827, KB 965) ambacho kinatilia mkazo au hapa, mimea kuchanua kwa haraka.

□“watauona” Huu inavyoonekana ni mwendelezo wa usanifishaji wa mimea.

**35:3-6** Aya hizi zinataja aina wa watu mbalimbali.

1. Waliosamehewa (kifasihi “mikono iliyo dhaifu”)
2. Walio dhaifu (kifasihi “magoti yaliyolegea”)
3. Walio na moyo wa hofu (kifasihi “wenye haraka”)
4. Walio vipofu (BDB 734)
5. viziwi (BDB 361)
6. vilema (BDB 820)
7. wasioongea (bubu) (BDB 48)

Pia inaelezea kile ambacho Mungu atafanya kwa ajiri yao wakati wa urejesho mpya.

1. Kwa ajili ya Namba 1 “itiwe nguvu” (BDB 304, KB 302, *Piel* KAULI SHURUTISHI)
2. Kwa ajili ya Namba 2 “yafanywe imara” (BDB 54, KB 65, *Piel* KAULI SHURUTISHI)
3. Kwa ajili ya Namba 3
  - a. kuwa wajasiri, BDB 304, KB 302, *Qal* KAULI SHURUTISHI
  - b. wasiwe na hofu, BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU lakini katika maana ya KITENZI AMRISHI
4. kwa ajili ya Namba 4 “macho ya vipofu yatafumbuliwa” BDB 824, KB 959, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
5. kwa ajili ya Namba 5 “masikio yatazibuliwa” KITENZI hiki hiki kama Namba 4
6. kwa ajili ya Namba 6 “watarukaruka kama Kulungu,” BDB 194, KB 222, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
7. kwa ajili ya Namba 7 “ulimi wake aliye bubu utaimba” BDB 943, KB 1247, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Huu ni ujumbe ambao Yesu aliumtuma kwa Yohana mbatizaji alipokuwa Gerezani (kama vile Mt. 11:4-5; Luka 7:20-22). Enzi mpya iliakisi huduma ya Yesu!

**35:4** tambuakile ambacho YHWH aliahidi kufanya kwa ajiri ya watu wake wa Agano.

1. Atakuja na kisasi, BDB 668, kama vile. 34:8; 59:17; 61:2; 63:4; Kumb. 32:25; Yer. 50:28
2. Ujira wake pia utakuja, BDB 168, kama vile 59:18 (mara mbili); 66:6, pia muhtasari katika 65:6

3. Atawaokoa, BDB 446, KB 448, *Hiphil KITENZI AMRISHI*,(kama vile 25:9; 33:22; 38:20; 45:17; 49:25; 59:1; 63:1,5,9; 64:5)

**35:6 “maana katika nyika maji yatabubujika”** Uoto uliostawi wa asili unaanza kwenye mist. 1,2. Ishara ya nje ya uwepo wa Roho wa Mungu na Baraka ni maajabu ya asili yanayoonyesha uzuri na ustawi (kama vile. mst. 7).

**35:7 “katika makao ya mbweha”** Toleo la Peshitta na toleo la KJV yanatafsiri neno hili (BDB 1072) “mnyama mkubwa.” Tumepata toka kwenye magombo ya bahari ya chumvi orodha inayotaja wanyama kwenye Agano la kale mara nyingi inarejelea sanamu zilizokuwa katika mataifa jirani, hivyo basi, hii labda inarejelea (1) eneo la jangwa au (2) makazi ya mashetani(kama vile. 34:11-15).

Sababu ya fasihi kwa ajili ya mstari wa shairi hili ni kwamba mapango ya mbweha sasa yamejazwa maji na yanaweza kustawisha majani.

▣	
NASB	“mahali pa pumziko”
NKJV	“ambapo kila mmoja atapumzika”
NRSV	“majani”
REB	“makazi yao”

Toleo la MT lina nenohen בְּכָתָה BDB 918, “mahali pa kupumzika.” Toleo la NRSV limebalisha kwenda לִבְכָתָה(tazama NIDOTTE,juzu. 1, ukr. 692-693). Gombo la toleo la DSSla Isaya lina neno “akalala chini.”

▣ **“patakuwa na majani, pamoja na mianzi na manyasi”**. Majani yatakuwa marefu kama mianzi na manyasi kuonyesha ukuaji wa kifahari wa Baraka za Mungu kama ishara ulimwenguni.

**35:8 “njia ya utakatifu”** Hii ni nadharia ya kawaida katika kitabu cha Isaya (kama vile. 26:7; 40:3-4; 42:13). Stiari yenye kufanana na makaribisho ya kifalme imetumika kuelezea ujio wa Masihi. Yohana mbatizaji alitangaza kuwa atatimiliza unabii wa Mal. 4:5 katika kuandaa njia kwa ajiri ya Bwana. Hii ni sitiari kwa ajili ya maandalio ya kuitengeneza njia, lakini inahusisha toba ya kiroho.

**35:9 “hapo hapatakuwa na Simba”** Ukweli kwamba wanyama wakali hawatakuwepo au wamebadilishwa kuwa wanyama wa kufugwa ni ishara ya Baraka za Mungu (kama vile. Isa. 11:6-9). Pia ni kinyume cha kitisho kutoka Law. 26:22.

▣ **“waliokombolewa”** Neno hili kwa mara ya kwanza limetumika katika muunganiko wa kuwaweka wakfu wazaliwa wa kwanza kwa Mungu (kama vile. Kut. 13:13,15). Wazo la kwanza hapa ni kuwakomboa kutoka utumwani kwa gharama iliyopangwa. Uhusiano kati ya “mkombozi” (BDB 145 I, KB 169, Qal KAULI TENDWA ENDELEVU) kwenye mst. 9na “waliokombolewa” (BDB 804, KB 911, Qal KAULI TENDWA ENDELEVU) kwenye mst. 10 imerudiwa katika 40:1-3. Tazama Mada Maalum katika 29:22.

**35:10 “watarudi”** KITENZI hiki (BDB 996, KB 1427, Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kina maana ya “kurudi” (yaani.,toba au kubadili mwelekeo). Wafasiri wengi wanalionia hili (na mst. 8) kama rejeo la kurudi toka uhamishoni huko Babeli (yaani.,hivyo kuna muunganiko na Sura 40-66). Hili kwa hakika linawezekana kwa sababu shairi la Isaya mara zote halikupangwa katika mpangilio wa matukio. Linaweza kuelezea “toba”kama mtindo wa maisha (yaani ., njia ya utakatifu).

▣ **“Sayuni”** Hili baadae lilikuja kufahamika kama jina kwa ajiri ya mji mzima wa Yerusalem (uliojengwa kwenye vilima saba), palipo na Hekalu la pekee, ingawa kijiografia Hekalu liko kwenye Mlima Moria, sio Mlima Sayuni.

- ▣ Waliorudi wanaelezewa kama  
1. Waliokombolewa na BWANA

2. Wanakuja wakiimba
3. Wanakuja na furaha ya milele
4. Vichwani mwao wana taji kama
  - a. kicheko
  - b. furaha
5. Hakuna huzuni
6. Hakuna kuugua

❑“furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao” Neno “milele”ni ‘olam(BDB 761). Angalia Mada Maalumkatika 32:14.

❑“huzuni na kuugua zitakimbia”Angalia Isaya25:8 na Ufu 21:4.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Aina hii ya furaha na Baraka za kimwili zinaonekana kutofatana nao walipokuwa wakitoka uhamishoni ,kama ni hivyo basi hii Sura inadokeza nini?
2. Eleza maana na tofauti kati ya maneno haya mawili “mkombozi” na “waliokombolewa”
3. Kwa nini ulimwengu uwe ishara ya Baraka na uwepo wa Mungu?

## ISAYA 36

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Senakeribu aivamia Tuda	Senakeribu ajivuna dhidi ya Bwana	Uvamizi wa Senakeribu	Waashuru waitishia Yerusalem	Uvamizi wa Senakeribu
36:1-3	36:1-3	36:1-3	36:1-6	36:1-10
36:4-10	36:4-10	36:4-10		36:7-10
36:11-12	36:11-12	36:11-12	36:11	36:11-12
			36:12	
36:13-20	36:13-20	36:13-20	36:13:20	36:13-20
36:21-22	36:21-22	36:21-22	36:21-22	36:21-22

### **MZUNGUKO WA TATU WAUSOMAJI (angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuvuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

### **KUJIFUNZA HISTORIA YA NYUMA (36-39)**

- A. Sura hizi zinaunda mpito wa fasih kihistoria (au kiambatisho, Jewish Study Bible, uk. 853) kati ya maisha ya nabii Isaya katika sura ya 1-39 (kipindi cha Waashuru) na kipindi cha Isaya ambacho kilishughulika na mambo yajayo, sura za 40-66 (kipindi cha Babeli na matukio ya siku ya mwisho). Ongezeko la kihistoria lenye kufanana linaonekana tena katika Yeremia 52, ambapo II Fal. 24:18-25:30 linajirudia.
- B. Kipengele cha Isaya ni chenye kufanana katika II Fal. 18:13-20:19, isipokuwa 38:9-20; pia kumbuka II Mambo ya nyakati 32.
- C. Hiki kipengele kinaonekana kuunda hitaji la mabadiliko yenye mantiki kutokana na msisitizo juu ya Ashuru(sura za 36 na 37) kwenda Babeli (sura za 38 na 39).

- D. Pamekuwepo na baadhi ya majadiliano kuhusu uhusiano wa Hezekia kukataa kujisalimisha kwenye madai na vitisho vya Senakeribuwa Ashuruna Hezekia kutotoa kodi kwake katika II Fal. 18:14-16. Lipo katika mazingira ya uwezekano kuwa Hezekia mwanzoni alitoa kodi na baadaye alikataa kufanya hivyo. Uhusiano kati ya hizi sura mbili ni za kufikirika tu.
- E. Sura hii na zenyenye kufanana nayo zimemanikia zaidi kwenye utumiaji wa neno “kuamini” (BDB 105, KB 120) kuliko muktadha mwingine wowote katika Agano la Kale.
  - 1. Isaya 36:4,5,6 (mara mbili), 7,9,15
  - 2. II Fal. 18:19,20,21 (mara mbili), 22,24,30; 19:10
  - 3. II Nya. 32:10

Maneno “kuamini” (קְעָמִין) na “kusadiki” (קָסָדֵךְ, angalia Mada Maalum katika 22:23) ni ya muhimu katika kuuelewa utendaji mzuri wa uhusiano binafsi ulioko katika agano. Ni zaidi ya utii!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 36:1-3

<sup>1</sup>Ikawa, katika mwaka wa kumi na nne wa kumiliki kwake mfalme Hezekia, Senakeribu, mfalme wa Ashuru, akapanda ili kupigana na miji yote ya Yuda yenye boma, akaitwaa. <sup>2</sup>Mfalme wa Ashuru akamtuma amiri toka Lakishi hata Yerusalem, kwa mfalme Hezekia, pamoja na jeshi kubwa. Naye akasimama karibu na mfereji wa birika ya juu, iliyo katika njia kuu ya kuuendea uwanda wa dobi. <sup>3</sup>Wakamtokea Eliakimu, mwana wa Hilkia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba ya mfalme, na Shebna, mwandishi, na Yoa, mwana wa Asafu, mwenye kuandika tarehe.

**36:1 “katika mwaka wa kumi na nne wa kumiliki kwake mfalme Hezekia”** Inaonekana tokea kwenye kuweka kumbukumbu za utawala wa hawa wafalme wa Yuda na uhusiano wao kwenye historia ya kidunia kuwa kuna kosa la kimuktadha kwenye neno “kumi na nne.”

kwa sababu II Fal. 18:1 inasema kuwa Hezekia alikuwa kaimu mwenza wa baba yake kati ya mwaka 729 na 715 K.K. na baadaye yeye mwenyewe kuwa mfalme tokea mwaka 715 mpaka 686 K.K., yawezekana kuwa hili linatakiwa kusomeka “miaka ishirini na nne ya mfalme Hezekia” (kama vile Gleason L. Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, ukurasa wa 207,211; E. J. Young, *Book of Isaiah*, ukurasa wa 540-542; *The Expositor’s Bible Commentary*, vol. 6, ukurasa wa 234; J. A. Motyer, *Tyndale OT Commentaries*, vol. 18, ukurasa wa 222).

Kwenye jedwali katika kiambatisho cha nne, #3 ya toleo hili kuna orodha ya tarehe tatu tofauti kwa ajili ya utawala wa Hezekia.

1. John Bright – 715-687 k.k.
2. E. J. Young – 727-699 k.k.
3. R. K. Harrison
  - a. kutawala kwa pamoja – 729-716/15
  - b. kutawala – 716/15-687/86

Hawa ni wanazuoni watatu wenye kuheshimika, lakini bado kuna utofauti. Uwe mwangalifu kwenye ushikiliaji mno wa tarehe za kutawala huku na kukaimu. Utafiti bado hauko katika mpangilio kwenye hoja hii kwa wakati muafaka. Tunatarajia habari mpya tokakwa watu wa elimu kale ambao wanaweza kutusaidia katika hili kulielezea vizuri!

### ▣“Senakeribu, mfalme wa Ashuru, akapanda ili kupigana na miji yote ya Yuda yenye boma, akaitwaa”

Tunajifunza toka kwenye nyaraka za Waashuru kuwa Senakeribu (aliyetawala toka mwaka 705-681 K.K.) alidai kuipiga miji 46. Kwa sababu ya kumbukumbu ya Waashuru ya utawala wa Senakeribu uvamizi wa Yuda katika mwaka wa 701 K.K unakifaa kifungu hiki.

**36:2 “Mfalme wa Ashuru akamtuma amiri toka Lakishi”** Kuna njia mbali mbali za kulielewa hili neno (BDB 913).

1. Jina sahihi (NASB, NKJV)
2. “mkadamu”

3. "amiri jeshi" (Peshitta, NIV)
4. "mfalme" au "Afisa mwandamizi" (NKJV footnote)
5. "mwandamizi mkuu (NJB)

kwa vyvyote vile alikuwa ni afisa wa ngazi za juu (tanbihi kwenye toleo la JPSOA) toka kwenye kambi ya Waashuru (kama vile II Fal.18:17).

Toleo la NIDOTTE, juzu ya 3, uk. 1029, kumeorodheshwa vyeo mbalimbali nya Waashuru.

1. Tart<sup>n</sup>n – amiri jeshi, kama vile II Fal. 18:17
2. Rab s<sup>r</sup>ris – jemedari mkuu,kama vile II Fal. 18:17
3. Rab s<sup>r</sup>q'h – kamanda wa kikosi, kama vile II Fal. 18:17
4. Rab Kisri – kamanda wa jeshi
5. Rab hanse – kamanda wa vikosi hamsini
6. Rab saqu – mwandamizi wa mfalme
7. Akkadia
  - a. tartan – kama vile #1 hapo juu
  - b. rabu sa r'si – mkuu wa matowashiau jemedari wa jeshi
  - c. rab s<sup>r</sup>q'h – kama vile #3 hapo juu
  - d. rab saqu – #6 hapo juu
8. Kiaramu – rb swq – mkuu wa matoashi

▣ "Lakishi" Huu ulikuwa ni mmoja wa miji yenye boma kwenye uwanda wa pwani ambaa ulitekwa na jeshi la Waashuru. Ulikuwa yapata maili therathini kusini mwa Yerusalem huko Shefela.

▣ "Naye akasimama karibu na mfereji wa birika ya juu,iliyo katika njia kuu ya kuuendeua uwanda wa dobi" Hii ni sehemu ile ile ambayo Isaya alimkabiri Ahazi katika 7:3 akiwa na ombi la kutoiamini Ashuru. Panaweza kuwepo na ushirikiano wa kimakusudi wa eneo la kijiografia kwenye jibu la Hezekia (imani, kama vile 37:14-20,30) dhidi ya jibu la Ahazi (kutokuamini).

**36:3 "Eliakimu . . Shebna . . Yo" Ikiwa mtu atalinganisha Isa. 22:15 na 22:20-24 inaonekana kuwa hawa watu wawili wamebadilishana ofisi.**

Tukitumia ufanano wa Kimisri inaonekana kuwa hawa watu wanawakilisha ngazi tofauti yamamlaka ya kiutawala huko Mashariki Karibu ya Kale.

1. Eliakim
  - a. NASB, NKJV, "msimamizi juu ya nyumba"
  - b. NRSV, TEV, JPSOA, "msimamizi wa nyumba"
  - c. REB, "mdhibiti wa nyumba"
  - d. NJB, "bwana wa nyumba ya mfalme"
2. Shebna
  - a. NASB, NKJV, JPSOA, "waandishi"
  - b. NRSV, NJB, "mwenye kuandika tarehe"
  - c. REB, "mfawidhi mkuu"
  - d. TEV, "katibu wa baraza"
3. Yo

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:4-10

<sup>4</sup>Yule amiri akawaambia, Haya, mwambieni Hezekia, kwamba mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru, asema hivi, Ni tumaini gani hili unalolitumainia? <sup>5</sup>Nasema, mashauri yako, na nguvu zako kwa vita, ni maneno yasiyo na maana; basi, unamtumaini nani hata ukaniasi mimi? <sup>6</sup>Tazama, unaitumainia fimbo ya mwanzo huu uliopondeka, yaani, Misri, ambayo, mtu akitegemea juu yake, humwingia mkononi na kumchoma; ndivyo alivyo Farao, mfalme wa Misri, kwa wote wamtumainio. <sup>7</sup>Lakini ukiniambia, Tunamtumaini Bwana, Mungu wetu, je! Si ye ye ambaye Hezekia ameondoa mahali pake mlimoinuka, na madhabahu zake, akawaambia watu wa Yuda na Yerusalem, Sujuduni mbele ya madhabahu hii? <sup>8</sup>Basi sasa, tafadhalii mpe bwana wangu,

**mfalme wa Ashuru, dhamana, nami nitakupa farasi elfu mbili, ikiwa wewe kwa upande wako waweza kupandisha watu juu yao.** <sup>9</sup>Wawezaje, basi, kurudisha nyuma uso wa akida mmoja wa watumishi walio wadogo wa bwana wangu, na kuitumainia Misri upewe magari na farasi? <sup>10</sup>Je! Nimepanda mimi, ili kupigana na mahali hapa na kupaangamiza, bila shauri la Bwana? Bwana ndiye aliyenambia, Panda upigane na nchi hii na kuiangamiza.

**36:4** Ujumbe wa Senakeribu ulisomwa kwa sauti mbele ya ukuta wa Yerusalem ili kila mmoja akapate kusikia na kuogopa (kama vile mistari ya 11-12)!

Hii sura ina matumizi matatu ya hiki KITENZI “sema” (BDB 55, KB 65).

1. *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. *Qal KAULI SHURUTISHI*
3. *Qal KAULI TIMILIFU*

▣“**ni tumaini gani hili unalolitumaini**” Haya ni maelezo yenyе umuhimu kwa ajili ya sehemu iliyobaki ya sura ya 36 na 37 kwa sababu ni kitu cha masihala katika neno la Kiebrania “amini” (BDB 105, KB 120, *Qal KAULI ILIYO TIMILIFU*, kama vile 12:2;26:3,4; 31:1; 32:9-11; 36:4,5,6 [mara mbili],7,9,15; 37:10) au swalı “ni nani unayemtumainia?” tambua kuwa mantiki ya Waashuru inasimamia juu ya ushindi wa kijeshi wa miungu ya mataifa mengi. Mlolongo wa shambulio la kisaikolojia linaonekana kuyanyoshea kidole matendo ya Hezekia kwa niaba ya YHWH ili kuubishia uwezo wake na kuubishia watu wasiamini katika Yeye (kama vile 36:4,5,7,10,15,18; 37:4,6,10,17,20 hasa., 23,29). Hili linaweka hatua, zaidi kwenye Danieli 3, kwa ajili ya YHWH kukabiliana na miungu ya Waashuru kwa kusudi kuwa dunia yote itambue kuwa YHWH ni Mungu (kama vile 37:20; 45:6; II Nya. 32:7-8).Swali ni kusudio la kithiolojia la sehemu ya fasihi!

**36:5**

<b>NASB, NJB</b>	“maneno matupu”
<b>NKJV</b>	“maneno yasio na maana”
<b>NRSV</b>	“maneno matupu”
<b>LXX</b>	“maneno ya mdomoni tu”

Toleo la LXX ni tafasiri ya wazi ya andiko la Kimasoreti (BDB 182 MUUNDO WA MANENO BDB 973). Hii ni lahaja kwa ajili ya mtu Fulani anayejaribu kuongea pasipo kufikiri (kama vile Mith. 14:23).

▣“**akaniasi Mimi**” Hili linarejerea kwenye ukweli kwamba Hezekia mwanzoni alikataa kutoa kodi kwa Ashuru (kama vile II Fal. 18:7), lakini baadaye inavyoonekana akaanza tena kutoa kipindi Senakeribu alipovamia (kama vile II Kgs. 18:14-16) na kwa mara ya pili tena akakataa kulipa kodi.

**36:6 “Tazama, unaitumainia fimbo ya mwanzi huu uliopondeka, yaani, Misri”** Inavyoonekana, Waashuru walipata taarifa juu ya mpango ulioiva kwa ajili makubaliano ya kijeshi na Wamisri. Isaya aliyapinga mwanzoni kabisamakubaliano haya (kama vile 30:1-5; 31:1-3).

**36:7 “Si ye ye ambaye Hezekia ameondoa mahali pake mlimoinuka”** Hili ni jaribio la kuubishia uhusiano wa Hezekia na YHWH (kama vile II Fal. 18:5). Msukumo wa hoja ni kuwa YHWH amemkasirikia Hezekia kwa kupaondoa mahali pa juu (kama vile II Fal. 18:7). Hata hivyo, hii ilikuwa ni kutokuelewana kwa Waashuru kwa sababu Hezekia alifanya kikamilifu kile kilichoamriwa katikaKumbukumbu la Torati mahali pa kuabudia kwa pamoja ambapo YHWH angalipachagua (kama vile Kumb. 12:2-5). Mahali pa juu pamekuja kuwa ni sehemu ya ibada ya miungu ya Ba’al naAsherah (kama vile II Fal. 18:4).

**36:8 “njooni mfanye patano na Bwana wangu”** KITENZI (BDB 786, KB 876) ni*Hithpael* KAULI SHURUTISHI ikionyesha zawadi ya ahadi ya kisiasa (kama vile II Fal. 18:23; Ayubu 17:3; Zab. 119:122). Dokezo ni,“ahidiana na YHWH na kumwamini Ashuru” (na kudokezea, miungu yao). Hili linachekesha, lakini kumbuka Yuda amekwisha kujaribu kutengeneza ushirikiano na Misri (kama vile mistari ya 6,9), ambao pia unajumuisha miungu ya Wamisri!

Imani ya Mungu mmoja ya Wayuda ilikuwa ikijaribiwia!

▣ “**name nitakupa farasi elfu mbili**” Haya ni maelezo ya dhihaka yakiegemea juu ya udhaifu wa jeshi la Yuda. Pamekuwepo na baadhi ya uwalakini wa kihistoria kuhusu uwepo wa mateso makubwa huko Yuda au Ashuru katika siku hizi za karibuni, kwa hiyo, watoa maoni wengi wanasema hili ni rejeo kwenye magari ya vibanda wazi hata kama lugha halisi inarejerea kwenye mateso makubwa.

**36:9**

NASB, TEV	“akida”
NKJV, NRSV	“kapteni”
NJB	“wanajeshi”
REB, Peshitta	“watumishi”
LXX	“gavana”

Neno (BDB 808, kama vile, II Fal. 18:24; angalia toleo NIDOTTE, juzu. 3, uk. 603) laweza kurejelea mtawala aliyechaguliwa karibuni wa miji ya Yuda iliyoshindwa vita. Kila akida wa serikali za mtaa alikuwa na kikundi kidogo cha kijeshi. Inavyoonekana Lakini pakajakuwa makao makuu ya utawala wa Waashuru. Kwa hiyo, madai ya wenye kukejeli Rabshaka yalikuwa ni kwamba Yerusalem haikuweza kujirinda dhidi ya jeshi la mgambo, kama lilivyokuwa jeshi la Waashuru.

**36:10 “je nimepanda mimi bila shauri la Bwana”** Haya ni maelezo ya Waashuru kuwa (1) hawakumuuliza Mungu wa Yuda na (2) kama Mungu alikuwa upande wao! Namna walivyoujua unabii kuhusu Mungu kuichagua Ashuru kuiadhibu Israeli, 10:5-7, hajulikani. Baadahi wanaamini nusu kwa nusu kuhusiana na 37:26.

Sura yenyewe inaonekana kujikanganya yenyewe.

1. “hawakumuuliza,” kwa maana iliyowazi “mbali na” (BDB 116)
2. “Bwana akaniambia”

Dhahiri Ashuru (yaani., Senakeribu) inajishaua yenyewe dhidi ya mapenzi ya YHWH na watu wake!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36: 11-12**

<sup>11</sup>Ndipo Eliakimu, mwana wa Hilkia, na Shebna, na Yoa, wakamwambia yule amiri, Tafadhali, sema na watumishi wako kwa lugha ya Kiashuri; maana tunaifahamu; wala usiseme nasi kwa lugha ya Kiyahudi, masikioni mwa watu wote walio ukutani. <sup>12</sup>Lakini yule amiri akawaambia, Je! Bwana wangu amenituma kwa bwana wako, na kwako wewe, niseme maneno haya? Hakunituma kwa watu hawa walio ukutani, ili wale mavi yao wenyewe na kunywa mkojo wao pamoja nanyi?

**36:11 “Kiarama . . . Wayudea”** Kiaramu (BDB 74) ilikuwa ni lugha ya kidiplomasia ya huko Mashariki Karibu ya Kale naneno “Wayuda” lapaswa kutafasiliwa “Waebriana” (BDB 397, kama vile. II Fal. 18:26,28; II Nya. 32:18).

Msukumo wa aya hii ni kuwa maakida wa Hezekia wanawaomba wawakilishi wa Waashuru kuzungumza katika lugha ya kidiplomasia ili kwamba watu wa mji wasijepata hofu.

**36:12** Hii ilikuwa ni hofu kuhusu matatizo yaliyoambatana na uvamizi (yaani., upungufu wa chakula na maji, kama vile II Fal. 18:27) kusababisha woga na hofundani ya Yerusalem. Hata kama Hezekia alimwamini YHWH, yawezekana wakazi wa eneo hawakumwamini.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:13-20**

<sup>13</sup>Kisha yule amiri akasimama akalia kwa sauti kuu kwa lugha ya Kiyahudi, akisema, Lisikieni neno la mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru. <sup>14</sup>Mfalme asema hivi; Hezekia asiwadanganye, kwa maana hataweza kuwaokoa;

<sup>15</sup>wala msimwache Hezekia kuwatia moyo wa kumtumaini Bwana; akisema, Bwana bila shaka atatuokoa, mji huu hautatiwa katika mkono wa mfalme wa Ashuru. <sup>16</sup>Msimsikilize Hezekia; maana mfalme wa Ashuru asema hivi, Fanyeni suluhu na mimi, mkatoke mnijie, mkale kila mtu matunda ya mzabibu wake na matunda ya mtini

wake, mkanywe kila mmoja maji ya birika yake mwenyewe; <sup>17</sup>hata nije nikawachukue mpaka nchi iliyo kama nchi yenu wenyewe, nchi ya nafaka na divai, nchi ya mkate na mashamba ya mizabibu. <sup>18</sup>Jihadharini, asije Hezekia akawadanganya, akisema, Bwana atatuokoa. Je! Yuko mungu mmoja wa mataifa aliyewaokoa watu wake na mkono wa mfalme wa Ashuru? <sup>19</sup>Wako wapi miungu ya Hamathi na ya Arpadi? Wako wapi miungu ya Sefarvaimu? Je! Wameiokoa Samaria na mkono wangu? <sup>20</sup>Katika miungu yote ya nchi hizi ni nani waliookoa nchi yao na mkono wangu, hata Bwana auokoe Yerusalem na mkono wangu?

**36:13-16** Kuna KAULI SHURUTISHI na KAULI AMRISHI mbalimbali zilizotumika katika ujumbe huu toka kwa Senakeribukupitia kwa Rabshaka (vitisho na ahadi).

1. Lisikeni, mst. 13 – BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. Hezekia asiwadanganye, mst. 14 – BDB 674, KB 728, KANUSHO*Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFUiliyotumika katika maana AMRISHI, kama vile. 37:10; hiki ni KITENZI cha aina ile ile kilichotumika katika Mwanzo. 3:13!
3. Wala msimwache Hezekia kuwatia moyo wa kumtumaini Bwana, mst. 15 – BDB 105, KB 120, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya AMRISHI
4. Msimusikilize Hezekia, mst. 16 – BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KUAMRISHA
5. Fanyeni suluhu na mimi, mst. 16 – BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI SHURUTISHI
6. Mkatoke mnijie, mst. 16 – BDB 422, KB 425, *Qal* KAULI SHURUTISHI
7. Kuleni, mst. 16 – BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI SHURUTISHI
8. Kunywени, mst. 16 – BDB 1059, KB 1667, *Qal* KAULI SHURUTISHI

**36:17** Tambua kuwa ahadi mbili za Senakeribu zinaelekezwa kwa watu watokao upande wa nchi ambao walikimbilia kwenye mji wa boma la Yerusalem kwa ajili ya ulinzi. Angaliwaacha wakae kwenye nchiyaowenye, lakini mst. 17 unaelezea, ni kwa muda mfupi tu. Angeyahurumia maisha yao, lakini bado wangelifanywa mateka. Hata kamawangekubali kushindwa kipindi hicho, bado wangaliondolewa kutoka katika nchi ya Yuda.

Hata hivyo, Ashuru iliwaua vijana kwa wazee hadharani!

**36:18 “Je! Yuko mungu mmoja wa mataifa aliyewaokoa watu wake na mkono wa mfalme wa Ashuru?”** Hapa pana changamoto ya kithiolojia. Gravu ya chuma imetupwa chini naYHWH ataichukua! KITENZI “okoa” (BDB 664, KB 717) kimetumika mara tano katika mistari ya 18-20. Cha kwanza na cha mwisho ni*Hiphil* KITENZIKISICHOTIMILIFU na vingine vile vitatu ni*Hiphil* KITENZITIMILIFU.

**36:19 “miungu ya Hamathi na ya Apardi”**

1. Hamathi ulikuwa ni mji katikati ya Shamu ambao mfalme wake alishiriki katika uasi dhidi ya Ashuru na akaja kupigwa naSargon II katika mwaka wa 720 K.K. na watu wake wakakimbilia Samaria (kama vile II Fal. 17:24).
2. Arpadi ulikuwa ni mji kaskazini mwa Shamu ambao mfalme wake alishiriki katika uasi dhidi ya Ashuru na kupigwa na Tiglath-pileser III katika mwaka wa 720 K.K. na majina kamili ya miungu yao hayajulikani.

▣“**miungu ya Sefarvaimu**” Wawezakuwa ni mji kaskazini mwa Babeli. Hili lilikuwa ni eneo ambalo Sargon II (722-705 K.K.) aliwapeleka mateka kwenda kukaa huko Samaria (kama vile II Fal. 17:24). Baadhi ya wanazuoni wanadhani inarejerea mji wa Samaria (mji wa Israeli uliotekwa, 722 K.K.). Toka kwa II Fal. 17:31 tunatambua kuwa miungu ya ustawi walioiabudu kwa kutoa dhabihu watoto wachanga ilikuwa “Adrammeleki” and “Anammeleki.” Jina la kwanza pia ni jina la mmoja wa mwana wa Sanakeribu ambaye aliuawa (kama vile 37:38). Namna walivyohusiana haijulikani.

▣“**je? Wameiokoa Samaria na mkono wangu**” Hili linafurahisha kwa sababu miungu wa Samaria imenorodheshwa tofauti na ile ya Yuda. Wote walimwabudu YHWH, lakini inavyoonekana ibada ya sanamu huko kaskazini ikajakuwa hatari au habari za Waashuru zilikuwa dhaifu kiasi kwamba wote hawakujua kuwa wanamwabudu YHWH (kama vile II Fal. 17:5,6,24).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 36:21-22**

<sup>21</sup>Lakini watu wakanyamaza kimya; wala hawakumjibu hata neno moja; maana ilikuwa amri ya mfalme, kwamba, Msimjibu neno.<sup>22</sup>Ndipo Eliakimu, mwana wa Hilkia, aliyekuwa msimamizi wa nyumba ya mfalme, na Shebna, mwandishi, na Yoa, mwana wa Asafu mwenye kuandika tarehe, wakaenda kwa Hezekia, na nguo zao zimeraruliwa, wakamwambia Hezekia maneno ya yule amiri.

36:22 “na nguo zao zikiwa zimeraruliwa” Angalia Mada Maalum: Ibada kwa walio katika huzuni katika 15:1.

## ISAYA 37

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hezekia anatafta Msaada wa Isaya 37:1-4	Isaya anahakikisha ukombozi 37:1-7	Hezekia anamuuliza Isaya 37:1-4	Mfalme anauliza ushauri wa Isaya 37:1-4	Nabii Isaya anaulizwa 37:1-4
37:5-7		37:5-7	37:5-7	37:5-7
	Hofu ya senakarebu Na maombi ya Hezekia 37:8-13		Waashuru anatuma tishio lingine 37:8-13	Mnyweshaji anarudi kwa Bwana wake 37:8-9a Simulizi ya pili ya shughuli Za Senakarebu 37:9b-13
Maombi ya Hezekia Katika hekalu 37:14-20		37:14-20	37:14-20	37:14-20
Mungu hujibu Kupitia Isaya 37:21-29 (22b-29)	Neno la BWANA juu ya Senakerebu 37:21-29 (22b) (23-25) (26-27) (28-29)	37:14-20	ujumbe wa Isaya kwa Mfalme 37:21-25 (22b-25)	Isaya anaangilia 37:21-29 (26-29) ishara kwa Hezekia 37:30-32
37:30-32	37:30-32	37:30-32	37:26-27 37:28-29 37:30-32	37:30-32 Unabii juu ya AShuru 37:33-35 (33b-35)
37:33-35	37:33-35 (33b-35)	37:33-35	37:33-35	37:33-35 (33b-35)
Waashuru Waaaribikiwa 37:36-38	kushindwa kwa Senakarebu na Kifo 37:36-38			Senakerebu anapewa adhabu 37:36 37:37-38

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk.wa xvi na kipengele cha utangulizi) KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Ayaya kwanza
6. Ayayapili
7. Aya ya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Mistari ya 1-7 ni miitikio ya Hezekia kwa ujumbe wa Waashuru katika sura ya 36.
- B. Haijulikani ikiwa mistari ya 1-7 na 14-20 ni miitikio miwili tofauti. Inaonekana kimuktadha kwamba baada ya mistari ya 8-9 Senakerebu anatuma ujumbe wa pili kuwasilishwa Yerusalem na mistari ya 14-20 ni miitikio ya Hezekia kwa ujumbe wa pili, ambayo ni sawasawa na ile ya kwanza. Yawezekana Hezekia alikuwa akitumaini YHWH na Misri katika mistari ya 1-7, lakini baada ya mistari 9 alitakiwa kutumaini YHWH pekee (kama vile mistari ya 14-20,30).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 37:1-4

<sup>1</sup> Ikawa mfalme Hezekia aliposikia hayo, alizirarua nguo zake, akajivika nguo za magunia, akaingia katika nyumba ya Bwana. <sup>2</sup> Akamtuma Eliakimu aliyekuwa msimamizi wa nyumba yake na Shebna, mwandishi, na wazee wa makuhani, wamejivika nguo za magunia, waende kwa Isaya nabii, mwana wa Amozi. <sup>3</sup> Wakamwambia, Hezekia asema hivi, Siku hii ni siku ya dhiki, na aibu, na matukano; maana watoto wa tayari kuzaliwa, wala hapana nguvu za kuwazaa. <sup>4</sup> Yamkini Bwana, Mungu wako, atayasikia maneno ya huyo amiri ambaye mfalme wa Ashuru, bwana wake, amemtuma ili amtukane Mungu aliye hai; na Bwana, Mungu wako atayakemea maneno aliyoyasikia; basi, inua dua yako kwa ajili ya mabaki yaliyobakia.

**37:1 “alizirarua nguo zake, akajivika nguo za magunia”** Hizi ni ishara za kuomboleza. Angalia mada maalum katika 15:23.

▣ “nyumba ya Bwana” Hii inamaanisha hekalu katika Yerusalem. Kwa hakika ni eneo gani la hekalu aliingia haijulikani. Makuhani tu na walawi walikuwa na ruhusa ya kuingia katika nyumba takatifu. Hatahivyo kulikuwa na eneo maalum lililowekwa kando kwa ajili ya ufalme kuwa karibu kadiri iwezekanavyo na kuangalia shughuli za ibada za kisherehe.

**37:2 “Eliakimu. . .Shebna”** Angalia dokezo katika 36:3,22.

**37:3 Hezekia kwa uwazi anafunua hali** (kama vile II Wafalme. 19:3).

1. NASB, NRSV , “siku ya taabu” (BDB 865 I)  
NKJV, “siku ya taabu”  
NJB, “siku ya mateso”  
LXX, “siku ya dhiki”
2. NASB, NKJV, NRSV, “siku ya maonyo” (BDB 407)  
NJB, “siku ya adhabu”  
LXX, “siku ya kuonywa”
3. NASB, “siku ya kukataliwa” (BDB 611)  
NKJV, “siku ya kukufuru”  
NRSV, NJB, “siku ya kaibishwa”  
LXX, “siku ya kuonywa”
4. LXX, Peshitta, “siku ya hasira”
5. “muda wa kuzaa, lakini pasipokuwa na nguvu ya kuzalisha”

Tungo hizi zote zinamaanisha matendo ya YHWH na wala sio Shamu. Hezekia alijua tatizo lilikuwa kutotii agano na kukosekana kwa imani. Shamu haikuwa tatizo halisi bali vyombo vya YHWH vya hukumu dhidi ya watu wakaidi wa agano.

**37:4** Hezekia alikuwa anatumaini kwamba YHWH alisikia kufuru (yaani “maonyo,” BDB 357, KB 355, *Piel/KITENZI JINA HALISI*, kama vile mistari 17,23,24) kujivuna kwa kiburi kwa Shamu (kama vile 36:15,18,20), angelilinda jina Lake (yaani, Ezek. 36:22-23).

▣“**mabaki**” Neno hili linaweza kutumika katika namna kadhaa kutegemea muktadha. Angalia Mada maalum katika 1:9.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 37:5-7

<sup>5</sup> Basi, watumishi wa mfalme Hezekia wakaenda kwa Isaya.<sup>6</sup> Isaya akawaambia, Mwambieni bwana wenu maneno haya; Bwana asema hivi, Usiyaogope maneno uliyoyasikia, ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru wamenitukana.<sup>7</sup> Tazama, nitatia roho ndani yake, naye atasikia kivumi, na kurudi hata nchi yake mwenyewe, nami nitamwangusha kwa upanga katika nchi yake mwenyewe.

**37:6** Tazama namna Isaya anavyoitikia kwa wajumbe wa Hezekia pamoja na maneno ya YHWH (kama vile mstari wa21)!

▣“**Usiyaogope**” Kauli hii (BDB 431, KB 432, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU* iliyotumika katika namna ya KUHAMASISHA) ni ujumbe unaojirudia rudia kutoka kwa Mungu kwa Viongozi wake (kama vile 7:4; 8:12; 10:24; 35:4; 40:9; 41:10,13,14; 43:1,5; 44:2;51:7; 54:4; Mwanzo 15:1; 21:17; 26:24; 46:3; Kut. 20:20; Hes. 14:9; Kumb. 1:21,29; 3:2,22; 7:18; 20:1,3;31:6,8; Yosh. 8:1; 10:8,25; 11:6; Waamuzi 6:23, n.k.).

#### 37:7

NASB, NJB,

LXX      “nitaweka roho ndani yake:

NKJV     “nitaagiza roho juu yake”

NRSV     “mimi mwenyewe nitaweka roho ndani yake”

TEV       “BWANA atasababisha mfalme kusikia”

REB       “nitaivunja shauku yake”

Peshitta    “nitatuma pigo dhidi yake”

Toleo la MT lina ruah (BDB 924), ambalo katika muktadha linamaanisha hisia za ndani au juu ya namna ya mwisho na kuuona mwisho wa jambo kabla halijatokea. Yule “mfalme mkuu”wa Shamu (kama vile 36:4) anadhibitiwa na Mungu wa Israeli!

▣“**atasikia kivumi, na kurudi hata nchi**”Huu ni mwitikio wa YHWH kwasababu Hezekia alimgeuza kwake kwa ajili ya msaada (kama Ahazi alivyofanya). Atawachanganya jeshi na kuwarudisha nyumbani (kama vile mstari wa 37). Baadhi wanashangaa ikiwa mstari wa 9 sio kutimilizwa kwa uvumi huu lakini inaonekana katika muktadha huu kumaanisha uvumi kwamba utamlazimisha kurudi shamu na sio kuamua kukutana na Misri kwa ajili ya vita.

▣“**nami nitamwangusha kwa upanga katika nchi yake mwenyewe**”Angalia mstari wa 38 kwa ajili ya utimilivu wa unabii huu kihistoria

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 37:8-13

<sup>8</sup> Basi yule amiri akarudi, akamkuta mfalme wa Ashuru anafanya vita juu ya Libna; kwa maana alikuwa amesikia ya kwamba ameondoka, akaacha Lakishi.<sup>9</sup> Naye alisikia habari ya Tirhaka, mfalme wa Kushi, ya kwamba, Ametoka ili kupigana nawe; naye aliposikia hayo, akatuma wajumbe kwa Hezekia, kusema,<sup>10</sup> Mwambieni Hezekia, mfalme wa Yuda, maneno haya, mjisema, Asikudanganye Mungu wako unayemtumaini, akisema, Yerusalem hautatiwa katika mikono ya mfalme wa Ashuru.<sup>11</sup> Tazama, umesikia habari ya mambo yote, ambayo wafalme wa Ashuru wamezitenda nchi zote, kwa kuziangamiza kabisa je! Utaokoka wewe?<sup>12</sup> Je! Miungu ya mataifa, ambao baba zangu waliwaangamiza, wamewaokoa? Gozani, na

**Harani, na Resefu, na wana wa Adini waliokuwa katika Telasari? <sup>13</sup> Yuko wapi mfalme wa Hamathi, na mfalme wa Arpadi, na mfalme wa mji wa Sefarvaimu, wa Hena, na wa Iva?**

**37:9-11** Hii inarudia 36:13-20.

**37:9 “Tirhaka, mfalme wa Kushi”** Kumekuwepo na baadhi ya matatizo ya kihistoria yanayounganishwa na mstari huu kwa sababu ya mtu huyu isipokuwa mdogo wa Farao wa Misri wa sasa (yaani Ufalme wa Kinubi wa ishirini na tano), Shebitku, mpwa wa Shabaka, alitawala kutokea mnamo 407/06 - 690 k.k. Tirhakah alifanyika Farao na kutawala mnamo 690 - 664 k.k. Alifahamika pia kama Mfalme wa Ethiopia (kama vile II Wafalme. 19:9). Hatahivyo hii inaweza kuwa cheo cha kijeshi au maelezo (ambayo yana maanisha kwamba mtu anatambua matukio ya baadaye au mtu kuitia nyaraka). Hivyo katika Andiko hili Tirhakah alikuwa mwakilishi pekee wa Farao aliyetumwa na jeshi.

**37:12-13** Kuna maeneo kadhaa ya kijiografia yaliyotajwa kwamba Shamu pale mwanzoni walikuwa wameyateka.

1. Gozan – Katika II Wafalme. 17:6; 18:11; I Nyakati. 5:26 huu unaitwa mto (yaani jimbo) laMesopotamiaambapo Tiglath-pilesr III aliwapeleka uhamishoni watu kutoka maeneo ya kikabila ya Reuben, Gadi, na Manasse. na baadaye zaidi ya kaskazini mwa makabila kumi kwa Sargon II.
2. Haran – Huu ulikuwa mji wa Shamu (kama vile Mwanzo. 12:4; 24:4) kwamba alikuwa ameasi na kuaribiwa naAsshur-dan III mnamo 763 k.k.
3. Rezeph – Huu ni mji mwingine wa muhimu wa Shamu uliotawaliwa na Shalmanezer III (858-824k.k.). Inawezekana ultawaliwa mara kadhaa lakini taarifa hazikuwa zimezagaa.
4. Telassar – Huu ni mji au ufalme wa Edeni ambaa ulitekwa na Tiglath-pilesr III. Ulikuwa karibu na Elam.
5. Hamath – Huu ni mji wa Shamu uliopakana na Israeli. Baadhi ya raia wake walipelekwa uhamishoni Israeli.
6. Arapad – Huu ni mji wa Shamu kaskazini, mji mkuu wa jimbo au ufalme kidogo (BitAgusi). Ulishindwa na Tiglath-pilesr III mnamo 740 k.k.
7. Lair – Huu ni mji wa Babeli kaskazini ambaa herufi zake ziko karibu na “jiji” (BDB 746, יָרֵא, NJB,NET Bible).
8. Sepharvaim – Angalia dokezo katika 36:19
9. Hena – Huu mji yawezekana upo juu ya Mesopotamia (kama vile ABD, vol. 3, ukurasa wa 137).
10. Ivvah – Hili eneo halijulikani. Baadhi ya wanazuoni wanalinganisha #8 na #9 na majina ya miungu ya wazawa.

Kusudi la kutaja miji hii kibayana (ambayo Hezekia lazima alikuwa akijua au ambayo ilikuwa njiani kutoka Shamu kuelekea Palestina ambayo Senakeribu aliiitawala) ilikuwa ni kuonesha kwamba hakuna ambaye angeweza kupinga jeshi la Shamu!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:14-20**

<sup>14</sup> Basi Hezekia akaupokea waraka katika mikono ya wale wajumbe, akausoma; kisha Hezekia akapanda, akaingia katika nyumba ya Bwana, akaunkunja mbele za Bwana. <sup>15</sup> Hezekia akamwomba Bwana, akisema, 16 Ee Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, ukaaye juu ya makerubi, wewe, naam, wewe peke yako, ndiwe Mungu wa falme zote za dunia. Wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi. <sup>17</sup> Tega sikio lako, Bwana, usikie; funua macho yako, Bwana, uone; uyasikie maneno ya Senakeribu, aliyopeleka ili kumtukana Mungu aliye hai. <sup>18</sup> Ni kweli, Bwana, wafalme wa Ashuru wameziharibu nchi zote, na mashamba yao, <sup>19</sup> na kuwatupa miungu yao motoni; kwa maana hao hawakuwa miungu, bali kazi ya mikono ya wanadamu; walikuwa miti na mawe, ndiyo sababu wakawaharibu. <sup>20</sup> Basi sasa, Bwana, Mungu wetu, utuokoe na mkono wake, falme zote za dunia zipate kujua ya kuwa wewe ndiwe Bwana, wewe peke yako.

**37:14** Hii kibayana taarifa za moja kwa moja zilizoko ndani sana za masimulizi ya kihistoria. Ni ya mchoro na ni ya kibayana. Wasomaji wanaweza ku YHWH, mahali fulani katika mazingira ya kihekalu(kama vile I Wafalme.8:33), Kufungua jumbe hizi za Waashuru kabla yake ili kwamba aweze kuzisoma. Hezekia anataja katika mstari wa 4

kwamba YHWH alisikia Rabshakeh akisoma ujumbe kutoka katika ujumbe kutoka katika mfalme wa Shamu. Hezekia sasa anataka kumkumbusha yeye juu ya kiburi na kukufuru tabia!

**37:16** Tazama vyeo na namna Hezekie anavyoweka tabia za YHWH.

1. Wewe BWANA wa majeshi
2. Mungu (*Elohim*) wa Israel, kama vile Yosh. 7:13,19,20
3. wewe uliyekaa enzini na uliye juu ya makerubi, kama vile Kutoka. 25:22; I Sam. 4:4; II Sam. 6:2; II Wafalme. 19:15; I Nyakati. 13:6; Zab. 80:1; 99:1
4. Wewe ni Mungu (*Elohim*), kama vile Kumb. 10:17
5. Wewe pekee, neno hili (BDB 94)linaashiria hali ya kuabudu Mungu mmoja hapa na uchaguzi wa YHWH juu ya Israeli kama chombo Chake cha ukombozi kwa wanadamu wote ulimwenguni.
6. wewe uliyefana mbingu na nchi, 42:5; 45:18; Mwanzo 1:1

Angalia Mada maalum: Majina ya uungu katika 1:1.

**37:17** Kuna KAULI SHURUTISHI katika maombi ya Hezekia inayotumika kama maombi ya kusihi ya hehima.

1. Tega sikio lake, BDB 639, KB 692, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI , kama vile Dan. 9:18
2. sikia, BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. fungua macho yako, BDB 824, KB 959, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile Dan. 9:18
4. angalia, BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. sikia , sawasawa na#2

Hezekia anatumia lugha ya kibinadamu (angalia mada Maalum katika 6:1) kumsihi Mungu amsikie, amuone na kuiitikia ujumbe wa kiburi na majivuno na wa kufuru wa Senakarebu.VITENZI hivi hivi vinatumika na Suleimani katika kuweka wakfu hekalu I Wafalme. 8:29,52; II Nyakati. 6:39-40; 7:15.

▣“Mungu aliye hai” Mstari huu ni wa kibinadamu (Angalia Mada maalum katika 6:1), ikitoa sifa kwa viungo vya mwili vya YHWHkama vile ni mwanadamu. Agano la Kale linawasilisha Mungu kama wa milele asiye kuwa na mwisho, roho idumuyo milele. Neno “Mungu aliye hai/aishiye” ni sitiari juu ya jina la YHWH tokea Kutoka 3:14, lenye kumaanisha “Mimi Niko Ambaye Niko.”

**37:18** Hakika kulikuwa na kipimo cha ukweli juu ya madai ya Senakerebu

**37:19** Ukweli wa mstari wa 18 unaonekana kutiwa chumvi kwa sababu miungu ya mji inayotajwa ilikuwa ni sanamu, sio Mungu wa pekee na wa kweli! Sanamu zilichongwa na mikono ya mwanadamu. Zilikuwa hazioni wala kusikia wala kuitikia (i.e.,v.yaani mstari wa 17)kama YHWH angeweza, ataweza na atadumu kufanya hivyo, would, and will!

**37:20** Mstari huu una VITENZI viwili.

1. kuwasilisha, BDB 446, KB 448, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, kama vile 25:9; 33:22; 35:4. Imetumika mara kumi nan ne katika sura za 40-66.
2. kufahamu, BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFUikitumika katika namna ya KUSHI. Angalia Mada Maalum: Kujua katika19:21.

Huu ni mstari muhimu sana na unaonesha kilele cha kusudi la matendo ya Mungu. Israeli ilikusudiwa kuwa ufalme wa makuhani (kama vile Kutoka. 19:5-6). Kutokea mwanzo wa wito wa Ibrahim (kama vile Mwanzo 12:3), Mpango wa Mungu ulikuwa kushughulikia ulimwengu mzima (kama vile 45:8,22). Angalia Mada Maalum katika 1:3.

▣“Wewe pekee ndiwe Mungu” Hii hakika ni ukiri wa upekee wa Mungu wa Israeli katika ulimwengu wa kale. Alikuwa Mungu peke yake. Hakuwahi kuweko mwingine (kama vile 43:11; 45:5,18,21-22). Hii ni ukiri wa kithiolojia wa kuwepo kwa Mungu mmoja!Tungo “ndiwe Mungu” haiko katika toleo la MT, lakini inajitokeza katika DSS, LXX, na inakuwa sambamba katika II Wafalme. 19:19

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:21-29**

<sup>21</sup> Ndipo Isaya, mwana wa Amozi, akapeleka ujumbe kwa Hezekia,  
akisema, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kwa kuwa umeniomba juu ya Senakeribu, mfalme wa Ashuru,

- <sup>22</sup> tamko alilolitamka Bwana katika habari zake ndilo hili;  
 Bikira, binti Sayuni, anakudharau, anakudhihaki sana;  
 binti Yerusalemu anatikisa kichwa chake juu yako.
- <sup>23</sup> Ni nani uliyemshutumu na kumtukana? Umeinua sauti yako juu ya nani,  
 na kuinua macho yako juu? Juu ya Mtakatifu wa Israeli.
- <sup>24</sup> Umemshutumu Bwana kwa watumishi wako,  
 kwa kuwa umesema, Kwa wingi wa magari yangu nimepanda juu ya vilele vya milima,  
 mpaka mahali pa ndani ya Lebanoni; nami nitaikata mirezi yake mirefu,  
 na misunobari yake mizuri, nami nitaingia ndani ya mahali pake palipoinuka,  
 palipo mbali sana, msitu wa shamba lake lizaalo sana.
- <sup>25</sup> Nimechimba na kunywa maji, na kwa nyayo za miguu yangu nitaikausha mito yote ya Misri.
- <sup>26</sup> Je! Hukusikia? Ni mimi niliyeyatenda hayo tokea zamani,  
 na kuyafanya tokea siku za kale; nikayatimiza sasa, iwe kazi yako kuangamiza miji yenyе boma,  
 ikawe chungu na magofu.
- <sup>27</sup> Ndiyo sababu wenyeji wao wakawa hawana nguvu, na kufadhaika,  
 na kuhangaika, wakawa kama majani ya mashamba, kama miche mibichi, kama majani juu ya dari, kama  
 shamba la ngano kabla haijaiva.
- <sup>28</sup> Lakini nakujua, kuketi kwako, na kutoka kwako,  
 na kuingia kwako; na ghadhabu yako uliyonighadhhibikia.
- <sup>29</sup> Kwa sababu ya kunighadhhibikia kwako,  
 na kwa sababu kutakabari kwako kumefika masikioni mwangu,  
 nitatia kulabu yangu katika pua yako, na hatamu yangu midomoni mwako,  
 nami nitakurudisha kwa njia ile ile uliyoijia.

**37:21-24** Huu ni mwitikio wa YHWH kwa imani ya Hezekia na ujumbe utokao Shamuwalokwenda zaidi ya kusudi la YHWH (kama vile 10:5) na alifanyika kiburi na mwenye kufuru.

1. Mstari wa 22, alidharau (BDB 100, KB 114, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), walikebehi (BDB 541, KB 532, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*), na alitikisa kichwa chake katika (BDB 631, KB 681, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) Yuda, hapa anaitwa
  - a. binti bikra wa Sayuni
  - b. binti wa Yerusalemu

Toleo la Peshitta, TEV, na REB yanaona mstari huu kumaanisha matendo ya Yuda kuelekea kubaki na Senakarebu lakini nafikiri inamaanisha majivuno ya Ashuru dhidi ya Yuda kwamba YHWH anayaelekeea. Swali ni nani anatenda “yeye (binti)” inamrejereea. Senakarebu ni “yeye (wa kiume)” wa mstari wa 22a, lakini “yeye (binti)” ingerejereea kwa

- a. Ashuru
- b. Yuda
2. Mstari wa 23, alimvamia Mungu wa Yuda (i.e., yaani Mtakatifu Pekee wa Israeli)
  - a. aliyeonywa, BDB 357, KB 355, *Piel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
  - b. aliyekufuru, BDB 154, KB 180, *Piel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
  - c. kupandisha sauti yake, BDB 926, KB 1202, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*
  - d. kuinua macho yako kwa kiburi, BDB 669, KB 724, *Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, kama vile 10:12
3. Mstari wa 24, anatukuza shughuli zake
  - a. magari ya farasi mengi yalikuja katika urefu wa milima kuelekea sehemu za ndani kabisa za Lebanonna
  - b. kukata mialoni yake na muelesi wake bora ulochaguliwa (Isaya anatumia maelezo mengi kwa miti)
  - c. Nitakwenda kwenye kilele chake cha juu, msitu wake mnene

Mstari wa 24 ni sawasawa na kiburi cha mfalme wa Babeli (that I think refers to Kwamba nafikiri inarejea kwa Merodachbaladan, kama vile 39:1), mentioned inikitajwa katika 14:13. Ikiwa ndivyo, basi yawezekana lugha hapa

pia inarejerea milima ya kaskazini ya miungu ya ya hadithi za kimiujiza za Wakanaani, angalia dokezo katika 14:13-14.

**37:21 “kwasababu umeniombea”** Hezekia anaitikia kwa imani na tumaini kwaYHWH, tofauti kabisa na baba yake, Ahaz. Hii inaonesha umuhimu wa kithiolojia wa maombi ya kusihi. Naamini kwamba Mungu amejipambanua mwenyewe kutenda kazi kwa kuitikia maombi ya watoto wake. Hivyo hatujapata kwakuwa hatuombi.

## MADA MAALUMU: MAOMBI YA KUSIHI

### I. Utangulizi

- A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
  - 1. Maombi binafsi, Mk 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
  - 2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk 11:17; Luka 19:46
  - 3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
- B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
- C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
- D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
- E. Nafasi ya maombi ni mtu ye yote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.
- F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
  - 1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
  - 2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
  - 3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
  - 4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
  - 5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba
- G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

### II. Taarifa za Kibiblia

#### A. Agano la Kale

- 1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
  - a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22ff
  - b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
    - 1) Kutoka 5:22-23
    - 2) Kutoka 32:9-14,31-35
    - 3) Kutoka 33:12-16
    - 4) Kutoka 34:9
    - 5) Kumbu. 9:18,25-29
  - c. Samweli akiiombea Israel
    - 1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
    - 2) 1 Samweli 12:16-23
    - 3) 1 Samweli 15:11
  - d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
- 2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
- 3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizotubia zinaathiri maombi yetu
  - a. Zaburi 66:18
  - b. Mithali 28:9
  - c. Isaya 59:1-2; 64:7

- B. Agano Jipya
1. Huduma ya kusih/kuombea ya Mwana na Roho
    - a. Yesu
      - 1) Warumi 8:34
      - 2) Waebrania 7:25
      - 3) 1 Yohana 2:1
    - b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
  2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusih
    - a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
      - 1) Warumi 9:1ff
      - 2) Warumi 10:1
    - b. Akiliombea kanisa
      - 1) Warumi 1:9
      - 2) Waefeso 1:16
      - 3) Wafilipi 1:3-4,9
      - 4) Wakolosai 1:3,9
      - 5) 1 Wathesalonike 1:2-3
      - 6) 2 Wathesalonike 1:11
      - 7) 2 Timotheo 1:3
      - 8) Filemon, uk. 4
    - c. Paulo analiomba kanisa limwombee
      - 1) Warumi 15:30
      - 2) 2 Wakorintho 1:11
      - 3) Waefeso 6:19
      - 4) Wakolosai 4:3
      - 5) 1 Wathesolanike 5:25
      - 6) 2 Wathesolanike 3:1
  3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusih
    - a. Kuombeana wao kwa wao
      - 1) Waefeso 6:18
      - 2) 1 Timotheo 2:1
      - 3) Yakobo 5:16
    - b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
      - 1) Adui zetu, Mt. 5:44
      - 2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
      - 3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
      - 4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
      - 5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16
- III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa
- A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
    1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
    2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
    3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Yuda 20
    4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15
  - B. Visababishi
    1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
    2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
    3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
    4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

- C. Mitazamo mingine
    - a. Usitahimilivu
    - b. Luka 18:1-8
    - c. Wakolosai 4:2
  - 1. Endelea kuomba
    - a. Mathayo 7:7-8
    - b. Luka 11:5-13
    - c. Yakobo 1:5
  - 2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
  - 3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zижиликаназо
    - a. Zaburi 66:18
    - b. Mithali 28:9
    - c. Isaya 59:1-2
    - d. Isaya 64:7
- IV. Hitimisho la kithiolojia
- A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
  - B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
  - C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

**37:22 “ametikisa kichwa chake nyuma yako”** Hiki KITENZI (BDB 631, KB 681, *Hiphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) inaashiria nahau ya kiebrania ya mtu kutikisa kichwa kama ishara ya kutokubaliana (kama vile II Wafalme. 19:21; Ayubu 16:4; Zab. 22:7;109:25; Omb. 2:15; Mt. 27:39; Mk. 15:29).

**37:25-29** Kwa hatua hii shabaha inageuka kutoka ushindi wa Ashuru(ingawa inawezekana kwamba mstari wa 25inarejerea madai ya majivuno ya Senakarebu, lakini mstari wa 26 hauwezi)kuelekea mafanikio ya YHWH.

1. Mstari wa 25, YHWH anashughulikia maji (yaani uhai, kama vile 11:15; 44:27)
2. Mstari wa 26-27, mipango ya kale ya YHWH kutumia Ashuru kuadhibu watu Wake (kama vile 10:5). Mstari wa 27unarejerea Israeli na kudhalilishwa na Yuda na kushindwa.
3. Mstari wa 28, YHWH alikuwa na maarifa juu ya hili kabla (sawasawa kabisa na Zaburi 139)
4. Mstari wa 29, madhara ya kiburi dhidi ya YHWH
  - a. kuweka ndoana katika pua yako
  - b. kuweka kifungo katika kinywa chako (Hizi ni sitiari kwa ajili ya uhamisho)
  - c. kugeuka kwa njia ambayo umeijia (kama vile 37:37)

**37:26 “Je hujasikia?Muda mwingi uliopita nalifanya,**

**Kutokeanyakati za kale nalilipanga** Hii inaonesha kwamba Mungu siku zote amekuwa na mpango wa kushughulikia sio tu Ashuru (10:5; Yer. 18:11), lakini pia na ulimwengu mzima (kama vile 14:24,26; 22:11; 25:1; 46:10-11;angalia dokezo kamili katika 12:5). Historia aitembe kwa nmna isiyoeleweka bali kwa mwendo wa imani kwamba viumbe vyote vimeumbwa na Mungu kuelekea kwenye makabiliano ya siku za mwisho na urejesho. Neno lilifasiriwa “siku nyingi zilizopita” (BDB 935) zinarejere mud aba nafasi. Inaweza pia kurejerea

1. muda mrefu mwingi uliopita, hapa
2. wakati uliopita, kama vile II Sam. 7:19; I Nyakati 17:17

**37:28 “Hasira yako dhidi yangu”** Hiki KITENZI (BDB 919, KB 1182, *Hithpael KITENZI JINA HALISI*) kinarudiwa katika mstari wa 29. Tazama kiashiria binafsi!Hiki KITENZI VERB katika *Hiphil* shina mara kwa mara kinatumika juu ya hofu na kutetemeka(kama vile 14:16; 23:11) au matukio ya siku za mwisho (kama vile 13:13). Inatumika juu ya HWH Mwenyewe katika Ezek. 16:43.

**37:29 “Nitaweka kitanzi change katika pua yako”** Hiki ndicho hakika Ashuru alichofanya kwa wengine. Alijaribu kuwatisha kwa majivuno ya ukatili ambao alikuwa amefanya kwa mataifa mengine. Aliwafunga watu waliotawala kwa kutumia ndoana katika pua zao, vinywa vyao au ndimi na kuwatemebeza kuelekea uhamishoni (kama vile II Wafalme.19:28). Mungu atawatendea hivyo pia wao.

## ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 37:30-32

<sup>30</sup> Na kwako wewe dalili ndiyo hii; mwaka huu mtakula vitu vimeavyo vyenyewe; na mwaka wa pili mtakula mazao ya mbegu za vitu hivyo; na mwaka wa tatu pandeni mbegu, kavuneni; mkapande mizabibu katika mashamba, mkale matunda yake. 31 Na mabaki yaliyookoka, yaliyobakia ya nyumba ya Yuda, yatatia mizizi chini, na kuzaa matunda juu. 32 Maana katika Yerusalemu yatatoka mabaki, nao watakaookoka katika mlima Sayuni; wivu wa Bwana wa majeshi utatimiza mambo hayo.

**37:30** “Hii itakuwa ishara kwenu” Hii ni muhimu kwasababu Hezekia ni mwakilishi wa Kimasihi (yaani, 7:14-16) kama Ahazialivyo kuwa (yaani 8:8c,10c). Mungu atamwonesha yeye ishara (BDB 16) hapa na katika 38:7 (kama livyofanya Ahazi katika 7:14). Hii ishara hasa inanahusiana na ahadi ya miaka mitatu ya urejesho kamili ya ardhi ya Yuda. Nafikiri 37:30-32 inatakiwa iwe aya tofauti iliyojitenga, kama inavyotakiwa kuwa 37:33-35 na 36-38. Mstari wa 30 una mfululizo wa KAULI SHURUTISHI kwa ahadi za YHWH za miaka mitatuya urejesho (yaani ahadi za agano za Kumbu kumbu la Torati 27-28).

1. kula – BDB 37, KB 46, *Qal* KITENZI JINA HALISI. Muundo huu unarudiwa katika mstari huu(*kethib*), lakini toleo la wanazuoni wa MT walipendekeza mabadiliko (*Qere*) kuwa *Qal* KAULI SHURUTISHI, ambayo inashabihiana katika mstari huu. Tofauti ni ndogo sana.
  - a. וְאֶכְלָה, MT
  - b. וְאֶכְלֵה, mabadiliko yanayopendekezwa
2. kupanda – BDB 281, KB 282, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. kuvuna – BDB 894, KB 1126, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. kupanda – BDB 642, KB 694, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. kula, *Qere*, angalia dokezo katika #1

Wazo moja lingine lililoongezeka inawezekana kwamba urejesho huu ulioahidiwa unahusiana na “Mwaka wa Jubilei,” Law. 25:10, angalia James M. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, ukurasa wa 96.

**37:31** “mabaki yaishiyo” Angalia Mada maalum katika 1:9.

▣ Sitiari za kilimo ziendelee. Yuda anaelezewa kama

1. anachukua mzizi imara
2. kuzaa matunda

**37:32** Wale watakaopona uvamizi wa Ashuru watafanya hivyo, sio kwa mipango yao wenye au utoshelevu lakini kwa shauku zao (kama vile 9:7; 59:17) Bwana wa Majeshi! Ahazi alipanga lakini Hezekia aliamini!

▣ “Shauku ya BWANA” Hii (BDB 888) inarejerea upendo maalumu wa YHWH na kujali kwa watu wake wa agano (mwanamke asiyekuwa mwaminifu Hosea 1-3). YHWH anafanya kazi kwa upendo kwa ajili ya Kusudi lake katika ukombozi (kama vile 63:15-19, ambayo yanahusisha wana wa Ibrahim, kama vile Mwanzo 12:1-3). Tungo ina maana ya kimasihi katika 9:7 na 59:17. Muktadha unaamua ikiwa (1) shauku ama (2) shauku katika fasiri iliyo bora. Neno linaweza kuwa aidha na kisawe hasi au chanya kwa kutegemea muktadha!

## ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 37:33-35

33 Basi, Bwana asema hivi katika habari za mfalme wa Ashuru, Yeye hataingia ndani ya mji huu, wala hatapiga mshale hapa, wala hatakuja mbele yake kwa ngao, wala hatajenga boma juu yake. 34 Njia ile ile aliyoijia, kwa njia hiyo atarudi zake, wala hataingia ndani ya mji huu; asema Bwana. 35 Nami nitaulinda mji huu, niuokoe kwa ajili yangu mwenyewe, na kwa ajili ya Daudi, mtumishi wangu.

**37:33-34** Hii ni hadi kwamba hakuna mashambulizi yatayotokea dhidi ya Yerusalemu. Kwa hatua hii jeshi la waashuru halikuwahi kuwepo kabla ya malango ya Yerusalemu, lakini bado katika miji yenye ukuta wa Shephelah

kama mwendo Fulani mbali, kama vile Lachish.

Kuna vitu kadhaa ambavyoYHWH ataviruhusu na kutoviruhusu kuhusiana na kuvamiwa kwa Ashuru juu ya Yerusalem.

1. jeshi la Ashuru halitokuja Yerusalem kulivamia
2. jeshi halitalenga mshale pale
3. jeshi halitakuja na ngao
4. jeshi halitatupa vizingiti nya njia
5. Ashuru watapigwa na kurudia njia walioijia

**37:35** Sababu zilizotolewa kwa vikwazo nya Ashuru na kurudi nyuma ni

1. YHWH mwenyewe atalinda (BDB 170, KB 199, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) mji (yaani taswira ya Vita Vitakatifu)
2. YHWH ataokoa/atauokoa (BDB 446, KB 448, *Hiphil TUNGO YA KITENZI JINA*)
3. YHWH anafanya
  - a. kwa ajili yake yeye mwenyewe (yaani mpango wake wa milele wa ukombozina heshima yake binafsi, kama vile Ezek. 36:22-38)
  - b. kwa ajili ya mtumishi wake Dudi (kama vile 9:7; 11:1; 16:5; 22:9,22; 29:1; 38:5; 55:3; II Samuel 7)

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 37:36-38**

<sup>36</sup>Basi malaika wa Bwana alitoka, akaua watu mia na themanini na tano elfu katika kituo cha Waashuri, na watu walipoamka asubuhi na mapema, kumbe, hao walikuwa maiti wote pia. <sup>37</sup>Basi Senakeribu, mfalme wa Ashuru akaenda zake, akarudi Ninawi, akakaa huko. <sup>38</sup>Ikawa alipokuwa akiabudu katika nyumba ya Nisroki, mungu wake, Adrameleki na Shareza, wanawe, wakampiga kwa upanga; wakakimbilia nchi ya Ararati; naye Esar-hadoni, mwanawe, akamiliki badala yake.

**37:36 “malaika wa Bwana alitoka”** Hii ni sawasawa na kuhuishwa kwa nafsi kwa kifo cha malaika aliywakilisha uwepo wa YHWH katika pigo la mwisho Misri katika Kutoka 11 na 12:23,29 (pia tazama II Sam.24:16).Hakuna “mvunaji mbaya.” YHWH hushughulikia uhai na mauti. Ni ngumu kutenganisha Ukuu na utawala wa Mungu kutoka katika hali za ulimwengu ulioanguka. Huu sio ulimwengu amba Mungu aliukusudia kuwa. Kifo ni matokeo ya uasi wa kibinadamu. Mungu huruhusu, hujua na kutekeleza mapenzi yake. Vyanzo nya pili vilivyo muhimu sana kwetu havikuwa sehemu ya mtazamo wa ulimwengu wa kale (yaaniMt. 6:25-27; 10:28-31), ambapo hapakuwa na utofauti kati ya nguvu zipitazo kawaida na zile za asili.

#### **MADA MAALUM: MALAIKA WA BWANA (BDB 521 kutengeneza BDB 217)**

Ni dhahiri kwamba Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kimwili katika muundo wa mwanadamu kwenye Agano la Kale. Swali juu ya Utatu Mtakatifu linakuja, mtu gani mionganini mwa Utatu aliyeikamilisha kazi hii. Kwa kuwa Mungu Baba (YHWH) na Roho Wake wamedumu katika hali ya kutokuwa katika mwili, inaonekana kuwepo na uwezekano wa kwamba udhihirisho huu wa kibinadamu ni Masihi aliyeuwepo kabla ya kuuvaa mwili.

Ili kufafanua ugumu anaokabiliana nao mtu katika kujaribu kutambua udhihirisho wa Mungu katika hali ya kimwili ya mfanano wa kimalaika orodha ifuatayo ina ufanuzi.

1. yeye malaika wa Bwana kama malaika (mara kwa mara “malaika wake”, “malaika,” “yule malaika,” hata “ngozo”)
  - a. Mwa. 24:7,40
  - b. Kut. 23:20-23; 32:34
  - c. Nah. 22:22
  - d. Fal. 5:23
  - e. 2 Sam. 24:16

- f. 1 Nya. 21:15-30
- g. Zek. 1:12-13
- 2. Malaika wa Bwana kujidhihirisha katika hali ya kimwili
  - a. Mwa. 16:7-13; 18:1-33; 22:11,15; 31:11,13; 48:15-16
  - b. Kut. 3:2,4; 14:19 (13:21)
  - c. Fal. 2:15; 6:22-24; 13:3-23
  - d. Hos. 12:3-4
  - e. Zek. 3:1-5
  - f. Mdo. 7:30, 35, 38

Ni muktadha tu unaoweza kutofautisha kati ya mbadala hizi mbili

■“**akaua watu mia na themanini na tano elfu katika kituo cha Waashuri**” Hii haikuwa kabla ya kuta za Yerusalem lakini inavyoonekana umbali kidogo katika kambi ya Waashuru (kama vile II Wafalme. 19:35). Herodotus, mwanahistoria wa kale anaweka kumbukumbu ya pigo hili na kumaanisha kwamba lilikuwa likihusiana na mapanya. Hukumu hii haikuua jeshi zima. Tukio hili linaaksiwa kwa mbele katika 31:8, pale ambapo inaelezwa kama kifo kwa upanga wa BWANA. Hatahivyo hapa inaonekana ni tauni. Kumbuka kuwa hili ni simulizi la za ushairi za utiaji chumvi na sio simulizi ya kihistoria. Wasomaji wa kimagharibi na wa kisasa hawaathiriwi na mtizamo wao wenyewe wa kidunia na kuzoma biblia (kitabu cha mashariki cha kale) kupitia chujio la ufahamu wao wa sasa wa historia na fasihi ambavyo siku zote vinasababisha mkanganyiko!

**37:37 “Ninawi”** Huu ulikuwa mji mkuu wa Ashuru iliokuwa katika Mto Hedekeli.

**37:38 “Nisroch mungu wake”** Hili ni jina lisisilojulikana.

1. Toleo la fasiri yaLXX ya herufi hisi sawasawa na mungu wa mji wa Ashuru, ambaye alikuwa mungu mkuu wa madhabahu ya Ashuru.
2. Inawezekana pia kwamba kupishana majina ya “Nusku” (BDB 652), wababeli na mungu mwanga na moto wa waashuru waliokuwa wakiabudiwa huko Harani na zikihusianisha na mungu mwezi (yaani mtoto wake).
3. E. J. Young anafikiri kwamba ilikuwa uharibifu wa kimakusudi wa jina Marduk. Angalia James M.Freeman, *Manners and Customs of the Bible*, ukurasa wa182.Tunajua kutoka katika nyaraka za kihistoria kamba kuna ombwe la miaka ishirini kati ya mstari wa 37 na 38.

Unabii huu ultimilizwa kibayana katika mnamo 681 k.kambapo wana wawili wa Senakarebu waliuwawa na kumuua na mtoto wa tatu kuchukua kiti cha ufalme.

■“**Esarhaddon**” Huyu ni mmoja wa watoto wa mfalme aliyetawala katika Ashuru tokea mwaka 681-669 k.k.

## ISAYA 38

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Uponyaji wa Hezekia Hezekia 38:1-3	miaka ya Hezekia Inaongezwa 38:1-3	ugonjwa na uponyaji wa Hezekia 38:1-3	ugonjwa wa mfalme Hezekia na uponyajiuponyaji wa 38:2-3	ugonjwa na Hezekia na uponyaji 38:1-3
38:4-6	38:4-6	38:4-6	38:4-6 [38:21-22]	38:4-6 [38:21-22 na 7-8]
38:7-8 Hezekia		38:7-8	38:7-8	wimbo wa
38:9-14 (10-14)	38:9-14 (10-14)	38:9-20 (10-15)	38:9-20 (10-15)	38:9-20 (10-15)
38:15-20 (15-20)	38:15-20 (15-19) (20)	(16-20)	(16-20)	(16-20)
38:21-22	38:21-22	38:21-22		

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kia ya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

- 11. Aya ya kwanza
- 12. Aya ya pili
- 13. Aya ya tatu
- 14. Nk

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kama Sura ya 36-37 inasimulia kipindi cha Ashuru, Sura ya 38-39 inaelekeza ushawishi wa watu Mungu kipindi cha Babeli.
- B. Na ikumbukwe kwamba kulikuwa na majimbo mawili ya “Babeli”
  - 1. Merodach-baladan II (721-710, 703-702K.K., kama vile2 Fal. 20:12; Isa. 39:11) wakati wa Hezekia (ambaye nafikiria ni mmoja anaerejelewa katika Isaya 13-14).
  - 2. Babeli Mpya chini ya Nabopolassar (626-605K.K.) na mwana wake, Nebukadnezza II (605- 562 K.K.), aliyesababisha kuharibiwa kwa Yerusalem na Hekalu mwaka wa 586 K.K. alitoa amri nyingi za uhamishoni kwa Yuda (605, 597, 586, 582 K.K.)

- C. Toleo la The Jewish Study Bible (ukr. 858) inasema , “matukio yanayoelezewa kwenye Sura ya 38-39 yanatangulia matukio yaliyoelezewa kwenye Sura ya 36-37 kwa angalau miaka kumi.” Hii ni kwa sababu Waashuru walimshinda Merodach-baladan II.
- D. Ugonjwa wa Hezekia na kuponywa kwake pia kumeandikwa katika 2 Fal. 20:1-11. Zaburi yake ni sawa na Zab. 6 na 118 au hata Yona 2. Zaburi ya Hezekia haijitokezi katika 2 Fal.20.

## USOMAJI WA NENO WA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 38:1-3

<sup>1</sup> Siku hiso Hezekia aliugua, akawa katika hatari ya kufa; na Isaya nabii, mwana wa Amozi, akaenda kwa mfalme, akamwambia, Bwana asema hivi, Tengeneza mambo ya nyumba yako; maana utakufa, wala hutapona.

<sup>2</sup>Basi Hezekia akajigeuza, akaelekeza uso wake ukutani, akamwomba Bwana,<sup>3</sup>akasema, Ee Bwana, kumbuka haya, nakusihu, kwamba nimekwenda mbele zako katika kweli na kwa moyo mkamilifu, na kutenda yaliyo mema machoni pako. Hezekia akalia sana sana.

**38:1-8** Huu ni mfano wa kweli kwamba ndiye anaetawala historia, na bado historia pia inaathiriwa na maombi yetu (kama vile. 37:21).lakini pia kumbuka kwamba huu ni wakati wa “muda wa ziada”wa maisha ya Hezekia na mwana wake mwovu na mrithi, Manase,alikuwa amezaliwa. Kwa njia nyingine majibu ya Mungu kwa Hezekia yalileta hukumu juu ya Yuda.Ni lazima tuombekatika mapenzi ya Mungu, kamwe hatuoni taswira kubwa.

**38:3 “kumbuka”** KITENZI(BDB 269, KB 269, *Qal KAULI SHURUTISHI*) ni KAULI SHURUTISHI ya kuuliza. Hezekia, kama Nehemia (kama vile. Neh. 13:14,22), alimuuliza Mungu achukue maneno ya kumkumbusha mtindo wake wa maisha ya imani. Inatia shaku kwamba katika Biblia wanadamu huomba kwa Mungu ili aweze kuzisahau dhambi zao, wakati Mungu anawataka walikumbuke neno lake.

Kumbukumbu za Mungu ni kumtetea ili awe mwaminifu katika neno lake na kila mmoja aishi katika Ahadi.

Fahamu kile ambacho Hezekia alikuwa anatetea.

1. Nimekwenda (BDB 229, KB 246, *Hithpael/KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) mbele zako katika kweli (kifasihi. “mkamilifu,” BDB 54). “nimekwenda” ni sitiari ya kibiblia ya mtindo wa maisha ya imani (yaani., Zab. 26:3; 86:11).
2. Nimetenda kwa moyo mkamilifu, hii ni sitiari ya kujiweka wakfu jumla.
3. Nimetenda mema machoni pako.

▣“**kwa moyo mkamilifu**” Maelezo haya kwa kawaida yanasisimulia utawala na maisha ya Daudi (kama vile1 Fal. 3:6; 9:4; 11:4; 1 Nya. 28:9); watu (1 Nya. 29:9); au Asa (kama vile1 Fal. 15:14). Hezekia anafikiliwa kuwa ni mmojawapo wa Wafalme wa Yuda aliyekuwa mcha Mungu (kama vile2 Fal. 18:5-6).

▣“**akalia sana sana**” Kuna baadhi ya maswali kama ni kwa nini Hezekia alifadhaika alipofikiria kifo chake: (1) hofu yake ilikuwa ni kufa katika umri wa kati, inaonekana kwenye mst. 10 au (2) jambo la kweli ni kwamba hakuwa na mrithi (kama vile mst. 19; 39:7; 2 Fal. 21:1). Ni jambo la kutia shaka kwamba,kama ikiwa , huu ni ukweli kwasababu hatuna Elimu kisaikolojia ya kuchambua maelezo ya watu katika historia. Na huzuni ni kwamba kipindi miaka kumi na miatano inaongezwa ndio kuzaliwa kwa Manase kunajitokeza na alikuwa Mfalme mwovu sana aliyetawala Yuda na anahuksika kwa ukaribu zaidi juu ya kupelekwa Yuda uhamishoni Babeli.

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 38:4-6

<sup>4</sup>Ikawa, neno la Bwana likamjia Isaya, kusema, <sup>5</sup> Enenda ukamwambie Hezekia, Bwana, Mungu wa Daudi, baba yako, asema hivi, Mimi nimeyasikia maombi yako, nimeyaona machozi yako; tazama, nitaziongeza siku

**zako, kiasi cha miaka kumi na mitano.** <sup>6</sup>Nami nitakuokoa wewe, na mji huu, na mkono wa mfalme wa Ashuru, nami nitaulinda mji huu.

**38:4-6** Ufunuo ni dhana ngumu sana kuielezea. Mafundisho ni muhimu kwa ajili ya imani yetu, lakini namna yanavyofanya kazi hailezewi.

1. maono
2. ndoto
3. matendo ya ishara
4. maelezo ya kuzungumza
5. kazi ya mhariri
6. hata tafsiri (yaani,toleo la LXX lilitotumika kwa kanisa la Mwanzoni, yaani , Isa. 7:14) Naamini Biblia ni kitabu cha kipekee. Kitabu cha Ifunuo wa kiroho. Katika Aya hii, kama vile mara kwa mara katika unabii, ujumbe ni maelezo yaliyozungumzwa haswa kutoka kwa YHWH. Mungu wa milele amejifunua mwenyewe katika Uumbaji wake Mkuu, mwanadamu.

**38:5 “Mungu wa Daudi Baba yako”** maelezo haya yanarejelea nyuma na muunganiko katika 37:35 na mbele zaidi katika 55:3. Daudi anawakilisha mfalme mkamilifu na YHWH akafanya Ahadi maalum kwake na familia yake, 2 Samuel 7; 1 Fal. 8:24-26. Mfalme wa nasaba ya Daudi bora zaidi ajae anatajwa katika 9:7; 16:5; 55:3.

**38:6** Sio tu Mungu atamhurumia Hezekia maisha yake, lakini pia atauhurumia mji wa Yerusalem! Tungo “nitakuokoa ” ni msamiati wa Vita takatifu. Mungu wa Agano anatenda badala ya watu wake wa Agano!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 38:7-8**

<sup>7</sup> Jambo hili liwe ishara kwako, itokayo kwa Bwana, ya kuwa Bwana atalitimiza jambo hili alilolisema;

<sup>8</sup>Tazama, nitakirudisha nyuma kivuli madaraja kumi, ambayo kilishuka juu ya duara ya Ahazi kwa sababu ya jua. Basi jua likarudi madaraja kumi katika hiyo duara, ambayo limekwisha kushuka.

**38:7-8 “liwe ishara kwako, itokayo kwa BWANA”**Hapa tena, hii ni ishara ya kimwili ya kumtia moyo Hezekiakwamba atamhurumia maisha yake (2 Fal. 20:9 maelezo yaliyojitosheleza). Inaonekana inasimulia:

1. mduara wa jua umechorwa utumike kama hatua za kumwongoza katika chumba cha siri cha mfalme
2. neno “hatua” lina maana “daraja” la mduara wa jua (kama vile. 2 Fal. 20:9-11,tafsiri ya toleo la JPSOA, tazama James Freeman, *Manners and Customs of the Bible*,ukr. 183)
3. Aina mojawapo ya Elimu ya Kisayari ya kushangaza

Lazima tuwe makini na imani inayokubali bila kuuliza juu ya hasa ni kwa nama gani Mungu anayafanikisha haya. Mungu mwenye uwezo mkuu anaweza kufanya chochote anachotamani ndani ya sheria za ulimwengu. Hata hivyo, hii inaweza kufanywa sawa na nguvu za ajabu za asilia kama vile unyevu-nyevu mwangi katika tabaka la mawingu. Ni dhahili kwamba baadhi ya miujiza ya jua katika Joshua 10:12-13 ni mwanzo zaidi wa mashairi kuliko asili. Tunaoamini katika miujiza lazima tuwe makini kwamba hatuna matokeo na hatukubaliani na miujiza. Mara nydingi Mungu hutumia asili kukamilisha vitu vya ulimwengu (yaani.,mapigo ya Misri). Katika ulimwengu wa kale kulikuwa hakuna tofauti kati ya ulimwengu na asili (tazama John L. Walton, *The Lost World of Genesis 1*).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 38:9-14**

<sup>9</sup>Haya ndiyo maandiko ya Hezekia, mfalme wa Yuda, alipokuwa hawezi, naye akapona ugonjwa wake.

<sup>10</sup>Nalisema, Katika usitawi wa siku zangu

nitakwenda kuingia malango ya kuzimu;

Nimenyimwa mabaki ya miaka yangu.

<sup>11</sup>Nalisema, Sitamwona Bwana,

yeye Bwana, katika nchi ya walio hai;

Sitamwona mwanadamu tena pamoja na hao wakao duniani.

<sup>12</sup>Kao langu limeondolewa kabisa, limechukuliwa kama hema ya mchungaji;

Nimekunja maisha yangu kama mfumaji;  
atanikatilia mbali na kitanda cha mfumi;  
Tangu mchana hata usiku wanimaliza.

<sup>13</sup>Nalijituliza hata asubuhi;  
kama simba, aivunja mifupa yangu yote;  
Tangu mchana hata usiku wanimaliza.

<sup>14</sup>Kama mbayuwany au korongo ndivyo nilivyolia;  
Naliomboleza kama hua;  
macho yangu yamedhoofu kwa kutazama juu;  
Ee Bwana, nimeonewa, na uwe mdhamini wangu.

**38:10-20** Zaburi hii iliandikwa na Hezekia. Alikuwa na ufahamu wa kutosha wa fasih ya hekima na aliinuliwa kwa kutumia Zaburi (kama vile 2 Nya. 29:25-30). Hata hivyo, haijitokezi katika mfanano wa 2 Fal. 20:1-11.

**38:10**

NASB            “katika usitawi wa siku zangu”

NKJV, TEV,

REB            “katika ukamilifu wa siku zangu”

NRSV            “katika adhuhuri ya siku zangu”

NJB            “katika adhuhuri ya siku zangu”

LXX            “katika urefu wa siku zangu”

Peshitta        “katikati ya siku zangu”

Toleo la MT lina neno מִזְמָר (BDB 198, KB 226 II), Ambalo lina maana “kukoma”, “kutulia kwa muda”, “mapumziko”, au “nyamaza”. Baadhi ya wanazuoni wanalionia hili kama linarejelea kipindi cha mapumziko ya siku. KB 226 I wanadai kuna muundo mwingine wenye asili moja wenye maana “nusu” (NIDOTTE, juzu. 1, uk. 972). Leo la LXX linatafsiri kama “katika urefu wa siku zangu” ambao kwa uhakika ni usomaji unaofanana.

▣“**malango ya kuzimu**” tazama mada Maalum:wafu wako wapi? katika 5:14. “malango ya kuzimu” yanatajwa katika Ayu 38:17; Zab. 9:13; 107:18; na Mt. 16:18 (ambapo “kuzimu” inaitwa “kuzimu”). Hii ni sitiari ya kifo kama Gereza.

▣“**nimenyimwa mabaki ya miaka yangu**” Umri wa maisha ya mtu ulionekana kama ishara ya kukubaliwa na Mungu (yaani., Musa, kama vile. Kumb. 34:7; Yoshua, kama vile Yoshua 24:29). Ikiwa mtu alikufa pasipo mtoto ilionekana kama ni hukumu ya Mungu (kama vile. Zab. 55:23; 89:45,46-48; Mith. 10:27).

**38:11** Waebrania wa kale hawakukitazama kifo kama muunganikano na ushirika na Mungu, bali ni utengano wa maisha na Mungu. Agano la kale lina mwanga mdogo wa kuonyesha maisha baada ya kufa. Hata katika Agano jipya kwa kiasi Fulani lina utaji katika eneo hili, ingawa itatupatia habari zaidi.

▣“**BWANA....BWANA**” Leo la MT lina neno *Yah* (יה) kama vile 12:2; 26:4) mara mbili, ambapo yawezekana likawa moja יהוה (יְהוָה). Gombo la Isaya katika toleo la DSS lina jina moja la *Yah*.

▣“**pamoja na hao wakaao Duniani**” Tafsiri hii inapatikana kwa wingi kwenye fasiri za Kiingereza. Leo la MT lina neno “kukoma” (yaani., “nchi ya wafu” BDB 293 אַדְל); limebadilishwa kwenda “Dunia” (BDB 317 דָּלֶת) likitokana na baadhi ya matoleo ya Kiebrania ya MSS na Alama za kiaramu Targums). Leo la Kiebrania la USB linafikilia ni masihala ya kimakusudi juu ya neno (uk. 93), nasio mkanganyiko wa kimaandiko. Tungo “wakaao Duniani” pia inajitokeza kwenye Zab. 49:1.

**38:12** Hezekia anatumia sitiari mbili kuelezea mwisho wa maisha yake mapema .

1. Hema langu limeondolewa (kama vile2 Kor. 5:1; 2 Pet. 1:13,14)
2. Nimekatiliwa kutoka kitanda cha mfumi

Kuna swali ni kwa jinsi gani neno la kwanza linatafsiriwa kwenye toleo la MT, דָּוֹר (BDB 189, KB 217).

1. Kukaa,muundo pekee unaopatikana hapa (BDB 190,namba 4, KB 217 I), NASB, NRSV, NJB, JPSOA, REB
2. kizazi,umri wa kuishi, maana ya kawaida ya asili (BDB 189, KB 217 II),toleo la LXX, Peshitta, NKJV, TEV

Pia kuna swali juu ya KITENZI (הַלְּגָ, BDB 162, KB 191). Kinaweza kumaanisha

1. “nimekunja” kutoka גָּלֵל, BDB 164 II, *Niphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, kama vile. 34:4 (maana iliyotumika hapa pekee)
2. “limeondolewa” kutoka הַלְּגָ, *Niphil KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, maana ya kipekee hapa,kwa kawaida labda ina maanisha
  - a. funua , weka wazi
  - b. kuondoka, kwenda mbali

Tafsiri nydingi za kiingereza zinatumia uchaguzi Namba 2, zikifuatiwa na toleo la MT,lakini Namba 1 inafaa muktadha vizuri.

▣“Tangu mchana hata usiku wanimaliza”Hii ni Lugha ya kinahau (kama vileAyubu 4:20; Zab. 73:14) ya kukamilisha kitendo.

**38:13**

NASB	“nautuliza moyo wangu”
NKJV	“nimefikilia”
NRSV, NJB	“nalia kwa ajili ya msaada
TEV	“nimelia kwa maumivu”
REB	“nimeteseka kwa maumivu”

Andiko la Kimasoreti lina neno “nimekunjwa” (yaani “nimeutuliza moyo wangu”), שׁוֹה BDB 1000, KB 1436, *Piel KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, lakini wafasiri wengi wana uhakika kuwa limebadilishwa kwenda שעַ BDB 1002, KB 1443 I, ambalo lina maana “kuita kwa ajiri ya msaada,” kama vile 58:9, ambalo linafaa zaidi.

▣“kama simba- aivunja mifupa yangu yote” Kifo cha Hezekiakilionekana kama ni mapenzi ya BWANA. Watu wenyewe kuamini imani ya Mungu mmoja katika Agano la kale walifikilia kuwa yote yanababishwa na Mungu mmoja. Watu wa kale hawakutambua sababu ya pili. Kiebrania kinatumia sitiari imara kuelezea matendo ya Mungu, hapa kinatumia Simba.

**38:14** Kama mst. 13 unaelezea nguvu za BWANA, mst. 14 unaelezea udhaifu wa Hezekia.

1. NASB, NJB, REB – “nilivyolia”  
NKJV – “lia”  
NRSV – “kilio cha nguvu”  
TEV – “sauti yangu ni dhaifu na ndogo”  
KITENZI hiki (BDB 861, KB 1050, *Pilpel/KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) kina maana ya “lia kama ndege,” “lia kama ndege.” Hapa imetumika kwa ndege na 10:14,lakini sehamu zingine, limetumika kama pepo wachafu (kama vile. 8:19; 29:4).
2. “omboleza” – BDB 211, KB 237, *Qal/KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*, kama vile. 16:7; 59:11; Ezek. 7:16; Nah. 2:7. Inarejelea huzuni kwa ajili ya hali iliyopo.
3. Macho yamedhoofika kwa kutazama juu
  - a. “yamedhoofika” – BDB 195, KB 223, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, limetumika kwa ajiri ya maombi kwa Mungu katika Zab. 79:8; 116:6; 142:6 (kama vile. NIDOTTE, juzu 1, uk. 951)
  - b. “kutazama juu” – BDB 928, linaweza kuwa ni sitiari kwa ajiri ya mbinguni (kama vile. 32:15; 57:15; 58:4)

4. kuonewa – BDB 799, muundo huu unapatika hapa pekee. The *Pua*/KITENZI muundo katika 23:12 lina maana ya “gandamizwa.” Labda Hezekia alikuwa anafikilia Zab. 103:6 au 146:7.

▣ “**Ee BWANA**” Toleo la MT lina neno*adon* (BDB 10), kama katika mst. 16, sio YHWH, kama kwenye mistari ya 3,4,5,7,11,20 (mara mbili), 22.

▣ “**uwe mdhamini wangu**” KAULI SHURUTISHI hii (BDB 786, KB 876, *Qa*/KAULI SHURUTISHI) Inasimulia maombi ya Hezekia yalikuwa katika msingi wa udhaifu wake. KITENZI kina maannisha dhamana (kama vileAyubu 17:3; Zab. 119:122). YHWH pekee ndiye aliyekuwa mdhamana na tumaini la Hezekia!

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 38:15-20

<sup>15</sup>Niseme nini?

Yeye amenena nami, na yeye mwenyewe ametenda hayo;  
Nitakwenda polepole miaka yangu yote, kwa sababu ya uchungu wa nafsi yangu.

<sup>16</sup>Ee Bwana, kwa mambo hayo watu huishi;  
Na uhai wa roho yangu u katika hayo yote;  
Kwa hiyo uniponye na kunihuisha.

<sup>17</sup>Tazama; nalikuwa na uchungu mwangi kwa ajili ya amani yangu;  
Lakini kwa kunipenda umeniokoa na shimo la uharibifu;  
Kwa maana umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako.

<sup>18</sup>Kwa kuwa kuzimu hakuwezi kukusifu;  
mauti haiwezi kukuadhimisha;  
Wale washukao shimonii hawawezi kuitarajia kweli yako.

<sup>19</sup>Aliye hai, naam, aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo;  
Baba atawajulisha watoto kweli yako.

<sup>20</sup>Bwana yu tayari kunipa wokovu.  
Basi, kwa vinubi tutaziimba nyimbo zangu,  
Siku zote za maisha yetu nyumbani mwa Bwana.

**38:15-20** Ubeti huu unafunua thiolojia ya Agano la kale juu ya kuzimu. Maisha baada ya kufa ilikuwa sio sehemu ya kutamanika.

**38:15 “Yeye amenena nami, na yeye mwenyewe ametenda hayo”** Hii inaaksi ukuu wenyewe Enzi wa Mungu mmoja wa Israeli. Amenena ,yametendeka (kama vile 55:11)!

**38:16** Msitri wa pili ni mgumu katika toleo la MT. Toleo la LXXlinakitafsiri kama “utahuisha pumzi yangu”; toleo la JPSOA linakitafsiri kama “pumzi ya maisha yangu imehuishwa.”

**38:17**

NASB	“wewe uitunzae roho yangu”
NKJV	“wewe upendae kuikomboa roho yangu”
NRSV	“wewe umeyashikiria maisha yangu”
NJB	“wewe umeyahifadhi maisha yangu”
REB, Peshitta	“wewe umeniokoa mimi”

Toleo la MT lina KITENZI “upendo” (קְרָב BDB 365 I, KB 362, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU), lakini inavyoonekana hakifai vizuri kwenye mstari huu wa shairi, baadhi ya wanazuoni wanafikiri ni “shikilia” קְרָב BDB 362, kama vile 14:6; 54:2; 58:1.

▣ “**Kwa maana umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako**” Zaburi hii inasimulia Faraja ya Hezekia ya kwamba amekombolewa kutoka kuzimu. Bado, kwa jinsi gani tabia za Kiyahudi, maafa siku zote yanahusiana na Dhambi.

Haijulikani ni kwa namna gani matendo yeote ya Hezekia yaliyoona na YHWH yalistahilisha kifo chake mapema. Hata hivyo, ni maelezo ya kushangaza kwamba Mungu alimsamehe na kusahau. Tafadhalii linganisha Zab 103:11-14; Isaya 1:18; 43:2-5; 44:22; Yeremia 31:34; na Mika 7:19. Huu ni ukweli wa muhimu sana –Mungu anaposamehe, Mungu anaposahau! Waamino wengi wanadai msamaha wa Mungu msingi wake ni katika Ahadi za Kibiblia, lakini bado hatujaipata furaha yake kamili ya usahafulifu wa Mungu!

## MADA MAALUM: MANENO YA MSAMAH

Hapa pana maneno mengi ya Kiebrania au nahau ambazo zinazelezea msamaha wa Kiungu wa dhambi na uasi wa mwanadamu.

1. “samehe,” “samehe,” (סָמֵה – BDB 699, KB 757, yaani, Kut. 34:9; Law. 4:20, 26, 31, 35; 5:10,13, 16, 18; 6:7; 19:22; Hes. 14:20; 15:25-28; 30:5,8,12; I Fal. 8:30, 34, 36, 39, 50; Zab. 25:11;103:3; Isa. 55:7; Dan. 9:19; Amosi 7:2 (neno hili mara zote linatumika kumhusu Mungu, na kamwe si wanadamu)
2. “nifute,” “ondoa,” (נִשְׁאָה – BDB 669, KB 724, yaani., Kut. 23:21; 32:32; 34:7; Hes. 14:18; Yosh. 24:19; Zab. 25:18; 32:1,5; 85:2; 99:8; Mika 7:18
3. “funika,” “lipia kosa,” – BDB 497, KB 493, yaani., ni cha kawaida katika kitabu cha Walawi; Zab. 65:3; 78:38;79:9; Isa. 6:7; 22:14; Yer. 18:23; Ezek. 16:63; Dan. 9:24
4. “ondoa,” “futa,” – BDB 562, KB 567, yaani, Neh. 4:5; Zab. 51:1,9; Isa. 43:25; 44:22; Yer. 18:23
5. “ponya,” – בַּרְפָּא – BDB 950, KB 1272, yaani., II Nya. 7:14; Zab. 41:4; 103:3; Isa. 6:10; 57:18; Yer. 3:22; 17:14; 30:17; Hosea 5:13; 14:4
6. “kutokuwapita kamwe,” – עַבְרָ – BDB 716, KB 778, yaani., Mith. 19:11; Amosi 7:8; 8:2; Mika 7:18
7. “osha,” – כְּבָשׂ – BDB 460, KB 459, yaani, Zab. 51:2,7; Yer. 2:22; 4:14
8. “jitakase,” – טַהֲרָ – BDB 372, KB 369, yaani., Law. 16:30; Zab. 51:7; Mith. 20:9; Ezek. 24:13; 36:25
9. “umezitupa dhambi zote nyuma yako,” – שְׁלֹךְ – BDB 1020, KB 1527, yaani., Isa. 38:17; Mika 7:19
10. “unisafishe,” – אַעֲנָה – BDB 306, KB 305, yaani., Zab. 51:7 (kidokezo hiki cha kujisafisha Kiungu cha KITENZI kilichozoeleka, kinapatikana hapa tu)
11. “sitiri uso wako,” – סְתַרְ – BDB 711, KB 771, yaani., Zab. 51:9
12. “kumbuka” (kinyume), זְכָר – BDB 269, KB 269, yaani., Isa. 43:25
13. “kuyakanyaga” (kifasihi “jizuie”), כְּבָשׂ – BDB 461, KB 460, yaani., Mika 7:19

**38:20 “Bwana yu tayari kunipa wokovu”** Angalia Mada Maalum: Wokovu katika 33:2. Tambua “Wokovu” hapa kunahusiana na ukombozi wa kimwili kutoka katika kifo ili kuruhusu kuabudu Hekaluni wakati ujao, kama vile. mst. 22; 2 Fal. 20:5, zaidi kama Zab. 23:6.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 38:12-22

<sup>21</sup>Maana Isaya amesema, Na watwae mkate wa tini, wakauweke juu ya jipu, naye atapona. <sup>22</sup>Tena Hezekia alikuwa amesema, Iko ishara gani ya kunionyesha ya kuwa nitapanda niingie nyumbani mwa Bwana?

**38:21-22** Aya hizi haziko katika toleo la DSSla Isaya, lakini zipo katika toleo la LXX. Muundo wake umeonekana mwanzoni kwenye habari yenyewe katika 2 Fal. 20:7. Toleo la NJB linaziweka katika tafsiri yake baada ya mst. 6.

**38:21 “Na watwae mkate wa tini, wakauweke juu ya jipu, naye atapona”** Tunafahamu kutoka kwenye nyaraka zingine za kale za Israeli kwamba Tini ilitumika kama dawa (pia katika lugha ya Ugariti). Hapa tuna ukweli halisi wa ugonjwa wa Hezekia(yaani., jipu). Kwa vyovyote ni aina ya ukuaji wa saratani au jipu lililokaa sehemu ya mashaka isiyo salama.

Tambua ya kwamba YHWH ndiye anayeponya, lakini tabibu huweka dawa (yaani., tini). Na tena watu wa kale hawatofautishi kati ya asili ya kiroho na asili ya kawaida. Asili zote ni matokeo ya Mungu. Anaonyesha wazi anahusika na neno lake, watu wake wa Agano, na kila mmoja mmoja !

Aya hii ina VITENZI AMRISHI vitatu.

1. watwae – BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI
2. Wakauweke (Kifasihi. sugua) – BDB 598, KB 634, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI
3. atapona – BDB 310, KB 309, *Qal* KITENZI AMRISHI

## ISAYA 39

<b>MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>NASB</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hezekia aonyesha Hazina yake	Wajumbe wa serikali ya Babeli	Ubalozi wa Merodach-baladan	Wajumbe toka Babeli	Ubalozi wa Wababeli
39:1-4	39:1-2	39:1-4	39:1-3a	39:1-2
	39:3-8			39:3-4
			39:3b	
39:5-8		39:5-8	39:4	
			39:5-7	39:5-8
				39:8

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurwa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

#### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

- 9. Aya ya kwanza
- 10. Aya ya pili
- 11. Aya tatu
- 12. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

Kwa ajili ya mjadala mzuri wa tarehe zenyewe za ujio wa hawa wawakilishi angalia Gleason Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, kur. 212-213.

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 39:1-4**

<sup>1</sup> Wakati huo Merodaki-baladani, mwana wa Baladani, mfalme wa Babeli, alipeleka barua na zawadi kwa Hezekia; kwa maana amepata habari kwamba amekuwa hawezi, na kwamba amepona. <sup>2</sup> Hezekia akawafurahia, akawaonyesha nyumba yake yenye vitu vyake vya thamani, fedha na dhahabu, na manukato, na marhamu ya thamani, na nyumba yote yenye silaha zake za vita, na vitu vyote vilivyoonekana katika hazina zake; hapakuwa na kitu nyumbani mwake wala katika ufalme wake asichowaonyesha. <sup>3</sup> Ndipo Isaya nabii akamwendea mfalme Hezekia, akamwambia, Watu hawa walisema nini? Nao wametoka wapi kuja kwako? Hezekia akasema, Wametoka katika nchi ilio mbali, wakaja kwangu toka Babeli. <sup>4</sup> Ndipo akasema, Wameona nini katika nyumba yako? Hezekia akajibu, Wameviona vitu vyote vilivyomo nyumbani mwangu; hapana kitu katika hazina zangu nisichowaonyesha.

**39:1 “Merodach-baladan”** Huyu alikuwa mwana wa mfalme Bit-Yakin, aliyeitawala sehemu ya kusini mwa Babeli (721-710,703-702 K.K.) na aliyeinuka juu ya Ashuru, mara mbili. Angalia Tambuzi za Muktadha sura ya 38.

▣ **“mfalme wa Babeli alipeleka barua”** Inavyoonekana huyu mfalme wa Babeli alikuwa akitafuta ushirikiano dhidi ya Ashuru na, bahati mbaya, kiburi cha Hezekia kilimsababishia kutenda mambo ya kijinga (kama vile mst. 2) katika kudhihirisha uwezo alionao wa mali kwa hawa wajumbe wa Babeli. Yumkini alikuwa akitafuta ushirikiano mpya wa kisiasa.

**39:2**

NASB, NKJV	“akawafurahia”
NRSV, TEV,	
REB	“akawakaribisha”
NJB	“akafurahishwa”
LXX	“akafurahia”

Toleo la MT lina neno “kufurahia” (BDB 970, KB 1333, *Qal KITENZI KISICHO TIMILIFU*), ambalo mara nyingi hutumika kwa maana ya majivuno (kama vile Ayubu 31:29; Zab. 35:15,19,24; 38:16; Mith. 24:17; Ezek. 25:6; Mika 7:8).

▣ **“Hezekia akajibu, Wameviona vitu vyote vilivyomo nyumbani mwangu; hapana kitu katika hazina zangu nisichowaonyesha”** KITENZI “onyesha” (BDB 906, KB 1157) ni *Hiphil KITENDO CHA WAKATI TIMILIFU*. Mfalme kiukweli alikuwa anajaribu kulinga/kuonyesha ubora wake. Angelazimika binafsi kuwasindikiza wao kwenye maeneo yote na sehemu takatifu (kama vile mst. 4).

**39:3-4** Je? Isaya alikuwa akitafuta habari? Nafikiri lilikuwa ni swali lisilohitaji majibu kumtikisa mfalme!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 39:5-8**

<sup>5</sup> Ndipo Isaya akamwambia Hezekia, Basi, lisikie neno la Bwana wa majeshi. <sup>6</sup> Tazama, siku zinakuja, ambazo vitu vyote vilivyomo nyumbani mwako, na hivyo vilivyowekwa akiba na baba zako hata leo, vitachukuliwa mpaka Babeli; hapana kitu cho chote kitakachosalia; asema Bwana. <sup>7</sup> Na baadhi ya wana wako utakaowazaa, watakaotoka kwako, watawachukulia mbali; nao watakuwa matowashi katika jumba la mfalme wa Babeli. <sup>8</sup> Ndipo Hezekia akamwambia Isaya, Neno la Bwana ulilolinena ni jema. Tena akamwambia, Maana itakuwapo amani na kweli katika siku zangu mimi.

**39:5** Hii ni alama ya kifasihi (“sikia,” BDB 1033, KB 1570, *Qal KAULI SHURUTISHI*) kwa ajili ya ujumbe wa kiungu, dhahili unahusiana na kitendo cha Hezekia cha kutokuwa na subira

**39:6** Hii aya ni unabii wa kuja kwa mateka wa Kibabeli chini ya Nebukadneza II (yaani., 605, 597, 586, 582 K.K.). inaonekana kuwa msukumo wa Kibiblia sio tu kwa ajili ya (1) majivuno ya Hezekia, lakini pia (2)ibada za sanamu za mwanae, Manase (kama vile II Fal. 21:1-18); na (3) kuendelea kutokuamini kwa watu na ibada ya sanamu.Tatizo kubwa hapa ni Hezekia akijaribiwa kuamini ushirikiano wa kisiasa tena, kama aliyokuwanao na Misri mwanzoni. Mtu anaweza kufikiri jibu la ombi lake katika sura ya 38 lingaliweza kumlinda katika aina hii ya shughuli.

**39:7** Hii aya inashangaza sana, sio kwa sababu ni unabii wa kweli, lakini kwa sababu Isaya mara nyingi aliamini katika utakatifu wa Yerusalem na familia ya Daudi (kama vile II Samweli 7).

Pia kumbuka kuwa Babeli ya wageni wa Hezekia sio ile Babeli iliyosababisha mateka wanne. Mashairi mengi ya Isaya ni yenye utata kuweza kuhusianisha na

1. Ashuru

2. Babeli
3. Babeli mpya
4. Matukio ya siku za mwisho

❑ “**watachukuliwa mbali**” Hili lilitokea kwa mfalme Yehoakini (kama vile II Fal. 24:15).

❑ “**maakida**” Neno (BDB 710) kwa maana iliyo wazi linamaanisha “matoashi,” lakini liliuja kurejerea kwa maafisa wa baraza kuu (kama vile Potifa alioa, Mwa. 39:1). Katika muktadha huu neno lazima lirejeree kwa

1. ishara ya uwakilishi wa mamlaka ya Babeli
2. eneo la nchi

**39:8 “neno la Bwana ulilolinena ni jema”** Haya ni maelezo yenyeye kushangaza. Huenda yanamaanisha kuwa Hezekia alitambua kiburi chake kilikuwa ndio chanzo cha hukumu ya Mungu ya haki na, kwa hiyo, ni haki, au laweza kumaanisha, kama katika mst. 8b, kwamba anafuraha kuwa hukumu haitatokea katika kipindi chake. Baadhi ya wanazuoni wamedai kuwa sababu ya furaha ya mfalme ni kuwa inamaanisha atakuwa na mtoto wa kiume.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani dhana ya imani inahusiana na ujumbe wa maakida wa Ashuru wenye kujirudia katika Isaya 36 na 37?
2. Je? Hezekia alilipa kodi kwa Ashuru na alikuwa na ushirikiano wowote wa kijeshi na Misri?
3. Kwa nini Isaya 37:20 ni ya muhimu?
4. Kwa nini Mungu alitoa ishara mbili kwa Hezekia?
5. Kwa nini Hezekia alihukumiwa vikali kwa kuwaonyesha maakida wa Babeli thamani ya vitu alivyokuwa navyo?

# **KIAMBATISHO CHA KWANZA**

## **UTANGULIZI WA USHAIRI WA KIEBRANIA**

### **I. UTANGULIZI**

- A. aina hii ya fasihi imechukua 1/3 ya agano la Kale. Hasa ni ya kawaida kwa "manabii"(wote lakini Hagai na Malaki wanao ushairi) na "vipengere vya "maandiko"ya sheria za Kiebrania.
- B. Ni tofauti na ushairi wa Kiingereza. Mashairi ya Kiingereza yametokana na ushairi wa Kiyunani na Kilatini, ambao kimsingi unaeleweka vizuri. Ushairi wa Kiebrania unaendana na ushairi wa Kikanaani. Hauna mistari yenye lafudhi ya mashairi ya Mashariki ya Karibu(lakini kuna kipimo cha shairi).
- C. Uvumbuzi wa mabaki ya kale Kaskazini mwa Israeli katika maeneo ya Ugariti (Ras Shamra) umewasaidia wanazuoni kuuelewa ushairi wa Agano la Kale. Ushairi wa tokea karne ya 15 K.K dhahiri una uhusiano wa kifasihi na ule ushairi wa Kibiblia.

### **II. TABIA ZA USHAIRI KWA UJUMLA**

- A. Ni wenyе kushikamana .
- B. Unajaribu kuelezea ukweli, mawazo au taswira ya uelewa.
- C. Kimsingi umeandikwa sio kwa kusimuliwa. Kwa kiasi kikubwa umeumbika. Huu muundo unaelezewa katika:
  1. Mistari iliyolingana (dhana ya ufanano)
  2. Kuyachezea maneno
  3. Ufasaha wa sauti

### **III. MUUNDO WENYEWE (R. K. Harrison, Introduction To The Old Testament, kur.965-975)**

- A. Askofu Robert Lowth katika kitabu chake, Lectures on the Sacred Poetry of the Hebrews (1753) alikuwa wa kwanza kuanisha ushairi wa Kibiblia kama mawazo ya mistari yenye kulingana. Wengi wa watafasiri wa leo wamepanga kuonyesha mistari ya ushairi.
  1. Visawe –mistari inaelezea mawazo yale yale kwa maneno tofauti:
    - a. Zaburi 3:1; 49:1; 83:14; 103:13
    - b. Mithari 19:5; 20:1
    - c. Isaya 1:3,10
    - d. Amosi 5:24; 8:10
  2. Namna ya utabainishaji – mistari inajaribu kuelezea mawazo tofauti kwa namna ya kutofautiana au akianza na mawazo chanya na baadaye hasi:
    - a. Zaburi 1:6; 90:6
    - b. Mithari 1:29; 10:1,12; 15:1; 19:4
  3. Uunganishaji wa maneno – mistari miwili au mitatu inayofuata huanzisha mawazo - Zab. 1:1-2; 19:7-9; 29:1-2
  4. Tamathari za usemi – sehemu ya ushairi unaoelezea ujumbe katika hali ya mtiririko. Hoja kuu hupatikana katikati ya maelezo.
- B. A. Briggs katika kitabu chake, General Introduction to the Study of Holy Scripture (1899) kimeanzisha hatua mpya ya uchunguzi juu ya ushairi wa Kiebrania:
  1. Kama ishara ya – kishazi kimoja chenyewe na cha pili kiistiani, Zab. 42:1; 103:3.

2. Upeo au ngazi ya juu – vishazi vinadhihirisha ukweli katika namna ya mtiririko, Zab. 19:7-14; 29:1-2; 103:20-22.
  3. kugeuzwa –mlolongo wa vishazi, mara nyingi kwa kawaida vinne huhusiana na muundo wa ndani wa mstari wa 1 hadi 4 na 2 hadi 3 - Zab. 30:8-10a
- C. G. B. Gray katika kitabu chake, *The Forms of Hebrew Poetry* (1915) anaanzisha wazo la vishazi linganifu zaidi kwa:
1. Ulinganifu kamili – ambapo kila neno katika mstari wa kwanza unarudiwa au kulinganisha na neno la mstari wa pili - Zab 83:14 na Isaya 1:3
  2. Ulinganifu usio kamili ambapo vishazi havina urefu unaolingana - Zab. 59:16; 75:6
- D. Siku hizi kuna ukuaji wa kuvitambua vipengere vya kimuundo wa fasihi katika Kiebrania kiitwacho tamathari za semi, zinazoonyesha namba witiri za mistari zenye kufanana zinazounda umbo la shisha ambapo mstari wa kati ndio unaosisitizwa.
- E. Aina ya vipengere vya sauti vinavyopatikana katika ushairi kwa ujumla, lakini sio mara nyingi katika ushairi wa kimashariki
1. vinashirikiana kwenye alfabeti (aina ya chemshabongo. Kama vile. Zab. 9,34,37,119; Mith. 31:10 na kuendelea; Lm. 1-4)
  2. vinashirikiana kwenye konsonanti (marudio ya silabu za mwanzo, kama vile Zab. 6:8; 27:7; 122:6; Isa. 1:18-26)
  3. vinashirikiana kwenye irabu (ushairi, kama vile Mwa. 49:17; Kut. 14:14; Ezek. 27:27)
  4. vinashirikiana kwenye urudiaji wa vina vya maneno yenye kufanana vikiwa na maana tofauti
  5. vinashirikiana kwenye maneno ambayo, yikitajwa, yanasiyika kama kitu kilichotajwa (mlio wa kitu)
  6. Ufunguzi na ufungaji maalum (jumuishi)
- F. Kuna aina mbalimbali za ushairi katika agano la kale. Baadhi unahusiana na mada na mwingine unahusiana na muundo.
1. Nyimbo za kuwakifisha - Hes. 21:17-18
  2. Nyimbo za kazini - (zimedokezwa lakini hazikuandikwa katika Amu. 9:27); Isa. 16:10; Yer. 25:30; 48:33
  3. Tumbuizo - Hes. 21:27-30; Isa. 23:16
  4. Nyimbo wakati wa kunywa – zilizo kinyume, Isa. 5:11-13; Amos 6:4-7 na zilizo chanya, Isa. 22:13
  5. Mashairi ya mapenzi – Wimbo ulio Bora, mafumbo ya kwenye harusi - Amu. 14:10-18, nyimbo za harusini - Zab. 45
  6. maombolezo -(dokezo lakini halikuandikwa katika II Sam. 1:17 na II Nya. 35:25) II Sam. 3:33; Zab. 27, 28; Yer. 9:17-22; Lm.; Ezek. 19:1-14; 26:17-18; Nah. 3:15-19
  7. Nyimbo za vitani - Mwa. 4:23-24; Kut. 15:1-18,20; Hes. 10:35-36; 21:14-15; Yosh. 10:13; Amu.5:1-31; 11:34; I Sam. 18:6; II Sam. 1:18; Isa. 47:1-15; 37:21
  8. Dua maalum au Baraka za wazee - Mwa. 49; Hes. 6:24-26; Kumb. 32; II Sam. 23:1-7
  9. Maandiko ya kimiujiza - Balaamu, Hes. 24:3-9
  10. Mashairi matakatifu – Zaburi
  11. Mashairi ya kuchemshabongo - Zab. 9,34,37,119; Mith. 31:10 na kuendelea na Maombolezo 1-4
  12. Laana - Hes. 21:22-30
  13. Mashairi ya kudhihaki - Isa. 14:1-22; 47:1-15; Ezek. 28:1-23

IV. MWONGOZO WA KUUTAFASIRI USHAIRI WA KIEBRANIA

- A. Tazama kiini cha sehemu ya wimbo au ubeti (hii ni kama aya katika lugha ya mjazo.) toleo la RSV lilikuwa ni tafasiri ya kwanza ya kisasa kuutambua ushairi kwa kutumia ubeti. Linganisha tafasiri za kisasa kwa ajili ya tambuzi zenyeku kusaidia.
- B. Tambua lugha ya kitamathari na uielezee katika lugha ya mjazo. Kumbuka aina hii ya fasihi ni ya mjazo, mengi yamebaki kwa ajili ya msomaji kuyajaza.
- C. Uwe na uhakika kulinganisha hoja ndefu ilibobe kwenye mashairi na fasihi zake za kimuktadha (mara nyingi kitabu kizima) na muundo wa kihistoria.
- D. Waamuzi 4 na 5 ni ya kimsaada juu ya namna ushairi ulivyoelezea historia nzima. Waamuzi 4 ni lugha ya mjazo na Waamuzi 5 ni ushairi wa tukio la aina ile ile (pia linganisha Kutoka 14 na 15).
- E. Jaribu kutambua aina ya ufanano uliohusika, ikiwa ni visawe, namna ya utabainishaji, au uunganishaji wa maneno. Hii ni muhimu.

# KIAMBATISHO CHA PILI

## MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO LA KALE

### I. UTANGULIZI

#### A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haiamini namna ya ya kutafsiri unabii. Kweli zingine zimekwisha weka wekwa bayana kama ilivyo kwa nafasi ya Waorthodox katika karne nyingi, lakini si katika karne hii.
2. Zipo hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale
  - a. Premornarchial (Kabla ya utawala wa Kifalme)
    - (1) Watu binafsi walioitwa manabii
      - (a) Ibrahimu – Mwanzo 20:7
      - (b) Musa – Hesabu 12:6-8; Kumbukumbu la Torati 18:15; 34:10
      - (c) Haruni – Kutoka 7:1 (Msemaji wa Musa)
      - (d) Miriam – Kutoka 15:20
      - (e) Medad na Eldad – Hesabu 11:24-30
      - (f) Debora – Waamuzi 4:4
      - (g) Wasiokuwa na majina – Waamuzi 6:7-10
      - (h) Samweli - 1 Samweli 3:20
    - (2) Rejea ya manabii kama kundi – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
    - (3) Kundi la Kinabii au ushirika – 1 Samweli 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nakadhalika.
    - (4) Masihi aitwaye nabii – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
      - a. utawala wa kifalme usioandikwa (wakimlenga mfalme);
        - (1) Gadi – 1 Samweli 22:5; 2 Samweli 24:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:29
        - (2) Nathan – 2 Samweli 7:2; 1 Wafalme 1:22
        - (3) Ahijah – 1 Wafalme 11:29
        - (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1, 7, 12
        - (5) Wasiotajwa – 1 Wafalme 18:4, 13, 22
        - (6) Eliya – 1 Wafalme 18- 2 Wafalme 2
        - (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
        - (8) Elisha 2 Wafalme 2:9, 12-13
      - b. Maandiko ya kale ya manabii (yanayo lenga taifa pamoja na mfalme); Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

#### B. ISTILAHI ZA KIBIBLIA

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Samweli 9:9. Rejea hii yenyewe inatuonesha mpito kutoka katika neno nabi. *Ro'eh* inatokana na istilahi ya jumla "kuona." Mtu huyu alizielewa njia za Mungu na mipango yake na aliulizwa kutambua mapenzi ya Mungu katika jambo lolote.
2. *Hozeh* = "muonaji"(BDB 302, KB 3011), 2 Samweli 24:11. Ni jamii ya neno lenye maana sawa na *Ro'eh*. Inatokana na neno "kuona." Njeo ya wakati uliopita ya neno hili ni "tazama" ambalo limetumika mara nyingi ikimaanisha manabii.
3. *Nabi'* = "nabii" (BDB 611, KB 661), inayohusiana na lugha ya Akkadia ya kitenzi *Nabu* = "kuita" na kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neon limetajwa mara nyingi katika Agano la kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili kabisa hajulikana kwa hakika japo "kuita" kwa wakati huu inaonekana kama mbadala mzuri zaidi. Yawezekana uelewa mzuri zaidi unatoka YHWH's yanayoleza mahusiano ya Musa kwa Farao kuitia Haruni. (rejea kutoka 4:10-16; 7:1; Kumbukumbu la torati 5:5). Nabii ni mtu anayezungumza kwa niaba ya Mungu kwa watu wake. (Amosi 3:8; Yeremia 1:7,17; Ezekiel 3:4).

4. Istilahi zote tatu zinatumika katika huduma ya Nabii katika 1 Mambo ya Nyakati 29:29; Samueli – *Ro'eh*; Nathan – *Nabi'* and Gadi – *Hozeh*.
5. Kifungu cha maneno, '*ish ha* – '*elohim*, "Mtu wa Mungu" pia ni namna pana ya kumaanisha mse maji wa Mungu. Inatumika mara 76 katika Agano la Kale kwa kumaanisha "nabii"
6. Neno "Nabii" kwa asili ni la Kigiriki. Inatokana na neno (1) *pro* = "kabla" au "kwa niaba ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza."

## **II. MAANA YA UNABII**

- A. Neno unabii lilikuwa pana kimaana katika lugha ya kiebrania kuliko Kingereza. Vitabu vya historia vya Yoshua, Wafalme (isipokuwa Ruth) vinatajwa na Wayahudi kama "Manabii walioipa". Wote Ibrahimu (Mwanzo 20:7; Zaburi. 105:15) and Moses (Kumbukumbu la Torati 18:18) wanatajwa kama Manabii (pia Miriam, Kutoka 15:20). Kwahyo kuwa makini unapokuwa unatazama maana kutoka katika lugha ya Kingereza!
- B. "Unabii kisheria kabisa waweza kusema ni ule uelewa wa historia unaokubali maana zile tu zinazohusiana na uungu, kusudi la kiungu, ushirika wa kiungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, toleo la. 3, ukurasa wa. 896.
- C. "Nabii si mwanafalsafa au mwana taaluma ya Theolojia, bali msaidizi wa agano aletaye neno la Mungu kwa watu wake ili kutengeneza hatima zao kwa kufanya mageuzi ya siku zao za sasa," Prophets and Prophecy, Encyclopedia Judaica toleo la. 13 ukurasa wa. 1152.

## **III. KUSUDI LA UNABII**

- A. Unabii ni njia ya Mungu kuzungumza na watu wake, kuwapa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini katika kuyaendesha maisha yao na matukio ya duniani. Ujumbe wao ulikuwa wa jumla. Ilikusudiwa kuonya, kutia moyo, kuhamasisha imani na toba, na kuwafahamisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Iliwashikilia watu wa Mungu katika maagano na Mungu. Katika hili inatakiwa iongezwe kuwa mara nyingi imekuwa ikitumika kufunua uchaguzi wa Mungu wa wasemaji (Kumbukumbu la Torati 13:1-3; 18:20-22). Hii ukiipa umaanani kabisa utagundua ilimaanisha Mesiya
- B. Mara nyingi nabii aliachukua historia na migongano ya kithiolojia ya siku zake na kuangazia hayo katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho. Namna ya muono huu wa siku za mwisho kihistoria katika Israel ni wa kipekee na katika hali yakeya uchaguzi wa kiungu na ahadi za kiagano.
- C. Ofisi ya nabii inaonekana kutengeneza usawa (Yeremia 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Urimm na Thummim inabadilika katika ujumbe wa mdomo kutoka kwa mse maji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupita mbali katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei mpaka baada ya miaka 400 baadae kwa Yohana Mbatizaji. Haieleweki namna ambavyo kipawa cha "unabii" kwa Agano Jipya kinavyoshabihiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Wakorintho. 12:10,28-29; 14:29,32,37; Waefeso. 4:11) sio vifunuo vya ufunuo mpya au maandiko, bali wasimulizi wa yajayo na wazungumzaji wa mambo ya mbele ya mapenzi ya Mungu katika hali za agano.
- D. Unabii hauna msingi sana au hausisitizi katika utabiri kwa asili. Utabiri ni njia mojawapo ya kutthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, ila lazima izingatiwe "chini ya asilimia 2% ya unabii wa Agano la Kale ni kuhusu wa kimasiya". Chini ya asilimia 5% kiuhalisia inafunua nyakati za Agano Jipya. Chini ya asilimia 1% inahusu matukio yajayo. "fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).
- E. Manabii wanawakilisha Mungu kwa watu, wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Haya ni maelezo ya jumla. Kuna utofauti kwa kama Habakkuki, ambaye anauliza maswali kwa Mungu.
- F. Sababu moja inayoleta ugumu kuwaelewa manabii ni kwasababu hatujui muundo wa vitabu vyao. Havina mfuatano unaoeleweka. Vinaonekana ni vyenye hoja na mada kweli lakini si kama vile mtu angetegemea. Mara nyingi hakuna mazingira ya wazi ya kihistoria wala muda maalumu, au mgawanyiko wa wazi wa mambo ya kiungu. Vitabu hivi ni vigumu

1. Kuvisoma kwa mara moja
2. Kufafanua kwa mada
3. Kug'amuwa kweli kuu au kusudio la mwandishi katika kila uungu.

#### **IV. TABIA ZA UNABII**

- A. Katika Agano la Kale inaonekana kukua kwa dhana ya "nabii" na "unabii". Hapo mwanzo katika Israeli kulitokea ushirika wa manabii, ukiongozwa na viongozi shupavu wenyewe uvuvio wa Mungu kama Eliya na Elisha. Kuna wakati neno "wana wa manabii," ilitumika kuzungumzia kundi hili (Il Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia ya kujawa na furaha ya kupiliza (1 Samweli 10:10-13; 19:18-24)
- B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita mara kwa manabii mmoja mmoja. Kulikuwa manabii (wa kweli na waongo) waliojitalbulisha pamoja na mfalme, na waliishi katika Kasri la Kifalme (Gad, Nathan). Pia, kulikuwa na wale waliojitegomea, wakati mwingine wasiokuwa na hadhi kabisa za jamii ya ki-Israeli (Amos) walijumuisha wote wanawake na wanaume (2 Wafalme 22:14)
- C. Nabii mara nyingi alikuwa mfunuaji ya hatima, anayefanya katika mazingira ya mwanadamu yanavyoenda. Mara nyingi jukumu la nabii ilikuwa ni kufunua mpango wa Mungu kwa uumbaji wake ambaao hauathiriwi na mwitikio wa kibinadamu. Huu mpango wa wa ulimwengu wa matukio ya mwisho wa nchi ni wa kipekee katika manabii wa Mashariki ya Karibu ya kale. Utabiri na Agano ni mapacha waendao pamoja katika ujumbe wa kinabii (rejea Fee na Stuart, ukurasa wa 150). Hii inamaanisha manabii husisitiza ujumuishwaji katika lengo. Siku zote, japo si kila eneo, hujielekeza katika kuambia taifa.
- D. Mambo mengi ya kinabii yakinolewa kwa njia ya kinywa. Baadae iliunganishwa kwa njia ya mada, mfululizo, au namna nyingine ya uandishi wa Mashariki ya Karibu ambaao imepotea huku kwetu. Kwakuwa ilikuwa kwa njia ya kinywa, haikuwa na muundo kama unaokuwa katika kazi iliyo andikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma na ngumu kuelewa bila kuwa na historia ya mazingira halisi.
- E. Manabii walitumia namna kadhaa kuwasilisha jumbe zao
  1. Matukio ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake mahakamani, mara nyingi ni kesi ya kutalikiana ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwasababu ya kukosa uaminifu wake (Hosea 4; Micah 6).
  2. Mazingira ya msiba – mzani haswa kwa jaili ya ujumbe wa namna hii na tabia zake "ole" inajitenga kama aina yake kivyake vyake (Isaiah 5; Habbakkuk 2)
  3. Matamko ya Agano la Baraka - asili ya masharti ya Baraka imesisitizwa na madhara yake, yote ya wema na ubaya, yanatajwa kwa ajili ya baadae (Kumbukumbu la Torati 27-28).

#### **V. MIONGOZO YA KUKUSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII**

- A. Tafta kujua lengo la kwanza la nabii (mwandishi) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa maandishi ya kiungu.
- B. Soma na tafsiri mambo yote, sio sehemu tu; fafanua na yaliyomo. Angalia inavyoshabihiana na mazingira ya unabii. Jariibu kufafanua kitabu kizima.
- C. Endelea na kufanya makisio ya utafsiri wa kawaida wa hadithi mpaka vitu katika habari vikuelekeze katika matumizi yaliyofichwa kimaana; hivyo badili lugha iliyo fichwa katika maandishi.
- D. Fafanua matendo ya kiishara katika ufahamu wa mazingira ya kihistoria na usambamba wa hadithi. Kuwa na uhakika wa kukumbuka maanadishi ya kale ya Mashariki ya Karibu si kama yale ya kisasa ya kimagharibi.
- E. kuwa mwangalifu wa utabiri
  1. Je unahusisha siku za mwandishi?
  2. Je uliwahi kutimia katika historia ya Israeli?
  3. Je ni kweli yamekwisha kuwa matukio yajayo?
  4. Je yana kutimizwa kwa sasa nab ado yanashubiri kutimizwa siku zijazo?
  5. Waruhusu waandishi wa Biblia wakuongoze katika majibu na sio waandishi wa kisasa.

- F. Vitu vya kuzingatia
1. Je utabiri umekidhi kigezo cha sharti la mwitikio
  2. Kuna uhakika kwa Yule ambaye unabii umemlenga? (Na kwa nini)?
  3. Je kuna uwezekano, wa kibiblia na/au kihistoria, wa kutimia mara mbili?
  4. Waandishi wa Agano Jipyä, chini ya uvuvio waliweza kumuona mesiya katika sehemu nyingi katika Agano la Kale kiasi ambacho hakipo kwetu. Wanaonekana kutumia aina hii ya mchezo. Kwakuwa hatujavuviwa basi ni bora tukawaachia utaratibu huu wao.

## VI. VITABU VYA KIMSAADA

- A. *A Guide to Biblical Prophecy* by Carl E. Amending and W. Ward Basque
- B. *How to Read the Bible for All Its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
- C. *My Servants the Prophets* by Edward J. Young
- D. *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic* by D. Brent Sandy
- E. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, vol. 4, pp. 1067-1078
- F. *The Language and Imagery of the Bible* by G. B. Caird

# **KIAMBATISHO CHA TATU**

## **MAPITIO MAFUPI YA KIHISTORIA**

Mapitio ya historia fupi ya mamlaka za Mesopotamia (tukitumia tarehe zenyenye kusimamia kimsingi juu ya John Bright's A History of Israel, uk. 462 na kundelea):

A. Himaya ya Waashuru (Mwa. 10:11):

1. dini na tamaduni kwa kiasi kikubwa zilishawishiwa na himaya ya Wasumeri/Wababeli
2. Orodha ya mfano ya watawala na makisio ya tarehe:
  - a. 1354-1318 Asshur-Uballit I:
    - (1) akaupiga mji wa Wahiti wa Karkemishi.
    - (2) wakaanza kuondoa ushawishi wa Wahiti na kuruhusu Ashuru kukua.
  - b. 1297-1266 Adad Nirari I (mtawala mwenye nguvu).
  - c. 1265-1235 Shalmaneser I (mtawala mwenye nguvu).
  - d. 1234-1197 Tukulti-Ninurta I—ushindi wa kwanza wa himaya ya Babeli kuelekea Kusini.
  - e. 1118-1078 Tiglath-Pileser I—Ashuru inakuwa tawala yenye nguvu huko Mesopotamia.
  - f. 1012- 972 Ashur-Rabi II
  - g. 972- 967 Ashur-Resh-Isui II.
  - h. 966- 934 Tiglath-Pileser II.
  - i. 934- 912 Ashur-Dan II.
  - j. 912- 890 Adad-Nirari II.
  - k. 890- 884 Tukulti-Ninurta II.
  - l. 890- 859 Asshur-Nasir-Apal II.
  - m. 859- 824 Shalmaneser III.
    - vita ya Qarqar katika mwaka wa 853
  - n. 824- 811 Shamashi-Adad V.
  - o. 811- 783 Adad-Nirari III.
  - p. 781- 772 Shalmaneser IV.
  - q. 772- 754 Ashur-Dan III.
  - r. 754- 745 Ashur-Nirari V.
  - s. 745- 727 Tiglath-Pileser III:
    - (1) wakaitwa kwa jina la kiti chao cha enzi cha Babeli, Pul, katika II Fal. 15:19
    - (2) mtawala mwenye nguvu sana
    - (3) wakaanzisha utaratibu wa kuwaondoa watu walioshindwa
    - (4) katika mwaka wa 735 K.K. palikuwepo na uanzishaji wa ligi ya "Syro-Ephramatic," ambayo ilikuwa ikijaribu kuunganisha rasilimali zote zilizopo za kijeshi za mataifa ya ng'ambo ya Yordani tokea kwenye vyanzo vya Mto Frati huko Misri kwa ajili ya kusudi la kubatilisha kuinuka kwa mamlaka ya jeshi la Ashuru. Mfalme Ahazi wa Yuda akakataa kuungana nao na kuvamiwa na Israeli na Shamu. Akamwandikia Tiglath-Pileser III kwa ajili ya msaada dhidi ya ushauri wa Isaya (kama vile Isa. 7-12).
    - (5) katika mwaka wa 732 Tiglath-Pileser III akavamia na kuzishinda Shamu na Israeli na kuweka mfalme kibaraka juu ya kiti cha enzi cha Israeli, Hoshea (732-722 k.k.). maelfu ya Wayahudi wakakimbilia huko Umedi (kama vile II Fal. 15-16).
  - t. 727- 722 Shalmaneser V—Hoshea akatengeneza ushirikiano na Misri na kuvamiwa na Ashuru (kama vile II Fal. 17)

- u. 722- 705 Sargon II:
    - (1) baada ya kuuzingira mji kwa muda wa miaka mitatu, kulikoanzishwa na Shalmanesa V, jemedari wake na mrithi Sargon II, akaupiga mji mkuu wa Israeli, Samaria. Zaidi ya watu 27,000 wakakimbilia Umedi.
    - (2) Himaya ya Wahiti pia ikapigwa.
    - (3) katika mwaka wa 714-711 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi dhidi ya Ashuru. Ushirika huu ulijulikana kama "uasi wa Ashdodi." Hata Hezekia wa Yuda mwanzoni alishiriki. Ashuru ikavamia na kuiangamiza miji mbalimbali ya Wafilisti.
  - v. 705- 681 Sennacherib:
    - (1) katika mwaka wa 705 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi baada ya kifo cha babaye, Sargon II. Hezekia aliunga mkono kikamilifu huu uasi. Senakeribu akavamiwa katika mwaka wa 701. Uasi ulishindwa lakini Yerusalem ikahurumiwa kwa tendo la Mungu (kama vile Isa. 36-39 na II Fal. 18-19.)
    - (2) Senakeribu pia akauweka chini uasi huko Elam na Babeli.
  - w. 681- 669 Esarhaddon:
    - (1) mtawala wa kwanza wa Ashuru kuivamia na kuipiga Misri.
    - (2) alikuwa na huruma kubwa kwa ajili ya Babeli na kuujenga upya mji wake mkuu.
  - x. 669- 663 Assurbanipal:
    - (1) pia uliitwa Osnappar katika Ezra 4:10
    - (2) kakaye Shamash-shum-ukin alitawazwa kuwa mfalme wa Babeli. Pakaja kuwepo na miaka mingi ya amani kati ya Ashuru na Babeli lakini palikuwepo na mipango ya chini kwa chini ya kudai uhuru iliyoripuka katika mwaka wa 652, ikiongozwa na kakaye.
    - (3) kuanguka kwa Tebesi, 663
    - (4) kushindwa kwa Elamu, 653, 645
  - y. 633- 629 Asshur-Etil-IIlani.
  - z. 629- 612 Sin-Shar-Ishkun.
  - aa. a.a. 612- 609 Asshur-Uballit II:- mfalme aliyetawazwa akiwa uhamishoni huko Harani baada ya kuanguka kwa Asshur katika mwaka wa 614 na Nineva katika mwaka wa 612.
- B. Himaya ya Babeli mpya:
1. 703- ? Merodach-Baladan: akaanzisha uasi mbalimbali dhidi ya utawala wa Ashuru.
  2. 652 Shamash-Shum-Ukin:
    - (a) mwana wa Esarhadoni na nduguye Ashurbanipal.
    - (b) akaanzisha uasi mpya dhidi ya Ashuru lakini alishindwa.
  3. 626- 605 Nabopolasor:
    - a. alikuwa ni mtawala wa kwanza wa himaya ya Babeli mpya.
    - b. aliivamia Ashuru tokea kusini wakati Kaizari wa Umedi akavamia tokea Kaskazini.
    - c. mji mkuu wa kale wa Ashuru, Ashurr uliangushwa mwaka wa 614 na mji mkuu maarufu wa Nineva ukaangushwa mwaka wa 612
    - d. mabaki ya jeshi la Ashuru yakakimbilia Harani. Hata wakaamua kumsimamisha mfalme
    - e. katika mwaka wa 608 Farao Necho II ( kama vile II Fal. 23:29) akaelekeea Kaskazini kusaidia mabaki ya jeshi la Ashuru kwa ajili ya kusudi la kuunda kinga ya ulinzi dhidi ya mamlaka inayoinukia ya Babeli. Yosia, mfalme wa Yuda mwenye maadili ya Kiungu (kama vile II Fal. 23), akakipinga kikundi cha jeshi la Misri kilichopitia Palestina. Kulikuwepo na vita ndogo huko Megido. Yosia alijeruhiwa

na kufariki (II Fal. 23:29-30). mwanae, Yehoahazi, akawa mfalme.

Farao Necho II akachelewa kuuzuia uharibifu wa majeshi ya Waashuru huko Harani.

Alishambuliwa na majeshi ya Babeli yaliyoamriwa na mwana wa mfalme

Nebukadneza II na alishindwa vibaya katika mwaka wa 605 huko Karkemishi juu ya mito ya Frati. akiwa njia kuelekea Misri akasimama Yerusalem na kuuteka nyara mji. Alimbadilisha na kumwondoa Yehoahazi baada tu ya miezi mitatu. Akamweka mwanae mwengine wa Yosia kwenye kiti cha ufalme, Yehoiakimu (kama vile II Fal. 23:31-35).

- f. Nebukadneza II akalifukuza jeshi la Wamisri kuelekea kusini kuitia Palestina lakini alipokea ujumbe wa kifo cha babaye na akaamua kurudi Babeli.

Baaadaye mwaka huo huo akarudi Palestina. Akamwacha Yehoiakini akiwa kwenye kiti cha ufalme wa Yuda lakini akawachukua mateka wakazi wengi na jamii ya familia ya kifalme. Danieli na rafikize walikuwa ni moja ya watu walifukuzwa.

4. 605-562 Nebukadneza II:

- a. tokea mwaka wa 597-538 Babeli rasmi ikaitawala Palestina.
- b. katika mwaka wa 597 safari nyingine toka Yerusalem ikatokea kwa sababu ya Yehoiakimu kushirikiana na Misri (II Fal. 24). Akafa kabla ya kuja kwa Nebukadneza II. Mwanae Yehoiakini alitawala kwa muda wa miezi mitatu tu mpaka pale alipokimbilia Babeli. Watu elfu kumi, akiwemo Ezekieli, wakaweka makazi karibu na mji wa Babeli kwenye mfereji wa Kebari.
- c. katika mwaka wa 586, baada ya kuendelea kucheza na Wamisri, mji wa Yerusalem moja kwa moja ukaangamizwa (II Fal. 25) na kundi kubwa la watu kukimbilia ikitokea. Zedekia, aliyewekwa mbadala wa Yehoiakini, alikimbilia na Gedalia akachaguliwa kuwa gavana.
- d. Gedalia aliuwawa na majeshi yaliyoasi. Na majeshi haya yalikimbilia Misri na kumrazimisha Yeremia kwenda nao. Nebukadneza akavamia mara ya nne (605, 596, 586, 582) na kuwafukuza Wayahudi wote walioonekana kubaki.

5. 562-560 yule mwovu-Merodaki, pia alijulikana kama Amel-Marduk

- akamwachia Yehoiakimu toka gerezani lakini alitakiwa kubaki huko Babeli (kama vile II Fal. 25:27-30; Yer. 52:31).

6. 560-556 Neriglissar.– alikuwa generali mkuu wa Nebukadneza aliyeuangamiza mji wa Yerusalem

7. 556- Labaski-Marduk

- alikuwa mwana wa Neriglisa lakini aliuwawa baada ya miezi minane tu

8. 556-539 Nabonidasi:

- (a) Nabonidasi hakuwa akihusiana na nyumba ya kifalme kwa hiyo akamwoa binti wa Nebukadneza II

(b) alitumia muda wake mwengine kulijenga hekalu la mungu wa mwezi Sin huko Tema. Alikuwa mwana wa kuhani wa kike wa mungu wa kike. Hii ilimsababishia uadui na makuhani wa Marduk, mungu mkuu wa Babeli.

(c) alitumia muda wake mwengine akijaribu kuutuliza uasi na kuimalisha ufalme

(d) alielekeea Tema na kuachia mambo yote ya kiserikali kwa mwanae, Belshaza, ndani ya mji mkuu huko Babeli (kama vile Dan. 5)

9. ? -539 Belshaza (mtawala mwenza)– mji wa Babeli ulianguka haraka mikononi mwa jeshi la Wamedi na Waajemi chini ya Gobryas wa huko Gutiumu kwa kuchepusha maji ya Mto Frati na kuingia ndani ya mji pasipo kuzuiliwa. Makuhani na watu wa mji waliwaona Waajemi kama wakombozi na warejeshaji wa Marduku. Gobryasi alifanywa kuwa gavana wa Babeli na Koreshi II. Huenda Koreshi II au Gobryasi ni “Dario Mmedi” wa Dan. 5:31 na 6:1. Jina Dario linamaanisha “mtu wa familia ya kifalme.”

- A. Himaya ya Umedi na Uajemi: Utafiti juu ya kuinuka kwa Koreshi II (Isa. 44:28; 45:1-7):
1. 625-585 Kaizari was the king of Media who helped Babylon defeat Assyria.
  2. 585-550 Astyages alikuwa mfalme wa Umedi. Koreshi alikuwa mwanae mkubwa kwa Mandane.
  3. 550-530 Koreshi II wa Anshamu alikuwa mfalme kibaraka aliyeasi.
    - (a) Nabonida, mfalme wa Babeli, alimuunga mkono Koreshi.
    - (b) Koreshi II akamwondoa kwenye kiti cha utawala Astyages.
    - (c) Nabonida, ili kurejesha usawa kwenye madaraka, alishirikiana na:
      - (1) Misri.
      - (2) Kroesa, mfalme wa Lidia (Asia Ndogo).
  4. 547- Koreshi II akaukabili mji wa Sardi (mji mkuu wa Lidia).
  5. November 2, 539, Gobryas wa Gutiumu, akiwa na jeshi la Koreshi, akaichukua Babeli pasipo upinzani. Gobryas akawa gavana wa Babeli.
  6. 539- kwenye mwezi wa kumi, Koreshi II “mkuu” binafsi akaingia kama mkombozi. Sera zake za wema kwenye makundi ya kitaifa yakaigeuza sera ya kitaifa ya miaka ya kuikimbia nchi.
  7. 538- Wayahudi na wengineo wakaruhusiawa kurudi nyumbani na kuyajenga makazi yao.
  8. 530- Mwana wa Koreshi, Kambiase II, akamurithi babaye.
  9. 530-522 kutawala kwa Cambiase II.– aliiongeza himaya ya Misri katika mwaka wa 525 kuwa moja ya himaya ya Umedi na Uajemi.  
– yawezekana alijua.
  10. 522-486 Dario I akaingia kwenye kutawala.
    - (a) alikuwa sio mmoja wa ukoo wa kifalme lakini alikuwa generali wa jeshi
    - (b) (b)aliimiliki himaya ya Uajemi akitumia mipango ya Koreshi kwa ajili ya maliwali wa Kiajemi (kama vile Ezra 1-6; Haggai; Zekaria)
    - (c) Akaweka sarafu kama Lidia.
  11. 486-465 kutawala kwa Ahusuero I:
    - (a) aliuangusha uasi wa Wamisri.
    - (b) akakusudia kuivamia Ugiriki na kutimiza ndoto ya Uajemi lakini akapigwa kwenye vita vya Thermopoly katika mwaka wa 480 na Salamisi katika mwaka wa 479.
    - (c) Mume wa Esta aliyeitwa Ahasuero katika Biblia aliuawa katika mwaka wa 465.
  12. 465-424 Artashasta I akatawala (kama vile Ezra 7-10; Nehemia; Malaki):
    - (a) Ugiriki ikaendelea kusonga mbele mpaka walipokabiliana na vita ya ndani ya Pelopanisia.
    - (b) Ugiriki ikagawanyika (Atheni - Pelopanisian).
    - (c) Vita ya ndani ya Uturuki ilidumu kwa muda wa mika 20.
    - (d) wakati wa kipindi hiki jamii ya Wayahudi iliendelea kuimalika.
  13. 423-404 Dario II akatawala.
  14. 404-358 Artashasta II akatawala.
  15. 358-338 Artashasta III akatawala.
  16. 338-336 Arsa akatawala.
  17. 336-331 Dario III akatawala.
- D. mapitio juu ya Misri:
1. Hyksos (mfalme wa wachungaji – mtawala wa Kisemiti)-1720/10-1550 K.K.
  2. Utawala wa karne ya 18th (1570-1310 K.K.)
    - a. 1570-1546 Amosi

- b. 1546-1525 Amenophi I (Amenhotep I).
  - c. 1525-1494 Thutmosi I
  - d. ? Thutmosi II
  - e. ? Hatshepsuti
  - f. 1490-1435 Thutmosi III
  - g. 1435-1414 Amenophi II.
  - h. 1414-1406 Thutmosi IV
  - i. 1406-1370 Amenophi III
  - j. 1370-1353 Amenophi IV (Akhenaten)
  - k. ? Smenkhare
  - l. ? Tutankhamun
  - m. ? Ay
  - n. 1340-1310 Haremhab
3. Utawala wa karne ya 19 (1310-1200 K.K.):
- a. ? Ramesesi I
  - b. 1309-1290 Seti I
  - c. 1290-1224 Ramesesi (Ramesesi II)
  - d. 1224-1216 Marniptah (Merenptah)
  - e. ? Amenmesesi
  - f. ? Seti II
  - g. ? Siptah
  - h. ? Tewosret
4. Utawala wa karne ya 20 (1180-1065 K.K.):
- a. 1175-1144 Ramesesi III
  - b. 1144-1065 Ramesesi IV – XI
5. Utawala wa karne ya 21 (1065-935 K.K.):
- a. ? Smenda
  - b. ? Heriho
6. Utawala wa karne ya 22 (935-725 K.K - Libya):
- a. 935-914 Shishaki (Shosenki I au Sheshong I)
  - b. 914-874 Osorkoni I
  - c. ? Osorkoni II
  - d. ? Shoshneki II
7. Utawala wa karne ya 23 (759-715 K.K. - Libya)
8. Utawala wa karne ya 24 (725-709 K.K.)
9. Utawala wa karne ya 25 (716/15-663 K.K. - Kushi/Nubi):
- a. 710/09-696/95 Shabako (Shabaku)
  - b. 696/95-685/84 Shebteko (Shebitku)
  - c. 690/89, 685/84-  
664 Tirhakah (Taharqa)
  - d. ? Tantamun
10. Utawala wa karne ya 26 (663-525 K.K. - Saitic):
- a. 663-609 Psammetichus I (Psamtik)
  - b. 609-593 Neco II (Necho)
  - c. 593-588 Psammetichus II (Psamtik)

- d. 588-569 Apries (Hophra)
  - e. 569-525 Amasis
  - f. ? Psammetichus III (Psamtik)
11. Utawala wa karne ya 27 (525-401 K.K. - Uajemi):
- a. 530-522 Cambyses II (mwana wa Korshi II)
  - b. 522-486 Dario I
  - c. 486-465 Ahusuaero I
  - d. 465-424 Artashasta I
  - e. 423-404 Dario II

\*kwa ajili ya kuutofautisha mfuatano wa matukio angalia Zondervan's Pictorial Bible Encyclopedia, juzuu ya 2 uk.

231.

E. Utafiti juu ya Ugiriki:

1. 359-336 Filipo II wa Makedonia:
  - a. akaijenga Ugiriki.
  - b. aliuawa mwaka wa 336.
2. 336-323 Iskanda II "mkuu" (mwana wa Filipo):
  - a. akamkimbia Dario II, mfalme wa Uajemi, kwenye vita ya Isus.
  - b. akafa mwaka wa 323 huko Babeli kwa homa akiwa na umri wa miaka 33/32.
  - c. magenerali wa Iskanda wakaigawa himaya wakati wa kifo chake:
    - (1) Cassender - Makedonia na Ugirik
    - (2) Lysimicus – Thrace
    - (3) Seleucus I - Shamu na Babeli
    - (4) Ptolemy – Misri na Palestina
    - (5) Antigonus - Asia Ndogo (hakudumu muda merfu)
3. Wajumbe wa utawala wa Uyunani waliokuwa wakitawala Shamu (Seleucids) dhidi ya majina ya watawala wote wa Makedonia walioko Misri (Ptolemies) kwa ajili ya kuidhibiti Palestina
  - a. Shamu (wajumbe wa utawala wa Uyunani):
    - (1) 312-280 Seleucus I
    - (2) 280-261 Antiochus I Soster
    - (3) 261-246 Antiochus II Theus
    - (4) 246-226 Seleucus II Callinicus
    - (5) 226-223 Seleucus III Ceraunus
    - (6) 223-187 Antiochus III the Great
    - (7) 187-175 Seleucus IV Philopator
    - (8) 175-163 Antiochus IV Epiphanes
    - (9) 163-162 Antiochus V
    - (10) 162-150 Demetrius I
  - b. Watawala wa Misri (Ptolemaic):
    - (1) 327-285 Ptolemy I Soter
    - (2) 285-246 Ptolemy II Philadelphus
    - (3) 246-221 Ptolemy III Eugegenes
    - (4) 221-203 Ptolemy IV Philopator
    - (5) 203-181 Ptolemy V Epiphanes
    - (6) 181-146 Ptolemy VI Philometor

c. mapitio kwa ufupi:

- (1) 301- Palestina chini ya mtawala Ptolemy kwa miaka mingi
- (2) 175-163 Antiokia IV Epiphanes, mtawala Seleucid wa karne ya 8, akataka kuwabadili Wayahudi kuwa Wayunani kwa nguvu:
  - (a) akajenga nyumba ya kufanyia mazoezi ya viungo.
  - (b) akajenga madhabahu ya wapagani ya Zeus Olympius ndani ya hekalu

**KIAMBATISHO CHA NNE  
(MICHORO)  
KIPINDI MUHIMU CHA MATUKIO YA AGANO LA KALE**

MALAKI

ARTAXERXES I (P)


XERXES I - AHASUERO (P)

EZRA  
7-10  
NEH.

ESRA

ESRA  
9

UKUTA WA YERUSALEMU - NEHEMIA  
KURUDI MARA YA TATU - EZRA



P - GEDALIA (P)  
 O - ZEDEKIA (J)  
 R - YETHOAKINI (J)  
 M - YETHOAKINII (J)  
 L - YETHOAHARI (J)  
 K - YOSIA (P)  
 J - MANASE (J)  
 i - HEZEKIA (J)  
 h - UZIA (J)  
 g - YEROBOAMII (I)

f - ATTABU (I)  
 e - YEROBOAMI (I)  
 d - REHOBOAM (J)  
 c - SULEIMANI (UM)  
 b - DAUDI (UM)  
 a - SAULI (UM)

1 - MNARA WA BABELI (A)  
 1 - GHARITA YA NUTTU (B)  
 1 - ANGUKO LA Mwanadaru (2)  
 1 - UUMBaji (1)

## **WAFALME NA MATUKIO YA WABABELI, WAAJEMI, NA WATAWALA WA KIYUNA**

- 612 K.K. Nineva ikaangukia mikononi mwa jeshi la Babeli Mpya (Nebukadneza)  
608 Pharaoh Necho II akamwenda Karkemeshi kuzuia kulanuka kwa  
mamlaka Babeli Mpya, Yosia mfalme wa Yuda, akajaribu kumuzuia  
Mauti ya Yosia na jaribio la mwanae, Yehoahazi kukikalia kitu cha ufalme  
Yehoiakimu, mwana mwengine wa Yosia, akafanya mbadala wa Yehoahazi juu ya mamlaka ya  
Farao  
Necho II ndani ya miezi 3  
Palestina na Shamu chini ya utawala wa Misri  
Mageuzi ya Yosia yakagonga mwamba
605. Nabopolosa akatuma vikosi kupigana na jeshi la Waashuru waliobaki na Wamisri huko  
Karkemeshi  
Nebukadneza akawafukuza kote mpaka kwenye nyanda za Palestina  
Nebukadneza akapata habari ya kifo cha baba yake (Nabopolosa) kwa hiyo akarudi Babeli kwenda  
kuvishwa taji ya kifalme  
Akiwa njiani kuelekea huko akawachukua Danieli na wafuasi wengine wa familia ya kifalme  
kuwapeleka uhamishoni
- 605 - 538 Babeli ikaikilia mamlaka ya Palestina, 597; 10,000 wakakimbilia uhamishoni huko Babeli  
586 Yerusalem na hekalu vikaangamizwa na wengi wao wakakimbilia uhamishoni  
582 kwa sababu wapiganaji wengi wa msituni wakamuua Gedaliana kutokana na kundi kubwa  
kukimbilia uhamishoni

## **WARITHI WA NEBUKADNEZA**

- 562 - 560 Mwenye hila-Merodaki akamfungua Yehoiakimu (ukoo wa kimasihii) toka kifungoni  
560 - 556 Neriglisa  
556 Labaski-Marduk akatawala  
556 - 539 Nabonida:  
  
Akatumia muda mwangi kumjengea hekalu mungu wa hasira, *Sin*. Hili likasababisha uadui na  
kuhanu wa Marduk.  
Akatumia muda wake uliobaki kuweka chini maasi yote na kuimalisha ufalme.  
akaelekeea Tema na kukabidhi mambo yote ya nchi kwa mwanaye, Belshaza  
Belshaza:  
Alitumia muda wake mwangi kujaribu kuimarisha utaratibu mzuri.  
Tishio kubwa la Babeli lilikuwa ni Umedi

## **KUINUKA KWA KORESHI**

- 585 - 550 Astyages alikuwa mfalme wa Umedi (Koreshi wa II alikuwa mjukuu wake kwa Mandane)  
550 Koreshi II, kibaraka wa mfalme, akamuasi  
Nabonida, ili kurejesha usawa wa madaraka, akashirikiana na:  
1. Misri

	2. Crecus, mfalme wa Lidia
547	Koreshi akaukabili Sardi (mji mkuu wa Lidia) na kuiteka Asia Ndogo yote
539	Gobiyasi akaichukua Babeli pasipo upinzani wowote (Dan. 5; Belshaza kaimu mwenza wa Nabonida;
	Pia Gobiyasi yumkini Dario Mmedi, Dan. 5:31).
Oct. 11, 539	Koreshi akaingia kama mkombozi baada ya mungu wa kike wa Nabonidusi, Zin

## **WARITHI WA KORESHI**

530	Koreshi akamrithi (Kambiasi II)
530 - 522	Utarwala wa Cambyses (magombo ya kisiwa cha Elefantino)
	Akaiongeza Misri katika mwaka wa 525 kwenye himaya ya Umedi na Uajemi
522 - 486	Dario akaingia madarakani
	Akaiongoza Himaya ya Uajemi pamoja na mpango wa Koreshi wa Gavana wa majimbo
	Akaweka mpango wa kutengeneza sarafu kama wa huko Lidia
486 - 465	Ahusuero I (Esta)
	Kuuangusha uasi wa Wamisri
	Alikusudia kuivamia Ugiriki, lakini akashindwa katika vita na Thermopoly mwaka 480
	Ahusuero I aliuawa katika mwaka wa 465
480	Vita ya Thermopoly
465 - 424	Artishasta I Longimanus (Ezra 7-10, Nehemia, na Malaki)
	Uyunani ikaendelea kusonga mbele mpaka walipokabiliana na vita ya Pelopanisia
	Vita ikadumu kwa muda wa miaka 20
	Wakati wa kipindi hiki jamii za Kiyahudi zikatengenezwa upya
423 – 404	Dario II
	Akaruhusu karamu ya mikate isiyochacha katika hekalu la Elephantino
404 - 358	Artishasta II
358 – 338	Artishasta III
338 – 336	Arses
336 - 331	Dario III

## **UGIRIKI**

359 – 336	Filipo II wa Makadonia akaijenga Ugiriki aliuawa mwaka wa 336
336 - 323	Iskanda Mkuu (mwana wa Filipo) Akamfukuza Dario II kwenye vita ya ISUS
	Alikufa mnamo mwaka 323 huko Babeli kwa homa baada ya kuzitwaa Mashariki ya Mediterania na Mshariki ya Karibu
	Makamanda wa Iskanda wakaigawa himaya yake wakati wa kufa kwake:
	1. Cassander - Makedonia na Ugiriki
	2. Lysimicus - Thrace
	3. Selects I - Shamu na Babeli
	4. Ptolemy – Misri na Palestina

### **Tatawa za Shamu dhidi ya Makedonia**

301	Palestina ilikuwa chini ya utawala wa Ptolemy kwa muda wa miaka 100
175 - 163	Antiochus Epiphanes Akataka kuwageuza Wayahudi kuwa Wayunani, akajenga ukumbi wa michezo ya viungo Akajenga madhabahu ya kipagani; makuhani wao wakatendwa visivyo
Dec. 13, 168	Hog akaauawa juu ya madhabahu na baadhi wakalifikiria hili kama chukizo lenye kuhuzunisha.

### **WATAWALA**

#### **BABELI**

626 – 605	Nabopolasa akafa (“Nabu, akasimama”)
	625 - 585
	Kaizari
605 - 562	Nebukadneza II (“Nebo, akaulinda mpaka”)
	585 - 550
	Astyages
562 - 560	Merodack muasi 550
	Koreshi II
556	Labaski Marduk
556 – 539	Nabonida
	Belshaza
539 -	Gobiyas

#### **UMEDI**

550 - 530	Koreshi II (mwaka wa 538 Umedi na Uajemi ukamiliki madaraka ya Himaya ya Akaemenia
530 - 522	Kambiasi II (akajiongezea Misri na Cyprus)
522	Gaumata, Smerdis (akatawala miezi 6)
522 - 486	Dario I (Hystaspes)
486 - 465	Ahusuero I (mme wa Esta)
465 - 424	Artashasta I (Ezra na Nehemia wakiwa huko Palestina)
423 -	Ahusuero II
424 - 404	Dario II Nothus

404 - 359	Artashasta II Mnemon
359 - 338	Artashasta III Ochus
338 - 336	Arses
336 - 331	Dario III Codomannus

## UYUNANI

359 – 336	Filipo II wa Makedonia
336 – 323	Iskanda Mkuu
323 -	Majenerali waliigawa Himaya

- 1. Kasanda - Makedonia
- 2. Lysimicus - Shamu
- 3. Seleucus I - Shamu na Babeli
- 4. Ptolemy - Misri
- 5. Antigonus - Asia Ndogo (aliuawa mnamo mwaka wa 301 K.K.)

Watawala wa Makedonia wakaitawala Palestina, lakini katika mwaka wa 175 - 163 utawala ukawa mikononi mwa watawala wa Shamu

175 - 163 Antiochus IV Epiphanes, mtawala wa nane wa Shamu

\*Tarehe na majina kwa kiasi kikubwa yamechukuliwa toka kwenye kitabu cha *A History of Israel* cha John Bright, kurusa za 461-471.

## WAFALME WA UFALME ULOGAWANYIKA

WAFALME WA YUDA(I NYA. 3:1-16; MT. 1:6-11)					WAFALME WA ISARELI				
MAJINA NA TAREHE	BRIGHT T	YOUNG	HARRISON	MAANDIKO YA BIBLIA	MAJINA NA TAREHE	BRIGHT T	YOUNG	HARRISON	MAANDIKO YA BIBLIA
Rehoboamu	922-915	933-917	931/30-913	1 Fal. 11:43-12:27; 14:21-31 2 Nya. 9:31-12:16	Yerohoboam I	922-901	933-912	931/30-910/09	1 Fal.11:26-40; 12:12-14:20
Abiya (Abiyamu)	915-914	916-914	913-911/10	1 Fal.14:31-15:8 2 Nya.11:20,22	Nadabu Baasha	901-900	912-911	910/09-909/08	1 Fal.14:20; 15:25-31
Asa	913-873	913-873	911/10-870/69	1 Fal.15:8-30; 16:8,10,23,29; 22:41,43,46 Yer.41:9		900-877	888-887	886/85-885/84	1 Fal.15:16-16:17; 2 Fal. 9:9 2 Nya. 16:1-6 Yer. 41:9
Yehoshefati	873-849	873-849	870/69-848	1 Fal.15:24; 22:1-51 2 Fal.3:1-12; 8:16-19 1 Nya.3:10 2 Nya. 17:1-12:1	Ela	877-876	888-887	886/85-885/84	1 Fal.16:8-14
(Yehoramukaimumwenza)	-----	-----	853-848	1 Fal.22:50 2 Fal. 1:17; 8:16; 12:18	Zimri (kamanda wa jeshi) Omri (kamanda wa jeshi)	876 876-869	887 887-877	885/84 885/84-874/73	1 Fal.16:9-20 2 Fal.9:31 1 Fal.16:15-28 2 Fal.8:26 Mika 6:16
Yehoram	849-842	849-842	848-841	2 Fal.8:24-9:29 2 Nya. 22:1-9	Ahabu Ahazia	869-850	876-854	874/73-853 853-852	1 Fal.16:29-22:40
Ahazia	842	842	-----			850-849	854-853	852-841	1 Fal.22:40,41, 49,51-53 2 Nya.18:1-3,19
Atalia (malkia)	842-837	842-836	841-835	2 Fal.8:26; 11:1-20 2 Nya.22:2-23:21 2 Fal.11:2-3; 12:1-21 2 Nya.22:11-12; 24:1-27	Ahazia Yehoramu	849-842	853-842	841-814/13	2 Fal.1:17;3:1-27;8:16-9:29
Yoashi	837-800	836-797	835-796			842-815	842-815	798-782/81	1 Fal.19:16-17 2 Fal.9:1-10:36 15:12 2 Nya.22:7-9 Hosea 1:4
Amazia (kaimu)	800-783	797-779	796-767	Yehu (kamanda wa jeshi)	801-786	798-783	798-782/81	2 Fal.13:9-13,25 2 Nya.25:17-25	
	-----	-----	791/90-767			801-786	798-783		

mweza wa Uzia)				2 Fal.12:21; 14:1-22 2 Nya. 25:1-28					Hosea 1:1 Amosi 1:1
(kaimu mwenza wa Yothamu)	750-742	-----	750-740/39	2 Nya.26:1-23 Hosea 1:1 Amosi 1:1 Zakaria 14:5	Yehosa	-----	-----	793/92- 782/81	2 Fal.13:13; 14:16,23-29 Hosea 1:1
Yothamu	742-735	740-736	740/39- 732/31	2 Fal.15:7, 32-38	(kaimu mwenza wa Yer. II)	786-746	783-743	782/81-753 753-752	Amosi 1:1; 7:9-11
(kaimu mwenza wa Ahazi)	-----	-----	744/43- 732/31	1 Nya. 5:17 2 Nya.26:23- 27:9 Isa.1:1;7:1 Hosea 1:1 Mika1:1	Yeroboamu II	746-745	743	752-742/41	2 Fal.15:10, 13-15
Ahazi	735-715	736-728	732/31- 716/15	Isa.1:1; 7:1ff; 14:28;38:8 Hosea1:1 Mika1:1	Zakaria	745	743	742/41- 740/39	2 Fal.15:14, 16-22
(kaimu Hezekia)	-----	-----	729-716/15	2 Fal. 15:30- 16:20 2 Nya.27:9- 28:27	Shalumu	738-737	737-736	740/39- 732/31	2 Fal.15:27-31 16:5
Hezekia	715-687	727-699	716/15- 687/86	Isa.1:1; 7:1ff; 14:28;38:8 Hosea1:1 Mika1:1	Menahemu	737-732	736-730	732/31- 723/22	2 Nya.28:6 Isa.7:1
(Kaimu mwenza wa Manase)	-----	-----	696/95- 687/86	2Fal.16:20; 18:1-20,21 2 Nya. 28:27- 32:33 Mith.25:1	Pekahia	732-724	730-722	722 K.K	
Manase	687/86- 642	698-643	687/86- 642/41	Isa.1:136:1-39:8 Hosea 1:1 Mika 1:1 Mt.1:9-10	Peka	724 K.K	722 K.K		
Amoni	642-640	643-641	642/41- 640/39	2 FAL. 20:21- 21:18; 23:12,26;24:2	Hosea				
Yosia	610-609	640-609	640/39-609	2 Nya.32:33- 33:20 Yer.15:4ff 2 Fal.21:18-26	Samaria kuangukia mikononi mwa Shamu				
Yehoahazi	609 (miezi 3)	609	609	2 Nya. 33:20-25 Yer.1:2 Zef.1:1 1 Fal.13:2-3					
Yehoiakimu	609-598	609-598	609-597	2 Fal.21:24; 22:1-23:30 2 Nya.33:25- 35-27					

Yehoiakini									
Zedekia	598/97 (miezi 3)	598	597	Yer.1:2 Zef.1:1 Mat.1:10-11  2 Fal.23:30-34 2 Nya.36:1-4					
Kuanguka kwa Yerusalemu mikononi mwa Babeli	597-586	598-587	597-587	2 Fal.23:34- 24:6,19 2 Nya.36:4-8 Yer.1:3; 22:18-23 25:1ff 26:1ff;27:1ff 35:1ff; 36:1ff Dan.1:1-2  2 Fal.24:17-25:7 25:27-30 2 Nya.36:8-9 Yer.52:31 Ezek.1:2  2 Fal.24:17-25:7 2 Nya. 36:10-11 Yer.1:3; 21:1-7; 24:8-10 27:1ff; 32:4-5; 34:1-22; 37:1-39:7; 52:1-11  Kitabu cha Maombolezo					
	586 K.K	587 K.K	587 K.K						

**Kwa ajili ya mjadala mzuri juu ya matatizo uwekaji tarehe angalia E. R. Thiele, *The Mysterious Numbers of the Hebrew Kings*.**

# **KIAMBATISHO CHA PILI**

## **KAULI YA KIMAFUNDISHO**

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachowenza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwaa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupohea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kuitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote turmesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambaa wanakombolewa kweli ingawa wakati mwengine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwengine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.

9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.”